سواحيلي

The Path to Happiness

Njia ya furaha

Riwaya njia ya furaha na maswali tatizi na falsafa ya maisha

Riwaya



Dr. Abdullah bin Salim Bahammam

2014 - 1435

Riwaya

Njia ya furaha

Riwaya njia ya furaha na maswali tatizi na falsafa ya maisha

Dr. A - S Bahammam

Njia ya furaha

Maswali tata..na falsafa ya maisha.

www.path-2-happiness.com

www.path-2-happiness.com

Kikongwe



www.path-2-happiness.com

1 Kikongwe

Kikongwe

(1)

Baada ya kukosa usingizi kwa muda mrefu Bwana huyu alichomoa karatasi na akaandika:

“Mpenzi Katarina mimi naondoka na sirejei kamwe! Nitamaliza matatizo yangu ambayo yamenizonga. Nakwambia wazi wazi! Naomba uniwiye radhi nawaomba watoto nao waniwie radhi.”

Na huyo akaondoka pale na kwenda zake.

Alikuwa anasitasita licha ya kuwa alikuwa anajiuliza kimoyomoyo mara nyingi hakuwa na ufumbuzi wa matatizo yake zaidi ya kujitoa uhai. Alikuwa anatembea kwa hatua ndogo ndogo akiwaza rohoni: “Hivi kweli mimi ni mgonjwa.” Daima, Katarina, anasema hivyo, akiwa ananishauri niwe mwenye imani na myakinifu. Hayo karejea mara nyingi.

- Pambana na maradhi ya wasiwasi, Joji wala usikate tamaa.

Na hata baba yake alikuwa anamwona kuwa anaumwa, alisema hayo na kumwambia kuwa maradhi hayo ya kurithi yametoka kwa upande wa mama yake. Na Kakhi, mkuu wake wa kazi amempa nasaha mara nyingi ili Joji atulie na ajiweke sawa. Bwana huyo ambaye ni Myahudi akimsemesha kama nduguye akisema mara nyingi huku anatabasamu na kumtania.

- Kipenzi changu Joji, nisikilize, wewe unajishughulisha nafsi yako bila faida yo yote ya yale unayoyawaza hayakuongezi kitu cho chote, tatizo kubwa ni kuwa fikra hizo zinakuzuwia na unashindwa kutumia uhai wako vema.
- Joji sasa ana miaka thelathini na nane, alimwoa Katarina ambaye ni Mwingereza mwenziwe. Lakini Katarina ana asili ya kutoka India. Ndoa yao imedumu kwa miaka kumi ambayo walipata watoto watatu; wa kwanza Maria (huyo angelikuwa na umri wa miaka kumi, lakini alifariki akiwa na miaka saba); Maiko (ana miaka minane) na Sali (ana miaka sita). Tangu alipofariki mtoto wake wa kwanza – Maria hajatulia. Daima amekuwa mwenye kuwaza tu nini maana ya maisha, nini mauti na sababu gani mpaka apende fikra za falsafa moja. Alizidisha maswali sana. Joji alizama katika kusoma falsafa na historia na akawa anasoma dini mbalimbali. Huenda usomaji wake huo mwingi ulimfanya asione ugumu kumwoa KatarinaMkatoliki, mwalimu wa mambo ya dini.

Joji alikuwa anamwona mkewe kuwa ni mtu mwenye imani na aliye

www.path-2-happiness.com

makini sana jambo ambalo yeye hakuwa nalo licha ya kuwa yeye alijinaki kuwa ni wa madhehebu ya Kiprotestanti. Na bado aliendelea kuwa anauliza mambo yote. Alikuwa anashangaa kuona bibi huyo alikubali mambo yote na yeye akaendelea kujiona kuwa anauliza maswali kwa sababu ana akili kitu ambacho Katarina mchaMungu hakuwa nacho. Alibishana naye mara nyingi na mijadala mingi ilihusu akili ambayo inawakilishwa naye, na imani na msimamo ambao unawakilishwa na Katarina, au wakati mwingine mjadala unakuwa kati ya ukweli wake yeye Joji na mambo ya kufikirika ya Katarina. Ama ubishi ukianzia kwa Katarina ulikuwa juu ya imani yake na kukubali kwake juu ya dini yake na shaka na maradhi ya Joji. Mwisho mabishano hayo yalikuwa yakiishia ukimya mrefu tu. Na kama isingelikuwa mapenzi baina yao wawili wangeli kuwa wamekwisha achana muda mrefu.

Na kwa mashaka aliyokuwa nayo Joji kuzidi hasa baada ya kifo cha binti yake mijadala ikaongezeka kuwa mikali na tete, maswali yaliyo kuwa yanajirejea yakawa: Kwa nini tuliumbwa? Na kwa nini tunaishi? Na wapi tunako kwenda? Maswali haya yalitawala fikra za Joji. Maswali haya yanaonekana kuwa ni mepesi, lakini ni mazito sana. Na wana falsafa wamepata kuzama katika maswali hayo, wakatumia akili zao na maarifa yao kutokana na uzoefu na mwangalio wao wa maisha na mazingira yaliyopo. Yeye akawa anaona kuwa majibu yake yote hapo ni mwanadamu kuwa huru na kuwa mwenye furaha.

Na pale alipokuwa njiani akielekea kwenda kujiua zilikuja hoja nyingi mbele yake kutokana na maisha yake. Hoja hizo zilipita mbele ya macho yake na kumkumbusha binti yake alivyokuwa anahangaika katika mwisho wa uhai wake akiwa katika gari la wagonjwa. Lakini umauti ulishinda na kumbwaga yule binti maskini–na ukachukua uhai wake na uzuri wake na kuondoka na roho yake na mwishowe yeye mwenyewe. Pia akamkumbuka mtoto wake wa kiume Maiko, ambaye alipata kumwuliza siku moja akiwa amechoka na shughuli nyingi:

- "Baba yangu kwa nini unakwenda kazini kila siku?"
- Ili nipate ujumbe kwa maisha yangu na pia nawe nikutimizie haja zako.
- Una maana gani kusema ujumbe kwa maisha yako?
- Kuwahudumia watu na kuleta manufaa kwa wanadamu.
- Kwa nini?

Aliguna Joji kwa swali hilo akihisi kuwa lina mgusa kwa undani kisha akamjibu.

- Kwa ajili ya jambo kubwa –huenda hulifahamu hilo wewe na hata mimi!
- Baba! Wewe mkubwa na hulijui hilo!. Mimi nikiwa mkubwa nitajua kila kitu na sinto acha jambo kubwa lipite vivi hivi nisilijue.
- Maiko…sahau hayo kijana wangu mpenzi.

Kisha akacheka na kujisemeza moyoni: Hizi ndizo nasaha nipewazo kila siku: "Sahau haya mambo na faidi maisha yako". Kisha akamwambia mwanawe:

- "Usiogope siku moja nitakujibu hilo."
- Baba! umemaliza masomo yako, na unasoma sana, na hujui!
- Ah! mwanangu mpendwa! Je umemaliza kazi zako za masomo ya shuleni?
- Ndiyo!
- Basi hilo bora. Usiku mwema.

Basi aliendelea kuwaza na kuwazua huku akiwa anasonga mbele na safari yake nzito. Inaonekana kuwa mimi ni mgonjwa kama vile asemavyo Katarina au napoteza muda wa maisha yangu kama vile vile asemavyo Kakhi, au nina wasi wasi kama vile anavyosema baba, au..zuzu kama asemavyo Maiko! Huenda yale ayasemayo Maiko ni kweli, lakini cha kuchekesha ni kuwa majibu yangu kwake yalikuwa kama wanavyonijibu wengine: Sahau, labda nilijifunza kukwepa kwa kukimbilia mbele kama watu wengi wafanyavyo!.

Akiwa njiani akielekea kwenye eneo alitakalo kujiua akakumbuka siku ambayo alishikwa na huzuni nyingi tena ya kutisha, basi alikunywa pombe sana mpaka akalewa chopi! Kisha akatoka anaendesha gari lake na akaenda akalikwamisha ukutani, akatoka huku anayumba na akiwa ameshika kitabu kiitwacho, "Falsafa ya Furaha" Askari wa usalama barabarani akamshika na kumwambia:

- "Wewe kitabu chako ni –Falsafa ya furaha au falsafa ya kujiua? Je hufahamu kuwa ni kosa kuendesha gari ukiwa mlevi?

Katarina akaenda kumtolea dhamana kwa polisi wa usalama barabarani, Katarina akamwambia:

- Hukupaswa kuendesha gari lako ukiwa umelewa.

Akamjibu kiutani:

- Je haukuwa huu ndio usia wako kwangu: Kusahau?
- Hapana siyo kwa njia hii.
- Kwa nini basi siku zote unakesha ukinywa?
- Ah! Mimi nakunywa kweli lakini najumuika kwa kumtumikia masiya kanisani.

Akasema akimkejeli:

www.path-2-happiness.com

- Ah! Kikombe kitakatifu na kinywaji chenye baraka! Au unakwepa mambo?
- Hivi sasa mabishano nawe tena yanachokesha; wewe unaogopa hata kuwaza, unakimbilia kinywaji na kukesha kwa ajili hiyo kama ninavyo fanya mimi, lakini huo ulevi wako unauvisha vazi la utakatifu.

Maneno ya Joji yalikuwa makali sana, mama yule akaangukiwa na huzuni na kisha akasema:

- Lakini mimi sihitaji daktari wa nafsi na akili kama wewe!
- Huenda hivyo! lakini nani anajua hilo?

(2)

Akiwa njiani njia aliyoichagua ambayo ni ndefu sana – akafika mahali akatikisa kichwa chake ili ajipange na apange fikra zake vizuri. Akawa amefikia kiwango cha kusita na akaingiwa na hofu; na anaangalia watu wanapita na wengine wanafanya mambo yao. Akaona kama vile watu hao ni chombo tu kinazunguka lakini hakina uhai wala hakuna maana yoyote. Akawa anajiuliza moyoni: Vipi watu wanakubali kuwa kama chombo kisicho na uhai? Na akiwa anaendelea na safari yake hiyo akamwona mzee Kikongwe akicheza kwa furaha na mjukuu wake. Mara akatanabahi, akatabasamu, na akacheka na akamsogelea yule mzee na akasema:

- Samahani kukukatisha na mambo yako. Je wewe ni mwenye furaha?

Kikongwe akainua kichwa akamwangalia kwa mshangao na akasema:

- Naam! Kisha akarejea kwenye mchezo wake na mjukuu wake.

Joji akamkatisha tena:

- Vipi? Yaani kwa nini wewe una furaha! Kwa nini unaishi?
- Kikongwe akamwangalia tena kwa jicho la kumchunguza na akasema:
- Mwenyewe umejibu swali lako.
- Vipi?
- Mimi ninafuraha, kwa sababu najua kwa nini naishi, hivyo tu kwa wepesi kabisa.
- Mimi kwa nini naishi? Niambie hilo tafadhali.
- Hebu jiulize mwenyewe hilo. Mimi siwezi kukujibia swali hilo. Hakuna atakaye kujibia isipokuwa roho yako mwenyewe, na maisha yako.
- Nakuangukia tafadhali niambie.
- Nimekwambia hili swali anajibu kila mtu aliye na roho yake na uhai wake tena kwa urahisi kabisa. Mimi siwezi kukuambia jambo ambalo nafsi yako haikinaiki nalo na wala maisha yako hayana hajanalo.

Kisha Akamfuatilia Kwa makini:

- Hivi wewe ndiyo umeingia katika baleghe hivyo unataka nikupe mafunzo ya jandoni juu ya maisha na ulimwengu, au umeamua kuwa mzigo kwa watu.? Tafadhali sana nipishe niache niendelee mchezo wangu na mjukuu wangu.
- Nakuomba mara nyingine tena. Hivi vipi nafsi yangu na maisha yangu vinaweza kunijibia swali hilo.
- Nahisi kuwa unasema kwa ukweli wala hunitanii, basi hebu niache nikuambie jambo moja. Kama ukiangalia mkataba wowote utaona kuna mipaka yake, makubaliano hayo yakiwa yamefungwa kwanza vizuri kwa kamba na kufanya makubaliano hayo mazuri tena yako sawa sawa. Vivyo hivyo maisha yako daima yamefungwa na kamba nzuri na hivyo ndivyo sababu ya maisha yako – na ndivyo tunaishi na pia kupata furaha.
- Vipi? niambie bwana!
- Kama kweli wewe ni mkweli basi ufunguo wa jawabu hilo upo katika utafiti, kudumu katika hilo na kuazimia na kujaribu ufikie huko!
- Nifikie wapi?
- Ufikie kwenye furaha!
- Kwa njia gani?
- Tafuta njia ya kuelekea kwenye furaha! Utajisahau na utajikuta unaona kuwa uhai wako na nafsi yako vina maana kwako na utaona ulimwengu una maana kubwa maishani mwako. Ewe bwana! Hebu niache usinipotezee muda wangu. Nataka nicheze na mjukuu wangu.
- Vizuri, safi sana! Mimi siijui njia ya kuelekea kwenye furaha, huenda nitaifuata hiyo njia nami nifikie furaha kama unavyosema kama njia hiyo ipo!
- Ipo! Vinginevyo maisha yasingelikuwa na maana. Kwa vyo vyote vile naomba uniarifu pale utakapo pata jibu la swali lako. Na jawabu hilo utalipata kama ni mtafutaji. Na utaelewa maana gani roho yako itavyo kujibu na jinsi uhai wako utakavyo kujibu utaikuta hiyo kamba ambayo italeta maana ya kila kitu maishani mwako.
- Natamani hilo linitokee –lakini waitwa nani? Na wapi unakoishi?
- Kama nitakuwa hai basi utanikuta hapa hapa na wakati kama huu katika siku ya Ijumaa. Nipe anuani yako na nitakutumia anuani yangu baadaye.

Kisha Kikongwe alimgeukia mjukuu wake na akamtupia mpira Joji alishangaa sana na akasema:

- Ahsante sana! Hii hapa anuani yangu.

Kisha akaondoka..

www.path-2-happiness.com

Akaondoka huku akihisi dhiki na shida ambayo hajawahi kuipata maishani, hata katika siku ambazo alikuwa ana choka sana na kubanwa na kazi. Akaamua kuwa apate kinywaji kidogo, pombe kidogo ili apate nguvu na kutuliza akili zake. Alikuwa anahisi kama kichwa kitapasuka, lakini akaongeza kinywaji mwisho akapata kizunguzungu na akaishiwa nguvu na akawa anaishiwa fahamu na akaanguka njiani na kuzimia.

Watu walikusanyika wakamzunguka na wakamwinua naye akajikaza kisha akawambia nyumbani kwake wapi.

Hapo mlangoni akamkuta Katarina analia, kilio kizito anamlilia mumewe Joji. Na pale alipomwona Joji alimkimbilia na akajitupa kifuani kwake na kilio kikubwa. Joji akasema akimwambia:

- Mimi huyu hapa niko hai kwa bahati mbaya si kufa.
- Shukrani zake Mungu kwa kuwa uko salama. Niliogopa sana: Hivi kwa nini ufikirie kujiua?
- Ili niondokane na usumbufu wa kelele na ghasia. Niliache lichombo ambalo linaitwa Joji –lichombo ambalo halijui maana ya kuwepo kwake na maisha yake, life roho yake na nafsi iondokane na mashaka ya kila wakati. Leo hii kama si yule Kikongwe ambaye nilikutana naye leo huko njiani na kama siyo ile pombe niliyo kunywa saa hii ningelikuwa nimepumzika saa hii na shida za maisha.
- He! Kikongwe gani huyo?
- Simjui, lakini alikuwa ni mtu mwenye furaha, ana tabasamu kwa raha na anajua kwa nini anaishi?
- Sielewe kile usemacho, lakini namshukuru bwana kuwa hapo ulipo uko salama.
- Hata mimi sikumwelewa yote aliyosema, lakini nilielewa kuwa kuelekea kwenye furaha inahitajia mtu aazimie na aamue na aanze kutafuta namna ya kufikia huko kwenye furaha.
- Njia ya furaha! Utafikika huko mpenzi wangu. Lililo muhimu usikazie sana mambo kupita kiasi, sisi bado tunakuhitaji.
- Hahahaha! Nitajaribu kujidhibiti nisichupe mipaka. Nitajitahidi kuitafuta njia mpaka nipate jibu na nitakuwa na furaha kama yule Kikongwe.

Katarina aliona jinsi Joji anavyohangaika na uso ukionesha mikunjo yake, akamshika mkono na akamsaidia wakaelekea mpaka wakafika chumbani kwao akajinyoosha kitandani akaanza kuwazua yale yaliyompata siku hiyo aliendelea hivyo lakini alizidiwa na usingizi akalala fofofoo.

MASWALI MENGI YENYE UTATA

www.path-2-happiness.com

2 MASWALI MENGI YENYE UTATA

MASWALI MENGI YENYE UTATA

(1)

Katarina alimgeukia Joji mara tu baada ya kuisha filamu ambayo walikuwa wanaangalia pamoja. Alifanya hivyo ili amwondoe katika ukimya ambao alikuwemo pengine akili zake zilikuwa zimekwenda mbali.

- Joji ..Joji…hivi hutaki kuondokana na matatizo uliyokuwa nayo?
- Unasema niniuna maana gani? Bila shaka nataka niondokane na matatizo yangu.
- Jirani yetu mpya aliniambia kuhusu tabibu nafsi mashuhuri anaitwa Tom Erickson.? Aliniambia kuwa yeye alipata kutibiwa naye.

Joji aligeuka katika kiti chake na akamwangalia mkewe na usoni alikuwa tayari kuna ndita ikiwa ni ishara ya kuwa hakuwa na utulivu tena wa nafsi. Kisha akasema kwa dharau…

- Vizuri sana, wataka niende kwa huyo tabibu kisha niseme –nieleweshe maana nasahau kwa nini niliumbwa na kwa nini naishi?
- Hapana! Bali mwulize akuambie njia gani utumie kufahamu kwa nini uliumbwa na kwa nini unaishi?
- Ili nijue jawabu!!!
- Ndiyo.

Joji alilaza kichwa chake kwa nyumahakukaa hivyo sana bali akaingiwa na wasiwasi na shida. Katarina akaliona hilo na akatambua kuwa Joji hapo alipo hana mawasiliano tena bali kaingiwa na wasi wasi na hofu tena. Basi akamwita kwa sauti kubwa.

- Joji!
- Naam, naamnilikuwa nataka kukuuliza huyo dokta Tom ni Mprotestanti? Au hamasa zako ni kwa sababu zingine?!
- Joji mpenzi! Hamasa zangu ni kutaka mimi nawe tuishi kwa furaha. Pengine una chukizwa na vile ninavyoikimbia nafsi yangu. Lakini hilo ni bora kuliko hivyo unavyoishi kwa wasiwasi na mashaka.
- Vizuri nilikwisha fanya uamuzi kuwa nitafute njia ya kuelekea kwenye furaha.

www.path-2-happiness.com

Sintokimbia na kujificha katika ndoto kuanzia leo, badala yake nitatafuta jawabu hilo…kisha Joji alitabasamu na akaongeza kusema: Lakini sitoifuata njia hiyo ndani kwa padri wa Kikatoliki. Jambo la kwanza nitamtafuta huyo daktari kwanza.

- Tutauliza habari zake na namwomba Mungu ajalie katika mikono ya daktari huyo tiba.
- Hahaha! Maana yake mimi ni mgonjwa ambaye anahitajia tiba –mimi siyo mwana falsafa anayetafuta majibu ya maswali!
- Tiba ndio njia ya kufikia majibu siyo kuwa wewe ni mgonjwa – kisha Katarina alimkonyeza na akajitupa kifuani kwake na akasema:Tumeelewana mpenzi?
- Tumeelewana!

(2)

Joji alikuwa makini sana kutaka kujua habari za dokta Tom kabla hajafanya mpango wa kuenda kumzuru. Alifungua mtandao wake wa – facebook akaona mikutano ambayo alipata kuhudhuria dokta Tom. Akaona aina na jinsi ya mihadhara aliyopata kusikiliza na ile aliyopata kutoa. Kisha akasoma yale waliyoandika wagonjwa wake kuhusu yeye, akapata picha ya alivyo dokta Tom, ni daktari makini wa magonjwa ya nafsi, mwerevu, mwenye taaluma pana, mpenzi wa falsafa, alikuwa ni mtaalamu aliyechanganya taaluma za kisasa za tiba na masomo mbali mbali ya falsafa.

Joji alifuatilia rai za wagonjwa wa Dk Tom na maelezo yao, kwa njia hiyo aliona kuwa tabia za Dk Tom na elimu yake vilikuwa haviendi sawa sawa, hususan na wagonjwa wake wa kike. Na pia akaona kuwa huyo si Mkatoliki kama alivyo kuwa anadhania, bali huyo bwana ni mpagani, haamini dini yoyote.

Joji alikuwa anacheleweshe kupanga siku ya kwenda kwa dokta Tom, aliakhirisha mara nyingi, hakuwa na haraka na hakupenda kwenda kwa dokta mwenye tabia yenye kutatanisha. Lakini alimwahidi Katarina kuwa atakwenda na akaendelea kutoa sifa zake mganga huyo kwa mkewe. Basi siku moja ghafla mkewe akamshtukiza na kumwambia amepanga waende siku hiyo kwa daktari saa kumi jioni na watakwenda pamoja. Kwa shingo upande alikubali, lakini hakuwa na raha kwa kukutana na daktari huyu! Alikuwa akijisemeza: Uzoefu mpya lakini utakaofeli, si tatizo halitonidhuri lakini utafunga mdomo wa Katarina.

Joji na Katarina wakaenda katika kliniki ya dokta Tom siku hiyo, ilikuwa ni kliniki tulivu kabisa, samani zake ni nzuri za kuvutia, rangi zake zimeshikana vizuri na zinafurahisha kuziangalia. Mahali pa makaribisho walikuta mtu mwenye sura yenye mikunjo mikunjo, amekaa ametulia mezani. Joji akamueleza kuwa walikuwa wamepangiwa kumwona dokta Tom saa hiyo, na akajibu kwa utaratibu kabisa:

- Naitwa Baraad, sijapata kukuona kabla ya leo. Nadhani daktari ana kazi sasa hivi.

Joji alimgeukia Katarina na akamuuliza?

- Je, hukuweka ahadi ya kukutana na daktari leo?
- Bila shaka nilikuja siku tatu zilizopita na kuweka ahadi!

Baraad akajibu kwa utani,

- naam …naam nilisahau nisamehe, kweli uliweka ahadi, tafadhali ingieni anawasubiri.

Joji na Katarina wakaingia ofisini kwa daktari huku Joji akishangazwa na kuchukizwa na tabia ya Baraad. Daktari aliwapokea vizuri, kisha akaomba akae na kila mmoja wao peke yao.

- Joji akasema:
- Lakini mimi tu ndiyo niliyepanga kukuona.
- Na Katarina mkeo, na watu wengine ambao wako karibu yako, hao watanisaidia sana katika kufahamu hali yako. Napenda nikae naye kwanza kabla yako kwa muda, kisha nikae nawe.

Joji alitoka akaenda chumba cha makaribisho akaketi kwenye kiti kimoja akiwa kimya tena kwa tabu. Baraad akaanza kumsemesha:

- Tom yuko na Katarina!
- Wewe nani kakwambia jina lake?
- Ah! bwana! siyo huyo mama aliyekuja hapa siku tatu zilizopita…kisha akatabasamu kiutani. Tom anakaa nayewawili tu peke yao, kwa kweli dokta Tom ni mwenye bahati sana. Mwanaume anayependeza anakaa na mwanamke mwenye mvuto wa nchi za Mashariki!

Joji akawa hana raha akatafuta jarida limshughulishe na kumweka mbali na Baraad ili kuficha hasira zake. Kisha Joji akakumbuka sifa mbovu za Tom na mahusiano yake na wagonjwa wake wa kike. Ilikuwa kidogo avunje ukimya, lakini akajikaza basi akaamua kunyamaza. Baada ya kimya kama dakika kumi hivi akatoka Katarina na huku akicheka na kumwita mumewe:

www.path2-happiness.com

- Mpenzi! daktari anakusubiri. Mimi nakwenda Kanisani kuna jambo nimepanga kulifanya huko.

Joji aliingia kwa daktari na ule uchangamfu wake ukapotea. Akapokelewa vizuri lakini katika uso mkavu wa daktari na akamwambia:

- Kwa nini unataka kujua nani aliye kuumba? Na kwa nini unaishi? Na unaelekea wapi?
- Kwa sababu nataka niwe na mpango wa maisha na roho yangu itulie nikijua maana ya maisha na uhai wangu.
- Mh mh! Hapa naona niko na mtu mwenye elimu kubwa msomi mzuri! Kwanini hutumii njia za wanafalsafa katika kufikiri na kuwaza?
- Sikuelewi, una maana gani?
- Vipi hufahamu ewe mwanafalsafa? Tunapotumia kujibu mambo kwa njia ya falsafa mambo yote yanajipanga kwa mpangilio wa maswali moja baada ya jingine na kuleta majibu yake vivyo hivyo.

Alinyamaza kidogo kisha akaendelea kusema:

- Ili kuweza kujibu maswali yako nitakuuliza maswali mengine, kwa mfano: ni wapi tunaweza kupata majibu ya maswali haya? Badala ya kutafuta na kuyaingia majibu moja kwa moja, tuangalie tunaweza kupata wapi? Ni yepi vigezo vya usahihi wake? Je huoni ya kuwa njia hii ndio ya mantiki ya kifalsafa nzuri zaidi?
- Huenda ikawa ni hivyo!
- Njia hii hutumika katika kuleta majibu ya maswali yako kutoka kwako mwenyewe –rohoni mwako! Kisha akatabasamu na kusema: Bila shaka hii ni njia bora kuliko njia ya Wakatoliki ambayo ni kukubali kila kitu bila ubishi au kutumia akili! Tukutane tena juma lijalo na ujitahidi uniletee majibu juu ya maswali mawili: la kwanza ni wapi tunaweza kupata majibu? Nini dhamana ya usahihi wake? Je tumekubaliana?
- Licha ya ubaya uliosema juu ya Ukatoliki ila ni jambo la mantiki na linaingia akilini, sawa tumeafikiana.

Joji alitoka hapo kwa tabibu na mara jicho lake likamwona Baraad ambaye alimuwahi kwa tabasamu lake zito la kijanja janja.

- Natumai kikao chenu kilikwenda vizuri, salamu zangu kwa Katarina!

(3)

Maswali ya Tom na njia zake za mazungumzo zilimwathiri sana Joji. Akawa anaendesha gari lake na huku anajizungumzisha. Mimi nilikuwa na maswali lakini Tom kaniongezea maswali kichwani mwangu!

Akaelekea kwenye mgahawa wa karibu ili akapate kikombe cha kahawa. Alifika mhudumu na akaiweka kahawa hapo mezani, lakini yeye hakuhisi chochote. Mhudumu alijaribu kumtanabahisha lakini Joji alikuwa amezama ndani ya mawazo mazito. Aliondoka mhudumu. Baada ya muda Joji alizindukana kuiona kahawa yenye vuguvugu hapo mezani. Alimuita mhudumu aje amlipe:

- Hivi unaamini kuwa sikuhisi pale ulipo kuja na kahawa, Ah! Wajuwa wakati mwingine akili zetu zinashughulishwa na maswali yetu ya ndani hata nafsi zetu na mtu anajisahau!
- Mtu kuwa na maswali mengi kichwani ni dalili ya kuwa ana akili na mtu aliye makini, lakini hali hiyo ikizidi, basi huo ni mkorogano wa mambo ya ndani yake, na mgongano kuhusu lipi lenye kukinaisha katika fikra za mtu.

Joji alishangazwa na maneno ya mhudumu na akaendeleza mazungumzo naye:

- Ni nini chanzo cha mkorogano huu – nipe rai yako!
- Vyanzo ni vingi. Vilivyo vikubwa ni kuwa mtu hakuangalia vitu vya msingi na kuviangalia kwa dhati yake na haswa vile ambavyo anaishi kwa ajili yake kama vile: Kwani tumeumbwa? Kwa nini tunaishi? Na wapi tunaelekea? Tatizo hili huwa limefichikana kwenye itikadi, utaratibu na wepesi wa maisha utatupa kuzama katika majibu ya maswali yale.

Joji alifungua macho yake kwa mshangao:

- Vipi mtu afikie majibu ya maswali hayo kwa wepesi?
- Watu wengi huyakimbia majibu ya maswali hayo kwa kuendekeza michezo na ulevi au kufanya uasherati na mambo mengine ya namna hiyo. Na kujiuliza kuhusu mambo hayo ni katika dalili nzuri ya mtu kuwa na utambuzi wa mambo, lakini…

Mhudumu aliitwa na mteja mwingine na akakata mazungumzo yao haya mafupi. Aliomba radhi kwa Joji na akachukua malipo yake ya kahawa na kuondoka.

www.path-2-happiness.com

Joji alitoka hapo akawa anazunguka na gari lakehajui anakwenda wapi, lakini hakuweza kusahau maneno ya mhudumu. Maneno hayo yalimpata akilini na kukamata hisia zake. Alikuwa anatamani yule mhudumu angelifikisha mwisho kauli yake. Na lau hilo lingemfanya alipie tena bei ya kahawa mara kumi hivi! Alikuwa anashangaa kuwa kwake na furaha sana alipokuwa anazungumza na mhudumu huyo licha ya kuwa ni mtu wa chini sana, kama vile ilivyo kazi yake ni ndogo, sura na umbile lake linaonekana kuwa ana asili ya Ugiriki basi kama sivyo ana asili ya Kilatini.

Baada ya kama saa hivi kupita, Joji alitanabahi kuwa bado hajatoka kule alipokuwa, aliamua kurudi katika mkahawa ule kwa mara nyingine, alifika akakaa mezani na akaagiza kahawa kama mwanzo. Akaja mhudumu mwingine akamwuliza kuhusu alipo yule mhudumu wa mwanzo.

- Ni yupi unayemkusudia Bwana?
- Nilikuwepo hapa kabla ya nusu saa hivi na alinipokea mhudumu mwingine.
- Pengine huyo ni Katu au Adam hao zamu yao imekwisha kama saa moja hivi, na sasa ni zamu yetu.

Joji akanywa kahawa haraka haraka na wakati akiondoka alimuuliza yule mhudumu:

- Lini watauwa kazini Katu au Adamu?
- Kesho saa tatu asubuhi watakuwepo mpaka saa kumi na moja au kumi na mbili jioni.
- Ahsante sana!

(4)

Joji alirejea nyumbani kwake na watoto wake wakampokea. Akawauliza mama yao yuko wapi. Maiko akamwambia kuwa bado yuko kanisani na pengine atachelewa kidogo hadi usiku.

Joji akaketi barazani akimsubiri Katarina arudi kutoka kanisani. Hakurudi mpaka saa nne usiku, yuko hoi anajisukuma, ananuka pombe, pamoja na kuwa alikuwa akitambua kilichokuwa pambizoni mwake. Pindi tu alipomwona Joji akamuuliza:

- Vipi habari kuhusu daktari?
- Ah! Ni daktari wa ajabu, pamoja ya kuwa kuna mambo ambayo yuko makini nayo. Joji akamgeukia Katarina na kumuuliza: Alikuwa anataka nini mlipo bakia pamoja?
- Sijui mpenzi, alikuwa ananikaribisha tu, kisha akajitambulisha yeye na uwezo wake, kisha akauliza kazi niifanyayo na maisha yangu kwa ujumla. Ni mwepesi kuelewana naye na ni mchangamfu sana.
- Na bila shaka ni mwenye umbile zuri! Je, hakukuuliza habari zangu hata kidogo?
- Aliniuliza pale nilipotaka kuondoka. Nikamweleza kuwa unapatwa na woga na unakuwa na fikra nyingi hasa juu ya maisha.
- Hilo tu?!
- Hilo tu! Muda mwingi alikuwa anazungumza habari zake na kuniuliza mambo yangu, kiasi gani alivyo na heshima zake.
- Mh mh! Meneno ya ajabu juu yake. Unamsema vizuri licha ya kuwa ni mpagani hana dini na anapiga vita dini zote na anaona kuwa mtu kuwa na dini ni maradhi, kwa kweli ni mpuuzi!
- Joji! Alikuwa ni mtu mwema kwangu! Hakuzungumza nami kabisa kuhusu mambo ya dini, hata baada ya kujua kuwa mimi ni mwalimu wa dini. Hata hivyo shida yako kwake si adabu yake wala dini yake!
- Ulikuwa na nani mnakesha jioni hii na mkinywa?
- Huna haja ya kuniusia, na ni haki yangu kutokujibu. Hata hivyo tulikuwa tuna hafla kanisani ya kumbariki padri.

Mara nyingi Joji hupata shida pale Katarina anapokesha kanisani na kuchelewa kurudi nyumbani usiku, na hasa anapo kunywa maana hilo linapingana na dini yake ambayo huyu bibi hutumia muda mwingi akiitumikia. Hata hivyo Joji alihisi kuwa alimkosea Katarina kidogo, Joji akabadilisha mwelekeo wa mazungumzo kwa kutania:

- Nilikuwa na maswali kadhaa, basi yule bwana akaniongezea tena maswali tele juu ya maswali yangu na kuzidi kunivuruga tu.
- Vipi?
- Badala ya kutoa majibu kwa maswali yangu, akaniuliza maswali mengine na akataka nimpelekee majibu.
- Maswali mengine?
- Naam! Nitapata wapi majibu ya maswali hayo, na je kipi kitahakikisha usahihi wa majibu hayo.
- Pamoja na kuwa ni maswali ya ajabu huenda akawa ni mwenye haki kufanya hivyo!

www.path-2-happiness.com

- Achana na hilo! Leo nimekutana na mtu mwingine wa ajabu. Kanichezea akili yangu sana. Kasema maneno yanayonigusa bila kukusudia. Kasema habari zile zile nilizofuata kwa yule daktari.
- Habari zile zile?!
- Eh! hiyo ni ajabu ya mambo!
- Kasema nini huyo mtu?
- Sielewi kwa uwazi wake, maana hakumaliza kusema maneno yake, ingawaje anaonekana kuwa ni mtu mwenye dini tofauti kabisa na alivyo Tom. Alikuwa akizungumzia wepesi wa kujibu maswali, na kuzama katika hili, maana ya maisha na furaha, kisha Joji akamkazia macho mke wake: kazungumza pia kuhusu watu wengi wanavyoyakimbia majibu kwa kuzama katika kunywa pombe na kukesha na mfano wa hayo!
- Kwa kuwa ni mtu wa dini, basi maneno yake yalikuwa mazuri, kidogo alikuwa mkali juu ya watu kukimbia ukweli wa majibu!. Katarina alitabasamu na kusema: Pengine alikuwa Mkatoliki! Mpenzi wangu unaonesha umechoka na huwezi kuwa makini na unachozungumza!
- Labda hivyo lakini alinigusa sana kwa hali zote. Tulale sasa kesho nina kazi nyingi.

Wakaondoka hapo barazani kwenda chumbani kulala kabla ya usingizi simu ya Katarina ikaita, aliangalia akiwa ni mwenye kubabaika, kisha akamjibu aliyempigia kwa maneno ya haraka haraka kisha akabakia kimya akisikiliza kwa muda mrefu kisha akakata simu.

- Ahadi yetu ni Jumatano saa mbili usiku, tutakesha pamoja kanisani.
- Nani huyo aliyepiga simu?
- Mtu ambaye anataka kujifunza Ukatoliki.
- Anajifunza katika mkesha!
- Mkesha kanisani na si katika jumba la dansi au unataka akajifunze dini makaburini. Hebu tulale acha mambo yako.

(5)

Kulipokucha Joji aliamka kabla ya Katarina na jambo la kwanza kichwani mwake ni habari za yule mhudumu ambae hajui siri ya kuvutika nae, aliazimia kwenda mkahawani kukutana nae tena. Mara akakumbuka simu iliyokuja kwa mkewe jana usiku. Aliifungua simu ya Katarina akanakili ile namba ya yule aliyepiga usiku kisha akairejesha simu mahali pale pake.

Joji aliondoka akaenda kazini mapema, alifanya hivyo kwa kuwa jana aliomba rukhsa atoke mapema na kazi zikarundikana mezani kwake wakati alipo kwenda kwa Dk Tom. Alipoingia ofisini kwake na kuanza kufanya kazi zake mara alipigiwa simu ya mezani. Huyo alikuwa ni Kakhi mkuu wake wa kazi.

- Habari za asubuhi!
- Njema bwana!
- Vipi ziara yako kwa dokta jana ilikuwaje?
- Hamna tabu! Ilikuwa salama, bado ndiyo mwanzo mambo yatabainika huko usoni.
- Vizuri! lakini unapoteza muda wako na fedha kwa kufikiria juu ya mambo haya ambayo ni kazi bure tu. Kwa upande wangu kama ungeniuliza ni nani atakayenilipa zaidi nitamfanya kuwa ni Mungu wangu kisha akacheka kicheko kikubwa, na akasema: hebu njoo kwangu kuna kazi iliyotokea jana.
- Sawa! nakuja baada ya saa hivi ikiwezekana.
- Vema! njoo baada ya saa moja.

Joji alipiga namba ile iliyotumika jana usiku ila hakutumia simu yake, alisikia sauti ya Tom upande wa pili. Joji hakukosea sauti aliyoisikia, alimsikia akisema: Hallo haloo nani mwenzangu? Je, unanisikia? Joji alikata simu mara moja, ghadhabu ilimmiliki, kwanini Katarina hakumwambia kuwa aliyempigia simu alikuwa Tom? Na kwa nini alibabaika? Kwa nini…? Je, ndivyo yalivyo maisha ni siri ndani ya siri na maswali mengi?

Joji akarejea kufanya kazi zake ili amalize kazi zake kwa haraka. Na baada ya saa moja kamili alifika ofisini kwa Kakhi, Khaki alisimama na kumkaribisha.

- Rafiki yangu! Vipi dokta kakutibu wasiwasi wako?

www.path-2-happiness.com

- Bwana mie sina wasiwasi wala mimi siumwi! Nilikwenda kwa dokta ili anipe majibu ya maswali yangu.
- Inaonekana kuwa maudhui hii ni nyeti sana kwako, nilikuwa na kudhihaki tu. Unajua rai yangu kuhusu hilo, achana na hayo kwa sasa, la muhimu napenda ujali namna ya kujiongezea mali zako na ufurahie maisha yako na raha zake.Nimekuita tukutane mimi nawe kwa sababu shirika linapanua shughuli zake na kuongeza utaalamu kutoka India limetutumia muwafaka wa sharti zetu, nasi kwa sasa tuna haja ya kuchukua watu kutoka kwao, kama ilivyo tuna haja ya kukuza uhusiano wetu na shirika la ugavi wa programu huko India. Ni lazima mtu mmoja aende India katika kipindi cha majuma mawili kuanzia sasa! Je uko tayari kusafiri?
- Haraka hivyo?
- Kwa bahati mbaya ndiyo. Mimi kwa bahati mbaya siwezi kwenda kwa sababu kutakuwa na kikao cha bodi baada ya majuma mawili.
- Nitaangalia vipi itakuwa nafasi yangu, na nitakueleza kwa siku mbili hizi kama ninaweza kwenda au vipi. Ningelipenda ungelinipatia nakala ya mkataba na makubaliano ndani ya mfumo wa mtandao; ili niuthibitishe na kuufanyia utafiti ili mambo yawe wazi kwangu.
- Hivyo basi miadi yetu ni juma lijalo! Ni vizuri ukajitayarisha na safari..kisha tabasamu na achana na huyo tabibu, nina jambo nitakalokushtukizia wiki ijayo.

Joji alitoka nakwenda ofisini kwake. Aliangalia ile mikataba na nyaraka za maelewano ya mwanzo ambavyo Kakhi alikuwa kamtumia tayari kupitia mtandao wa ndani wa shirika. Joji aliitamania sana hiyo safari, lakini alikuwa ameshughulishwa na mambo matatu: Mhudumu, daktari pamoja na Katarina!

Toka asubuhi ya leo alikuwa ameazimia kwenda kumwona mhudumu. Ama tabibu miadi yake naye ni kabla ya safari, na inawezekana kabisa kuomba miadi nyingine siyo ile iliyopangwa, Lakini Katarina!? Hivi inaingia akilini kuwa mkewe ambaye ni mchaMungu anafanya khiyana ndani ya ndoa yao kwa Tom mpagani? Vipi hilo. Hapana mbona haliwezekani!!

Muda wa kazi ulipomalizika Joji alielekea kwenye mkahawa wa jana ili akaonane na mhudumu wake wa jana. Alipofika na kumwona basi nafsi yake ikatua akashangaa kuhusu hilo, kisha akaketi mezani na yule mhudumu akaja kutoa huduma:

- Naam! nikusaidie nini kaka!

- Kahawa! Samahani! hivi wewe waitwa Katu au Adam?
- Naitwa Adam kaka!

Mhudumu alindoka kwenda kuleta kahawa na mara aliporudi Joji akaanza kusema:

- Hivi waweza kupata muda tukakaa na kuongea mimi na wewe?
- Samahani kaka sitoweza, natamani kukuhudumia, lakini nina majukumu mengi.
- Vipi Je, ninaweza kukusindikiza unapo maliza kazi zako.
- Ah! huo ni ukarimu wako kwangu hilo nalikubali! kwa uchache leo sitalazimika kupanda mabasi... muda wangu wa kazi una kwisha baada ya nusu saa.
- Sawa basi nitajivuta kidogo kidogo katika kunywa kahawa ili niisubirie iishe, nitafurahi kukusindikiza.
- Ahsante sana kwa hilo, kwa idhini yako.

Joji akawa anakunywa kahawa yake pole pole, huku akikumbuka yale maneno ya Adam yaliyomtingisha, akawa anajiuliza: mhudumu huyu ananishangaza sana, amewezaje kunieleweshа kwa haraka wakati hanifahamu? Alijuaje kuwa nina matatizo ya kifikra kuhusu kadhia nzito kama hizi? Nina hamu ya kujua majibu yake…kwa undani zaidi na kwa wepesi..ehe falsafa iliyoje!

Adam alitokea na kukatisha mawazo ya Joji na akamwambia huku akitabasamu na akiwa amevaa nguo za kawaida baada ya zile za kazi akasema:

- Mimi niko tayari! Je tuondoke?
- Nami pia, Je wataka kwenda nyumbani kwako au tukapate kahawa hapa hapa au twende tukapate chakula cha jioni katika hoteli ya karibu?
- Kama umenipa uchaguzi katika hayo basi nachagua la tatu.
- Kuna hoteli ya furaha hapa karibu nafikiri itatufaa.
- Hiyo inafaa kabisa! Jina lake lina mvuto yaani furaha jina zuri sana na watu wengi hawaipati hasa katika zama zetu hizi kuna tabu tupu na mashaka.
- Maneno ya Adamu yaligonga kifuani kwa Joji aliona kama vile alikuwa amelengwa yeye lakini aliamua kumezea asijibu kitu.

www.path2-happiness.com

(6)

Joji na Adam waliingia hoteli ya furaha na wakaikuta kuwa inafurahisha kweli; kwa rangi zake na mapambo yake vilikuwa vinapendeza. Mipangilio yake ilikuwa ina mweka mtu katika furaha na raha.

Walikaa mezani na akawajia mhudumu akiwa na orodha ya vyakula (menu) na Joji akamwambia Adam;

- Tafadhali, chagua chochote.
- Nakula samaki aliyekaangwa na mboga mboga.
- Na mimi niletewe steki ya nyama ya ng'ombe na viazi mviringo.

Na mara tu alipoondoka mhudumu Joji akamwambia Adam:

- Haya bwana tuko katika furaha hoteli, furaha ambayo watu wengi hawaipati katika zama hizi kama unavyo sema wewe.
- Hahahaha! naam, mashaka na wasiwasi yanauwa maana halisi ya maisha. Watu wamekuwa kama ala na ngao katika mashine isiyofanya kazi harakati zao hazina maana zimefungwa wala hazina athari. Na hawaoni raha na utamu wa maisha, wao wamekuwa kama mashine au vyombo vya kufanyia mambo hawajui furaha ya maisha ambayo ndani yake wanaishi wala hawajui mwelekeo wao ni wapi.
- Hivyo wewe ni miongoni mwa wafuasi wenye kukimbia wasiwasi na shaka na kujisalimisha maishani kibubusa?
- La! hapana siyo hivyo. Kukimbia kunamfanya mtu akaishi maisha magumu zaidi hata akijidhihirisha kinyume chake. Hebu angalia hapa mtu wa kwanza ana njaa kisha anasema ana njaa na wa pili ana njaa akipiga miayo lakini anasema anataka kulala!
- Hahaha, wote wawili wana njaa!
- Wa kwanza ana akili na mwerevu anajua mwili wake unahitaji nini na anaweza kuishi na nafsi yake.
- Niambie kwa ukweli kabisa hivi wewe una furaha?
- Hahahaha! unataka jawabu kwa wepesi huu? Naam. Furaha ni muono wa nafsi zetu na maisha yetu na ulimwengu na maumbile yake kwetu katika nafsi zetu.
- Naogopa usije ukawa una furaha kama alivyo mke wangu ambaye ni mchaMungu kama wewe ulivyo ambayo (kwa maelezo yako) anayakimbia majibu kwa

kukesha na kunywa!. Kisha akakaa kimya kidogo, akaendelea kwa kusema: nini maana ya maisha uonavyo wewe?

- Mtu anaye kwepa maswali ya msingi hawezi kujihisi kuwa na furaha kamwe hata akiwa mtu wa dini kama asemavyo yeye. Ama swali juu ya maana ya maishajibu lake ni mrejesho wa upangaji wa maswali matatu: Kwa nini tumeumbwa? Kwa nini tunaishi? Ni wapi tunakoelekea?
- Nini jawabu la maswali hayo?
- Hivi wadhani kuwa yupo mtu anaye hisi na kuonja raha ya furaha anaishi kwa furaha lakini hajui majibu ya maswali haya!
- Ni jibu kwa uwazi. Je unafahamu majibu ya maswali haya?
- Mimi nadhani nina majibu ya wazi na yenye kukinaisha kwangu. Lakini siyo majibu ya kukuorodheshe wewe mawazo. Wewe unajua sana zaidi yangu juu ya mambo haya. Mimi ndio kwanza bado mwanafunzi katika Chuo Kikuu ninasoma mambo ya dini mbali mbali. Lakini wewe ni mhandisi mkubwa. Halafu majibu ya maswali hayo yanatokana na vile roho zetu na maisha yetu zinavyotoa majibu hayo. Hata kama ningelikuambia jibu, je lingekuwa na maana yoyote kama siyo sehemu ya roho yako na fikra zako?
- Ah! wewe unanikumbusha kikongwe mmoja nilikutana naye njiani. Alikuwa anasema kuwa ana furaha na akaniambia hayo unayosema sasa.
- Je, unakusudia kuwa mimi ni mwenye busara kama azungumzavyo mtu aliyepata uzoefu mkubwa wa maisha na akafahamu, au unadhani kuwa mimi ni mtu ninayecheza na falsafa ya maneno matupu yasiyo na maana. Kwa namna yoyote ile majibu ya maswali yanatokana na azima yako binafsi.
- Hayo ndiyo maneno ya yule kikongwe! niazimie nini?
- Azimia kupata majibu ya maswali haya kutoka katika nafsi yako ili uwe na furaha maishani mwako kisha akamkazia macho Joji: hebu nikuuliza swali: hivi unafikiri wapi tunaweza kupata majibu hayo?
- Ah! sasa umehamia kule alikojikita dokta, hivi sasa hapo ulipo ni kama dokta!

Kicheko kikamtoka Adam, na akaendelea na maneno yake:

- Hahahaha! wewe mbona unachanganya mambo hivi? Dokta gani huyo unayemsema? au yule kikongwe alikuwa ni dokta?.
- Ah! samahani Ah! inaonekana kuwa nimechoka. Hapana huyo ni Kikongwe,

www.path-2-happiness.com

Mimi naenda kutibiwa kwa dokta kwa lengo la kupata furaha. Haya maswali miye yamenichosha na hivi nimo katika hali ya kusumbuka na masikitiko.

- Maswali hayo yamefikia kiasi cha kukutia masikitiko na kukosa raha kiasi cha kutafuta dokta? Nakuhakikishia kuwa hutopata jibu nje ya nafsi yako na maisha yako. Kwa ujumla nini maneno yanayofanana na ya dokta?
- Alisema: Kabla ya kuanza kutafuta majibu lazima tujue hayo majibu yatatoka wapi?
- Kwa mwangalio wangu hii mimi naona kuwa ni njia sahihi na nyepesi. Na jambo likifanywa kwa wepesi huwa ndio ufunguo wa ufumbuzi wake na mwanzo wa kuelekea kwenye uhakika wa mambo. Ama kuyafanya mambo magumu ni dalili ya kushindwa, tabu na kuchoka, inaonekana dokta wako ni mweledi wa mambo na ni mzuri. Je, ndivyo alivyo?
- Kwa ueledi wa mambo na kutumia mantiki ni sawa, lakini kwa uzuri sidhani hivyo, ni mtu ambaye hafurahishi na inaonekana kuwa huyo bwana hana tabia nzuri.
- Utafanya nini?
- Sijui, nafikiria kuendelea naye hadi nipate matokeo yake, hata hivyo nijibu: hivi majibu tutayapata wapi?
- Samahani, sitaki kupingana na daktari, daktari amekwambia nini?

Joji alicheka kwa jibu la Adam, pamoja na kuhisi kuwa anamsukuma kutoa majibu, joji alikuwa akifurahi kwa namna Adam anavyozungumza na kukwepa mtego wake hataki kutoa majibu, ndivyo inavyoonesha, lakini kwa nini hivyo?

- Aliniambia: tafuta majibu mwenyewe, na akaniuliza kuhusu: majibu tutatoa wapi? Nini dhamana ya usahihi wa majibu yenyewe?
- Mwanzo mzuri, unavutia na mwepesi na wa ndani kabisa, hata hivyo mimi siyo dokta wa kusema hayo ndiyo au kupinga hilo na kuweka sawa rai ya dokta.
- Wapi tutapata majibu haya?
- Tafuta katika roho yako pale unaposoma madhehebu na dini mbali mbali.
- Katika madhehebu na dini mbali mbali!!
- Naam katika madhehebu; na kama sio katika madhehebu na dini mbali mbali, je, wataka tutafute katika upagani?!

- Kiasi gani nachukia upagani! Ni kuchanganyikiwa kwa akili na elimu.
- Kama ni hivyo hatuna budi kutafuta katika madhehebu na dini mbali mbali.
- Kuna uwezekano wa kusafiri kwenda India, penye fikra mbali mbali na dini mbali mbali, je, unadhani kwenda huko kutanisaidia kupata njia mbali mbali?
- Mimi sio daktari kukuambia sawa au la, inafaa kumuuliza daktari, hata hivyo wacha nikuambie rai yangu kwa uwazi kabisa: Ni vizuri kufahamu njia mbali mbali za fikra na dini mbali mbali na madhehebu katika kupata majibu ya maswali haya, kadiri yatakavyokuwa mepesi ndivyo yanavyo karibia ukweli wa mambo.
- Ni fanyeje ili kuweza kutumia madhehebu hizo na fikra tofauti hizo?
- Naona uanze kwa kuangalia mambo kwa ujumla.
- Vipi hivyo?
- Tunaweza tukafuata njia mbili: Njia ya kwanza inayofuata mambo ya dini na nyingine ile ambayo inafuata upagani. Kama tulivyozungumza hapo kabla mimi ni moja ya njia hizo, njia inayofuata mambo ya dini, nadhani nilikuambia kuwa mimi ni mwanafunzi wa masomo ya Kidini?

Akaja mhudumu na vyakula walivyokuwa wameagiza, Joji akawa anataka wakomee hapo ili asimkere mgeni wake! Mgeni ambaye anakaa naye kwa mara ya kwanza, lakini alikuwa amemzoeya sana kama kwamba walikuwa wanafahamiana kwa muda mrefu.

- Sasa sipendi nikusumbue katika kipindi hiki cha chakula. Kwa kweli mimi nahitajia unisaidie, pamoja na kuwa ni hivi karibu tu nimekufahamu ufahamu wa juu juu, lakini hisia yangu navutika sana na mazungumzo yako na nataraji kwa hilo sitokuwa nakusumbua.
- Hahahaha! hunisumbui kabisa, inanitosha mwaliko wako wa chakula na haswa zaidi katika hoteli ya furaha! cha muhimu ule kwanza.

Walipokuwa wanakula, Joji alijaribu kubadilisha mwelekeo wa mazungumzo yao, akaona kuwa wakati umefika wa mazungumzo kuhusu chakula, huenda muelekeo wao wa mazungumzo kuhusu falsafa ukapungua kidogo..hata hivyo muda mrefu haukupita ila mazungumzo yao ya awali yakarudia..kwake Joji ana ufedhuli wa kujua na Adam mjanja wa kukwepa kutoa majibu.

- Kwa nini njia ya dini ni bora kuliko ya upagani? Kwa mnasaba daktari wangu ni

www.path-2-happiness.com

mpagani na anapinga dini zote na kuzidharau.

- Pamoja na kufahamu kutoka kwako kuwa yule daktari ni hodari, ila naamini kuwa wapagani ndio watu wenye dhiki na wenye kukimbia nafsi zao. Ama kwa nini njia ya dini kuliko ile ya upagani? Hili lina vidokezi vingi tunaweza kuvifupisha katika nukta zifuatazo:
- Kwanza: Je, inawezekana kufahamu kwa nini tuliumbwa kuliko anavyofahamu muumba wetu? Kwa njia nyingine ni kuwa si mimi wala wewe kutaka kuelewa kwa nini tuliumbwa ila kutoka kwa muumba mwenyewe. Njia ya upagani inakataa uwepo wa muumba na Mola wa walimwengu.
- Pili: Upagani unajipinga wenyewe katika kila hali ya umbile lake. Unadhani kuwa ulimwengu unakwenda kulingana na vitu vidogo vidogo ambavyo havibadiliki – atom – ambavyo vilitokea ghafla bila mpangilio au muumba.
- Tatu: Hao wapagani wanaficha imani kwa Mungu ndani ya nafsi zao, lakini linadhihiri mara wafikwapo na jambo au msiba, jambo la kwanza watakalosema ni–Ah Mungu wangu!
- Nne: Nakwambia kwa uwazi kabisa hivi upagani ni jambo la ukweli au ni nia yakutaka kukwepa ukweli wa mambo? Hata wakikwepa mazigazi tatizo roho na nafsi zao bado zipo zinawasuta.
- Hoja moja tu hapa inatosha kuvunja upagani! Na je, Kama zitakusanywa zote upagani hautasimama. Nadhani naafikiana nawe, hakuna haja ya kukamilisha. Upagani ni njozi tupu mtu akiufuata anajiona ana maarifa na elimu kubwa lakini ni kazi bure hamna kitu bali ni kupoteza muda na akili tu– huko ni kuweka misingi ya uongo tu – mtu anajiongopea yeye mwenyewe kabla hajaanza kuwaongopea watu. Naongezea hapo sasa tufuate dini gani? Maana dini ziko nyingi wingi wake kama idadi ya watu. Kisha akacheka na akasema: Pengine hizo dini ni nyingi kuliko watu wenyewe!
- Naafikiana nawe kabisa, wanasema idadi ya dini zilizopo ni zaidi ya elfu kumi (10,000) na katika dini moja kama vile Ukristo kuna makundi 33,830, lakini si afadhali tuangalie kwa ujumla wake?
- Ah una maana gani?
- Tumeweka mafungu mawili ya mfumo na njia ya kuendea jambo hili moja la wale wenye kuamini kuwepo muumba na la pili la wapagani au siyo hivyo?

- Bila shaka!
- Basi kwa mwangalio wa jumla dini na imani ni mafungu mawili. Ama kuna dini ambazo ni mfumo ambayo asili yake ni kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu na kuna dini zingine ambazo zimechipuka hapa hapa ardhini ikiwa ni utunzi wa mwanadamu.
- Nimeelewe nini unalenga. Sasa ni aina gani kati ya hiyo ni bora?
- Achana na rai yangu, je hukuniambia kuwa utasafiri kwenda India.
- Naam, sasa safari yangu ina uhusiano gani na mazungumzo yetu?
- Bara Hindi lina utajiri mkubwa wa fikra na dini mbalimbali na madhehebu nyingi zinginezo kutoka ardhini na nyengine za mbinguni. Ukiwa India unaweza kupata fursa ya kulinganisha baina ya dini ya kutoka mbinguni na zile zilizozuliwa hapa ardhini. Utaziona ziko vipi kiuhalisia na siyo kusikia habari za kusifiwa tu ziko vipi.
- Pamoja na kuwa msimamo wangu uko wazi juu ya hilo sioni tatizo kama kuakhirisha mjadala mpaka nitakapo rejea kutoka India. Lakini ninaswali moja: hivi unaamini kuwa kwa utaratibu huu nitaweza kufikia kwenye majibu ya maswali haya!
- Uongofu na mafanikio ni fadhila zake Mwenyezi Mungu. Kama ukiwa mkweli katika utafiti wako nadhani utafikia kilele; la muhimu ni kuwa uwe na utashi na ukweli na weka mwelekeo wako katika hayo, na hakikisha kuwa unachukua mambo kwa wepesi na sio kwa uzito wake, na katika hali ya furaha na siyo katIka hali ya huzuni.
- Umerejea katika maneno ya kikongwe.
- Naweza kumwona wapi kikongwe huyu?. Hakika kanikonga roho yangu.
- Sijui! Kwa hakika sijui. Nilikuwa katika hali mbaya, naye ndiye aliyechukua namba yangu ya simu na kusema atanipigia lakini mimi sikuchukua namba yake. Kwa mnasaba huu je waweza kunipa namba yako na anuani yako ya barua pepe?

Adamu aling'oa kipande cha karatasi kutoka kidaftari kidogo ambacho alikuwa nacho. Aliandika namba ya simu yake na anuani ya barua pepe na anuani ya face book yake na kumpa Joji:

- Niwie radhi, mimi ni mhudumu tu wa mkahawa kama unavyoelewa –sina kadi

www.path-2-happiness.com

yangu binafsi, ningekupa.

- Ah! Hii inatosha kabisa, maana nataka kukuona mara nirudipo kutoka safari ya India je tumekubaliana?

- Tumekubaliana.

SHAKA YA KUSALITIWA



www.path-2-happiness.com

3 SHAKA YA KUSALITIWA

SHAKA YA KUSALITIWA

(1)

Siku hiyo Katarina hakukesha Kanisani kama kawaida yake bali alikaa nyumbani akimsubiri Joji arudi. Si kawaida ya Joji kuchelewa kama leo. Mara Joji alipofika, Katarina alimpokea mlangoni na akamwuliza kwa nini kachelewa. Jicho la Joji likaangukia kwa Katarina, mara akakumbuka uhusiano wake na Tom na mawasiliano yao ya siri lakini akawa muadilifu akajibu swali lake vizuri tu; akaona bora acheleweshe mambo ataeleza mambo kwa utulivu baadaye.

- Nilikwenda kwa mhudumu ambaye nilikuelezea habari zake jana na tukapata chakula cha jioni pamoja.
- Kikao kilikuwaje? Je rai yako kwake iko vile vile?
- Mkutano ulikuwa mzuri; yule bwana ni mwanafunzi wa mambo ya dini, lakini anazungumza kwa lugha nyepesi na ya kukinaisha kabisa, na..
- Inatosha..inatosha, basi, sifa hizo zinatosha jamani. Inaonekana kakukosho roho sana. Hahaha hiyo ni hali ya kawaida kwa mwanafunzi wa mambo ya dini ni lazima awe hivyo. Je kakuambia nini huyo bwana?
- Maneno yake yanafanana na yale ya mzee kikongwe yule niliye kutana naye hapo nilipokuwa nimekusudia kujinyonga. Je wamkumbuka?
- Ndiyo!
- Na maneno hayo yatafanana na yale ya yule mpagani. Dokta Tom. Hili ni jambo la ajabu, maneno ya mtu wa dini kufanana na maneno ya mpagani!?
- Naona unamwita daktari kuwa ni mpagani. Mimi sikudhania kuwa yuko hivyo licha yakuwa nilikaa naye.
- Unakusudia pale tulipokwenda mimi na wewe? Au kuna kikao kingine?
- Joji! ndiyo kikao pale tulipokwenda mimi na wewe. Nilimweleza kuwa shughuli zangu ni kufundisha dini Kanisani lakini hakuniletea maneno ya upinzani wala ubishi. Bali alivutiwa nayo.

www.path-2-happiness.com

- Yule anajisifu kuwa ni mpagani, na hayo waweza kuyaona ndani ya face book yake Joji akamkazia macho mkewe (kisha akasema): Nadhani ana jambo kuhusu maudhui yako ya dini.
- Una maana gani?!!
- Wala! wala hamna kitu, bali ni fikra tu imeibuka kichwani mwangu. La muhimu hapa ni kuwa nitakuwa na safari ya India; Unasemaje?
- Nzuri sana, safari hiyo iko lini?
- Baada ya siku kumi hivi.
- Wewe unajua kuwa mimi nina asili ya India na hasa huko Delhi.. India ni nchi yenye maajabu mengi, Joji, utasahau matatizo yako mengi, na mwishowe utahisi utulivu. Sasa unafanya nini kuhusu miadi yako na daktari?
- Tuna miadi Jumatatu, nitamwomba miadi mingine ipelekwe mbele zaidi mpaka nikirudi.
- Vizuri.

(2)

Tangu Joji afahamu uhusiano kati ya Tom na Katarina alikuwa hapati usingizi, pia alitumia muda mwingi akijutia nafsi yake kimya kimya. Lakini siku ya Jumatano asubuhi akapata wazo kuwa anafumanizi siku hiyo jioni saa mbili usiku kwa kuwa alisikia miadi hiyo ikipangwa kwa simu baina ya Katarina na Tom. Siku hiyo alifanya upesi kupiga simu katika kliniki ya Dk Tom na akamuomba Baraad kumuwekea ahadi ya kukutana na Dk jioni ikiwezekana.

- Leo haiwezekani.
- Kwanini?
- Hahaha, kwa kuwa daktari ana ahadi muhimu sana leo saa mbili usiku.
- Ni muhimu kiasi hiki?
- Huenda ikawa ni hivyo, kilichokuwa muhimu ni kuwa huwezi kutanguliza ahadi uliyokwishaweka kabla, kisha baada ya hapo akacheka kicheko kikubwa.
- Nitakuja saa moja unusu, na akichelewe mgonjwa katika ahadi ya saa mbili basi mimi nitaingia badili yake.
- Hahaha, nimekuambia haiwezekani, na ahadi hiyo aliyokuwa nayo Dokta sio hapa kwenye kliniki…na kwa istihzai akasema: unaonekana una hamu sana ya kuja muda huu, najua unalotaka!! Njoo nitakujulisha yote uyatakayo, na

kukutatulia matatizo yako, kisha akacheka kicheko kikubwa kama cha mwanzo, kisha akaendelea kusema: nitakusubiri na usichelewe.

Muda wa kazi wa Joji ulimalizika na akatoka upesi kumuwahi Adam, suala la Tom na Katarina lilimtia wasiwasi sana, akaona njia nzuri ni kupata ushauri wa Adam katika jambo hili. Alisimamisha gari lake mbele ya mgahawa, na akawa anasubiri kwisha kwa muda wa kazi wa Adam, wakati huo akijiuliza katika nafsi yake kuhusu sababu yake kuwa karibu na Adam na kujihisi furaha kiasi cha kumtaka ushauri wa mambo yake binafsi pamoja ya kuwa si muda mrefu tokea wamefahamiana.

Adam aliliona gari la Joji likisimama, akabadilisha nguo zake za kazi na kutoka mara moja, Joji alipomuona alimtaka apande garini ampeleke nyumbani kwake, Adam alilipokea jambo hilo.

- Adam..ulishawahi kumshuku mtu uliokuwa naye karibu? Aliuliza Joji.
- Hapana, sijawahi lakini ni jambo gumu!
- Je umeoa?
- Hapana.
- Vipi uhusiano wako na wanawake?
- Sina uhusiano wowote na wanawake! Unataka nini na kukusudia Joji?
- Je si nilishakwambia kuwa daktari wangu si mwenye tabia njema?
- Ndiyo.
- Na je sijawahi kukuambia kuwa mke wangu anakunywa sana pombe na kukesha katika mikesha yenye shaka hali ya kuwa ni mwanamke mwenye dini?
- Ndiyo!
- Aah, nimeanza kushuku uhusiano usiokuwa mzuri baina yake na mke wangu, je kwa hilo ni kwa sababu ya kuwa mimi ni mwenye wasiwasi?

Adam alikaa kimya kwa muda akimuangalia Joji mwenye huzuni, kisha akasema:

- Sijui niseme nini, najua huzuni na hisia ulizonazo..lakini asili ya mambo ni kuwa na muamala mzuri na watu na kuwadhania vizuri, na kwa sababu bado hujawa na hakika usifanye haraka kuwatuhumu watu.
- Ana ahadi nae leo ya mkesha!
- Je una hakika na hilo? Kisha ulishawahi kunieleza kuwa anakunywa sana pombe na kukesha, kuna tofauti gani ya kuwa katika mkesha akiwa na Tom au mwengineo?

www.path-2-happiness.com

- Uhusiano wa Tom na wagonjwa wake siku zote ni wa mashaka mashaka, naye si mtu mwenye tabia nzuri, na Katarina hali kadhalika mikesha yake ni ya mashaka mashaka vile vile, kisha mke wangu aliamua kunificha kuhusu uhusiano huu na …maneno ya Baraad yalikuwa ya kushangaza sana!
- Baraad huyu ni nani?
- Huyu ni sekretari wa Tom, ni mtu asiyependeza kwa tabia vile vile, na huwa anagundua vitu vya ajabu kabisa na vyenye kuchukiza.
- Sasa hivi ni saa moja usiku, kwa nini usimpigie simu Katarina na kumualika chakula cha usiku katika hoteli ya kifahari.
- Nitajaribu hilo!

Joji alimpiga Katarina, na akajaribu kuficha sauti yake yenye mkwaruzo wa hisia kali, na akamuomba Katarina na kumshawishi chakula katika hoteli ya kifahari kama alivyotoa ushauri Adam. Katarina aliomba samahani na akamtaka wafanye siku nyingine na kutoa sababu ya kuwepo hafla kanisani ambayo hawezi kuikosa.

- Unaona, amekataa kwa kisingizio cha hafla kanisani!
- Kumbe ni hafla kanisani, kwanini sasa unamtuhumu?
- Cha kusikitisha ni kuwa fedheha za hafla za kanisa ni nyingi. Hutoa harufu yake.
- Huenda ikawa ni hivyo lakini sijui!

Joji alifika nyumbani kwa Adam, alimshukuru kwa wema wake na kwa msaada wake na kuwa pamoja naye.

- Sijui ni kwa nini ninakukera kwa mambo binafsi! Naomba upokee samahani yangu.
- Usiombe msamaha, natamani kama naweza kukusaidia lolote, tutaonana wakati mwingine…hata hivyo ninapenda kukuambia kitu: tahadhari na Baraad uliyenihadithia mambo yake, usimuache akuchezee, mara nyingi tunakuwa katika hali ya udhaifu pindi shaka inapotutamalaki.
- Kwa kweli nimechoka na ni bora nikapata ufumbuzi kabla ya saa mbili kufika! haya tutaonana.

(3)

Simu ya Joji ililia …mpigaji alikuwa ni Baraad, Joji hakuwa tayari na katika hali isiyomruhusu kupokea maelezo yenye kuchukiza kutoka kwake. Hata hivyo kulia kwingi kwa simu kulimfanya kuipokea na kumjibu na kuona anachokitaka kutoka kwake.

- Hallo..uko wapi? nakusubiri, Tom ameshakwenda katika ahadi yake muhimu!
- Kaenda wapi?
- Katika ahadi yake, unataka kujua nini?
-
- Nimechoka!
- Hahaha, njoo, nina utatuzi wa matatizo yako.
- Una utatuzi? vizuri nitafika mara moja.

Joji alifika kwenye kliniki, alimkuta Baraad akimsubiri, akaanza kuongea nae kwa lugha ya hasira.

- Yuko wapi Tom?
- Ametoka muda si mrefu.
- Pamoja na nani?
- Wewe unajua, karibu tukae katika ofisi ya Tom!
- Mimi sijui lolote, unataka nini kwangu?
- Tom ametoka na Katarina.
- Nini kinanipa dhamana kwamba hudanganyi!
- Mimi sidanganyi!

Joji alijikuna kichwani, hajui la kufanya, kisha akanyanyua kichwa chake ghafla na kukodolea mkoba wa kike uliokuwa juu mezani, mkoba ulifanana na wa Katarina, akamgeukia Baraad na kufoka:

- Ni nini hiki?
- Hahaha, je inawezekana Katarina kasahau mkoba wake?! Hii ni dalili ya ukweli niliousema kwako.
- Wamekwenda wapi?
- Wana mkesha…nadhani kanisani.
- Lakini Tom hana dini..
- Kwa nini usiende pamoja nao? Kwa kuwa wana jambo lao haliwezi kufanyika kwa kuwepo kwako? Akacheka kwa sauti kubwa…kisha akaendelea: ewe rafiki yangu najua hisia uliyonayo, nina kitu kitakachokusaidia katika msongo wako

www.path-2-happiness.com

huu wa nafsi.

- Ni nini hicho?
- Kidonge kimoja cha furaha, nadhani ulishasikia kuhusu heroin, hata hivyo naamini kuwa hujui kiwango cha furaha anachohisi mtumiaji wake, kidonge kimoja tu kitakupa furaha unayoitafuta, je utahitaji?
- Kidonge kimoja tu!

Baraad alihisi kusalimu amri kwa Joji, alimuomba amsubirie kwa dakika chache, ili amletee kidonge cha furaha. Alipoondoka aliahidi kuwa hatachelewe kurudi, wakati huo Joji bado alikuwa katika hali ya msongo wa nafsi, mara alipoondoka Baraad alihisi kuwa huru. Alitoa simu yake na akaangalia simu ya mwisho aliyoipiga na akaona namba ya Baraad, Katarina na Adam, kisha akampigia Adam papo hapo.

- Ndio Joji.
- Nimethibitisha lile nililokuambia.
- Chukulia mambo kwa wepesi wake, hata ukithibitisha kutoka kwao pamoja, je hilo lina maana anakusaliti?
- Adam, kwa hakika nimechoka, Baraad ameniacha kwa muda kidogo huenda baada ya muda akaniletea kitakachonituliza kichwa changu.
- Ni kipi hicho kitakachokutuliza?
- Ameniambia ni kidonge cha furaha, kidonge kimoja tu!
- Mihadarati! mwendawazimu nini? Je sikukwambia kuwa watu wanaweza kutuchezea tunapokuwa na shaka na wasiwasi…Joji una nini? huku ni kukimbia matatizo, je unadhani utapata furaha kwa kukimbia matatizo? nakuomba njoo huku mara moja.
- Ole wangu, na huyu bado hajarudi, vizuri, vizuri.

Joji alifika katika nyumba ya Adam, alikuwa katika hali ya kusononeka na kuonewa huruma, Adam alimkaribisha ndani. Nyumba ya Adam ilikuwa ni ndogo, lakini ilikuwa nyumba iliyopangika vizuri, Joji alikaa katika moja ya viti na Adam akamtengenezea kikombe cha chai, Joji baada ya kunywa chai ile akahisi ahueni.

- Unajisikiaje sasa? unaonaje tufanye mazoezi pamoja?
- Mazoezi! huu si wakati wake.
- Mara nyingi natembea au ninakimbia kila siku kiasi cha kilomita tatu hadi tano, na katika siku ambayo sikufanya mazoezi ni leo, njoo Joji jirani na nyumba yangu

pana sehemu nzuri ya kutembea.

- Vizuri.. hamna neno!

Adam alimgeukia Joji wakiwa wanatembea, akawa anamuelezea faida za mazoezi na haswa katika kujenga ari, mara akaona macho ya Joji yakitokwa na machozi.

- Unadhani mazoezi yanaweza kumpa mtu furaha kwa mtu aliyeharibikiwa na kuvunjika moyo kama mimi, nifanye mazoezi huku mke wangu akiwa amekumbatiwa na mtu mwingine?
- Mazoezi humfanya mtu awe na ari, hata hivyo ikiwa peke yake haitoshelezi na haimfurahishi mtu, furaha inatokea ndani mwetu, si sehemu nyingine bali ndani ya mioyo yetu, hailetwi na mazoezi wala mihadarati na vilewesho vingine!
- Kwa hakika nilikuwa katika hali ya udhaifu mno na Baraad akawa ananichezea.
- Tusiwape fursa watu wabaya kutuchezea wakati wa udhaifu wetu!
- Kwa hakika ninahisi kuvunjikwa kwa moyo kwa ndani nami nikiwa natembea nawe nahisi mauti ya roho yangu mara kwa mara.
- Ulikuwa ukifanya nini siku za nyuma inapokujia hali hii ya huzuni kama hii?
- Nimekumbuka, nilikuwa nakunywa kidonge cha kutuliza hali hii nilichopewa na daktari wangu zamani, ingawaje kidonge hicho kinanifanya nihisi usingizi.
- Kidonge kinachotuliza kutoka kwa daktari mtaalamu na sio kutoka kwa jambazi, je vidonge hivi unavyo sasa hivi?
- Ndio, vipo kwenye gari.
- Turudi nyumbani ili uchukue kimoja.
- Nitarudi nyumbani nichukue.
- Kichukue, na leo ulale kwangu.
- Nilale kwako na sijui Katarina yupo wapi?
- Usifanye shaka yako ndio dalili ya kumhukumu, huenda alikuwa na Tom kwa kumshawishi Ukristo!.
- Huenda, lau ningehakikisha hilo, hilo ni jepesi kuliko shaka niliyokuwa nayo.

Joji alilala usingizi mzito tokea kidonge kilipoanza kufanya kazi..aliamka saa nne asubuhi na akamkuta Adam keshamtayarishia chai ya asubuhi…

- Habari za asubuhi, chai tayari.
- Hivi ni saa ngapi?
- Ni saa nne.
- Samahani, nimekucheleweshe kazini, nami nimechelewa kazini kwangu.

www.path2-happiness.com

- Usijali, nimeshaomba ruhusa kazini, nawe ni msaidizi wa mkuu halitokudhuru hilo.

Joji alikunywa chai pamoja na Adam, alimshukuru kwa wema wake kwani alihisi kuwa na utulivu mkubwa na hali ya afadhali kuliko ya jana yake.

- Vizuri, inabidi upate utulivu zaidi, mabadiliko yasiyotarajiwa ni moja katika mambo yanayoondosha furaha ndani ya moyo wa mtu.
- Una maana gani?
- Kwa mfano kama utaweza kujibu maswali ya msingi utaweza kushughulika na matatizo yako katika hali iliyokuwa bora zaidi, hali yako ya ndani itakuwa nzuri katika kushughulika na msongo wa nafsi.
- Una maana kuwa maudhui ya Katarina ni ndogo?
- Hapana, sina maana hiyo, ninachomaanisha ni kuwa furaha iliyo ndani ya nafsi zetu zinaondosha shaka zetu na hutatuwa matatizo madogo madogo tuliyonayo, na hivyo unajimakinisha katika kufikia kwenye furaha na kufikia njia itakayokuwezesha kujibu maswali yako, na wakati huo utaona jinsi gani unavyoweza kuyafasiri maisha zaidi na muono wako kwa ujumla.
- Nakuahidi katika hilo pamoja na kuwa sikufahamu baadhi ya mambo katika mazungumzo yako.
- Maelezo yangu yako wazi, tilia maanani kadhia kubwa zaidi katika maisha yako kwa njia nyepesi na kwa undani zaidi, wakati huo utaona furaha ikitoka katika roho yako na utatatua matatizo yako.
- Huenda ikawa hivyo, asante sana, nimekutaabisha …nitakwenda kazini sasa, na leo nina ahadi na daktari.
- Jitahidi kukaa na Katarina na Tom katika hali ya kawaida, kwani si muda mrefu utasafiri kwenda India, na utakaporudi katika kila mazungumzo kuna tukio lake, na hakikisha kufanya mambo yako kwa wepesi na katika hali ya kawaida na bila kuyakuza, katika hali ya furaha bila ya kuwepo kwa huzuni.
- Nitajaribu.

(4)

Joji aliondoka kwenda kliniki ya dokta Tom katika ahadi yake ya jioni ile, alipoingia tu alikutana na macho makali ya Baraad.

- Umetorokea wapi jana?
- Sikutoroka, nilikuwa nina kazi.
- Kwanini hukunisubiri?
- Mimi nachukia mihadarati, na nachukia kuyakimbia matatizo yangu.
- Mhmh, vizuri. Je umepambana na matatizo yako?
- Nina miadi na Tom, je yupo au niondoke?
- Hahaha..yupo, mimi nina hakika kuwa utahitaji kidonge cha furaha, na utakirudia siku nyingine, karibu daktari anakusubiri, ana hamu ya kukutana na mume wa Katarina!

Joji aliiingia kwa Tom na akamkuta akionekana kuwa ni mchovu, alimkaribisha ndani na akampa chai, kisha akamuomba samahani kuwa alikuwa katika mkesha jana usiku hadi usiku sana; kwa hiyo hajihisi vizuri na amechoka…Joji alishangazwa na maneno ya Tom, mara nyingi madaktari wanatahadharishwa na kukesha, Tom akabadilisha mazungumzo na akionesha kuwa hajali, kisha akamgeukia Joji akimuuliza akitaraji kuwa hajapata majibu ya maswali yake.

- Je umepata majibu ya maswali yangu ya msingi?
- Ndio na hapana.
- Vipi, hebu nibainishie.
- Nina majibu niliyokinaika nayo, lakini si majibu kamili.
- Haya nieleze, majibu tunayapata wapi?
- Jibu: kwanza tuamini maswali mepesi na si mazito yake, na wakati huo tutayapata majibu moja kwa moja na kwa wepesi.
- Njia ya falsafa inajengwa siku zote katika kuyafanya mambo kuwa magumuili tu kuonesha kuwa tuna akili na tunajua mengilakini sio kuyafanya kuwa mepesi.
- Lakini wepesi una kina, na kuweza kujibu maswali kwa undani kabisa, nadhani ni hivyo?!

www.path-2-happiness.com

- Nadhani umeanza kuyafanyia maudhui yetu falsafa…kisha akasema kwa sauti ya kuonesha changamoto: wepesisha swali kama utakavyo, wapi tunaweza kuyapata majibu ya maswali yetu haya?
- Nimechunguza yaliyomo na viumbe, nikaona ya kuwa hatuwezi kuyapata kwa vitu visivyo na uhai wala wanyama..kumebakia nini?
- Hahaha, watu!

Joji alimuangalia kisha akamwambia kwa msisitizo..

- Umesema kweli, kwa watu au kwa Mola wao aliyewaumba.
- Siamini kuwepo kwa muumba wa watu!
- Hawa viumbe wametokea wapi kama hawakuumbwa?!
- Sipendi kuikera nafsi yangu kwa maswali haya, tusema kwa bahati, au kimejiumba chenyewe, tuseme jambo lingine lolote!
- Huku ndiko kukimbia maswali, na huu sio mfumo wa falsafa ewe mwanafalsafa! Mambo yote uliyoyataja hayawezekani na si mantiki; kitu hakiwezi kujiumba na kuiumba akili yake mwenyewe, na haiwezekani kuwa mambo haya yamejitokezea hivi hivi tu kwa umakini huu tunaouona. Sina zaidi ya hapo, kisha Joji akaamka kwenye kiti alichokalia, na akaendelea kusema: Nitafuata njia yako, na tutaona tutafika wapi, tuyaweke maswali yetu hadi yatufikishe katika ukweli hata ikiwa hatukinaishwi nayo hapo mwanzoni.
- Hukujibu maswali yangu..majibu ya maswali yetu tutayapata wapi?
- Ni nani aliyeumba watu; kwa sababu yeye ndiye anayewajua kuliko wanavyojijua.

Tom alikaa kimya muda mrefu, kisha akanyanyua kichwa chake na kusema:

- Maneno yako yananifurahisha pamoja na kutofautiana nawe, sitojadiliana nawe kwa uliyosema, lakini nitaendelea kukuuliza maswali ambayo yatabainisha makosa yako, tujaalie kuwa uliyoyasema ni sahihi..Je huyo Mola wa watu ambaye atatujibu ni Mola wa Budha au Jua, au Masiya au roho mtakatifu au…? miungu ya watu ni mingi na hubadilika mara kwa mara; tutawezaje kujua mungu wa haki kutokana na miungu yote hiyo? Je hujui kuwa dini ni nyingi mno?!
- Najua, zipo zaidi ya dini kumi elfu (10,000), Ukristo ni dini na ni dini moja yenye zaidi ya makundi 33,830.
- Mimi nipo mbele ya mtu mwenye kufanya mjadala, mwenye maarifa mengi na mtu msomi, nitazingatia kuwa jibu lako ni sahihi, hebu tukamilishe: ni nini

dhamana ya kuwa jibu hilo ni sahihi?

- Uwepesi wake: Iwe ni nyepesi au rahisi na isiwe ngumu, ituletee furaha, isigongane na akili na mantiki au elimu au kugongana na nafsi zetu kwa ndani, na kuenea katika maeneo yote ya maisha yetu.
- Jibu sahihi, jepesi na makini..ina maana jibu lolote linaloelekea kuwa kweli, lakini halituletei furaha au kwenda kinyume na akili au mantiki, au kuwa gumu, au halienei katika maisha yote ya mwanadamu hatulikubali!
- Naam..bila shaka!
- Vizuri, ukipata jibu hili mimi nipo pamoja nawe, kisha alitabasamu na akasema: nitakupa maswali mapya, na utabaini ukweli wa majibu yetu na usahihi wa njia yetu na makosa yake …kisha akatabasamu na kusema: pamoja na kuafikiana nawe kuhusu dalili potofu wanazoamini wakana dini na kumkana Mwenyezi Mungu, ila naendelea kuamini kuwa hakuna Mungu..kwa jumla tutapita katika njia hatuijui itatufikisha wapi, swali langu kwako: ni Mungu gani huyo tutakayechukua majibu kutoka kwake? na katika njia ya dini gani?
- Turahisishe maudhui yetu: kuna makundi mawili ya dini na fikra za watu zinapotoka, dini za mbinguni na dini za ardhini, je wewe unauliza kuhusu lipi katika hayo?
- Umesema kweli..dini ni nyingi, ni vizuri kurahisisha mambo kwa kugawa katika makundi makubwa, kwa hakika sikufikiria hilo, wewe utasafiri kuelekea India hebu tubadilishe swali kwa: Ni dini ipi iliyo bora: dini za ardhini za watu au za mbinguni? Na baada ya kila jibu tutaingia katika vipengele vyake kulingana na majibu yako katika ahadi yetu baada ya wiki mbili, nadhani utaona dini zilivyo huko India na kitakupelekea pale nilipo kwenye ukanaji na kujitenga na dini zote.
- Nitasafiri kwenda India! umejuaje?

Tom alibabaika, akitaka kitu cha kumtoa katika mtego huo, hakuweza!

- Nimejua kutoka kwa…nimejua kutoka kwa Katarina..nilimuona kwa bahati kanisani.
- Vizuri kwa mkanaji dini anayepinga Mungu kwenda kanisani!
- Nimekwenda kanisani kusoma tabia za watu wenye kuabudu, na sio kufanya ibada.
- Mhmh, umemuonaje Katarina.

www.path-2-happiness.com

- Mwanamke mwenye akili, mfanya ibada. Bado fikra za mashariki zikiwa zimemtawala kwa roho yake na umbile lake.
- Inaonesha umevutiwa nae.
- Kwa kweli nimevutiwa na kuabudu kwake na yakini aliyokuwa nayo, nakupongeza, anakupenda sana.
- Mkanaji dini anapenda waamini? jambo la ajabu kabisa!
- Huenda ikawa hivyo, kisha akajaribu kubadilisha maudhui: hushibishwi na uzuri wa Wahindi na sasa unataka kusafiri kwenda India?
- Sifahamu unalosema?
- Haikutoshi uzuri wa Katarina, unakwenda sasa kutafuta starehe na wahindi wengine wazuri! na kucheza nao?!
- Achana na hili..mimi nitasafiri kujua hizo dini na mifumo ya maisha, kadhalika kuingia katika mikataba ya kazi, kwa heri, ahadi yetu ni baada ya wiki mbili.
- Tumeafikiana, nina hakika utaachana na kila dini utakayojaribu kuwa nayo karibu, nakutakia kila la kheri na faida na starehe za huko India.

(5)

Katarina alimpokea Joji mlangoni, na alipohisi kufika kwake alisimama upesi upesi..akamkaribisha, akamjibu kwa hali ya kupooza na kwa sauti ya chini isiyo na furaha…akajaribu kumbembeleza..

- Umenipa wasiwasi, ulikuwa wapi jana, hukulala nyumbani?!
- Wewe hukurudi jana isipokuwa usiku sana, inakuhusu nini mimi kulala nyumbani au nje.
- Ndio, jana tulichelewa kanisani, hafla ilikuwa ni muhimu na nzuri kabisa.
- Bila shaka ilikuwa nzuri kwa kuwepo kwake.
- Unamkusudia nani?
- Ulikuwa na nani katika hafla?
- Wengi, wengi tu.
- Ni nani katika waliohudhuria ninaowafahamu?
- Joji, haya ni maswali ya uchunguzi? hata hivyo nitakujibu: Padri Morris, Sali,

Peter, Hillary, Simpson na…

- Tom mtanashati!
- Naam…! na daktari Tom alikuwepo, alikuja kuzidisha imani na yakini kwa Bwana wake na alihudhuria misa yote pamoja nasi!.
- Vizuri sana..mkanaji Mungu anahudhuria misa, au anafurahia kunywa, kucheza na mkesha?
- Wewe unanidharau na kulidharau kanisa, una maana gani? na ni nani aliyekuambia amehudhuria mkesha? nakusudia?
- Hapana, sikudharau wala kulidharau kanisa, yeye ndiye aliyeniambia kuwa alifurahia mkesha pamoja na Katarina mzuri anayepagawisha watu, na Tom ambaye anataka kuzidisha imani yake ndiye aliyenihamasisha kwenda India nikastarehe na uzuri wa wanawake wa Kihindi na kucheza nao!
- Yeye ndiye aliyesema hivyo!
- Ndio, nini kigeni kuhusu hilo?
- Hakuna! lakini…
- Mimi nimechoka na nataka kulala, samahani nakwenda kulala chumbani.

Asubuhi Joji aliamka mapema kwenda kazini, akamkuta Kakhi akimsubiri..

- Nipe habari nzuri, umeamua nini Joji?
- Nitakwenda India mwisho wa wiki tukimaliza mapatano ya kazi baina yetu, nimeshapanga mambo yangu.
- Vizuri sana, tutahitaji vikao virefu vya mara kwa mara; ili kuweza kujua vipengele vya mkataba inayotakiwa, kadhalika kujua hali za watu kule.
- Baada ya saa nitakuwa kwako tuanze vikao vyetu leo kwa muda wa saa tatu na kesho kwa muda huo huo.

Kakhi alikuwa anachunga na kujali maslahi ya faida itakayopatikana kwa kuingia mikataba na mashirika ya huko India; kwa hivyo basi aliona kuna umuhimu mkubwa wa kumueleza tabia za watu huko ambao watakutana na Joji, hakuacha dogo wala kubwa analolijua ila alimwambia Joji.

- Je una maelezo mengine yoyote unataka kujua?
- Hapana, sina, mambo yamenifungukia zaidi, pamoja na kuwa mshikamano ambao msingi wa faida unasimamia hautoshi bali ule uliosimama katika maslahi

www.path-2-happiness.com

ya pande mbili zaidi ndio utakaodumu zaidi na wenye nguvu zaidi.

- Kuhusu faida ni kupata zaidi na kwa matumizi madogo…kisha akatabasamu, mimi nahitaji faida ya mali zaidi na wewe utapata faida zingine zinazotokana na misingi imara ya kihisia.
- Tumeafikiana!!
- Nimesahau kukujulisha ule mshangao wangu niliokusudia.
- Mshangazo gani?
- Je unakumbuka kuwa nilikwambia kuwa nitakushtukiza na jambo ambalo litakusahaulisha maswali yako, na yatakusahaulisha daktari wako pia.
- Ni lipi hilo?
- Jaribu starehe za India.
- Unakusudia starehe gani?
- Mbona wewe mpumbavu wakati mwingine, jaribu wanawake wa India, na watakujibia kila swali utakalouliza…Maiko atakutayarishia kila kitu. Maiko ni Mkuu wa Shirika la Ajira nililokuelezea..kisha akacheka kicheko chenye kuonesha dharau ndani yake, na akasema: Je sijakwambia kuwa yeye ni Mkristo mwenye dini tena sana.

Joji alijiuliza ni nini sababu ya kufanana kwa Tom na Kakhi! Na ni kufanana kwao kwa kupenda mali na ile hali ya ukanaji dini? Au ni ule ukweli ambao anaukimbia?...Ah kwa hakika ukweli huu unababaisha!! Hata hivyo nimekusudia kuufikia..

- Jumatano asubuhi ndio safari yangu, je unataka chochote kwangu?
- Safari njema, na nakutakia ufanikiwe uingie katika mikataba yenye faida ya kimali na maslahi zaidi na sio misingi ya kimaadili, na nakutakia starehe na wanawake wazuri.

Joji aliliona sana suala la tamaa na fikra za utajiri kwa mkuu wake wa kazi Kakhi, na haswa zaidi katika vikao vyake nae walipokuwa wakizungumza safari yake kwenda India. Katika vikao vile Kakhi alimuusia sana wauze programu zao huko India na ajitahidi kupata wafanyakazi wataalamu watakaotumika kwa gharama nafuu zaidi, India ina soko kubwa kwa idadi yake kubwa ya watu, na katika yenye kulitofautisha soko hili na soko lingine ni kuwepo kwake wafanyakazi rahisi. Joji mara kwa mara alikuwa akisikiliza akiwa kimya na

hakutaka kuingiza maneno yake katika maneno ya Kakhi yasiyofahamu katika maisha zaidi ya mali na wanawake na maneno yake yote yanatembea humo.

Kakhi alimwambia Joji kuwa Maiko ndiye atakayempokea uwanja wa ndege na kumuonya na uamini wake, kisha akaendelea kusema:

- Haituhusu anakuwa nani, madamu anatupa fursa ya kuingia katika mikataba na kubadilika…na kwa kicheko cha kubeua aliendelea kusema: huku ndiko kuamini kwa kutumia akili, atakayenifurahisha zaidi basi nipo tayari kumtumikia na kumuabudu.

Alisimama ili aondoke, Kakhi alimkonyeza Joji na akamwambia kuhusu usia wake wa mwisho kwake: Usikose kustarehe na uzuri wa India; ni uzuri wa kipekee, Joji akamjibu kwa kumpuuza:

- Unakusudia uzuri gani?
- Uzuri wa wanawake wa Kihindi na michezo yao ya kimashariki.

Joji alichezesha midomo yake kwa hasira, akaaga na kuondoka mara moja.

Joji alirejea nyumbani kwake akiwa amechoka, akamkuta Katarina akimsubiri katika isiyokuwa ada yake, leo hakukesha kama ilivyo ada yake.. alimkabili kwa tabasamu na kumbembeleza.

- Mpenzi wangu umechelewa, nimekusubiri masaa mawili?!
- Nilikuwa na vikao virefu pamoja na Kakhi kuhusu safari yangu.
- Kweli! nimesahau, hukuniambia kikao chako jana na daktari Tom kilikuaje?
- Nilimjibu kwa yale majibu ya yule mhudumu! nilikinaishwa nayo na kadhalika naye alikinai na majibu yale.
- Vizuri sana..la muhimu ni kuwa mnakwenda sawa.
- Amenipa pia maswali mapya!
- Maswali gani hayo mapya?
- Nimwambie ni dini gani iliyo bora zaidi ambayo tutaweza kuchukua ndani yake, na Mungu yupi ambaye atatupa majibu yetu.
- Majibu yako wazi. Mungu, na masiya na roho mtakatifu, hawa watatu ni mmoja wao ndie aliyemuumba mwanadamu, na anayesema kinyume na hivyo basi amekana..kisha akaanza kucheka.
- Ameninasihi kuangalia dini wakati nikiwa India. Kisha baada ya hapo nimwambie

www.path-2-happiness.com

ni dini gani sahihi za mbinguni au ardhini (za wanadamu)?

- Safiri na utaona India maajabu yake usiyoweza kutarajia; ni nchi ya maajabu, na utarejea ukikiri maneno yangu.
- Na vipi kuhusu usia wa Tom wa kustarehe na wanawake wa India?!

Katarina alijaribu kuficha wasiwasi wake.

- Usimtii katika hilo, mpenzi wangu.
- Je unanishuku?

Katarina alitabasamu, na akapata nafasi ya kubadilisha maudhui.. akanyanyua kichwa chake na akamuangalia Joji..

- Asili yangu ni India na pamoja na hayo sikuiona India kwa zaidi ya miaka ishirini, je unaweza kuniletea zawadi kutoka India?
- Kwa furaha kabisa…unataka nini?
- Nataka msalaba uliotengenezwa kwa mkono.
- Nitakuletea msalaba uliokuwa bora kutoka India, lakini nina sharti dogo.
- Karibu, sema.
- Nataka usiku huu wa leo uwe usiku bora zaidi kwetu..haya twende tukalale.

India... Nchi ya Maajabu



www.path-2-happiness.com

4

India... Nchi ya Maajabu

India... Nchi ya Maajabu

(1)

Akiwa uwanja wa ndege baada ya Joji kumaliza kukaguliwa pasipoti yake na kuingia alimkuta Maiko akimsubiri, aliweza kumfahamu pindi alipomuona kwani alishatuma picha yake katika barua pepe. Maiko alimkaribisha Joji kwa shauku na akamuuliza kama angependa kwenda hotelini, au amchukue katika matembezi ya kuona mji.

- Nakushukuru, hata hivyo nipeleke hotelini, nimechoka safarini, suala la matembezi tulifanye kesho asubuhi kabla ya kwenda ofisini.

Joji alimuona Maiko kuwa ni mtu mtanashati mno na hutangamana na watu kwa hali ya juu kabisa. Joji alichukuliwa na gari la kifahari linalothibitisha kabisa kuwa mwenye gari hilo ni tajiri katika nchi yenye ufukara wa hali ya juu.

Katika siku iliyofuata, kwenye milango ya saa moja asubuhi, Joji alishuka toka chumbani kwake katika hali ya uchangamfu kabisa. Usiku uliopita alilala kwa muda wa kutosha, alimkuta Maiko akiwa mapokezi anamsubiri, ni kama vile alivyomuona jana, mtanashati ambao unamvuta mtu wa pili kumwangalia. Joji alimsalimu Maiko na wakaondoka pamoja kuelekea kwenye gari.

- Unaonaje tufanye matembezi kwa muda wa saa moja, kisha baada ya hapo tutakuwa tumefika ofisini saa mbili na nusu?.
- Vizuri, ningependa kuijua India.

Muda wote wakiwa njiani Maiko alikuwa akimuelezea Joji kuhusu majumba aliyoyaona na makanisa kwa kujifaharisha kuwa India ni nchi yenye historia kubwa, ila Joji aliona kuwa Maiko hapendi kuzungumzia baadhi ya majumba makubwa pamoja na Joji kumuuliza. Kadhalika alikuwa hapendi kuzungumzia masanamu ya budha yaliopo kila mahali. Maswali mfano wa hayo mara nyingi aliuliza na Maiko alikuwa akimhadaa katika majibu mara kwa mara, kana kwamba anataka kusema kuwa nchi ya India ni nchi ya Kikristu peke yake. Joji alitosheka kwa kuuona mji na hakuongeza chochote katika ziara hiyo, akakumbuka maelezo ya Kakhi kuwa Maiko ni mtu mkatoliki mwenye siasa

www.path-2-happiness.com

kali.

Saa mbili na nusu Joji na Maiko waliwasili ofisini, walikaa hapo hadi saa tano wakizungumzia masuala ya kazi, miradi na mikataba, kwa hakika Maiko alihisi hali ya utulivu mkubwa kuwa na Joji, alinyanyua kichwa chake ghafla na akasema:

- Wewe ni mkristo kama mimi, kwanini tunamwachia Kakhi Myahudi kucheza na mikataba ya wafanyakazi wote, unaonaje mchezo uwe katika mikataba ya wahindu, mabudha na waislamu tu, na tukashurutisha kuwa mikataba ya wakristo kuwa bora zaidi, sitaki myahudi huyu kutuibia!
- Je, ni uadilifu kumuibia Mhindu, Mbudha na Muislamu?!

Maiko alifedheheka na kukaa kimya..na wakaendelea na kazi zao hadi saa moja, hapa Joji aliomba wapumzike kwani alishachoka.

Njiani wakielekea hotelini walirejea katika njia ile waliojia, na pindi Joji alipoona jumba kubwa alitaka kumuuliza Maiko kwa mara nyingine:

- Ni nani aliyejenga jumba hili lenye kuvutia?
- Waislamu …wabakaji.
- Na hii ni nini?
- Hekalu la Mabudha mataahira…wanaabudu mawe na watu mfano wetu.

Baada ya Joji kuhisi hali ya wasiwasi aliokuwa nao Maiko kwa maswali aliyomuuliza aliamua kunyamaza muda wote wakiwa njiani..

(2)

Joji aliafikiana na Maiko kuwa ampitie saa kumi; ili wapate kwenda kwenye chakula cha mchana pamoja, kwani alimuandalia hafla ndogo ya kumkaribisha, pindi alipotoka chumbani kwake kwenda chini na baada ya kupanda gari Maiko alimuuliza Joji:

- Kuna ada na desturi anayoitaka Kakhi mara anapotujia, sikuona ukiulizia!
- Ni lipi hilo?
- Tuakhirishe jibu hadi tutakapofika hotelini, nadhani utafurahishwa na maandalizi yenyewe!

Walifika hoteli ya Taj India, hoteli ilikuwa inaonesha kila ufakhari katika kila kona yake. Joji alipendezwa na sehemu yenyewe na uzuri wake. Alivutiwa kwani ilikuwa ya kiasili kabisa na akavutiwa na udi uliokuwepo pamoja na kwamba hapendi harufu za udi. Maiko kuona vile alitabasamu akamwambia

mbawa zake mahususi zitakuwa nzuri zaidi.

Katika mbawa moja maalum hapo hotelini, Joji aliwaona wasichana wawili wazuri na umri wao unakaribia miaka ishirini, walikuwa wakiwasubiri wao na pindi walipowaona walitabasamu, alipeana nao mikono huku wakitabasamu, Maiko akamkonyeza Joji na kumpiga piga mabegani:

- Unaonaje mazingira haya?
- Nzuri sana.
- Kila mara anapokuja Kakhi namleta hapa kwa ajili ya chakula cha mchana, kisha anawachukua wasichana wote au mmoja wao anakwenda nao hotelini, na kumalizia usiku mwanana.

Joji hakuonesha furaha na alijibu kwa upole kabisa:

- Kweli mazingira ya kuvutia, ama kwa upande wangu ni uzuri wa mahali hapa tu.
- Ajabu, hukuvutikwa na hawa wasichana wawili?!
- Kweli wao ni wazuri bila shaka, cha kushangaza ni wewe! Mimi sio Kakhi!
- Una maana gani?
- Unadhani anachokifanya Kakhi ni jambo zuri nifanye mfano wake?
- Kakhi hafungi mikataba ila kwa njia hii!
- Hiyo ni rushwa kwangu ili nisaini mikataba!
- Samahani, unataka nini?
-
- Mimi ni mtu niliyeoa, sitaki kumsaliti mke wangu, je Maiko haya siyo mafundisho ya Ukristo?!
- Ndiyo..ndiyo!

Alikuja mhudumu na menyu na akampa Maiko, akazungumza nao kihindi akaondoka pamoja na wale wasichana wawili, kisha akamgeukia Joji kwa tabasamu bandia:

- Je nikuagizie au utaagiza mwenyewe?
- Nichagulie, wewe unajua zaidi.

Joji alitaka kubadili hali ya kikao kile, akakumbuka kuwa Katarina alimtuma zawadi na alimkumbusha mara kwa mara, alisema zawadi ile inamkumbusha ushindi wa wakristo kuwashinda Waislamu washenzi huko India, kisha baada ya hapo India kugawika kwa Pakistani na Bangladeshi; na hivyo kumwambia Maiko:

- Wewe unawajua watengenezaji wazuri wa msalaba, je unaweza kunielekeza

www.path-2-happiness.com

sehemu nikanunue kwa ajili ya mke wangu?

- Watakuletea chumbani kwako..kisha akakumbuka: nitakujulisha bei yake, sio rushwa!
- Unajua, pamoja na kuwa mimi ni mkristo mprotestanti ila ni kuwa sijui ukristo, nadhani wewe ni muamini mzuri, je, unaweza kunikinaisha na dini yangu?
- Ukristo ni dini ya mbinguni, imetoka kwa Mungu muumba, sio kama dini za ardhini walizotunga wanadamu.
- Una maana dini gani hizo?
- Dini kama vile Ubudha, Uhindu, Umajusi na nyinginezo, hapa India kuna mamia ya dini kama hizo.

Joji alikumbuka mazungumzo yake na Adam, akapendelea aendelee kumuuliza Maiko maswali, ili apate mtazamo wake kuhusu dini, na vipi anafasiri kuwepo kwake.

- Ni nani anayethibitisha kuwa ukristo ni dini ya mbinguni na sio ya ardhini?
- Historia inathibitisha hilo pamoja na mapokezi ya ushuhuda mbali mbali, ukimuuliza Mhindu atakuambia kuwa ukristo ni dini ya mbinguni na dini yake ni ya watu na inaendelezwa na watu…
- Nadhani katika hali ya kawaida kabisa ni kuwa dini za mbinguni ni bora kuliko dini za ardhini.
- Vizuri sana, neno kawaida, ni maelezo mazuri hayo! Ndio hilo ni sahihi zaidi, je kuna shaka katika jambo hilo?!
- Haya ni maneno ya wakristu wote, hata hivyo katika hali ya kawaida ningependa kulihakikisha mwenyewe na ikiwezekana kuona.

Baada ya siku kupita, siku iliyokuwa na matukio mengi, Joji alielekea hotelini, na pindi alipojilaza kitandani, akawa anarejea yale yote yaliyopita, hakujihisi ila pale alipokuwa akilirejea jina la Adam: "Hakikisha kuwa unarahisisha mambo bila mafumbo, huku ukiwa na furaha bila huzuni".

Alifungua Televisheni na akakuta kipindi kwa lugha ya Kihindi ikiwa na tarjumi kwa lugha ya kiingereza, kipindi kile kilikuwa kinazungumzia Uhindu, mafundisho yake na maadili yake mazuri. Kipindi kile kilikuwa kinahimiza kuwa dini ya Kihindu ni mchanganyiko wa dini ya Aryans ambayo inanasibishwa na kutukuza nguvu za maumbile ya asili, na dini ya Kihindu ya zamani, dini ambayo inahimiza vitu vilivyokuwa vikipendwa na watu wa India wa zamani, na baada ya kupita muda kuna maendeleo yaliyotokea na

kukawepo aina ya muungano, wakaanza kuogopea kuondoka kwa maslahi ya baadhi ya tabakakatika kuandika baadhi ya fikra katika masuala haya, na fikra hizi baadae zikajulikana kama ni Fida na Veda. Veda ni kitabu kitukufu zaidi kwa Wahindu; maana yake ni:Kanuni au hekima, wakawa wanaandika kanuni na hukumu hizi, na muradi wake ni: kuwapa tabaka la Ari au waliokuwa weupe zaidi sifa ya ziada iliyokuwa kinyume na ile ya wale weusi, kanuni hizi zinawapa wachache sifa hizo zikaanzwa kuandikwa, sifa hizo sikazidi na kuwa nyingi, na ikawa ngumu kuzihifadhi kanuni hizi moyoni ni ngumu, hivyo wakasema: 'Zinafaa kuandikwa, wakaanza kuandika, uandishi uliodumu kwa karne kumiyaani miaka mia moja (100)na ikawa ni hali ya kuendelea hadi hapo baraza kuu la makuhani wa Kihindu kuhitimisha kwa azimio kuwa haiwezekani kuongeza kitu katika kitabu hiki. Na kama si kuhitimisha kwa azimio hili basi uandishi wa kitabu ungeendelea na yangeongezwa mengi zaidi. Kitabu hiki ni kikubwa mno lina mijaladi mingi, kipindi kiliendelea kuelezea kuwa yenye kuashiria kuwa dini hii ya Kihindu haifai sehemu nyingine isipokuwa India tu, na kuwa Wahindi walipitisha azimio kuwa wanazuoni wao kuwa kuwa Uhindu ni dini maalum ya Wahindu, na kuwa uhindu ukitoka nje ya India sio Uhindu tena, Joji akacheka kwa dharau kuhusu dini hii yenye kasumba hata kwa sehemu, hata hivyo aliiizuia nafsi yake:

- Kwa hali yoyote hii ni kadhia ya watu, na si kutoka kwa Mungu, hili ni kwa hali ya kawaida tu! kama kwamba naanza kuliona ninalolitafuta, hata hivyo bado halitoshi…

(3)

Saa mbili asubuhi Maiko alikuwa ameshafika katika ahadi yake akimsubiri Joji katika mapokezi. Pindi alipomuona Joji akija mbele yake alitabasamu, alimsalimia kwa lugha ya kusisitiza na kumwambia:

- Leo hii tuna kazi ndefu, leo ni kama jana, Je, upo tayari?
- Bila shaka nipo tayari, ndilo nililojia.

Wakiwa njiani Joji aliona sanamu la aina yake ambalo halifanani na la Budha, akageuza shingo yake na kuliangalia kwa kina, Maiko akamwambia huku akicheka:

- Una nini? Huyu ni mungu miongoni mwa miungu, si nilikuambia kuwa dini za wanadamu kila siku zinatengeneza miungu wapya.

www.path-2-happiness.com

- Nataka kukaa na mtu mwenye kuabudu dini hizi.
- Hahaha, leo hii tutakula chakula cha mchana na mwanamke mkurugenzi wa uendeshaji katika shirika, naye ni Mbudha.

Walifika kwenye shirika wakashughulishwa na kazi walizoendea, Maiko aliona kuwa kuna tofauti kubwa kati ya Joji na Kakhi, Joji alishughulishwa na mambo ya dini na akiulizia mara kwa mara, na ni mwenye kupenda kujua zaidi, ni mtu mwenye misimamo yake anayoiheshimu, tofauti kabisa na Kakhi mpenda mali na wanawake. Walipomaliza kazi zao mnamo saa sita mchana, Maiko alimsogelea Joji na akamwambia kwa sauti ya chini:

- Tukimaliza nataka nikuambie kitu.
- Hamna neno, niambie.
- Wewe hufanani na Kakhi kabisa, pamoja na kuwa mnafanya kazi katika shirika moja.
- Hahaha, unakusudia wale wasichana wa pale hotelini?
- Ndio huyu ni mmoja tu, na kuna wengi mfano wake.
- Vizuri, unadhani ni nini sababu ya tofauti hii kwa mtazamo wako?
- Ni dini bila shaka.
- Na wewe, je si mtu wa dini na unamwendekeza Kakhi?
- Huenda ikawa, lakini si lazima ninachofanya kikawa sawa.

Maiko alisimama ili kuondoka, kisha akamgeukia Joji:

- Je hupendi kukutana na Jiyotsana?
- Ni nani huyo Jiyotsana?
- Ndiye yule mkurugenzi mbudha..Je, unajua maana ya Jiyotsana?
- Hapana, sijui.
- Maana yake ni: mwanga wa mbalamwezi, kisha akatabasamu na kusema: Hahaha, umri wake hivi sasa unafikia miaka sitini, na sie mtu wa kutoa rushwa.
- Bila shaka ningependa kukutana nae, je, anaweza kula pamoja nami hotelini saa kumi?
- Inawezekana, na baada ya kukutana nae utaona neema ya ukristo..

Joji alipoteremka kutoka chumbani kwake kwa ajili ya ahadi ya chakula cha mchana, alimuona mwanamke mwenye umri mkubwa akimsubiri, alikuwa na mikato katika paji lake na anaonesha kuwa ni mwanamke aliyechanganya baina ya uchina na uhindi, au ndivyo alivyo kama alivyodhania, alimsogelea na kumsalimia:

- Karibu, BiJiyostana.
- Asante, nami nimefurahi kukutana nawe.

Alimwalika kula nae chakula Buffet (mgahawa ambao walaji hujihudumia wenyewe) pale hotelini, alimshukuru. Alionekana wazi kabisa kuwa ni mwanamke mwenye kujiheshimu na mwenye tabia njema.

Joji alichagua meza ya pembeni na akamkaribisha kwa kumwambia:

- Maiko kanihadithia mengi kuhusu wewe.
- Nami kadhalika, Maiko kanihadithia kuhusu wewe, aliniambia kuwa uliomba ule nami chakula cha mchana kwa kuwa ungependa kujua kuhusu Ubudha!
- Ni kweli kabisa.
- Kabla ya kuzungumza, katika hilo kuna kitu kimenivutia kwako, bali na wafanyakazi wote hulizungumzia katika shirika.
- Ni nini hilo?
- Kuwa wewe sio kama Kakhi.
- Wamejuaje?
- Habari imeenea kuwa umekataa kutofautisha baina ya mnaswara, mbudha, mhindu na muislamu kuhusu mikataba, kama ilivyoenea habari ya kuwakataa wasichana wale wawili! Na mfano wa hayo.
- Je wamefurahishwa na hayo?
- Kwa uchache mimi kama mbudha, ndio..sana.
- Nafahamu kuhusu kutoichezea mikataba lakini vipi kuhusu hiana?
- Sisi Mabudha tunachukia hiana na matamanio, bali tunaona kuwa mambo machafu yanatokana na sababu tatu zifuatazo: Kwanza: Kujisalimisha na matamanio; moja katika usia wa Budha ni: “Usipoteze uhai, usiibe wala kubaka, usidanganye, usinywe kilevi, usizini, usile chakula kilichoiva kabla ya wakati wake, usicheze wala usihudhurie ngoma na hafla za nyimbo, usiende kwa daktari, usilale katika kitanda chenye godoro na haswa laini, Usichukue dhahabu wala fedha.”
- Ni usia mzuri kabisa, lakini nina baadhi ya maswali: Kwanini usiende kwa daktari, wala usichukue dhahabu wala fedha? Au usilale katika kitanda chenye godoro! Je, ni ukomunisti huo?
- Kuipa nyongo dunia ni alama kuu za ubudha, nayo inajumuisha vile vile kuacha kuoa na utajiri, kuihama nafsi, na mfano wa mambo hayo kama ulivyosikia; ima ushikamane na dunia au uikimbie.
- Nashangazwa na alama kubwa za ubudha ni kutokuishi maisha ya furaha hapa

www.path-2-happiness.com

duniani, tabia ya mwanadamu ni kupenda mali, kutamani mwenza wa jinsia nyingine…, na huyo budha ni nani?

- Nilikwambia ima dunia au kuikimbia, kuipa nyongo dunia ni mama wa mambo ya kheri. Ama kukujibu kuhusu nani Budha? Hilo ni swali gumu kulijibu!
- Itakuaje jibu kuhusu Budha likawa gumu? Je, Yeye si Mungu wenu? Au Mtume wenu au Mkweli ambae nyote mnajinasibisha?!
- Umesimama katikati ya ugumu, sisi hatujaafikiana kama yeye ni Mtume, Mkweli, Mungu, Mtoto wa Mungu, au mwalimu au vyovyote vile..
- Inaingia akilini?!
- Kaskazini ya China inatofautiana na Kusini yake, na vivyo hivyo tofauti ya Burma (Myanmar) na Cylon katika kulielezea hilo. Kwa ujumla si hili, bali muhimu ni wewe mwenyewe kujiweka katika hali nzuri katika nafsi yako na roho yako ili uwe Budha.
- Na kuitakasa Nafsi ni mtu asioe wala asikusanye mali, na kuvaa mavazi duni?
- Ndiyo hasa, wala asiibe, wala asidanganye, kulewa wala kuua.

Joji hakushindwa kuona alipokuwa akizungumza na Jiyotsana mavazi yake aliyovaa yaliyovutia, alitamani kumuuliza kuhusu rai yake kuhusu mavazi yake na utanashati wake:

- Je hilo linampasa kila anayefuata Budha?
- Ndio..kisha akatabasamu: Kwa kiasi fulani, mazingira ya maisha yetu yanatushinda katika kufuata usia huu wenye hekima.
- Kwa maana hiyo ni usia wa kimaadili tu, wala haufai kwa maisha ya watu wengi?!
- Kwa kiasi fulani hata nyie hali kadhalika.
- Una maana gani?
- Kusema ukweli Maiko ni mtu wa dini sana. Hata hivyo anawapelekea wasichana Kakhi katika kila ziara aifanyayo huku! Na anacheza na mikataba ya wafanyakazi! Nawajua wakristu wengi wenye kunywa pombe, je, haya si makosa mliyonayo?
- Umesema kweli, hata hivyo mimi nataka kujua dini yenyewe tu.
- Hakuna tofauti kwangu mimi, nadhani tunafanana.

Baada ya hapo akawa anafuta mdomo wake akiashiria kuwa kamaliza kula, Joji alimuita mhudumu na akamtaka alete bakula la tamu tamu za kihindi, kisha akaendelea na mazungumzo yake:

- Hamjaafikiana kuhusu Mungu wenu au ni mtume wenu au..au..je mmeafikiana kuhusu sheria na hukumu za dini yenu na wasia?

- Kwa hakika wasia huu tunauongeza mara kwa mara.
- Mnauongeza?!
- Naam, Ubudha ni dini inayokuwa na nyakati; hii ni dini tuliyoitengeneza sisi na sio ya mbinguni kama mnavyodai dini yenu ya kikristu, pamoja na kuwa baadhi yetu wanadai kuwa ina asili ya kutoka mbinguni, hata hivyo mimi nashuku juu ya jambo hilo.
- Je utaniruhusu nikuulize swali la moja kwa moja pamoja jepesi japokuwa linakera?
- Sawa uliza, Mabudha wanapenda wepesi wa mambo.
- Je, mnaamini kuwa dini iliyotoka mbinguni ni bora au ya ardhini (iliyotungwa na mwanadamu).

Jyostana alichukuwa muda kujibu, kisha akanyanyua kichwa chake:

- Sitaki kudanganya..bila shaka kama ya mbinguni ni bora zaidi..hili ni kwa ajili misingi, hata hivyo waumini wengi wa dini za mbinguni ni watu wabaya zaidi… kisha akatabasamu: chukua mfano wa Kakhi Myahudi, na kwa uchache Maiko, ambao wanachezea mali za watu na kuiba.!
- Umesema kweli..umesema kweli, kama ni hivyo kwa nini usiingie katika dini ya mbinguni ili uwe mwema zaidi?
- Nimezaliwa na baba na mama Mabudha, na kwa ajili hiyo mimi ni Mbudha, lakini hatujui!! Huenda baada ya kufa kwangu nikawa Myahudi, Muislamu au Mkristo.
- Baada ya kufa?!
- Ndio..roho yangu itahamia kwa mtu mwingine baada ya kufa kwangu, na umri wangu sasa ni miaka sitini.
- Je unaamini kuwa roho ya marehemu huingia katika mwili wa mtu mwingine.
- Hapana, lakini ipo katika dini yetu.

Uchovu ulianza kujionesha wazi kwa Jyostana kutokana na maswali na majibu haswa ni kwa sababu ilikuwa ni baada ya muda wake wa kazi kumalizika, aliomba kikao chao kiishe, kwani mwili wake hauwezi kukaa zaidi.

- Je kuna maswali mengine au jambo ninaloweza kukutumikia?
- Hapana, asante, ulilolifanya ni kubwa sana, nimejifunza kwako mambo mengi.

Aliaga na kuondoka.

Maiko aliwasiliana na Joji jioni na kumwambia kuwa atakuta msalaba alioutaka katika mapokezi pale hotelini, na baada ya hapo akamtania: pana risiti hapo hotelini ili usidhanie kuwa ni rushwa!

www.path-2-happiness.com

Joji alimshukuru na akacheka bila kuona tatizo katika maneno ya Maiko.

- Je umeona neema ya ukristo baada ya kukutana na Jiyostana?
- Ndio.
- Ungeendelea kukaa nae sana ungesikia mambo ya ajabu yanayoweza kukutia mvi, Je, amekuelezea kuhusu mambo yao ya kufikirika na falsafa ya dini yao?
- Mambo yao ya kufikirika! Hapana.
- Hahaha, hilo ni bora. Vinginevyo usingerudi tena India, hata hivyo ulichosikia kinatosha kukuonesha kuwa ukristu ni bora zaidi.
- Una maana dini zote za mbinguni?
- Hili ndilo nilionalo, tutaonana rafiki yangu.

Joji alimaliza usiku wake katika chumba hoteli, akipitia tovuti mbali mbali katika intaneti huku akiangalia Televisheni hadi usingizi ulipoanza kumchukua akajilaza kitandani. Ilikuwa ni siku yenye kuchosha kwa upande wake. Haukuwa uchovu wa kiwiliwili tu, lakini kichwa chake kilikuwa kizito kwa majukumu aliyonayo pamoja na majibu ya maswali yake binafsi ambayo ndio yalikuwa na msukumo wake wa kuja kwake India. Katika yote hayo usia aliopewa na rafiki yake Adam haukumuacha: "Hakikisha mambo yako unayachukuliwa kama yalivyo." alihisi raha sana kwa hilo kwani leo imembainikia udhaifu mkubwa wa dini zilizotungwa na watu, na umbali wa dini hizi kutoafikiana na ubinadamu na hilo aliyakinisha yeye. Hivyo basi ni vipi mtu kama sisi atueleze sababu ya kuumbwa kwetu.?!

(4)

Asubuhi siku pili, Joji aliamkia katika soko kubwa la kompyuta hapo Delhi, alipanda hadi ghorofa ya tano, katika ofisi ya Mutwi ambaye anamiliki maduka mengi ya Kompyuta na programu zake.

Joji alikutana na ofisi ya kawaida kabisa, hata hivyo ilikuwa ni ya kawaida lakini ya kifahari kwa wakati mmoja, harufu ya udi wa kihindi ilijaa kila sehemu, Joji aliingia na kukutana na mtu wa mapokezi na kuulizia ofisi ya Mutwi, naye akamjibu:

- Sheikh Mutwi, upande wa kulia, mlango wa mwisho kulia, utakutana na ofisi ya sekretari wake.

Joji aliondoka akiwa analitaja lile jina mara kwa mara huku akishangazwa: Sheikh Mutwi!! Sheikh! Ina maana gani?! Alimsalimia sekretari, ambaye

alikuwa yupo kwenye kompyuta anafanya kazi, ambapo alijieleza na kutoa kitambulisho chake cha kazi, na kumjulisha kuwepo kwa ahadi na Mutwi.

- Karibu sana, Sheikh anakusuburi takriban tokea dakika tano zilizopita.

Joji aliangalia saa yake, kweli ilionesha kuwa ni saa mbili na nusu na dakika tano. Hadi alipoingia katika ofisi ambayo pamoja na kuonesha ukubwa wake ila ilikuwa haina mpangilio, Mutwi alisimama na kumkaribisha, akamshukuru kwa wema wake na wakaanza mazungumzo yao ya kazi.

- Je unaweza kunielezea upana wa mashirikiano tunayoweza kuyafanya pamoja?
- Kwa ujumla ni chochote kinachoweza kuleta mapato kwangu na faida kati yetu.

Joji alifurahia hali hii ya kawaida (ya Mutwi kutokuwa na makuu), alimpa mkono na akafuatia kwa kicheko:

- Tumeafikiana..haya ni makubaliano ya haraka zaidi katika historia, lakini yatupasa kufahamu: Ni njia gani itakayotupatia faida sote?
- Nadhani majibu hayo yanaweza kutolewa na ndugu yangu Karimullah, ni mjuzi zaidi yangu katika kipengele hiki, unaweza kujadiliana nae, hata hivyo kwa sasa hayupo. Kutaneni kesho saa tatu asubuhi, na muandikiane vipengele vya makubaliano yetu.
- Je umeshatembelea Delhi na pembezoni mwake? Kama sivyo ni haki yetu kukutembezakama mgeninaweza kukutayarishia matembezi haya.
- Nimetembea mwendo mfupi kwa muda wa saa moja na nusu.
- Kama ni hivyo hukuona kitu chochote cha maana; India ni nchi kubwa sana na ina mengi..je utanikubalia kuwa mwenyeji wako?
- Nitafurahi kwa hilo.
- Kama ni hivyo twende, tukimtegemea Mungu.
- Mpaka wapi?
- Matembezi, tutaaanzia Taj Mahal.

Joji akiwa na Mutwi walishuka chini na kuliona gari zuri la Mutwi likiwa na dereva wake akiwasubiri, Mutwi alikaa nyuma pembeni ya Joji.

- Njia kuelekea Taj Mahal inachukua muda wa saa nzima na nusu, njia haikuwa na msongamano wakati huu, njia yenyewe kuelekea Taj ilikuwa ni sehemu ya matembezi vile vile, ama Taj yenyewe ni katika maajabu ya dunia, sitokuelezea kuhusu Taj bali utaiona mwenyewe.
- Nani aliyeijenga?
- Mfalme Shah Jihan, nayo ni mfano wa majengo ya Kiislamu India.

www.path-2-happiness.com

- Kiislamu?!
- Ndio.
- Samahani, hawa waislamu si ndio wale waliopora ardhi ya India, nao ni watu wakatili?!

Kusikia hivyo Mutwi alitabasamu..

- Naam..naam tumeiba India, na tukawauwa watu wake, na tukaipokonya kheri zake!
- Nasikitika sana, kumbe wewe ni Muislamu?
- Naam, nilikuwa nakudhania unajua hilo.
- Samahani kwa swali langu, lakini hivyo ndivyo tunavyosikia kuhusu waislamu.
- Usijali, Mimi wala wenzangu hatukuja toka nje ya India na tukaingia India kupoka kheri zake…mimi ni mzawa wa India mtoto wa mzawa wa India na .., na ukitaka kujua nani aliibia India utaona utakapofika Taj Mahal, ni nani aliyekata johari zake?
- Ni nani?
- Muulize muongozaji watalii tutakapofika..na natarajia hilo halitakushitua, mimi najua propaganda dhidi ya Waislamu wala sishughuliki kujibu, na nadhani historia ndogo ya India utakayosoma itakubainishia hilo.
- Vipi?
- Unaweza kuandika historia ya India kwa kuangalia katika Intaneti, na utaweza kujua ni nani aliiteka India na kuiba, je ni waislamu ambao ni wakazi wake wa asili, au waliokuja..kisha baada ya hapo angalia maisha waliyokuwa nayo watu wengine katika hukumu ya dola ya Kiislamu..kisha akakumbuka na kucheka: pamoja na kuwepo makosa mengi, moja wapo ni katika Taj Mahal tunayoiendea sasa hivi, alijenga kaburi la mke wa Shah Jaan.
- Wewe unazungumza kwa hali ya kawaida kabisa!
- Kawaida katika mtazamo wa maisha ni moja katika anuani za maisha ya furaha na kuridhika.

Joji alifurahishwa sana na matembezi yale na suala la wizi wa johari ulifanywa wakati wa utawala wa Waingereza, Mutwi hakupenda kuumiza hisia za mgeni wake, Joji alipenda tabasamu la Mutwi na usafi wa nafsi yake, lakini alihisi kitu kimoja kwake, Mutwi kwani alimuacha Joji mara tatu peke yake katika matembezi yale na kila wakati akimwambia: Nisubiri nakwenda kuswali kisha narudi, kama kwamba hakuwa ni mtu mwenye nidhamu na

mpangilio mzuri katika matendo yake.

Matembezi yalimalizika, Joji alifika hotelini kwake saa mbili usiku akiwa amechoka, alikoga na kwenda kitandani kulala, hata hivyo kabla ya kulala akakumbuka jambo na kumpigia Maiko kutaka ushauri wake kuhusu mazingira ya maafikiano atakayofanya na Mutwi.

- Halo..ndio, nataka ushauri wa haraka, inaonesha Mutwi mwepesi kuingia katika makubaliano, je ni wepesi wenye hadaa?
- Pamoja na kuwa sina raha na Mutwi ila namuona kuwa ni mkweli, lakini vile vile ni mtu asiyekuwa na nidhamu katika kazi yake, na lau angeweza kuwa na nidhamu nzuri katika kazi yake angekuwa na matokeo tofauti sana.
- Kakhi alikuwa akiniambia kuwa Mutwi ni mtu mgumu lakini nimemuona kinyume chake.
- Ndio, ni mgumu katika dini yake, lakini ni mpole na mwepesi katika mikataba yake, kisha akacheka na kuendelea: ni mgumu kwa sababu hakumuunga mkono Kakhi katika tamaa yake na wanawake wake, ndio maana hakukubaliana na Kakhi pamoja na vikao vyao vingi pamoja, na sasa unajua sababu ya mtu mwenye dini kama mimi kumletea Kakhi wanawake wazuri!
- Kesho nitakaa nae ili kuingia nae katika mkataba, je una nasaha zozote za kunipa?
- Abadan..sina kitu kingine, roho mtakatifu atakulinda, je utapenda nikuchukue matembezini kesho?
- Asante..nikihitaji kitu nitawasiliana nawe.
- Kwa heri.

(5)

Asubuhi, pindi Joji alipokuwa akipata kifungua kinywa katika sehemu ya kulia hapo hotelini, alikuwa anaongea na mhudumu aliyekuwa akizungumza kiingereza kibovu:

- Jina lako nani?
- Naitwa Kapoor.
- Inasemekana kuwa India ni nchi ya dini mbali mbali, dini yako ni ipi?
- Uhindu
- Vizuri, dini yenye maadili mazuri.
- Ndio, kweli kabisa.
- Je ni kweli hawezi mtu mwingine wa nje kuingia katika dini yenu isipokuwa tu

www.path-2-happiness.com

mtu anayekaa India, na ndio maana inaitwa Hindus?
- Ndio, dini hii tumeitengeneze iwiane na mtu anayekaa India tu.
- Mmetengeneza dini?!!
- Ndio, tumeitengeneze itufae!
- Ni yupi Mungu wenu mnayemuabudu?
- Sisi ni matajiri dunia nzima kwa kuwa na miungu mingi!! Tuna idadi kubwa sana ya miungu, na huenda pengine tukahitaji vitabu vingi zaidi kuorodhesha majina ya miungu yetu, kiasi cha kumfanya mwandishi Will Durant (aliyeandika kitabu Historia ya Ustaarabu) kusema: Kuhesabu na kuorodhesha miungi itahitaji pengine vitabu mia moja.
- Ajabu kabisa.
- Sisi tunaabudu vitu katika anga, na tunavifanya kuwa miungu kama vile jua, nusu ya baadhi ya miungu yetu zina wasifu wa Malaika na nusu nyingine zina wasifu wa shetani.
- Mungu yuko karibu zaidi na shetani!
- Baadhi za hirizi ni miungu, kuna aina ya ndege ambayo ni miungu na kadhalika baadhi ya wanyama.
- Mnyama Mungu!
- Kwa mfano Tembo ni mungu (Janisha), ndani yake kuna mchanganyiko wa tabia za kibinadamu na mnyama, na nyoka anayeua kwa kugonga mara moja tu ni mungu (Naja), na sisi tunawapa nyoka hawa maziwa, lozi na tunawafanyia sherehe za ibada.
- Mnawaabudu vipi miungu yote hii?!
- Kwa wingi wa miungu tulionao tumewaweka katika makundi matatu au moja katika sehemu tatu.
- Moja katika sehemu tatu..kama vile wakristo!.
- Huenda tukawa tumechukua haya kwa wakristo, sisi tunaiendeleza dini yetu wenyewe, au huenda nyie mmechukuwa kwetu.
- Mhmh, malizia…
- La muhimu ni kuwa miungu watatu au mmoja katika sehemu tatu nao ni: Brahmanae ndiye muumba, Vishnu huyu ndie mwenye kuhifadhi na kuuokoa ulimwengu na Shiva nae ni Mungu wa maangamizi.
- Dini ya maajabu kabisa! lakini hukuzungumza kuhusu ng'ombe?! Nimesikia kuwa nyie…

- Hahaha, nitakuambia kama anavyosema Ghandi: Ng'ombe ni mungu wetu na tunampenda kuliko tunavyowapenda mama zetu, mama yangu ananinyonyesha mwaka mmoja au miwili na ninamtumikia umri wangu wote, wakati ng'ombe ananihudumia miaka yote na hataki kwangu isipokuwa chakula chake tu. Mama yangu anapokufa ninagharamikia maziko yake, wakati ng'ombe anapokufa tunafaidika na vitu vyake vyote hadi mifupa yake.
- Je ibada zenu hizi zinawapeleka peponi baada ya kufa?
- Kwetu sisi hatuna pepo wala moto.
- Kama ni hivyo aliyetenda mema atalipwaje na aliyefanya ubaya ataadhibiwaje? Au wote wako sawa?
- Mtu mzuri atalipwa baada ya kifo chake kwa roho yake kuhamia kwa mtu mwema, na huenda akaungana na Mungu Brahma katika safari yao, ama aliyefanya uovu ni kuwa roho yake itahamia kwa mtu muovu atakayepata mateso hapa duniani.
- Je mnaweza kutofautisha hapa duniani baina ya mtu mwema mtiifu na mkosaji?
- Ndio, na baadhi yetu wana nafasi ya uungu hapa duniani.
- Vipi hilo?
- Brahma ameumba watu katika makundi mbali mbali kutokana na sehemu za kiwili wili chake, wale Brahmins aliwaumba kutokana na uso wake, na ndio maana wanakuwa ni watu wa kufikiri sana na kutumia hekima, ama Kshathriyas wameumbwa kutokana na mikono yake; na hivyo basi hao ni watu wa kutumia nguvu, watu wa kupigana na mambo ya jeshi, Vaishyas wameumbwa kutokana na mapaja yake; na hao mara nyingi kazi zao ni kuhudumia jamii katika mambo ya biashara, viwanda na kusimamia chakula, na Shudhras wameumbwa kutokana na miguu yake; nao ni wafanyakazi na watumwa na wana kazi zao. Ama ibada za Shudhras na kuhudumia tabaka tatu kubwa zilizotangulia, ama waliokuwa hawaingii katika tabaka hizo nne hawaingiii katika sehemu ya dini ya Uhindu.
- Je, nikiwa katika tabaka la Shudhras je naweza kupanda cheo nikaingia katika Brahmins, au kama wewe ni katika kundi la waliotengwa unaweza kuingia katika dini ya Uhindu?
- Muhali kabisa..ibada ya Shudhra ni kuhudumia tabaka tatu za juu, na waliotengwa (maluuni) hawapo katika sehemu ya mpangilio wetu.

Joji alishikwa na mshangao, na akahisi kichefuchefu kwa ubaya wa dini hii, lakini alitengeneza tabasamu na kumuachia Kapoor na kutoa hela kidogo na kumpa, akasimama aondoke kwa ahadi ya kukutana na Karimullah, kwani

www.path-2-happiness.com

asije akachelewa ahadi yake pamoja nae.

Njiani, alikumbuka maneno ya Maiko alipomwambia ubaya wa dini zilizotungwa na mwanadamu (dini za ardhini) na lau angeendelea kukaa zaidi na Jiyostana basi angeichukia India yote na asingependa tena kurudi. Kwa kweli dini zote hizi zipo kinyume kabisa na mantiki ya akili na maumbile halisi aliyoumbwa nayo mwanadamu. Hata hivyo ubaya huu ni kwa dini hizi za ardhini au ni dini zote kama alivyosema Dr. Tom: "Utarudi ukiwa umechukia dini zote" hali ya Maiko mwenye dini haitofautiani na ya Kakhi, na wote hawamshindi Mutwi pamoja na vurugu yake! Alikuwa na hakika kuwa dini ya haki haikinzani na akili wala maumbile halisi wala mantiki, je dini ya namna hii ipo au la..?

(6)

Saa tatu kamili Joji alifika katika ofisi ya Sekretari wa Mutwi, aliomba kuonana na Karimullah, akaambiwa kuwa anamsubiri katika ofisi ya Sheikh, alipoingia akakutana na ndugu wawili Karimullah pamoja na Mutwi wanazungumza, walimsimamia na kumkaribisha. Alimuangalia usoni Karimullah lakini hakumfurahia, hata hivyo hakujua kwanini!

- Karibu ofisini kwangu, mimi nipo tayari kuandaa na kutengeneza mkataba.

Mutwi akawakatisha:

- Baada ya kumaliza ningeomba kukuona wewe Joji kabla ya kuondoka.
- Na mimi kadhalika kabla sijaondoka nataka kukuaga.

Joji alikwenda akifuata na Karim katika ofisi yake, ilikuwa ni ofisi kubwa lakini ya kawaida kabisa.

- Ndugu yangu amekuambia kuwa tupo tayari kwa maafikiano yatakayopelekea faida kwa pande mbili.
- Ndio..wewe unafanana na mtu..!
- Nafanana na Usamah bin Laden! Hahaha, wewe si mtu wa kwanza kuniambia hivyo.
- Natamani usiwe mfano wake.
- Mimi ni kama yeye Muislamu, lakini natofautiana nae kwa kuwa mimi ni Mhindi na yeye ni Muarabu.
- Yaani sio kama yeye muuwaji gaidi.
- Wachana na hayo; yeye ni gaidi kwa sababu hawawapendezi wala haafikini nanyi.

- Vipi? Si yeye na wafuasi wake wanalipua mabomu katika treni, nyumba nakadhalika huko kwetu?!
- Maraisi wenu wameua mara nyingi zaidi kuliko alivyofanya bin Laden lakini hamuwaiti kuwa ni magaidi, bali nchi nyingi za magharibi zimeuwa watu wengi sana katika nchi walizotawala na hamuwaoni kuwa ni magaidi, kisha akatabasamu na kusema: na wakati alipokuwa akipigana na adui yenu Mrusi mlimuita shujaa sio gaidi…hebu tuingie katika kazi yetu.

Joji alihisi kuwepo na ombwe kubwa baina yake na Karimullah, akaazima mazungumzo yoyote ya nje, amalize kazi yake tu, na kwa haraka sana akajizungumzisha kuwa huenda Tom akawa mkweli, hawa waislamu wanamtetea gaidi mkubwa katika historia ya mwanadamu!

- Vizuri, haya sio maudhui yetu.
- Je una muswada wa mapendekezo ya mkataba wetu, au nikupe mapendekezo kutoka kwetu?
- Ninao mswada wetu lakini nipe wa kwako niusome.
- Tafadhali pokea.
- Naomba dakika chache niusome.

Joji alianza kusoma mswada ule, akaona kuwa vipengele ni vyepesi na vinafahamika, vimedhibitiwa kiasi, na ni bora kuliko mswada wake uliomtesa kuutayarisha, lakini unaotoa uhuru mkubwa kwa washirika wake; alimgeukia Karimullah aliyeshughulishwa na kusoma kitabu.

- Nimeuona kuwa ni mzuri kabisa, ila nina maoni machache.
- Ruhusa ni yapi hayo.
- Je huoni kuwa kuna uhuru mkubwa wa shirika lenu, na ucheleweshaji wa fedha kutoka kwetu!
- Hivi ni vipengele viwili: kwanza uhuru; ili niweze kushughulikia eneo pana la ugavi na kwa bahati mbaya mpangilio wetu si mzuri. Ama suala la ucheleweshaji wa fedha ni kwa sababu hatutaki kuahidi uongo katika mkataba wetu pamoja nanyi.
- Hutaki kusema uongo, una maana gani?
- Kwa kukuahidi ninakwenda kinyume na ahadi, na kama siko huru, nitahitaji kila mara kuomba samahani kwa sababu zisizo za msingi za uongo na hili ni jambo nisilolitaka, si mimi wala nyinyi. Hata hivyo masharti haya yanafanya soko lenu kuwa kubwa zaidi; na hivyo basi mtapata faida kubwa zaidi na katika mkataba

www.path-2-happiness.com

kwa ulipaji wa benki kuna dhamana kamili.
- Je tunaweza kutoa malipo ya kila miezi mitatu, tumekubaliana?
- Tumekubaliana, nami napenda kuwa sawa pamoja nawe, ili asitujie tena Kakhi mara nyingine.
- Kwanini hamumtaki Kakhi?
- Nitaomba samahani kutokujibu ili isikukere.
- Hutonikera kabisa, niambie kwa nini?
- Hafikirii kabisa ila faida ya mali tu, na kwa njia ambayo si nzuri sote na yeye tunapata hasara, nadhani kuwa misingi mizuri inawafanya wote kupata faida, kama ilivyo tabia yake nyingine ya kutaja wanawake ambayo sisi hatuikubali, samahani sisi watu wa mashariki tuna jihifadhi zaidi.
- Si neno, naafikiana nawe kwa mengi unayosema, tumeafikiana na ninasubiri mikataba ipigwe mihuri na ubalozi wa Uingereza, nami yangu nikirejea nitaipiga mihuri katika ubalozi wa India huko kwetu.
- Nakushukuru, na nisamehe nilichosema kuhusu mkuu wako wa kazi.
- Usijali, nataka kumuaga Mutwi Rahman kabla sijaondoka.
- Haya twende.

Joji aliingia na Karimullah waliingia kwa Mutwi Rahman, alimkaribisha Joji na kumchangamkia, kisha akamuuliza:

- Je mmemaliza mkataba?
- Ndio.
- Je ilikuwa nyepesi na kawaida kabisa kama nilivyokuambia?
- Kawaida kabisa.
- Kila jambo jepesi ndilo lenye kufanikiwa, na kila lililo gumu linakuwa kinyume na akili, maumbile halisi aliyoumbwa nayo mwanadamu na dini hali kadhalika… kisha akaendelea kusema: Kwa sababu mmemaliza, Joji unapenda nini India nikupeleke uone? Kutalii India nchi yenye maajabu ni vizuri.
- Asante sana..ningependa kurudi hotelini mapema leo hii; nina kazi katika intaneti nataka kufanya.
- Kama upendavyo, kisha akafungua droo akatoa vikasha viwili vya kifahari vyenye mafuta ya aliudi, na akasema: Hii ni zawadi yangu kwako, kisha akamuwekea katika mfuko wa kifahari, na akamwambia: Dereva anakusubiri akupeleke hotelini kwako.
- Ukarimu huu wa nadra ni wa watu wa mashariki tu, nakushukuru sana, kisha

akachukua mfuko na kuondoka zake.

(7)

Joji alimkuta dereva akimsubiri, pindi alipomuona akija akamfuata na kumuelekeza kwenye gari, na kumfungulia mlango:

- Karibu mheshimiwa.
- Asante sana. Jina lako nani?
- Steven.
- Oh, jina la kizungu.
- Mimi ni Mkristo, ndio maana jina langu kama la kizungu.
- Ukristo uliingia lini India?
- Miaka mingi sana.
- Je ukoloni na misafara ya kimishonari ina nafasi katika hilo?
- Bila shaka, vinginevyo India yote ingekuwa ya Waislamu.
- Waislamu! Unakusudia wangeichukua India yote kwa ugaidi wao?
- Hapana, wewe hujui ujinga wa dini za ardhi (zilizotungwa na watu), ni dini mbovu na zenye vichekesho, kama sio misafari ya kimishonari, watu wote wangekuwa Waislamu kwa mapenzi yao.
- Nimefahamu baadhi yake, lakini dini za mbinguni hazitofautiani nazo!
- Ajabu! Utakuwaje mkristo kisha ukasema hivyo? Hii ni lugha ya waliokufuru!
- Nachukia ukafiri na najua inavyojikinza yenyewe kwa yenyewe, hata hivyo hizi dini zinazodai zimetoka kwa Mungu hazitofautiani na hizi za watu walizojitungia wenyewe.
- Ama sisi wakristo tunataka kuwatoa watu katika shaqawa yao, na tunawahakikishia usafi, na tabia njema, na sikubali mtu kutuhumu dini yangu katika hali yoyote ile, wala sikubali hilo kutoka kwa mtu kama Mutwi Rahman ambaye ni Muislamu pamoja na kuwa mimi ni dereva wake, pamoja na kuwa hajawahi kunifanyia hivyo hata mara moja, sembuse kutoka kwa mkristo kama wewe?! Lakini huenda ikawa hivyo kwa sababu wewe ni mprotestanti! Hata ikiwa hivyo sikubali!.
- Sikukusudia kuutuhumu ukristo! Kwanini niutuhumu nami ni mmoja wao! Ninachokusudia ni matendo ya watu wenye dini hizi zinafanana na watu wenye kuabudu dini walizotunga wenyewe, na wanaboronga katika mambo mengi mfano wa dini walizojitungia watu..
- Sijafahamu!

www.path-2-happiness.com

- Je tunaweza kubadilisha maudhui haya, na kumalizia sehemu ya safari yetu kujua historia ya India?
- Tumekaribia kufika, kwa ufupi Pakistan na Bangladesh na India zilikuwa nchi moja, kisha Pakistani na Bangladesh zikajitenga na India.
- Kwa nini zilijitenga?
- Kwa dhulma waliyokuwa wakiona waislamu wakifanyiwa na Wahindu, kisha kidogo kidogo wakajitoa kutoka India, vinginevyo India ingekuwa ni nchi ya Kiislamu.
- Wewe unawatetea sana Waislamu pamoja na kuwa wewe si katika wao! ..je ni kwa sababu unafanya kazi kwao au unawaogopa?
- Hahaha, pengine!

UDHAIFU

www.path-2-happiness.com

-

5 UDHAIFU

UDHAIFU

(1)

Ilikuwa ni saa saba adhuhuri pale Joji alipowasili hotelini na kuamua kwenda chumbani kwake kwa ajili ya kuoga na kubadilisha nguo zake ili arudi kwa mara nyingine kula chakula cha mchana katika Kafeteria ya pale hotelini. Na alipoanza kushuka chini mara simu iliita ghafla ilikuwa ni Katarina anampigia:

- Hallo..mpenzi wangu.
- Habari yako Joji, na vipi huko ugenini nchi ya maajabu?
- Ni nzuri na mimi mzima wa afya hapa, na hakika nimemaliza kazi yangu na zimebaki siku mbili tu ili kujua zaidi kuhusiana na mji huu mzuri.
- Vizuri, na vipi maswali ya dokta?
- Hahaha, wakati mwingine nahisi Tom yupo sahihi, pindi aliposema ukijiweka karibu na dini utaziacha zote, na nahisi mambo yameanza kujitokeza na kuwa wazi kwa kiasi fulani.
- Kila unapoukaribia Ukatoliki utafurahishwa nao, kadhalika roho mtakatifu atakufurahisha.
- Achana na suala hili, Maiko mwenye kuonekana mfuasi mzuri wa Ukiristo ndio mwenye kuniletea wasichana wa kustarehe nao, na wote hao kwa pamoja Maiko, Kakhi na Tom sijapata kumuamini yoyote kati yao.
- Kuwepo kwa mfano mbaya hakumaanisha ubaya wa fikra ya asili, bali huenda ni uthibitisho kuwa asili si mbaya, na hata kama kutakuwa na mfano mbaya, basi elewa kuna makumi ya mifano mizuri!
- Umesema kweli, cha muhimu kwanza ni hali za watoto wetu. Vipi hali ya Maiko na Sali?
- Wapo katika hali nzuri, na sote sisi tunahamu ya kukuona hivi karibuni.
- Na mimi pia nina hamu nanyi ya kukuoneni karibuni.

Katika Kafeteria ya pale hotelini chakula kiliandaliwa vizuri, na watalii wengi kutoka sehemu mbali mbali za nchi walikuwepo hapo. Wakati huo Joji alikaa pembezoni akiwa katika meza ndogo akipata chakula peke yake. Jicho lake likaangukia kwa msichana mzuri wa Kihindi wa miaka ishirini

www.path-2-happiness.com

na kitu hivi, mwenye nywele nyingi nyeusi, mwenye macho yenye wanja, na mwenye mwanya wa kutabasamu na kung'aa, alikuwa akiwaangalia watalii wenye kuangaza macho yao, na wakati mwingine akitabasamu nao huku akiwarembeshea macho na vitimbi mbalimbali vya kuwavutia.

Haijulikani nini kilimvutia Joji kwa uzuri wake na mvuto wake pale aliporudiarudia kumtazama yule msichana, na aliamua kushughulika nae kwa chakula na fikra badala ya kushughulika na kazi za intaneti alizotakiwa kuzimaliza na kujikuta akishughulika na yule msichana aliyekaa ghafla katika meza yake.

- Kwa jina naitwa Omela, natokea Delhi au kwa jina lingine nafahamika Mrembo wa kufitini. Nimevutiwa nawe pindi nilipokuona macho yako yananivuta ulipokuwa umekaa peke yako, je ungependelea nikuondolee upweke wako?

Joji aliinua macho yake kumwangalia yule msichana aliyekuwa nusu uchi, tumbo lake lilikuwa wazi, na kivazi chake kilikuwa kifupi sana kisichofunika chochote, uso wake ni kama kipande cha mwezi, na nywele zake za hariri na mwenye tabasamu la kuvutia, na haijulikani nini alifurahishwa nacho sana pale alipomujia na kukaa nae katika meza yake.

- Jina langu ni Joji, nimetokea Uingereza, nakushukuru kwa utu wako, kisha alikaa kimya kidogo akajaribu kushindana na nafsi yake na kuishinda huku akitamani kuwa nae, lakini inavyoelekea kufanya hivyo kutasababisha mambo mengine kutokea… Samahani nasikitika nipo na kazi sana, na hii ndio mara yangu ya kwanza tangu kufika kwangu India kukaa peke yangu hapa.
- Upole wako, vazi lako na muonekano wako ni mzuri, je utapendelea tustarehe pamoja?
- Utulivu wako ni mzuri na mimi nafurahishwa na maneno yako, ila baada ya muda mfupi nitakuwa na kazi.
- Samahani….unaonekana mpole mwenye tabia nzuri, mimi nina vyeti ambavyo vinaonyesha sina ukimwi.

Alinyoosha mkono wake na kumpa mkononi mwake huku akiukandamiza mkono wa Joji. Joji alihisi ni kama umeme umepenya katika moyo wake, lakini pamoja na yote hayo aliushinda moyo wake na nafsi yake na kurudisha mkono wake kwa upole.

- Nimekuelewa – asante sana, mimi nina mke.
- Je mke wako unae hapa India?

- Hapana yupo Uingereza.
- Wengi wanaokuja kutokea Ulaya, Marekani pamoja na dini zao mbali mbali bado wanapenda maisha ya starehe hapa….na uzuri wa India upo katika maeneo mengi.
- Nakushukuru na kwa kweli wewe ni mzuri unaovutia sana lakini pamoja na hayo nakushukuru.
- Wewe ni mgeni lakini ni mgumu, na wewe ni mtu wa kwanza katika maisha yangu kukutamkia na kukupa moyo wangu halafu unanikataa…

Omela aliondoka kwa haraka, pale pale Joji alijiuliza moyoni mwake kwa mshangao….je mtu huitwa mgumu ambae anasita kumfanyia hiana mke wake na mwenye kuheshimu misingi yake, Hahaha huenda ikawa ni hivyo….. haya ndio maisha yanavyoonekana machoni mwetu kila siku hupita mambo ya ajabu, tusiyoweza kuyatafsiri au huenda yanafasirika kwa njia zetu. Laiti Kakhi angekuwa katika nafasi yangu angefurahi sana usiku huu wa leo akiwa na mwanamke mzuri kabisa!!

(2)

Pindi Joji alipomaliza kula chakula chake, aliangalia saa yake, na kukuta ni saa kumi na nusu kwa majira ya India, sawa na saa za tano asubuhi Uingereza. Na akakumbuka kuwa Katarina alimpigia simu kabla ya masaa manne, yaani saa moja asubuhi na sio kawaida yake kuamka mapema hivyo!

Alipanda ngazi kuelekea chumbani kwake na kuchukua komputa yake ili amalizie kazi zake, alifungua email yake katika sehemu yake ya Face book alimtumia Kakhi akimpa habari nzuri ya kwamba ameingia mikataba na kampuni mbili, kisha akafungua barua hizo zilizopo katika email, baada ya hapo alifungua face book ambayo hakuiangalia kwa muda wa siku tatu na kukuta idadi kubwa ya makala, picha na marafiki wapya, akakuta dokta Tom amemtumia ujumbe wa kutaka urafiki, alimkaribisha na baada kufungua alikuta picha nyingi na kwa mshangao wa ghafla wamepiga picha na Katarina! wakicheka na kula chakula kwa pamoja huku ameandika chini yake 'pamoja na Katarina' aliangalia tarehe yake na kukuta inakuwa saa kumi na mbili kwa majira ya London na baadhi ziliandikwa saa kumi na moja na dakika ishirini na tano sawa na tarehe hiyo 15/7….

Wasiwasi ulimshika, kumbe pale Katarina alipompigia simu mapema asubuhi alikuwa pamoja na Tom mpaka saa kumi na moja na nusu, kwa maana

www.path-2-happiness.com

hajalala bado! Damu ilichemka katika mishipa yake na kuinua simu akimpigia Katarina na kukuta simu yake imefungwa, alimpigia Tom ambaye alipokea kwa sauti ya uchovu:

- Ndio Joji, Katarina amenijulisha kwamba umeanza kujitenga na kila dini.
- Wakati gani amekwambia?!!
- Alipokupigia tulikuwa pamoja nae, kisha nikampeleka nyumbani, nakupongeza kwa hakika ni mzuri.
- Mlikuwa mkifanya nini?
- Tulikuwa na sherehe Kanisani, je sijakujulisha kwamba mimi nafanya utafiti kuhusu wanadini?

Joji alifunga simu na kujitupa kitandani kwa mshangao wa tukio hilo, na kujikuta yupo mapokezi akimtafuta Omela, na hakumkuta, alimuuliza muhudumu wa hoteli wapi alipo, alitabasamu na kumjulisha kwamba leo ana oda nyingi, na yeye ameelekea muda mfupi chumbani kwa mtalii wa Kichina.

Joji alimuliza kwa sauti ya kufoka!

- Nini wanafanya?!
- Alijibu Hahahaa, nitajuaje mimi?

Joji alijihisi vibaya kwa swali lake, na kujikuta mwenye wasi wasi sana, hajui la kufanya…alipanda kwenda chumbani kwake…Nia yake kubwa kwa muda huo ni kutaka kumuonyesha Katarina kwa njia yoyote ya malipizo kutokana na hiyana yake, aliamua kuwasiliana na Maiko ili amletee wasichana wawili wazuri aliowaona pale Kafeteria, lakini alisema na nafsi yake ya kwamba: Achana na mambo hayo hayatakunufaisha shikamana na misingi ya tabia yako na usiwe kama Kakhi au Tom, na fikra nyingine ikimwambia, 'Hii misingi ya tabia yako imekupa faida gani…..hakuna kitu?

- Hallo…Maiko
- Hallo Joji, umenishtua, sio kawaida yako kunipigia simu muda huu.

Joji alizinduka na kuangalia saa na kukuta ni saa saba na nusu.

- Samahani, sikutanabahi kama muda umekwenda hivi bali nimetamani kukujulia hali tu na huenda nitakupigia kesho, asante Maiko.
- Nashukuru kwa simu, tutawasiliana kesho.

Joji aliendelea kuwaza kwa hasira pale chumbani kwake na baadhi ya matusi na laana zikimtoka hajui la kufanya, shaka na wasiwasi kwa mke wake zimedhoofisha haiba yake….Alitaka kulipizia kwa Omela, bahati mbaya

hakumpata, mwishowe mtu mwingine alifaulu kumpata Omela. Mtu asie na kasumba kama yeye na asiye mkakamavu na misingi ya tabia ambayo inatufanya turejee nyuma na kufikiri mara nyingi, na wanakuja wengine na kupatiliza fursa kwa anasa na uzuri.

Na kwa wakati huo Joji akakumbuka siku za nyuma Katarina na Tom walipokesha, na kufungua intaneti na kutafuta ukurasa wenye picha za Tom za zamani na kukuta ameweka picha za mkesha wa ukurasa wake na picha hizo zinaonyesha kufanana na hafla ya hivi karibuni; zinazojulisha sehemu ile ile, ambayo huenda ikawa ni kanisani, kisha akajiuliza: Ni kanisa gani hili lenye kuruhusu upuuzi huu!!

Kisha akakumbuka alivyoishi na mkesha huo uliopita. Na ni kwa namna gani Baraad alipotaka kumfanya 'teja', hapo alikumbuka maneno ya Adam, "Laiti ungeshinda mambo yako ya msingi na kutatua matatizo yako kwa njia bora, nafsi ingekuwa ni imara zaidi kutatua mazito" na kauli yake ni kuwa, "Usiweke shaka yako ndio dalili ya kumtia hatiani pengine kuwa kwake na Tom ni kwa ajili ya kumlingania kwenye Ukristo". Na usia wake mwingine kwake ni "Angalia au zingatia mambo muhimu ili nafsi yako na maisha yako yawe ndio jibu la matatizo yako kwa urahisi, na wakati huo utapata furaha na kumaliza yanayokusibu." Na kauli yake ni: "Jaribu kutangamana na Katarina pamoja na Tom kwa njia ya kawaida, kwani wewe hivi karibuni utakuwa ni mwenye kusafiri kuelekea India na kurudi kwako utahadithia kila tukio, na hakikisha unayachukulia mambo kama yalivyo (kama kawaida) bila huzuni, na kwa furaha bila hasira." Joji alijiuliza mwenyewe: Hivi Adam yupo pamoja na Katarina, au anamtetea kwa vile ni mtu wa dini kama yeye? Nitawasiliana nae ili niangalie nini anachonificha mtu huyu!!

- Hallo, nani mwenzangu?
- Ni mimi Joji kutoka India.
- Naam karibu mmagharibi kutoka mashariki, vipi hali zenu?
- Ni katika hali mbaya, Katarina amekesha usiku wote mpaka asubuhi ya leo pamoja na Tom.
- Umethibitishaje hilo?
- Kupitia Tom mwenyewe, kwa sababu ameweka picha yake katika mtandao wake unaweza kufungua na utaona picha ya Katarina.
- Ni nini kigeni? Je ulihakikisha kuwa alikesha nae mara iliyopita?

www.path2-happiness.com

- Naam, lakini…..
- Ok, muhimu utafanya nini? Usiwe dhaifu mbele ya shaka na kuchanganyikiwa, angalia malengo yako ya safari, iwe malengo ya kikazi au malengo ya kutatua maswali yanayo kuzunguka.
- Natamani nilipize kisasi kwa Katarina kwa njia yoyote ile.
- Nimekueleza tangu mwanzo, usiachie mtu akuchezee pindi unapokuwa katika hali ya udhaifu na kuchanganyikiwa kwako, narudia tena kukueleza, tukiwa katika hali zetu za udhaifu, tunashindwa kushikamana na msingi yetu. Na pale tunaposhikamana na misingi yetu tunazidi kuwa na nguvu.
- Nitastarehe na msichana wa Kihindi na zaidi yake, na nitamtumia picha hizo ili kuumiza moyo wake kama alivyoniumiza mimi.
- Wewe kwa hili utakuwa unaunguza moyo wako tu, na kisasi cha aina hii ni pigo kwa watu dhaifu, na utaidhuru nafsi yako na utu wako zaidi kuliko utakavyo muumiza Katarina, na inawezekana asidhurike kwa hilo. Yeye amekusaliti na Tom ni nani mwenye madhara zaidi yeye au wewe?
- Ni mimi.
- Hapana bali yeye ndie alieharibu dini yake na heshima yake, na wewe haikudhuru chochote. Lakini kwa upande wangu pengine isiwe kama unavyofikiria.
- Kwa nini unamtetea? Au ni kwa vile ni mwana dini kama wewe?
- Sifikirii kama ana maadili ya dini kama ana kusaliti kama unavyosema, na hata kama itatokea hivyo, na kama hajakusaliti hilo suala jingine, kisha kwanini mimi nimtetee hali mimi simjui kabisa? Na sikujua kama ana dini ila kupitia kwako sasa hivi, na wewe ulikuwa unasema anakunywa pombe na kukesha tu, na hukuniambia kwani mwanadini, kisha nina maslahi gani katika hilo? Pia wewe ndio ulioniambia na sio mimi niliekupigia simu!
- Samahani Adam, sio nia yangu kukuudhi, ila nimefedheheshwa sana, na nimeamua kumuonyesha Katarina kwa kutembea na Omela.
- Najua sio lengo lako kunidhalilisha ila mashinikizo yasituhamishe katika misingi yetu, na ni nani huyo Omela?
- Ni msichana mrembo alienitaka nikamkataa na sasa namtafuta sana ili niwe nae kwa sasa.
- Na kwa nini ulimkataa?
- Si kutaka kuchafua utu wangu kwa matamanio… au kwa kuwa mjinga na mpumbavu!

- Kwa hiyo sasa unajiandaa kudhalilisha utu wako?!
- Nifanyaje sasa?
- Rudi katika utu wako, na tafuta majibu kwa matatizo yako makubwa, tembea katika njia ya furaha, na utafika na kushinda mitihani yako.
- Mimi nitarudi London baada ya siku mbili na ni muhimu kukutana nawe.
- Nakusubiri:

Joji alimaliza maongezi kwa kukata simu hali ya kutojua nini anakifanya, alifungua kompyuta yake ili afungue ukurasa wa face book wa Adam, na hapo alikuta katika hali ya kawaida kabisa, makala zake ni ndefu, naye Joji akiwa katika hali mbaya ya kinafsi isiyomruhusu kusoma makala kama hizi, mara ghafla macho yake yakageukia makala yenye kichwa cha habari: "Somo kwa ajili ya rafiki yangu anaefuata furaha." Aliandika Adam makala hayo kabla ya siku nne…

Somo kwa rafiki yangu mwenye kutafuta furaha:

Nimefahamiana hivi karibuni na mtu mwenye misingi bora anaetafuta faraja kwa yale yaliyompata, naamini ni mkweli katika utafiti wake, lakini msongo wake ni mkubwa, nimemfahamu kupitia kisa chake hicho na nimependelea nikushirikisheni kwa faida zifuatavyo:

1.Mwenye kutafuta furaha ni juu yake kufuata njia yake; na haiwezi kufikiwa furaha hiyo kwa mali, cheo au kurithiwa, na ili afikie furaha hiyo hakuna budi kujituma na kudumu ili kuifikia.

2.Hatafurahi kabisa au kuwa mwenye furaha mtu ambaye hatajibu maswali makubwa: Nani katuumba? Kwa nini ametuumba? Kwanini tunaishi? Na mwisho uko wapi? Na mtu ambaye hatayapatia ufumbuzi maswali haya, hatapata katu furaha ya milele.

3.Baadhi ya watu wanatia uzito na ugumu njia ya furaha, halafu wanasema: hatutavuka vikwazo hivi, na laiti wangerahisisha mambo wangefikia katika furaha kwa wepesi zaidi.

4.Baadhi ya watu wanasahau malengo yao kwa matatizo madogo na malengo madogo ya karibuni, na wakati huo wanaishia kati kati ya njia bila kufikia kabisa malengo ya furaha.

5.Haifai kukatisha misingi yetu njiani, kwani misingi ndio minara yetu kuu ambayo hatupaswi kuivuka, na mwenye kutaka kuivunja atavunjika mwenyewe, na minara itabaki bila kubadilika.

www.path2-happiness.com

6.Mtafiti anapokuwa mkweli na nafsi yake, akajituma na akadumu na kusubiri, basi atapata uwepesi katika mambo yatakayomfungulia njia.

Somo bado ni kubwa na nitaendelea na makala hayo kipindi kijacho pengine itakuwa karibuni.

Ni mimi: Adam.

(3)

Baada ya Joji kusoma makala ya Adamu alikuwa mbali huku akijiuliza kwa mshangao: Kwa nini Adam ameandika habari zake na hakumfahamisha jambo hilo, wala hata hakuashiria jina lake? Na Adam hajaenda kinyume juu ya yale aliyoniambia, alikuwa muwazi kwangu lakini hakujali hisia zangu wala hali yangu ya nafsi! Katika hali hii nikipata kidonge cha Heroin au nikipata wasaa wa kumpata Omela nitasahau yote niliyokuwa nayo, na kusahau ni njia ya kuelekea katika furaha…ah, je ni kweli njia hizi ni kimbilio la matatizo au ni suluhisho sahihi wanalotumia watu wapevu ambao hawapotezi fursa yoyote? Ama kweli nipo katika mtanziko!

Simu iliita chumbani, alinyanyua mkono wa kujibia, upande wa pili wa simu alikuwa mhudumu katika mapokezi, akimjulisha kuja kwa Omela…

- Je una muhitajia aje kwako?

Joji alitulia kitambo kirefu hajui la kumwambia…

- Sijui!
- Nini?
- Nashuka kuja kumuona sasa hivi.

Alishuka mapokezi huku akijiuliza: Je kushuka kwake ni kumlipizia Katarina au kujimaliza mwenyewe, kama anavyodai Adam? Je awatii Kakhi na Tom? Au amtii Adam? Wakati akiwa katika lindi la maswali hayo yasiyokuwa na majibu, ghafla lifti ikawa imesimama mkabala na mapokezi, na alipofungua mlango ghafla Omela amemsimamia mbele yake na mara tu alipomuona alitabasamu kwa furaha kubwa lililofanya uso wake mzuri kuzidi kung'aa na kuzidi kupendeza.

- Karibu Omela, unaonaje tukakaa pale kwenye kiti kile?
- Haa haa, hamna neno.

Mara baada ya kukaa tu Omela alianza kutabasamu..

- Nimejihisi mwenye furaha kubwa pale mhudumu aliponileza unanihitaji.

- Kwa nini?
- Kwa sababu nilihisi umenidhalilisha pale uliponikataa, na sikuwa mwenye mvuto kwako.
- Sijakudharau bali nilikushukuru, na sikukuambia wewe sio mzuri, bali wewe ni mzuri sana kama jina lako lilivyo.
- Kwa nini hatukai chumbani tukastarehe pamoja ikiwa ….kisha alimkonyeza.
- Nataka tuongee kwanza.
- Juu ya nini? Au tuongee nini?
- Je inawezekana nikuulize maswali mepesi lakini yenye maana kubwa kwangu? Na naomba uwe mkweli na muwazi sana kwangu.
- Usijali nitakuwa mkweli kwako, ila sijajua kwa nini unanipelekea huko?
- Je wewe ni mwenye furaha na maisha yako?

Kimya kilitanda kwa Omela huku akitafakari na kutazama chini….

- Nimekuahidi kuwa mkweli na sitokuficha kitu na kwenda kinyume na ahadi yangu, japokuwa sikutegemea kukutana na swali hili, ikiwa furaha hiyo unayoizungumza ni kwa maana ya kucheka, kutabasamu, kucheza, kuwa na mali pamoja na uzuri, basi kwa hayo mimi ni mwenye furaha kubwa.
- Nakusudia ndani ya moyo wako je unajisikia furaha? Kwani baadhi ya watu wanacheka lakini ndani ya mioyo yao kumejaa huzuni kubwa.
- Nimekuahidi ukweli kana kwamba umeingia moyoni mwangu kabisa, na mimi najiepusha na huzuni za ndani kwa kutafuta mali, kucheka, kucheza na kufanya mapenzi ili niepukane na huzuni iliyo ndani ya moyo wangu.
- Ni zipi sababu za matatizo na huzuni hizi pamoja na uzuri ulionao, mali na afya njema bali na hata kustarehe pia?
- Sijui, huenda ni maisha ya hovyo ninayoishi, kwani maisha yangu hayana thamani kabisa.
- Je unatafuta maana ya maisha yako? Au maongezi haya hayakuhusu?
- Hapana, kwa hakika ni vigumu kupata majibu, majibu maana yake ni kupata furaha, nami sistahiki.
- Kwa nini hustahiki?
- Kwa sababu mimi ni mdoli watalii wananichezea, na mimi nawachezea kwa ajili ya starehe ya mpito tu.
- Na kwa nini umefurahi pale uliposikia nakutafuta?
- Kwa sababu mchezo wangu wa kukutega umeshindwa, nami sijazoea kupoteza

www.path-2-happiness.com

na kupata hasara maishani mwangu milele.
- Unajua kwa nini nilikuwa nakutafuta?
- Hapana kisha akatabasamu na kusema: Usiniambie ulikuwa unanitafuta ili uniulize maswali haya?!
- Hapana sio kwa ajili hiyo, bali ni kwa ajili ya kushuku kuwa mke wangu ananisaliti na nikaamua nimlipizie kwa kustarehe na wewe.
- Haa haa alicheka kidogo kwani sijakwambia kuwa mimi ni mdoli tu wa kuchezewa tu kwa muda, unamlipizia mkeo kwa hila zangu za mpito, kweli mimi ni duni?!
- Nisamehe, bali wewe ni mzuri wa kupindukia, lakini kwa upande wangu, utu wangu ulikuwa unanizuia kufanya mambo kinyume na heshima yangu.
- Na kwa sasa ni penzi la kisasi umesahau utu wako! Mimi ni rahisi kiasi gani katika macho ya watu!
- Samahani, sina nia ya kukudhalilisha ila hii ndio kazi yako unayoifanya.
- Wewe hujasema ila ukweli tu! Wakati mwingine mwanadamu hajijui mwenyewe na kwa hakika nimebakisha wiki mbili kutimiza miaka miwili nafanya kazi hii, na hakuna mtu alienirudisha nilipomsogezea nafsi yangu, na mara ngapi nilijihisi mzuri machoni mwao. Na baada ya kumaliza haja zetu naondoka, na wewe ndio mtu wa mwanzo kuniweka wazi kwa hili, akanifanya kupambana na nafsi yangu.
- Samahani. Narudia kusema, sio nia yangu kukudhalilisha au kukutia kasoro.
- Huenda…lakini ukweli ndio huo!!
- Una maana gani?
- Mara nyingi tunakimbia nafsi zetu na tunaogopa kuona uhakika wake.
- Sijafahamu!

Joji alinyoosha mkono wake na kushika mkono wa Omela na kumvuta upande wake, lakini Omela aliondoa mkono wake kwa upole huko macho yake yakitoa machozi na kusema:

- Kucheza na kukimbia maisha ni uovu kwa vyovyote utakavyo onyesha ushupavu.
- Achana na hayo nisamehe kwa yale niliyotamka.
- HaaHaa. Je utaachana na mipango yako ya kumlipizia mkeo.? Sina thamani kiasi hiki!
- Nini unataka? Je unakusudia kukataa kupanda juu kwa ajili ya kustarehe mimi na wewe ili tuondokane na huzuni zetu?
- Ndio, mara hii mimi ndio sitaki.
- Ni ipi dini yako?

- Sina dini mimi, na je kuna mwenye dini ya kweli anaefanya mambo mfano wangu?
- Mke wangu ni mwanadini, lakini ananisaliti na mtu mwingine!
- Ama dhana na shaka yako si kweli, au yeye anasema uongo na unafiki hali ya kuwa hana dini, au anajinasibisha na dini mbaya, hivi inaingia akilini niwe na Mola ananiona na kunihesabu halafu niwe nawinda wanaume? Jua ya kwamba baba na mama yangu ni mabudha, lakini mimi nimeachana na ubudha kwa utata wake na ugumu wake wenye kuchukiza kwa hiyo nikawa bila dini.
- Vipi unaishutumu dini ya wazazi wako?
- Hiyo ni dini yetu tuliyoianzisha na kuibadilisha kama tutakavyo. Kwa hivyo ukitaka unaweza ukasema hakuna dini ya Budha kwa sababu hiyo ya kubadili badili! Bali sheria zote zilizobadilishwa zinatokana na sheria za dini zilizopita kwa hiyo mabadiliko na uzushi huo hata kama ni mbaya hauna kikomo…nitaondoka hapa hotelini na huenda nisirudi tena.
- Kwa nini usirudi?
- Sitarudi mpaka nione sababu inayonipa maana ya maisha yangu na kunifanya niheshimu nafsi yangu, nakushukuru sana kwa mara nyingine tena.
- Wapi unaenda sasa?

Omela alisimama na kutoka bila kujibu swali lake.

(4)

Joji aliamka hali ya kuwa amechelewa kuwasiliana na Maiko… alimuitikia kwa sauti nzito yenye mikwaruzo iliyochoka..

- Je bado umelala? Una nini? Umelala na kuamka umechelewa, je hayo umejifunza kwa Kakhi?
- Achana nae nina siku na nusu hapa India nimebakisha, kwa kitu gani utaniusia?
- Kuna bustani nyingi, makanisa, nyumba za ibada, makumbusho na masoko…. katika hayo unataka kutembea wapi?
- Bora makanisa na nyumba za ibada.
- Usisahau kutembelea kanisa la Saint James kwani zuri na maarufu.
- Na vingine? Je kuna sehemu za ibada za Waislamu, Wahindu na wengineo?
- Ijapokuwa sipendi, ila msikiti mkubwa uliopo Delhi umejengwa kwa miaka sita ni mzuri na wenye mandhari nzuri ya kuvutia.
- Nakushukuru nitapata kwanza kifungua kinywa kisha nitatembelea sehemu mbili

www.path-2-happiness.com

hizi.
- Kabla hujamaliza chai nitakuwa nimeshafika hapo hotelini.
- Usisumbuke, nitachukua taxi.
- Haa Haa, sio hongo hii, tumeshamaliza kutiliana sahihi mkataba, nitakuwa hapo baada ya nusu saa.

Kabla Joji hajamaliza chai yake na huku akijaribu kusahau kusalitiwa na mke wake, pamoja na maongezi yake na Omela na kuhusu kumuhadithia shaka yake kwa mkewe, ghafla alipigiwa simu na Maiko akimjulisha yupo mapokezi, alimalizia chai yake na kwenda kuonana na Maiko…walisalimiana na walichukua gari kuelekea kanisani.

- Jana nilikukumbuka nilipokuwa ninaongea na mhudumu wa kihindu wa hoteli.
- Nini wamekuambia kuhusiana na mimi?
- HaaHaa, nilikumbuka maneno yako kuhusu Jiyostana mbudha, siku hiyo ulinieleza kuwa lau nitakaa nae muda mrefu sitotamani tena kurudi India karibuni!
- Haa haa, kweli…kweli dini hizi zilizoanzishwa na watu katika zama za ujinga, kila moja ikija kutatua shida za wafuasi wao, au kuleta haki na usawa katika tabaka fulani kwao, lakini kwa mtazamo wa leo zimekosa thamani…Achana na dini hizi ili nikufahamishe kuhusiana na kanisa la Saint James ambalo tutalifikia muda sio mrefu, kanisa hilo lilijengwa na James Skinner mwaka 1836 C.E. ni kanisa kongwe katika sehemu hii, lina mandhari ya kipekee na uwanja wake ni katika viwanja vizuri kabisa.
- Umesema ni kanisa kongwe katika sehemu hii?
- Ndio, ni karibu miaka 200 hadi 300 hivi.
- Na kabla ya miaka 300 hakukuwepo na Ukristo India ?!
- Ukristo nchini India umekuja kwa njia mbili: Njia ya kwanza ni: njia ya Mtume Tom katika Injili ya Yohana naye ni mmoja katika mitume kumi na mbili wa Masiya katika karne ya kwanza ya A.D Na njia ya pili ni: njia ya kimishionari wa Kimagharibi kati ya mwaka 1500 mpaka 1975 A.D ni dini ya tatu India baada ya Uhindu na Uislamu, na idadi yao inafikia 24 milioni.
- Tu, ni idadi ndogo ukilinganisha na wakazi wake.
- Ndio idadi yao ni kama asilimia 2.3 na kwa idadi hii tu kuna maandamano ya hasira yanayofanyika mara kwa mara kuhusu kuongezeka idadi ya wakristo, wahindu wanahisi kuwa ukristo unapewa nguvu sana kwa mali inayotoka nje.
- Na je ni sahihi watu kuingizwa kwenye dini kwa mali?

- HaaHaa kwa kiasi fulani mpaka watu waondokane na itikadi mbaya za Kihindu.

Joji na Maiko walifika kanisani na kushuka ndani ya Kanisa wakiangalia kwa mazingatio; uzuri wa jengo, picha, pamoja na masanamu na minara yake, kweli ni nzuri, wala hakukuwa na alama ya Ibada hapo ni kana kwamba ilikuwa ni alama kuu ya Kihistoria tu. Maiko alikuwa akilisifia kanisa hilo kwa Joji kwa sifa nyingi mpaka walipomaliza ziara yao, wakapanda gari, hapo akamwambia:

- Nini rai yako?
- Linavutia kweli.
- Je sijakueleza hivyo? Sasa tunakwenda wapi?
- Tumekubaliana tunakwenda Msikiti wa Delhi sasa.
- Vizuri! Japo sehemu hiyo Siipendi lakini twende kwa ajili yako.
- Kwa nini huipendi?
- Waislamu sio watu wazuri ni wabaya sana.
- Vipi? Je wamewalazimisha watu kuingia katika dini hiyo kwa nguvu?
- Ukweli, hawajawalazimisha watu kuingia katika dini yao ya watu ambao hawajastaarabika.
- Kwani wamewarubuni kwa kuwaingiza kama Wakristo?!
- Najua lengo lako lakini hili pia sio.
- Watu wameikubali vipi dini hii?
- Oh, watu wameikubali dini hii kwa njia ya wafanya biashara wa Kiarabu waliokuja India kufanya biashara.
- Yaani watu waliingia katika Uislamu kwa maingiliano na wafanya biashara wa Kiarabu, kwa mapenzi yao tu, na sio kulazimishwa!.
- Ni kweli kwa bahati mbaya, ni rahisi kuwadanganya watu na kuwachezea, kwa ajili ya kukikimbia tabaka la chini la wahindu lenye chuki watu wakaingia katika Uislamu walipoingiliana kwa mara ya kwanza na wafanyabiashara wa Kiarabu, kisha baada ya hapo wakaja tena kwa njia ya vita.
- Vita?!
- Ndio, vita vya kwanza vililetwa na mtu anayeitwa Muhammad bin Qaasim Athaqafii katika mwaka 700 hivi A.D.
- Takriban ni kati ya miaka 1500 hivi!
- Waliongezeka mpaka ikawa ni dini ya pili nchini India.
- Ni ngapi idadi yao?

www.path-2-happiness.com

- Ni zaidi ya watu 180,000,000 ni sawa na asilimia 14.5 ya wakazi wake.
- Ni idadi kubwa! Na hii inamaanisha kama Pakistani na Bangaladesh hawakujitenga pengine wengi wao wangekuwa ni Waislamu.
- Ndio, lakini walihisi kudhulumiwa na Wahindu na kuanza mapinduzi yaliyopelekea Pakistani kujitenga, hapo alitabasamu na kusema: Hii ni bora kwetu, kwa hakika Waislamu walitawala India kuanzia mwaka 1001 A.D na utawala wao ulidumu kwa miaka 300 hivi.
- Je waliwalazimisha watu kuingia Uislamu kwa muda huo?
- Hapana, ila walikuwa ni madhalimu, walijenga majumba makubwa ya kifahari kati kati ya watu maskini na wanyonge.
- Aliniambia hayo Mutwi Rahman tulipokuwa katika ziara ya TajMahal!
- Hayo ni katika uadilifu wa Mutwi Rahman, waliwadhulumu watu riziki zao ijapokuwa hawakulazimisha watu kuingia katika dini yao, kwa kifupi kila tawala zilizotawala India zilidhulumu na huenda Uislamu ulikuwa na uadilifu kidogo nchini India kuliko ushirika wa Wahindu na Waingereza waliouita Ushirika wa Wahindi wa Mashariki na uharamia wa wazungu. Waislamu na wahindu walikuja juu sana na kuwa kinyume nao.
- Kwa maana hiyo Wahindu walipenda hukumu ya Kiislamu?
- HaaHaa, kwa masikitiko ndio, walikubali na hawakuwa wote ni madhalimu, isipokuwa dhulma ilitokea mwishoni mwa utawala wao, kama walivyokuwa watawala wa Kiislamu (pamoja na dhulma yao) walikuwa ni bora kuliko shirikisho la Wahindi wa Mashariki na Waingereza ni mategemeo yangu halitakuudhi hilo.
- Historia inaandikwa kama ilivyo, na sio kama tunavyotaka.
- Mapinduzi ya Waingereza yaliendelea mpaka walimteka mtawala wa Kiislamu na kuua wanae, na wakavileta vichwa vyao juu ya meza ya chakula, halafu wakaupiga vita Uislamu na kutupilia mbali mafundisho yake na kupora utajiri wa Wahindi.
- Unyama ulioje huu…ziko wapi haki za binaadamu?
- Haki za binadamu huenda tukazisikia tu katika mikutano na vikao. Ama uhalisia wake ni kitu kingine. Muhimu tumekaribia msikiti ambao ulikuwa ni makao ya mikutano ya Kimapinduzi dhidi ya Waingereza, na sehemu hii palitolewa wito wa jihadi kutoka kwa wanachuoni wa Kiislamu, na kwa wito huo watu walijiandaa baada ya hapo…na unaitwa msikiti wa Jihan Nama au msikiti wa Jamah, na ujenzi wake ulichukua muda mrefu na kukamilika mwaka 1656 A.D Mfalme wa

Munguli 'Shah Jihaan aliamrishwa ujengwe, ni katika misikiti mikubwa barani Asia unatosha watu 25,000 wenye kusali.

- Basi ni Msikiti mkongwe!
- Huenda, ni jengo zuri limejengwa kwa staili ya kiManguli lenye minara mitatu na ni hilo hapo mbele yako tumeshalifikia.

Walishuka wakaangalia uzuri wa jengo lake. Na Maiko alikuwa sio mwenye kufurahia usifiaji wa Joji. Joji alifanya haraka haraka kuliangalia jengo ili kuheshimu hisia za Maiko ambaye alikuwa mpole pamoja nae.

- Je ungependelea kwenda sehemu nyingine.
- Nashukuru, huenda muda umekwenda sana.
- Lakini bado hujafanya uadilifu!
- Kwa nini?
- Umetembelea kanisa na msikiti, na hujatembelea sehemu ya ibada ya Wahindu!
- Nilikuwa nataka kufika huko, ila nahisi kama nakusumbua.
- Sehemu hiyo ipo karibu na njia yetu, je utapenda kuona sehemu hiyo?
- Bila shaka, ikiwa haitakucheleweshe shughuli zako, ila mimi safari yangu ni kesho na nitakuwa na faragha kwa ajili ya kufunga mabegi yangu na sitatoka sana..
- Jina la hekalu la Wahindu ni Akshardam, hutembelewa kila siku na maelfu ya wakazi na watalii wa kimataifa, nalo ni hekalu kubwa kabisa la Wahindu katika Delhi, ujenzi wake ulianza mwaka 2000 A.D na kukamilika mwaka 2500 A.D, nalo ni hekalu la kisasa lenye kupendeza, wameweka nakishi ya miungu yao kwenye kuta.
- Je wamenakishi wanyama na wengine?
- Haahaa, ndio, walichorwa miungu yao, mfano wa wanyama na wanawake wachezaji dansi, bali kuna zaidi ya masanamu 20,000, kwani sikukuambia kuwa dini hizi za watu zinachekesha, inavyoonekana kila walipokuwa wakipendezwa na kitu wanakifanya Mungu. Wewe upo katika nchi ya maajabu, kuna waoabudu panya na wana sehemu zao za ibada na kuna wanaoabudu nyoka na wana sehemu zao za hata hivyo tumeshawasili katika jengo lenyewe la Wahindu.
- Yaelekea ni jengo la kuvutia sana.
- Sahihi, hakika imejengwa kwa mawe, hawakutumia matofali au kokoto na limepambwa kwa mapambo ya thamani kubwa tushuke tuangalie kwa haraka ili tusichelewe hotelini.

www.path-2-happiness.com

Joji alipendezwa sana na jengo hilo, lakini alijihisi kuchefukwa kwa kuona masanamu mengi, walizunguka lile jengo kwa haraka, na katika njia ya kurudi..

- Jengo zuri, lakini wingi wa masanamu ni kitu kinachochefua!
- Ndio, umesema kweli.
- Cha ajabu hata kanisani kuna masanamu, ama msikitini hakuna masanamu ndani yake!
- Lakini sanamu la kanisani ni la Yesu na sio la wanyama.
- HaaHaa, umesema kweli, pamoja na yote hayo na kushukuru, safari yetu ya leo ilikuwa nzuri sana.

Kutokana na kuzama na safari yake ya leo, Joji alisahau kidogo maudhui yake na Katarina pamoja na Tom kidogo, na alijihisi utulivu na raha, inaonekana kama vile alichoambiwa na Adam kilikuwa sahihi: Kwamba: "Zingatia mambo yako muhimu…." Safari yake hii ilikuwa ni hatua mojawapo mbele kufikia furaha, kwa hakika dini zilizoanzishwa duniani haziwezi kujibu maswali yake; vipi litajibu wakati chenyewe kinakikosa, yenyewe inajibadilisha mara kwa mara kulingana na mazingira, ili kufikia utulivu wa kidini unaotarajiwa na watu.

Ilimjia fikra kumuandika Adam ujumbe, alifungua kompyuta yake na kumwambia:

"Rafiki yangu Adam… Nakushukuru kwa nasaha zako, pia nisamehe kwa mazungumzo yangu mabaya.

Umesema kweli: Kwa hakika nimefaidika kwa nasaha zako sana. Nimeshinda jaribio langu la kutaka kulipiza kisasi lililonitawala. Kwani nimejishugulisha zaidi na mambo muhimu na kuachana na mambo madogo madogo, kwa hakika nimeendelea kujishughulisha kwa siku yote nzima, na ninaweza kujibu swali lako na la dokta pia kwa uwazi zaidi. Dini za duniani hazijibu swali lolote; hizo ni rai tu za watu ambao hawakutuumba, basi vipi watajua kwa nini tumeumbwa?.....Narudia shukrani zangu kwako na mimi kesho narudi, nitafurahi kukutana nawe nakushukuru kwa mara nyingine.

Ni mimi rafiki yako Joji.

Kisha baada ya hapo alijilaza kitandani akifurahia siku yake kwa kushughulikia malengo yake makubwa..

(5)

Joji aliamka mapema akaoga… aliangalia saa na kukuta bado masaa manne kuelekea uwanja wa ndege, akajisemeza 'nitaangalia nini ninachoweza kufanya katika masaa haya', lakini kwanza nipate chai…

wakati akiwa amekaa katika meza ya chai, mara akamuona yule mhudumu wa KihinduKapoor aliyeongea nae jana na kumuita…..

- Kapoor akaseme, Karibu Mheshimiwa.
- Na wewe karibu, nilikuchelewesha muda uliopita, lakini nina maswali nataka kukuuuliza kama una muda kama utakubali (kama hutajali)?
- Hakuna tatizo, inaonekana una hamu ya kuwajua Wahindu… na huu ni mtindo mpya wa watu wa magharibi.
- Na je Uhindu ni mtindo?!
- Naam, Uhindu na Ubudha ni model huko kwenu Ulaya na Marekani, wanakuja huko kukimbia maisha mabaya ya kimaada yenye kumfanya mtu ni chombo au mashine ya kulimbikiza na kukusanya, wanakuja huku wakitafuta maisha ya kiroho na tabia na hawajui zaidi ya hapo.
- Vizuri sana. Lakini nataka nikuulize swali; Je wewe na Wahindu wengine mnayo furaha kwa ujumla?
- Huenda Mabrahma ambao wanawakandamiza watu ndio wenye furaha, hata hivyo sidhani kama ni sahihi. Ama kwa upande wangu mimi ni Shudhra ni mtumishi tu, huu ni katika upande wa kitabaka, ama kwa upande wa imani, sisi tunaikimbia imani yetu na wingi wa miungu wetu kushughulika na mambo ya kiroho na kitabia zaidi na kujivua na dunia na Mungu pia, kwani hujasikia kuhusu Ghandi?
- Ndio, alikuwa mtu safi.
- Alitaka kuasi Uhindu kwa hivyo wahindu wenye kasumba wakamuuwa.
- Na kwa nini alitaka kuasi dini yake?
- Kwa sababu alisema haiwezekani kuishi sawa sawa kwa imani yetu kamili, samahani huenda ni kwa (kulingana na mtindo huu) umevutiwa na Uhindu na mimi nakuharibia hilo.
- Na kwa nini usibadili dini yako?
- Mimi nimezaliwa na wazazi wa Kihindu…kisha alitabasamu akasema: Sitaki kuwa Ghandi mwingine.
- Je utachukua zawadi hii ya pesa kwa sababu nimekupotezea muda wako mwingi?
- Asante, nakushukuru.

www.path-2-happiness.com

Joji alienda chumbani kwake akaanza kukusanya mabegi yake, wakati anajiandaa simu iliita, upande wa pili alikuwa Karimullah….

- Oh! Joji, mimi ni Karimullah.
- Oh! Karibu, Karimullah.
- Nimekuja jana sijakukuta nilitaka kukusalimia, niliacha mkataba wenye muhuri pale mapokezi kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini India, kama tulivyo kubaliana una safiri lini?
- Asante sana,. Nilitaka kuusahau nitauomba sasa hivi, safari yangu ni baada ya masaa mawili…
- Je ungependa nikupeleke au nikusindikize mpaka uwanjani?
- Nashukuru, ila nimekubaliana na Hoteli wanitafutie gari.
- Ok, sawa, nasubiri kopi ya mkataba kutoka Ubalozi wa India London wenye muhuri. Kwa heri.

Joji alirudisha mkono wa simu, na akawasiliana moja kwa moja na mapokezi akitaka kuletewa nyaraka zake…aliweka simu na kufikiri: Kwa nini hafurahishwi na Karimullah ijapokuwa hakuwa na kasoro anayoiona kutoka kwake, je ni kutokana na kufanana na bin Laden? Au ni kwa sababu ya umahiri wake katika kupatana? Au kwa ajili ya maneno kuhusu Mkurugenzi wake Kakhi? Au ni kwa jambo lingine asio lijua? Ni fikra za ajabu….au ni kwa vile sijasahau ulipuaji wa Treni mjini London Au ni kwa ajili labda ya athari ya vyombo vya habari? Cha msingi ni kuwa sifurahishwi na nae wala sijui ni kwa nini.

Aliacha kuwaza pale nyaraka zake zilipoletwa kutoka mapokezi…alizigeuza geuza na kuziangalia na zote zilikuwa sawa bila upungufu kama anavyotaka. Na hakuna kilichobakia isipokuwa muhuri wa Ubalozi wa India London. Aliangalia saa yake akakuta wakati wa kuondoka kwenda uwanjani umekaribia.

Aliwasiliana na mapokezi kwa ajili ya kujiandaa kutoka, na akawataka wawahishe gari nusu saa kabla ikiwezekana, ili kuepukana na foleni njiani au jambo lolote lisilotarajiwa.

Joji alikuwa akiangalia barabara za India kupitia dirishani, njia nzima imejaa masanamu, na alikuwa akijiuliza: Siwezi kuabudu au kutafuta ufumbuzi wa maswali yangu kupitia mawe na watu…naishukuru India iliyoniongoza katika njia ya kwanza ya safari yangu kuelekea kwenye furaha, ilikuwa safari yenye vivutio na starehe pamoja na yote niliyoyapitia.

NI KIPINDI CHA UGAIDI NA MISUKOSUKO

www.path-2-happiness.com

6

NI KIPINDI CHA UGAI-DI NA MISUKOSUKO

NI KIPINDI CHA UGAIDI NA MISUKOSUKO

(1)

Joji alirejea kutoka India, ni safari iliyokuwa nzuri sana, iliyojaa mafunzo, majadiliano na maswali, na haikuwa ni safari yake ya kwanza kikazi, lakini pamoja na hivyo ni safari iliyokuwa na mafanikio makubwa, ndio safari iliyofunga mikataba mikubwa kwa haraka zaidi.. na India ni miji ya kuvutia. Alipokuwa kwenye ndege aliitafakari sana safari yake kwa kina, kwa mapenzi yake na nchi ya India pamoja na watu wake, ila alichukizwa na kuwepo kwa itikadi mbaya za dini, huku akijiuliza: Hivi kupenda India ndio suluhisho la maswali yake? Au ni kwa ajili ya Katarina mwenye asili ya India? Lakini haijapita muda alirudi katika hali yake ya kawaida, na jeraha lake kwa Katarina bado halijafutika katika moyo wake.

Ndege iliwasili London na kukusanya mizigo yake, na kuelekea katika ukumbi wa mapokezi, na ghafla akaonana na Katarina pamoja na watoto wake waliokuja kumpokea, alijisikia ni mwenye furaha kupita kiasi huku akicheka na kucheza cheza na familia yake njiani…..

- Hujatueleza..mpenzi wangu, vipi India?
- Ni mji mzuri pamoja na watu wake ni wazuri pia.
- Huu ni uzuri wa macho yako.
- Kweli, ilikuwa ni safari nzuri maishani mwangu.
- Vizuri, nini umekipenda kupitia safari hii?
- Kila kitu kilikuwa kizuri, na cha ajabu hakuna hata kitu kimoja nimekiweka kichwani katika safari hii, na kwa nini? labda huenda kwa wema wa watu wake, au huenda ni kwa ajili yako mpenzi wangu…au labda ni kwa ajili ya kutiliana saini na kampuni kwa haraka zaidi sijui kwa kifupi tu nimevutiwa sana na safari hii

Alimgeukia mwanae Maiko…

- Unajua? Unanikumbusha Maiko wa India unafafana nae sana, halafu akatabasamu na kusema: lakini wewe mwanangu ni zaidi yake kwa uzuri…Ila wewe Sali, unanikumbusha uzuri wako sawa na uzuri wa Omela.

Muda ulikwenda sana mpaka walipofika nyumbani kwao, na hapo watoto walienda kulala vyumbani mwao, baada ya baba yao kuwaahidi kuwasimulia

www.path-2-happiness.com

safari yake kesho yake. Na Joji alienda chumbani kwake na kumkuta Katarina amejipamba kwa nguo nzuri akimsubiri….

- Omela uliosema ana fanana na Sali ni mzuri sana.
- Ndio kweli.
- Umejuaje? Je umesikia nasaha za Tom na Kakhi?
- Wewe ndio unatakiwa kunihabarisha kwanza, lini umeonana na Tom?
- Sijaonana nae, ila tulikutana katika hafla kanisani kabla ya siku mbili, kwa nini unalikwepa swali langu, ni nani Omela?
- Omela ni msichana tuliekutana nae hotelini ghafla tu, ni mzuri sana, amesema kuwa maana ya jina lake ni uzuri uliopindukia lakini niambie umekesha na Tom mpaka muda gani?
- Tumekesha mpaka saa za mwisho, lakini unadhani nitaamini kukutana nae ilikuwa ni kwa ghafla tu, halafu hujalisahau jina lake?
- Ndio, ilikuwa ni ghafla tu, na je unafikiria nitaamini mkesha wako kanisani ulikuwa mpaka saa moja asubuhi?
- Nani aliyekuambia kuwa tulikesha hadi asubuhi? Je unanishuku? Haikuwa ni bora mimi ndie niliyetakiwa kukufuatilia nyendo zako na wanawake hao wazuri?
- Nataka kulala samahani…..

Joji alilala kitandani na kuelekeza mgongo wake kwa Katarina kwa sababu maongezi yao yalichafuka, akaamua kulala….na Katarina nae alifanya hivyo hivyo kama Joji na kwa kumpa mgongo wake huku Joji akijiuliza, Je nilikuwa mkali? Je ni kweli alikuwa katika hafla kanisani? Je nimemvunjia heshima yake? Kisha akasema: Huenda nimemtia adabu na kumuadhibu pia nimemshuku kama alivyonishuku, kisha alijidai kulala mara baada ya muda akapitiwa na usingizi na kulala.

Asubuhi ilipofika aliamka na kukuta tayari Katarina amemuandalia chai na chakula anachokipenda …akasahau hasira za jana na kumfurahia.

- Karibu mpenzi wangu.
- Asante mpenzi wangu, halafu sijakupa zawadi yako, subiri kidogo nitakupa Rozari uliyoitaka.
- Nashukuru mpenzi wangu…ni nzuri sana, nilifikiri umesahau!
- Vipi nitasahau maombi yako mpenzi, hichi ndicho kitu muhimu zaidi nilikusudia kukuletea kutoka India.
- Roho mtakatifu alikuwa nawe akikulinda kwa kuchukua Rozari hii, vipi kuhusiana

na ufumbuzi wa maswali?

- Ilikuwa ni safari nzuri iliyopelekea kujua dini, fikra, na mila mbali mbali.
- Je umetembelea kanisa la Saint James? Limejengwa vizuri sana!
- Ndio, nimetembelea… ni zuri kweli nilifikiria Wakristo ni wengi India, lakini nimeshtushwa kwa idadi yao kuwa ndogo sana.
- Ndio umesema kweli, kwa masikitiko, watu hawakubali kubadili dini zao za Kihindu kwa wepesi mpaka kuwe na vitisho vya kigaidi, kwa ujumla Kanisa linafikiria kubadili mikakati yake kukabiliana na hali hii.
- Magaidi !! Unakusudia Waislamu?
- Ndio, ni wabaya na waovu.
- Ijapokuwa katika moja ya mikataba yetu kulikuwa na kampuni ya Waislamu, pamoja na wema wao, muamala wao mzuri, ukweli wao na maadili yao, ila kwa ukweli sijapendezwa nao, na miongoni mwao jina lake ni Karimullah na sijajua kuwa nini imetokea hivyo!
- Nafsi yako ni safi na nzuri inapenda mema, ni vigumu kuipenda nafsi yenye kuua na kupenda kuangamiza.
- Huenda ikawa hivyo, ijapokuwa walikuwa ni wazuri na wepesi katika kufanya nao kazi, lakini ni watu walioshikamana na maadili yao.
- Kwa nini, je hakuna Wakristo uliokutana nao?!
- HaaHaa: Ndio, nimekutana na Maiko mwenye dini, na sijui kwa nini nilipendezwa nae ijapokuwa tabia yake ilikuwa si nzuri!
- Mwenye dini bila tabia nzuri?!
- Ndio, ana dini sana lakini mwenye ubaguzi, pia hana tabia nzuri, kwa masikitiko Kakhi alimuomba anitafutie wanawake wa Kihindi na avuruge mikataba ya wafanya kazi, na yeye akakubali hilo.
- Oh!! Mtu wa dini halafu anakuletea wasichana!
- Ndio, kisha akaendelea kuelezea mpaka Katarina aliporidhika: Cha ajabu alishangaa kukataa kwangu.
- Anapora haki za watu na kunitaka nizini! Huu sio Ukristo ni lazima tupambanue kati ya Ukristo na Wakristo.
- Ndio, bila shaka huu ndio ukweli kwa hali zote mbili kwa upande mwingine kama ulivyosema: Ni lazima tutenganishe kati ya fikra za watu na dini, ili tusiinasibishe dini na makosa ya watu. Na kwa upande mwingine: Je hayakuwa matendo ya watu yanatokana na fikra na dini zao? Na kitu chochote kikizidi kupita kiasi ni

www.path2-happiness.com

dalili ya tatizo katika dini na fikra zao pia?
- Ndio, lakini rafiki yako Maiko ana tatizo lake kipekee.
- Huenda… kila wenye dini husema hivyo.
- Na vipi kuhusiana na ufumbuzi wa maswali ya dokta?
- Nafikiri majibu ya maswali hayo yako wazi kwa upande wangu.
- Kwa hivyo…tumesha maliza tatizo?
- Tumemaliza kujibu maswali ya dokta tu, lakini kujibu swali la Mungu ambae ameleta dini za mbinguni bado, kwani tupo njiani ili kufikiria lengo kuu na hapo tutafika katika furaha tunayoitaka.
- Endelea na utafika katika lengo mpenzi, na vipi umehakikisha ufumbuzi wakati nakusudia ufumbuzi wa kweli kutokana na dini za mbinguni?
- Jibu halikuhitaji kuwa na fikra nyingi, bali nimefahamu kupitia dini nyingi za Kihindi ambazo sio za mbinguni, na hazina tija kwa watu wake, na hata kwa binadamu wote, ni dini zilizowafanya wafuasi wao kwenda kinyume na asili ya mwanadamu sambamba na kupingana na uadilifu na hekima, pia nimegundua hata sisi huku Ulaya tunazo dini hizi na zipo kwa wingi ila hazina tija sana, kwa ujumla hizi ni fikra zangu na nitasikitiza fikra ya Tom nitakapo kutana nae.
- Lini utakutana nae?
- Baada ya siku nne, kisha akaendelea: Nimechelewa kazini kama nilivyokucheleweshe mpenzi wangu.
- Nimewaambia leo nitachelewa, nilidhani na wewe huendi kazini leo.
- Hapana, nitaenda japo kwa saa kadhaa ili kukabidhi baadhi ya kazi. Samahani mpenzi naomba idhini yako, tutaonana baadae nikirudi.

(2)

Joji alienda kazini.. na aliingia moja kwa moja kwa mkurugenzi wake Kakhi ambae alimkaribisha kwa hamu kubwa….

- Ni mafanikio yalioje makubwa uliyo yapata kupitia safari hii?!
- Mikataba ilifanikiwa kama ulivyotaka, lakini umejuaje?
- Maiko ametutumia ujumbe wa shukurani, na kutujulisha kuwa mikataba imekamilika… ijapokuwa Maiko ana dini pia anafanya vizuri kazini na anajibu maombi kwa matakwa ya watu…kisha alitabasamu: Ama huyu Mutwi Rahmaan ni mgumu kiutendaji, hebu niambie umefanyaje kutaamali nae?
- Tumekubaliana na kuwekeana saini kwa kugongwa mhuri wa Ubalozi wa

Uingereza nchini India, na umebaki Muhuri wa Ubalozi wa India London.
- Siamini macho yangu! Umekubaliana nae vipi?!
- Tumekubaliana nae kwa wepesi sana na kwa maendeleo mazuri, na anafikiria faida kwa wote, ijapokuwa yeye ni asiye na mpangilio wa mambo yake, ila aliniacha nifanye maafikiano na ndugu yake Karimullah, ni kazi iliyokuwa imepangwa vizuri, ijapokuwa sijafurahishwa.
- Siamini unayo yasema ijapokuwa mkataba huu hapa mbele yangu nauona, ama kwa upande wangu sio Mutwi Rahmaan au Karimullah wanao nivutia, sijui wanayaangaliaje maisha, kama kwamba wapo vitani daima, huenda ni kwa sababu ya tabia za imani yao kwani wao ni Waislamu. Hebu niambie habari za wasichana wangu? Je huoni haya kulala na wasichana wangu Joji?
- Sija lala na wasichana wako wala wengine.
- Kwa hivyo…..Maiko atakuwa ni mwenye kulaumiwa na hakuwa mwema kwako kama anavyokuwa kawaida yake na mimi?
- Kinyume chake alikuwa ni mkarimu sana kwangu, ila mimi ndio nimewakataa wanawake.
- Siamini mwenye akili kupoteza nafasi yake hiyo ya kipekee, nilitamani kusafiri kwa ajili ya kustarehe na wasichana hao, ni wazuri, laiti kama sio kikao cha idara, sijui ni lini utaishi maisha yako na kutumia fursa, na laiti ungemaliza mikataba yote ningesema hutasafiri tena, nini maana ya kusafiri India bila kustarehe na wazuri huko, je uliwapata waliokuwa wazuri zaidi kuliko anaokuletea Maiko na hivyo kuachana na wasichana wangu?
- Ndio, Omela alikuja hotelini na kunitaka, ni msichana mzuri sana, Haa Haa alicheka, lakini nilikataa.
- Sijajua unavyoyaona maisha na starehe zake?!
- Bali ni nini maana ya maisha? Na nini kuishi? Na kwa lipi umeumbwa? Ikiwa tunatumia umri wetu na muda wetu kwa kuzikimbiza nafsi zetu na kupata matamanio?
- Ha haa, ni muhadhara mzuri wa kumueleza dokta wako, niache mimi na haya, unapaswa kupanga mambo yetu baada ya mikataba hii, na kampuni inakushukuru sana kwa kupata mafanikio hayo.
- Nitaanza kazi ya kupanga na masiku machache nitamaliza, na mimi naishukuru kampuni, kwa kweli ilikuwa ni safari nzuri sana
- Pamoja na kuwa mimi sioni uzuri wa safari hiyo kwako, ila napenda kukwambia

www.path-2-happiness.com

subiri safari nzuri zaidi kama utataka.

- Safari nyingine tena?!
- Ndio, kuelekea miji Mitukufu.
- Miji gani hiyo?
- Japo mimi siamini kama ni mitukufu, ila wenye imani ya dini za mbinguni tatu wanaamini hivyo nayo ni: Yerusalem, jamaa zangu wote wapo huko na wananiita huko mara nyingi sana, lakini nahisi wao wameshikamana na dini kupita kiasi! Mama yangu ni Myahudi, ila mimi bado sijakubaliana na dini zote, kwa hakika shirika la usalama la Yerusalem limekubaliana na kuafiki mbinu zetu tulizowaonyesha baada ya kuwatumia, na ukitaka nenda wewe, na kama huendi nitaenda mimi, ijapokuwa napenda wewe uende, kwani wewe unaonekana una uwezo wa kufanikisha mikataba… unayo wiki moja kufikiria.
- Sawa, nitaangalia halafu nitakujulisha.

(3)

Joji alirudi kwake baada tu yakumaliza kazi zake…njiani kulikuwa na msongamano kupita kiasi, hali iliyopelekea kufika nyumbani baada ya masaa mawili na nusu badala ya dakika za kawaida anazotumia….alifika nyumbani akiwa mchovu na Katarina alimkimbilia kumpokea…

- Namshukuru Mungu kwa kufika salama, nilikuwa na huzuni juu yako.
- Sijui nini kimetokea njiani, leo nimechukua masaa mawili na nusu!
- Leo Metro ya chini ya ardhi ilisimamisha kabisa shughuli zake.
- Kwa nini?
- Kwa shambulizi la kigaidi ndani ya Metro, tunamshukuru Mungu halijatokea katika sehemu za vituo la sivyo wangekufa maelfu ya watu.
- Je kuna yeyote aliyeumizwa?
- Wameuliwa watu wawili mume na mke walioana kabla ya siku mbili na watu wawili wanaume, mwanamke mmoja na mtoto wamejeruhiwa.
- Ni mioyo gani walio nayo hawa Magaidi wa Kiislamu!

Joji alishika rimoti ili afuatilie habari kupitia Televisheni….

- Nini kinachokujulisha ni Waislamu? Acha tufuatilie habari katika Televisheni.
- Hakuna wengine wasiokuwa na mioyo zaidi yao waliofanya hivyo.

Joji alifuatilia habari katika Televisheni, mlipuko ulitokea kabla ya masaa manne takriban, na kila mchambuzi au mtangazaji waliafikiana kwamba ni magaidi wa Kiislamu waliotekeleza shambulio hilo, lakini bado taarifa kamili haijatolewa mpaka sasa hivi. Na hali ya Usalama ilikuwa tete nchini kote Uingereza. Na watu wote walikuwa wanakimbilia kurudi majumbani mwao, njia zote zikiwa zimefungwa.

- Inaonekana rai yako ni sahihi, waliotekeleza shambulio hilo ni magaidi wa Kiislamu, ijapokuwa taarifa rasmi bado haijatolewa mpaka sasa kuhusiana na hilo.
- Niamini, hakuna wenye mioyo migumu ila ni wao tu, na wanadai wanapigania dini juu ya hilo.
- Wanaua watu kwa jina la dini?!
- Ndio, wanadai hiyo ni Jihadi na ni ibada kwao ya kuua watu na kuwaadhibu, we angalia tofauti kati ya dini hii ya nguvu na uzuri na mapenzi ya Ukristo, Kristo anajitolea mwenyewe kufa kwa ajili ya wanadamu, na wafuasi wake hivyo pia. Ama wafuasi wa Muhammad hakuna walijualo isipokuwa kuua tu.
- Ninashangazwa sana na Waislamu hawa, na huenda ndio sababu iliyo nipelekea kutokuwa na mapenzi sana kwa Karimullah.
- Nashukuru Mungu umetoka salama kwao, hawajakuua wala kukulipua.
- Haahaa, fikiria Mutwi Rahmaan ajifungie milipuko halafu aniripue kwa hakika alikuwa ni mpole kwangu na amenipa zawadi ya mafuta mazuri ya Kihindi.
- Usiyatumie huenda yakawa na sumu, hakikisha kwanza kama yanatumika kwa ajili hiyo.
- Mimi sipendelei manukato, nimemletea Adam aliniomba nimletee, lakini nitahakikisha hayana madhara kwa rafiki yangu Adam.
- Hakikisha usalama wake kwanza kabla ya kumpa rafiki yako Adam, Hawa magaidi hawaaminiki katu.
- Umenikumbusha, sijamtembelea Adam tangu nimerudi na nilimuahidi kumtembelea baada ya kurudi.
- Je yeye ni Mprotestanti au Mkatoliki?
- Kumbuka sijui! Sijamuuliza wala hajaniambia, nitajaribu kuonana nae kesho na nitamuuliza…je tutakesha leo au tuna lala moja kwa moja?

www.path-2-happiness.com

- Mkesha mzuri na mpenzi mzuri zaidi.

Asubuhi Joji aliamua kutokwenda kazini, aliamua kufanyia kazi zake nyumbani kwa simu na intaneti, na metro haijafanya kazi isipokuwa kidogo tu, na msongamano bado upo. Aliwasiliana sana na Adam lakini simu yake ilikuwa imefungwa. Alifungua Televisheni ili kujua habari za mlipuko na magaidi…. Serikali ilifungua au kuziruhusu baadhi ya metro kufanya kazi. Na makundi ya Waislamu walishikiliwa wakiwemo Wahindi, Wapakistani na Waarabu pamoja na Waingereza wanaoishi London, na bado habari zinaashiria Waislamu wapo nyuma ya shambulio la Kigaidi. Na miongoni mwa watu majeruhi ni Muislamu muhindi alikuwa akielekea upande wa Metro hali ya kuwa ni mwenye kutiliwa shaka, pia kumekutwa kitambulisho cha mpakistani katika sehemu hiyo, ila upelelezi bado unaendelea… hata hivyo Serikali imewakumbusha raia wote na wanaoishi humo kukaa au kuchukua hadhari kwa mtu yeyote anayeweka kifurushi katika sehemu yoyote ya raia, au sehemu maalumu na hasa sehemu ikiwa ni Muislamu.

Joji alimalizia kutazama habari, na kuvaa nguo tayari kwa kumtembelea Adam mgahawani…hakumkuta kule na kumuulizia na kufahamishwa na mhudumu mwingine kwamba amepata likizo ya siku tano.

- Tangu lini ameanza likizo? Na unajua kwa sababu gani amechukua likizo?
- Amechukua kwa madai kuwa anataka kumalizia utafiti wake chuoni, na alipumzika tangu siku tatu zilizopita.

Joji alienda nyumbani kwa Adam na kugonga mlango bila kufunguliwa, na kuweka ujumbe mlangoni unaosema kwamba: 'Nimekuja lakini bahati mbaya sijakukuta', kisha akarudi nyumbani kwake…. Alimkuta Katarina akifuatilia habari.

- Je kama lolote jipya kuhusiana na shambulio la Metro?
- Hakuna jipya, bado wanamtafuta gaidi wa Kipakistani, ila hofu imetanda kwamba London itashambuliwa tena kwa shambulizi jingine.
- Natamani wamshike leo ili watu watulie na roho zao, nyoyo gani wanazo hawa?!
- Je umekwenda kazini leo?
- Hapana, bado njia za Metro zilifungwa kwa muda wa asubuhi, ila nilimtembelea rafiki yangu Adam sijamkuta, yupo katika likizo ya utafiti wake.

- Je kesho utakwenda kazini?
- Ndio… Bila shaka, nina baadhi ya kazi, halafu nina ahadi ya kukutana na dokta Tom.
- Safari hii una majibu maalumu na ya wazi kwa dokta?
- Ndio, nahisi uwezo wa majibu ndio ulionisukuma kwa mara ya kwanza na hii ni mara ya pili.
- Upo sahihi siku zote, roho mtakatifu yupo nawe na kukupa nguvu.
- Najua hata maswali yake mapya yatakavyokuwa.
- Unajua?!
- Naam, inaelekea sina uchaguzi wa kutosha, na sijui ni mbinu za Tom kutaka kuniingiza au imetokea tu ghafla, au ni uwezo wa roho mtakatifu kama usemavyo?
- Vipi ?
- Mwanzo majibu yalikuwa wapi tutayapata, na ilikuwa wazi sana kwangu kwamba hakuna pa kuyatoa ila kwa muumba pekee. Na wazo la kupinga ni wazo la fujo na vitu visivyokuwa na tija, je yawezekana kuunda utaratibu unaotokana na fujo na vipi kiumbe aliyeumbwa atajua kwa nini ameumbwa? Ukanaji dini unakwenda kinyume na akili, maumbile na dini hata kama itamchanganya msomi mwenye fikra ya kustaarabika. Ilikuwa ni kujiuliza baadaye nani muumba? Na tumezigawa dini na fikra za watu kuhusu muumba katika makundi mawili: Dini za kidunia na dini za mbinguni. Na ilikuwa wazi kwangu na hasa baada ya safari yangu India ni kwamba dini za kidunia bado hazijafaulu kwenda sambamba na maumbile ya kibinadamu pamoja na wafuasi wao hata kama kuna maendeleo ya wanadamu, bali ni upotevu wa hali ya juu usioendana nao na kwa sasa swali lililopo ni: Je dini za mbinguni zinaweza kutupa majibu muwafaka zinazoendana na maumbile ya mwanadamu kisomi?
- Je sijakwambia Ukristo ndio suluhisho la mwanadamu?
- Na Vipi kuhusu Uyahudi na Uislamu?
- Je mpenzi wangu huenda ukawa Muislamu ukiwa umevalia milipuko katika Metro za chini ya ardhi?
- Haa Haa huenda nikawa Myahudi kama Kakhi ambae hashughulishwi na lolote isipokuwa mali na mapenzi.

www.path-2-happiness.com

(4)

Kwa muda huo wote, Joji alijaribu kuwasiliana sana na Adam lakini simu yake ilifungwa hali iliyopelekea kujisikia vibaya, alitaka kukutana nae kabla ya kwenda kwa Dokta… akamtumia ujumbe unaosema: "Nimerudi kutoka India na nimekuletea zawadi, naomba kukuona, je unaweza kunipigia?" Lakini hakupata jibu lake….

Muda wa kukutana na dokta ulifika, Joji alikwenda kliniki, Baraad alikuwa mapokezi, alipomuona Joji alimkaribisha…

- Vipi habari za India pamoja na wasichana wao?
- Ni mji mzuri sana na maajabu…samahani naomba kumuona Tom muda wangu umefika.
- Inaelekea una haraka, au hutaki kuongoe nami..hakuna shida!
- Je unaniruhusu kuingia kwa Tom?
- Ruhusa karibu..karibu, kumbuka utarudi kwangu siku moja.

Joji aliingia kwa Tom na alikaribishwa kwa mapokezi makubwa kupita kawaida, Tom alifurahi sana kwa kumuona na kumwambia Joji hivi:

- Nimefurahi sana kukuona na mara ngapi nilikusubiri kukuona na kupata ushauri wako na majibu yako.
- Ulikuwa una subiri maoni yangu na majibu yangu?!
- Unaweza kuona mshangao kile ninachokisema lakini huo ndio ukweli wake… ndio inaonekana falsafa yako imeafikiana na utafiti wangu wa kielimu pamoja na utafiti wangu wa kidini, kwa hivyo naenda kanisani kuhudhuria baadhi ya vipindi vya elimu ya dini…kisha alitabasamu na kusema: kwa ujumla achana na hayo. Je umeachana na kila dini kama ulivyo tarajia?
- Ndio, bila ya shaka…
- Vizuri kama nilivyotarajia.
- Acha nikamilishe (samahani) nimeziacha dini zote za duniani.
- Una maanisha nini?
- Nina maana kuwa lazima tutafute majibu makuu kuhusiana na Mungu muumba, kama zinavyosema dini za mbinguni.

- Kwa haki gani kuzithamini dini za mbinguni kuliko za duniani?
- Sio mimi niliofanya hivyo, bali wenye dini wenyewe wanajua kuwa dini zao bado hazijakamilika na wanaendelea kuziboresha na kuziendeleza.
- Kuziendeleza?!
- Ndio, wanaziboresha kwani wanajua ni za watu wenyewe na vipi watajibu maswali mazito ya watu mfano wetu, na pengine sisi tuna wazidi kielimu kuliko wao, na vipi binadamu atajua maisha wanayoishi bila muumba alie waumba, na haiwezekani wajiumbe wenyewe, na hata wanyama tu hawawezi, je huoni dini hizi za duniani ndio chimbuko la ukafiri katika ulimwengu?
- Unasema kama vile dini za mbinguni hazina shaka!
- Ndio, ni kweli….sijajua swali lako ni katika kuchagua kati ya dini za mbinguni au duniani, na uchaguzi huo sio wa shaka.
- Wewe ndio ulioweka chaguzi hizo na sio mimi.
- Na wewe umekinaishwa nazo na umerekebisha swali, kwa ujumla sisi tunakwenda njia ya sawa ya kielimu pamoja na kutopendezwa kwangu, na wakati wowote ule tutakuwa tumeacha kufuata dini za mbinguni, na wakati huo tatarejea katika ukafiri wa kupinga dini na Mungu.
- Sidhani kama hilo linatimia, ukafiri ni njia ya dhulma yenye kutisha haimfikishi mtu katika furaha ya kweli, na kwa hivyo makafiri wengi maisha yao yameishia kwa kujinyonga.
- Haa haa, una maanisha na mimi nitajiua muda sio mrefu?! Ni kwa nini sasa wenye dini nao wanaamua kujiua?
- Nategemea wewe unajua giza lililotanda katika ukafiri, na ndio maana umeanza utafiti wako kuhusiana na dini, ama swali kwa nini wenye dini wanajiua? Ni swali ambalo mimi najua jibu lake sio la lazima sana.
- Cha msingi kwa sasa hivi ni kufanya utafiti kuhusu dini za mbinguni, ikiwa tutafikia kuona kuwa hazitupi majibu kuhusiana na hilo ni lazima tupate ufumbuzi, ijapokuwa mimi kafiri ila nimetosheka kwa yale unayosema kuhusiana na ukafiri, isipokuwa sina budi na uchaguzi huo na sitoacha uchaguzi wangu moja kwa moja.
- Zimebaki dini tatu tu.
- Je tutaujadili Uislamu wa vitisho tena?
- Sijui, kwa sababu wewe hutaki kuachana na uchaguzi wako?!

www.path-2-happiness.com

- Ndio ….umesema kweli, nadhani wewe utafikia hatua ya kujificha katika milima ya Torabora kama bin Laden
- Ijapokuwa nauchukia sana ugaidi, na hakika kuwa sio akili wala dini wala moyo, isipokuwa njia ya elimu yenye uadilifu ndio itakayotufikisha huko.
- Bila kupoteza wakati, uamuzi ni wako wa kuchagua iliyokuwa bora kati ya dini tatu, napendekeza kuitanguliza ile iliyoridhiwa na wengi.
- Dini zote tatu, tumekubaliana.
- Nakusudia Uyahudi, kwani Nabii Mussa anakubaliwa na Wayahudi, Wakristo na Waislamu.
- Nimeelewa, nadhani ni vizuri kuangalia upande mwingine kabisa.
- Vipi tena ewe Mwanafalsafa?
- Kwamba Waislamu wanamuamini Musa, Issa pamoja na Muhammad kinyume chake Wakristo hawaamini wengine isipokuwa Musa na Issa na Wayahudi hakuna wanayemkubali isipokuwa Musa tu.
- Ni mtazamo sahihi kabisa wa kutofautiana, ila mimi bado nashauri ya kwamba tuanze na Uyahudi kwani ndio dini ya mwanzo ya mbinguni.
- Sawa nakubaliana na wewe kabisa.
- Ni matarajio yangu uwe na wakati wa kutosha kuangalia kila dini, kwani wewe unazungumzia historia na falsafa, fikra, dini na uhalisia wake kwa wakati mmoja na ukimaliza kutafiti Uyahudi usiuponde au kuunga mkono mpaka utafiti Ukristo na ukimaliza kuutafiti Ukristo, utafiti na Uislamu, halafu alitabasamu na kusema, ikiwa una lengo la kwenda huko Tora bora!
- Vizuri, swali langu ni hivi; ni njia ipi utatumia kujua dini hizi?
- Kusoma pamoja na utafiti ndio njia kuu isiyoisha, na ikiwa utajuana na wanazuoni wa dini hizi itakusaidiana sana. Natamani ungesafiri kwenda Tel Aviv kama ulivyoenda India ili ujue vizuri Uyahudi kwa ukaribu.
- Na cha kushangaza ni kuwa kuna safari fupi ya kuelekea Tel Aviv ila bado sijaamua kwenda mpaka sasa hivi.
- Bado sijajua matatizo yako kwani umetoka India ila kama utapata wasaa wa kwenda Tel Aviv itakusaidia sana na ukitaka kuujua Ukristo uende Roma, na Uislamu uende Makka ila magaidi hawatakuruhusu kuingia humo!

- Maneno yako yamenitia hamasa ya kusafiri kuelekea Tel Aviv ila nitaangalia kwanza halafu nitakujulisha nilichoamua.
- Inaelekea una bahati, kwani wanawake wa Kiyahudi, ni wazuri sana ni wanawake waliochanganya damu zao kwa kila maumbile, baada ya kustarehe na Wahindi na sasa ni zamu yako kustarehe na wanawake wa Kiyahudi, bahati iliyoje kuipata kwako!

Joji hakufurahishwa na maneno ya Tom na aliamua kumtia hasira kwa kumwambia….

- Kwa nini usistarehe na wagonjwa tofauti tofauti, na kwa nini usistarehe na wanawake wenye kupenda kukesha kwenye sherehe ili kutimiza au kukamilisha utafiti wako?!
- Nimekuelewa sana unacholenga, Katarina ni mzuri na uzuri wake ni kuwa anajitolea kutumikia dini yake, usigeukie kulia wala kushoto.
- Au huenda unapenda kustarehe na wanawake wa Kihindi na ndio maana unajilazimisha kufanya utafiti wako usiku kucha mpaka asubuhi.
- Pia nimekuelewa sana unachomaanisha, mpaka asubuhi kwa sababu ya moto uliozuka na kuunguza jengo karibu na kanisa. Halafu Tom alimgeukia kwa hasira na kusema: Ijapokuwa nina historia ndefu kuwa na mahusiano na wanawake ila kwa Katarina ni tofauti kabisa hana upuuzi huo zaidi ya kutangaza ukatoliki wake.
- Unataka kuniambia katika kukutana kwenu na kukesha kwenu mnatafiti dini, Ukristo na Imani tu?!
- Hapana, Kanisa linatumia sherehe ili kuwavuta watu na kuwaelimisha dini.
- Na kupitia sherehe hizo ndipo kunazuka visa vya mapenzi.
- Ndio umesema kweli, lakini Katarina pamoja na uzuri wake hayupo hivyo lengo lake lipo wazi, nalo ni kulitumikia kanisa na kuwapa elimu zaidi watu kumuamini Kiristo.
- Mh mh, Na juu ya hilo mnakunywa pombe pamoja ili imani izidi na kujitolea mhanga kwa ajili ya binadamu?!
- Ijapokuwa unatumia kauli sio nzuri zinanichukiza ila mimi nitaeleza uzuri wa Katarina kwangu, hakika ameuvuta moyo wangu kwa mara ya kwanza tangu miaka kumi na tano. Kweli nimekunywa pombe katika sherehe ya kanisa na mimi ni mpingaji ila nimeshangazwa na Katarina kwa kunywa pombe ijapokuwa ni

www.path-2-happiness.com

mfuasi wa dini.

- Nini kinachotokea pindi imani ilipofika kwenye lengo lake, na kujitoa muhanga kwa ajili ya wanadamu?!
- Acha nisema kweli tu, pamoja na Katarina kutaka kuzidisha kunywa na mara tu baada ya kumaliza tatizo la moto jirani, alichoka na kunywa kupita kiasi.
- Na wakati huo mkakesha na mkajichanganya pamoja!
- Joji, hakukuwa na kitu chochote cha aibu kati yetu, isipokuwa baada ya Katarina kunywa sana alijisikia kizunguzungu hali iliyonipelekea kumchukua mpaka katika gari na kumsubiria mpaka azinduke, na ndio sababu iliyotufanya kuchelewa mpaka asubuhi, na akanishukuru sana na huku akishangazwa na hali hiyo, na ikadhihiri huruma yangu kwake na kumbusu, halafu nikajisikia nimekosea kwa tendo langu hilo na yeye hakufurahishwa kwa hilo pia.
- Vizuri ni mapenzi mazuri na ni wajibu wangu kukupongezeni!
- Tulikuwa naye muda mrefu rafiki yake na jirani yake Sali, na unaweza kuthibitisha haya nisemayo kutoka kwake, pia na katika mtandao wangu wa facebook; kuna picha zote tulizopiga usiku huo, sikulazimishwa kusema yote hayo, ila nimependelea niwe muwazi kwako ijapokuwa kauli yako sio nzuri na sijajua kwa nini nataamali na wewe kwa njia hii, labda na mimi najihisi nina tatizo kama lako au tofauti na hilo.
- Tatizo hilo hilo langu?!
- Hakika utashangaa kile ninachokuambia ila nina jambo linanishughulisha moyoni mwangu tangu zamani, na tangu mwaka sasa limezidi na bado sijajua nini sababu, lakini cha kushangaza tangu umerudi na majibu pamoja na utafiti wangu wa dini tatizo hilo limeanza kupungua na sijui ni kwa nini?
- Je ni kwa sababu ya kuuliza na kuyajibu au ni kwa sababu nimetembelea kanisa na kuamini au vyote hivyo? Kuhusiana na dhiki na huzuni. Je zinatoka wapi? Na vipi maswali yanakupata ambayo yana kuvunja vunja?
- Yameanza kupungua sana, labda ni kwa sababu ya kujishughulisha kutaka kuyapatia ufumbuzi wake kutafuta njia ya furaha na safari zangu kuondokana na matatizo yanayonisumbua moyoni mwangu.
- Maelezo haya ni mazuri ya “Katika kufikia kwenye furaha”.
- Ndio, njia ile aliyoniambia kikongwe niliyekutana naye njiani, halafu akaitilia

uzito yule mpokeaji wageni pale penye mgahawa.

- Kila mtu anataka kufuata njia ya furaha na nafsi inaifikiria, ila ukweli utabaki hivyo hivyo.
- Nini unakusudia?
- Kila mwenye dini au dhehebu au kundi wanadhani wapo katika njia ya kuelekea furahani, na wao tu peke yao wapo katika njia hiyo! Kisha alitabasamu na kusema: Hii ni dharau ya hali ya juu
- Lakini bila shaka mimi na wewe hatupo katika njia ya furaha, vinginevyo tusingekuwa katika hamumu hii na ghamu hii ambayo tunaishi nayo!
- Lililo muhimu, niache nifanye majumuisho kwa yale tulio simamia kwayo…. Ni kwamba furaha ya kweli ndio itakayojibu maswali makubwa, na kuwa Muumba ndie atakayetupatia majibu ya maswali na sio binadamu; kitu kinachofuta kabisa wazo la kukana dini, na Muumba huyu ndie mwenye dini za mbinguni na sio za duniani, na sisi ndio tuamue ni dini ipi ndio dini sahihi.
- La msingi wafuasi wa dini hii ya mbinguni ndio walio katika furaha ya kweli, na naamini mimi naelekea huko kama Katarina alivyo sema tangu mwanzo, ila mimi sitaki kufanya haraka na kufunga mjadala, ukizingatia kwamba na yeye amepunguza kuandamwa na maswali magumu na vizuizi vyake, na ukizingatia nachukua uangalizi wa kina na wepesi juu ya mambo magumu.
- Hapana shaka kwamba Katarina mwenye kujitolea muhanga kwa kila kitu katika kufikia njia ya Mola anastahiki kujua ukweli, lakini acha kwanza tutimize malengo yetu, na nasubiri mpaka utakaporudi kutoka Tel Aviv ili tuendelee na hayo.
- Tumekubaliana, nimekuchelewesha leo…na kuomba niondoke na kama muda upo tutaonana baada ya wiki mbili kama nitasafiri na ikiwa sijasafiri tutaonana wiki ijayo.
- Ila makubaliano yetu ni baada ya wiki mbili ili upate kuwaelewa Wayahudi na jitahidi kwenda miji hiyo mitukufu ili uzidishe ujuzi wako.
- Fikra nzuri ya “miji mitukufu”!
- Ndio… ni miji mitukufu kwa kila dini za mbinguni na mara nyingi vita na mivutano ya dini hizo zinatokea humo.
- Nitajitahidi kwenda, pamoja na kujaribu kupangilia mambo yangu.

Joji aliachana na Tom na nje alimkuta Baraad akimsubiri na usoni mwake

www.path-2-happiness.com

akiwa na tabasamu lenye dharau.

- Vipi habari ya Katarina? Je utampeleka Torabora?
- Tora bora?!!
- Usiwe mwepesi wakuchezea maneno!
- Nini unakusudia?
- Sikusudii chochote, Katarina na Tom wote ni wazuri wenye mvuto wa kupendeza, na unaweza kusafiri, uwe imara na usiwe dhaifu.

Joji hakumjibu na alitoka akiwa na hasira, alikuwa makini kwa maongezi yao kati ya Tom na Baraad. Je unadhani Baraad amesikia maongezi yangu na Tom? Au yeye ni katika wale wanaoitwa telepathia? Au ni nini?!

(5)

Joji aliendelea kuwasiliana na Adam lakini bila majibu yoyote yale, wasiwasi na hofu zilianza kumuingia Joji, alikwenda nyumbani kwa Adam zaidi ya mara moja lakini hakumpata…Katarina aliona wasiwasi aliokuwa nao Joji…

- Unaonekana ni mwenye dhiki..kimetokea nini?
- Sijamuona rafiki yangu mhudumu Adam, na nimewasiliana nae sana, na nimekwenda kwake mara nyingi!
- Ulikuwa unahofia isije ikawa imempata tatizo kutoka kwa magaidi, nilipokuona ghamu nimekuogopea sana, inaelekea unampenda sana Adam?!
- Pamoja na upole wake na hali yake ya kawaida lakini amenisaidia sana, na kwa kweli najihisi utulivu sana kwa mazungumzo nae.
- Wenzake kazini wanasemaje?
- Yupo likizoni kwa ajili ya utafiti wake wa chuoni; kwani yeye ni mwanafunzi anasomea mambo ya dini kama nilivyokujulisha hapo kabla.
- Lini likizo yake inakwisha?
- Itakwisha kesho kutwa, hata hivyo nina hamu sana ya kukutana nae, ili anishauri baadhi ya mambo..hata hivyo nilitaka kukushauri wewe kuhusu lengo la safari yangu Yerusalem au wanapopaita Tel Aviv.
- Aah unakusudia nchi takatifu?!
- Ndio; huenda nikaenda kwa ajili ya kutiliana mkataba na shirika la ulinzi la

Kiyahudi.

- Iweje hivyo nawe sasa hivi unaingia kutoka safarini, nahofia usije ukapata shida na machovu kwa wingi wa safari
- Sitopata tabu, hata hivyo nilitamani kukaa nawe na Maiko na Sali kwa muda mrefu, na sikuwa ni mwenye kuhamasika na safari hii hadi nilipokutana na Tom leo hii ambae alinihamasisha sana kusafiri.
- Kwa nini?
- Anasema: Utaujua Uyahudi kwa ukaribu zaidi.
- Katika hili amesema kweli, bali dini zote tatu za mbinguni utazijua; hiyo ni ardhi iliyobarikiwa kwa dini zote za mbinguni.
- Nini rai yako wewe?
- Sijatanabahi na nukta aliyoizungumza Tom, ukiona utapata faida safari na nitafurahi kwa hilo kwa ajili yako na nitakusubiri mimi na wanangu kurudi kwako.
- Alichokisema Tom kinaingia akilini, hata hivyo bado sijahamasika sana, na hata ikiwa hivyo nitaifanya iwe fupi sana.
- Wewe ni mwenye bahati sana umesafiri katika nchi ya maajabu, na sasa unataka kusafiri katika nchi muhimu sana ya vyanzo vya vita vingi na mapambano!
- Bali mimi ni mwenye bahati ya kuwa na mke mzuri.
- Ninapenda kukupa zawadi yako
- Zawadi gani hiyo?
- Utakaporudi na kupumzika kidogo, tuchukue likizo na tusafiri sote kwenda Roma, ili ukamilishe safari zako zote; yaani baada ya nchi za maajabu na kisha nchi ya mapambano, na baada ya hapo nchi ya makanisa, ili uweze kuufahamu ukatoliki katika makazi yake ya asili, na ili uweze kufikia unayoiita njia ya furaha.
- Na baada ya hapo nitakuwa nimeshaujua ukristu kuliko anavyotaka Tom, kisha akaendelea: Inaelekea kuwa kesho nitamjulisha Kakhi kuwafiki kwangu safari hii, natamani nisisafiri hadi ile hali ya hatari inayoikumba nchi itakuwa imekwisha kwani inasumbua sana, na kadhalika kuhakikisha hali zenu ndio nisafiri, au hadi wale magaidi majambazi watakapohukumiwa.
- Bado uchunguzi unaendelea kwa yule Mpakistani ambae ndie wanayemdhania kuwa amelipua, wameshawakamata marafiki zake wote na wenye kumzunguka.

www.path-2-happiness.com

- Watakwenda wapi? leo au kesho wote watakamatwa, ni kiasi gani nachukizwa na watu hawa magaidi!

Joji alipofika tu alielekea katika ofisi ya Kakhi, ili amjulishe kuwa amewafiki safari ile, na matamanio yake kuwa safari iwe fupi na ikiwezekana isiwe zaidi ya siku nne tu…

- Siku nne zinatosha kabisa.
- Je majukumu yangu yako wazi yanafahamika?
- Ndio, shirika la Yerusalem la ulinzi na usalama ndilo linalotaka kuingia mkataba nasi, nao ni mkataba wa ulinzi wa kielektroni, tumekubalina nao katika kila kitu takriban.
- Kwa nini usiwatumie mkataba kisha wakasaini kuliko mtu kusafiri.
- Mhusika wao wa teknolojia ana maswali mengi; ni maswali ya ndani yenye kutaka maelezo ya kina, kadhalika kwa ukweli wanahitaji kukinaishwa; hadi sasa dada huyo mhusika ndie pekee aliyegoma mkataba kusaini, maamuzi ya mwisho yanategemea kukubali kwake. Yeye ndie atakayepitisha.
- Kama ni hivyo inabidi nijue kadhia zote za teknolojia kwa undani zaidi, na inabidi nisome maelezo yanayohusiana na upinzani wake katika maandikiano yenu naye.
- Ndio, hili ni muhimu mno, na mwishowe watasaini mkataba watake au wasitake.
- Unaonesha kujiamini kabisa!
- Ndio, kwa sababu nyingi; Kwanza: Mayahudi wana Phobia na magaidi wa Hamas, na uwezo wao hata katika teknolojia, na kwa hivyo wataingia mikataba na sisi au hata na wasiokuwa sisi.
- Wana haki zote, magaidi hawana mioyo, unaonaje tuliyonayo hapa London?
- Lakini Mayahudi ni magaidi zaidi kuliko Hamas na wengineo!
- Huenda ikawa hivyo, sijui, ninachokijua ni kuwa magaidi wa London walitamani wafe watu wengi sana kama sio mamia basi maelfu bila ya sababu yoyote ile kutoka katika moyo, au dhamiri au dini!
- Achana na ugaidi kwa sasa, ama sababu ya pili: Ni kuwa Levi ndie mhusika wa kitengo cha teknolojia cha shirika la kiyahudi na mkuu wake ni Myahudi vile vile.
- Sijafahamu? Kwa nini kuwa kwake myahudi pamoja na mkuu wake ni myahudi ina maana watasaini wote mkataba.

- Pamoja na kuwa dini yao ni Uyahudi nawajua walivyo, mkuu wake wa kazi anaitwa Benjamin ambae anataka kuingia mkataba pamoja nasi kwa maslahi maalum, wala huyu dada mhusika wa teknolojia hawezi kumkatalia akitakiwa kufanya hivyo, vinginevyo hatompa mahitaji yake; dada yule anamtii sana bosi wake kwa ajili ya dini.
- Kwani na wewe sio Myahudi?!
- Ndio, mama yangu ni Myahudi; na kwa hali hiyo mimi vile vile ni Myahudi, na hii ni sababu ya tatu; na kwa hivyo wamewafiki kuingia nami mkataba, hata hivyo mimi ni msekula dini haina maana kwangu ila kama itaniletea maslahi ya mali na starehe, ha ha ha, kwa fikra ni kuwa Levi ni msichana mdogo tu ana umri wa miaka 25 tu, na ni miongoni mwa wasichana wazuri kabisa duniani, na ukitaka kustarehe nae ongea na Benjamin na atakuletea siku hiyo hiyo. Ama Benjamin nimeshakubaliana nae yeye binafsi kiasi cha Dola 100,000 yake binafsi ili awafiki kusaini mkataba.
- Je 100,000 Sio nyingi sana?!
- Nyingi sana, lakini niliongeza thamani ya mkataba kuwa 150,000 Dola, na akakubali ili muradi apate cha kwake.
- Ni mmomonyoko wa kimaadili kiasi gani huu! Hii ni hiana ya shirika na kwa nchi, hii sio biashara!
- Mali kwetu ni kitu kingine bwana, sisi mayahudi ni wafanya biashara wa kweli, na ndio unaona tunatamalaki biashara ulimwenguni, hakuna anayeweza kushindana nasi katika mali na biashara yeyote.
- Maneno yako yananiogofya kuhusu dini ya Uyahudi, na haiba ya wayahudi.
- Ha ha ha, wanasema: Ukimsalimia myahudi rejesha mikono yako baada tu ya salamu, ukiikuta ipo kamili, basi hakikisha kuwa bado unajua kuwesabu sawa sawa, cha msingi ni kuwa mpe Benjamin laki moja na utaona mambo yanavyokwenda kwa wepesi.
- Tutamaliza mazungumzo yetu na kuhusu muwafaka na mazingira yake baada ya kuusoma mkataba na maelezo yake.
- Vizuri, weka nafasi yako baada ya wiki kutokea sasa, na wiki hii kwa pamoja tutamaliza maafikiano yetu na vikao vyetu.

Joji alijikuta akiendelea kusoma maelezo ya mkataba na vipengele vya

www.path-2-happiness.com

maafikiano, kadhalika na yale maelezo ya fani mwisho wa muda wake wa kazi, alitoka hali ya kuchelewa na ilhali bado hajamaliza kazi yake, kwa muda wote huo alijaribu kumpigia simu Adam mara nyingi na kila akipiga simu yake ilikuwa imefungwa. Alirejea nyumbani kwake na akaendelea kufuatilia habari; alikuwa anatamani yule Mpakistani akamatwe kabla ya safari yake.

Alisikia kwenye taarifa ya habari kuwa kuna uwezekano wa mhusika mwingine kabisa wa mlipuko, na kuna watu wengine wapya waliokamatwa, na wote hawahusiki na ugaidi wa Kiislamu, bali wahusika ni harakati za SIITA iliyoparaganyika. Katarina alikaa pembeni yake akiulizia kipya kilichojiri..

- Ni kitu cha kushangaza habari hizi za kigaidi kuwa kuna uwezekano wa mhusika mpya wa shambulio hili la ulipuaji!
- Haya ni maneno ya kupoteza malengo tu, hawafanyi hivyo isipokuwa Magaidi wa Kiislamu tu.
- Harakati za SIITA zinazotaka kujitenga ndie mtuhumiwa mpya..
- Huenda ikawa ni mbinu ili magaidi wasogee kisha waanze kuwasiliana; ili waweze kumkamata yule Mpakistani, na ndio maana wakatangaza hivi.
- Katika ulimwengu wa siasa kila kitu kinawezekana!

(6)

Joji alishughulishwa katika siku iliyofuata kwa ajili ya safari yake, na kutayarisha mikataba, alikuwa kila mara akiwasiliana na Adam, lakini simu yake ya mkononi ilikuwa mara zote haipatikani, alimtumia barua pepe na barua nyingine katika face book yake. Kulingana na mazungumzo ya mhudumu mwenzake kazini Adam alitarajiwa kuanza kazi leo hii. Alitamani sana kumuona Adam kabla ya wakati huo; kwake ina maana kubwa..

Alipomaliza muda wake wa kazi ofisini …Joji alipitia kwenye mgahawa, na akamuulizia Adam..lakini hakumpata!

- Hakufika leo.
- Je likizo yake haijesha?
- Ndio imekwisha, lakini hakufika kazini, wala hakufanya mawasiliano yoyote, na hii si ada yake kabisa!
- Je unatarajia atakuja lini?
- Sijui, alitarajiwa kuanza kazi leo, asiyekuwepo huwa ana udhuru.

- Asante, akija mjulishe kuwa Joji alipita kumuuliza zaidi ya mara moja.
- Vizuri, vizuri.

Joji alirejea nyumbani kwake, lakini akiwa na hofu kuhusu Adam, kutoweka kwake ghafla kumemtia wasiwasi, hakuna njia iliyobaki ya kuwasiliana nae isipokuwa ameitumia: simu, barua pepe, face book, kumfuata kazini, hata nyumbani kwake mara nyingi, lakini zote hakukuwa na athari yake!

- Karibu mpenzi wangu, je, umeonana na sahibu yako Adam?
- Sijampata, wala hakwenda leo kazini pamoja na kuwa likizo yake imekwisha!
- Nataraji isiwe imempata ajali ya ugaidi.
- Nami nataraji hivyo, je kuna mpya? Je, wamemkamata aliyelipua?
- Kwa bahati mbaya..habari zilizopita hivi punde zinazungumzia kuachiwa huru watuhumiwa wote Waislamu leo hii!
- Wamewaachia maharamia!
- Wanasema kuwa uchunguzi umebaini kuwa mlipuaji ni miongoni mwa wanaharakati wa SIITA waliojitenga.
- Ha ha ha, umenikumbusha aliyoniambia Karimulah mtu ambae sikupendezwa nae: “Gaidi ni yule ambae hakubaliani nanyi, lakini akikubaliana nanyi huwa ni shujaa” huenda akawa ni mkweli..!
- Bado sijakinaishwa, na naamini ya kuwa aliyelipua ni Mpakistani, je hawakusema mwanzo kuwa kamera zilichukua picha yake?!
- Huenda Karimullah akawa ni mkweli, je walimkamata mtuhumiwa huyo mwanaharakati wa SIITA?
- Ndio, na wanasema kuwa ni tukio la kisiasa na sio la kigaidi.
- Kuwabadilisha watuhumiwa tumefahamu hilo, ama kubadilisha tukio kutoka ugaidi kwenda jinai hapo hatujafahamu?!!
- Anakuwa ni gaidi ikiwa mtekelezaji wa tukio ni Muislamu.
- Ha ha ha, haya ndio maneno hasa aliyosema Karimullah mwenyewe, cha msingi ni kuwa London imekuwa ya salama baada ya kukamatwa kwa majambazi.

Simu ya Joji ililia, akaipokea haraka, alitamani mpigaji awe ni Adam, na kweli alikuwa yeye Adam, alipokea kwa hamu.

- Mwishowe Adam, nimeingiwa sana na hofu kwa ajili yako.
- Ha ha ha, nilikuwa katika jukumu fulani dogo na nimemaliza sasa hivi.
- Je umemaliza utafiti wako?
- Bali imekuwa ya kina zaidi, achana na hilo vipi hali yako?

www.path-2-happiness.com

- Katika hali nzuri, nataka kukuona, je nije kwako sasa hivi?
- Nimechoka katika kazi niliyoimalizia, unaonaje ukaja ninapomaliza kazi zangu kesho?
- Sawa, tumekubaliana, nitafika kwako kabla ya saa kumi na moja, nitakualika katika chakula cha jioni, katika hoteli ya furaha.
- Sawa, nitakusubiri kesho.

Joji alikata simu, na hisia za furaha zikamrejea tena..

- Unaelekea una furaha baada ya kuongea na mhudumu!
- Ndio, sijui kwa nini hivyo, katika mazungumzo yake napata hisia za ukweli katika mazungumzo yake, upole na umakini wake.
- Je, ni Myahudi au Mkiristo? Au ni Mkatoliki au Mprotestanti?
- Sijawahi kumuuliza hilo, nikikutana nae nitamuuliza swali hilo.

Katika ahadi waliyowafikiana Joji alimsubiri kwa gari lake mbele ya mgahawa kwa dakika kadhaa kisha Adam akatokea na kupanda gari pamoja nae..

- Ulikuwa wapi, umenitia hofu?
- Asante kwa wema wako, samahani sana, sikuweza kujibu barua zake kwa mazingira yaliyojitokeza, nipe habari nzuri ya njia ya furaha? Na majibu ya maswali yako? Na safari yako ya India..
- Safari ya India ilikuwa na faida nyingi sana, nimefurahishwa sana, tutamalizia mazungumzo yetu tukifika hotelini.
- Hamna neno, tumekaribia.

Walipofika hotelini Joji na Adam walikaa katika meza ndogo iliyotayarishwa kwa ajili ya watu wawili, na mhudumu akafika na orodha ya chakula. Adam akawa anaangalia huku akizungumza na Joji.

- Hoteli hii ni nzuri..
- Inaelekea kuwa ni hoteli unayoipenda sana..
- Jina lake linanivutia, kwani napenda furaha, na ninahisi kuwa ni mahitaji ya kila mwenye akili katika dunia hii, hata mwenye hoteli ni mgeni, sijui ni wa nchi gani?
- Hoteli za Wamalaysia ni chache hapa Uingereza, hii ni hoteli ya Mmalesia, je ulipata kwenda Malaysia?
- Hapana..
- Malaysia ni nchi ambayo nataraji kuzitembelea, sikuwahi kwenda huko, wanasema kuwa tabia nchi ni nzuri kama watu wake walivyo, watu hawa ni watu

wa kawaida sana hawana makuu na tabia zao ni nzuri.

- Upole, ukawaida wakati mwingine ni dalili ya umakini na wakati mwingine ni dalili ya kutokujua.
- Hapana, hii ni dalili ya umakini, Malaysia ni nchi inayoendelea kwa kasi haswa katika mawanda yetu ya teknolojia.
- Napenda ukawaida wenye umakini, kisha akatabasamu na akasema: Au umakini wa upole, kamilisha mazungumzo yako kuhusu safari yako ya India..
- Tuagize chakula kwanza..

Joji alimuita mhudumu na wakaagiza chakula chao, na mhudumu akawakaribisha na akaondoka.

- Safari yangu ya India imejibu maswali yangu kwa uwazi, na ninaamini kuwa ninapita katika njia ya furaha.
- Vizuri sana!
- Safari yangu iliingiwa dosari na matatizo ya Katarina na Tom ambayo nimekuelezea, nami nakushukuru sana kwa ushauri wako; nilikuwa katika hali mbaya ya kinafsi, na inaelekea kuwa maneno yako yalikuwa sahihi.
- Maneno gani?
- Uliniambia: Huenda shaka nilizokuwa nazo zikawa si sahihi, kwani Tom aliniambia kisa chenyewe kwa usahihi wake, na sijui kwa nini mara hii nimemwamini, na ninahisi kuwa amekuwa tofauti na kubadilika.
- Kila mtu anaweza kubadilika na kuwa katika hali nzuri zaidi madamu tu wamepata fursa ya hilo..kisha akatabasamu na akasema: Na vipi kuhusu ubora wa dini kati ya dini za wanadamu na za mbinguni?
- Bila shaka ya kuwa dini za mbinguni ni bora kuliko za wanadamu.
- Inaelekea kuwa una hakika na hilo.
- Ndio, nami nimeona mkanganyiko uliopo katika dini za ardhi, dini za wanadamu ambayo hata akili haiwezi kufikiria, kisha akacheka na kusema: hebu fikiria kuna watu wanaoabudu panya, na kuna wanaoabudu mende, na wanaoabudu mawe, ulimwengu wa ajabu kabisa. Bila ya shaka kuwa Mungu ambae atajibu maswali yangu hawezi kuwa panya, mende au sanamu au mnyama.
- Kwa maana hiyo una hakika kuwa ni dini za mbinguni ndio sahihi?
- Hapana, bila ya shaka, itakuwa ima ni Uyahudi au Ukristu au Uislamu…
- Ni hatua ipi ifuatayo utaifuata?
- Ni kuanza utafiti wa kujua dini hizi za mbinguni moja baada ya nyingine, na

www.path-2-happiness.com

nitaanza na Uyahudi…kwa mnasaba ni ipi dini yako rafiki yangu?

- Unatarajia itakuwa ipi? Jina langu ni Adam kwa jina la baba wa wanadamu wote, na jina la baba yangu ni jina la baba wa Mitume yote na dini zote za mbinguni (Ibrahim).
- Vipi hilo?
- Adam ni jina la baba wa wanadamu wote, na Ibrahim ni jina la baba wa Mitume yote, na katika kizazi chake ni Musa, Isa (Yesu) na Muhammad.
- Na wewe unamfuata yupi katika mitume hiyo?
- Unaonaje tuipitie dini moja hadi nyingine katika dini hizo tatu, huenda nikabadilisha dini yangu!
- Inaelekea wewe ni Mkatoliki kama mke wangu…Ha ha ha, chakula kimeshafika.. Unajua? inaelekea umeniathiri katika hilo, nimejiona kuwa nakariri maneno yako kuhusu ukawaida, pamoja na kuwa tabia ya falsafa siku zote ni kuyafanya maneno kuwa magumu na sio kuyawepesisha..na tabia zetu sisi Waingereza wakati mwingine kwa bahati mbayatunafanya mambo kuwa magumu badala ya kuyarahisisha.
- Ukawaida, upole, tabasamu, furaha ni maneno yenye kuungana na kuingiliana daima.
- Na katika mtiririko huo huo, ni kuwa ugumu, migongano, huzuni na uovu ni maneno yenye kulingana, sijakuambia kuwa daktari amependekeza nisafiri kwenda Tel Aviv ili nipate fursa ya kuusoma Uyahudi na kuufahamu vizuri, nini rai yako?
- Vizuri, utasafiri kuelekea miji mitakatifu!
- Je, sijakuambia kuwa wewe ni Mkatoliki?
- Huenda safari yako ikawa na manufaa makubwa kufahamu kuhusu dini hizi tatu, na sio kuhusu Uyahudi peke yake.
- Ni sawa na aliyoniambia Katarina vivyo hivyo pindi nilipomjulisha kuhusu safari yangu ya Tel Aviv
- Sio lazima niwe Mkatoliki ili nikuambie hayo, hili ndilo linaloafikiana na dini zote za mbinguni..Hii ni ardhi ya mapambano, na ninaamini kuwa safari yako itakuwa yenye faida kubwa ili kujua zaidi kuhusu Uyahudi na dini nyinginezo, pamoja na kuwa hilo halitoshelezi na kusoma.
- Unakusudia nini?
- Umebakia muda gani wa safari yako?

- Siku nne.
- Napendekeza usome, tusome kwa pamoja kuhusu Uyahudi, dini kubwa, tukufu.
- "Uyahudi dini kubwa tukufu"! je wewe ni Myahudi?
- Wafuasi wote wa dini tatu kubwa wanaamini kuhusu Musa, hii haiwezi kuwa ni dalili, kwa nini tusizungumze bila kuwa na hisia za nyuma, achana na dini yangu, huenda nikawa Myahudi, Mkristo au Muislamu!
- Kwa mnasaba wa kunitajia Uislamu nimekumbuka udi ulioniagiza.
- Bei gani?
- Ha ha ha, ni bure, nilipewa zawadi na Muislamu, na sihusiki ikiwa ni bomu au kuna sumu ndani yake, kama alivyonitahadharisha mke wangu, Katarina.
- Ha ha ha, kwa maana hiyo nikijipaka nitakuwa gaidi?
- Tulikuwa katika hali ya hofu ya ugaidi kwa sababu ya milipuko hapa London, ikiwa ni bomu basi itakuwa ni hali ya jinai na sio ugaidi.
- Kwa nini ni Jinai na sio kigaidi?
- Ni jambo lenye kuchekesha, sijui kwanini, inaelekea kuwa sisi kama alivyoniambia Muislamu mmoja India kuwa: "Ugaidi ni pale mnapokuwa hamuwafikiani wala hampendezwi."
- Ugaidi ni ugaidi tu, haina dini wala nchi yoyote inaweza kusifiwa kwa ugaidi, hudhani kuwa hata sisi katika miamala yetu ya kawaida pamoja na wake zetu na watoto wetu tunakuwa magaidi, na kadhalika nchi zinaweza kupiga vita ugaidi lakini hapo hapo nao wakawa ni magaidi kwa miamala yao. Nguvu, mauaji ya kutisha yanagongana na Abc za akili na dini, hata ikifanywa na mtu yeyote!
- Inaelekea unazungumzia kufungwa na kukamatwa kwa baadhi ya Waislamu bila dhambi yoyote kwa milipuko hii ya karibuni.
- Sawa sawa, hadi sasa hivi pamoja na uhakika wao wa kuwa hawahusiki lakini bado idadi ya waislamu ipo jela, je huu nao sio ugaidi?!
- Bila ya shaka ndio, lakini sijui kwa nini naamini kuwa Waislamu wengi ni magaidi?
- Hiyo ni hali ya kawaida kabisa kuwa na mtazamo huu, nami vile vile ni muhanga wa tamalaki ya vyombo vya habari na siasa za kigaidi.
- Kwa vipi? Unakusudia nini?!
- Ufalme huu wa vyombo vya habari unatengeneza namna ya kufikiri kwetu na mtazamo wetu kwa wengine, na hiyo inafanyika kwa utambuzi wetu na hata bila

www.path-2-happiness.com

ya utambuzi wetu hali kadhalika. Je huoni ya kuwa nchi nyingi za kikoloni huziona nchi zilizozitawala kuwa ni nchi za watu waberiberi wanaostahiki kuuwawa! Je huo ni mtazamo wa watu kuwaangalia watu wa mataifa mengine kuwa ni wauaji na watu wabaya majambazi, na mtazamo wa dini moja kwa nyingine ni mtazamo wa kuwa wao ni wauaji na magaidi.

- Swadakta, lakini unaelekea mwenye hamasa sana, kisha akatabasamu na kusema: Je wewe ni Muislamu?
- Ha ha ha, chunga sana nisije kukulipua sasa hivi pamoja na hoteli yako hii.
- Usijali nilikuwa nakutania, rafiki yangu.
- Nami hali kadhalika, tumechelewa, tuondoke unipitishe nyumbani.
- Haya twende.

YERUSALEM NCHI ZA DINI NA VITA MBALI MBALI



www.path-2-happiness.com

7 YERUSALEM NCHI ZA DINI NA VITA MBALI MBALI

YERUSALEM NCHI ZA DINI NA VITA MBALI MBALI

(1)

- Pamoja na kuwa muda wangu wa kukaa Israeli ni mdogo sana, lakini nitajaribu kutembelea sehemu za Wakristo na alama zao mbali mbali za kumbu kumbu pamoja na kukutana na Wakristo.

Joji alimaliza matayarisho ya safari yake, alijitahidi kumaliza mapema sana, kwa lengo apate muda wa kutosha usiku kwa ajili ya watoto wake na mke wake. Tokea aliporudi kutoka India kazi zilimnyima nafasi ya kukaa na wanawe, kadhalika na vikao virefu vya Kakhi katika kupitia mikataba, akizidisha na kupunguza katika maelezo yake. Hili ni mbali na muda mwingi anaoutumia katika kusoma kuhusu Uyahudi kabla ya safari yake akitamani kutumia ziara yake kwenda nchi ya vita mbali mbali kutafuta majibu ya maswali yake makubwa, na isiishie katika kazi zake tu.

Katarina mpenzi wangu. Je unahitaji chochote kutoka Tel Aviv?

Nakutaka utembelee Kanisa la Kiama, na Kanisa la Bikira Maria na usali ndani yake.

Nimesoma kuhusu Kanisa la Kiama, hili ni kanisa lililojengwa na mfalme mkuu Helen mama wa Mfalme Constantine mwaka 335 A.D. Kanisa lilikamilika kujengwa juu (yenye kulia kama njuga) katika sehemu mbaya iligunduliwa ile ambayo inasemekana kuwa ndio ambayo Bwana Masiya Yesu alisulubiwa. Kanisa lilijengwa kwa muda wa miaka 270, kisha Wafursi waliliunguza walipoiteka Yerusalem, kisha mtawa Modest aliyekuwa rais wa makazi ya watawa akalijenga tena wakati ule katika mwaka 617 A.D. Kanisa hilo lilikarabatiwa mara nyingi, haswa wakati wa Constantine mwaka 1048 A.D. pindi watu wa msalaba walipoteka Yerusalemu mwaka 1099 ambapo walikusanya sehemu mbali mbali za kuabudia katika Kanisa moja ambayo ndio hii iliyosimama leo hii. Pamoja na hayo yote lakini sio tukufu kwetu sisi Waprotestant, ila mimi nitalitembelea na kuswali kwa ajili yako, lakini

www.path-2-happiness.com

nitajitahidi kuswali katika Kanisa la bikira Maria vile vile, je unataka kitu kingine?

- Asante, inaelekea umesoma mengi kuhusu Yerusalem?
- Sio sana naendelea kusoma.
- Yerusalem ni sehemu muhimu sana kwa Wakristo na sio Wayahudi; ndani yake pana msalaba wa Yesu, na kuna makanisa mengi ya Kihistoria.
- Ahah.. ni kiasi gani nilikuwa natamani kutembelea alama hizi za kumbu kumbu mwenyewe kisha nisali kwa ajili ya Bwana.
- Kama ni hivyo kwa nini usije na mimi?
- Kwa sasa siwezi, nina shughuli nyingi kazini, kanisani, huenda huko mbeleni baada ya kutuondoshea dhulma tuliyonayo.
- Dhulma?!
- Mayahudi katika kudhihirisha wanachodai kuwa ni urithi wao wa kitamaduni huko Yerusalem wamedhalilisha Makanisa na Wakristo huko Yerusalem.
- Historia ya Yerusalem ni historia yenye kusisimua na migongano yote ya dini za mbinguni, kwa mnasaba katika yanayosemwa kuhusu Yerusalem ni kuwa ilishaangamizwa mara mbili, na kuzungukwa kwa kutekwa mara 23, na kushambuliwa mara 52, kisha wakatekwa na kushambuliwa tena hadi kupoteza ardhi yao tena mara 44. Bado dini mbali mbali za mbinguni zinatarajia vita vikubwa, kwa kweli ni ardhi ya vita, lakini nashangazwa na maneno yako…. Uingereza ndio iliyowapa Mayahudi! Kama ni hivyo basi dhulma iko wapi?
- Kwa masikitiko ndio, ila ni kuwa kinachokusudiwa –au kinachoitwa kuwa ni – Ahadi ya Balfour ilikuwa na sababu za kisiasa na migongano mikubwa.
- Ilikuwaje na ni zipi sababu hizo?
- Miongoni mwa sababu zake ni: Uingereza kuingia katika vita vya kwanza vya dunia (19141918); ambapo Uingreza ilikuwa na haja ya msaada wa Mayahudi (kisiasa na kisayansi/kielimu) wakati wa vita vya kwanza vya dunia, kisha wakati huo huo harakati za Wazayuni zilikuwa zinatafuta atakayesaidia mradi wake wa kusimamisha nchi ya Taifa la Wayahudi katika ardhi ya Wapalestina.
- Ni mabadilishano ya kimaslahi tu?!
- Hapana, kulikuwa na sababu zingine huko Ulaya: Hamu ya watu wa Ulaya ilikuwa ni kuwaondosha Mayahudi Ulaya; kwani kundi kubwa la Mayahudi halikuweza kuchangamana (na watu wengine) katika sehemu walizokuwa wakiishi, na walikuwa wakiishi kama vile kiwiliwili kilichojitenga na dola, na

sababu nyingine ilikuwa na lengo la kupanda nguvu nyingine iliyokuwa tofauti huko Palestina ambalo ni daraja linalounganisha Misri na Afrika na baina ya Waarabu na Waislamu huko Asia, na sababu nyingine ni kusawazisha nguvu; nafasi na utawala wa Wayahudi katika baadhi ya nafasi muhimu katika Dola ya Ukhalifa ya Otoman ambayo ilikuwa inahatarisha nchi za Ulaya, na hivyo basi Uingereza ilitaka kuirithi dola hii.

- Unaibebesha Uingereza makosa yote!
- Hapana kabisa, mimi nabebesha makosa siasa yoyote ambayo haifikirii dini, Je, haikuwa ni kipaumbele kuiteka Yerusalem na kuifanya makao makuu ya Ukristo?
- Hivyo kinachotakiwa ni kukalia kwa mabavu katika njia nyingine chini ya Wakristo badala ya Mayahudi!! Ama mimi natofautiana nawe katika rai na naamini kuwa sehemu katika ile ahadi ya Balfour ni ya kidini.

(2)

- Ni ipi sababu ya kidini kwa mtazamo wako?
- Tafsiri potofu ya mafundisho ya Kikristo ndio ambayo imeifanya harakati za Uzayuni kuenea sana ndani ya kanisa la Kristo na wanasingizia na kuhalalisha matendo yao ya kibaguzi na kijambazi kwa jina la dini.
- Samahani hili halipo katika Ukatoliki.
- Swadakta liko kwetu – Protestant – sana tena sana, kuna makundi mengi kwetu yanayoamini kuwa kusimama kwa taifa la Israel mwaka 1948 lilikuwa ni jambo lisilozuilika; kwani linatimiza utabiri wa kitabu kitakatifu cha Agano lote la Kale na Jipya, na ni utangulizi wa ujio wa Masiya kwa mara ya pili ardhini kama vile mfalme aliyeshinda. Wazayuni Wakristo wanaamini kuwa ni wajibu wao kuwalinda Mayahudi kwa ujumla na haswa dola yao ya Kiebrania, kisha akatabasamu –na kusema:Ukweli ni kuwa wewe unaukosoa Uprotestant na sio Uingereza, kwa ujumla Israel ni kitu kilicho kweli hivi sasa, na tunaishi na taifa hilo.
- Lakini makanisa yetu na sehemu zetu tukufu na maaskofu wetu wasiteswe.
- Dhulma ni mbaya sana kwa hali zote, iwe ilikuwa ni kwa Mayahudi au Mkristo, na hii sio mara ya kwanza ambapo Wakristo wanateswa na Mayahudi, ama sivyo?!
- Kweli kabisa, kuanzia Yesu ambaye alijitoa mhanga kwa ajili ya wanadamu, ambae aliuawa na Mayahudi, kisha wafuasi wake kuteswa, hadi ndugu zetu wakateswa huko Yerusalem.

www.path-2-happiness.com

- Ha ha ha, inaelekea nimeingia katika vita vya dini na mauaji yake kabla hata ya kufika Yerusalem, haya na tulale kabla ya muda kututupa, itabidi niende uwanja wa ndege usiku wa manane.

Joji aliwasili Tel Aviv asubuhi ya alhamisi saa mbili unusu asubuhi na alikuwepo kumpokea, aliona machoni mwake mng'ao unaodhihirisha kuwa ni mtu mjanja mjanja na mwenye uwezo mkubwa wa akili.

- Hallo – Karibu katika nchi takatifu Yerusalem.
- Asante –ni kiasi gani mimi ni mwenye furaha kwa kufika kwangu katika mji huu mtakatifu.
- Kakhi amenijulisha kuwa safari yako itakuwa fupi siku nne tu.
- Ndio, sipendi safari za mfululizo, kabla ya kuja kwangu huku nilikuwa India, lakini Kakhi akanisisitiza kwa kunitukuza kwa ziara yangu katika mji mtakatifu.
- Nimetayarisha kila kitu, mkataba utasainiwa baada ya siku mbili; hivyo usijali sana, kuwepo kwako tu ni kuhakikisha kuwa mikataba imepitia njia zote za kawaida.
- Hii ni nzuri.
- Je, utaenda hotelini au kwenye shirika?
- Hotelini, ili niweke mkoba wangu, kisha tuelekee kwenye shirika moja kwa moja.
- Vizuri, kesho kutwa ni jumamosi na Levi hafanyi kazi jumamosi, huenda ukahitaji kufanya nae kikao leo au kesho, Levi ni mwanamke mwenye dini sana na mtaalamu mzuri wa teknolojia na anachokijali yeye zaidi ni kuwa programu ya ulinzi iwe na nguvu zaidi kuliko uwezo wa magaidi kuiingilia na kuivamia.
- Programu ya ulinzi ambayo tumewapeni ni nzuri sana na yenye nguvu, hivyo msihofie hilo.
- Kama ni hivyo mthibitishie hilo Levi, na kujali kwako kulinda amani ya Israeli, kwani hili ndilo analolijali zaidi, bali unaweza kushangazwa na mazungumzo nae ambayo yanaweza kukupeleka mbali kwenye mazungumzo ya kiitikadi, kifalsafa na sio kwenye fani ya teknolojia pekee.
- Kiitikadi na kifalsafa?!
- Ndio, na hii ndio sehemu ya tabia yake mbaya, kwa ujumla kama kuna tabu sana ya kutangamana nae nijulishe, kisha akatabasamu na kusema: Pamoja na inadi yake harudishi matakwa yangu.
- Vizuri.

Walifika hotelini, Joji akaweka begi lake, kisha akateremka mara moja kwa

na akaelekea kwenye shirika…..Jengo la shirika lenyewe halikuwa kubwa lenye kuvutia, bali lilikuwa la wastani lakini lenye wafanyakazi lukuki, ama ulinzi ndani ya jengo la shirika ulikuwa mkali pamoja na mtaa mzima.

Walikwenda katika ofisi ya , ambaye baada tu ya kufika aliwasiliana na Levi na kumtaka afike.

- Matatizo yatakuja sasa hivi.
- Matatizo! Kwa nini?
- Kasumba yake ya dini humfanya asifahamu maisha kwa njia sahihi, na ni mpenzi sana wa mijadala wala haoni tabu nayo, ingawaje mwishowe hulainika kwa kutumia nguvu.

Baada ya dakika chache akatokezea msichana mzuri sana akiwa amevaa nguo za heshima lakini hazikuweza kuficha uzuri wake, akamtambulisha kwa Joji:

- Levi ni mkuu wa kitengo cha teknolojia katika shirika letu… kisha akamuashiria Joji; na huyu ni Joji ndie mhusika wa kitengo cha Programming katika shirika la Advance Electronic huko Uingereza.
- Karibu sana, asante kwa kufika kwako, nahitaji maelezo mengi ya kitaalamu kutoka kwako.
- Sawa nitafurahi kuyajibu.
- Mnaweza kufanya mkutano wenu katika chumba cha mikutano mkipenda.
- Vizuri, mr. Joji karibu.

Joji na Levi walikwenda katika chumba cha mkutano, kilikuwa ni chumba kidogo lakini kilichopangwa vizuri na cha kifahari.

- Karibu.
- Asante sana, inaelekea bado haujatulizwa na Programu ya Ulinzi ambayo shirika letu limewapeni?
- Hapana, hili silo kusudio, lakini nilitaka kuwa na tumaini tu. Kwani usalama wetu kama Mayahudi na ulinzi wetu ni jambo muhimu sana na linalonishughulisha sana.
- Programu hii ni katika programu yenye nguvu sana ya ulinzi, lakini hisia yangu ni kuwa nyie mna woga unaowafanya mshadidie sana suala la ulinzi.
- Unakusudia nini?
- Ulinzi niliouona kwenye mtaa mzima na kwenye jengo lenu hili sijawahi kuuona katika maisha yangu hapo kabla.

www.path-2-happiness.com

- Sisi ni watu tulioteswa sana katika historia yote, na nadhani jambo langu la msingi ni kuona kuwa kuna ulinzi wa kutosha kwa watu wangu kadiri iwezekanavyo.
- Vizuri, kama ni hivyo jukumu langu litakuwa ni kuwasaidia katika suala hili la teknolojia ya ulinzi.
- Kutusaidia! Kwa nini utusaidie?
- Sifahamu! niwasaidie kwa programu ya pekee ya ulinzi ambayo tutaingia katika mkataba ambao utasainiwa.
- Samahani nilichozoea ni kuwa watu wote wapo dhidi yetu sisi Mayahudi.
- Mimi ni Mwingereza Mkristo tena Mprotestant, kwani hukumbuki kuwa aliyewapa nchi hii ni Balfour, Mwingereza Mkristo tena ni Mprotestant?
- Hii ni nchi yetu na ardhi yetu, na hakuna mtu aliyetupatia na ni wajibu wetu kujilinda wenyewe.
- Inaelekea unapenda sana mjadala, je unataka nikuambie ukweli?
- Ninapenda sana mjadala na ukweli naupenda na ninautaka.
- Kama unapenda ukweli kama usemavyo, wewe unatoka wapi? Inaelekea wewe ni Mzungu?!
- Mimi ni Mwisraeli.
- Je baba yako na mama yako wamezaliwa Israeli?
- Wazazi wangu ni Waustria na walikuja hapa mwaka 1970, na mimi nikazaliwa hapa Israeli, kwa hivyo mimi ni Mwisraeli pamoja na kuwa nina uraia wa Austria.
- Ataendelea kuwa Myahudi katika taifa lililochaguliwa. Inaelekea wewe ni mwana dini sana!
- Hivyo basi wewe ni Mwaustria unailinda Israeli na mimi Mwingereza nakupatia Programu ya Ulinzi.
- Lakini mimi ni Myahudi na wewe ni Protestanti!
- Je baba yako ni Myahudi?
- Hapana, alikuwa Mkristo asiyeamini Mungu lakini Uyahudi unakuja kwa njia ya mama na sio wa baba.
- Ukweli ni kuwa nimekuja Yerusalem kwa mambo mawili. Kwanza Kusaini mkataba, na Pili: Nataka kuujua Uyahudi, kwani huenda nikawa Myahudi, Je, tunaweza kuzungumzia zaidi na kwa kina kuhusu dini?
- Kwa furaha kabisa, isipokuwa haiwezekani ukawa Myahudi kama mama yako sio Myahudi.
- Kwa vipi?

- Sisi ni taifa lililochaguliwa, tumechaguliwa na Mungu katika damu yetu na itikadi.
- Kwa hivyo basi nyinyi hamlinganii dini yenu (hamuitangazi ili watu waingie)?
- Kamwe, ila tunawalingania wasiokuwa sisi ili watuhudumie sisi taifa lililochaguliwa.
- Yaani wawe wanawatumikia nyie tu!!
- Hapana utumishi bila ya malipo.
- Malipo ya kusaini mkataba wa ulinzi, mnatulipa malipo stahiki tuliyokubaliana, huu sio utumishi! Huku ni kuuza na kununua.
- Na kama sio mkuu wenu wa shirika Myahudi basi shirika lenu lisingechaguliwa kutupatia ulinzi huo.
- Lakini Kakhi ni Msekula!

Wakati huo mfanyakazi akagonga mlango, na Levi akamuuliza Joji angependa apewe nini.…

- maji na kahawa….unaonaje tukianza maudhui tokea mwanzo wake?
- Karibu, inaelekea unajali sana kujua dini mama, Uyahudi ambayo ni dini mama ya dini zote za mbinguni.
- Una maana dini mama wa dini za mbinguni ni Uyahudi na Musa anaaminiwa na Mayahudi, Wakristo na Waislamu.
- Ndio, waliofuatia baada ya hapo watu walitofautiana kuhusu wao, Mayahudi hawamuamini Yesu na Wakristo hawamuamini Muhammad.
- Tunaweza kusema kuwa Waislamu huamini wote, na Mayahudi hawaamini zaidi ya mitume yao… achana na hilo, nataka kujua kutoka kwako Uyahudi kwa undani zaidi, Je unaweza kunisaidia?
- Unaelekea wewe kuwa ni mwanazuoni wa dini nyingi na sio mtaalamu wa Programming! Karibu.

Joji alikusudia ndani ya nafsi yake kupambana na Levi na kumvuta kidogo kidogo; ili aweze kujua kwa undani kuhusu Uyahudi kwani hataki apate kutoka kwake maelezo ya juu juu tu bali ukweli.

- Ni ipi itikadi ya Mayahudi kuhusu mungu? Wanamueleza vipi, au wana mjuaje?
- Sifahamu unachotaka kukijua? Lakini mungu ndie muumba na mtoa riziki.
- Nimesoma mambo mengi kuhusu sifa ya mungu kwenu ambazo sijazifahamu bali zimeniletea matatizo; katika nilichosoma katika Agano la Kale: “Na maneno ya Mungu kwa Samueli yalikuwa: Nimejuta kwa nini nimemfanya Saoli Mfalme.” Na katika agano la kale kitabu cha ‘Kutoka’ nimesoma: “Akasikika minong’ono

www.path-2-happiness.com

yao Mungu akakumbuka agano lake pamoja na Adamu, Isaka na Yakobo." Kadhalika nimesoma katika kitabu cha Hesabu kauli yake Mungu. "Ondoka sasa ukawapige na uwaharamishie mali zao, na usiwasamehe, bali muue kila mwanamme na mwanamke na mtoto na anayenyonya na ng'ombe na mbuzi na ngamia na punda." Na mifano mingi kama hiyo, mara nyingi najiuliza: Je, Mungu anajuta, anasahau na kukumbuka na anaamrisha kuuwa na kutosamehe? Ni mungu gani huyu?

- Inaelekea unasoma sana, lakini tatizo lako unachagua la kusoma, ulilolisema ni sahihi na mengineyo mengi lakini jambo hilo sio haswa kwa Uyahudi tu? Hata nyie mna zaidi ya mara tatu ya hayo yetu.
- Ha ha ha, swadakta tunayo mifano mingi ya namna hiyo ndio maana nafikiria kuwa Myahudi, unaonaje tumalizie mazungumzo yetu kuhusu itikadi za kiyahudi baadae, nilitaka tumalizie suala la mikataba leo hii na kesho; kwani kesho kutwa ni Jumamosi na nyie hamfanyi kazi.
- Kweli kabisa: Jumamosi ni siku ya mapumziko na ibada, bali katika wasia kumi yamekuja mafundisho ya kudumu na kulihifadhi jambo hili nayo ni siku ambayo Mungu alimaliza kuumba mbingu na ardhi na akapumzika Jumamosi.
- Alipumzika?!
- Ndio alipumzika, inaelekea una hisia kali katika baadhi ya matamshi kuhusu Mungu, hili ni tatizo lako.
- Huenda ikawa hivyo, la msingi tumalize mjadala wetu kuhusu mkataba kwa muda wa siku mbili, nami nimeanza kuhisi uchovu leo hii kwani nimetokea uwanja wa ndege hadi kwenye shirika lenu.
- Unaweza kwenda kupumzika sasa hivi, tumalize mazungumzo yetu jioni ukipenda.
- Je haitokuwa dhiki kama tutamalizia mazungumzo yetu hotelini baada ya saa kumi unusu?
- Bila ya shaka….nitakuja hotelini kwako saa kumi unusu.
- Kama ni hivyo tule pamoja, huenda ukawa na utulivu zaidi, na ukapunguza ukali wako katika kuamiliana nami.
- Sifahamu unakusudia nini?! Wewe umenishambulia sana leo, samahani kama nimekukosea.
- Mimi ndie wa kuomba msamaha kama nimekushambulia, kwa mtu mwenye uzuri kama wewe haifai kushambuliwa na kukerwa.

- Huu ni wema wako, lakini mashambulio yako ya hapo kabla nimeyapenda kuliko kujitenga kwako hivi sasa –kisha akatabasamu na kusema: Mimi naishi maisha yangu kwa ajili ya Mungu tu.
- Kabla ya kuondoka nataka kumsalimia .
- Sawa, karibu.

Waliondoka pamoja kwenda ofisi ya , akawauliza swali kuhusu mkutano wao….

- Mjadala ulikuwa mzuri na wenye faida.
- Nawaombeni ruhusa ili nirejee kwenye kazi zangu?
- Karibu ewe Levi, lakini Joji ni mgeni wetu ni lazima tumkirimu.
- Vizuri, kwa heri.
- Tumekubaliana niende hotelini kupumzika kidogo, na Levi atakuja hotelini tumalizie mjadala.....nimefahamu kwa nini sisi tuna haja ya siku mbili kwa uchache ili kusaini mkataba, yeye anapenda mjadala sana.
- Fikra ya kumaliza mjadala hotelini ni nzuri, kwani inaondosha baadhi ya urasimu.
- Ndio, lakini Levi anaelekea mgumu sana!
- Pamoja na ugumu wake lakini ni mwema na tabia yake ni nzuri, na nitamjulisha aache inadi yake na ukali wake wa kutoshawishika kabla ya kuja kwake kwako leo hii.
- Hamna neno, naomba ruhusa, nahisi nimechoka kidogo.
- Karibu, dereva atakupeleka hotelini.
- Karibu, dereva atakupeleka hotelini.

(3)

Joji alifika hotelini saa saba na nusu mchana alipanda chumbani mwake na kujinyoosha kitandani hakukawia akawa amelala, hakuamka hadi ilipotimu saa kumi na robo… aliosha uso wake haraka haraka na kubadilisha nguo zake. Mara simu ikalia chumbani…alikuwa ni mhudumu kwenye mapokezi ambae alimjulisha kuwa kuna mwanamke anayemsubiri jina lake Levi….

Joji aliteremka haraka akamuona Levi na nywele zake nyekundu, na nguo zake

www.path-2-happiness.com

zisizo za kazini inayoonesha namna anavyojiheshimu lakini nguo zile ni za mkesha.Joji alimpa mkono; akatabasamu tabasamu ang'avu iliyoonesha uzuri wake na kumvutia sana…

- Unaonekana mzuri zaidi kuliko ulivyokuwa asubuhi!
- Asante kwa rai yako.
- Tafadhali twende tukale, natumalizie mazungumzo yetu wakati tutakapokuwa tunakula.

Walichagua meza ya peke yake iliyojitenga pale hotelini, wakakaa hali ya kuelekeana… Joji alimuita mhudumu na wakaagiza walichotaka…

- Unaonaje wakati wa kula tusizungumze chochote kuhusu kazi?
- Kama utakavyo…
- Wewe ni mzuri sana, je umeolewa?
- Hapana, bado, nilidhani mnatofuatiana na Kakhi.
- Ki vipi?
- Wewe unajali sana mambo ya dini na torati na injili, wakati ambapo Kakhi hajali isipokuwa mali na wanawake..
- Ni kweli lakini ni kitu gani ambacho tunafanana?
- Nilidhani hupendi mali sana, wala uzuri haukushughulishi….
- Ni nani ambae hajali wala hapendi mali na uzuri? Lakini sijafahamu una kusudia nini!
- amezungumza nami baada ya kutoka kwako kuhusu makusudio ya mkutano kufanyika hotelini.
- Unakusudia nini?
- Wewe ni kama Kakhi unataka starehe…starehe tu.
- Nibainishie zaidi!
- Usijifanye mjinga, mimi nipo tayari.

Joji alijifanya hajui kinachoendelea, na hafahamu mafumbo yake…

- Nami nipo tayari vile vile kumalizia mjadala wetu, lakini baada ya kumaliza chakula changu.
- Vizuri, lakini je ungependa mjadala motomoto?
- Kama upendavyo.
- Sipendi kumkatalia jambo , vile vile kama upendavyo.
- Ni nini uhusiano wa katika mjadala wetu?!

- Niache niseme… Nyie wanaume hamjali chochote isipokuwa ni ngono tu.
- Inaelekea kuwa mimi nazungumzia jambo fulani na wewe unazungumzia jambo lingine kabisa!

Joji alianza kufahamu vizuri zaidi, na akaunganisha mazungumzo ya Levi na maneno ya Kakhi na , na pindi walipotoka hotelini kula chakula Joji alielekea kwenye bustani iliyopo nje na kumwambia Levi:

- Napendekeza tukae katika bustani ya hoteli kama utaliona hilo linafaa?
- Bustanini!! Kama utakavyo!!!!
- Inaelekea ni sehemu nzuri na inafaa kupeana ukweli.
- Ndio ni sehemu tulivu, lakini ipo wazi mbele za watu, unataka nini?
- Ninataka tujadiliane.
- Je unanifanyia mzaha? Nimekuambia kuwa amenizungumzia na mimi tayari nimeshajitayarisha.
- Nami nipo tayari tuanze mjadala, kisha akaendelea; kuna sintofahamu kutoka kwa : Mimi sio Kakhi.
- Nilichofahamu kutoka kwa kuwa nyie ni wamoja; na ndio maana nimejitayarisha kama uonavyo.
- Je hukuniambia kuwa hupendi kusifiwa kwa mapenzi na kuwa maisha yako ni kwa ajili ya Mungu tu!
- Mimi…mimi nimekubali kumhudumia Mungu.
- Kumhudumia Mungu! Vipi?
- Jambo muhimu zaidi katika ibada ya Mungu ni: Kutumikia Dola ya Israeli na kuwatumikia watu wake wateule wa Mungu.
- Na wewe kwa masikitiko ni mwanamke rahisi sana? Je huna uwezo kuwa huru katika nafsi yako kwa uchache!
- Kwa sababu umeanza kunishambulia, nitazungumza kwa ukweli: mwanamke katika Uyahudi ana sehemu yake maalum, wala muamala wake si kama wa wanaume, na sipendi kuzungumzia hilo, je tunaweza kubadilisha maudhui?
- Sijafahamu, nami sipendi kuzungumza hilo wakati wewe hupendi hilo, lakini hukuniambia hapo kabla kuwa wewe unapenda mjadala!
- Mimi napenda sana mjadala, lakini nahofia kufahamika vibaya… nataraji unifahamu kwa njia sahihi.
- Tafadhali, haya niambie.
- Jinsia na mwanamke katika Uyahudi inahitaji maelezo, kwa mfano kiasili kwetu

www.path-2-happiness.com

sisi mahusiano ya kawaida yaliyo sahihi kuhusu jinsia (ngono) yanatakiwa yawe kwa lengo la kuzaa tu, nayo ni kati ya mke na mume. Hata hivyo kwa masikitiko –mwanamke amedhalilishwa na hufanywa kama mtoto mdogo au mwenda wazimu au mnyama, naye hutumika kwa starehe tu, imekuja kwenye Talmud: "Kwa hakika mwanamke ni mkoba uliojaa mavi"….kisha akageuka kwa hasira, na kusema: Je hili ndilo utakalo?! Je unataka ukidhi haja yako kwenye mkoba huu?!

- Samahani kwa kukukera, naliona hili jambo ni la dhulma sana na ubaguzi, na tukamilishe mazungumzo yetu kwa utulivu na kitu gani kinachokulazimisha uwe hivyo?
- ! na kumtii!
- Sifahamu! Nini uhusiano kilichopita na utiifu wako usio wa mipaka kwa .
- ni mume wa mama yangu.
- Baba yako!
- Hapana, hapana, baba yangu alikufa kwenye bomu la gaidi Muislamu… hivyo baba yangu mdogo akamrithi mama yangu, kwani imekuja kwenye Torati: "Imefaradhishwa kwa mwanamke mjane kwa ndugu wa mume wake."
- Amerithiwa na ndugu ya baba yako? Kwani hiyo ni bidhaa ili irithiwe?!
- Ndio, kwa masikitiko hulazimishwa kuolewa na ndugu wa mume wake.
- Samahani sio kwamba sikuamini, lakini unachozungumza sikiamini! Na nadhani unaikosoa sana torati pamoja na kudai kuwa wewe ni Myahudi na mwenye dini!
- Aah huenda nikawa nimezidisha kubwabwaja! na sipendi mazungumzo haya, lakini wewe ndie unayetaka! Kisha akapumua na kuangalia chini: Pamoja na kujali kwangu kutokusema chochote hadi hivi sasa.
- Je kuna zaidi ya yale uliyoyasema?!

Macho mazuri ya Levi yalijaa machozi, akahema na kusema:

- Kwa kuwa wewe ndie uliyetaka, kwa bahati mbaya ndio! Ushahidi wa wanawake mia moja ni sawa na ushahidi wa mwanamme mmoja! Mwanamke ni kiumbe shetani, na yupo chini kuliko mwanamme!...Imekuja kwenye torati: "Ni wajibu kwa mwanamme asipite baina ya wanawake wawili au mbwa wawili au nguruwe wawili, kama vile ambavyo haipasi kwa wanaume wawili kumruhusu mwanamke au mbwa au nguruwe kupita mbele yao." Kila siku asubuhi naomba kwa unyenyekevu: "Hongera kwako Ewe Mungu kuniumba kulingana na matakwa yako" na mwanamme anaomba, "Hongera kwako ewe Mungu kuwa hukuniumba

mpagani au mwanamke wala mjinga."

Joji alikuwa akimuangalia Levi mzuri na macho yake mazuri ya kibuluu yaliyojaa machozi akimsikitikia, kadhalika akausikitikia moyo wake na macho yake na akahisi uhusiano mkubwa wa aliyekuwa akizungumza pamoja na hisia zake Levi za ndani.

- Nakuomba msamaha…Je, tunaweza kubadilisha maudhui; kwani nimechoka sana, na nisamehe kwa kukukera.
- Nilikuambia hilo toka mwanzo.
- Lakini mambo haya yote hayamuhusu mwanamke katika Uyahudi peke yake?
- Hapana kabisa… Ni kwenye Uyahudi pekee, ama katika dini zingine ni mambo mengine!! Nataraji hutoghadhibika na kukerwa, mwanamke katika Talmud (nacho ni kitabu cha pili baada ya torati) kinasema: Mwanamke asiyekuwa Mwisrael si chochote isipokuwa ni mnyama tu; hivyo basi kuzini nae sio kuvunja sheria; kwani anatokana na kizazi cha wanyama.
- Kasumba ya aina gani hii! Lakini nirudie kusema kuwa sijakinaishwa bado na unayosema, mimi nimesoma kuhusu Uyahudi, na nimesoma sehemu mbali mbali katika torati, lakini pamoja na hayo nahisi unaifasiri torati kama utakavyo.
- Sijui kwa nini nimeanza kujielezea na kubwabwaja sana lakini kwa kuliweka wazi: Sisi hatusomi torati kama msomavyo injili.
- Kwa vipi?
- Torati ni ufunuo kutoka kwa Mungu, wakati ambapo talmud ni sherehe (maelezo) ya torati, wala hatuwezi kuifahamu torati peke yake ukiiweka kando talmud, lakini sipendi kukukera na hilo.
- Na ni nani aliyeandika talmud?
- Imeandikwa na kalamu nyingi sana zaidi ya miaka elfu moja, kwa nini maswali haya?
- Kwa sababu nimekerwa sana, nahurumia hali ya mwanamke, na samahani sijakinaishwa na ulichosema kuhusu mwanamke.
- Mengi niliyokuambia nimeyatoa kutoka kwenye torati je unataka kutoka kwenye talmud?! Talmud ina mkusanyiko wa vijitabu sitini na nne (64), je ungependa kusikia chochote kilichomo ndani yake?
- Kama halikukeri hilo, tafadhali nijulishe.
- Kama ni hivyo sikiliza mambo ya ajabu sasa… katika moja ya vitabu vya Talmud: Ikiwa mbwa atamrukia msichana wakati anapofanya usafi kwenye ardhi na

www.path2-happiness.com

akaingiza utupu wake na kumwingilia basi msichana huyo hazingatiwi kuwa ni mchafu, na anaruhusiwa kuolewa na Rabi (mwanasheria wa sheria za kiyahudi) hata aliyekuwa katika daraja la juu kabisa! Na talmud imeweka umri wa msichana anayefaa kufanya tendo la ndoa akiwa na miaka mitatu tu na siku moja!! Yaani msichana katika umri huu anafaa kuwa mke wa rabi. Ama umri wa mtoto wa kiume ambao unamruhusu kujamiiana inaelezwa na vitabu vya talmud kuwa ni miaka tisa na siku moja, ama baadhi ya rabi wamesema ni miaka minane na siku moja. Katika sehemu nyingine talmud inasema: Mtu anaposimama kujamiiana pamoja na msichana mdogo wa miaka mitatu na siku moja haizingatiwi kuwa ni tendo la jinsia!! Kwa sababu ni kama yule mtu kuweka kidole chake kwenye jicho la msichana!! Ama kijana wa kiume wa umri wa chini ya miaka tisa na siku moja kwa kufanya tendo la ndoa pamoja na mwanamke aliyekwisha baleghe jambo hilo halizingatiwi kuwa ni zinaa!! Kwa sababu ni kama vile amemjeruhi kwa ujiti!! Kama ambavyo talmud haizingatii kuwa tendo la jinsia pamoja na wanyama kuwa ni zinaa wala mtendaji haadhibiwi! Na mwanamke ambae anafanya jinsia na wanyama hazingatiwi kuwa amezini wala haadhibiwi bali anayeadhibiwa ni mnyama! Hali kadhalika haizingatiwi tendo la ndoa na uume uliolala kuwa ni zinaa wala haadhibiwi!

- Samahani, hii inatosha; nimeshapatwa na kichefuchefu na mazungumzo haya, lakini nina swali na nisamehe kwa mara nyingine kuzungumza nawe kwa uwazi "Wewe ni mtu mwenye dini au unalipa kisasi juu ya dini ya Uyahudi?!" Narudia kuomba samahani lakini sidhani kuwa Wayahudi wote wako hivi!
- Ndio…Mayahudi wote hawako kama nisemavyo, kuna masekula kama sahibu yako Kakhi ambao hawajali torati wala talmud, na kuna makundi mengine mbali mbali, lakini kwa masikitiko nikuwa sisi ni miongoni mwa familia za dini sana na mimi ni mtu wa dini. Hata hivyo sijui kwa nini nimekuambia yote hayo! Huenda nimekuwa nabwabwaja sana kuhusu nafsi yangu na huenda nikawa nimekosea, na huenda nilikuwa nataka kujitetea kwa kuwa kwangu dhaifu kuwa nimekuja kukupa mwili wangu na nilikuwa najihisi kudhalilishwa.
- Sijakusudia kukudhalilisha na hii sio tabia yangu, lakini anataka nini kunituma kwako?
- Sijui kwa nini haswa, kila ninachokifahamu kutoka kwake ni kuwa una fedha ambayo bado hujampa, na amefahamu kutoka kwako kuwa hutompa hizo fedha hadi nije kukufurahisha kwa kiwiliwili changu.

- Kiwiliwili chako ni kizuri sana, kiasi gani natamani kustarehe nacho, lakini… mimi nimeoa na ninachojali ni misimamo yangu, huenda nikawa nashadidia kuliko inavyopasa, na samahani kwani amenifahamu kwa makosa, mimi sikumwambia hivyo, na hainipasi kusema hayo.
- Kwa masikitiko mimi ni bidhaa… macho yake yakajaa machozi na hakuweza kumiliki nafsi yake na kuanza kulia: Huenda amekufahamu hivyo kwa sababu ya Kakhi.
- Samahani, nyamaza. Nini uhusiano wa kilichotokea na Kakhi?
- Kila anapokuja Kakhi anaongea na na mimi nalala kwake siku moja au mbili, Kakhi ni Myahudi; na ana mikataba, mali na wanawake, hivyo basi ni lazima mwakilishi wa Kakhi ahudumiwe kama vile anavyohudumiwa Kakhi, ni udhalili kiasi gani huu!

Joji hakujua aseme nini na haswa alipomuona Levi akilia.. alinyamaza tu huku akiuangalia uzuri wake, kisha akamsikitikia, akahisi dhambi kwani yeye Joji ndie aliyemsukuma katika mazungumzo haya yaliyomjeruhi…..

- Futa machozi yako Levi.. Nisamehe sitorudia maneno haya tena unaonaje tukapate kahawa?
- Usiombe msamaha… wewe hujakosea.

Walikwenda kwenye mkahawa uliopo hotelini – wakati huo Joji aliazimia kubadilisha maudhui na kuwa mbali na matamanio ya kiwiliwili

- Una hofu gani ya kusainiwa mkataba wa ulinzi na shirika letu?
- Sina hofu yoyote.
- Nimetakiwa nije kutoka Uingereza kwa ajili ya kujibu maswali yako.
- Ha ha ha, ukweli ni ili kumletea fedha zake, ikiwa una fedha na ukishampa , basi zingatia kuwa mkataba umeshasainiwa.
- Ukweli ninazo, je nikupe wewe au ?
- Mpe …kisha akatabasamu kwa huzuni; hata wewe unawatumikia na Kakhi pamoja na kupingana na misimamo yako!
- Kwa masikitiko unachosema ni sahihi, kinachotakiwa tuzungumze kuhusu bidhaa yetu na sio kwa rushwa…
- Kama ni hivyo Uyahudi sio mbaya kuliko Ukristo!
- Huenda, na kwa sababu umekuwa mkweli na mimi kwa kiasi hiki hebu sasa nikueleze ukweli wangu.
- Ukweli gani?!

www.path-2-happiness.com

- Mimi nipo katika msafara wa kutafuta furaha na hiyo inatokana na hofu na wasiwasi ulionipata baada ya kushindwa kujibu maswali makubwa, nimeanza kufanya utafiti kuhusu dini mbalimbali, utafiti wangu sasa unahusu Uyahudi, kisha utafuatiwa na Ukristo na mwisho kwenye Uislamu.
- Furaha ni neno zuri, lakini linaelekea zaidi kuwa la wanaume katika Uyahudi, ni kiasi gani natamani kuwa mwanamme!
- Kwani hukufuata dini ili uwe mwenye furaha?
- Bila ya shaka, lakini huenda ikawa furaha ya akhera tu.
- Sasa kwa nini usibadilishe dini yako?
- Uyahudi ni bora kuliko Ukristo na Uislamu, ni dini kongwe zaidi, na watu wake ni wateule, yote niliyokuambia, huenda ikawa ni kubobojoka kwa sababu ya hisia yangu ya kudhalilishwa, samahani. Je huhisi kudhalilika unapotoa rushwa na kwenda kinyume na msimamo wako?!
- Ndio, mara nyingi maisha yanatubadilisha kuwa ni vifaa wanavyochezea watu, Ha ha ha, lakini huoni kuwa wachezaji wote huwa ni Mayahudi?!
- Ha ha ha, kitu cha kawaida kabisa kwani sisi ni taifa lililochaguliwa…unanitaka niache Uyahudi!
- Pamoja na kuwa uzuri wako umejitokeza kwa mara nyingine, na ya kuwa suala la mkataba na maafikiano na maswali mbali mbali tumeyamaliza, Je, utaona kero lau kama tutazungumzia kuhusu Uyahudi zaidi? Tusiingie tena kuhusu maudhui ya mwanamke, mimi nataka kufahamu zaidi juu ya dini yenu kongwe.

Simu ya Joji ililia, aliyepiga simu alikuwa ; Joji akamuomba Levi apokee simu.. alitaka kujua maendeleo ya Joji na Levi, na makutano yao yalikuaje…

- Mimi nipo katika hali nzuri na Levi vile vile, na tunaendelea kujadiliana katika kazi zetu.
- Ha ha ha, hamjamaliza bado?
- Bado…huenda tukamaliza leo.
- Mnaweza kumalizia leo au kesho hotelini ukitaka, sisi tupo kuwahudumia.
- Vizuri, lakini nataka tukutane kesho ikiwezekana, nina cheki yenu ili tusaini mkataba.
- Muda utakaomaliza na Levi mimi nipo kukusubiri.
- Asante nitakupigia tupange muda.
- Nitasubiri mawasiliano yako, na napendekeza Levi akutembeze katika mji mtakatifu kesho ukipenda.

- Sawa, nitapanga nae kuhusu hili.
- Sawa, nakuacheni kwa baraka za Mungu.

Joji alimaliza mazungumzo, na akaangalia macho mazuri ya kibuluu ya Levi…

- anataka kuwa na uhakika na cheki yake.
- Na kuhakikisha kuwa nimetekeleza yote aliyotaka nifanye.
- Alitoa pendekezo zuri.
- Sidhani kama anaweza kuja na pendekezo zuri, kwani amependekeza nini?
- Tutoke kesho ukanitembeze sehemu takatifu.
- Vizuri…lakini kitu cha kushangaza, wakati mwingine huja na pendekezo zuri kwa mtu ambae humtarajii hilo.
- Sasa hivi ni saa kumi na mbili, ukipenda tumalizie mjadala wetu kuhusu Uyahudi, na kesho nitakusubiri asubuhi kwa ajili ya matembezi ya sehemu takatifu za Kiyahudi.
- Vizuri, tumalizie mjadala wetu na napendekeza ziara yetu katika sehemu takatifu iwe kesho kutwa yaani Jumamosi, kisha akacheka kwa kuona haya: Tutakwenda kuangalia sehemu takatifu, na ukitaka kitu kingine ni leo au kesho tu.
- Kitu kingine …nimefahamu, wewe ni mzuri sana, lakini nimekuambia kuwa nimeoa na misimamo yangu inanikataza.
- Nikuambie ukweli, hao Wakristo waliooa na wenye dini zao hawakatazwi kufanya mambo haya.
- Ndio, kwa masikitiko umesema kweli, lakini hilo kwangu halinipendezi, hiyo ni hiana kwa mke wangu, kama nilivyokuwa sipendi afanye yeye hali kadhalika na mimi sipendi kufanya.
- Sio nakusifu tu lakini wewe ni mtu mzuri, nimefurahishwa nawe sana.

Waliendelea kuangaliana kwa muda na hakuhisi pindi mikono yake ilipokamata mikono yake milaini, kisha Joji akatanabahi na kuondosha mikono yake na kusema kwa aibu.

- Asante sana, wala sidhani kama kuna jambo lenye kuhitaji shukrani, la muhimu mimi naona ni vizuri ziara yetu kama ulivyosema iwe Jumamosi.
- Vizuri, tumalize mjadala wetu.
- Nataka kufahamu zaidi kuhusu torati na talmud.
- Kama nilivyokuambia sisi tunasema kuwa torati imetoka kwa Mungu. Ama talmud ni sherehe (maelezo) au ubainisho na kanuni mbali mbali za torati ambazo

www.path-2-happiness.com

zimenakiliwa kwa njia ya mazungumzo na baadae kuandikwa.

- Yaani talmud ni maneno ya watu!
- Ndio, isipokuwa huwezi kufahamu torati bila kuisoma talmud, sisi sio kama Wakristo kama nilivyokuambia hapo kabla.
- Kwa nini msirejee moja kwa moja katika maneno ya Mungu yaliyomo kwenye Torati?
- Nimekuahidi kuwa mkweli nawe, hata torati yenyewe ina matatizo mengi, umeona maneno yaliyoandikwa kuhusu mwanamke.
- Itakuaje maneno ya Mungu yawe na matatizo? sijafahamu bado!
- Kwa masikitiko sisi tunasema kuwa inatoka kwa Mungu lakini kuna dalili zenye kuthibitisha kuwa upotofu umeingia ndani yake.
- Dalili za upotofu? Ipo wapi nakala yake ya asili?
- Torati ya asili imepotea, lakini kuna nakala tatu tofauti, na baadhi zina jumla zilizozidi zenye kugongana na nakala hizo ni: Nakala ya Kigiriki; nayo ni nakala ambayo imebaki kuwa inazingatiwa kwa Wakristo hadi karne ya kumi na tano na wakati huo huo walikuwa wakiona ile nakala ya Kiebrania kuwa imepotoshwa, hadi hivi sasa Kanisa la Kigiriki linaizingatia kuwa ni nakala sahihi vivyo hivyo makanisa mengine ya mashariki.
- Ama nakala ya Kiebrania ambayo inakubaliwa zaidi na Wayahudi na Waprotestant, ina jumla ya safari 39 (vitabu 39), na kulikuwa na makubaliano ya Wakristo juu ya usahihi wa ile nakala ya Kigiriki (Kiyunani) hata katika karne ya kumi na tano, na ya kuwa nakala ya Kiebrania ilipotoshwa na Wayahudi mwaka 130 A.D. kwa makusudi kwa lengo la kuwatia shaka kuhusu ukweli wa nakala ya Kiyunani ambayo Wakristo wakiitegemea wakati ule, kama ilivyoongezwa kuwa upotofu huo ulikuwa unawakusudia Wakristo na Mayahudi wa Samaria kwa pamoja. Hata hivyo baada ya kujitokeza kundi la Protestant katika karne ya kumi na sita mambo yakabadilika; Waprotestant wakaelekea kukubali nakala ya Kiebrania na kusema kuwa nakala ya Kiyunani imepotoka, na mwishowe nakala ya wasamaria; na wasaramia ni kundi la Kiyahudi lililokuwa likiishi katika milima ya Nablus na nakala yao ina vitabu saba tu katika Agano la Kale na kilichozidi baada ya hapo Mayahudi wa Saamira waliona kuwa ni ziada iliyoongezwa (Feki). Na ndani yake kuna jumla mbali mbali na Paragrafu ambazo hazipo katika nakala nyinginezo. Baadhi ya wahakiki wa Kiprotestant wanaizingatia hii zaidi kuliko ile ya Kiebrania pamoja na kuwa katika baadhi ya sehemu wanaitanguliza kuliko

ile ya Kiebrania.

- Historia ya ajabu sana na migongano yenye kusisimsha lakini ni mambo gani yaliyopotoshwa…tuache maudhui ya mwanamke na mambo ya jinsia.
- Mambo mengi!!! Miongoni mwayo ni ile tuliyoitaja asubuhi kuhusu sifa za mungu ambayo hayamfalii, na maovu na machafu na mapungufu ya mitume na….
- Samahani kwa kukukata maovu na mapungufu kwa mitume?!
- Ha ha ha, unajua!! Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu nazungumza hivi, ukweli mimi nashangazwa na nafsi yangu sana, lakini nahisi kufurahishwa kufanya hivyo je hili linatokana na kushindana au ni wasiwasi wa shetani?! Sijui ila najihisi mwenye furaha kufanya hivyo, niache nikupe mifano: Katika torati Nuhu ameelezwa kuwa anakunywa pombe na kukaa uchi; imekuja ndani yake: "Nuhu alikuwa mkulima akilima mizabibu na kupanda na kunywa pombe na kukaa uchi ndani ya hema lake."
- Ama kuhusu Lut: "Aliishi na binti zake wawili pangoni, binti yake mkubwa akamwambia mdogo: Baba yetu amezeeka na katika ardhi hii hakuna mwanamme wa kutuingilia, tumnyweshe baba yetu pombe, tujamiane nae, wakafanya wakabeba mimba kwa watoto wawili Mawaab na Amuun." Na mfano wa hayo mengi nadhani mifano hii miwili inatosha.
- Samahani Levi, lakini kwa nini unarejea mara kwa mara katika masala haya ya jinsia kila tukiachana nayo?
- Kwa sababu nimeiahidi nafsi yangu kuwa mkweli nawe na wewe ndie uliyeniuliza.
- Napenda tuingie maudhui mengine.

Levi alitabasamu na mashavu yake yakawa mekundu kwa haya kiasi cha kuonesha uzuri wake zaidi.

- Ha ha ha, tafadhali maswali yako yasiwe kuhusu jinsia na mwanamke.

Ombi la Joji halikuwa kwenda mbali na kadhia za jinsia ila kutoroka kuukodolea uzuri wa msichana aliye mbele yake; hakutaka kabisa kusikia hisia za mwili wake na kiu kikubwa kwa uzuri wa kupindukia ulio mbele yake. Hivyo basi aliogopea kumfanyia hiana Katarina na kwenda kinyume na misimamo yake mwenyewe, kisha akakumbuka maneno ya Adam mashuhuri "Furaha katika wepesi (ukawaida)": akajisemesha mwenyewe: Laiti ningeweza kuishi na misimamo yangu kwa wepesi, akajaribu kubadilisha maudhui.

- Uliniambia kuwa wewe ni kutoka Austria.
- Ha ha ha, hapana, nimekuambia Israel.

www.path-2-happiness.com

- Ndio, nakusudia wazazi wako kutoka Austria, niruhusu nitoe takwimu za Uingereza kulingana na Mayahudi; katika mwaka 1945 Wayahudi walikuwa asilimia 38. Waislamu asilimia 58 na Wakristo asilimia 8. Na kuwa idadi hii kubwa ya Wayahudi ilikuwa ni kwa sababu ya kuhama kiasi cha wayahudi 50,000 hadi 60,000 baina ya miaka 19201945. Sasa mnawaonaje Waislamu na Wakristo kuwa ni magaidi na nyie ndio mliohamia na kukalia kwa mabavu ardhi yao?!
- Samahani … nyie Waingereza ndio mnaokalia nchi za watu kwa mabavu, na nyie ndio mliotupa ardhi yetu na kuturudishia haki yetu.
- Kwa nini Uingereza imerudisha haki yenu kama msemavyo, je ni huduma ya bure kwenu tu?!
- Ninachojali ni ardhi yetu tu na tumerejeshewa, ama kwa nini Uingereza ikatuhudumia hilo ni swali lenu na sio langu…. Pamoja na kuwa Uingereza na Ulaya zimetuhudumia lakini wakati huo huo zimetuuwa sana. Je, hujui hilo?
- Unakusudia yale maangamizi makuu yanayofahamika kama Holocaust?!
- Sisi ni watu tuliodhulumiwa sana na kuteswa sana katika historia, ama Holocaust ni moja tu ya mtiririko huo wa kuteswa.
- Usiku wa jana tu kabla ya kuja huku mke wangu ambae ni Mkatoliki alikuwa ananihadithia mateso ya Wakristo kutoka kwa Mayahudi, kila taifa wanahisi kuteswa.
- Swadakta…..hata washenzi Waislamu magaidi waliomuua baba yangu wanasema kuwa wanateswa, lakini historia na hali halisi inakupa ukweli wa mambo.
- Wewe umesema unapenda mjadala wala huoni vibaya kuambiwa ukweli, je huoni kuwa Waislamu wameteswa, mmewafukuza na kukalia nchi yao na kuwaua!!
- Magaidi wanastahiki hili na zaidi, na nani aliyefanya hivyo! Ni nyie kabla yetu, hivyo msitukosoe.
- Umebadilika, sasa unashambulia tu. Ndio, sisi ndio tuliofanya hivi kabla yenu, kwani huoni kuwa wanateswa?
- Nimekuambia kuwa wanastahiki hivyo na zaidi ya hayo; wao ni washenzi, wapo nyuma, wanyama magaidi….
- Lakini huoni kuwa hata Wakristo Wapalestina nao wanateswa na sio Waislamu peke yao!
- Unakusudia Israel na sio Palestina.
- Ndio, huoni kuwa Wakristo Israel wanateswa na Mayahudi!
- Usighadhibike, Wakristo wanaweza kwenda nchi yoyote Ulaya au Marekani

kama hawapendezwi na muamala wetu!!
- Ha ha ha, maneno yako makali yenye kukata na yana kinzana kabisa na uzuri wako, sitarajii uzuri wote huu unasema maneno makali kama haya!
- Asiyekuwa tayari kutuhudumia juu yetu kumuua!
- Haya ndio mafundisho ya kitabu kitakatifu?!!
- Ndio, ndani ya torati tunasoma:
- Amesema Bwana Mungu wa Israeli; “Kila mmoja na abebe upanga wake na atembee kila sehemu mlango kwa mlango na amuue ndugu yake, rafiki yake na jirani yake.” Vile vile imeandikwa: “nikamsikia anasema: Nendeni mjini nyumba yao wapigeni. Msiwaonee huruma wala kuwasamehe. Waueni Wazee, vijana, wa kike na wa kiume, watoto, wanawake pamoja na wasichana.” Kadhalika imeandikwa: “Sasa nendeni muwapige na waharimishieni kila walichonacho wala usiwasamehe bali muueni mwanamme na mwanamke, mtoto na anayenyonya, ng’ombe, mbuzi, ngamia na punda”. Je inakutosha maandiko haya au niongeze?
- Samahani…inaelekea nimekughadhibisha, tulia kidogo bila shaka huu ndio ugaidi wenyewe usiovumilika!
- Mimi nimetulia nimekuambia hapo kabla kuwa haya ni maneno ya Mungu yaliyomo ndani ya torati na sio maneno yangu!

Joji alimuita mhudumu, na akataka amletee juisi ya chungwa na kumgeukia Levi ambae alijaribu kuficha wasiwasi wake na hasira zake…

- Unataka nini ili utulie zaidi?
- Juisi ya ndimu tafadhali.

Joji alinyamaza kwa muda akiwa anamuangalia Levi usoni akiwa anahema kwa nguvu, na kufikiria uzuri aliokuwa nao Levi na upole wake na mazungumzo aliyokuwa akizungumza yasiyokuwa ya huruma…nae Levi alikuwa ni kama mtu aliyepigwa kichwani akawa amejiinamia chini kisha akanyanyua kichwa chake huku akitokwa na machozi….

- Baba yangu amekufa, na nimebaki kuwa mwanasesere wa , yote hayo kwa sababu ya mateso ya kihistoria tuyapatayo, kisha unataka niamini kuwa hawa magaidi Waislamu wanateswa!?
- Karibu… kunywa juisi ya ndimu na tuachane na maudhui haya madamu yanakukera…
- Hayanikeri, na unaweza kukamilisha, na mimi mtulivu mno sasa hivi.
- Kwa ukweli, je wewe unakinishwa na maandiko ya torati uliyo yataja?

www.path-2-happiness.com

- Ukweli ukweli… hapana.
- Kwa nini?
- Je, sijakuambia kuwa torati imejaa upotoshaji, ukatili huu hauwezi kutoka kwa Mungu mwenye huruma!
- Umesema kweli… Mungu ni mwenye huruma sana kwa waamini wake.
- Ili nikurejeshe tena katika jinsia na mwanamke hebu sikiliza yaliyozungumzwa katika andiko hili la torati: “Kuanzia sasa waueni watoto wa kiume na kila mwanamke aliyeingiliwa na mwanamme, ama watoto wa kike na wanawake ambao hawajaingiliwa waacheni kwa ajili yenu.” Kisha Levi akatabasamu kwa mara nyingine na akasema: chukua andiko hili tena: “Wakawausia wana wa wakisema: Nendeni katika mashamba ya mizabibu na jificheni humo, Na subirini hata watakapotoka wasichana wa Shilo kwa ajili ya kucheza nendeni upande wao, watekeni kwa ajili yenu kila mmoja mwanamke mmoja kisha torekeni nao katika ardhi ya i.” Kisha Levi akacheka kwa dharau na kusema: Tumerejea tena kwenye jinsia na wanawake isipokuwa maelezo ya sasa yanahusu kuuwa na kutekwa! Je, tuache tena maudhui haya?
- Jambo la kushangaza kabisa! Siamini ninachokisikia! Ndio, tuachane na maudhui haya vile vile, lakini samahani ni nani hawa watoto wa kike wa Shilo? Ni nani hao Shilo?
- Shilo ni Wakristo au masaya katika moja ya tafsiri tuliyo nayo, la msingi ni wale wanawake ambao sio Wayahudi kama vile wanawake wenu na wanawake wa Kiislamu, nisamehe kwani umenifedhehesha, na hivyo akili yangu kuchanganyikiwa.
- Hamna neno, nadhani wakati umetutupa, nakualika chakula cha usiku ili upate utulivu kisha uondoke…
- Ooh …sijatanabahi na muda, sasa hivi ni saa tatu usiku, ikiwa inatoka kwako hamna neno nawafiki, vinginevyo naomba niondoke ukiniruhusu.
- Sipendi mazungumzo kwa njia hii, mimi sijaja nikuamrishe nimekuambia kuwa nimefurahi kwa ukweli wako, nimefaidika sana nawe katika njia ya kuelekea furaha, na mimi napenda kukaa nawe ukiwa katika hali ya matakwa yako mwenyewe.
- Asante sana kwa wema wako, tutaonana kesho.
- Tumekubaliana tuonane kesho kutwa Jumamosi!
- Ziara yetu kutembelea sehemu takatifu za Kiyahudi ni kesho kutwa, lakini

tunaweza kukamilisha mjadala wetu kesho ukipenda?

- Tutakutana kesho nitakapokuja kukutana na asubuhi, lakini ningependa kulitemblea Kanisa la Kiyama na Kanisa la Bikira Maria ikiwezekana.
- Kanisa la Kiyama (la siku ya mwisho) sio kanisa la Kiprotestant na wewe unaniambia kuwa ni Mprotestant… kisha akasema: je unanidanganya?
- Kwa nini nikudanganye? Nitalitembelea kwa sababu nimemuahidi mke wangu Mkatoliki kuwa nitalitembelea.
- Wewe unampenda mke wako sana, nitakutumia dereva saa mbili asubuhi ili akulete ofisini uonane na , na ujitahidi kutoka mapema ili uweze kuyaona makanisa hayo mawili kwani kesho ni Ijumaa.
- Ina maana gani kuwa kesho Ijumaa?
- Ina maana kuwa ulinzi na vizuizi barabarani ni vingi, ili wahakikishe kuwa magaidi hawawezi kulipua wakati wanapokwenda kuswali swala ya Ijumaa.
- Saa mbili nitakuwa tayari ili kuelekea ofisini…kisha akasimama na kumpa mkono Levi akiwa anamuangalia machoni, na kusema: nakushukuru sana na nisamehe kwa kukusumbua.
- Mimi haswa ndio wa kukushukuru kwa ukarimu wako na wema wako na ukweli wako na uaminifu wako kwa mkeo na misimamo yako.
- Nawe ni mtu mzuri kabisa.
- Ni kiasi gani nami natamani kwenda pamoja nawe katika njia ya furaha ambayo unaiendea, ila mazingira yangu hayanisaidii.
- Nani anajua? Huenda ukaweza…Tutaonana kesho asubuhi ewe mrembo.

Joji alikula chakula chake cha usiku haraka baada ya kuondoka Levi na sura ya Levi bado ilikuwa machoni mwake, alikuwa akihisi kuwa karibu nae, lakini hakujua ni kwa nini? Je ni kwa sababu ya uzuri wake wenye kufitinisha? Au kuwa kwake mkweli? Au ni kwa sababu tu ya kuvutiwa nae? Alijihisi akiwa ana babaika, anakumbuka tabasamu lake… machozi yake…. Ghadhabu zake na hasira…..yote hayo yalibaki akilini mwake.

Alimsikitikia ya kuwa ni mmoja katika wahanga wa mafundisho yaliyopotoshwa yenye kiza… vipi maskini yule atawezaje kukabiliana na dhulma na mipaka na hata uhuru wake kuchupwa pamoja na haki zake kwa jina la Mungu!!

Alipanda chumbani kwake, na kufungua television akijaribu kumsahau Levi na uzuri wake ili aangalie habari, habari ya magaidi kulipua London

www.path-2-happiness.com

ilianza kupungua, lakini aliona na kusikia katika habari hizo kuwa wahusika wa ulipuaji huo walikuwa ni wafuasi wa harakati za SIITA zilizojitenga, na ya kuwa yule Mpakistani aliyekuwa anatafutwa amepatikana; kwani aliogopea tukio lile na kujificha sehemu katika pambizoni mwa London, ambapo baadae aliachiwa huru kwa kuthibitishwa kuwa hakuhusika na chochote… kuhusu Mpakistani yule Joji alijisemea nafsini mwake: Kumethibitika kutohusika kwako ewe Karimullah.

Kisha baada ya hapo ilikuja habari za matayarisho ya serikali ya Israeli kuhusu siku ya kesho Ijumaa. Katika taarifa hiyo serikali iliwakataza watu wote walio chini ya miaka hamsini wasiswali katika msikiti wa Aqswa kwa kuhofia ulipuaji….

Joji alizima televisheni na kufungua barua yake pepe, na kurudisha majibu ya barua alizopokea, kisha aliamua kuandika baadhi ya maandiko ya torati aliyoambiwa na Levi kisha kuzituma kwa Tom pamoja na Adam. Alimaliza kuandika na kuzituma wakati huo ilikuwa ni saa tano usiku, akajiegemeza kitandani alale, lakini ile fikra yake kwa Levi ilikuwa bado haijaondoka, Joji alijiuliza Je, alikosea alipokataa kulala nae! Ingekuwa furaha ya kiasi gani kama angemkubalia, kwani Levi alikwisha kuwa tayari kwa hilo. Hii haikuwa ni mara yake ya kwanza kwani Levi alikwisha wahi kufanya hivyo na mkuu wake wa kazi ambae ni Kakhi, ni maadili gani haya ambayo yanatunyima ladha ya maisha?! Wala Joji hakufahamu kwa nini, muda huo huo akakumbuka wivu wake na hasira zake alipofikiria kuwa Katarina alikuwa akimfanyia hiana pamoja na Tom. Alijisemesha moyoni: Ni mgongano gani ninaoishi? Napenda kufanya hiana lakini wakati huo huo naichukia na ninatoa rushwa na nawaona wanaopokea kuwa hawana maadili, ni kiasi gani natamani kunyooka kwa roho yangu, fikra zangu, maisha yangu na furaha zangu na maadili yangu…

(4)

Ilipofika saa mbili asubuhi Joji alikuwa ameshamaliza staftahi yake, alipanda chumbani kwake huku akimsubiria dereva afike. Ilipotimia saa mbili kamili simu ilipigwa kutoka mapokezi na kumjulisha kuwa kuna mtu anayemsubiria hapo mapokezi. Alipoteremka kwa mshangao akamuona kuwa aliyekuwa akimsubiria ni Levi na si dereva kama Levi alivyomjulisha jana,

- alifurahishwa sana kumuona na kutabasamu kisha kumpa mkono….

- Sikutaka kukusumbua
- Wewe unastahiki…..Kama ambavyo mjadala wako unanipendeza sana.
- Asante sana kwa kunisifu na tabia yako nzuri, je yupo ofisini hivi sasa?
- Anakusubiri ofisini, nimemjulisha kuwa utakwenda kwake.
- Asante, kwani nimesahau kuwasiliana nae.
- Alitabasamu tabasamu zuri lililong'arisha uso wake….
- Baada ya kutoka kwako tu na kabla ya kufika nyumbani alinipigia simu ili ahakikishe kama nimelala kwako, hakuamini nilipomwambia kuwa wewe sio Kakhi na wewe hutaki hilo, nikamjulisha kuwa utakuja asubuhi na anaweza kuhakikisha hilo mwenyewe.

Alimuangalia kwa makini huku akisema:

- Nani aliyesema kuwa sikutaki?!

Levi alibabaika na usoni mwake ulionekana mgongano wa hisia zake, rai, fikra na matamanio yake…

- Unakusudia nini? Je kuna chochote kilichobadilika baada ya kuondoka kwangu?
- Ha ha ha, nakutaka wewe na elimu pamoja na utamaduni ulionao na akili na maadili yako. Ama kiwiliwili chako ni johari ambalo natamani kuliangalia kwa umakini na ni kama ua natamani kulinusa, lakini ni fedheha kumuangalia mwanamke kama kiwiliwili tu, na sipendi kukukosa kama nilivyokuwa sipendi kuacha misimamo yangu.
- Levi alifuta kwa mkono wake wa kushoto paji lake la uso akiwa ananyanyua fundo la nywele zake.
- Ah ah ….sijui kwa nini nimekuwa nina hofu sana?
- Je ulimwambia kuwa tumechukua fikra yake ya kwamba tutakwenda kutembelea sehemu takatifu?
- Hapana, mjulishe wewe.
- Kwa kweli, sijihisi utulivu na , na ninahisi kudhalilishwa kwa kuwa naachana na misimamo yangu na kumpa rushwa, hata hivyo ni kwa sababu sijalifikiria jambo hili kwa utulivu kabla ya kuja kwangu vinginevyo ningekataa, kwa ujumla tumalizie maudhui sasa hivi na baada ya kurejea kwangu tutaendelea kwani kwa kila tukio lina mazungumzo yake.
- Vizuri, kwa sababu hujampa fedha ndio maana anadhania sijafanya kazi yangu vizuri.
- Maisha ya hovyo ambayo mtu anaachana na misimamo yake kwa ajili ya mali au

www.path-2-happiness.com

tamaa ya ngono au kwa sababu ya cheo!

- Ninaweza kuonekana kama najigonga mwenyewe, lakini kama sio watu kuachana na misimamo kwa ajili ya mali, matamanio ya kijinsia, basi Israel isingesimama, na kuendelea na kubakia hadi hivi leo.
- Ni kiasi gani najihisi kuwa ni mtu wa hovyo nami nikielekea kutoa rushwa, na sijui kwa nini sikufikiria jambo hili aliponiambia Kakhi!
- Kwa hali yoyote ile tumeshafika kwenye shirika, utakuta mikataba yote ipo tayari kwa ili usaini.
- Natamani tumalize haraka, nahitaji baada ya kumaliza dereva anichukue kutembelea makanisa.
- Samahani.. siwezi kukuchukua kukupeleka kwenye makanisa mwenyewe, dereva atakusubiri ili akupeleke.

Joji na Levi waliingia kwa naye alisimama kumkaribisha Joji na kumpa mkono hali ya kuwa ametabasamu…

- Siku yenu ya jana ilikwenda vipi? Na usiku wenu ulikuwaje?
- Ilikuwa ni siku yenye shughuli nyingi ambapo tumemaliza shughuli yetu na Levi.
- Ndio… Levi amenijulisha kuwa upo tayari kusaini mkataba, na ya kuwa umejibu maswali yake yanayohusiana na mambo ya teknolojia, kisha alimgeukia Levi na kusema: Unaweza kumalizia kazi zako hivi sasa kiasi cha mimi na Joji kusaini mkataba.
- Nitaondoka; kwani nina kazi…kisha alimgeukia Joji: utakapomaliza kazi zako utamkuta dereva akikusubiri.
- Kwa nini dereva? Unaweza kumchukua Levi? Kwani hakukufaa? hakukupendeza?
- Tumekubaliana kutekeleza mapendekezo yenu kutembelea sehemu takatifu kesho pamoja, ama leo ningependa kutembelea makanisa matakatifu.
- Vipi ilikuaje jana na Levi?
- Nzuri sana.
- Nilishangaa aliponipigia simu saa tatu unusu usiku na kunijulisha kuwa yupo karibu na nyumbani, ulikuwa unaweza kuchukuwa wakati nae zaidi madamu umenisifia kuwa amekuwa mzuri kwako.
- Tulimaliza mjadala wetu saa tatu usiku kisha akaondoka, na nilikujulisha kwenye simu kuwa nataka kukuona ili kusaini mkataba na kumaliza maudhui haya…hii ni cheki nakupa imetoka kwa Kakhi.
- Asante sana wewe pamoja na Kakhi, na hii mikataba ipo tayari kusainiwa.

- Tumemaliza?
- Tumemaliza mikataba, lakini umebakiwa na siku tatu kwetu, mimi pamoja na Levi tupo tayari kukukirimu.
- Asante kwa ukarimu wako.
- Hata baada ya kumaliza matembezi yenu kesho pamoja na Levi anaweza kuja mkakesha naye hotelini na yeye Levi yupo tayari kwa hilo.
- Nadhani nitakuwa mchovu baada ya matembezi, nitahitaji kupumzika na kulala mapema, na sitoweza kukesha!!
- Ha ha ha, jaribu akustareheshe Levi… alipokuwa akija Kakhi kusaini mikataba hakuwa akipumzika kabisa ila tu alipokuwa akistareheshwa na Levi.
- Tumeshatia saini mkataba na tumemaliza, je ninaweza kuzungumza nawe maudhui mengine yasiyokuwa na mahusiano na mikataba?
- Sijafahamu unachokitaka? haya uliza.
- Nitasema kwa ukweli kabisa bila ya kukuonea haya: Kwa nini unachukua fedha ili usaini mikataba? je hii sio rushwa?
- Ha ha ha, kama unapenda ukweli, kwa nini nawe na Kakhi mnastarehe na Levi ili kusaini mikataba?! je hii nayo sio rushwa ya kijinsia?!
- Ndio, ni rushwa ya kijinsia, na hiyo ndio moja ya sababu mimi kukataa kufanya hivyo.
- Kakhi hakuwa hivyo, bali akitaka kwa uwazi kabisa, ama kutaka kwako jana ilikuwa ni kwa ishara, pamoja na kama ulivyosema kuwa hukustarehe na Levi na hili ni tatizo lako wewe na kama ni rushwa kama usemavyo kwanini basi umenipa mimi?!
- Inaelekea maneno yako ni sahihi na yenye mantiki, kwa nini nitoe kama ni rushwa kwa ujumla je mali na wanawake wanakuletea furaha?
- Bila ya shaka, furaha ya duniani ni matamanio ya kijinsia, mali na utawala … kisha akapumua na kusema: hata kama matamanio haya yenyewe yatatuletea tabu na mashaka?!
- Sijafahamu itakuwaje ni starehe za maisha na raha zake zikatuletea mashaka na tabu?
- Hii ni migongano ya maisha ewe rafiki yangu, mambo ya kijinsia, mali pamoja na utawala ni mambo yenye furaha katika maisha ya kihisia, lakini wakati mwingine yanadhulumu na kuzipa tabu roho zetu, sawa sawa na zilivyo sikukuu zetu zilizokuwa mbali kabisa na furaha. Je sikukuu hazitarajiwi kuwa ni siku zenye

www.path-2-happiness.com

furaha zaidi katika masiku yetu? Nitakujibu ndio, lakini sisi kwetu sikukuu zetu ni siku za huzuni kwetu.

- Inakuaje hilo?
- Levi anaweza kukujibu zaidi yangu … Ha ha ha, nae ni mzuri hali kadhalika, unaweza kukamilisha mjadala nae, katika sehemu ambayo itakupa utulivu.
- Nakushukuru sana.

Joji alitoka kwa , na akamuuliza sekretari ilipo ofisi ya Levi, kisha akaenda kwake… aliingia ofisini mwa Levi, akaanza kwa kumuuliza kwa shauku:

- Kimetokea nini kati yenu?
- Nahisi kudhalilika, nimempa rushwa, na tumesaini mkataba.
- Je, umezungumza nae kuhusu rushwa au kuhusiana nami?
- Ndio, tumezungumza kuhusu wewe sana, samahani bado ananiaridhia kiwiliwili chako… kisha akatabasamu, na kusema; kipya ni kuwa kanitaka nikuulize baadhi ya maudhui.
- Kuniulizia mimi?!
- Nilipomzungumzia rushwa alinifedhehesha kuwa mimi na Kakhi tunachukua rushwa, lakini sio rushwa ya mali bali ya kijinsia, kisha akanifedhehesha kwa mara nyingine kuwa mimi ndie ninayetoa rushwa na yeye ndie anayepokea, sote tupo sawa.
- Kwa masikitiko ni kuwa mwanadamu wakati mwingine anao uwezo wa kujadili na kuhalalisha makosa yake.
- Unamkusudia nani?!
- Namkusudia , kisha akanyamaza kidogo na kusema: Na mimi vile vile, na samahani na wewe hali kadhalika.

Joji aliangalia chini ya sakafu kwa masikitiko na kusema:

- Umesema kweli .. muda wa kuwa falsafa yetu ya furaha zetu katika maendeleo yetu badili ya falsafa yetu ya kuhalalisha makosa yetu na rushwa?
- Lakini hukunijulisha unachotaka kuuliza?
- amenijulisha kuwa hii ni tabia ya maisha; nayo ni magumu, furaha na starehe zake ni katika yanayotupa tabu roho zetu, mfano wake ni kama sikukuu zetu zenye kuhuzunisha ambazo zilitakiwa ziwe zenye kufurahisha.
- Huenda ikawa katika hali ya upotofu ambayo tumezungumzia hapo kabla, yaani kuwa Uyahudi ni dini ngumu, tatizo sio katika ufahamu wako, bali ni katika ugumu wa ukweli uliopo katika Uyahudi, la msingi ni kuwa sikukuu za kiyahudi

ni sikukuu zisizokuwa za furaha bali ni za huzuni mara nyingi.

- Kwa nini?
- Sikukuu zimewekwa maalumu kwa sababu ya ibada, na ibada ya Mayahudi ni ibada ya kulia na huzuni, je hukuwahi kusikia kuhusu ukuta wa kilio?!. Lakini sikukuu zetu muhimu zaidi ni zile tuziitazo Jumamosi ya Jumamosi yaani siku ya kusamehewa ambapo tunafunga zaidi ya masaa ishirini na nne usiku na mchana wala hatufanyi jambo lolote isipokuwa kuabudu tu. Sikukuu zetu ni nyingi sana, pamoja na haya Mayahudi wengi na haswa zaidi masekula wanazingatia sikukuu hizi kuwa ni siku za likizo na furaha tu, na wao hawafanyi ibada ila mambo ya juu juu tu.
- Hili sio muhimu, je inawezekana tuwe na maisha magumu kiasi cha kukosa furaha ila katika yale yanayotupa shida na kutuumiza?!
- Kwa masikitiko mara nyingi swali hili ninajiuliza na sikuweza kulijibu pamoja na kuzama kwangu katika torati na talmud. Huenda ikawa hivyo kutokana na ugumu wa nafsi ya kiyahudi au dini ya Kiyahudi, na huenda hili likanihitajia mimi nielimike zaidi ili nifikie katika majibu.
- Sijui… lakini nachukia mambo kufanywa magumu, na nadhani halitupeleki popote isipokuwa kwenye tabu tupu.
- Nami nachukia mambo kufanywa kuwa magumu, lakini ndio nimeshatumbukia, kwa hali yoyote ile umechelewa kwa Dr. Habib na sasa hivi ni saa nne na muda umeshakutupa mkono, bora umfuate yupo nje anakusubiri.
- Ni nani huyo Dr. Habib?
- Ni mtafiti wa dini mbali mbali ni Mkristo Mkatoliki… Nimemchagua kwa kuwa naamini ni mtu atakayekufaa kusuhubiana nawe.

Joji alinyamaza kwa muda, hakupenda kumuacha Levi, alijaribu kujaza macho yake uzuri wa Levi, nywele zake zinazoanguka mabegani, macho yake yenye kuthibitisha uhai wake na kiwiliwili chake na mwendo wake unaovutia... Je nilikosea pale nilipokataa kulala nae ili niondoshe kiu nilichokuwa nacho kwenye kiwiliwili changu? Je ni kweli alichokisema kuwa starehe za kiwiliwili zinaipa tabu roho, ooh, nimesahau kujadiliana nae kuhusu jambo hilo!

Levi nae alihisi muangalio wa Joji kwake ni kama vile mtu aliyemkumbatia katika kila sehemu ya kiwiliwili chake, hakujua kwanini alisisimkwa kwa muangalio huu, je Joji anamtaka astarehe nae? Sasa kama ni hivyo kwa nini alimkataa pale mwanzo? Au ni yeye Levi alikataa ili Joji amfuatilie lakini

www.path-2-happiness.com

hakufanya hivyo, kisha naye Joji kwanini alimkataa na huku akimuangalia kwa matamanio, je amebadilisha rai yake? Huenda ikawa hivyo, je amfungulie maudhui ili alale kwa Joji leo hii, au afanye nini?!!!

- Nakushukuru sana, na nitakusubiri kesho saa mbili asubuhi.
- Asante sana Joji.

Joji alitoka na kumsalimia Dr. Habib ambae alimkaribisha, kisha wakaondoka kwenda kwenye gari lake….

- Tutaelekea kwanza katika Kanisa la Kiama (ufufuo), kwani leo ni Ijumaa na kuna vizingiti vingi barabarani; na huenda tukachukua masaa mawili.
- Masaa mawili?!
- Kwa bahati mbaya ndio, kawaida ni mwendo wa dakika arobaini na tano hivi tu, lakini kwa kuwa leo ni Ijumaa njia zote hufungwa kutokana na uchunguzi barabarani.
- Pamoja na tatizo la wakati kuwa mkubwa na lenye kuchosha lakini jambo hili linastahiki usumbufu huu. Ugaidi umekuwa ni balaa kwa wanadamu.
- Ugaidi wa Waarabu Waislamu.
- Ugaidi gani unaouzungumzia?
- Samahani, mimi ni Muarabu Mkristo tena Mkatoliki na sio Muislamu, lakini ugaidi wa kweli ni wa dola ya Kiyahudi, kwa nini inawakataza watu kuswali katika misikiti yao, kuna ugaidi gani watu kuswali katika misikiti yao?!
- Samahani, mimi sio mtaaalamu wa historia wala siasa wala dini, na inaelekea mbele yangu kuna mtaalamu, lakini hao Waislamu si ndio ambao wanajilipua wenyewe, na wanalipua treni na mabasi kuwaua Mayahudi?!
- Swadakta wao wanafanya hivyo, lakini ni kwa nini mtu anafikia kufanya hivyo na kujiua mwenyewe?
- Katika uzoefu nilionao ni kuwa mtu hawezi kujiua ila atakapofikia katika hali akaona kuwa mauti ni bora zaidi kwake kuliko uhai.
- Sasa ni nini kilichowapelekea Waislamu kufanya hivyo?
- Sijui kilicho wapelekea kufanya hivyo?
- Ni dhulma, mateso, nchi yao kukaliwa kimabavu na udhalili.
- Unaelekea unawatetea sana Waislamu.
- Kamwe, mimi sio Muislamu, lakini nawatetea wakazi wote miongoni mwa Waislamu na Wakristo, ambao heshima yao imeondolewa na kuibwa ardhi yao na haki zao, fikiria sisi Wakristo tunafukuzwa na kuhama Palestina na sehemu

zetu takatifu zinadhalilishwa.

- Lakini nyinyi hamlipui kama Waislamu?
- Sisi ni wachache hapa pamoja ya kuwa tunadhalilishwa ila ni afadhali sana kuliko wanavyofanyiwa Waislamu; na yote inatokana na nafasi ya Wakristo ulimwenguni.
- Sasa kwa nini wasiwajali Waislamu kama walivyo sehemu nyingine ulimwenguni?!
- Kwa uwazi na kwa ufupi: Sisi tunaishi katika ulimwengu ambao hauheshimu isipokuwa nguvu tu.. achana na hilo….je unajua Kanisa la Kiama?
- Ndio, kiasi fulani, nimesoma sana habari zake.
- Vizuri, pamoja na kuwa wewe ni Mprotestant kama alivyo nijulisha Levi.
- Ndio, inaelekea Levi amekujulisha kila kitu.
- Namjua Levi tokea miaka mitano iliyopita, na sijamuona alivyomjali mtu kama alivyokujali wewe.
- Ama mimi ni jana tu ndio nimefahamiana na Levi, nashukuru kwa wema wake… umefahamiana vipi na Levi?
- Alinijia akiwa amechoshwa na dini yake ya Uyahudi na alikuwa anataka kuwa Mkristo, alijadiliana nami sana kuhusu Ukatoliki, Levi ni mpenzi wa mjadala.
- Je alibadilika tena kuwa Mkristo?
- Bila shaka hapana, hakukinaishwa na Ukatoliki wala Uyahudi pamoja na kuwa yeye ni mtu wa dini sana, na ametoka katika familia ya watu wenye dini, na mtu anayebadilisha dini na kuwa Mkristo anaweza kuuwawa au kufungwa au kuadhibiwa kwa adhabu yoyote ile.
- Kwa nini hakukinaishwa na Ukatoliki.
- Huenda ni kwa sababu ya migongano iliyopo ndani yake, na huenda ikatokana na tabia ya ugumu wa Uyahudi ulivyo.
- Na huenda ikatokana na tabia ya ugumu wa Ukatoliki.
- Ha ha ha, huenda ikawa hivyo.
- Levi amenijulisha kuwa wewe ni mtafiti wa mambo ya dini mbali mbali.
- Ndio, mimi ni mwalimu wa Chuo Kikuu nafundisha somo la historia ya dini mbali mbali.
- Je unaweza kunihadithia historia ya dini mbali mbali Palestina?
- Maudhui ni mepesi sana, pamoja na ugumu wa kisiasa na wa kidini uliojificha ndani yake.
- Napenda wepesi huo … nieleze wepesi wenyewe ulivyo.

www.path-2-happiness.com

- Kwa hali ya wepesi kabisa…bila ya shaka ardhi hii ilikuwa imekaliwa kabla ya dini zote, na kila dini ya mbinguni imepita katika ardhi hii takatifu, Uyahudi uliutangulia Ukristo na Uislamu. Kabla ya dini zote hizi kulikuwa kuna watu wanaishi, na kila dini iliyopita ikachukua sehemu ya ardhi hii kwa watu wake kuwa katika dini hiyo, na wote waliweza kuishi pamoja, lakini Uyahudi uliokuja hivi karibuni wakataka wenyewe tu –waishi peke yao na wawaondoshe wengine na wawauwe.
- Je Waislamu hawakuwafukuza watu hapo kabla?
- Kamwe, Makanisa yetu hayakudhulumiwa tokea wakati alipofika Omar bin alKhatwab.
- Vipi kuhusu vita vya msalaba?
- Vita kati ya dini mbili na kati ya wakazi wa asili Waislamu pamoja nao baadhi ya Wakristo na kati yao na watu wa msalaba walipokuja kutoka Ulaya, hata hivyo kabla ya hapo watu walikuwa wakiishi pamoja kabla ya kuja watu wa msalaba kutoka Ulaya.
- Je Wakristo nao hawakuwatesa Mayahudi.
- Pamoja na kuwa mimi ni Mkristo ila ni kuwa katika zama zetu Wayahudi waliteswa Ulaya na sio Palestina, ama nchi hii ni nchi ya kusameheana… Ama hapo zamani dola ya Warumi iliwauwa Wayahudi na kuhalalisha damu zao baada ya Issa kupewa utume na Wayahudi kumkadhibisha.
- Inaelekea Uarabu wako unakuvuta uwaonee huruma Waislamu zaidi, kwa sababu Uislamu ni dini ya Waarabu, kuliko hata kwenye Ukristo wako!
- Huenda ikawa hivyo, lakini Uislamu sio dini ya Waarabu, Waislamu wengi sio waarabu, nami ni muarabu lakini sio Muislamu, ama kisomi ningependa hata majibu yangu yawe kwa njia ya usomi. Waarabu walifika Yerusalem kabla ya Uislamu, je Ibrahim hakuwa ni baba yake Yaqub na Ismail? nao walikuwepo kabla ya Uislamu na kabla ya Uyahudi?!
- Samahani kukukatisha, inaelekea mitaa ya hapa ni ya kizamani sana.
- Ndio, tumekaribia mji wa kale ambao una kanisa la Kiama, je hukuona kuwa tumepita zaidi ya vituo kumi na tano vya uchunguzi.
- Nasikitishwa na kuhuzunishwa na hali ya watu wazima kuwa katika foleni ya kupekuliwa!
- Kilichonisaidia mimi ni Ukristo na nafahamika na askari wa barabarani ndio maana tumepita haraka. Ama watu wazima ni kuwa kuna ambao umri wao chini

ya miaka hamsini wanakatazwa kwenda kuswali leo –yaani wanakatazwa kuingia kanisa la kiama hata kama ni mimi na wewe basi tusingeruhusiwa kutokana na taratibu za hapa.

- Inaelekea mji huu wa kale una hazina ya kumbukumbu nyingi za Ukristo!
- Ndio, hata Waislamu pia.
- Na Wayahudi kadhalika.
- Wao wanasema hivyo, lakini historia na hali halisi haiwaungi mkono… kisha akatabasamu na kusema: ila ni kuwa nguvu wanayotumia kuungwa mkono ni muhimu zaidi katika ulimwengu huu unaotawaliwa na sheria za msituni.
- Unaelekea kuwakosoa sana Wayahudi!
- Elimu inasema hivyo, lakini huenda nikawa nawakosoa wao kwa sababu wameichukua ardhi yetu kwa mabavu na wameninyima uhuru wangu wa kuabudu.
- Acha hayo kwani kila dini inaona hilo, nadhani tumefika katika kanisa la kiama, au vipi?
- Ndio, unaweza kuona kuba yake na misalaba yake kule, tutamalizia sehemu zilizobakia kwa kutembea.
- Huogopei Waislamu?
- Ukiokoka na Yahudi basi mambo mengine ni mepesi tu, je umewahi kusikia Muislamu amemuua Mkristo Yerusalem?

Walitembea pamoja kidogo, mara mbele yao likajitokeza Kanisa kubwa la kale limejiinamia mbele yao, Joji alishangazwa na mjengo wa Kanisa, na akaendelea kuliangalia kwa mshangao.

- Utashangaa zaidi ukiingia ndani.
- Tuingie basi.

Walipoingia Joji aliangalia nakshi juu ya ukuta iliyoonesha Yesu akiwa msalabani, na chini yake picha kubwa ya Bikira Maria na picha ya Josefu Seremala.

- Naamini kuwa picha hii ingefaa zaidi katika Jumba la Makumbusho! Je picha kama hizi zinafaa kuwekwa makanisani, sehemu maalumu za ibada?
- Hii ni tabia yenu nyie Waprotestant hampendi picha makanisani…kisha akatabasamu kwa kebehi na kusema: Mnafanana na Waislamu katika hilo!
- Kwa mara ya kwanza mtu ananiambia tunafanana na Waislamu, wakati mara zote tunaambiwa tunafanana na Wayahudi.

Joji aligeuka na kuangalia kwa umakini mkubwa na kwa mshangao –kuba

www.path-2-happiness.com

iliyopitisha mwangaza uliokuwa ukienea, na kugawanyika katika mianga kumi na mbili.

- Hii ni nzuri sana, ni miongoni mwa maajabu ya ulimwengu, mwanga huu unaoshuka kutoka kwenye kuba inawakilisha jua ambalo linapiga kwenye uwazi uliokuwa katikati ya kuba uliokuwa kileleni, inatokeza na kububujika mianga kumi na mbili, na hii ni dalili iliyo wazi kuwa Yesu amesimama kama alfajiri ya siku mpya, na mitume kumi na mbili: ni kama vile mianga ya imani katika ardhi. Kuba hii ilijengwa na kukamilika tarehe mbili Januari mwaka 1997.
- Nzuri sana, unahisi roho ya imani unapofika sehemu hii takatifu.
- Pamoja na kuwa nyinyi Waprotestant hampendi sehemu hii sana!
- Ha ha ha ni nani ambae hapendi sehemu ambayo ndani yake kuna mbao ambayo Yesu amesulubiwa!
- Kanisa hili wanaolijali zaidi ni Wakatoliki na Waorthodoksi.
- Waislamu walilivunja hapo kabla! Na wewe unasema kuwa Waislamu hawakuvunja sehemu yoyote ya ibada!
- Umesema kweli –lilivunjwa na utawala wa Fatimi…, na katika historia vile vile aliuvunja Uislamu kama alivyo uvunja Ukristo, pamoja na hayo waliruhusu lijengwe baada ya miaka arobaini…Mimi sio Muislamu wala sioni tabu yoyote kuzungumzia dhulma za Waislamu ambazo zilikuwepo katika historia, hata hivyo huwezi hata mara moja kuzilinganisha na dhulma za Mayahudi. Kwa masikitiko nasema kuwa hata kulinganisha na dhulma za Wakristo kwa Mayahudi, kwa mnasaba mtu wa kwanza kujenga kanisa hili ni mtu kutoka Syria na sio Ulaya jina lake lilikuwa ni “Zinobious” mwaka 336 A.D.
- Ajabu, hakuna watu wengi kanisani.
- Kwa sababu misa inafanywa siku ya Jumapili kama ujuayo, na leo Ijumaa na njia nyingi hazipitiki ila kwa tabu, vinginevyo hili ndilo kanisa linalotembelewa na watu wengi zaidi duniani na sehemu takatifu zaidi Ulimwenguni.

Joji alisali kanisani akitekeleza ahadi ya Katarina, na wakatembea sehemu mbalimbali za kanisa hilo pamoja na Habib ambae alikuwa akijibu maswali yake na kumuelekeza vivutio mbali mbali vya kanisa …kisha wakaondoka ili kwenda katika kanisa la Bikira Maria–Habib alipoangalia saa yake ilionesha kuwa ilikuwa ni saa nane kasorobo….

- Nataraji tusije kuchelewa zaidi, tuna muda wa saa hadi saa unusu kufika katika kanisa la Maria, na kurudi tutahitaji saa hadi saa na nusu nyingine, ni matarajio

yangu turejee kabla jua halijazama…

- Vizuri, samahani ningependa kupumzika garini kidogo kwa muda wa nusu saa hivi, najihisi uchovu.
- Vizuri, pumzika.

Joji alijilaza kwenye kiti na kufunga macho yake, alihisi matukio ya safari hii (ya Yerusalem) yakienda mbio mbio, alikumbuka kuwa alimaliza lengo lake la kwanza la safari yake kwa haraka sana, na akakumbuka lengo lake la pili, nalo ni kubaini njia ya furaha, alikumbuka mazungumzo yake na Levi na na Habib vile vile, yote hayo yalikamilika kwa muda wa siku moja na nusu tu. Sasa hajui kutatokea nini baada ya siku mbili na nusu zilizobakia.. alimkumbuka Katarina, Tom na Adam, kiasi gani alitamani kama angekuwa nao wote na wakasikia mazungumzo na mijadala yake, alihisi kupata dozi kubwa kichwani mwake kiasi cha kutoweza kuweka na kuanisha rai yake binafsi katika maarifa na taarifa alizoona na kuzisikia. “Alikumbuka pia maswali yake mbali mbali na akamshukuru Mungu kuwa hayamsumbui tena kama ilivyokuwa hapo kabla pamoja na kuwa hajayasahau…Je hili linatokana kwa sababu anafanya kazi katika njia ya furaha? Lakini maswali yake mbali mbali kuhusu njia ya furaha na maarifa yake mengi bado yanamchosha vile vile, wakati akiwa katika fikra hizi mbali mbali na migongano mara usingizi ukamchukua na akaingia katika ulimwengu wa ndoto.

(5)

Joji alipoamka, aliweka kiti chake vizuri na kumuangalia Habib:

- Samahani inaelekea nilikuwa nimechoka!
- Inaelekea hivyo.
- Oh, nimelala muda wa saa nzima! Muda gani umebakia tufike kanisani?
- Imebakia robo saa hivi tu…..kisha akaendelea huku akitabasamu: Inaelekea kuna migongano mingi ya ndani, kuanzia Katarina, Tom, Adam, Kikongwe na Maiko, Jiyostana, Kakhi na Levi…
- Umeyatoa wapi majina haya?!
- Ulikuwa unayataja mara kwa mara ulipokuwa umelala.
- Inaelekea nimechoka kweli, nahisi matukio na maarifa mbali mbali kuingiliana kichwani, kadhalika nahisi mwili wangu mzito sana.
-

www.path-2-happiness.com

- Ikiwa mtu hajaweza kutatua kadhia zake za ndani na fikra zake basi zitaingia kwenye nafsi yake na roho yake na kumsumbua.
- Hili huenda likawa ndio tatizo langu haswa.
- Kwa mnasaba nimefurahishwa na neno ulilotumia mara kwa mara.
- Lipi hilo?
- Njia ya furaha, ulikuwa unasema mara kwa mara nataka njia ya furaha, neno zuri sana.
- Unaonaje tuzungumzie kuhusu njia ya furaha, nataka kukuuliza swali?
- Karibu uliza.
- Je wewe ni mwenye furaha?
- Swali kubwa sana, je linawezekana kujibika?
- Ndio, nadhani linawezekana.
- Dini zote, fikra nyingi na madhehebu tofauti zinataka hilo.
- Wewe ni mwalimu wa historia ya dini mbali mbali ni dini ipi ipo karibu zaidi na furaha?
- Kwa mara ya kwanza naulizwa swali hili kubwa…kwa muda mrefu nimejitahidi kufikia jibu hilo, na bado naendelea kufanya utafiti huo.
- Je unadhania mtu anaweza kufikia njia hiyo bila haja ya kuwa na dini?
- Hili haliwezekani kabisa, elimu itathibitisha kuwa watu wengi katika hao wakanao dini ni wagonjwa wa maradhi ya nafsi na maradhi ya kiakili na ya kuwa wao ni waongo kwa ukanaji wao wa dini.
- Sijafahamu …waongo katika ukanaji wao wa dini?!
- Yaani wanajifanya kukana dini, na ndani ya nafsi zao wanamuamini Mwenyezi Mungu Muumba, mtoa riziki, ukweli wa ukanaji dini ni kuikimbia dini na majukumu yake… si dini wala itikadi.
- Ikiwa dini ndio njia ya furaha, kwa nini basi hawezi kunijibu swali hilo mtafiti na msomi wa dini mbali mbali.
- Ni haki yako kusema haya, nami naendelea na utafiti wangu, na hivi karibuni nitafikia kwenye jibu.
- Niahidi kuwa utaniambia utakapofikia kwenye jibu hilo.
- Ninakuahidi, inaelekea unafuatilia mambo ya dini mbali mbali kama alivyonielezea Levi.
- Sipendi migongano, wala sipendi kuyafanya mambo kuwa magumu, napenda akili, roho na kiwiliwili ziwafikiane, kadhalika pamoja na misimamo na raha

zake, na napenda ukawaida pamoja na umakini.
- Vizuri, napenda unachokipenda, unaelekea ni mwana falsafa, ni lazima tumalize mjadala wetu lakini inaelekea kuwa tumefika katika kanisa la Maria Magdalena, hili hapa mbele yako.
- Ni uzuri ulioje mjengo wake!
- Hii ni fani ya ujenzi kutoka Russia, amejenga Alexandria, Mrusi na Kuba yake ya dhahabu yenye kupendeza juu ya jabali la mzaituni.
- Kama ni hivyo ni Kanisa la karibuni sana?
- Ukililinganisha na kanisa la kiama, ndio bila shaka, Kanisa la kiama limejengwa mwaka 335 A.D na kanisa la Bikira Maria limejengwa mwaka 1886 A.D. na baina ya kanisa hizi mbili ni miaka 1500.
- Nashangazwa kuwa alama za dini yetu ya Ukristo zimewekwa miaka mingi baada ya kufa kwa wenyewe kitu ambacho mtu anaweza kushuku utukufu wake!
- Kwa masikitiko maneno yako ni sahihi kwa asilimia mia moja, bali hata kitabu kitakatifu ni hivyo hivyo. Tafadhali karibu ndani kwani tumefika na hayo mengine tutamalizia tutakaporudi, natamani tumalize upesi kwa ajili ya kurudi kabla ya jua kuzama.
- Vizuri, tumalize haraka iwezekanavyo.

Walitembelea kanisa haraka haraka, na kitu kilicho mvutia Joji zaidi ni kuwepo kwa picha nyingi katika sakafu la kanisa, na Joji jambo hilo halikubali kama linafaa katika nyumba za ibada…kama vile alivyovutiwa na mapambo mazuri na kuba zake saba zilizokuwa zinamulikwa na jua, lilikuwa ni jengo zuri, Joji aliswali haraka haraka kisha wakatoka.

- Jengo zuri sana.
- Ndio; ni katika majengo mazuri sana.
- Ama nyie Wakatoliki mnapenda sana picha katika sehemu za ibada, ama mimi sioni kama hii inafaa katika sehemu ya ibada na yananikumbusha mahekalu ya wapagani.
- Kwanza:Kanisa hili si la Kikatoliki bali la Kiorthodoksi. Pili: Nimekuambia kuwa katika hili mnafanana na Waislamu.
- Siyo Kanisa la Kikatoliki?! Kwa nini basi Katarina mke wangu ametaka nisali humo?
- Sijui.
- Kwa kuwa wewe ni mtafiti na mwanazuoni wa dini mbali mbali; je unaweza

www.path-2-happiness.com

kunielezea tofauti iliyopo kati ya Orthodoksi, Ukatoliki na Uprotestant kwa mtazamo wako?

- Swali gumu na jibu tata.
- Kwani hupendi mambo mepesi? Ni wepesishie mimi.
- Nitajaribu, lakini kwa ujumla kuna tofauti mbali mbali na makundi mengi sana, nitafupisha kwa muhtasari katika makundi matatu makubwa uliyoyataja:
- Kwanza: Orthodoksi, yaani ni rai iliyokuwa sahihi au ya haki au iliyojulikana au iliyokamatana na asili ya dini na zote zinafanana nazo ni asili ya mwanzo, na ndani yake limetoka Ukatoliki; na maana yake ni, 'ya jumla' au ya ulimwengu tokea mwaka 451 A.D. na kutoka katika Ukatoliki likagawika Uprotestant baada ya harakati za islahi za kidini zilizoongozwa na Martin Luther ambazo zilisambaa Ulaya ya Magharibi kati ya karne mbili; karne ya kumi na nne na kumi na saba.
- Hivyo basi asili ni Orthodoksi na sio nyinyi Wakatoliki?
- Ndio, pamoja na kuwa tukiwalinganisha nanyi, sisi ndio wa asili na wa mwanzo zaidi kwenu Waprotestant, Ha ha ha, la muhimu Orthodoksi huitwa kanisa lao kuwa ni Kanisa la Mashariki au Kanisa la Kiyunani au Kanisa la Roma la watu wa Mashariki na wafuasi wao ni watu wa Roma ya mashariki; yaani mashariki ya Ulaya kama vile Warusi, nchi za Balkani na Ugiriki, makao makuu ya kanisa ni mji wa Constatinople, na wenye kufuata madhehebu haya ni kanisa la Misri, Armania na wa Ethiopia, ama idadi yao inafikia watu bilioni moja.
- Inaingia akilini watu milioni elfu moja!
- Ukatoliki, na kanisa lao linaitwa kanisa la Magharibi, na nchi hizo za Magharibi ni kuanzia Latin katika nchi za Italia, Ubelgiji, Ufaransa, Hispania, Ureno, Brazil. Kadhalika wana wafuasi–Ulaya na Amerika ya Kaskazini na Kusini, Afrika na Asia na wanadai kuwa mwanzilishi wake ni Mtume Peter mkubwa wa wafuasi wa Yesu, na ya kuwa Mapapa wa Roma ni wafuasi wao; na wanadai wao kuwa mama wa Makanisa na walimu wao. Kanisa hili linafuata utaratibu wa Kipapa na linaongozwa na Papa, na mkusanyiko wa Makanisa una haki ya kutoa matakwa ya Kipapa nayo kwa muono wao ni matakwa ya Kiungu; kwa sababu Papa ni mfuasi wa Peter mwanafunzi wa MasiyaYesu na wasii wake, na kwa ajili hiyo yeye ni mwakilishi na Mungu, huyo basi matakwa yake hayana mjadala na wafuasi wa madhehebu haya wanafikia milioni elfu moja (Bilioni moja).
- Vizuri, kamilisha kuhusu Uprotestant.
- Uprotestant; huitwa Kanisa la Kiinjili kwa maana ya kuwa wafuasi wa kanisa

hili wanafuata injili na wanaifahamu wao wenyewe bila hata ya kuwafuata watu wengine au kundi jingine, wala hawaamini kuwepo kwa ufunuo wala maono kwa watu wa kanisa, kwa ujumla wao ni wakristo, kwani wanaamini itikadi za msingi, na hawaamini kuwepo kwa siri nyingi za kanisa na ibada mbali mbali na sala zilizoratibiwa kanisani na mambo ya kuiga tu kwa mkumbo ….na walikataa baadhi ya vitabu katika kitabu kitakatifu na itikadi mbali mbali zilizoonekana kuwa ni takatifu.

- Mnataka kututoa kwenye Ukristo, hamna neno, ni nini tofauti za kimsingi kati ya makundi hayo matatu?
- Nimetaja tofauti za kimsingi na uliposema: Mnataka kututoa katika Ukristo, ukweli ni kuwa tofauti ni nyingi mno baina ya makundi haya kiasi cha kuwa wengine wameona kuwa ni dini tofauti na sio dini moja yenye makundi mbali mbali.
- Vipi? Nibainishie?
- Kila itikadi ya Kikristo ina tofauti na makundi mengine, na haiwezekani kuzichambua na sisi tukiwa garini, wao wanatofautiana kuhusu Mungu kuhusu Yesu na kuhusu kitabu kitakatifu na kuhusu ibada mbali mbali na mengineyo mengi sana.
- Itakuaje dini ikawa ni moja na tofauti zikawa nyingi kiasi hiki? Hapana shaka kuwa mojawapo ni sahihi.
- Fikra ya kuwa mojawapo ndio sahihi ndio kisa cha vita na ugomvi kutoka katika makundi haya.
- Vita?!
- Ndio, vita vilivyoua mamilioni ya watu, kwa mfano vita vya miaka thelathini kati ya mwaka 1618 hadi 16 48 vilivyopiganwa kati ya Protestant na Katoliki na nchi zingine washirika zilizoungana nazo, na vita hivyo viliondosha roho nyingi za Wazungu wa Ulaya yapata mamiloni ya watu, bali nchi ya Ujerumani peke yake walikufa nusu ya watu wake na wakazi wake kupungua kutoka watu milioni ishirini hadi kufikia milioni kumi na tatu na nusu!

Mazungumzo yale yalimchoma sana Joji; kwani anachukia ugaidi wa sura zote. alijiuliza: Je, njia ya furaha inaweza kuwa imejaa damu? Rehema zako Mungu wangu, wanadamu hawawezi kuwa na furaha katika unyama wa aina hii…

- Unyama gani huo?!

www.path-2-happiness.com

- Historia imethibitisha kuwa tofauti za kidini na itikadi mara nyingi zinabadilika kuwa ni migongano katika uhalisia, tukipenda jambo hilo au tukikataa.
- Historia ya ugaidi inasumbua sana!
- Ndio kwa masikitiko, na mara nyingi migongano ya kidini huwa ni mikali zaidi na yenye kuchosha kuanzia vita vya Mayahudi vya kuwatesa Wakristo na kumuua Yesu, kisha Wakristo nao kuwatesa Mayahudi, kisha Mayahudi tena kuwatesa Wakristo na Waislamu.
- Kwa mara nyingine tena hukutaja mateso waliyoteswa Wakristo na Wayahudi na Waislamu.
- Kwa sababu jambo hilo silijui katika historia, je unaweza kunipa mifano?
- Waislamu kuvunja Kanisa la Kiama.
- Kuna matukio mengi kama haya, mimi nazungumzia mateso ya jumla na mauaji na kuwakataza watu wasifanye ibada, Uislamu umekataza kuvunja nyumba za ibada na makanisa ya Wakristo na kuwaua, kilichotokea katika hayo huwezi kuita ni mateso.
- Inaelekea wewe ni Muislamu uliyejificha katika Ukristo.
- Ha ha ha, huenda ikawa hivyo, nani anajua, huenda nikawa Muislamu au Protestant siku moja. Je sikukuambia kuwa nyie mnafanana na Waislamu hampendi masanamu wala picha katika sehemu za ibada, kisha akamgeukia Joji na kusema:Au huenda nikawa pamoja nawe katika njia ya furaha, umenikumbusha… ni kipi kisa cha njia ya furaha?!
- Njia ya furaha kisa chake ni kirefu mno.
- Nifupishie na unielezee.
- Kwa ukweli nimechoshwa sana na maswali yenye utata kuhusu maisha, maswali yenyewe ni: Kwa nini tumeumbwa? Nani katuumba? Kwa nini tunaishi? Mwisho wetu ni nini? Na nikafahamu kuwa sitoishi maisha ya furaha hadi nijibu maswali haya yenye utata; hivyo basi nikaanza kutafuta njia ya furaha, kisha akatabasamu na kusema: Na yale majina uliyoyasikia kutoka kwangu usingizini yalikuwa ni majina ya watu niliokutana nao katika njia hii ya furaha.
- Na je ziara yako ya mji mtakatifu na mijadala yako ni sehemu ya utafiti wako wa njia ya furaha?
- Nimekuja kikazi, lakini kilichonisukuma zaidi ni hicho ulichokisema.
- Lini utaimaliza njia hii?
- Sijui, lakini nasisitiza kufikia, kisha akatabasamu na kumgeukia, na kusema: Na

njia ya furaha yenyewe ni njia nzuri!
- Inaelekea mimi, wewe na Levi kuna kufanana sana.
- Ki vipi?
- Alinijia mimi akitafuta furaha lakini si katika Uyahudi, hata hivyo Ukatoliki haukumkinaisha na mimi nilikuwa Muorthodoksi na kubadilika kuwa Mkatoliki na bado naendelea na utafiti.
- Ujaribu Uprotestant – huenda ikawa ni kimbilio lako, mara nyingi namwambia mke wangu Mkatoliki kuwa dini yenu ni ngumu kwa ibada nyingi na siri nyingi zisizo za kimantiki.
- Huenda ikawa hivyo, umefikia wapi katika njia ya furaha?
- Samahani, je, tumekaribia hotelini? Nadhani naumwa, mwili wangu wote ni mzito sana na nahisi kizunguzungu kwa mbali.
- Hamna neno, mungu akubariki, imebakia robo saa hivi.
- Nakushukuru sana nimefaidika sana nawe.
- Bali wa kushukuriwa ni Levi aliyenitambulisha nawe, nawe itabidi umshukuru, kwani amekujali sana.
- Ndio, Levi ni msichana mzuri na katika wasichana wachache wa aina hii, nami namshukuru sana.
- Kama vile unampenda, kwani hukuniambia kuwa umeoa?
- Ndio, mimi nimeoa, ni msichana mzuri sana, lakini pamoja na uzuri wake wa kupindukia naipenda roho yake zaidi kuliko ninavyokipenda kiwiliwili chake.
- Inaelekea wewe una mapenzi ya KiPlato (yaani mapenzi ya taamuli)!
- Ha ha ha, au ni mtu mgumu au mgonjwa kama wanavyonisema wanaonifahamu.
- Katika jamii yetu ya kimada, kiwiliwili hutangulizwa kuliko roho, katika ibada na katika starehe vile vile, hii ni kwa wengi wetu na huenda ikawa kwa Wayahudi ni zaidi.
- Kwa vipi?
- Muono wa Kikristo huangalia mambo kwa njia ya kiroho zaidi, lakini jamii yetu ya kimada hujali zaidi furaha za kiwiliwili juu ya hesabu ya furaha za kiroho, historia ya Uyahudi inathibitisha kuwa wao wana muono wa kimada katika kila kitu; Kuhusu mungu, siku ya mwisho, tabia na maadili ya watu, kila kitu kinaweza kuuzwa na kununuliwa, na sikusudii kuuza na kununua mali tu.
- Je sijakuambia kuwa unaukosoa sana Uyahudi?.
- Unaweza kujadiliana na Levi kuhusu hilo; yeye ni msichana mzuri wa Kiyahudi

www.path-2-happiness.com

na yeye hawezi kuukosoa Uyahudi, na unaweza kuiangalia historia na hali halisi ilivyo.

- Umenipa hoja kama ilivyo ada yako, je tumefika kwani nimechoka sana?
- Dakika chache tu tutafika.

Simu ya Joji iliita alikuwa ni Levi kwa sauti yake nzuri.

- Hallo Joji.
- Hallo Levi.
- Safari yenu imekuaje?
- Nzuri sana, kwa nini isiwe hivyo nami nipo katika usuhuba mzuri wa Dr. Habib!
- Natarajia kuwa uchaguzi wangu ulikuwa mzuri.
- Nzuri kabisa, asante sana.
- Nilitaka kutumaini hali yako kabla jua halijazama na kuingia Jumamosi.
- Nashukuru hali yangu ni nzuri, asante kwa mawasiliano, na nakushukuru kwa mipango yako mizuri, kesho tutaonana saa ngapi?
- Muda wowote utakaotaka, natamani sana tuonane.
- Nami hali kadhalika, ahadi yetu kesho saa tatu, nimechoka kidogo na ninataka kupumzika zaidi.

Joji alihisi kubabaika na akamuangalia Habib akamuona ametabasamu.

- Pole, Mungu akuhifadhi, je nikuitie daktari?
- Asante Levi nakushukuru sana, utanikuta katika afya njema na mchangamfu nikiwa tayari saa tatu.
- Kwa heri.
- Asante, kwa heri.
- ….Mazungumzo mazuri kabisa yenye hisia za ndani!!
- Unakusudia nini ?
- Hamna kitu, Levi ni msichana mzuri sana kama usemavyo.
- Unakusudia nini?
- Nilikuwa nakutania tu, inaelekea Levi amevutiwa nawe sana, kama wewe ulivyovutiwa nawe, na kila mmoja katika ninyi anajitahidi kumpendezesha mwingine kwa roho yake na kwa fikra zake na maadili yake …kisha akatabasamu na kusema:Na kila mmoja amevutiwa na kiwiliwili cha mwenzake vile vile, hivyo chunga mipaka isije ikawa mapenzi ya roho yakahamia katika mapenzi ya kiwiliwili, au kuthubutu kufanya jambo msilolitaka na kuondokana na kujivua na misingi yenu ya kimaadili ambayo Levi amenihadithia, kwa ujumla tumefika

hotelini.

- Asante kwa nasaha zako za kweli lakini ambazo ni ngumu, karibu tafadhali tule chakula pamoja, sote hatujala hadi sasa.
- Wewe umechoka, nami hali kadhalika, nataraji utanisamehe kwa hili.
- Asante, nimefaidika nawe sana, hii hapa ni kadi yangu, kuna mawasiliano yangu, natumaini mawasiliano baina yetu yataendelea…..Ha ha ha, kesho nitakuwa na Levi siku nzima na si vibaya ukawa mlinzi wetu.
- Najua kujali kwako tamaduni, fikra, na maadili, lakini nakutahadharisha kama nilivyomtahadharisha Levi kuchanganya mambo wakati mwingine, hali kadhalika sisi ni wanadamu na tuna udhaifu wetu wa kibinadamu, asante sana natamani kuonana kabla ya kusafiri kwako… hii ni kadi yangu..tafadhali nijulishe kila mara umefikia wapi katika njia yako ya furaha.

Joji alipanda chumbani akiwa amechoka sana –alikoga kwanza –kisha kama ilivyo ada yake alifungua Televisheni na kuangalia taarifa ya habari ambayo haikuwa na habari mpya, kisha akafungua kompyuta yake ili afuatilie barua zake pepe, alipata barua kutoka kwa Adam ikisema;

"Baada ya maamkizi:

Nimeangalia nukuu za torati zilizochafuliwa ulizonitumia na nikaona hazivumiliki wala haziaminiki, asante kwa kunitumia na tutazungumzia baada ya kurejea kwako, nataraji utaendelea kunitumia barua kama hizi; Mimi nimefaidika nazo sana."

Kisha aliona barua kutoka kwa Tom inayosema:

"Baada ya maamkizi:

Ama nukuu mbali mbali za torati; nilikuambia hapo kabla kuwa dini zote hazifai hazina manufaa yoyote, na ulikaribia kubadilisha rai yangu kabla ya kuja barua hii, nadhani umeanza kukinaishwa na maneno yangu, na usisahau kuwa Wakristo wanaamini Agano la Kale ambayo ndio torati unayoikosoa, ahadi yetu ni Jumanne saa nane mchana ili tujadiliane hilo, kama una mambo mengine nitumie."

Joji alitaka kumtumia uzoefu alioupata leo hii, lakini hakuweza; uchovu ulimzidi sana na akaamua kuwatumia wote pamoja barua fupiBaada ya salamu aliandika:

- "Nimesoma majibu yako na nitajaribu kuwatumia habari moja baada ya nyingine, leo nilishughulishwa sana kama jana, na ilikuwa ni kuhusu itikadi za dini mbali mbali, na migongano ya dini mbalimbali na mateso ya dini moja kwenda kwa wafuasi wa dini zingine. Kadhalika na tofauti kati ya makundi mbali mbali ya

www.path-2-happiness.com

Kikristo na mengineyo, na kwa sababu ninajihisi uchovu sana, nitajaribu kesho kukutumia nilichofikia.”

Alifunga kompyuta yake na kujitupa kitandani, hata hivyo alishangazwa kuwa pamoja na uchovu wote alionao lakini Levi na tabasamu lake angavu pamoja na macho yake ya kibuluu havikumuacha akilini mwake. Alikumbuka maneno ya Habib kuwa wakati mwingine mambo huchanganyika lakini pamoja na hofu yake alijiamini na kumuamini Levi vile vile.

MATAMANIO NA MISIMAMO

www.path-2-happiness.com

8

MATAMANIO NA MISIMAMO

MATAMANIO NA MISIMAMO

(1)

Joji aliamka saa mbili unusu asubuhi, mwili wake ulikuwa ni mzito na uchovu, usiku ule homa ilipanda na hakuweza kulala na ikabidi aombe kishusha joto hapo hotelini. Alijivuta na kusimama, kisha akaoga na kujisikia aina fulani ya uchangamfu. Alishuka chini kwenye mgahawa hapo hotelini na kupata kifungua kinywa kisha alipata na kishusha joto kwa mara nyingine na hapo akahisi hali yake kuwa nzuri zaidi na uchangamfu kuongezeka.

Alipanda chumbani kwake mara nyingine ilipotimu saa tatu na dakika kumi hivi, alipofika tu simu ikawa inaita, alikuwa ni Levi kwa sauti yake nzuri.

- Uko wapi? nimekuhofia, nimekupigia mara nyingi lakini hupokei…
- Samahani, niliteremka kupata kifungua kinywa na nimesahau simu yangu chumbani.
- Sio tabia yako kuchelewa katika ahadi.
- Sikuweza kulala vizuri jana usiku, huenda nimepatwa na maradhi.
- Mungu akuponye, je ungependa nikupeleke kwa daktari?
- Hapana, asante, na samahani kwa kuchelewa. Najiona afadhali kwa sasa.

Joji aliteremka mapokezi na kumuona levi akiwa amevaa mavazi mazuri yenye heshima, lakini haufichi uzuri wake – akapeana nae mkono na kumkaribisha…Levi akamwambia kwa shauku:

- Nasisitiza ukamwone daktari, haifai kunyamazia hali hii.
- Asante Levi, hali yangu ni nzuri hivi sasa na kama tukienda kutembelea sehemu takatifu nitashukuru kwa hilo.
- Kama utakavyo, la msingi ni kuwa katika hali ya furaha na starehe… leo tutatembelea sehemu mbili au tatu hivi, unaonaje?
- Napendekeza tuanze na kilicho muhimu zaidi, hata tukiweza kumaliza ziara za sehemu mbili itakuwa inatosha. Kilicho muhimu zaidi ni kukaa na wewe na kuzungumza na sio ziara pekee.
- Hata mimi kilicho muhimu ni hilo vile vile, tutaanza mwanzo katika ukuta wa kilio ‘Wailing wall’ na Mlima Yuria, kisha baada ya hapo tutatembelea kaburi la mfalme Daud katika Mlima Zayoni, na tukipata wasaa zaidi tutatembelea makaburi ya zamani ya Mlima Zaituni.

www.path-2-happiness.com

-
- Sawa kabisa, nataraji ziara yetu iishe kabla sijaanza kujihisi vibaya na uchovu mwingi.
- Vipi ilikuaje pamoja na Habib?
- Uchaguzi mzuri kabisa kutoka kwako, inaelekea kuwa unanifahamu vizuri.

Macho yakakodoka na kung'ara na meno kuonekana na kutabasamu…

- Mh mh… kiasi fulani, Habib amefunguka katika mambo mengi na ni msomi na anajua anachokifanya.
- Umesema kweli, nimefaidika nae sana.
- Naye anakusema hivyo hivyo.

Joji kwa mshangao:

- Vipi na lini?
- Alinipigia jana mara tu alipokuwacha hotelini, na akaniambia kuwa amejifunza mengi kutoka kwako…amekusifia sana na sikuwahi kumsikia kama alivyokusifu kwa mtu mwingine.
- Huu ni katika ukarimu wake, ila muda wote tulikuwa kwenye mjadala wa nipe nikupe.
- Ikiwa mfano wa mazungumzo yako pamoja nami, ni mazungumzo matamu yaliyojaa!

Joji alijihisi akiwa na furaha akiwa anasikiliza maneno yake matamu kwa sauti yake nyororo…..na mwili wake wenye fitna na kwa roho yake iliyokuwa nzuri.

- Ha ha ha, mnatofautiana kidogo, wewe ni mwema sana, mzuri, nae hayupo hivyo, hata hivyo nakushukuru kwa kunichagulia. Vile vile nakushukuru kwa kujali kwako na kutaabika nami, cha muhimu ni kuwa malengo ya safari yetu ya msingi yakamilike, nayo ni kuingia mkataba na kusaini na kutambua njia inayopelekea katika furaha.
- Nakushukuru sana, bado unakumbuka mkataba? Mimi nilishasahau kabisa, kwa mnasaba huo kikao chako na Benjamin kimemchanganya.
- Kwa vipi?
- Sijui, lakini baada tu ya kuondoka aliniita na kuniambia: "Huyu ni katika watu wa ajabu ambao nimekutana nao katika maisha yangu." Nikamuuliza kwa nini? Akaniambia: "Ima huyu ni mwendawazimu au ni mtawa".
- Ha ha ha, sina uchaguzi mwingine wa tatu! Sitaki kuwa mwenda wazimu, la

kusikitisha siwezi kuwa mtawa na mimi ninampa rushwa.

- Sijui kwa nini ameathirika na nilichomwambia, kila mara akikariri kuniambia kuwa sisi tunakosea tunadhani kuwa dunia ni mali tu, na hili lilikuwa jambo la kwanza katika maisha yangu kusikia haya kutoka kwa Benjamin.
- Kwa kweli….pamoja na kutokuwa na raha nae, maneno yake hata mimi yameniathiri vile vile, Je, ni kweli starehe ya mwili ni adhabu ya roho? Je, hakuna njia ambayo nitakutana na raha, matamanio na kuondoka kwa maumivu?
- Ni kiasi gani natamani kuipata njia hii.
- Hivyo wewe ni kama alivyonieleza Habib unatafuta njia ya furaha?
- Neno zuri sana (ulilolisema), lakini ni ipi njia ya kuelekea kwenye furaha kwa muono wako?
- Ni ile njia ambayo ulikuwa ukiitafuta kabla ya muda kidogo na unatamani kuipata, nami ndio hiyo hiyo ninayoitafuta tokea muda mrefu.
- Nami nina muda mrefu ninaitafuta vilevile … kisha nikatabasamu na kumuangalia machoni mwake, na akasema, ukaribu ulioje wa roho zetu?!
- Habib aliniambia hivyo, kwa nini usiwe Mkatoliki?
- Fikra niliyokuwa nayo ni kuukimbia Uyahudi na mazonge yake na upotofu wake, lakini lengo sio kutoka kwenye mafundisho ya Uyahudi na kuingia katika mafundisho mengine na kutoka kwenye upotofu huu kwenda kwenye upotofu mwingine, vinginevyo ni bora kubakia kwanye Uyahudi, dini ya zamani na yenye utukufu zaidi.
- Kuwa mkweli kama ulivyonizoesha, je hii ndio sababu pekee? Au kuna sababu nyinginezo?!
- Ukweli….. Kubadilisha dini sio jambo rahisi unadhani ni miamala gani anayofanya aliyebadilisha dini pamoja na wale wanaomzunguka, mfano mimi na Banjamin? Je, unadhani nitabaki na kazi yangu (baada ya kubadilishwa dini) walau siku moja?
- Hivyo wewe unamuogopa yeye?
- Nilikuambia bado sijakinaika, kwa ukweli nahofia kubadilisha dini yangu… uhuru una makato yake ya gharama….gharama za juu!
- Lakini hatuna budi kulipa gharama hizo; Pili tupate uhuru wetu, hakuna kitu mfano wa uhuru wetu.
- Bado naendelea kutafuta maamuzi sahihi, au njia ya furaha, na nitakapokinaishwa na hilo huenda nikachukuwa maamuzi kwa ujasiri, na huenda nikawa muongo

www.path-2-happiness.com

kwa hilo, sijui itakuwaje…..sijui!
- Je, unamuogopa Benjamin?
- Bila shaka! Je unadhani maamuzi sahihi ya kijasiri, au kwa lugha nyingine kwa mazungumzo yako njia ya furaha ndiyo ambayo itakufikisha kwenye Ukristo?
- Una uwezo usio wa kawaida kugeuza meza katika mazungumzo yako, sijui kwa nini?
- Je, sijakuambia kuwa roho zetu zinaruka pamoja, leo huenda zikaungana pamoja.
- Ehe umeshaanza kuwa mwanafalsafa! ewe mwanamke mzuri vipi roho zikutane?
- Ha ha ha, sijui, ila ninavyofahamu ni kuwa kama inavyoungana miili basi na roho zinaungana vilevile, na ya kuwa roho yangu inaruka na yako.
- Ni bora roho ziruke kwa furaha kuliko kuruka kwa shaka.
- Swadakta, hata hivyo tuachane na hili….zimebaki dakika kadhaa kufika katika ukuta wa kilio (Wailing Wall), au kama wanavyouita Waislamu Ukuta wa AlBuraq nayo ni athari ya mwisho iliyobakia ya hekalu ya Mfalme Solomon kwa muono wa viongozi wa dini wa kiyahudi (Rabbi). Wayahudi walikatazwa kuingia katika msikiti wa Qudsi tokea hekalu lilipoharibika; hivyo basi ukuta ni sehemu ya karibu zaidi katika sehemu ya hekalu ambayo Wayahudi wanaweza kuswali ndani yake kulingana na Sheria za Kiyahudi za kisasa. Jina la ukuta unaolia limeitwa kwa kunasibishwa na ibada za kuomboleza ambazo zinafanywa hapo
- Tokea lini (mambo haya)?.
- Kabla ya karne ya kumi na sita Mayahudi walikuwa wakiswali na kutekeleza na ibada zao za misiba katika hekalu la Solomon katika sehemu tofauti panapozunguka sehemu tukufu ya Yerusalemu, kisha baada ya hapo wakawa wanakusanyika kila mwaka mbele ya jiwe karibu na ukuta fulani katika eneo tukufu Yerusalemu ndilo baadae likaitwa ukuta wa kilio (Wailing Wall) au kama wanavyouita Waislamu ukuta wa Buraq.
- Ni nini ukuta wa Buraq?
- Ni mtukufu vile vile kwa Waislamu, wanasema kuwa Mtume wao alipandishwa mbinguni kutokea pale, safari ya Mtume wao huyo ilianzia Makkah kwa njia ya nyumbu aitwae Buraq ambae safari hiyo iliishia hapo na kutoka hapo kwenda juu.
- Je, mnawaachia Waabudie hapo?
- Tumewaachia sehemu zote tukufu za Yerusalem na bado wanashindana nasi katika ukuta wetu! Kisha Waislamu hawana toba ya kuabudu athari wala hawapendi masanamu na hawaabudu vitu vyenye kuabudiwa.

- Habib alikuwa ananikejeli na kuniambia kuwa sisi Protestant ni kama vile Waislamu hatupendi sanamu na picha.
- Hili ndilo lililobakia katika hekalu zetu za kuabudia zilizo vunjwa, na tutatoka kuieleza dunia na kuonesha athari zenye kuthibitisha hilo.
- Miaka yote hii hamjapata athari yoyote ile na bado mnataraji kupata?
- Hahaha, hata kama hatukupata basi tutatengeneza!
- Kama ni hivyo inaonesha hujakinaishwa bado?
- Sijaridhishwa au bado, hiyo ni hali ya shaka, baadhi za tafiti zinaonesha kuwa, kwa mara ya kwanza watu waliswali kwenye ukuta ilikuwa ni wakati wa dola ya Ottoman, na sio kama nilivyokuambia kuwa ilikuwa kabla ya karne ya kumi na sita. Ama Waislamu wanasema kuwa huu ni uongo ulio wazi, kilicho muhimu ni kuwa hii ni sehemu tukufu kwetu, kisha alimgeukia Joji na akasema:Ni vigumu kuifurahisha roho yako na kuizoesha katika hilo. Je, ungependa tuishi bila ya kufanya ibada?
- Leo unaonekana tofauti kabisa na jana.
- Leo ni siku ya ibada na sisi tunaelekea katika ukuta wa kilio, na yatupasa tuteremke sasa hivi na tukamilishe safari yetu kwa kutembea.
- Natamani tusitembee sana kwenye jua hili, athari za uchovu zimeanza kujitokeza kwangu.
- Nataraji haitokutokea kwani wewe sio Myahudi.
- Kwa vipi?
- Vaa kofia hii.
- Hamna sio neno, hahaha, usinichore ninapovaa kwani Katarina atakasirika.
- Unaelekea unampenda sana Katarina!
- Ndio, kwa sababu ni mwanamke mwenye dini, msomi na moyo wake mweupe kama wako.
- Natamani kumpata mtu kama alivyo anayejali dini, usomi na fikra… tutapinda hapo kulia, kisha kulia tena na tutakutana na ukuta na tutawaona watu wakiwa wanalia.
- Nimevaa kofia ya Kiyahudi lakini sijui kuigiza kulia kama wao.
- Hilo sio muhimu, wengi mfano wake hawawezi kuigiza, utawaona wengine wengi wakilia au wanajua kuigiza kulia….wewe unaweza kuendelea; wanawake hawaruhusiwi kuingia.
- Kwa vipi? siwezi kuingia kama hutoingia.

www.path-2-happiness.com

- Ingia, mimi na kusubiri, unataka niingie kisha nifukuzwe kama mbwa, tafadhali ingia peke yako.

Joji alitembea safari iliyobakia peke yake, na akaanza kuhisi uchovu wa hali ya juu, hadi alipofika kwenye ukuta…. Idadi ya Mayahudi wengi waliokuwa wakilia ilikuwa ni kubwa na kuna wengine wengi ambao hawajui kulia vizuri (huenda hawakujifunza jinsi ya kulia vizuri)…. Alisimama pembeni yao akiwaangalia, hata hivyo alijihisi akiwa na dhiki, na akataka kuondoka haraka; na haswa zaidi kwa sababu uchovu uliongezeka, na joto lake la mwili likaongezeka, aliangalia pambizoni mote na hakumuona mwanamke yeyote, akajihisi vibaya na akachukizwa kukaa zaidi aliamua kurudi, lakini hatua zake zilikuwa nzito na athari za uchovu zilishaanza, alijivuta kwa kujibeba hadi alipofika kwa Levi, ambae alimkuta amekaa akimsubiri njiani.

- Umerudi mara moja.
- Nimechoka sana, Je tunaweza kurudi kwa gari mara moja?
- Vizuri, kama utakavyo.
- Au unaweza kuleta gari hapa?
- Inaonesha umechoka sana… samahani haiwezekani kuja na gari, unaweza kuniegemea, haya twende.

Uchovu ulikuwa wazi sana kwa Joji, Levi aliweka mkono wa Joji shingoni mwake ili amuegemee, alijitahidi kuinua mkono wake wakati anatembea lakini uchovu ulimzidi uzito, aliinamisha kichwa chake mabegani kwa Levi, upepo unapovuma ulipeperusha nywele zake usoni mwa Joji, na harufu ya mwili wake puani mwake, nywele zake mkononi mwake, na wakati mwingine mashavu yake kukutana na ya kwake.

- Samahani sana, nimekuchosha mara iliyopita na sasa hivi tena…inaelekea nadeka.
- Usijali…cha muhimu ni kufika kwenye gari upesi….kuna hospitali ipo karibu hapa tutaelekea, baada ya hapo utakamilisha kudeka kwako na kupata tumaini.

(2)

Levi alimpeleka mbio Joji katika kitengo majeruhi hapo hospitalini, Joji alipigwa sindano ya kutuliza maumivu ambayo ilimpelekea kulala mara moja…Levi alikwenda kwa daktari kuulizia hali yake.

- Ana nini?
- Usiogope, nimempa dawa ya usingizi apumzike kidogo, baada ya saa moja hivi tutajua matokeo ya vipimo vyake, kisha akatabasamu na akasema: unaelekea kuogopa sana, Je, ni mume wako au mpenzi wako?
- Ni rafiki yangu tu.
- Kwa hali yoyote baada ya saa moja matokeo yatakuwa tayari na ninaamini ataamka kabla ya muda huo.

Levi alikaa pembeni ya Joji, na akaanza kumuangalia pale alipolala akawa anamfuta kipaji chake na kupapasa nywele zake, alikuwa akihisi hisia kali kwake… baada ya muda Joji alifungua macho yake, na mkono wa Levi ukiwa bado unapapasa nywele zake.

- Nipo wapi?
- Ashukuriwe Mungu kwa kuamka, tupo hospitali, nawe upo katika hali njema.
- Yuko wapi daktari?
- Atakuja baada ya muda, akiwa pamoja na matokeo ya vipimo, pumzika kidogo usijichoshe… Joji.

Joji alishika mkono wa Levi ambao ulikuwa una mpapasa usoni na kwenye nywele, kisha akampapasa kwa upole….

- Nakushukuru sana Levi, sikutarajia kukuchosha hivi….
- Usiseme hivyo, nipo kwa ajili yako.

Dakika kadhaa zilipita hawakuzungumza chochote mbali ya lugha ya ishara na ya kugusana ambayo ilikuwa ni kubwa kuliko lugha ya mantiki….hadi alipofika daktari kumuangalia Joji….

- Umeamka Joji? mpenzi wako…samahani rafiki yako alikuhofia sana.
- Ehe daktari kuna habari gani?.
- Matokeo ya awali yanaonesha umeshambuliwa na virusi vikali, ama vipimo vingine vitatoka kesho.
- Lini ninaweza kuondoka?
- Baada ya saa moja au kesho ukipenda, muda utakavyojihisi vizuri, na utakapotoka nesi atakupatia dawa zako, haya nawaaga.

www.path-2-happiness.com

- Samahani Joji kaa hapa hadi kesho; hii ni dhamana zaidi ya afya yako.

Joji aliuminya mkono wa Levi kwa nguvu, na kumuangalia kwa amani….

- Asante sana Levi, nataraji kwenda hotelini, na naomba samahani kwa kutokamilisha msafara wetu.

Levi aliuondosha mkono wake na akaweka kifuani kwa Joji, kisha akaunyanyua na kuubusu..

- Nakuomba msamaha

Levi alibabaika sana na uso wake kuonekana na haya pamoja na hisia ya furaha na uchangamfu aliokuwa nao Levi alitabasamu…..na akamuomba asifanye haraka; kwani leo ni Jumamosi na bado ni mchana na jua bado halijazama…

- Unaomba msamaha kuhusu nini? Usiombe msamaha, muhimu uwe katika siha njema.

Levi alimaliza taratibu za kumtoa Joji hospitalini na akapokea majibu ya vipimo vilivyokwisha kuwa tayari na dawa na akaweka ahadi ya kesho saa 4 asubuhi.

- Je, ni lazima aje mwenyewe au naweza kuja kumchukulia matokeo ya vipimo vyake?
- Machovu yakimrudia njooni pamoja, vinginevyo inatosha kuja peke yako kesho kuchukua majibu yaliyobakia.
- Kama ni hivyo nitakuja kuchukua majibu kesho, Je, ataondoka na gari la wagonjwa au gari langu?
- Kwa gari lako, utaondoka akiwa anatembea kama utakavyoona… kisha akamgeukia Joji na kumwambia: tafadhali unaweza kwenda.
- Basi subiri nitasogeza gari mlangoni.

Levi alirudi, akamshika Joji mkono na kumpeleka hadi kwenye gari, alimfungulia mlango na akabaki pembeni yake ili amsaidie…akamuangalia kwenye macho yake ya kibluu na yote yakiwa katika upole

- Asante Levi, sijui nikushukuru vipi…..

Pole pole – kwa hisia asiyoikusudia – alimgeukia, na kukaribia mwili wake, akamkumbatia na kumbusu kwa muda mrefu; alibabaika sana pamoja na tabasamu lililojaa alijaribu kulificha..

- Samahani leo ni siku ya ibada tu, huna haja ya kunishukuru; mimi nafanya kinachoniambia dhamira yangu.

- Samahani sana labda nimekukera, sikujua jinsi ya kuonesha shukrani zangu kwako ndio maana nikakubusu.
- Huu sio wakati wake …unaweza kupumzika kwa sasa… kisha akatabasamu tabasamu la mchawi: Kakhi alikuwa akinibusu sana (kumbatia) na hakuwa akiomba samahani: ni kiasi nilikuwa nikimchukia.
- Samahani; sikukusudia kukuchukiza, sijui kwa nini nimefanya hivyo, huenda ulikuwa ni wakati wa dhoofu wangu, kwa sababu ya maradhi, au huenda kama alivyosema Habib: Kuvutiwa kwa roho nzuri kumechanganyika na kuvutiwa na mwili mzuri.
- Au huenda ikawa ni kuchanganyika kwa roho ambayo tulikuwa tunaizungumzia, hata hivyo achana na maudhui haya, unajisikiaje sasa?
- Najihisi kuwa na haya kwako na kwa nafsi yangu, matamanio yangu yameonesha udhaifu wangu, niamini sikuwa na nia ya kukukera au kukuaibisha bali nilitaka kuonesha na kutoa yaliyo moyoni mwangu.
- Naomba funga maudhui haya, nimekwambia kuwa Kakhi alinikumbatia na si hivyo na kunibaka vile vile zaidi ya mara moja na wala hakuomba msamaha, bali baya zaidi ya hilo nilikuwa nikijihisi wakati mwingine naona raha pamoja na Kakhi mchafu fikiria nikiona raha pamoja na kulazimishwa kuachia misimamo yangu. Huenda ikawa Benjamin alikuwa mkweli ya kuwa sisi tunafurahisha viwiliwili vyetu huku tukidhulumu na zikiumia roho zetu.
- Huenda hatukupata njia ambazo roho zetu zitanyooka pamoja na miili yetu, na hivyo basi roho zetu zikafurahisha miili yetu na miili yetu ikafurahisha roho zetu.
- Huenda ikawa muradi wake ‘njia ya kuelekea kwenye furaha, usisahau kunijulisha ukiifikia, vinginevyo sitokusamahe.
- Nitakapomaliza safari yangu, inaelekea kila ambaye nitakutana nae anasubiria matokeo, nina kariri kuomba radhi kwako na shukran nyingi kwako Levi.
- Tutafika hotelini baada ya dakika chache, na ninakutaka upumzike chumbani kwako, na nitawaambia wakuletee chakula cha usiku –chumbani; kwani chakula cha mchana umeshachelewa, na ikifika asubuhi watakuletea kifungua kinywa…. na mimi nitakwenda hospitali kuchukua matokeo ya vipimo, kisha nitakuletea. Lini unasafiri?
- Nimeweka lijamu ulimi wangu, asante sana, safari yangu ni saa kumi na mbili jioni.

Walifika hotelini, Levi akapanda nae chumbani na kumlaza kitandani….

www.path-2-happiness.com

- Napenda kukaa pamoja nawe, lakini naogopa kukuchosha kwa mazungumzo yetu na hivyo nitaondoka.
- Huwezi kujua kiasi cha furaha yangu kwa mazungumzo nawe, lakini nakuruhusu uondoke ili upumzike, kwani nimekuchosha sana.
- Jua limezama, na ninataka kufanya kitu lakini sijui, unaweza kufasiri unavyotaka.
- Sijafahamu!

Levi alimsogelea Joji na kumkumbatia na akambusu kwa muda mrefu…. Joji alijihisi kama ule mmea uliopo jangwani inaponyeshwa na maji, pamoja na kuchoka kama angeendelea kukumbatiwa angeendelea ukaribu zaidi….

- Jumamosi yetu imekwisha, nitakuachia tafsiri ya nilichokifanya; mimi sijui kwa nini nimefanya hivyo, kwa heri.

Tendo la Levi lilikuwa la ghafla sana kwa Joji, hakufahamu tafsiri ya tendo lake, kama alivyokuwa hajafahamu tafsiri ya tendo lake yeye mwenyewe alipomkumbatia je, ni kweli matendo yetu yanafanyika bila ya khiari! Au yakuwa udhaifu wa maradhi ndio sababu? Au ndio mchanganyiko wa kiroho ambao unaweza kufasiri hilo? Au ni matamanio ya kijinsi na makosa? Au ni mchanganyiko baina ya mchanganyiko wa kuvutiwa kwa roho na mwili kama alivyosema Habib?...Sababu yoyote ile iwayo lakini inabainisha udhaifu wa mwanadamu… au huenda ikabainisha haja zetu ya Yesu kusafisha madhambi yetu kisha baada ya hapo hisia zake zikaondoka akimfikiria Levi na akakumbuka alipokuwa nae na khofu yake, baina ya hali yake hiyo simu yake ikalia, upande wa pili alikuwa ni Katarina…

- Mpenzi, vipi hali yako sasa hivi?
- Hali nzuri, nimetoka hospitali sasa hivi na naendelea vizuri, nani aliyekuambia kuwa mimi ni mgonjwa?
- Maradhi yako, maradhi gani? Ninachokifahamu ni kile alichoniambia Tom jana katika hafla kanisani kuwa ulimwambia umechoka sana.
- Tom tena?
- Mpenzi wangu bado unanishuku
- Abadan, hali yangu ni njema na kesho narejea, ndege itaondoka saa kumi na mbili jioni.
- Tutakusubiri na gari la wagonjwa.
- Hakuna haja ya hilo, mimi ni mzima.
- Usijali tunataka kutumaini hali yako… sitaki kurefusha jaribu kupumzika sasa,

kwa heri kwa jina la Mungu

- Kwa heri mpenzi wangu kwa jina la Mungu

Joji alimaliza mazungumzo akiwa anafikiria majaliwa ambayo yamemfanya Katarina kuwasiliana nae baada ya kumkumbatia Levi, ili amkumbushe Tom alipomkumbatia na ghadhabu yake kwa hilo, na akajiuliza: Je sisi ni unyoya katika mvumo wa upepo au ya kuwa majaliwa yanampelekea katika jambo asilolifahamu? Je raha ya kiwiliwili ina maana ya huzuni na tabu kwa roho na misingi yake! Jehaiwezekani kukusanya pamoja! Inaelekea kuwa siku za usoni pana matukio mengi ambayo hatuwezi kuyatabiri.

Katika hali hiyo alifika mfanyakazi na chakula cha usiku chumbani kwake, na akaingia mhudumu akiwa anatabasamu na akamsalimia Joji…

- Inaelekea yule mwanamke anakupenda na kukujali sana, alihakikisha mwenyewe kuwa chakula ni kizuri, na akatupa maelekezo tukukumbushe kuhusu dawa zako, na hakuondoka hadi alipohakikisha kuwa tumepanda na chakula chako.
- Vizuri, asante sana.

Joji alikula chakula upesi upesi… kisha akajilaza kitandani akifikiri siku hii ya leo, alitamani kuangalia barua zake hata hivyo aliona ni bora kucheleweshe hadi kesho.

(3)

Joji hakuamka ila saa tatu asubuhi, pale pindi mtumishi alipogonga mlango wa chumba chake akimletea kifungua kinywa.

- Haya ni maelekezo ya mpenzi wako, kwani aliwasiliana nasi kabla ya nusu saa ahakikishe kuwa tumekutayarishia kifungua kinywa, kadhalika alitupigia jana saa nane usiku; ili ahakikishe kuwa tumewasiliana nawe ili uchukue dawa zako… wewe una bahati sana kumpata mwanamke mzuri kama yeye anayekupenda bali ni ashiki wako.

Asante Joji, hakumjibu akiwa anarejea maneno: Mwanamke mzuri, mwenye kupenda, kisha alipata istiftahi yake, na akawasha Kompyuta yake ili aangalie barua pepe na kujibu yale yanayopaswa kujibiwa kisha akamuandikia barua Tom na Adam kuwajulisha maradhi yake, na yakuwa atarudi leo hii London, na baada ya hapo akawauliza: Je, wanajua chochote kuhusu furaha za roho au ya kuwa roho haina isipokuwa mateso na ya kuwa starehe zote ni za kiwiliwili tu? Je, unaweza kuzifurahisha, au inapasa ili kuzifurahisha roho zetu basi

www.path-2-happiness.com

viwiliwili na akili zetu ziteseke?

Levi alikwenda hospitalini, ili kupokea matokeo ya vipimo, daktari akamjulisha kuwa virusi vilivyompata Joji ni virusi ilivyokuwa nadra sana na kitaalamu kwa mara ya kwanza huingia kichwani, kwa maana hiyo wapo katika hali mpya. Daktari alipendekeza arudi tena hospitali baada ya wiki moja hadi siku kumi, kwani haiwezekani kutabiri kitakachotokea katika hali ya Joji, kwani virusi hivyo vinaweza kuibuka upya na kupata nguvu mpya na hivyo basi wakati wowote inaweza kutokea jambo ambalo itampasa kuwa karibu na daktari. Levi alilia sana akihofia hali ya Joji, na hakujua cha kufanya, akawasiliana na Habib ambaye alimfuata Levi hospitalini, alikuwa akijiuliza au akimuuliza Habib; kwa nini anajali sana hali ya Joji? Je anajali kwa sababu ya matamanio ya kiwiliwili kwa mtu aliyekataa kufanya nae mapenzi na hivyo kutaka kumhurumia kwa sababu ndizo huruma za kike? Au ni mshikamano wa kiroho kwa fikra yake, tabia yake na elimu yake? Au ni kwa sababu ya mchanganyiko wa kufanana katika utafiti wa njia itakayopelekea kwenye furaha? Alikuwa akimuuliza maswali hayo Habib naye….nae akijaribu kumuuliza, kisha wakaondoka pamoja kuelekea kwa Joji hotelini.

Simu ya chumbani kwa Joji ilipigwa akiwa anaendeea kusoma barua pepe zilizomfikia, akapokea huku upande wa pili Levi akisema:

- Je utaturuhusu tuje chumbani kwako?
- Karibu sana.

Aliingia Levi akiwa na tabasamu lililoficha huzuni ndani yake, Joji alimkaribisha na akampa mkono.

- Nipo na mgeni, je utamruhusu?
- Usiweke mipaka baina yetu, mgeni wako ni mgeni wangu, karibu.

Habib aliingia na Joji alimkaribisha kwa furaha, alifurahi kufika kwake.

- Inaelekea ulipata ugonjwa kwa sababu yangu; maradhi yalikuanza ulipokuwa pamoja nami, na Levi yupo mbali na hilo.
- Levi yupo mbali na kila aibu; Yeye ni tohara kuliko tohara yenyewe.
- Lugha ya mapenzi katika hadhira yangu.
- Ha ha ha, nimesahau kuwa wewe ni mlinzi wetu

kwa tabasamu la kichawi, akiwa anaona haya, akiwa ana muangalia Joji…

- Sijafahamu uliposema kuwa Habib ni mlinzi wetu, mlinzi katika nini?
- Usijali…. Joji anataka kutuharibia tu….kisha akamgeukia Joji: Na kumuuliza kuhusu afya yake sasa.
- Katika hali nzuri kama unavyoona, nipo katika hali nzuri, Jana nilichoka sana na Levi nikamsumbua na kuchoka pamoja nami.
- Hakunichosha kabisa, ila sikujua nifanye nini? Mara nyingi nababaika katika hali kama hizo katika mazingira magumu nataraji kuwa mimi ndie ambaye sijakuchosha, ilikuwa ni bora kufuta ile ziara yetu pindi uliponijulisha uchovu wako, huenda kwa kutokufahamu vizuri ndio sababu!
- Hukukosea kabisa, na kilichotokea kwangu ni jambo la ghafla.
- Daktari ameshauri kuwa ukae hospitali siku mbili au tatu, unaonaje?
- Ndege inaondoka saa kumi na mbili kwa maana natakiwa kuondoka hapa baada ya masaa mawili na nusu kutoka sasa na wewe unaniambia siku mbili au tatu!
- Joji nakuomba siku mbili au tatu tu ili tupate kutumai hali yako zaidi.
- Hali yangu ni nzuri, nini ripoti ya mwisho ya daktari?
- Mpe ripoti yake Levi, ripoti ni nzuri, na yeye anataka kupata tumaini tu.

Joji alichukuwa ripoti kutoka kwa Levi akiwa anamuangalia machoni, na akamuahidi kuwa ataiangalia nafsi yake na kwenda hospitalini mara tutakapofika London.

- Itapasa kwenda kwa daktari mara tu utakapofika London ili tutumai hali yako Joji.
- Katarina mke wangu ameshajua hali yangu na kuwa atanisubiri kwa gari la wagonjwa Uwanja wa ndege, nimeshawasiliana nae asifanye hivyo lakini amesisitiza hilo, ana inadi mfano ewe Levi.
- Vizuri alivyofanya hivyo Katarina, ili apate kutumai hali yako, mbele yetu tuna masaa mawili takriban, kwa hivyo inanipasa kula chakula cha mchana, kisha tayarisha mkoba wako wa safari.
- Chakula cha mchana baada ya saa moja hivi kwa pamoja tutakwenda kula hapo katika mgahawa wa hoteli, nawaalikeni wala msinirudishe, na wala sihitaji zaidi ya robo saa baada ya chakula cha mchana ili nikoge na kutayarisha mikoba yangu.
- Tumewafiki ili mradi iwe chumbani kwako na sio katika mgahawa hapo hotelini; ili tusikuchoshe.
- Oh oh ewe Levi…. ningependa kutembea kidogo, wala hainichoshi kula mgahawani.

Habib, akiwa anajaribu kuondosha upweke uliojificha baina yao….

- Ili tutumie muda uliobakia, lete habari za njia ya furaha?

www.path-2-happiness.com

- Hii ni mara ya pili nasafiri kwa ajili hiyo ewe Habiib katika kutafuta njia ya furaha, mbali ya vikao mbalimbali na majadiliano na mikutano mbalimbali, maudhui haya yamenikamata. Wakati wangu na juhudi yangu yote nimeipotezea hapo, na nataraji kupunguza juhudi kwa mafanikio.
- Levi: Mafanikio yako ni mafanikio yetu sote, tunasubiri matokeo ambayo yatafikia hapo.
- Habib: Safari yako ya kwanza ilikuwa wapi?
- Nitawaambieni katika mpangilio kama asemavyo Katarina: Nchi ya ajabu, kisha nchi ya vita na mauaji, kisha nchi za Makanisa.
- Habib Nchi ya maajabu tunaifahamu kuwa ni India, na nchi ya vita na mauaji ni hii uliopo sasa, nchi ya Makanisa ni ipi?
- Rome na Vatican, ndio safari ijayo inayonisubiri.
- Habiib: Ziara yako ya Yerusalem inaweza kuwa imekusaidia; kwa kuwa ni uzawa wa dini na rejea zake katika migogoro yake, na Vatican unaweza kusawiri maana ya ziara yako; kwani ni sehemu muhimu kwa Wakristo pamoja na tofauti za dini zao, ama India kwanini ulikwenda na ikawa safari yako ya mwanzo?
- Kwa sababu swali langu la mwanzo lilikuwa Je, dini za mbinguni ni bora kuliko dini za ardhini? Ndio maana nikaenda India, kisha swali lililofuata….
- Levi: Samahani kwa kukukata ulitarajiwa swali la kwanza liwe: Je, ni bora kuwa na dini au kupinga dini ni bora.
- Swadakta, lakini nilikuwa naona na bado ninaona kuwa kumkana Mungu na dini ni maradhi ya nafsi baada yake inafuatia Falsafa ya kusadikisha hata hivyo ndani ya nasfi zao wanaamini kuwepo kwa Mungu, na huwezi kupata maradhi yaliyokuwa makubwa zaidi na mabaya zaidi kuliko kumkana Mungu.

Habib alitabasamu akiwa anamuangalia Levi, kisha akasema:

- Swadakta, lakini ulipaswa kutafuta hili kwa njia ya kielimu zaidi.
- Nimetafuta ukweli, nimetafuta! Lakini unanitaka nisafari ili nione hilo?
- Habib; Ha ha ha, safiri ndani ya maisha ya mkana Mungu yoyote, na utahakikisha unachokisema!! Sijui wanawezaje kustahmili!!
- Levi: Ndio maana wengi wao ni wenye huzuni na wenye kujua mara kwa mara.
- Niache nikamilishe, suali la pili limekuja baada ya kujua kuwa dini za ardhini ni za uongo, yaani dini za mbinguni ni bora? Hivyo basi safari ya nchi takatifu ilikuwa ni kuuangalia Uyahudi kwa karibu kisha akamgeukia Levi na kusema; Na baada ya kufika hapa nimefurahishwa na usuhiba wako.

- Hivyo basi mazungumzo yetu juzi kuhusu Ukristo na madhehebu yake mbalimbali na vita iliopo baina ya madhehebu hayo tumeharakisha kabla ya safari yako ya tatu?
- Ndio, lakini ni haraka ya mahali pake, safari ya tatu itakuwa Vatican; ili kujua vilivyo dini ya Ukristo.
- Imebaki kujua dini ya Uislamu vilivyo.
- Ghadhabu ilikuwa wazi katika uso wa Levi, na akasema: Dini ya Wanyama, nenda Makka ili uifahamu, hawatokuruhusu kuingia kadiri utakavyofanya.
- Ha ha ha, punguza ghadhabu zako, ukweli ni likuwa natamani kukutana na Waislamu hapa Yerusalem (Qudsi), usisahau kuwa wakazi wengi hapa ni Waislamu, lakini sikuweza kwa sababu ya upungufu wa muda wa safari, kisha haya maradhi, kwa ujumla huenda nisihitaji safari ya kwenda nchi za Kiislamu.

Habib alimwangalia Levi machoni.

- Ama suala la wasiokuwa Waislamu kukatazwa kuingia Makkah ni sawa na Wayahudi kuwakataza Waislamu kuingia katika ukuta wa kulilia au ni kama wanavyozuiwa wanawake kuiingia. Au mfano wake kukatazwa kwa vijana kuswali katika msikiti wa Aqswa siku ya Ijumaa, au…..
- Joji, polepole sijakuambia kuwa wewe ni Muislamu uliyejificha katika Ukatoliki!
- Levi: Ha ha ha, huyo ndivyo alivyo siku zote, nasasa hivi nina mtu wa mfano wa dini yangu dhidi yako ewe daktari.
- Usitake msaada wa Joji dhidi yangu; yeye anaondoka leo hii, na sisi tutaendelea na mjadala wetu, hata hivyo kwa ajili ya uadilifu ni kufanya utafiti kama anavyofanya Joji kuhusu Uyahudi, Ukristo vivyo hivyo ufanye kuhusu Uislamu. Je, sikukutaka ewe Joji ufanye utafiti kuhusu ukanaji Mungu? Je ukanaji Mungu kwenu nyinyi ni bora kuliko Uislamu?
- Ha ha ha, huenda ikawa hivyo.
- Tumechelewa, Je, tukutangulie mgahawani au tuteremke pamoja?
- Yatupasa tumsaidie kushuka kwani yeye bado amechoka.
- Asante Levi, tangulieni nitakuja sasa hivi kwani nitaingia maliwatoni.

Habib na Levi walitangulia mgahawani, wakachagua meza nzuri, wakakaa wakimsubiri Joji, na wakati huo huo Habib akaanza kuzungumza…

- Nina wasiwasi kuwa umevutiwa sana nae kuliko inavyotakiwa.
- Kwa nini?
- Samahani kukuingilia lakini jinsi mnavyoangaliana inatia shaka na jinsi

www.path-2-happiness.com

mnavyoangaliana ni kama vile wapenzi wawili.

- Sijui kwanini tumefikia hapo! Pamoja na kwamba nilikwambia kuwa tokea mwanzo amekataa maingiliano yoyote ya kimapenzi, na aliniambia kuwa anampenda mke wake na analiona jambo hilo ni kama vile kufanya hiana.
- Nilikuambia kuwa usichanganye baina ya kuvutia kwa roho na tabia na kuvutiana matamanio yanayotokana na silika ya jinsia.
- Jana lilitokea jambo la ajabu sana, nilimbeba baada ya kuanguka, kisha akanibusu kwa mara ya kwanza, baada ya kumuweka kitandani chumbani kwake nami nikambusu.
- Busu kwa bahati mbaya ni jambo la kawaida kabisa katika jamii zenu wote, lakini kilichokuwa si cha kawaida ni kuachana na misimamo yenu.
- Sina tafsiri ya kilichotokea, nadhani ni kama unavyosema, au ni udhaifu wa mwanadamu.

Mara akafika Joji akakaa mezani pamoja nao.

- Mgahawa wa buffet umefunguliwa, je mngependa tusimame tuchukue chakula chetu?

Walipokaa mezani kwa mara nyingine baada ya kuchukua chakula chao. Habib alipendekeza kuwa Levi na Joji waendeleze mjadala, kwani hiyo ni fursa nzuri na wamekutana wote watatu pamoja…

- Tuendelee tuliposhia, mimi nashauri usafiri haswa kwa ajili ya kuwajua Waislamu.
- Pamoja na kuwa natofautiana nae daima, ila kwa hili nawafikiana nae kwa sasa, kwani kautetea ukanaji Mungu kama alivyoutetea Uislamu.
- Ha ha ha, siwezi kuutetea ukanaji Mungu wala Uislamu, mimi nazungumia suala la mfumo wa Kielimu ili kufikia kwenye ukweli.
- Mara nyingi ninaposafiri ninakutana na mijadala ya namna hii, kadhalika inabidi niwe na tabia ya kusoma kwingi. na kufikiri kwa kina na kushauriana na watu baada ya kurudi kwangu, ila mara hii nimepambana na maarifa mengi na elimu nyingi kuliko wakati wa kuyafikiria, huenda kazi hiyo ya kufikiri nikaifanya baada ya kurejea kwangu na haswa ya kuwa safari yangu ilikuwa na utajiri mwingi na faida lukuki

Levi akiwa anaangalia macho ya Joji kutafuta dalili.

- Je naweza kuuliza swali ambalo nataraji lisikukere?
- Karibu, uliza.
- Je utakapokinaishwa kuwa Uyahudi au Ukatoliki, Orthodoksi au hata Uislamu

au Uprotestant kuwa ndio njia ya furaha.Je, utahamia moja kwa moja huko, au utaanza kufikiria faida na hasara zake?.

- Mimi nadhani kuwa mahesabu yote ya faida na hasara yataishia pindi nikipata njia hiyo ya furaha; kwani hiyo ni faida halisi, Je, kuna faida iliyo na furaha kuliko njia hii …cha msingi ni kupata.

Habib alimuangalia Joji kwa kumkazia na kumwambia:

- Utaipata, mwishowe utaipata, lakini naingiwa na mashaka na unachokisema…
- Unashuku katika nini?
- Ninashuku kwa wepesi wa hilo, na kutokuwepo mahesabu ya faida na hasara, baadhi ya maamuzi ni magumu…!!
- Vipi?
- Niachie niikaribishe fikra yangu kwako, wagonjwa wote wa sukari wanajua kuwa kula sukari kwao inawadhuru hata hivyo bado wanatumia! Na kila mnene anafahamu kuwa kula chakula kwa wingi si katika siha na ni madhara kwao lakini hata hivyo wanakula.
- Ni nini uhusiano wa hilo?
- Kubadilisha dini ni kugumu kuliko kubadilisha ada ya chakula, bali ni kubatilisha maana ya maisha na sababu zake na ndio zenye kuiharakisha na kuisukuma, kisha akamgeukia Levi akasema: Nadhani Levi analifahamu hili vizuri, kwa hali yoyote mwishowe utaipata hiyo njia.
- Kwa nini una hakika namna hii? Si nyote mnatafuta na hamjaipata hadi sasa hivi?
- Huwezi ukashikilia namna hii kisha usiipate, kisha anakuwa mbali na ukarimu wa Mungu Je, hawezi kumsaidia anayetafuta ukweli?
- Unanikumbusha kikongwe niliyekutana nae aliyekuwa akisema hivyo hivyo.
- Kikongwe alisema nini?
- Mtashangazwa nitakachokisema, niliamua kwenda kujinyonga, nikakutana nae akielekea kuwa ni mtu mwenye furaha, nikamuuliza je wewe ni mtu mwenye furaha? Akanijibu ndio, nikamuuliza tena nitaifikiaje njia hii ya furaha? Kwa ujumla yeye ndie wa mwanzo aliyeniambia na kulitaja neno hili “Njia ya furaha.”
- Alikujibu nini?
- Hakunijibu kitu bali aliniambia: Ukiwa unaloshikilia hilo na kuazimia utalipata.
- Hukuwasiliana nae baada ya hapo?
- Kwa bahati mbaya sikuchukua namba yake wala anauani yake yeye ndie aliyechukua namba yangu na anuani yangu, hata hivyo hakunipigia.

www.path-2-happiness.com

- Samahani, muda wako Joji unakwenda upesi, inabidi umalize chakula chako na kutayarisha mikoba yako upesi.
- Sitochelewa …robo saa nitakuwa tayari… kisha huyo akapanda chumbani.
- Nimevutiwa na ujasiri wa Joji na wepesi wake wa mambo.
- Hata mimi.
- Kwangu mimi naweza kuvutiwa nae itakavyo, kwa kuwa mimi ni mwanamme, ama wewe jichunge.
- Nyie Waarabu mnatofuatisha baina ya mwanamme na mwanamke!
- Waarabu au Wayahudi? Mimi nadhani tumefunga mjadala wetu, lakini vimebaki baadhi ya vitu tofauti huwezi kuvifuta.
- Mfano wa nini?
- Ha ha ha, mfano wa kuwa mimi sio mzuri kama wewe, nami si mwanamke, na wewe sio mwanamme, unataka kubadilisha tabia tufanye nini, na itabakia kuwa kila mmoja ana nafasi yake tofauti, na utaendelea kubakia ni binti mzuri unayeweza kufanya mjadala na mimi mwanamume ninayeweza kujadiliana. Ama kuwafanya wanawake kama mbwa au uchafu au najisi…hili haliwezi kutoka kwa mtu au kwa dini ambayo inawaheshimu waamini wake.
- Ninakifahamu unachokusudia vizuri, na ninaomba uache kunikosoa.
- Samahani, lakini cha muhimu ni kubakiwa na kuvutiwa na fikra zake na kukishikilia na tabia na roho yake na sio kiwiliwili chake, na ulishamwambia hilo, na hii ndio maana ya mimi kuwa mlinzi wenu.
- Aah, nimefahamu maana ya mlinzi, nitaingalia nafsi yangu, inatosha kilichotokea jana.

Joji aliteremka upesi, na kumaliza taratibu za kuondoka hapo hotelini, na akaelekea hadi kwa Levi na Habib ambao walikuwa wakimsubiri.

- Inaelekea kuwa wakati unatutupa mkono, je tuondoke?
- Ndio, naogopea foleni au vituo vya ukaguzi njiani.
- Mungu akuhifadhi, Levi atakusindikiza, Ama mimi unanisamehe nina ahadi sehemu, hata hivyo usiache kutujulisha maendeleo yako na "Njia ya Furaha."
- Je, hutokamilisha ulinzi?
- Ha ha ha, hakuna wa kuwalinda isipokuwa Mungu, wala hakatazi mtu kitu mfano wa misimamo yake.
- Nitasogeza gari mlangoni ili kubeba mikoba.
- Nakushukuru Joji, umetufurahisha, nasubiri kusikia habari zako. Mungu akulinde

usisahau kwenda hospitali ya karibu pindi ufikapo London, kadhalika usisahau kuchukua sindano ambayo anayo Levi.

- Sindano gani?
- Sindano ambayo unaweza kuitumia ndani ya ndege ikitokezea umepatwa na uchovu, ni sindano uliyopewa na daktari.
- Asante sana.

(4)

Joji alitoka na kumkuta Levi akimsubiri kwenye gari, na mikoba ipo tayari garini, akapanda wakaondoka kuelekea uwanja wa ndege.

- Tutakukosa Joji, hujakaa nasi isipokuwa siku chache tu, ila ni kuwa umetuachia kumbukumbu kubwa isiyosahaulika.
- Bali tabasamu linalong'ara na elimu yako na fikra zako hazisahauliki, nimefaidika nawe sana, na nimekuchosha sana, asante sana.

Macho ya Levi yalijaa machozi…

- Nami nitakosa mijadala yako na mazungumzo yako na mtazamo wako, nitarejea katika mateso ninayoishi nayo.
- Hastahiki mfano wa Benjamin machozi haya.
- Si tatizo iwe ni Benjamin au ni Mayahudi wote, la kweli lipo ndani, mimi sijui njia ya furaha, na nilikuwa nahisi furaha nyingi katika mjadala wetu.
- Mjadala wetu utaendelea pamoja, kadhalika mjadala wetu utaendelea pamoja na Habib vile vile. Unajua! Wewe ni mkweli kwani mimi tokea nilipoanza kupita katika njia ya furaha sikupatwa na humwona ambaye ilikuwa hainiachi.
- Nachukulia hii kuwa ni ahadi kutoka kwako ya kunijulisha utakapofikia katika safari yako ya njia ya furaha, nami nitakujulisha tulipofikia na Habib.
- Ahadi lakini kwa sharti.
- Sharti lipi?
- Kufuta machozi yako na kutabasamu, ningependa kuuona uso wako ukiwa na tabasamu.
- Tumewafikiana, na naomba msamaha wako kwa yaliyojitokeza jana nilipokuwa nakuaga, niamini sikujua kwa nini nimefanya hayo.
- Nimekufahamu vizuri, nami kama wewe sikujua kwa nini nimefanya mfano wake tulipokwenda katika ukuta wa kulilia. Ha ha ha, huenda kwa sababu sikuweza kulia pale ukuta wa kulilia.

www.path-2-happiness.com

- Kwa nini hukulia?
- Kwa nini nilie? Nilie katika hekalu ambalo hawakupata bado leo hii dalili ya (ukweli wake) pamoja na yote waliyofanya!
- Huoni kuwa unavuka mpaka wa kupetuka mstari mwekundu unapozungumzia dini yangu?
-
- Ha ha ha, samahani, unisamehe niliyoyafanya nami nipetuke mipaka kuhusu Protestant, kwani wao ni majambazi wameua mamilioni ya Wakatoliki huko Ulaya. Je umeridhia na kunisamahe ewe bibie?
- Nimekusamehe bwana wangu, lakini kwa sharti.
- Rudia tena, sharti gani hilo?
- Nipate tumaini kuhusu hali yako kesho, walau kwa barua.
- Tumekubaliana.
- Tumeshafika, huu ndio uwanja wa ndege wa Ben Gurion umechukua jina la waziri mkuu wa kwanza wa Israel, na kwa taarifa uwanja huu uliwahi kushinda tuzo la uwanja wa ndege bora Mashariki ya Kati.

Joji alimaliza taratibu za safari na Levi akawa ana msubiri, alipotaka kuingia mlango wa kuondokea, Levi alimpa mkono ukiwa na sindano na kumwambia: Hii ni kutoka kwa daktari, utakapohisi joto ghafla limepanda juu au utakapohisi uchovu tumia, itakupa utulivu hadi utakapofika London.

- Asante sana.

Macho ya Levi yalijaa machozi, na akatoa mkono kumpa Joji kisha akasema: Asante sana kutoka moyoni mwangu kwa muda wote tuliokaa pamoja, Joji alimpa mkono na mkono wake mwingine kuweka juu ya mkono wake, na akahisi kuwa atampoza mpenzi wake wa miaka mingi anayefahamiana nae, lakini pamoja na hayo yote alikuwa juu ya matamanio yake kama alivyokuwa Levi juu ya matamanio yake.

- Nakuaga na Yesu akuhifadhi.
- Nakuaga na Mungu akuhifadhi.

Kisha akageuka nyuma na moyo wake ukimkata kwa kuachana na Joji.

www.path-2-happiness.com

BAINA YA UHAI NA KIFO

9 BAINA YA UHAI NA KIFO

BAINA YA UHAI NA KIFO

(1)

Joji alipanda ndege na moyo wake ukiwa umeshughulishiwa na Levi, aliuteka moyo wake pamoja na kuwa muda wa kukaa kwake ilikuwa siku nne tu.. Ni nini siri yake?! Alionekana kama Malaika tohara katika jamii dhalimu na ngumu, alikumbuka mijadala ya Levi kuhusu mwanamke na haki zake zilizosulubiwa katika Uyahudi, dini gani hii ambayo imemrithisha mwanamke kama vile chombo cha matamanio na wanamzingatia kama vile uchafu na mbwa harithi, na ya kuwa hana haki zozote? Na akakumbuka mjadala wa kupotoshwa kwa torati na chuki yao kwa Waislamu wauaji wa baba yao na kwa kizazi kilichochaguliwa ambacho kinaua na kuiba na kupoka watoto wa Shilo, alikumbuka hadithi kuhusu athari zisizokuwepo ambazo ndizo dalili ya kweli ya kuwepo kwa Uyahudi katika eneo hili…alitabasamu akiwa anakumbuka maneno ya Levi kuwa hatohama kutoka kwenye mazonge ya Uyahudi na kuelekea kwenye mazonge ya Ukatoliki wakati akiwa katika kumbukumbu hiyo alikatishwa na abiria aliyekuwa pembeni yao:

- Hii ni sindano ya nini mkononi mwako ewe Bwana?
- Nimepewa na daktari, na akanitaka nipande nayo kwenye ndege; kwani huenda joto langu likapanda ghafla.
- Je naweza kuiona?
- Chukua, je wewe ni daktari?

Aliiangalia ile sindano, na akasoma maelekezo yaliyopo kwenye karatasi iliyokuja na sindano.

- Mimi ni mfamasia, inaelekea kuwa sindano hii ni muhimu sana, kwa ujumla ni dawa iliyokuwa nadra kutumika.
- Kwa nini unatumia? Sijui, daktari hakunijulisha.
- Sijui, lakini sindano hii hutumika kwa ajili ya hali za dharura sana; kwa lengo la kupunguza aina ya virusi ambao ni vigumu kuwamaliza.
- Nadhani hii inatokana na marafiki zangu kunijali mimi, hata hivyo afya yangu ni njema.
- Huenda ikawa ni hivyo, hata hivyo sidhani kama ni sahihi, sindano hii haiuzwi ila kwa maelekezo maalumu ya daktari na katika hali za dharura mno.

www.path-2-happiness.com

- Labda, sijui, hata hivyo siha yangu ni nzuri.
- Siha ya mtu na afya yake ni taji juu ya vichwa vya watu wenye afya nzuri, haioni isipokuwa mgonjwa tu, samahani kwa kukusumbua.
- Si hivyo. Nakushukuru.

Joji alijisalimisha na kumbukumbu zake kwa mara nyingine… moyo wake ulikuwa kwa Levi, alihisi kuwa anahitaji kumshukuru kwa yote aliyomfanyia, pia alimkumbuka Habib ambaye usuhuba nae ulikuwa mzuri pamoja na kuwa alikuwa ni mwarabu, alikuwa na mijadala nae kuhusu Waislamu, na alipomwambia: Wewe ni Muislamu uliyejificha nyuma ya Ukatoliki… Ama kwa hakika safari hii ilikuwa imejaa mambo mengi na yenye kufurahisha sana… mara mhudumu wa ndege akamkatiza.

- Samahani, unapenda chakula gani zaidi? kuku au nyama?
- Nyama

Msafiri mwengine aliyekuwa jirani yake aligeuka na kumwambia:

- Inaelekea uko mbali sana!
- Ooh… ndio, safari yangu hii ilikuwa nzuri na nimejifunza mambo mengi.
- Umekaa Yerusalem muda gani?
- Siku nne
- Siku nne tu!
- Ndio, lakini kama kwamba nimekaa miezi, siwezi kamwe kuwasahau watu wazuri niliokutana nao, nimejifunza kutoka kwao mengi katika ardhi hii tukufu.
- Je wewe ni Myahudi?
- Hapana ….kwa nini?
- Mimi ni Myahudi….Samahani, lakini hakuna mwenye kuhisi hali ya raha hapa Yerusalem asiyekuwa Myahudi, kwani nchi imetayarishwa kwa ajili yao. Ama Wakristo na Waislamu hali zao si nzuri, hivyo uliponiambia kuwa umefurahishwa na uliokutana nao nikafikiri ni Myahudi?!
- Nimekutana na Myahudi na Mkristo Yerusalem, wote hawa walikuwa ni watu wazuri sana.
- Maneno haya yanafaa kusemwa Uingereza, Ama TelAviv dini ndio inayowaendesha watu na mataifa.
- Wewe ni Myahudi, je ninaweza kukuuliza?
- Uliza, usijali
- Je wewe umekinaishwa na mafundisho ya torati?

- Hapana, huwezi kuifahamu vizuri ila baada ya kufahamu mafundisho ya Talmuud.
- Vizuri, je nakuhusu mafundisho ya talmuud? Je umekinaishwa nayo?
- Ha ha ha, hapana vile vile, lakini hili ndilo mbeleko letu.
- Samahani, mgongano huu haukukeri ndani ya nafsi yako?
- Hakuna asiyesumbuliwa na hilo, hata hivyo watu wanatofautiana katika kuyachukulia mambo yanayowakera.
- Kwa vipi?
- Mimi naukimbia mgongano huu kwa kujishughulisha sana na kazi zangu na kuna watu wengine wanaukimbia kwa kunywa pombe au kwa kujishughulisha na wanawake mbali mbali, na wengine wanaukimbia kwa kufanya utafiti wa kielimu katika kadhia hii na wengine kwa kuzidisha sana kuabudu.
- Vizuri, umekuwa mkweli sana wa nafsi yako.
- Asante sana.
- Lakini linabaki swali; je huku kukimbia kunapelekea raha na utulivu au hapana?
- Nadhani kwa maafikiano ya watu wenye kutumia akili zao vizuri na kuwa ambae ataishi bila ya dini atakuwa mgonjwa; na hivyo basi kukimbia ni njia ya jitahada za kukimbia maradhi ya wakanao dini na dhulma yake na kuwa mbali na mgongano wa dini.
- Ila yule ambaye kimbilio lake ni la utafiti wa kielimu wa kadhia hii, au sivyo?
- Ndio, ila mimi sipendelee hilo, kwani linakufanya uwe na huzuni na ghamu na mgongano katika kufikiri.
- Kama kwamba unaniambia hakuna suluhisho ila kukimbia tu?
- Ndio na hapana.
- Ha ha ha, kwa vipi?
- Naam; Mimi sijui suluhisho lingine ila kwa kukimbia tu, na ni hapana; kwa sababu haiwezekani Mwenyezi Mungu akatuwacha hivi hivi tu tukapotea na huu mgongano na kukimbia.
- Unaelekea zaidi kuwa ni mwanafalsafa na sio mfamasia.
- Kitakachonichosha ni kutafuta kwangu ukweli, njia za kisomi na kielimu zinagongana na ninachokisema, na nimejifunza katika ufamasia nisizungumze kitu ila kwa njia ya kisomi.
- Kutafuta ukweli au kama ninavyopenda kuuita njia ya furaha ni yenye kufurahisha wala haihuzunishi.
- Njia ya furaha! Maelezo mazuri.

www.path-2-happiness.com

- Samahani kama nitakukata, je huoni kama ndani ya ndege kuna baridi? Najihisi baridi sana.

Mfamasia aliweka mkono wake juu ya kipaji cha uso cha Joji kuhisi joto lake, kiwango chake cha joto kilikuwa kikubwa.

- Huenda kwa ajili hii ukawa umepewa sindano hii uliyokuwa nayo, unajihisi vipi sasa?
- Baridi imezidi, nahisi uchovu sana, usijali baada ya muda hali itakuwa nzuri, je umependezwa na njia ya furaha?
- Achana na njia ya furaha kwanza, je unaweza kunipa hiyo sindano na katarasi ya maelezo ya daktari?
- Hii, chukua tafadhali.

Mfamasia alimuulizia mhudumu kwenye ndege kama kuna daktari, akamjibu hapana, alitarajiwa kuwepo lakini amechelewa.

- Hamna neno, nitampiga sindano mwenyewe; kwani nimepata mafunzo ya kutosha kuhusu huduma ya kwanza, nyongeza ya kuwa mimi ni mfamasia vile vile, hata hivyo atapoteza fahamu kidogo na naamini hatoamka ila baada ya kufika kwetu, je unaweza kumuagizia gari la wagonjwa itusubirie uwanja wa ndege wa London.
- Inaelekea hali ya hatari, hakuna haja ya hilo, mke wangu ananisubiri na gari la wagonjwa, nadhani umezidisha zaidi.
- Sijazidisha, hata hivyo sipendi kuvuka mipaka ya njia za kielimu katika kushughulikia mambo mbali mbali.

(2)

Joji aliamka kutoka kwenye usingizi mzito na kujikuta yupo hospitalini London, pembeni yake akiwemo Katarina huku akitabasamu.

- Namshukuru Bwana kwa usalama wako mpenzi.
- Nipo wapi? yuko wapi yule mfamasia?
- Wewe upo hospitalini London, lakini ni nani huyu mfamasia?
- Hospitalini? yuko wapi yule abiria niliyekaa nae pamoja kwenye ndege?
- Ooh, nimefahamu, hakuondoka hadi alipokufikisha kwenye gari la wagonjwa, na akahahikikisha afya yako, alichukua anuani yako na kuondoka, namshukuru Bwana Mungu.
- Unaendeleaje mpenzi wangu, nimekutamani sana, samahani kukutaabisha na kukusumbua, sikujua kuwa itafikia kiwango hiki.

- Daktari amesoma ripoti yako na akachukua sampuli ya damu yako na wakaangalia hapo hospitalini kwa eksirei na wakasema kuwa watahakikisha vipimo hapo kesho.
- Tutakwenda wakati gani nyumbani?
- Sijui, baada ya kutoka matokeo ya vipimo. Amesema watatujulisha lakini kwa uchache ukae hospitalini kwa muda wa wiki nzima kama walivyosema.
- Wiki nzima?!
- Cha msingi sio wiki, bali ni kutumaini afya yako, na wanashangaa ni kwa nini hukubaki hospitalini huko?
- Walitaka sana hilo na wakajaribu, lakini niliwakatalia….kwani kuna nini huko?
- Nitachukuwa likizo na kukaa pamoja nawe, huenda huu ni munasaba wa kukaa pamoja; nina hamu sana ya kukaa nawe.
- Nami hali kadhalika nahitaji hilo sana, natamani turudi pamoja nyumbani.
- Tutatoka karibuni, usihofu mpenzi… je umetembelea Kanisa la Kiama?
- Ndio…na nilikuahidi kulitembelea, kadhalika nimetembelea Kanisa la Bikira Maria.
- Furaha iliyoje kwa kila anayesali katika Kanisa hili lililobarikiwa kiasi gani natamani kulitembelea.
- Nimeswali kwa ajili yako kama nilivyokuahidi, lakini kuna furaha gani katika hili?
- Sijui furaha nyingine zaidi kuzama katika kumuabudu Mungu.
- Vivyo hivyo ndilo wanalosema Mayahudi wa siasa kali hata ikiwa sikukuu zao na ibada zao ni za huzuni na kilio!
- Kweli kabisa, lakini wao wanamuabudu Mungu kwa dini iliyokwisha futwa na kuisha baada ya kudhihiri Masihi Kristo amani iwe juu yake, bali walimpiga vita na kumuuwa Masihi Kristo na kuwaadhibu wafuasi wake.
- Je kwani Wakristo hawaiamini torati kwani ndilo Agano la Kale?
- Ndio, wanaiamini.
- Sasa kwanini uniambie kuwa ni dini iliyokwisha kwa kudhihiri Kristo?
- Unaelekea kuhamasika sana na Uyahudi, kama dini imekwisha, yamebaki mafundisho tu ya torati.
- Iwaje uamini na upate mwongozo wa mafundisho yaliyokwisha potea?
- Yaliyokwishabadilishwa nani aliyekuambia hivyo?
- Maelezo yamekuja katika torati kuhusu watoto wa kike wa Shilo:

www.path-2-happiness.com

- Akawausia watoto wa Benjamin kwa kusema: “Nendeni Kromu na jificheni humo na subirini hadi watakapotoka wasichana wa Shilo ili kucheza nendeni kwa haraka kwao, na kila mmoja wenu amteke mmoja kisha torokeni nao hata kwenye ardhi ya Benjamin”, je unawajuwa hawa wasichana wa Shilo? Je unaamini kuwa maandiko haya ni ya Mungu?
- Nawajua vizuri watoto wa Shilo, sipendi kuzungumzia hilo, ni maelezo ambayo tunaweza kuyapata kwa maelezo ya Maaskofu na Mapapa.
- Imekuja katika torati vile vile: “Alisema Bwana Mungu wa Israil: Kila mmoja wenu abebe panga lake na azungukie sehemu mlango hadi mlango na amuuwe ndugu yake, rafiki yake na jirani yake” Je, maneno haya ya kikatili yanaweza kuwa ni ya Mungu?
- Samahani napenda ubadilishe maudhui, nayajua vizuri maandiko haya na mengine mfano wake, na sipendi kuyajadili, kadhalika wewe unatakiwa upumzike.
- Kwa nini?
- Nimekuambia sipendi kuzungumzia maudhui haya…Nadhani unao muda wa kutosha hapa hospitalini wa kutafiti na kusoma.
- Umesema kweli la muhimu niwe na kompyuta, kadhalika napenda kununua baadhi ya vitabu, nataka kusoma kuhusu Ukristo na madhehebu yake mbali mbali.
- Vizuri sana, huenda ukawa Mkatoliki.
- Huenda ikawa hivyo!
- Kusoma kwako huku kutakuwa kitangulizi kizuri cha safari yetu, umeshasahau mpenzi wangu?.
- Sijasahau, nitajaribu kesho pamoja na daktari ili iwe karibu iwezekanavyo, hata hivyo inabidi muda wangu huu wa kuwepo hospitalini niutumie vizuri kwa kusoma.
- Usijali sana kukaa kwako, nitakuwa pamoja nawe na kuzungumza pamoja.
- Kiasi gani nakupenda mpenzi wangu Katarina.
- Nami hali kadhalika, Je, utaniruhusu niondoke sasa hivi nije kesho? Usiku unaingia, na mimi tokea jana nipo hapa.
- Samahani, nimekuchosha, nitakusubiri kesho mpenzi wangu, lililo muhimu ni kuwa nileteeni kompyuta yangu na simu yangu iwe jirani nami, nataka kumalizia baadhi ya kazi zangu.
-
- Nitaweka kompyuta yako na simu yako mezani hapo karibu yako, lakini kwa

sharti usijichoshe, nataka upumzike mpenzi wangu, tutaonana kesho.

Joji hakutaka kulala, bado ilikuwa ni mapema mno, aliamua kusoma kidogo, na kuanza kusoma barua pepe zake na kukutana na barua ya Levi ikimtaka kumuelezea kuhusu afya yake, akamjibu na kumuelezea kilichotokea, na akamshukuru mno kuhusu sindano aliyompa, na mapokezi yake, na kila alichompa. Na akamkumbusha kuwa hakusahau ahadi yake, lakini hata hivyo alikuwa bado hajawasha kompyuta na simu yake ila muda mfupi tu uliopita. Kadhalika alimuhakikishia kuwa yupo katika ahadi yake aliyompa kuwa ataendelea kumpa habari za njia ya furaha, na akamtaka amtolee shukurani nyingi Habib vile vile.

Alikutana na barua nyingine kutoka kwa Adam inayoelezea kuhusu starehe ya kiwiliwili kwa mateso ya roho ikisema:

“…ikiwa roho haitopata furaha pamoja na kiwiliwili, basi nilichokiita furaha ya kiwiliwili ndio huzuni ya kiwiliwili na ya kiroho, na falsafa hii itaendelea kubakia kuwa ni falsafa nyeusi, falsafa ambayo inazingatia kuwa maisha ni huzuni na hakuna furaha ndani yake. Swali linalojitokeza hapa je tumeumbwa ili tupate tabu na kuhuzunika au tumeumbwa ili tuwe na furaha? Ule muono wa kuwa sisi tumeumbwa ili tupate tabu ni muono uliokuwa wa karibu sana na muelekeo wa wakanao kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ambao unamtuhumu Mola kwa kila upungufu au dini za wanadamu za kipagani zilizo mbali kabisa na ufahamu wa tabia ya Mwenyezi Mungu na tabia ya mwanadamu na tabia ya dini, au kwa dini ambazo zimeathirika na upagani kwa sababu ya kubadilishwa kwake na kuchafuliwa mafundisho yake. Kwa ujumla muono huu unakupa sura ya mtu mwenyewe asiye na furaha na migongano ya ndani aliyokuwa nayo kuliko hata ilivyo rai ya kisomi au ya kifalsafa au hata ya kidini….nataraji utakuwa umeshawasili kutoka safari yako, baada ya mapumziko ya safari yako tutaonana ili tuendelee kujadiliana katika hilo.”

Joji alimaliza kusoma barua na akairejea mara ya pili, kisha akajisemeza: Adam kama ilivyo ada yake, sijui ni kwa sababu yeye ni mwanafalsafa mkubwa au ni kwa sababu yeye ni Mprotestanti au ni Myahudi? Na sijui ndani ya maneno yake –pamoja na udogo wa umri wake na ukawaida wa kazi aliyokuwa nayo nayaona kuwa ni maneno ya kawaida lakini ya kina katika wakati huo huo? Amesema kweli Adam: Roho haiwezi kuwa na furaha peke yake kadhalika kiwiliwili hakiwezi kupata furaha peke yake: Mwanadamu ni kitu kimoja kilichokamilika na kumgawa ni aina ya ujuu juu wa kadhia za kina kabisa,

www.path-2-happiness.com

yaani ni starehe gani ya kiwiliwili ya kupita ambayo itafuatiwa na maradhi ya kiroho na ya kiwiliwili, na starehe gani ya roho katika utawa na kuyaacha hata ikiitwa kuwa ni ya kimaadili au ya kiroho kama ilivyo utawa wa KiBudha. Ama kwa hakika njia ya kuelekea furahani ni lazima roho iungane na akili pamoja na kiwiliwili, muungano ambao utaufanya ufurahi na sio kuuadhibu, ili baada ya hapo kiwiliwili kwe furahani na kustarehe kwa akili iliyo nyoofu iliyozungukwa na furaha ya kiroho itakayofanya kuwa juu! Baadhi za dini zimeikimbia hali hii, hali ya starehe ya kiwiliwili ili ufurahishe roho, na dini zingine vile vile zimekimbia starehe za roho ili zishughulike na kiwiliwili tu. Na zote hizo hazikuweza kuzifurahisha sio kiwiliwili wala roho hali kadhalika.

Joji aliangalia saa yake, ilikuwa inaashiria saa mbili, hivyo akampigia Adam.

- Ndio Adam, nimeshafika London lakini nipo hospitalini, na ndio maana siwezi kuonana nawe, Je, unaweza kuja kunitembelea ili tumalizie falsafa yako na mjadala wetu?
- Pole sana… Nitakutembelea, na sito kukera na mjadala wangu au falsafa yangu kama unavyoiita, nataraji nisikuchoshe.
- Sijakusudia hivyo, kwa hakika ninafurahishwa na mjadala wa pamoja nawe na falsafa yako, hivyo usinielewe vibaya.
- Nami sijakusudia kuwa nimeghadhibika kwa maneno yako, hili jambo ni la kawaida na dogo na mimi ninapenda mambo madogo ya kawaida, nitajaribu kukutembelea kesho jioni.
- Nitakusubiri Adam, natamani mazungumzo nawe
- Ha ha ha, tutaonana kesho, inaelekea unachanganya baina ya hamu ya mazungumzo na hamu ya kunywa kahawa, kwa heri.

Joji alizima simu akawa anafikiria…Ni siri gani inayomfanya avutike na Adam? Yeye sio Mwingereza anaweza kuwa ni Myunani au Mtaliano au ni mtu kutoka Latini; ila napata tatizo kutoka kwake; Itakuwaje kama Levi atanikuta na Adam?. Atamuonaje? Ha ha ha, je Adam ataweza kuwa na subira akimwona na yale macho yake ya kibluu na nywele zake nyekundu? Au atakuwa kama vile (Kakhi) mwingine, nasaha zake ni nadharia tu kama walivyo watu wengi? Ha ha ha bali kama ndio nilivyo mimi?! Kwa ujumla kesho itafika, na nitamueleza kila nililo kutana nalo…

(3)

Nesi alimwamsha Joji mapema, na wakati huo huo akimuwekea kifungua kinywa mezani mwake.

- Muda gani atafika daktari?
- Saa tatu asubuhi daktari atawazungukia wagonjwa, la msingi ni kuwa ukihisi kupanda kwa joto niambie upesi, sisi tutapima joto kila baada ya saa moja kuanzia saa mbili ambapo nguvu ya ile sindano uliyopewa inapokuwa imekwisha.
- Asante, inaelekea kuwa swala la joto ni la hatari na linaangaliwa mara kwa mara.
- La msingi ni kuwa ukihisi kupanda kwa joto mwilini mwako au ukihisi baridi tujulishe upesi.
- Vizuri, vizuri.

Joji alimaliza staftahi yake, alikaa akifikiria maneno ya nesi, na akakumbuka jinsi Levi alivyomtahadharisha kuhusu sindano alipokuwa akimpa… alihisi hali ya hofu na – akisubiria kuja kwa daktari ambaye alifika chumbani saa tatu na nusu.

- Je unaweza kunijulisha hali yangu?
- Uchunguzi wetu hadi sasa hivi ni sawa na matokeo ya uchunguzi uliopita uliofanyiwa Yerusalem.
- Samahani, sijui matokeo ya uchunguzi wa vipimo vya Yerusalem ni yepi hayo?
- Kuna virusi vimeingia katika mishipa ya akili, na ghafla bila ya onyo lolote lina sababisha kupandisha joto, hivyo basi tunalazimika kukubakisha hospitalini pamoja na kuwa upo katika hali ya kawaida kabisa na husumbuliwi na tatizo lolote, hivyo basi joto la kiwiliwili chako likipanda tunalazimika kukupa sindano yenye kutuliza na kushusha joto, ambayo nguvu yake inadumu kwa muda wa siku moja hadi mbili.
- Hadi lini nitakuwepo hospitali?
- Kwa sasa hivi siwezi kujua, kwa ujumla ni kuwa kuna vipimo vingine ambazo tunasubiria matokeo yake, ambayo yatakuwa tayari baada ya siku mbili zijazo, katika hali yoyote ni kuwa haitozidi zaidi ya wiki mbili, kama jambo lingine halitojitokeza.
- Ni nini sababu ya virusi hivi?
- Hadi sasa haijulikani, hata hivyo usijali, tutajaribu kukupa utulivu kadri iwezekanavyo, kadhalika tutakujulisha maendeleo mara kwa mara, hayo ndio ninayofahamu hadi sasa kuhusu maradhi yako.

www.path-2-happiness.com

- Nakushukuru kwa muamala wako mzuri.

Daktari aliomba ruhusa na kuondoka…Joji alichukua Kompyuta yake, ili apange muda wote atakapokuwa hapo hospitalini autumie vipi. Joji aliamua kuwa muda atakaokuwa hapo hospitalini autumie kwa ajili ya kujisomea, haswa kwa sababu yupo katika njia ya furaha, ambapo anahitaji kufahamu kuhusu dini muhimu zaidi ambayo ndio dini yake, akaanza kujiuliza huku akiitilia shaka nafasi yake akiwa katika hali ya kukariri maneno. "Kuijua dini yangu! Kuujua Ukristo na madhehebu yake, kama alivyokwisha toa maamuzi autumie muda wake mwingi –kujadiliana na Katarina; ambaye ni mwanazuoni wa Kikristo. Kadhalika pamoja na Tom na Adam, vile vile na katika mijadala mbali mbali kwa njia ya barua pepe na Levi na Habib ikiwezekana. Kisha baada ya hapo akachukua muda kusoma na kila kundi asingeweza kumaliza.

Ilipopindukia usiku wa manane Katarina alifika hospitalini akiwa na Maiko pamoja na Sali, Joji alifurahi sana kuwaona, alikuwa na hamu nao, aliwakalisha pembeni yake ili aweze kuwatania na kuwachezea. Joji alikuwa katika hali ya furaha pindi alipokuwa akicheka nao, na hapo hapo akakumbuka furaha yenye kufurahisha roho na kiwiliwili kwa pamoja na akajua ya kwamba hali hii ya starehe hupata kwa kukaa pamoja na wanawe. Akajizungumzisha lau kama watu wote watafahamu kitakachowaletea furaha ambacho kitafurahisha roho na kiwiliwili na hapa ndipo hatima ya furaha itakapofikiwa…..

Aliwaangalia watoto wake wawili… kisha ikamjia fikra akilini….

- Nini kinachokufurahisha zaidi ewe Maiko katika maisha?
- Kucheza na wewe baba, na ninapenda mpira wa miguu.
- Na wewe Sali?
- Nami napenda kucheza nawe baba, na vile vile napenda kuchezea midoli.
- Na mimi napenda kucheza nanyi, je kuna chenye kuwafurahisha kingine zaidi ya michezo?

Maiko kwa mshangao:

- Wakati mwingine napenda kufurahi lakini sijui kwa nini? Na wakati mwingine nahisi tabu na sijui kwa nini? Ni kwa nini baba?
- Wewe unadhani kwa nini Maiko?
- Huenda ikawa furaha kwa sababu nimemsaidia mwenzangu shuleni au rafiki yangu, na tabu na huzuni kwa sababu ya jambo nililofanya.

Tabasamu kubwa lilijitokeza kwa Katarina kwa mjadala huu mzuri wa

kifamilia. Kisha Katarina akasema: Mpenzi wangu huenda furaha inakuwa kwenye moyo tunapowapenda watu na kuwatakia kheri.

- Una maana kuwapendea watu kheri, hata kama hatujafanya jambo lolote mama.
- Ndio, na mfano wake kuwachukia watu na kuwataka shari, hata kama hatujawafanyia lolote.

Joji alipendelea mjadala ule uendelee zaidi kisha akasema: Maiko na Sali kama ni hivyo kwa nini watu wasijifurahishe wenyewe na wachague wenyewe huzuni na tabu?

- Maiko: Kwa sababu wao ni wapumbavu.
- Sali: Au ni kwa sababu hawajui.
- Katarina: Au yanaweza kuwa yote mawili, na nyongeza ni kuwa uongofu na kufanikiwa katika kufanya ya kheri na furaha zote ni neema kutoka kwa Mungu.
- Joji: Kama ni hivyo, basi ni bora tukatafuta njia ya kuelekea kwenye furaha.
- Maiko: Nimekusikia ukimwambia mama kuwa utasafiri kwenda Yerusalem; ili kutafuta na kufanya utafiti ilipo njia ya furaha, je njia hiyo ya furaha ipo Yerusalem tu?
- Ha ha ha, sivyo mwanangu, ninachokitafuta ni haki, na safari yangu kikazi inanipeleka Yerusalem kwenda kuingia mikataba ya kazi huko, na ni fursa kwangu kutumia fursa hiyo kujifunza, na kufahamiana na watu.

Sali alisema bila kujitambua:

- Siwapendi wakazi wa Yerusalem.

Joji katika hali ya mshangao:

- Kwa nini?
- Kuna msichana ninasoma nae shule anasema, jamaa zake mara kwa mara wanakwenda Israel na haswa katika mji wa Yerusalem, na anasema kuwa Israel yote ni mauaji na magereza na adhabu na milipuko, na kwa sababu hiyo siipendi wala sipendi watu wake.

Katarina alishangazwa na maneno ya binti yake, kisha akasema: hakuna mwenye akili anayependa ugaidi na mauaji. Sheria zote za ardhini (za wanadamu) na za mbinguni (kutoka kwa Mungu) huamrisha uadilifu na wema.

Alipokuwa akizungumza Katarina Joji alikumbuka ubudha, na sheria mbali mbali za Agano la Kale kuhusu mauaji ya wanawake na watoto wa Shilo, kisha akatabasamu na kusema:

- Yerusalem kuna watu wazuri wa kila dini katika wayahudi, wakristo na waislamu

www.path-2-happiness.com

- Sali: Kwa hivyo basi simpendi Levi binti wa Kiyahudi, yeye anapenda mauaji haya na magereza.
- Joji: Ni nani huyu Levi?
- Mwenzangu ninasoma nae shule, binti wa Kiyahudi.
- Joji: Vizuri ni vizuri enyi wanangu kupenda na kuwachukia watu kwa misimamo yao au tabia zao, na sio kwa sababu ya maumbo yao wala nchi zao.
- Maiko: Nami simpendi mwenzangu David, yeye hazungumzi chochote isipokuwa Pombe.

Joji alimuangalia Katarina kwa muono wa kumuibia…kisha akatabasamu….

- Ehe katika pombe kuna nini Maiko?
- Sijui, ninachokijua nikuwa inapoteza akili ya mtu.

Uso wa Katarina ulionesha kubabaika, akafanya haraka kumjibu mwanae…

- Umefanya vizuri Maiko, ni kweli, vile vile ni haramu katika dini yetu kama ilivyokuja katika Agano Jipya, “Pombe na kilevi usinywe.”

Katarina aliona jicho la mshangao kwa Joji, hivyo akabadilisha maudhui.

- Ulikutana na daktari ewe Joji?
- Ndio.
- Kuna mpya?
- Hakuna mpya, inaelekea ni vipimo vile vile na matokeo ya hospitali ya TelAviv, nami sikujua matokeo ya vipimo vile vya TelAviv.
- Ajabu, je daktari kule hawakukujulisha matokeo ya vipimo?
- Kwa huduma nilizokwenda kutoa huko, kuna mmoja wa wafanyakazi wake aliyefuatilia vipimo hospitali, na hivyo basi Levi ndie aliyekuwa akijua majibu ya vipimo vile, nilijaribu kutaka kujua ukweli akakataa na hakunijulisha ili nisije kupata mshtuko.
- Wivu ulijitokeza usoni mwa Katarina, na akasema; inaelekea Levi ni mzuri na mwenye kukujali sana!!
- Sali: Baba ikiwa Levi huyo kama yule mwenzangu shuleni basi sio mzuri wala si mwema.
- Joji: Levi alikuwa mwema sana kwangu.
- Katarina: Mayahudi wanawake ni wepesi sana kijinsia (kama ilivyo katika Agano la Kale.
- Maiko: Je katika Agano la Kale inahimiza matendo ya kijinsia ewe mama.
- Katarina: Nilikuwa nakutania Maiko, kisha akamgeukia Joji na kusema: Au sivyo

Joji?!

- Ndio….mama yako anapenda sana utani…hakuna dini ya haki inayohimiza kuuwa watu au kunywa pombe au ngono zembe wala hatuamini kwa hili juu ya dini ya haki.

Katarina alifahamu ujumbe wa Joji pindi alipokuwa anaongea na Maiko, akajaribu kubadilisha maudhui kwa mara nyingine na kusema:

- Nitaondoka sasa hivi Joji; niwapeleke watoto nyumbani kwani tumechelewa, kisha nitarudi upesi kwako.
- Nitakusubiri mpenzi wangu…..kisha akawageukia wanawe na kusema: mnitembelee kila baada ya siku mbili kwa uchache enyi mashujaa, ninawapenda.

(4)

Joji alisalimu amri na fikra alizonazo, baada ya kuondoka kwa Katarina na watoto wake na kubakia peke yake. Alianza kujiuliza: Je nitaendelea katika maisha yangu yote kuwa katika migongano ya kifikra na falsafa na dini mbali mbali?! Kwa nini dini hizi zisikubaliane katika furaha kwa kila mwanadamu?! Kwa nini watu wasifuate dini ya hakika ambayo itawafurahisha watu wote?! Kwa nini wanadamu wote wasiishi katika amani ndani ya nafsi zao?! Na amani wao kwa wao?! Kisha akatabasamu huku akijisemesha: Huenda nimebadilika na ghafla nimekuwa Plato mwanafalsafa mkubwa. Ajabu maisha haya wakati mwingine yanatubadilisha kuwa ‘kufikirika’ ambayo haipo ila katika akili za watu! Nafikiria kama watu wote wataweza kumfikia Mungu wao bila ya tabu yoyote, huenda maisha yakawa ya uchovu, au huenda tulikuwa ni viumbe vingine na sio wanadamu kwa udhaifu wao. Tukifikia wakati huo shari haitokuwepo, bali hata kheri haitokuwepo vile vile, kwani kheri haitofahamika ila kwa kuwepo shari, bali kuwepo vyote ni dalili kuwa sisi tupo katika maisha haya. Aakh…..ni kiasi gani mwanadamu anapotea katika falsafa yake na fikra zake kama hatokuwa amefahamu maana ya maisha yake na maana ya mauti yake na wapi atakwenda?

Joji alikuwa akisubiri kurejea kwa Katarina pamoja na kuwa si muda mrefu tokea aondoke, hali kadhalika alikuwa akisubiria ziara ya rafiki yake Adam…. alifungua kompyuta yake, kisha akaangalia barua pepe, akakuta barua kutoka kwa Kakhi akimshukuru kufani –kisha kazi zake na akamwambia kuwa alijua maradhi yake kutoka kwa mke wake, na kuwa leo au kesho

www.path2-happiness.com

atakuja kumtembelea, kisha baada ya hapo akaingia katika facebook ya Adam, na hakuomba urafiki ili Adam asije kutanabahi kuwa Joji anasoma kila analoandika. Ndani ya face book ya Adam alipambana na makala yake ya pili yenye anuani "masomo kutoka kwa rafiki yangu mtafuta furaha2…." Ambapo ndani yake aliandika yafuatayo:

"Rafiki yangu mtafutaji anashikilia kuijua njia ya furaha, na nimejifunza kutoka kwake yafuatayo:

1. Mambo makubwa; kama vile kutafuta furaha, inahitaji juhudi kubwa na mitihani mingi.
2. Kushikilia jambo kunatengeneza fursa mbali mbali, kila anapozidi rafiki yangu kushikilia huzalika mbele yake fursa ya kusoma na kujifunza mambo mapya.
3. Ushindi mkubwa na mafanikio ayapatayo mtafutaji kuhusu furaha ni kuishinda nafsi yake, na sio kuyashinda matukio ya maisha yake.
4. Pamoja na nguvu na kushikilia kwake rafiki yangu na azima aliyokuwa nayo, lakini ninachokihofia anachokitaka kiasi cha kutosha.

Subirini mafunzo yafuatayo hivi karibuni….salamu zangu kwenu nyote Adam."

Joji alirejea kusoma yaliyoandikwa kwa mara nyingine tena kwa utulivu na umakini zaidi, alikuwa akihisi kuwa Adam anajua yanayopita kwenye fikra zake, na akawa anajisemesha anakusudia nini aliposema mtihani mkubwa? Na pale, alikuwa na maana gani aliposema: Mwanadamu aishinde nafsi yake? Je Adam anajua kuwa rafiki yake amefeli mtihani wake na akauza misimamo yake na kutoa rushwa? Je anajua kuwa alimbusu na kumkumbatia mwanamke mzuri? Na alikuwa anataka kumfanyia hiana mke wake? Je anajua kuwa hadi sasa hajachukuwa maamuzi ya kuondoka katika shirika linaloongozwa na mtu asiyekuwa na maadili kama Kakhi, bali humsaidia wakati mwingine kutoa rushwa? Kisha nini maana ya nukta ya mwisho? Kwa nini aniogopee mimi kujua kila ninachokitaka na sijui ninachokitaka? Je haikuwa sawa kujua kila anachokitaka, ina maana bila shaka ni kujua anachokitaka? Ni kweli anataka kuwa kafiri mpinga Mungu aliyepotea, wala sio ubudha au Uhindu uliopotea akiabudu ng'ombe au maelfu ya miungu. Wala hataki awe Myahudi mgumu hivyo ni nini anataka? Inaelekea kuwa hofu ya Adam ipo sehemu yake, atajaribu kujadiliana nae leo kuhusu hilo bila ya kumjulisha kuwa amesoma kutoka kwenye web site yake chochote kile; ili aendelee kuandika kwa uhuru zaidi.

Joji alihisi kuwa chumba kinazidi kuwa baridi, alisimama apunguze, na hapo hapo akahisi uchovu, na nesi alimwona katika hali hiyo na akamjia upesi upesi.

- Je unahisi baridi?
- Kidogo, huenda joto limepungua.
- Hali ya hewa ipo sawa haijabadilika, jinyooshe kitandani, nitawasiliana na daktari na kukuletea sindano upesi, dakika moja tu.

Nesi aliondoka upesi na akarejea akiwa na sindano ya Joji…

- Hii ni sindano mpya uliyoandikiwa na daktari.
- Mpya?!
- Ndio, hii inachukua muda mrefu kuliko ile ya mwanzo, lakini utapoteza kumbukumbu kabisa, samahani kwa hilo, inatakiwa nikupige upesi, je unaweza kunyoosha mkono?

Nesi alimpiga Joji sindano dakika chache zilizofuata alipoteza fahamu akawa hahisi chochote.

Katarina aliporudi alimkuta Joji katika hali hii. Alikaa pembeni yake akisubiri azinduke, alikuwa akimuangalia alivyojilaza kitandani, alihisi mapenzi yake kwake Joji. Katarina anafahamu wema kwa Joji na mapenzi ya Joji kwake. Hata hivyo haachi kujadiliana nae, wala hataki kujisalimisha kwa Mungu kama wasemavyo Wakatoliki…..Alikaa akifikiri, hata hivyo yeye Katarina anapenda kufanya nae mijadala, pamoja na kuwa mwenyewe Katarina anababaika sana na kujihisi vibaya. Maswali mengi ya Joji kwake hayana majibu yaliyokuwa wazi, ni bora angejisalimisha kwa Bwana ili apumzike na maswali yote haya na mijadala hii, au huenda ikawa kujisalimisha ni aina ya kukimbia na kutoroka majibu kwa njia isiyokuwa ya Kimantiki. Ni ukweli usiopingika kuwa migongano iliyopo kwenye Ukatoliki inamsumbua wakati mwingine, lakini hata Uyahudi au Uprotestanti ni hivyo hivyo kuna migongano kama hiyo, na huenda ikawa ni mingi kuliko ya Ukatoliki! Si bora basi kujisalimisha bila ya mjadala ni raha zaidi kwake yeye kuliko aina hii ya ukimbizi? Wakati mwingine kukimbia ni bora kuliko mapambano ambayo mwisho wake ni hasara, hata hivyo kwa nini mapambano yasipelekee ushindi na kupata faida? Ooh…Nisamehe ewe masihi, sijakusudia kuwa hujatukomboa lakini… hapo

alimkumbuka Levi binti mzuri wa Kiyahudi ambae alimzungumzia…

www.path-2-happiness.com

ana muamini sana Joji na anajua misimamo yake na uaminifu wake kwake. Hata hivyo kwa nini amerejea kutoka Yerusalem na mazungumzo ya jinsia na wanawake kisha akatabasamu huku akifikiri wivu wake kwake, na wivu huu uko wapi pindi alipokubali Tom ambusu, je Joji sio ndie mwenye haki zaidi katika hilo? Kwa nini ninywe pombe na mimi ninajua kuwa Agano Jipya linakataza, bali ndivyo ninavyowafundisha wanangu! Ole wangu kwa nini nimemwambia hayo alipokuwa anajadiliana nami…

Wakati Katarina anaendelea kuzama katika kufikiri, alisikia sauti ya mtu akimwambia nesi: Yuko wapi, Joji ewe binti mzuri? Muangalio wake kwa yule nesi ulikuwa ni mbaya zaidi kuliko hata maneno yake….Yule nesi alimuashiria yule mtu chumba cha Joji na alipoingia tu alikwenda kumpa mkono Katarina.

- Hallo, je wewe ni mke wa Joji?
- Ndio, mimi ni Katarina, karibu, wewe ni nani?
- Mimi ni Kakhi, mwenzake Joji kazini, nilimpigia simu jana na kuniambia yupo hospitali, vipi hali yake?
- Nzuri… inaelekea ana homa, joto lake limepanda na hivyo wamempa sindano yenye kutuliza na kushusha joto lake; amelala na kupoteza hisia ya waliomzunguka.
- Huelekei kuwa ni Mwingereza!
- Mimi ni Mwingereza lakini mwenye asili ya Kihindi.
- Ha ha ha, uzuri wa Mashariki uko wazi, ndio maana Joji akatosheka na hili pindi alipokwenda India….
- Ametosheka na nini?
- Ametosheka na wanawake wazuri wa Kihindi, ha ha, ha kwa ujumla nakupongeza, inaelekea Joji anakupenda sana.

Hasira ya dhahiri ilikuwa katika uso wa Katarina

- Hii ndio mara ya kwanza nakuona, huenda Joji alikuwa anaficha uzuri wako kwangu, hata hivyo nina bahati ya kufahamiana nawe, nipo tayari kukuhudumia kwa lolote na hata kama utataka kufanya kazi katika shirika letu tupo tayari.
- Asante sana, mimi ni mwalimu wa dini, na nimejitoa kwa ajili ya Kanisa.
- Kwetu sisi malipo ni zaidi na huenda ni bora zaidi na kuna raha zaidi.
- Mimi nimejitolea kwa Kanisa nasitaki kuacha kazi yangu.
- Ni juu yako kufikiri, Joji amelihudumia shirika sana na bodi ya menejimenti imefurahishwa nae na uzuri wa kazi yake, haswa baada ya hii safari yake ya mwisho TelAviv. Hebu fikiri, safari zote mbili zilizofuatana ameweza kusaini

mikataba inayotakikana, na kwa uhodari wa hali ya juu na kwa maridhiano na wakala wetu.

- Huenda hili limetokana na maelekezo yako; kwani wewe ndie mkuu wake wa kazi.
- Huenda, sidhani hivyo, na haswa katika maudhui ya wanawake.

Katika hali hii mara mtu akagonga mlango chumbani na kuuliza:

- Samahani ….je hiki ni chumba cha Joji?
- Ndio, na huyu hapa mwenyewe, hanafahamu, mimi ni mke wake, karibu, nani wewe?
- Mimi ni Adam rafiki yake, alizungumza na mimi leo akiwa katika afya njema. Amepatwa na nini?
- Maradhi yake yanaibuka ghafla na joto lake limepanda; kinachofanya apewe sindano ya kutuliza na kuunguza joto lake, na ndio inayomfanya muda mrefu kuwa katika hali hii ya kupotewa na fahamu….
- Nasikitishwa na hali yake, je kuna lolote ninaloweza kulifanya kumsaidia rafiki yangu?
- Asante kwa hisia zako njema, tafadhali karibu uketi
- Asante!

Adam alielekea kwa Kakhi amsalimu, Kakhi akampa mkono wa dharau Adam akamwambia kwa haya:

- Samahani…sijafahamiana nawe?
- Mimi ni Kakhi, mkuu wake Joji katika shirika, na wewe ipi kazi yako?
- Mimi ni Adam mhudumu katika Mgahawa, na rafiki yake Joji.
- Mhudumu?!

Uso wa Adam ukabadilika na kuwa mwekundu, na akaficha hasira zake, kisha akazungumza kwa upole wa mwenye hasira:

- Unaweza kumuuliza atakapozindukana! Pamoja na kuamini kuwa urafiki unajengwa juu ya ukumbi wa nafsi na roho na fikra na sio ukuruba wa mali!

Katarina aliingilia mazungumzo yale upesi, na alikerwa sana na maneno ya Kakhi:

- Si neno Adam, Joji alinizungumzia sana kuhusiana nawe! Kwa hakika anafurahia urafiki wenu, rai yako na hekima zako.
- Huu ni katika wema wake na tabia zake nzuri, kisha akamwangalia Kakhi na akaendelea kuzungumza: Vinginevyo yeye ni mhandisi na mtaalamu mkubwa, na

www.path-2-happiness.com

mimi ni mhudumu tu!!

Kakhi kwa jeuri na dharau

- Kweli kabisa
- Kakhi tafadhali mheshimu rafiki yake Joji.
- Ha ha ha, unaniambia mimi hivyo kwa ajili ya mtu ambae kipato chake hakizidi mfagizi wangu.
- Yeye ni rafiki wa Joji, kisha mali sio kila kitu, unadhani kuwa thamani ya mtu inalinganishwa na mali?
- Unafanana na Joji….ama mimi hainipendezi kukaa na muhudumu, cha msingi Katarina ofa yangu ipo pale pale uje ufanye kazi pamoja nasi…hii ni kadi yangu na kuna namba yangu, na ukitaka chochote wasiliana nami, kwa heri na ugueni pole.
- Nakuomba samahani Adam kwa kila kilichosemwa.
- Hakuna haja ya kuomba samahani, thamani yangu ipo ndani yangu, na sio kama anavyosema yeyote kuhusiana nami, kisha wewe hukusema chochote ili uombe msamaha.
- Inaelekea Joji ana haki kwa mengi aliyosema kuhusu wewe.
- Asante sana, huu ni wema wako na wake.
- Amenieleza sana kuhusu kushikamana kwako na dini na hekima yako na nasaha zako.
- Joji ni mtafuta ukweli kabisa, na atafikia lengo lake; Mungu ni mkarimu hamuangushi mtu anayetaka kumfikia.
- Maneno ya kina kuhusu imani ya Mungu, lakini usihofie akiacha dini zote kwa jinsi anavyoona migongano iliyopo!
- Sidhani hivyo.
- Kwa nini unajiamini hivyo?
- Hakuna mgongano katika dini ya kweli na atafikia huko.
- Je wewe ni Mkatoliki au Mprotestanti?
- Samahani, sitojibu swali lako.
- Ni swali tu.
- Nitakuja kumtembelea Joji wakati mwingine, kwa sasa nitaomba ruhusa.
- Atafurahi sana Joji kwa ziara yako kesho, hivyo usichelewe.
- Nitajaribu kesho au kesho kutwa, nitawasiliana nae kesho ili nijue hali yake, kwa heri

Athari ya sindano iliyomlaza ilianza kupungua kidogo kidogo….Joji akaanza kuwahisi waliomzunguka, ila alikuwa anahisi mzito sana, na alikuwa anaanza kufungua macho yake. Alipokuwa katika hali hiyo alikuwa amekwisha sikia yaliyokuwa yakipita baina ya Katarina na Kakhi na Adam, baadhi ya mazungumzo yalikuwa wazi kwake na mengine yalikuwa yamechanganyika hakuyafahamu vizuri. Baada ya kuondoka Adam alijihimu kufungua macho yake na alikuwa ameanza kujisikia vizuri, hata hivyo aliamua kuyafunga macho tena baada ya kusikia sauti ya mtu aliyekuwa akija chumbani. Alipotoa salamu Joji alimfahamu kutokana na sauti yake, alikuwa ni daktari Tom.

- Vipi hali ya mwanafalsafa wetu?
- Hallo Tom, Kwa bahati mbaya amejiwa na homa ya ghafla; wamempa sindano ya kutuliza, hajazindukana bado.
- Namtakia siha njema, Joji ni mfano wa nadra, pamoja na kuwa nagombana nae sana, ila ni kuwa mimi nafaidika nae sana kuliko anavyofaidika nami.
- Wewe ni mwema, amepata nafuu sana tokea alipoanza kuja kwako.
- Bali mimi ndie ambae nimekuwa mzuri sasa, huenda wewe na Joji hamnifahamu vizuri, mimi nilikutwa ni daktari mchezaji, hamu yangu kubwa ni wanawake na starehe. Na wala sijui kwa nini falsafa za Joji na kusoma kwangu kuhusu dini mbali mbali kwa muda huu, kadhalika ziara yangu kanisani pamoja nawe imebadilisha sana maisha yangu? Naomba sana samahani kwa busu nililokupiga, niamini sikuwa na kusudia wala sikuwa najua ninalofanya?
- Maudhui yenyewe yamekwisha kabisa, huenda kosa kubwa likawa kwangu; nilikuwa nimekunywa sana siku ile.
- Kwa hali yoyote ile sisi tunapenda tufanyie falsafa maneno yetu, makosa yetu yakuwa sio hatujui au ya kuwa sisi tumelazimishwa au sio hiyari yetu, achana na hayo, hebu niambie, daktari anasemaje kuhusu hali ya Joji?
- Mambo hayako wazi kabisa, lakini natamani yawe wazi kwa timu ya madaktari baada ya siku mbili zijazo.
- Atakuwa katika hali nzuri, na Mungu atamlinda.

Joji alijifanya kama ni mzito wa kufungua macho yake, kana kwamba ndio kwanza anaamka….akiwa anauliza kinachoendelea….

- Joji mpenzi wangu umeamka.
- Tokea muda gani niko hivi?
- Tokea muda wa masaa matatu, na nesi ameniambia kuwa umepiga sindano kabla

www.path-2-happiness.com

ya kuja kwangu kwa muda mfupi, tunamshukuru Mungu kwa hali yako..kisha akamgeukia Tom na kusema: daktari wako amekuja kukujulia hali.

- Hali yako Joji?
- Nzuri, vipi hali daktari wangu?
- Hali nzuri nilimuuliza Katarina kuhusu siha yako, na akanipa tumaini, sitaki kukuchosha, nitakuja wakati mwingine kukutembelea.
- Nipo hospitalini, lini kikao chetu kijacho?
- Muda utakaotaka, na itakuwa hapa chumbani.
- Vizuri, hivyo itakuwa hivi karibuni.
- Kama utakuwa na muda hospitalini basi tumia muda huo kujisomea kuhusiana na dini mbali mbali za mbinguni, ili kikao chetu kiwe na manufaa zaidi.
- Vizuri, tumekubaliana.

Katarina alitabasamu akiwa ameshika moja ya vitabu vilivyokuwepo pembeni ya Joji, kisha akasema:

- Alishaanza hilo tokea jana.
- Vizuri sana Joji.
- Nitajaribu muda mrefu niwe hapa kwenye mjadala –kisha alimgeukia Katarina na kutabasamu na kusema: Katarina hapendi mjadala na anakasirika upesi.

Katarina alibadilika na kuwa mwekundu.

- Ninawaahidi ya kuwa sitofunga mjadala huu.
- Ha ha ha, vizuri, nitakuja kukutembelea zaidi ya mara moja, nikipata wasaa; ili nijadiliane nawe, nakutakia ponyo la haraka, na mimi naomba ruhusa.

Alipoondoka Tom, Katarina alimgeukia Tom huku akitabasamu.

- Samahani mpenzi kukata mjadala wenu, lakini nisaidie nisifanye hivyo.
- Nilikuwa natania.
- Hata hivyo unayo haki katika hilo… nilitaka kukuuliza; huyu mwendawazimu anayejiita Kakhi, mkuu wako wa kazi ni nani?
- Kafanya nini Kakhi?
- Alifika hapa leo, alifanya mambo ya kipumbavu na ukosefu wa adabu, na kama sio kujizuia kwa ajili yako ningemfukuza.
- Kunijali! ungemfukuza tu hata hivyo kafanya nini?
- Macho yake, jinsi anavyoangalia watu ni upumbavu mtupu, muamala wake na watu ni wa hovyo, fikiria alikuwa anamdharau Adam, eti kwa sababu ni mhudumu tu, na yeye Kakhi ni mkuu wa shirika! Na anazungumza na nasi vibaya!

- Je Adam alifika?
- Ndio, lakini Kakhi hakumtendea vizuri hata kidogo, hata hivyo Adam alikuwa ni mwenye adabu.
- Adam ni mtu tofauti kabisa na alivyo Kakhi.
- Pamoja na kuwa umri wake sio mkubwa na kazi anayofanya ni ya kawaida tu, huzungumza kwa hekima ya watu wazima na wanafalsafa.
- Kama ni hivyo nilisema kweli nilipokuambia kuhusu Adam?
- Umesema kweli katika kila ulichoniambia na hata kile ambacho hukuniambia, mimi nakupenda Joji, Kakhi ameniambia kuwa wewe upo kinyume nae kabisa kuhusu wanawake, nami najua ujinga wake na heshima yako.
- Na Omela mwenye kufitini wanaume na Levi mzuri?
- Mimi nakuamini sana mpenzi wangu, niamini mimi ni mwenye imani na tabia zako, je wewe unaniamini?
- Ndio.
- Pamoja na mkesha wangu na Tom?
- Tom alinijulisha kilichotokea baina yenu katika mkesha wa mwisho.
- Niamini sikujua ilitokea vipi?
- Aah, makosa yetu mengi hutokea na hatujui yametokea vipi? Mimi nakuamini kwa dini yako na tabia yako mpenzi wangu.
- Mimi nakupenda Joji.

Katarina aliangalia saa yake na kusema:

- Inapasa niondoke sasa hivi, nitakuja kesho.
- Nitakusubiri kesho, umeniahidi mjadala, na itakuwa nitakachojadiliana nawe ni yale yaliyokuja kwenye Injili: “Pombe na kilevi usinywe.”
- Tumekubaliana mpenzi nitakuwa muwazi kwako kuhusu hilo.
- Tumekubaliana.

(5)

Katarina aliondokaJoji alifumba macho yake; akijaribu kukumbuka alichokisikia mwanzoni pindi alipotaka kuamka, maneno ya Tom yalikuwa wazi zaidi kuliko ya mwingine yeyote yule, na alichokisema kuhusu kubadilika kwake na kufaidika na Joji. Habari hizi zilimstua, na akahisi ukweli wake.

Kadhalika alikumbuka kidogo katika maneno ya Kakhi na dharau yake kwa Adam, na akakumbuka utulivu wa Adam na muamala wake. Kisha

www.path-2-happiness.com

akatabasamu kwa ndani aliposikia Kakhi na bodi ya shirika likimsifu kwa kufanikisha mikataba kisha akajiuliza: Je anao ujasiri wa kutosha ili ajiuzulu kazi yake baada ya kutoka hospitalini, ili aachane na kuwa chombo kisichokuwa na maadili kinachotumiwa na Kakh, au mapenzi ya mali kwake na cheo kitaghilibu misimamo yake?

Katika hali hiyo ya kuogelea kwenye fikra, alisikia sauti ya nesi akizungumza nae:

- Hallo, vipi homa yako ikoje sasa?
- Hali yangu kwa sasa ni njema.
- Tulitaraji utazindukana kabla ya muda wako.
- Kweli … nimezinduka muda kidogo uliopita, hata hivyo nilijihisi kuchoka; nikaendelea kufumba macho.
- Hamna neno, joto lako kwa sasa ni zuri, haya naomba ruhusa kutoka.
- Asante, na nakuomba samahani kwa mgeni wangu kukukosea adabu, mke wangu ameniambia kilichotokea.
- Sikuwa mimi, ni mwenzangu, hata hivyo tumezoea hali hii na kuwepo na watu mfano wake, usijali hilo, na kushukuru kwa muamala wako mzuri….Jina langu ni Zinta, kama utanihitajia unaweza kuniita muda wowote nikuhudumie.
- Zinta jina lako ni geni kidogo!
- Asili yetu Austria na sio Uingereza.
- Namjua Mwaustria mwema kama wewe.
- Inashangaza, Waustria ni wachache Uingereza.
- Levi sio wa Uingereza, bali nimejuana nae Tel Aviv.
- Yahudi! Mayahudi wameharibu Ulaya, tumewatoa na kuwakabidhi Palestina na Yerusalem.
- Inaelekea una kasumba dhidi ya Mayahudi!
- Huenda ikawa hivyo, lakini wewe hukuishi sana na Mayahudi. Kwa ujumla ukinihitaji niite wakati wowote, chakula chako cha jioni kitaletwa sasa hivi; hukula chakula cha mchana na inabidi upumzike.
- Asante kwa wema wako.
- Asante bwana Joji.

Asubuhi ya siku iliyofuata Joji aliamka mapema akiwa mchangamfu jambo alilokuwa akilikosa siku za hivi karibuni, kiasi cha kutamani ikiwezekana aondoke hospitalini, kwani alikwisha choshwa na kukaa pale. staftahi yake

ilikuja mapema, alikula kisha akaamua kujishughulisha na kusoma kwa bidii akitaraji kuja kwa daktari, ambapo atalinganisha baina ya Uyahudi na Ukristo na atasoma hali ya mwanamke katika Ukristo huku akilinganisha hilo katika Uyahudi. Yote haya anaweza kujadiliana na Katarina na kuandikiana kuhusu maudhui haya na Habib pamoja na Levi.

Daktari aliingia na kutoa salamu, kisha Joji akaanza kumuuliza:

- Je kuna mpya kuhusu vipimo?
- Hapana, baadhi yametoka na mengine tunasubiria, hata hivyo usijali na kuhofia.
- Sihofii kamwe, ni swali tu nauliza, na vipi hivyo vilivyotoka?
- Tunasubiria hivyo vingine kabla hatujahukumu, sitaki kukusumbua, lakini huenda ukahitajia operesheni.
- Operesheni?.
- Nimekuambia usihofie, ponyo itabakia katika mikono ya Mungu na sio mikononi mwetu bali sisi ni sababu tu.
- Niamini sihofu kabisa, lakini nashangazwa na hali yangu kufikia kiwango hiki!
- Najua hilo, nesi ameniambia kuwa muda wote unashughulika na kusoma na kufanya mjadala, na hakuwahi kukuona ukiwa na huzuni, hili ni zuri sana… sisi tunasubiria matokeo kesho au kesho kutwa.
- Tusubiri matokeo, na mimi ninaamini yatakuwa ni ya kheri tu.
- Vizuri, je unaweza kunielezea kwanini una imani kubwa sana hivyo?
- Bila ya shaka Mungu anatuhurumia zaidi kuliko tunavyojihurumia.
- Kama ni hivyo, basi wewe ni mtu wa dini, watu wenye dini kwa ujumla ni wenye uwezo wa kupata raha zaidi na furaha; na wenye kututaabisha ni wenye maradhi ya kukana Mungu ambao wanadhani kuwa dunia ndio kila kitu kwenye maisha yao.
- Samahani, sikukusudia ninachokisema, nilichokusudia ni kuwa Mungu anatuhurumia sana duniani, pamoja ya kuwa nilichokisema kina maana ya kina zaidi, nayo ni kwamba waamini wana maisha mengine akhera, lakini hili ni maalumu kwa wafuasi wa dini za mbinguni tu.
- Inaelekea wewe ni mwanafalsafa, nami nina kazi…lakini niambiwe kwa ufupi: Kwa nini hilo haliwezi mwenye kufuata dini ya Ubudha au Uhindu?
- Kwa sababu hawaamini kama kuna maisha yajayo bali wanaamini kuwa roho zao zinahamia kwa wengine.
- Ha haha hizi ni itikadi za watu wa kale, pamoja na utamu wa mazungumzo lakini

www.path-2-happiness.com

nalazimika kuondoka, kila la kheri.

Joji alizama kusoma na kufanya uchambuzi, hakukatishwa na chochote isipokuwa simu kutoka kwa Adam akitaka kujua hali yake.

- Hallo vipi Adam, Katarina alinijulisha kuhusu ziara yako, asante sana.
- Je kuna chochote naweza kukusaidia ewe rafiki yangu?
- Neno zuri 'rafiki yangu', nimefurahishwa sana nawe ningekuwa nahitaji kitu ningekwambia …. Samahani nimekumbuka kitu nakitaka kutoka kwako.
- Karibu, kwani wewe unanifurahisha na kunihisi kuwa sisi ni marafiki.
- Ombi langu ni kuwa tuonane, nina mijadala mingi nataka kutoa kwako.
- Nitakuja kesho, sio leo, samahani kwa hilo, leo tuna kazi kubwa mgahawani; kuna mfanyakazi mmoja hayupo.
- Vizuri…hamna neno, tutaonana kesho.

Katarina alifika pindi Joji alipomaliza mazungumzo, aliingia chumbani akiwa na tabasamu kubwa.

- Mpenzi wangu ameamkaje leo?
- Nzuri, katika hali njema, vipi hali yako?
- Namshukuru Bwana Mungu kwa neema zake.
- Ni neema gani ya Bwana uliyopata?
- Neema ya kuwa muamini mwenye dini na nikishughulishwa Kanisani… na …. na neema ya kuwa wewe ni mume wangu.
- Hivyo basi kuwa na dini kwa muono wako ni neema?!
- Je kuna shaka kuhusu hilo? sio mbaya kuliko mtu kutokuwa na bwana ambaye utatulizana kwake.
- Vipi kuhusu mkanaji Mungu kwa muono wako?
- Ukweli na bila kuficha…rai yangu ni kuwa ukanaji Mungu ni maradhi kabla ya kuwa ni dini ya mtu. Ni maradhi ya nafsi na roho, ni maradhi ya akili na mantiki, na ni maradhi ya ulimwengu na viumbe vyake.
- Nakubaliana nawe kabisa, lakini kuna neema gani kama mumeo ni mgonjwa?
- Nakusudia wewe mume wangu, na sikusema neema ya kuwa wewe ni mgonjwa.
- Kuna neema gani katika hilo?
- Kuna wanaume ambao hawawathamini wanawake wala kuwapa hadhi zao bali wanawadharau, sio wanaume waaminifu kama ulivyo mume wangu.
- Je haikuwa kumdharau mwanamke inakwenda sambamba na dini ya mtu?!

- Kwa vipi?
- Kila muda ambao dini inaongezeka ndipo dharau kwa mwanamke inapoongezeka.
- Kwa mara nyingine, ni nani aliyekuambia hivyo?
- Ni mafundisho ya Kiyahudi yanamuelezea mwanamke kwa sifa chafu mbali mbali.
- Wewe unasema kuhusu Uyahudi; kwa nini basi unaeneza maneno hayo kwa Ukristo pia?
- Je si kwamba Paulo amesema katika waraka wake wa kwanza kwenda kwa Wakorintho: "Na wanawake wanyamaze katika makanisa, hawaruhusiwi kuzungumza, bali wawe wanyenyekevu."
- Leo unaelekea kuwa ni mwanazuoni mkubwa wa itikadi za dini na mambo ya kimungu.
- Kwani sijakwambia kuwa nitatumia muda huu kusoma tu kuhusu Ukristo muda wote nilipo hapa hospitalini, hata Tom alilisema hili nawe ukiwepo.
- Vizuri… hili litakuzidishia uamini wako….na linaweza likakubadilisha kutoka Uprotestanti kwenda Ukatoliki…
- Huenda ikawa hivyo, hata hivyo turejee kwenye maudhui yetu, je si ukweli kuwa hali ya mwanamke kwenye Ukristo ni mbaya kama ilivyo kwenye Uyahudi?
- Nimekuahidi kuwa mkweli, na nitaendelea kwenye mijadala, nitaendelea pamoja na kuchukizwa nayo.
- Sipendi uendelee kwa unachokichukia, naamini kwamba mimi nitakusamehe na mjadala.
- Hapana, nitaendelea, na mimi naona kuwa kama unavyohitajia kujisalimisha kwa bwana, na mimi nahitaji kutumia akili na kufikiri.
- Nakubaliana nawe, hakuna imani bila kujisalimisha kwa bwana, lakini bwana muadilifu hawezi kutukalifisha kwa mambo yenye kugongana au kwa yale ambayo hayaingii kwenye akili zetu.
- Vipi?
- Je dini inaweza kuja na kitu ambacho hakiingii akilini?
- Mfano wa nini?
- Mfano wa kuwa bwana ni dhaifu, au yakuwa anawahitajia waja wake, au huuliwa na waja wake, atakuaje huyu Mungu?!,
- Pamoja na hatari ya maelezo yako lakini ni hoja tulivu.

www.path-2-happiness.com

- Unakusudia nini?
- Hii sio maudhui yetu, maudhui yetu ni mwanamke katika Ukristo au sivyo?
- Haswa….ndio.
- Ukweli ni kiasi gani nimetamani kama ningekuwa mwanamume, mwanamke katika Ukristo nafasi yake ni duni kuliko mwanamme.
- Ooh, mfano wa Uyahudi?
- Huenda ikawa hivyo, kwa uchache. Torati na Talmudi zimeharibiwa kuna mafundisho yenye upogo ndani yake na yamejaa mawazo ya kijinsia yasiyovumilika…. Ama Injili mwanamke ni duni kuliko mwanamme, na kuna mambo mabaya kuhusu mwanamke lakini hayafikii yale yaliyopo kwenye Uyahudi.
- Nimeona ombwe katika maandiko hayo katika Agano la Kale.
- Mfano wa nini?
- Mwanamke anarithiwa kama kilivyo chombo.
- "Watakapokaa ndugu pamoja na mmoja wao akafa, na hakuwa na mtoto, mke wa aliyekufa hafai kwa mtu wa nje, bali ni kwa ndugu wa mumewe na ana haki ya kumuingilia, na kumfanya mke wake. Atafanya yote yanayomwajibikia ndugu wa mume." Na mwanamke harithi "Wamezungumza (wana wa Israel) wakisema: Mtu atakayekufa akiwa hana mtoto wa kiume basi miliki yake ihamishiwe kwa binti yake." Na kuhusu mwanamke mwenye hedhi: "Kila mmoja wao ni najisi, afue nguo zake na akoge maji, na ataendelea kuwa najisi hadi jioni." Inatosha au niendelee?
- Tosha tosha… ukweli ni kuwa Ukristu umemkomboa mwanamke katika mengi ambayo yalikuwa katika Uyahudi pamoja na kuwa hedhi yake kwetu ni mbaya vile vile, lakini sisi ni bora kuliko kwenye Uyahudi.
- Kwa vipi?
- Imempa mwanamke haki zake; kwa mfano Uyahudi, katika zama za Masihi walikuwa wakitoa talaka kwa sababu za kipuuzi, hata kama mwanamke ataharibu chakula. Masiya alipokuja akanadi kuwa talaka haitolewi ila kwa tatizo la zinaa, na hivyo kumkomboa na utawala wa mwanamme ambae atamtaliki kwa sababu yoyote ile na wakati wowote ule, na hivyo kumsalimisha na kuchezewa.
- Vizuri… Je unaweza kukamilisha kwa mfano mwingine.
- Kwa hakika kitabu kitukufu kimejaa maandiko kama niliyotaja; ila vile vile kimejaa maandiko mengine yanayotoa dalili ya kumtukuza mwanamke.

- Ni maandiko gani hayo yaliyokuja kutoka kwa Mungu? Kwani haiwezekani maandiko yakapingana na hapo hapo yakawa ni sahihi?
- Umeyaingilia maudhui makubwa, nami nimechoshwa na mjadala mrefu, niamini sikimbii mjadala.
- Ni maudhui gani hayo magumu tuyazungumze wakati mwingine?
- Ni maandiko gani ni ya Mungu na yapi ya watu?
- Tufunge mjadala kwa sasa, tutajadiliana wakati mwingine.
- Je utanielezea kuhusu kanisa la Kiyama sasa?
- Kama utakavyo, nimekwenda kanisani kama nilivyokuahidi, nilikwenda siku ya Ijumaa, na kulikuwa na msongamano mkubwa njiani.

Alikatishwa na Baraad aliyekuja kumtembelea Joji.

- Hallo Joji … hallo Katarina.
- Karibu!
- Nimejua kuhusu ugonjwa wako, na nimekuja kukutembelea, huenda ukanihitajia:
- Asante.

Baraad alimgeukia Katarina akiwa na tabasamu bandia na kusema:

- Ooh Katarina yupo hapa, nilidhani upo na Tom.
- Unakusudia nini?
- Hamna kitu, usikasirike bibie.

Joji alikaa vizuri, na kusema:

- Sidhani kama hii ni kazi yako.
- Huenda ikawa, lakini mara nyingi Tom ana mzungumzia Katarina na uzuri wake, na hivyo nilitarajia atakuwa nae.

Joji katika hali ya ghadhabu.

- Wewe ni muongo, na huna adabu.
- Tom aliniambia vile vile kuwa wewe unataka kwenda Tora bora, je ananiongopea na hili vile vile?

Macho yalimtoka Katarina kwa mshangao: Tora bora!?!

- Usinifanye nikatoka kwenye tabia yangu ya kawaida, asante kwa ziara yako Baraad, naomba uondoke upesi, nataka kupumzika.
- Nitaondoka lakini ole wenu Tom asiwachezee kwa maneno yake matamu, yeye ni mtaalamu wa kuwachezea watu kwa maneno yake. Mnaweza kuwauliza wanawake aliokwisha wachezea. Ama wewe Joji kama nilivyokujulisha nina dawa ya matatizo yako, nasubiri simu yako, kwa heri.

www.path-2-happiness.com

Alipoondoka tu Baraad… Katarina alijiangusha kwenye kiti, huku akiwa amevimba kwa hasira.

- Nimemchukia sana mtu huyu.
- Nami namchukia vile vile, asie na maadili wala utu.
- Lakini alikuwa anakusudia nini?
- Katika jambo gani?
- Je ni kweli unataka kwenda Tora bora?
- Ha ha ha, je unajua Tora bora?
- Ndio, milima ya magaidi huko Pakistan na Afghanistan, cha msingi kuna nini?
- Kuna jambo si la kawaida limetokea, Tom alikuwa akinijulisha kuhusu dini mbali mbali na kuhusu Uislamu, kisha akaniambia huku akinitania: Ukisilimu utakwenda Tora bora, na cha kushtusha pindi tu nilipotoka ofisini kwake nilikutana na Baraad naye akaniambia: Je utakwenda Tora bora!?
- Yeye na Tom ni waongo wanayoyasema kuhusu mimi usiwaamini.
- Najua uongo wa Baraad, ama Tom amenijulisha kuhusu busu, na kuniambia kuwa hajakusudia lolote, na sijui kwa nini nimemuamini?
- Kwa bahati mbaya maneno ya Tom ni sahihi, hili limetokea na wa kulaumiwa ni mimi, kama nisingekuwa nimelewa asingethubutu kufanya alichofanya.
- Huenda sikufahamu alichofanya Tom, kwani jambo lilitokea bila utambuzi wake, lakini nashangazwa na kudumu kwako kunywa pombe!
- Ukweli: ni…….
- Kisha nashangazwa na maneno uliyomwambia mtoto wetu Maiko kuhusu pombe: "Pombe na kilevi usinywe."
- Mtu anaweza kucheza na mantiki ya makosa yake anayoyafanya, lakini nitakuwa mkweli nawe na nafasi yangu.
- Samahani kukukatisha, unakusudia nini kucheza na falsafa ya mantiki ya makosa:
- Mafundisho mengi ya dini tusiyoyafahamu, na mengi katika mafundisho hayo ambayo tunayafahamu, tunakwenda kinyume nayo. Tatizo ni kuwa sisi hatukubali makosa yetu, na hivyo basi kuibua tafsiri ya kimantiki au ya kifalsafa au hata ya kidini ili tusionekane kama tunakosea. Mfano mzuri wa hilo ni Pombe katika Ukristo.
- Je unaweza kunibainishia vizuri?
- Kimsingi pombe imeharamishwa katika Agano la Kale na Agano Jipya. Katika Agano la Kale: "Hafai kwa mamluki kunywa pombe wala wakubwa kulewa;

wasije wakanywa na kusahau majukumu yao na kubadilisha hoja ya kila mwana madhila." Katika Agano Jipya: "Msinywe pombe ambayo, ni kivutio cha uovu bali jazeni kwa roho."

- Vizuri, hiyo basi ni haramu, kwa msingi huu uharamu wenyewe wa wote au vipi?
- Usinikebehi, nitakuwa mkweli kwako, maandiko yamekuja kuwa manabii wamekunywa vile vile pombe, sisi kanisani tunakunywa na tunaifanyia falsafa ya kuwa masiya Yesu alisema kuhusu nafsi yake katika Injili akimfundisha Yohana: "Mimi ni mzabibu wa kweli." Na akasema kuhusu wafuasi wake: "Nyinyi ni matawi." Kama ilivyo juisi ya mzabibu kwenda kwenye matawi yake ili kuzilisha. Hivi ndivyo Bwana wetu Masiya alivyochukulia juisi ya mzabibu akaashiria damu yake tukufu ambayo tunainywa, na hivyo basi ikaingia kwenye mishipa yetu ili kuitukuza damu yetu na kiini cha miili yetu kwa ndani. Bwana Masiya hakutupa juisi ya mazabibu tupate utamu wake tu na kulewa; bali ametupatia kwa lengo tukufu lenye kutoharisha, haijui isipokuwa waamini tu.
- Ooh, falsafa iliyobuniwa.
- Usinikebehi, vinginevyo sitokamilisha.
- Ha ha ha, vizuri vizuri, kwa hivyo basi unywaji pombe umetukuzwa!
- Unaona jinsi tunavyotumia falsafa na mantiki na hatutaki iwe ni dini kwetu?
- Hili linakubalika katika dini zilizotungwa na wanadamu, wanaandika wanavyotaka, lakini halikubaliki kwa dini kutoka mbinguni, dini kutoka kwa Bwana Mungu.
- Aah, usipate shida na mjadala, mimi nalazimika kwenda nyumbani ili kuwapokea Maiko na Sali, na nitajaribu kurudi baadae…wakati huo tutamalizia mjadala wetu, lakini nihurumie kidogo kwenye mjadala, kwani ndani ya nafsi yangu naungulika na hivyo kunichosha, haswa zaidi kama kuna migongano ya ndani ya nafsi zetu kabla ya kuwa kwenye dini zetu.
- Nitakusubiri mpenzi wangu, na nakuomba msamaha kama nimekukera, hata hivyo sipendi ujikalifishe, na kama hutoweza kuja leo hamna neno….

Katarina alimbusu Joji kwenye paji lake la uso na kwenye mashavu yake, kisha akaondoka… alikuwa mwenye furaha sana na mazungumzo yaliyokwisha fanyika. Kwa mara ya kwanza aliamini kuwa ameweza kujieleza na hivyo basi akili yake kuishinda nafsi yake. Kadhalika Joji alikuwa katika furaha kuu, kwani aliweza kugundua uwezo wa juu usio wa kawaida wa Katarina wa kifalsafa na kimantiki na wa kielimu, uwezo ambao umejificha katika

www.path-2-happiness.com

kujisalimisha tu kwa imani yake Joji alijilaza akirejea mjadala ule kwenye nafsi yake. Ulikuwa mjadala wa kina, kisha akatabasamu alipokumbuka pindi pale Katarina alipoweza kumalizana na lile swali: Kwa nini tunakunywa pombe kwa njia ya ubunifu kabisa, na hakufedheheka kwa tendo lake.

MATARAJIO MEMA

www.path-2-happiness.com

10

MATARAJIO MEMA

MATARAJIO MEMA

(1)

Joji alijiunga katika kundi la wanaosoma kuhusu Ukristo, alichokiangalia zaidi kwa kina ni usahihi wa Agano Jipya na la Kale na vilivyoongezwa juu yao. Alihisi kuwa alikuwa akiogopa kuangalia maudhui haya kwa sababu yalikuwa ni nyeti. Hata hivyo hapana budi kuyaangalia kwa kina; ili ahakikishe usahihi wa kitabu chake kitukufu. Ni jambo gumu kitabu kitukufu kitiliwe mashaka na sisi kudumu katika hali hiyo. Joji aliendelea kusoma hadi muda wa chakula cha mchana kilipowadia akiwa anasoma….nesi alimpitia akampima joto lake, akiwa ameshughulishwa na kusoma, nesi alimwambia:

- Kana kwamba wewe ni mwanafunzi unaengojea mitihani?
- Ha ha ha, ndio mimi ni mwanafunzi wa shule ya maisha, na mitihani yangu ima nifaulu; ili niwe mwenye furaha, au nifeli; ili niwe mwenye huzuni.
- Unaelekea ni mwanafalsafa!
- La msingi ni kupasi mitihani.
- Kupasi mitihani ya maisha ni ngumu, watu wengi kwa bahati mbaya wanafeli.
- Kwanini?
- Kwa sababu wenyewe wanataka kufeli, wala hawataki kufaulu.
- Ima wewe unafanya falsafa au unakwenda kinyume na ukweli wa mambo kwa njia ya ajabu.
- Bali ni kweli nafanya falsafa, je utaniruhusu niondoke kwani nina kazi.

Joji alitabasamu kwa mshangao akishangazwa na mazungumzo yake mwenyewe, jinsi gani alivyojirusha kwenye falsafa ya kina kabisa, kisha akamaliza mazungumzo yake na kuondoka upesi….”Nini maana ya watu wengi kupenda kuanguka kwenye mitihani yao maishani” Je inaingia akilini?! Kwa hali yoyote ile yupo nae hospitalini, na atamuulizia hilo muda atakapoonana naye.

Tom aliingia chumbani kwa Joji akiwa amezama kusoma. Joji hakutanabahi kuingia kwake, hadi aliposimama pembeni yake na kumgusa mabegani huku akitabasamu……

- Lazima utakuwa umeufahamu Ukristo pamoja na madhehebu yake mbali mbali.
- Tom –Karibu sana.

www.path-2-happiness.com

- Vipi hali yako leo hii?
- Vizuri, kama unavyoniona, sikutarajia kama utafika leo.
- Nimechagua muda ambao hakuna anayeweza kudhania kama nitakuja kwako na Katarina hayupo.
- Kwa nini?
- Nahisi kuwa nimekosea kumbusu, na sijui kwa nini nilifanya vile, na nahisi kuwa hutopendezwa nikimbusu, kama ambavyo hutoniamini ninayokuambia, una haki zote kufikiri hivyo.

Joji alitabasamu na kusema:

- Hilo jambo ni dogo, lakini kwa nini umemwambia Baraad kuwa unampenda Katarina na kuwa unambusu kila mara, na una starehe naye?
- Mimi nimesema hivyo?
- Haya ndiyo anayosema mkuu wa ofisi yako "Baraad" alipokuja kunitembelea leo hii.
- Hukuniamini hapo zamani vipi utaweza kuniamini leo hii? Yeye ni muongo kabisa na mwenye kutia aibu.
- Unayemzungumzia ni mkuu wa ofisi yako, na siku ile asubuhi aliniambia akiwemo Katarina, je hukumwambia vile vile kuwa nitakwenda Tora bora? Je alibuni kuwa tulizungumza mambo haya?
- Ah ah, nitalazimika sasa kukueleza baadhi ya mambo ambayo sikutaka kufanya hivyo.
- Haya niambie.
- Nilikuwa najua kuwa Baraad ambae ni mkuu wa ofisi yangu ni sekretari mbaya na asiyekuwa na maadili mazuri, lakini nilimnyamazia kwa sababu alikuwa akinisaidia pindi nilipokuwa nacheza na wanawake hapo kabla. Niamini kuwa tokea uanze kunitembelea hospitalini nimeanza kubadilika na sijui kwa nini? Na tokea hapo nikawa makini kusoma, kutafiti, na kujadiliana katika mambo ya dini na yanayoleta furaha. Hili halikumpendeza Baraad na mara nyingi aliniambia hivyo, bali alinitishia na picha za baadhi ya wagonjwa wangu wa zamani alizokuwa nazo…kisha baada ya muda nikagundua kuwa ameweka kamera akinichunguza na kuchukua sauti ndani ya ofisi yangu. Hivyo basi kwa njia hii anapiga picha na kunasa sauti na pia mawasiliano yangu yote yanayoendelea katika Kliniki. Yote haya nimeyafahamu siku tatu tu zilizopita na ilitokea purukushani nguo kuchanika katika maudhui haya na nikamtishia kumfukuza, nae akanitishia kusambaza

picha zangu, na yote aliyorikodi ambayo yapo katika website moja kwa moja, na hii maana yake ni kufutiwa leseni yangu kama daktari. Na sijui cha kufanya kwa sasa. Je utaamini niliyokuambia sasa? Kama hutoamini unasamehewa kwa hilo.

- Pamoja na kuwa inaonekana kuwa ni kisa cha kufikirika lakini kwa kiasi kikubwa nina ushahidi wa kuyaamini.
- Ushahidi gani?
- Mara ya mwisho nilipokuja kwako nilipotoka tu Baraad alinikabili, na kuniambia kuhusu Tora bora, na mimi nina hakika kuwa hukuondoka ofisini kwako muda ule na yeye hakuingia kwako.
- Kwa nini hukuniambia?
- Nilishangazwa sana na hali hiyo nikajisemesha: Huenda ulikuwa ni mpango wenu wa pamoja au jambo mnaloliita telepathia.(1)
- Niamini nilishakuambia ukweli kamili, maamuzi ni yako.

Nesi aligonga mlango na kuingia upesi…

- Samahani kuwakatisha, daktari anataka kuongea nawe haraka, anakuja sasa hivi.
- Aingie, kuna jambo gani?

Daktari akaingia….

- Samahani Joji kwa ziara ya ghafla lakini jambo lenyewe ni la haraka.
- Ndio daktari.
- Vipimo vyote vilivyobakia matokeo yake yametoka muda si mrefu, na wewe unahitaji kufanyiwa operesheni haraka iwezekanavyo, kesho muda kama huu.
- Inaelekea jambo hili ni la hatari.
- Ukweli nalazimika kukuambia ndio, na ndio maana nimekuja wakati huu, unao muda wa kufikiria, na kusaini uthibitisho wa kuafiki kwako kabla ya saa sita mchana hapo kesho.
- Kufikiri na kusaini…na kuthibitisha!
- Inapasa nikuelezee kwa urefu na uwazi, virusi ambavyo vinapandisha joto lako tumevigundua kuwa vinaharibu sehemu ya ubongo wako kila muda ambapo joto lako linapopanda, na hilo linaweza kutokea tena kesho saa mbili usiku, na hiyo ina maana ya kuwa halitokujia hilo ila tutakapokuwa tumeanza operesheni, kufaulu kwa opresheni hii ni asilimia 60 tu kwa bahati mbaya.
- Na hiyo asilimia 40 iliyobakia?!
- Inaweza kutokea uharibifu katika baadhi za sehemu ya ubongo wako.

(1) Uwezo wa kupashana mawazo/fikra bila kutumia njia za hisia za kawaida.

www.path-2-happiness.com

- Hilo lina maana gani?
- Samahani siwezi kulitabiri hilo kwa sasa… inaweza isitokee chochote, na yanaweza kuingia mambo mengine.
- Kinachotakiwa sasa kwangu ni kuwafiki na kusaini uthibitisho wa hilo!
- Ndio.
- Kama sitoafiki itakuwaje?
- Itabidi usaini uthibitisho kuwa ulitakiwa kufanya hivyo ukakataa pamoja na kuwa kwa dhana yangu ni kuwa operesheni ni bora zaidi kwako, pamoja na kuwa kadhia hii ni nzito kwetu, je una swali lingine?
- Hapana, isipokuwa kama kutajitokeza habari mpya muhimu katika jambo hili.
- Hapana jingine, kwa ujumla sijazungumza nawe ila baada ya kuongea na timu ya madaktari na hii ndio rai yao wote, kama utakuwa na swali wakati mwingine, unaweza kumuuliza nesi, naye atawasiliana nami moja kwa moja ili nijibu swali lako lolote lile, na natarajia utapata muda wa kufikiria na kusaini uthibitisho kabla ya saa sita mchana.
- Nitafikiri na kushauri na kukujibu.
- Chukulia jambo hili kwa wepesi na hali ya kawaida bila ya khofu kama ulivyonizoesha; maisha, mauti na maradhi ni maumbo mbali mbali ya nafsi ya mwanadamu katika maisha yake ya kila siku, inapasa kuishi na hali hizo, nakuomba ruhusa nitakuja asubuhi saa tatu kukuona, na kama utakuwa na jambo la kuuliza kabla ya hapo mwambie nesi, anipigie.
- Asante.

Daktari aliondoka na Joji alipigwa na ukimya hadi alipokatwa na sauti ya Tom…

- Joji…maisha hayana maana kama mtu hatokuwa katika furaha, kama ambavyo mauti hayana maana kama hatutoamini ufufuo na hesabu, kitu cha ajabu falsafa ya mauti na uhai!
- Bali cha ajabu ni falsafa ya kuwepo kwetu! Kwa nini tumeumbwa? Na tunaelekea wapi!
- Kama ni hivyo unafikiria nini?!
- Nilikuwa nafikiria: Je mimi nataka maisha au mauti?
- Haihitaji kufikiri, hakuna asiyetaka maisha.
- Kwa nini basi kujinyonga? Je sio kweli kwamba idadi ya watu wanaotaka kujinyonga inaongezeka duniani kote? Nami siku moja si nilikuwa natamani

kujinyonga?

- Ajabu ya jambo hili kwako, mwenye kujinyonga anamaliza huzuni yake kwa huzuni, ama mtu mwenye furaha hahitaji kufanya hivyo kamwe.
- Nilipokwenda kutaka kujinyonga dunia yote ikawa dhiki kwangu juu ya upana wake, na nilikuwa katika huzuni kubwa mpaka nikawa nataka kuondosha huzuni yangu kwa huzuni kama ulivyosema.
- Kwani bado upo kwenye huzuni, ili ufikirie kama unahitaji mauti au uhai?
- Ukweli ni kuwa tokea nianze safari yangu ya njia ya furaha nami nahisi furaha na huwa naiambia nafsi yangu. Vipi nitakapofikia furaha itakuwaje?
- Kama ni hivyo shikamana na uhai ili upate furaha.
- Mimi nahitaji uhai, lakini swali ni kwamba: Je uhai unanihitajia? Nimemuona Maria akipigana akitaka maisha, lakini mauti yalimpiga mweleka…..
- Mtumainie Mungu atakusaidia.
- Ha ha ha inaelekea sasa wewe ni mwenye kujiamini, mwenye dini ewe Tom!
- Je si kukuambia kuwa nimebadilika? Niamini sikutarajia kubadilika, bali sijapanga kufanya hilo, na sijui kwa nini nimebadilika lakini ninakuambia ni kweli nimebadilika.
- Pamoja na hali niliyokuwa nayo, lakini nina swali: Je ulikuwa ni mwenye furaha zaidi hapo kabla au sasa?
- Naweza kujibu swali lako ulilonitumia kwenye barua pepe hapo kabla kuhusu starehe ya kiwiliwili na kiroho, nilikuwa ninafurahisha kiwiliwili changu kwa huzuni ya roho yangu, na hivyo basi kiwiliwili changu kinaumia hali kadhalika.
- Na sasa hivi?
- Sijafikia kwenye hiyo furaha bado, lakini siko katika ile hali ya huzuni kama ilivyokuwa kabla.
- Je ungekuwa katika nafasi yangu ungetamani mauti au uhai?
- Uhai bila ya shaka, kama ungeniuliza hapo kabla ningekuambia natamani mauti… huzuni ya mauti huisha kwa huzuni ya uhai.
- Nakumbuka pindi nilipokutana na kikongwe njiani nikienda kujinyonga, alikuwa ni mtu mwenye furaha sana, alikuwa akicheza na wajukuu zake, laiti ningechukua anuani yake.
- La muhimu kwa sasa, ni kusaini uthibitisho wa kukubali operesheni, madaktari wanajua zaidi kuliko sisi ila nakushauri umshauri Katarina kwanza.
- Na hii ndio rai yangu vile vile…pamoja na kuwa ni lazima kupanga mambo

www.path-2-happiness.com

yangu. Nafasi ya kufeli operesheni hii ni asilimia 40.

- Kuwa na matumaini rafiki yangu na haiwi ila unachokipenda, na si vibaya mmoja wetu akajitayarisha na chochote kinachoweza kutokea, utasimama kutoka kwenye maradhi yako na utafikia furaha hata hivyo usisahau kunichukua, nitakuacha ufikiri katika maudhui haya na nitakuja kesho kukujulia hali yako.

Joji alijilaza akitafakari maana ya mauti ambayo huenda yakamfika, mauti ambayo yalimfika Maria mwanae wa kike mbele ya macho yake. Mauti yana maana gani? Bali maisha yana maana gani? Je mauti ni raha au suluhiho la matatizo ya dunia? Au ni mwisho wa furaha duniani? Ikiwa jibu ni hilo la mwanzo basi bora mauti, na ikiwa ni hili la pili hii ina maana kuwa amekwisha fikia kwenye furaha na ameshaifahamu, alitabasamu kwa dhihaka akiwa anafikiria kwa njia hii, na akajisemesha: Inaelekea kuwa nitakufa huku nikiendelea na falsafa ambayo haitonifikisha popote.

Fikra zake zilikatwa na sauti ya simu ikilia, akiangalia ilikuwa ni Adam…

- Hallo.
- Ndio Joji nilipenda kujua maendeleo yako na vipi afya yako?
- Nipo baina ya uhai na umauti, sijui katika hayo iliyo karibu na mimi?
- Sijakufahamu bado, kwani vipi?
- Asilimia 60 ya maisha na 40 ya mauti au kilema.
- Sijafahamu kitu, kama unatania mimi sipendi utani wa namna hii.
- Laiti ningekuwa nafanya utani, lakini huu ni ukweli… huenda kesho nikafanyiwa operesheni na uwezekano wa kufaulu ni asilimia 60.
- Tunamshukuru Mungu kwa hali zote.
- Kiasi gani natamani kukuona leo.
- Leo tena haiwezekani; muda wa kutembelea wagonjwa umekwisha, kwa nini hukuwasiliana nami mapema?
- Sijui, je unaweza kuja kunitembelea katika muda wa kutembelea wagonjwa kesho asubuhi?
- Bila ya shaka nitakuja, lau ningeweza kuja sasa hivi ningekuja, lakini nakuhakikishia kuwa umri wa watu upo katika mikono ya Mungu na sio katika mikono ya madaktari pamoja ya kuwa wao ndio sababu muhimu.
- Sijui; je nayaogopea mauti au nipo tofauti? ambacho ninakifahamu ni kuwa umauti ni ukweli ulio mpana ambao unarejea upya utaratibu wa maisha kwa ukamilifu.

- Usihofu, wala usitishike; Mungu hutuhurumia sisi zaidi kuliko hata nafsi zetu.
- Niamini sijui, ninaogopa au nina wasiwasi? Au nina nini? Ninachokihisi ni kuwa ni lazima niyapangilie maisha yangu kwa mara nyingine, unaona dharau yangu kwangu mwenyewe?
- Dharau gani?
- Ninapoogopea maisha nimeamua kuyapanga maisha yangu upya, je haikuwa vizuri kufanya hayo hapo kabla nilipokuwa nayapupia, na sio wakati huu tena ambapo nipo nje yake?
- Hata hapo kabla ulijitahidi kuyapanga, na kwa hali hiyo inabidi uyapange yaliyobakia, hata hivyo hayo yaliyobakia anayafahamu Mungu pekee….na mimi napenda matarajio mema na nachukizwa kabisa na tabia ya mtu kukosa rajua.
- Kwa hakika nipo katika kukanganyikiwa, je unatarajia kuwa nitakufa?
- Utaishi apendapo Mungu, na utabakia hadi upate furaha uitafutayo katika njia yake, na wakati huo ndipo utakapoona maana ya maisha haya ya duniani na ya baada ya mauti.
- Maelezo mazuri, “Maisha yetu baada ya mauti”, hili nitajadiliana nawe kesho, samahani ninalazimika kumpigia Katarina nimjulishe.
- Ndio…. Ni lazima ushauriane na mke wako, samahani kama nimrefusha mazungumzo, na kuaga kwa jina la Mungu, kwa heri.
- Ni kiasi gani nakushukuru Adam, nitakusubiri kesho, kwa heri.

Joji alimaliza mazungumzo yake na maneno ya Adam yakiendelea kugonga kichwa chake, alijikuta akikariri maneno yale bila kujijua: “Umri wetu upo katika mikono ya Mungu na si katika mikono ya madaktari. “Mungu anatuhurumia zaidi kuliko hata nafsi zetu. “Napenda matarajio mema na sipendi dege baya,” “Tunapokuwa wenye furaha, maisha yetu ya duniani na maisha yetu baada ya umauti yanapata maana….” Hakufahamu kwa nini maneno ya Adam ya kawaida lakini ya kina yanatingisha nafsi yake kila mara? Je siri ipo kwenye maneno yenyewe au kwenye ukweli wa Adam mwenyewe? Au ni kwa sababu amekanganyikiwa na hawezi kuitawala nafsi yake.

Joji alikatishwa na mtiririko wa fikra zake, ni lazima ampigie Katarina na kumjulisha ili apate ushauri wake.

- Hallo Katarina, nimekutamani sasa na nilikuwa nakusubiria leo hii.
- Nilikuwa nakuja kwako isipokuwa jambo dogo limenichelewesha.
- Salama lakini!

www.path-2-happiness.com

- Sali alikuwa na kazi za nyumbani alizopewa shuleni na akaomba msaada wangu.
- Uko wapi sasa?
- Nyumbani, kuna nini Joji?
- Nilikuwa nataka kukushauri katika jambo tu; daktari ameniambia kuwa naweza kufanyiwa operesheni kesho kama nitakubali.
- Kesho, haraka hivyo? Ni operesheni ya nini?
- Alichoniambia ni kuwa ni bora kufanya operesheni kesho saa mbili usiku.
- Mpenzi wangu, unasema nini? Ninakuja sasa hivi hospitalini.
- Nadhani ni bora uje kesho asubuhi.
- Ni operesheni ya nini?
- Operesheni ya kichwa.
- Kichwa!!! Je ni ya hatari?
- Huenda ikawa hivyo, cha msingi ni kuwa daktari ameniambia kuwa bora ifanyike pamoja nakuwa uwezekano wa kufanikiwa ni asilimia sitini tu, na nini rai yako?
- Sijui, nitasali kwa ajili yako usiku wote, na asubuhi nitakuja na Maiko na Sali.
- Nitakusubiri mpenzi wangu, kwa heri!

Katarina alijitupa kitandani pake na kulia kilio kikubwa hakuweza kuvumilia kufikiria kutoweka kwa Joji kutoka katika maisha yake…itakuwaje kama operesheni itafeli… itakuwaje kama atakuwa mlemavu…vipi na vipi……? Kisha akasimama akiomba na kumsalia Joji…..

Ama kwa upande wa Joji fikra zake zilihamia kwa Katarina na watoto wake, na sehemu kubwa ya fikra hizi zilikuwa kuhusu mali zake, alitabasamu huku akikumbuka kuwa amejadidisha bima yake ya maisha; kinachomaanisha kuwa fedha nyingi zitakwenda kwa Katarina na wanawe….Kama ilivyo katika mkataba wa shirika lake utampa fedha nyingi, haswa ya kuwa alipata maradhi akiwa katika safari ya kikazi na hilo anaweza kulithibitisha. Shaka yake ipo kama Kakhi atampa chochote atakapokufa, kwani Kakhi hafikiri chochote isipokuwa katika nafsi yake tu, katika hali hiyo ya fikra mbali mbali mara lepe la usingizi likamchukuwa.

(2)

Joji aliamka mapema, alipata kifungua kinywa huku akihisi kichwa kizito kwa fikra na mawimbi ya maswali, ambapo mwishoni alikubali afanyiwe operesheni, hata hivyo hofu ilimtawala….anatakiwa afanye nini kabla ya operesheni… Katarina na wanawe hakuwasahau katika mawazo yake….

Muda wa kutembelea wagonjwa ulipoanza asubuhi ile mara Adam akawa ameshaingia chumbani akiwa na tabasamu.

- Nipe habari nzuri, vipi afya yako?
- Nzuri...hakuna mpya, namsubiria daktari, nataraji atafika hivi punde, pamoja na kuwa bado sina kitu.
- Swadakta, si kwa uwezo wa daktari kufanya kitu, bali wanadamu wote hawawezi kufanya kitu.
- Hivyo ni nani mwenye uwezo wa amri yake kwa kila kitu?!!
- Mungu ndiye mwenye kumiliki kila kitu.
- Ni yupi mungu wako Adam?
- Mungu wangu ndio Mungu wako na walimwengu wote, achana na hili kwanza.
- Kama ni hivyo wewe ni Protestant?!
- Utakapofika kwenye furaha katika mradi wako wa furaha, nitakuwa pamoja nawe.
- Hili linategemea kama nitaishi baada ya operesheni.
- Kuwa ni mwenye matumaini mazuri …tarajia mema, ni kiasi gani nachukia mtu aliyekosa rajua.
- Dunia yote imesimama juu ya matarajio mabaya, kwa nini unakataa?
- Hapana dunia imesimamia matumaini mazuri, achana na ushirikina.
- Kweli….Je huna hisia mbaya na namba kumi na tatu?
- Hapana kabisa, sina. Mwenye kuongoza ulimwengu ni Mungu tu, kwa mnasaba huo huo ni kuwa Wachina wana hisia nzuri sana na namba kumi na tatu; Kwa sababu makato yake ya sauti yanafanana pamoja na maana ‘Lazima niishi’, hivyo jambo halifai kuwa ni la kishirikina juu ya ushirikina, na kuwa mbali na mfumo wa Mwenyezi Mungu.
- Kwa kuwa wewe ni Protestant usiwe na hisia mbaya na tarehe kumi na tatu (13), hata ikiwa itawafikiana na siku ya Ijumaa? Je hujui kuwa katika historia ya masiya, kikao chake cha mwisho cha siri kilimkutanisha na wanafunzi wake, kabla ya Yahudha hajamfanyia hiana na kutaja alipojificha, siku hiyo ilikuwa ni Ijumaa na idadi ya waliohudhuria ilikuwa ni watu kumi na tatu.

www.path2-happiness.com

- Siamini ushirikina, nimekuja kukujulia hali sio kujadiliana nawe kuhusu matumaini au kukosa rajua, na napenda rafiki yangu aishi daima akiwa na matarajio mema.
- Unatarajia vipi niwe na matumaini wakati uwezekano wa kufaulu operesheni ni asilimia sitini tu?!
- Mungu wetu ni mwenye huruma na mkarimu, nae katika mikono yake anamiliki kila kitu, madaktari ni sababu ya hayo tu, ukitarajia mema utakuwa ni mwenye furaha tele, na inawezekana ukaishi katika hali bora zaidi, na hata asilimia ya kufaulu operesheni ni nzuri. Ama ukitarajia mabaya hali yako itakuwa mbaya, na halitokufika na kukupata isipokuwa alichokuandikia Mungu mrahimu kwako, una nini Joji kwani hauko hivi?
- Nilitaka kukuambia hivi nione utasema nini, hata hivyo mimi nachukia ushirikina na udajali na najifunza kwako mapenzi ya kutaraji mema…lakini niambie: Itakuwaje mtu aliyekuwa na mfano wa hali yangu akataraji mema?

Katarina akiwa pamoja na Sali na Maiko walifika na kuingia chumbani kwa hamu sana na haraka hadi kitandani kwa Joji.

- Vipi Joji usijali, hali yako vipi sasa?
- Baba vipi hali yako, tunakuhofia!
- Baba una nini?

Hayo yalimuathiri Adam na kumfanya aondoke aiwachie familia fursa ya kukaa pamoja na baba yao kabla ya muda wa operesheni….

- Nitaomba ruhusa ya kuondoka, na samahani kwa usumbufu.
- Oh Adam, samahani sikutanabahi uwepo wako.
- Hapana, hapana usiondoke, nataka ubakie, labda kama una haraka.
- Sina haraka, lakini sipendi kuwakera.
- Hakuna usumbufu wowote ule, tutafurahi kuwepo kwako….

Joji aliwasogeza karibu Maiko na Sali na akawakalisha pembeni kitandani… nae akiwauliza kuhusu habari za shule na nyumbani….

- Hali zetu nzuri baba, lini utarudi nyumbani?
- Mama ametuambia utarudi baada ya siku tatu na baada ya hapo tutasafiri pamoja kwenda Roma.
- Nimeshanunua tiketi, safari yetu ni baada ya siku kumi.
- Umenunua tiketi?! Kwa nini? Sidhani kama hali yangu itaniruhusu.
- Usihofu, utakuwa katika hali nzuri.

- Nini rai yako Adam?
- Maamuzi yaliyobarikiwa, na yatakuwa kwa uwezo wa Mungu….na hili ndilo jibu la swali lako.
- Swali gani?
- Hukuwa unaniuliza: Unatarajia vipi mema katika hali kama hii?
- Kumuachia mambo yetu Mungu ambaye ni Mwenye huruma sana na mkarimu hutufanya tujihisi raha katika maisha yetu.
- Katarina akizuia machozi machoni mwake: Usiku mzima nilikuwa nalia na kusali kwa ajili yako, kisha nikaona kulia kwangu hakutonufaisha, lakini dua zangu ndizo zingeweza kukusaidia, na nimechelewa kidogo ili nithibitishe safari yetu leo asubuhi, unaonaje Joji?
- Ni mwenye furaha sana kwa ajili yako Katarina, sawa
- tumekubaliana….Sali mtoto mzuri niambie: Je umehamasika kwenda Roma?
- Sana baba, nataka kuona Trevi Fountain.
- Ni ipi hiyo chemchem ya Trevi?
- Ni chemchem kubwa, tulijifunza kwenye somo la Jiografia.
- Na mimi nataka kuona ngome ya Saint Angelo, ni ngome, iliyojengwa kwa majivu ya wafalme, ambayo baadae ikawa makumbusho, kama tulivyosoma katika somo la Jiografia.
- Ama mimi nataka kutembelea Cathedral ya Mtakatifu Patrick.
- Inaelekea mambo yote yamepangwa vizuri…nataraji yote yatafanikiwa.

Watoto wale wawili walipiga makelele kwa furaha, walimbusu baba yao…. Wakati huo Adam alikuwa amekaa pembeni chumbani, akiwapa fursa kuzungumzia mambo yao ya safari kwa hamasa na furaha…na mwisho Katarina akawaambia wanawe:

- Sasa hivi ni saa tatu, dereva yupo nje anawasubiri.
- Vizuri ….kwa heri baba!
- Kwa herini wapenzi wangu……

Joji alimgeukia Adam aliyekaa peke yake.

- Samahani Adam, je hukujihisi mwenye dhiki?
- Na kitu gani?
- Safari yetu ya Roma; Wewe ni Mprotestant na sio Mkatoliki.
- Hapana kabisa, bali nakuhimiza, ili upate kujua Ukristo kwa pande zote mbali mbali.

www.path-2-happiness.com

- Wewe ni mtu wa ajabu Adam.
- Muda ambao tutakuwa wakweli katika utafiti wetu kuhusu njia ya furaha, basi juhudi zetu zote na maarifa yoyote ya zaidi itatung'arishia zaidi nia yetu, inatupasa tulichunge hilo. Je sikukuhamasisha kwenda India na Jerusalem hapo kabla? Je, baada ya hapo kuna mpya gani?
- Kilichokuwa kipya ni kuwa sisi na Wakatoliki tuna vita vikubwa na kisasi… Je wewe Mprotestant hukuwaua miongoni mwao mamilioni katika vita vya miaka thelathini?
- Mauaji ya namna hii hayapendi yeyote, kisha ni nani aliyekuambia kuwa mimi ni Mprotestant? Huenda nikawa Mkatoliki? Utakaporudi kutoka safari yako nitakujulisha.
- Inaelekea wewe ni Mkatoliki, kuna nukta ambazo mnakutana na Katarina… Nitaujua Ukatoliki katika masomo yangu siku hizi na katika safari yangu, hata hivyo hisia yangu ya mwanzo ni kuwa Ukatoliki una Upagani mwingi, nami sipendi makanisa yake ambayo yamejaa masanamu na picha mbali mbali utadhani ni mahekalu ya wapagani.
- Na unapenda Uprotestant ambao unaua watu?!
- Hili ndilo ambalo linanithibitishia sasa kuwa wewe ni Mkatoliki.
- Haya sio makusudio yangu, katika utafiti wako katika njia ya furaha, tafuta haki popote iwapo na dhehebu lolote, na wakati huo utapata furaha, raha na tumaini.

Katarina alirejea chumbani baada ya kuwasindikiza wanae.

- Naomba msamaha kwa kuchelewa, Maiko na Sali walitaka niwachukulie Juisi na sandwitches kabla ya kwenda kwa dereva.
- Nakushukuru Katarina kwa mpangilio huu wa safari, nafsi yangu ilishaondosha hofu ya mauti yaliyokuwa yananinyemelea.
- Pindi roho ya mwanadamu inapopaa, na hakika zinapodhihirika mbele yake, na kujua kuwa mauti hayamkwepi, na yakuwa yanaweza kumfika muda wowote basi mtu huyu hawezi kuwa mtumwa wa matamanio ya maisha na starehe zake, na hayamuathiri mtu huyo yaliyomo duniani; kuathiri akili yake na hamu zake. Mtu anayejitambua na kutambua maana ya uwepo wake anaweza kwa kutumia matarajio yake kufahamu kwa wepesi kuwa anaishi ili afe, na ya kuwa anakufa ili aishi milele, baada ya hapo.
- Falsafa nzuri kabisa, tunaishi ili tufe, na tunakufa ili tuishi, lakini tatizo lipo kwenye maumivu ya umauti.

- Yesu alivumilia maumivu kwa ajili ya mwanadamu, maumivu ni kipengele cha msingi katika kumuokoa milele, na kuvumilia kwetu maumivu ni dalili kuwa tunampenda Masiya.
- Kama ni hivyo basi dunia ni ya nini?
- Faida ya kuwepo duniani ni kutumia muda wako katika kumtumikia Bwana na kumhudumia Bwana tu.
- Nini rai yako Adam?
- Katika nini?
- Ya kuwa maisha yetu yote yawe katika kumuhudumia Bwana na kutafuta radhi zake.
- Nakubaliana kabisa na hilo…isipokuwa kumhudumia Bwana sio katika sala peke yake.

Katarina kwa mshangao:

- Vizuri sana, mara nyingi tunasahau –kwa bahati mbaya hata mapadri –kuwa maisha yote ni ibada ambayo yanapasa kuwa kwa Mungu.

Joji kwa tabasamu la dhihaka.

- Swali linalobakia ambalo linakariri mara kwa mara ni nani anayemuabudu Mungu mwenye huruma haswa? Na ni nani anayemwabudu sanamu, na kuliita kuwa ni Mola wake? Mungu wake?

Adam kwa himizo:

- Huenda swali hili likawa ndilo swali la hatari zaidi katika historia.
- Joji unakusudia tofauti iliyopo baina yetu kuhusu Mungu.
- Unakusudia nini?
- Sisi Wakristo tunakubaliana kuwa Mungu yupo katika nafsi tatu, na wamekubalia kuwa ya kwanza katika hizi tatu ni Bwana, na ya pili ni Mwana, na ya tatu ni Roho Mtakatifu, na wote watatu ni Mungu mmoja……hata kama baada ya hapo tutatofautiana kuhusu tabia ya mwana na roho mtakatifu.
- Sijakusudia hilo wala haikuniingia akilini, na jaribu kufikiria hilo, ambalo sikufahamu ni kuwa vipi watatu watakuwa mmoja, na mmoja watatu, wapo sawa sawa katika kiini tofauti, katika sifa na katika tabia, na pamoja na hayo yote ni Miungu!
- Hili ni moja katika kadhia kubwa na nzito katika Ukristo, na shauri hili tulizungumzie huko Roma, ni maudhui magumu ambayo hatuwezi kuyazungumza sehemu kama hii.

www.path-2-happiness.com

- Hamna neno, pamoja na kuwa mimi hali kadhalika sifahamu ni jinsi gani Mungu ambaye maisha yetu yapo kwa ajili yake hatumjui vizuri bali ni vigumu kumfahamu. Wakati mwingine sioni tofauti baina yetu na wapagani!!
- Niamini, sikimbii mjadala, hili ni tatizo la kila Mkristo, vyovyote awavyo madhehebu yake, hivyo ni vizuri tuyajadili kwa kina tukiwa Roma.

Adam akitabasamu:

- Mimi nakubaliana na Katarina, haya ni maudhui ya hatari yenye utata, ni katika maudhui muhimu sana, wala haifai kuyajadili haraka haraka kwa njia hii, kwani mwenye akili hawezi kuendelea katika dini anayoiona mwenyewe kuwa ni ya kipagani, wala haiwezekani katika dini za mbinguni ikawa ni ya kipagani.
- Ha ha ha, na mimi vile vile nakubaliana nanyi Wakatoliki wawili, pamoja na kuwa ninaamini kuwa kila Mkristo anahisi upagani wakati mwingine.

Katarina kwa mshangao.

- Je wewe ni Mkatoliki ewe Adam?
- Wakati mwingine huniita Mkatoliki na wakati mwingine huniita Protestant.
- Ha ha ha, nimehakikisha sasa kuwa ni Mkatoliki…..

Daktari aliingia chumbani akimkuta Joji akicheka…… alikaribia kitandani mwa Joji na kusema:

- Nilikuwa nina hakika nitakukuta mwenye furaha kama hivi pamoja na niliyokuambia.
- Karibu, kwa nini ulikuwa na hakika kiasi hiki?
- Msomi yeyote na mtu mwenye dini ni lazima atakuwa ni mwenye kujisalimisha zaidi kwa Mungu kuliko mwingine yeyote.
- Lakini Mungu ni nani?
- Nilikuambia hapo kabla kuwa wewe ni mwanafalsafa, mimi ni Mkristo na nakwepa maudhui haya; mimi siyafahamu pamoja na jitihada kubwa niliyofanya kuhusu hilo, lakini ni mwenye hakika ya kuwepo Mungu, mwenye huruma, mkarimu na mwenye uwezo na hili mimi linanitosha…
- Lakini mimi sihisi kama inanitosha kabisa, iweje nimuabudu nisiyemfahamu?
- Wewe unafanya falsafa, cha msingi je umesha saini uthibitisho wa kufanya operesheni?
- Hapana, lakini ipo tayari kwa kusainiwa, au sivyo Katarina?
- Je kuna uwezekano mwingine wa kufaulu kwa operesheni?
- Kuna hospitali Ujerumani ambayo ni bora zaidi kwa operesheni hii, lakini

kwa hali zote haiwezekani kukuhamisha hospitali nyingine yoyote, operesheni hii inapaswa kufanywa leo hii. Jana tumewasiliana na mshauri wetu aliyepo Ujerumani na akatupa matumaini makubwa, ama uwezekano wa kuzidi asilimia kufaulu operesheni sijui chochote kipya.

- Sasa unatunasihi nini?
- Kusaini uthibitisho haraka, tutaanza uchunguzi wa awali kwa ajili ya operesheni saa mbili usiku.
- Nani atakayefanya operesheni hii?
- Mkuu wa upasuaji Dr. Steve Maiko, yeye daktari mtaalamu mshauri.
- Unaweza kutupatia karatasi za kusaini, kama kuna jambo lingine la kutunasihi ni vizuri.
- Hamna, ila ningependa uendeelee kuwa katika hali ya furaha hadi operesheni, katika majaribio yangu ambayo sio rasmi ni kuwa nafsi ya mtu mwenye matumaini huwa ni mwenye mafanikio zaidi katika operesheni yake.
- Vizuri…..huenda ikawa unaafikiana na Adam kuhusu matarajio mema.
- Nadhani ya kuwa watu wote wenye akili wanakubaliana katika hilo ukiwemo wewe vile vile.
- Bali huenda Katarina ametushinda sote kwa kututayarishia tiketi ya safari baada ya operesheni.
- Vizuri sana wewe huhitaji baada ya operesheni zaidi ya wiki moja ya mapumziko na kwa ajili ya kufuatilia hali yako, kisha baada ya hapo unaweza kuondoka. Pamoja na kua tunashauri kutosafiri ila baada ya siku kumi baada ya operesheni.
- Tunamshukuru Mungu, baada ya siku kumi kutokea sasa hivi, nadhania nimekadiria vizuri tarehe za safari.
- Ndio, hili ni jambo zuri kwako… Unajua Joji nakupa hongera kwa kuwa na mke na marafiki zako wazuri. Karatasi za uthibitisho zitafika muda sio mrefu ili uzisaini, na tutaanza matayarisho ya operesheni, nakutakia mafanikio katika afya yako.

Baada ya daktari kuondoka, Joji alimgeukia Katarina na kusema…

- Tunaelekea kufanya operesheni, na sina muda mrefu kabla ya operesheni, nataka kuweka vizuri mambo yangu.
- Vizuri, unakusudia nini?
- Nimeandika maelezo ya mali zote ninazomiliki ili zisipotee baada ya kufa kwangu, na zote nimeziandika kwako na kwa wanangu tu.

www.path-2-happiness.com

- Usiseme hivyo Joji….utaishi na utaamka salama.
- Samahani kukukatisha, pamoja na matarajio mema niliyokuwa nayo nakuthibitisha kuwa utatoka salama, jambo hili ni muhimu sana; na kama hutofanya hivyo huenda baadhi ya mali zako zikapotea. Na pia huenda ukamzuia mkeo na haki zake kama kweli baadhi ya mitazamo ya kanisa itafanyiwa kazi.
- Sikufahamu, unasemaje! hivyo na wewe ni mtu mwenye dini?
- Vipi kuhusu baba yako na mama yako?
- Sijawaona yapata miaka kumi.
- Huenda ikawa huu si wakati wake…. Lakini hili ni kosa bila shaka.
- Naafikiana nawe, nimezungumza nao zaidi ya mara moja, natamani kama wangekuwepo.
- Inaelekea leo hii mnaafikiana nami, ninawaahidi nikizinduka baada ya operesheni nitakwenda kuwatembelea kabla ya safari yangu… Inaelekea operesheni itakuwa ni mwisho wa maisha yangu.
- Lau kama utawaashiria katika wasia wako itakuwa ni kheri zaidi.
- Ndio, kitabu kitakatifu kimeusia kuhusu wazazi wawili: Hakika Mwenyezi Mungu ameusia akisema: “Mkirimu baba yako na mama Yako.”
- Kwa bahati mbaya wasia katika kitabu kitakatifu wakati mwingine unagongana, kwa mfano nimesoma unachosema na nimesoma vile vile: “Ikiwa mmoja anakuja kwangu wala hambughudhi baba yake au mama yake au mke wake au watoto wake na ndugu zake au hata nafasi yake, basi mtu huyu nafasi kuwa mwanafunzi wangu.”
- Katika Ukatoliki kukiwepo na mgongano katika akili zetu kama ulivyotaja, basi maudhui hayo hupelekewa Papa ili kukata maamuzi, ama Waprotestant wanataabika sana katika hilo.
- Mtaturejeshea Upapa unaochukiza, unaoondosha akili; cha msingi, tutajadili hili baadae. La msingi turudi pale tulipokuwepo, nitawaongeza wazazi wangu katika usia, kulingana na wasia wenu, na mtakuwa ni mashahidi wa usia huu baada ya muda kidogo.
- Hili ni jambo muhimu, pamoja na uhakika wangu kuwa utatoka salama kwa ruhusa ya Mungu.
- Kadhalika nimeifanyia upya bima ya maisha yangu kabla ya mwezi mmoja hivi, na hili vile vile ni dhamana yenu baada ya kufa kwangu.
- Mwenye dhamana ni Mungu tu, hizi ni sababu tu.

- Kuhusu nyumba…
- Kilichokuwa muhimu ukiandike kila unachokitaka kwenye wasia na muhimu zaidi sasa ni kumlilia Mungu kwa dua akuponye na kufaulu operesheni, na mimi nina hakika na hilo…kisha akatabasamu na kusema: “Usisahau, nataka uniletee zawadi kutoka Roma.”

Katarina alifuta machozi yake yaliyojaa bila kuyakusudia, kisha akatabasamu kwa maombi ya Adam…

- Ndio…lililokuwa muhimu zaidi ni kunyenyekea kwa Mungu kwa dua, na zawadi gani utakayo Roma?
- Ha ha ha, hakuna udi wa Kihindi au wa Kitaliano, wala sitokuletea zawadi za Kikatoliki kutoka Vatican.
- Sitaki hili wala lile, nahitaji zawadi mbili, ya kwanza ni mkoba wa ngozi uliokuwa mzuri sana lakini rahisi sana, kama sio rahisi siutaki. Ya pili ninahitaji picha kubwa ya mchezaji Cannavaro, kwani yeye ni historia ya mpira wa miguu Italia.
- Mkoba wa ngozi wa kifahari lakini rahisi sana, sidhani kama inawezekana….Ha ha ha ila kama tutampata Mutwi Rahman huko Italia.
- Aliyemdharau Mutwi Rahman India, atamdharau Mutwi mwingine Italia.
- Kwa mara ya kwanza nimegundua kuwa wewe ni mwana spoti!
- Cannavaro alifuzu kwa tuzo la mchezaji bora katika Kombe la Dunia lililopita, na wahakiki na wakosoaji wa mpira wa miguu huko Italia wanaamini kuwa yeye ndie mrithi wa mfalme wa mpira wa miguu wa zamani wa Italia, Franco Baresi, kwa ujumla napenda kucheza michezo mbali mbali kuliko kushuhudia, hili ndilo ombi langu.
- Hata ukitaka msalaba kutoka Vatican nitakuletea mimi, ikiwa Joji hatokuletea.
- Kiasi gani mnaafikiana nami.
- Asante mimi nataniana na rafiki yagu, je mwaniruhusu niondoke?

Wakati huo huo Tom aliingia ndani na kuona tabasamu na vicheko vingi.

- Inaelekea kuna habari mpya Joji, nipe tumaini.
- Hakuna jipya ila ni kuwa rafiki yangu anataka nimletee zawadi kutoka Roma; mkoba wa ngozi wa Kitaliano wa kifahari sana lakini ni rahisi sana, tulikuwa tunacheka kwa ajili hiyo.
- Kutoka Roma?! Utakwenda Roma kufanya operesheni huko?!
- Kwanza nakutambulisha kwa rafiki yangu Adam, na Adam na kutambulisha kwa daktari wangu na rafiki yangu Tom, operesheni yangu itakuwa leo na nitasafiri

www.path-2-happiness.com

baada ya siku kumi kwenda Roma kutembea pamoja na mpenzi wangu Katarina na watoto wetu, na sijui nitamletea vipi mkoba?

- Ni uzuri ulioje wa matarajio haya mema, kuna kilichobadilika kuhusu maudhui ya operesheni?
- Hapana, lakini muono wangu wa maisha umebadilika kwa hisia ya matarajio mema aliyoniletea Katarina, na ambayo nimejifunza kutoka kwa Adam.
- Ni kiasi gani tuna haja ya kujifunza matarajio mema, maradhi mengi ya nafsi suluhisho lake ni kuwa na hisia ya matarajio mema, lakini kuna ugumu katika kujifunza kwake.
- Kaa na Adam, atakufundisha, ana hazina nyingi.
- Kama ni hivyo nafurahishwa na mwanafunzi wake na kujifunza kutoka kwake.
- Ukweli ni kuwa majibu mengi ambayo nayafanyia falsafa ninapokuwa nawe kwenye kikao nimeyapata ima kutoka kwake au kutoka kwa Katarina…. Nakumbuka katika niliyokuambia: Tuchukulie mambo kwa wepesi wake bila uzito, hili nimelipata kutoka kwa Adam.
- Vizuri sana, nukta hii haswa imebadilisha sehemu ya kufikiri kwangu na tabia yangu baada ya kuisikia kutoka kwako, tabia yangu au hata masomo yangu nimekuwa nikiyachukulia kwa ugumu wake.
- Joji anajua kusifia ila ni kuwa mimi nakaa nae na kujifunza kutoka kwake, mimi ni mhudumu tu mgahawani, nae ni mwalimu wangu.

Katarina kwa tabasamu:

- Kwa kuwa tumeanza kusifiana; hii ni juhudi ya Tom ambae alimaliza tatizo la maswali pekuzi yaliyokuwa yakimchanganya Joji.

Tom kwa mshangao:

- Samahani ili kupata hakika, je operesheni ni leo?
- Inaelekea hujaniamini, ndio….inaelekea bado unahitaji somo kuhusu matarajio mema, mambo yangu yote nimeshayapanga, nahitaji nipate muda wa nusu saa hivi pamoja na nafsi yangu, ili niandike baadhi ya karatasi, kwani uhai na mauti yapo katika mikono ya Mungu.
- Operesheni ni saa ngapi?
- Matayarisho yataanza saa kumi na moja jioni, na operesheni saa mbili usiku.

Adam aliangalia saa yake…

- Nawaombeni ruhusa sasa hivi, inabidi niende mgahawani.
- Nakushukuru sana Adam, wewe ni rafiki bora.

- Subiri kidogo Adam, hii ni kadi yangu natamani kufahamiana nawe zaidi na kukaa pamoja.
- Ni muhimu sana mkutane pamoja…..Adam inaelekea Tom amebadilika je sijakuambia hapo kabla….
- Ni bahati kukutana nawe, samahani mimi sina kadi.

Kisha akatoa karatasi na kuandika jina lake na namba yake na kumpa Tom, kisha akaaga.

- Pamoja na muda mfupi niliomfahamu Adam, nimemuona kuwa ni katika marafiki bora.
- Ni mtu mzuri, nilipokuwa kwenye usingizi mzito na alipokuja Kakhi kunitembelea alionesha dharau kubwa kwake kwa sababu ni mhudumu, nae hakumwambia kitu, alichomwambia ni kuwa thamani yake ipo kwenye nafsi yake, inatoka ndani mwake, sio kutoka nje.
- Ni muhimu nikutane nae na kufahamiana nae zaidi….kitu kizuri ni kuwa umekinai kuwa nimebadilika.

Simu ya Joji ililia, aliomba ruhusu kwa Tom na Katarina na kunyanyua, upande wa pili alikuwa mkuu wake wa kazi Kakhi….

- Inaelekea hali yako ni njema sasa, nilikutembelea ukiwa katika usingizi mzito, vile vile alikuwepo mhudumu, vipi hali yako sasa?
- Hali yangu nzuri, na mhudumu ni rafiki yangu, wala si ruhusu yeyote kusema yanayomchukiza.
- Ha ha ha, nakupa habari nzuri…..menejimenti imeamua kukupongeza kwa kuweza kwako kusaini mikataba mitatu mikubwa kwa muda wa mwezi mmoja.
- Nawashukuruni nyote, huenda ni kwa sababu nimetoa rushwa.
- Achana na hiyo, lini utaanza kazi? Hukuomba likizo.
- Sijui, leo nitafanyiwa operesheni, na baada ya hapo nitasafiri kwenda Roma kutembea, nitakaporudi nitaomba likizo, kisha nitaamua niendelee na kazi au la?
- Inaelekea una hasira au umechoka, sijawahi kukuona ukizungumza hivi.
- Kwa bahati mbaya nimevuka mipaka ya misimamo yangu, na nimekuwa chombo cha kutoa rushwa kwa Benjamin.
- Kweli kabisa wewe una wasiwasi kwa sababu ya operesheni nitakupigia wakati mwingine, kwa heri.
- Kwa heri.
- Nini mpenzi wangu?

www.path-2-happiness.com

- Kakhi, kinyume kabisa na Adam, hana adabu wala maadili!
- Wengi mfano wake katika jamii yetu kwa sababu ya kuthamini fedha tu na kukana kwao Mungu na kuwa mbali na dini.

Tom akiongezea:

- Kuwa mbali na Mungu ndio matatizo makubwa ya wanadamu ninavyodhani, na katika sababu kuu ni hofu na kupotea pamoja na majanga.
- Angekuwa Katarina anasema hivi; nisingeona ajabu, lakini kulisema Tom hili ni jipya!!
- Ha ha ha, je sijakuambia kuwa umekinaishwa kubadilika kwangu, na kwa upande mwingine tafiti zote zinathibitisha hivyo, lakini majanga ya kweli yapo kwa watu wa dini.
- Unakusudia Upapa wa Katoliki.
- Ninafahamu unacholenga, nimekuja tu kukujulia hali naomba mnipe ruhusa nitakuja kesho kukutembelea.
- Asante Tom, nimefurahishwa na ziara yako.

Alipoondoka tu Tom…..Katarina alimgeukia Joji.

- Kweli Tom amebadilika sana.
- Ndio, dini hubadilisha kila kitu kwa mwanadamu.
- Vizuri sana, inaelekea nawe Joji umebadilika vile vile.
- Huenda ikawa hivyo!
- Nitakwenda nyumbani kwa ajili ya watoto, kisha nitatenga muda kukuombea, na nitarejea saa kumi na moja.
- Ni muhimu urudi nitakuwa nimemaliza kuyaandika katika karatasi ili nikukabidhi.

(3)

Joji alishughulishwa na alizama kuandika wasia wake, na kuhesabu mali anayomiliki, kwa muda wa saa moja alikuwa ameshamaliza. Kisha aliamua kuwaandikia marafiki zake wamuombee dua nakusali kwa ajili yake, na akawajulisha kuhusu operesheni atakayofanyiwa. Alipenda dua ziwe katika dini na madhehebu mbalimbali, huenda akajibiwa yule aliyekuwa katika haki. Alituma kwa rafiki zake, akikusudia haswa Habib Mkatoliki na Levi Myahudi –alitanabahi kuwa hana rafiki Muislamu, kisha akamkumbuka Mutwi Rahman na kumtumia na alipokumbuka India alimkumbuka Mbudha Jiyostana, lakini alijisemesha: Hawa ni wapagani, wao wanatengeneza Miungu

yao, sidhani kama wananufaisha na kudhuru, nami nauchukia sana upagani… kisha akazima kompyuta yake.

Simu yake ililia, ilikuwa ni namba ngeni, akaitika.

- Hallo habari.
- Hallo Joji, tunataka kujua hali yako.
- Ndio, nani mwenzangu.
- Inaelekea umenisahau, mimi ni Levi kutoka Tel Aviv.
- Ahaa, ok ok, nitamsahau vipi aliyenifanyia wema na kujifunza kutoka kwake? Nimekutamani sana Levi. Samahani sikuijua sauti yako, na sikutarajia kama utawasiliana nami.
- Vipi habari za operesheni? Nina wasiwasi sana na hali yako…
- Nashukuru hisia zako, nitafanyiwa operesheni leo, matarajio yangu ni kuwa itafaulu ila nimewatumia barua mniombee na kusali kwa ajili yangu.
- Nitasali kwa ajili yako, lakini kwa bahati mbaya, nitasali Kiyahudi.
- Kwa nini unasema bahati mbaya?!
- Tokea uje huku nimekuwa nikisoma kuhusu madhehebu na dini mbali mbali pamoja na fikra mbali mbali; nami nitafute njia ya furaha, na bado ninaendelea kusubiri maelekezo yako kufikia furaha.
- Nadhani umezidisha kidogo, mimi ndie ambae nimejifunza kutoka kwako, ni wewe uliyenifunza kuwa mkweli wa nafsi yangu….kabla sijasahau vipi rafiki yetu Habib?
- Nipo nae hapa pembeni, anataka kuzungumza nawe.
- Ha ha ha, mwambie ulinzi hadi kwenye simu. Habib ni mtu mzuri Levi jaribu kudumisha usuhuba wetu, rafiki ni mtu muhimu sana kwa mwanadamu.
- Ha ha ha, kuna habari huenda Habib akakujulisha…La muhimu tutasali kwa ajili yako, nakutakia siha njema na nataraji utawasiliana nasi baada ya operesheni, huyu Habib ongea nae.
- Hallo Joji, Mlinzi hapa, tupe habari nzuri, unaendeleaje na afya yako?
- Leo nitafanyiwa operesheni, nitakuwa katika hali njema, vipi habari yako wewe, nimekutamani sana?
- Sote tu wazima, na sisi tunakutamani sana, ziara yako ilikuwa ni ufunguzi wa mawasiliano na mijadala yetu.
- Huku ni kutojikweza Dr.….Mimi najifunza kutoka kwako, na mazungumzo yako kuhusu madhehebu mbali mbali ya Kikristo bado yanavuma masikioni mwangu

www.path-2-happiness.com

kwa mnasaba nitatembelea Roma na Vatican wiki inayofuata.
- Vizuri sana, kamilisha safari yako ya furaha, umetuahidi kutupa habari zako.
- Bila shaka, nitawapa habari ya safari yangu ya furaha; kwani hata Levi nimemuahidi hilo.
- Nitakuambia habari inayofurahisha….huenda nikamuoa Levi.
- Ooh, hongera, je ndoa itakuwa Kikatoliki au Kiyahudi?
- Ha ha ha, ndoa haitofanyika ila baada ya miezi kadhaa bado kuna matatizo madogo madogo, huenda ikawa katika njia ipelekayo katika furaha vyo vyote iwavyo, Kiyahudi au Kikatoliki au Kiprotestanti.
- Tunamuomba Mungu atusaidie kutuonesha njia ya kuelekea kwake.
- Kwa amani ya Bwana, tunasubiri utupe tumaini ya afya yako na njia ya furaha, kwa heri.

Joji alikuwa mbali huku akifikiri…hakutanabahi na sauti ya nesi, ikimwambia:
- Inabidi uondoke ukafanye baadhi ya vipimo.

Joji aliangalia saa yake ilikuwa ni saa kumi na moja kamili, Joji alimaliza baadhi ya vipimo na uchunguzi, na kurejea chumbani…alipoangalia saa yake ilionesha saa kumi na mbili unusu, Katarina alikuwa bado hajafika, alimpigia na akajibu kuwa yupo mlangoni hospitali anaingia, dakika chache akawa ameingia huku akiwa ni mwenye huzuni na kuomba samahani kulikuwa na tatizo katika gari lake, na hivyo kulazimika kupanda basi na ndicho kilichomchelewesha.
- Nilipatwa na wasiwasi nilipoona umechelewa.
- Nami nilihofia nisije kuchelewa zaidi ndio maana nikaliweka gari pembeni na kupanda basi.
- Chukuwa hii bahasha, ina makaratasi yote na nyaraka mbali mbali ambazo utazihitajia kukitokea lolote baya kwangu.
- Utakuwa katika hali nzuri apendapo Mungu.
- Kuna kitu ambacho sijakiandika.
- Kitu gani?
- Nataka ukamilishe utafiti wangu kuhusu njia ya furaha kwa ajili yako na watoto.
- Utakamilisha njia hiyo mwenyewe, na utafanikiwa muradi wako, Mungu hatokuacha kamwe, wewe ni mwenye tabia njema na maadili.
- Futa machozi yako….kisha nipe ahadi Katarina.
-

- Nina kuahidi kuwa nitakamilisha utafiki wa njia ya furaha pamoja nawe Mungu akipenda na utafiti wa mwanzo utakuwa pindi tukiwa katika safari yetu Roma.
- Nakupenda Katarina.

Kisha akamsogelea na kumkumbatia…na Katarina akaangua kilio.
- Nami nakupenda Joji.
- Kuwa mwenye matarajio mema kama ilivyo ada yako, je umeshaweka nafasi ya hoteli Roma?
- Ndio.

Kwa mara nyingine tena nesi aliingia chumbani na kumchukua Joji akamalize uchunguzi…Joji alimshika Katarina mkononi kwa nguvu na kumtaka arudi nyumbani, na kumuombea….
- Nenda nyumbani mpenzi wangu baada ya muda watanichukua kwenda kwenye nusu kaputi na operesheni itachukua masaa matatu…huna haja ya kukaa, nitakuwa katika hali nzuri, usijali…
- Usiseme hivi, mimi nakupenda Joji tutasafiri pamoja kwenda Roma, na tutapata njia ya furaha.
- Mama unaweza kuondoka sasa, tutawasiliana nawe baada ya operesheni, tunayo namba yako.
- Bwana akulinde Joji, na akubarikie katika umri wako na maisha yako.

Joji alipelekwa kwenye chumba cha operesheni na moyo wake ukitiririka hofu ya Katarina na wanawe, hakuiogopea nafsi yake kamwe, alikuwa akifikiria dunia itakuaje lau kila mmoja hamu yake itakuwa ni kwa ajili ya nafsi yake tu? Ni jambo lisilo vumilika, kubeba huzuni za watu na maumivu yao hupunguza katika nafsi ya mtu uwezekano wa maumivu. Vivyo hivyo maisha, atakayeishi kuhudumia watu na kuwafurahisha atakuwa na furaha na atakayeishi kwa ajili ya nafsi yake atapotea njia…Daktari alikata fikra zake zilizokuwa zinatiririka akimwambia:
- Nakutaka uwe katika hali ya utulivu kabisa, uchunguzi wa mwanzo ni mzuri sana, halitokuwa ila kheri tupu.

(4)

Operesheni ilimalizika usiku wa manane, ilichukua muda wa masaa manne, Katarina alikuwa akipiga simu hospitalini kila baada ya saa moja, wala hakutulia ila baada ya daktari kumpigia simu alipotoka chumba cha

www.path-2-happiness.com

operesheni, na kumjulisha kuwa mambo yamekwenda vizuri na ya kuwa matokeo ya operesheni yatakuwa tayari baada ya masaa kumi na mbili, naye Joji hatozindukana ila baada ya muda huo takriban….

- Poa bibiye, na wajulishe wengine wanaopiga simu, kwani mawasiliano hayakatiki hospitalini.
- Ni nani wanaopiga simu?
- Ni Adam na Tom…kama unawajua tafadhali wajulishe.
- Vizuri, nitawajulisha wasali kwa ajili yake.

Ilikuwa inakaribia saa kumi na mbili siku inayofuata…. Joji alianza kuzinduka, na kutingisha mkono wake katika hali isiyokuwa ya kawaida, na kutoa maneno yasiyofahamika Katarina, Adam na Tom waliokuwa wamekaa wamemzunguka hawakujua analosema….ila maneno machache tu: Njia ya furaha, kwa nini tumeumbwa, uhai…kifo.

Daktari alifika kuangalia hali ya Joji, Katarina akasimama upesi. Daktari akatabasamu.

- Najua hofu yako bibiye….nakupa habari nzuri ya kuwa uchunguzi wote ulikuwa mzuri, tunatarajia kuzinduka baada ya muda mfupi.
- Lakini daktari, yeye anazungumza maneno yasiyofahamika?
- Msiogope! Bado hajaondokana na nusu kaputi na akaweza kuzungumza kwa uwazi, hiyo itakuwa ni alama ya kufanikiwa operesheni. Kesho tutamuondoshea mashine, akiweza kutingishika kisha kusimama, hii itakuwa ni dalili kuwa operesheni imefanikiwa kwa asilimia mia moja. Akizindukana tu, tutampa vitulizo vya maumivu kila baada ya masaa matatu, na baada ya hapo mtamuona akiwa mzima kabisa. Kuweni na matumaini.
- Asante sana, Mungu atamuhifadhi.
- Kwa mnasaba ni kuwa akiwa katika nusu kaputi kila mara alikuwa akirejea maneno “Njia ya furaha”, ni nini hiyo njia ya furaha aliyokuwa akisema?
- Ni njia anayoifanyia utafiti, imemshughulisha sana, anataka kuigundua.
- Ni mmoja katika watu wachache waliofika katika hospitali hii akiwa mwenye furaha, kwa nini basi anatafuta furaha?
- Alianza kuwa na furaha pindi alipoanza utafiti wake huu.
- Atapata kwa uwezo wa Mungu. Haya kwa herini.

Alipotoka tu daktari, Tom alimgeukia Joji aliyelala chini ya uangalizi wa mashine na akanong’oneza kwa masikitiko.

- Kabisa utapata njia ya furaha Joji, nami nitakuwa nawe, nilipita njia nyingi, njia zenye tabu, ukanaji wa Mungu na sikuambulia chochote isipokuwa huzuni na ghamu tu. Hata hivyo hadi wakati huu sijakinaishwa na dini yoyote, pamoja na kukinaishwa kuwa Mungu mwenye huruma ndie aliyetuumba na ndie mwenye uwezo wa kutuongoza.
- Mimi nina hakika ewe Tom utaipata.
- Nitaipataje Adam?
- Nasema ulichokisema kuwa Mungu Mwenye huruma hamuweki mbali anayetaka kuwa nae karibu, na hivyo basi sote; mimi, wewe na Joji tutapata tunachokitafuta.
- Nawe unatafuta njia hiyo?
- Huenda hivyo!!!

Joji alianza kufungua macho kwa tabu. Katarina alitanabahi na akasogea karibu nae.

- Mpenzi wangu Joji je unanisikia?
- Ndio.
- Namshukuru Mungu kwa salama yako, tulikuwa tuna wasiwasi sana nawe, Adam na Tom hawa hapa wamekuja kukujulia hali.
- Asante.
- Tunakutakia kila la kheri upone haraka.
- Nami nakutakia kila la kheri upone haraka, daktari ametupa habari nzuri kuwa operesheni imefanikiwa.
- Je unataka chochote mpenzi wangu?
- Hapana.
- Naona tumuache, tusimtie uzito, ataamka pole pole.
- Kweli kabisa, nashauri mimi na Adam tuondoke na ubaki wewe pembeni yake.
- Nakushukuruni sana, atawapigia mwenyewe leo awajulishe hali yake mwenyewe.
- Je Adam unayo gari au ungependa nikupeleke?
- Hapana, sina gari, wala sipendi kukutaabisha, nitachukua basi.
- Panda nami, nataka kuzungumza nawe kidogo, kwa heri Katarina.
- Kwa heri.

Baada ya kuondoka kwa Adam na Tom kwa nusu saa….Joji alifunua macho yake tena, wakati Katarina akiwa mbali na kuwaza….

- Katarina.
- Joji mpenzi wangu vipi hali yako?

www.path-2-happiness.com

- Nzuri…Kama kwamba nilimuona Tom na Adam?
- Wameondoka sasa hivi, baada ya kujua hali yako, walikuwepo hapa tokea mapema asubuhi sana…..Vipi mpenzi hali yako?
- Saa ngapi?.....Nasikia maumivu kichwani.
- Inakaribia moja usiku, usijipe tabu nitamwita daktari sasa hivi.

Daktari alikuja upesi alipoitwa na nesi.

- Inaelekea hali yako ni nzuri Joji.
- Kuna maumivu makali kichwani.
- Hamna neno, utapewa kitulizo cha maumivu, na yote yataondoka, hii ni hali ya kawaida, kwani sehemu ya kichwa kilifunguliwa, hali hii ni nzuri inatupa matumaini.
- Ameanza kuzungumza vizuri, pamoja na uzito.
- Hizi ni dalili za kufanikiwa operesheni, tumaini, na Joji vile vile atumaini.
- Asante.

Daktari alimpiga Joji sindano ya kutuliza maumivu…kisha akamgeukia Katarina, na akamnasihi aondoke, kwani Joji atalala muda wa masaa mawili baada ya sindano kwa uchache.

- Bali nitasubiri pembeni yake.
- Akisha amka atapigwa sindano nyingine kwa masaa mawili au zaidi, maamuzi ni yako.
- Mpenzi wangu nenda.
- Nitasali kwa ajili yako siku nzima.

Saa moja unusu asubuhi Joji alikwisha zinduka, alizungumza na nesi kwa lugha inayofahamika iliyo wazi kabisa, pamoja na kuwa alikuwa anaendelea kulishwa kwa kutumia mashine ya kulishia, na muda huo ilikuwa bado hajapewa chakula…

Katarina alimpigia simu na kuzungumza nae na kumtuliza, na akamtaka awapitie Adam na Tom, nae akawapitia kisha Joji akawasiliana na Habib na Levi…baada ya hapo akajisalimisha katika fikra zake kuhusu njia ya furaha na safari yake ya Roma.

KUELEKEA NCHI YA MAKANISA

www.path-2-happiness.com

11

KUELEKEA NCHI YA MAKANISA

KUELEKEA NCHI YA MAKANISA

(1)

Afya ya Joji ilianza kuwa nzuri na kubadilika kidogo kidogo, na dalili zote za kufanikiwa kwa operesheni zilidhihiri, tokea siku ya pili aliweza kusimama kutoka kitandani mwake baada ya kuondolewa mashine, hata hivyo aliendelea kulishwa, wala hakuanza kupewa chakula…Katarina alikuja na watoto wamjulie hali, walifurahi sana walipomuona katika hali nzuri, akiwa anazungumza nao kwa furaha, na katika hali hiyo ya furaha Joji hakusahau kutuma barua ya kuwajulisha hali yake wale waliomjulia hali yake jana na akawaomba wamuombee dua, kwani huenda sababu ya kufanikiwa operesheni ile imetokana na dua ya mmoja wao..huenda ikawa hivyo!

Joji aliendelea kusoma na kujitayarisha na safari yake ya Roma akiwa na elimu kubwa kuhusu ukristo na madhehebu yake, na alishangazwa kwa nini akazaliwa kuwa ni Mprotestant, ila hajui elimu ya dini yake isipokuwa kidogo sana, mengi anayoyafahamu amejifunza kwa Katarina Mkatoliki, au kutoka kwa Habib ambaye ni Mkatoliki vilevile pindi alipokuwa Yerusalem, au kutokana na kusoma kwake hivi karibuni katika utafiti wake wa 'Njia ya furaha,' hakuweza kusoma dini yake hapo kabla, mfano huo ni sawa na wakristu wengi ambao hufuata dini ambayo hawaifahamu, bali utawaona wengi wao mfano wake yeye Joji hawajui zaidi ya jina tu.

Kwa hakika kusoma kuhusu Ukristo ilikuwa ni jambo lenye kusisimua, haswa alichokisoma kuhusu tofauti na mvutano mkubwa uliotokea baina ya madhehebu ya Kikristu: Tofauti kali za kiitikadi, mgongano wa kitabia na wa kiibada na kadhalika mgongano wa kijeshi na wa kivita. Alikuwa akifikiri kwa kina, kwa nini migongano hiyo? Je, Katarina ni mkweli alipomwambia kuwa tatizo lipo kwenye Protestant na sio kwenye Ukatoliki kwa kuwa Ukatoliki ndio uliotangulia, lakini alikumbuka kuwa Orthodoksi ilikuwa kabla ya Ukatoliki katika historia ya Ukristo, na kwa misingi ya ukaribu anaweza kuwa na haki kwa kuwa karibu zaidi na zama za Yesu. Hata hivyo kitabu kitakatifu hakikuandikwa wala kuhifadhiwa wakati wa maisha ya Yesu..hivyo basi ni madhehebu gani yaliyokuwa ni sahihi zaidi? Alitamani sana kuzungumza na mtu, akaamua kuwasiliana na Adam, hivyo akampigia..

www.path-2-happiness.com

- Hallo Adam
- Aha aha…tunamshukuru Mungu kwa kupona kwako.
- Asante Adam, natamani tuonane hivi karibuni.
- Nitakuja kwako kesho ikiwa ni sawa kwako?
- Vizuri, lakini nina swali; je nimalize vikao vyangu na Tom au hapana?
- Naona ukamilishe, lakini kwa nini swali hili? Na kwa nini sasa?
- Sijui, wakati mwingine nahisi kuwa hakuna jipya!
- Una maana gani kuwa hakuna jipya?
- Sijui, ni hisia ngeni tu.
- Hata mimi sijui kwanini vile vile, ninachokijua ni kuwa kwa asili ni kuendelea madamu hakutotokea jambo jipya, haswa kwa kuwa ipo wazi kuwa wewe mwenyewe unafaidika sana, kama ambavyo Tom amebadilika na kuwa katika hali nzuri zaidi kama usemavyo.
- Umesema kweli, na sijui kwa nini nipo nae katika hali ya utulivu na raha na natengamana nae kama rafiki na sio kama daktari? Kwa ujumla haya ni mawazo yanipitayo, nitampigia nipate miadi nae, hata hivyo ningependa kujadiliana nawe kabla ya kikao hichokama itawezekanahuenda tukazungumza baadhi za kadhia.

Joji alimaliza mazungumzo, na akampigia simu Tom moja kwa moja, akimtaka apate nae kikao kabla ya safari yake ya Roma, na ikiwezekana kikao hicho kifanyike hospitali. Alimkubalia, kwani hakutaka kumchosha.

- Basi ni bora iwe kesho kutwa asubuhi, kwani daktari amenijulisha kuwa nitaondoka baada ya siku tatu muda wa jioni.
- Kama utakavyo Joji

Katarina alikuja pindi joji akiwa amezongwa na kusoma…alitanabahi kuingia kwake alipokuwa tayari chumbani na kutoa salamu kwa sauti kubwa yenye kushawishi, kisha akakaa pembeni yake akampiga busu shavuni..

- Nimefurahi mno, hali yako ni nzuri kama alivyonijulisha daktari.
- Naam, mimi nipo katika hali nzuri, vipi habari ya safari ya Roma?
- Takriban kila kitu kipo tayari, nafasi ya ndege, ya hoteli na ahadi za kukutana na watu mbali mbali, pamoja na misafara ya kitalii ya pamoja.
- Vizuri, unakusudia nini unaposema vikao pamoja na watu mbali mbali?
- Ninajua ukitakacho, nimeratibu baadhi ya vikao pamoja na maaskofu na ziara ya Vatican.
- Hili silo nilitakalo mimi, bali ulitakalo wewe.

- Ndio, mimi nataka, ila sikuiratibu tu hivi hivi ila baada ya kujua kuwa wewe kadhalika unaitaka.
- Swadakta, asante sana mpenzi wangu.
- Je, utakaa pamoja na daktari Tom kabla ya safari yetu au baada ya safari yetu?
- Kabla ya safari, kikao kesho kutwa hapa hospitalini…inaelekea unajali sana kikao?
- Swadakta, sijui kwanini nahisi kuwa wewe umeanza kuwa na furaha tokea uwe na vikao vyako na Tom.
- Hii tu ndio sababu?!
- Naam, hii tu ndio sababu..au ni kwa sababu mimi ninahisia kuwa Tom ameanza kuwa ni bora kuliko hapo kabla, sijui kwa nini?
- Nami kadhalika nina hisia hiyo hiyo, lakini nina hofia asiwe ananidanganya.
- Yote yanawezekana, lakini mimi naelekea kuona kuwa amebadilika kikweli, pamoja na kuwa yote yanawezekana.
- Lakini kama anatudanganya lengo lake ni nini hasa katika hilo?
- Sidhani kama ana maslahi katika kutudanganya, hivyo naamini kuwa yeye ni mkweli katika mabadiliko yake.
- Nami kadhalika, lau si yule mkuu wa ofisi yake Baraad.
- Namchukia mtu yule, sijui kwa nini namuona kuwa ni mtu ambae hakuna mtu anaweza kukaa nae?
- Hata Tom anamlalamikia!
- Huenda, lakini hili halinikinaishi! Badala ya kumlalamikia, kwa nini asimfukuze na kustarehe nae.
- Kweli, huenda kuna sababu nyingine, sijui! Kwa jumla nilikuwa nataka kusimamisha vikao vyangu na Tom.
- Sidhani kama ni sawa, hata hivyo uamuzi ni wa kwako.
- Rai yako ndio rai ya Adam vile vile, ananiambia: Umeianza njia na inavyotakiwa uikamilishe, na hili limemfanya Tom nae awe katika hali nzuri, na Adam akaendelea kuniambia kuwa umekuwa nae muda wote nae akiwa na tabia mbaya, na leo hii ameanza kubadilika na kuwa katika tabia nzuri unataka kumuacha.
- Maneno yenye mantiki kabisa na hoja yenye nguvu.
- Kukubaliana kwenu mara kwa mara kunanithibitishia kuwa Adam ni Mkatoliki na sio Mprotestant.
- Ha ha ha, au huenda alikuwa ni muongo kwa kuwa Ukatoliki uko karibu kabisa

www.path-2-happiness.com

na haki na ukweli kuliko Uprotestant.

- Huenda ikawa hivyo, nimekusanya maswali mengi na vilinganishi huenda tukayajadili hayo huko Roma.
- Fikra nzuri, kwani tutakuwa katika makao makuu ya Ukatoliki, bali kituo kikuu cha Ukristo duniani.
- Huenda ukawa katika kituo kikuu cha Ukatoliki, lakini sio katika kituo kikuu cha Ukristo, kwani sisi hatuamini Upapa wenye mateso.
- Usiseme hivi tena, masuala haya tutajadiliana tukiwa Roma kama tulivyokubaliana? Uhisi kuwa unaukosea Ukatoliki? Je, unataka na sisi tukueleze jinsi tunavyoukosoa Uprotestant uliotoroka?
- Uliotoroka!! Wasifu mzuri wa Uprotestant! Huoni kuwa sijakasirika kama wewe pamoja na uliyosema!!
- Ha ha ha, huenda hivyo kwa sababu unafahamu kuwa huu ndio wasifu sahihi wa Protestant, nyie ndio wale mnaotunga dini yenu mnavyotaka, na mnafahamu kitabu kitakatifu mnavyotaka, na huu ndio ukimbizi ambao ninaukusudia!
- Huenda ikawa kama mlivyosema, au ni kwa sababu sisi tupo huru zaidi kuliko udhalimu wa kanisa la Roma na chuki za msamaha wa madhambi.
- Tumekubaliana tuyajadili yote tukiwa Roma, je unataka tukatishe mjadala?
- Ha ha ha, tumekubaliana, nataka uhakikishe na daktari kama tutahitaji kitu ili tusafiri kwa muda uliopangwa, kwani mimi nimehamasika sana na safari.
- Makusudio yako ni kuwa umehamasika kukutana na maaskofu!!

Joji alikaa vizuri kisha akatabasamu na kusema:

- Ndio; niwakinaishe mbele yako kwa makosa ya dini yake.
- Pamoja na kujua dharau yako, mimi najitahidi sana kuwa kati na kati katika safari hii, Je unaweza kunisaidia mpenzi wangu?
- Wewe unajua jinsi gani moyo wangu unavyomili mpenzi wangu, nikikushinda kwenye hoja, wewe unanishinda kwenye mapenzi, amini kuwa nitafanya jitahada kile ninachoweza.
- Ninakupenda Joji, nitakwenda sasa hivi kwa daktari kuulizia hali yako pamoja na maudhui yetu ya safari.

Aliporejea Katarina baada ya saa moja alimkuta Joji amezama katika kusoma…

- Aakh…je usomacho ni muhimu kiasi hiki?!
- Ndio, nasoma kuhusu Martin Luther na John Cavin, wao ndio watu muhimu zaidi

wenye athari kubwa katika Uprotestant.

- Unakusudia ndio walioandika na kuitengeneza dini ya Uprotestant.
- Swadakta kwa kiasi kikubwa, hata hivyo walifanya hivyo; ili wamalizane na maradhi ya Ukatoliki na tabia zake zinazochosha…
- Wewe unaamini kuwa Uprotestant umetungwa?!
- Kwa bahati mbaya ndio, ili iondokane na wimbi la ukanaji mungu ambalo limelinganiwa na Ukatoliki kwa siri zake na upapa wake, kiasi cha kuwa baadhi ya watu ambao wamekusanya baina ya dini na ujinga na upungufu wa akili! Je unataka tuzungumze hilo sasa hivi?
- Ooh..mara moja maudhui yamekuwa kuhusu Ukatoliki, tutajadili tukiwa Roma, na hapo utakinaishwa kuwa Uprotestant ni dini iliyotungwa na upotoshaji wa dini ya Ukristo.
- Swadakta, Uprotestant ni upotoshaji wa Ukatoliki, na ndio maana kila mmoja anamuona mwenzake kafiri, na huuwana vile vile…hata vikundi vya Kiprotestant vinakufurishana, je unajua kuna idadi ipi ya makanisa na madhehebu ya Kiprotestant?
- Hapana, je zinafika makundi mia moja kwa mfano?
- Huenda ikawa hivi, naona habari hii imekufurahisha. Ni kati ya ishirini na nane elfu hadi arubaini elfu katika makanisa na madhehebu.
- Madhehebu na makanisa elfu arubaini!!

Joji alioneshwa kuchukizwa na maneno yale, kipaji chake cha uso kilijikunja, na akaamua kukaa vizuri, na akashusha pumzi na kusema:

- Kwa bahati mbaya, ndio, na hili linanikumbusha vikundi mbali mbali vya dini zisizo za mbinguni, kama nilivyoona baadhi yake nchini India, na kwa bahati mbaya vile vile kuwa mkweli na nafsi ni ngumu sana!
- Je sijakuambia kuwa Uprotestant ni tungo tu! Kisha akatabasamu na kusema: Hata hivyo tutajadili hayo huko Roma kama tulivyokubaliana.
- Zaidi ya mara moja unasema uyatakayo, kisha unamalizia kuwa mjadala wetu utaendelea Roma, kisha akatabasamu na kusema: Hamna neno, kwa ajili yako tu, daktari anasema nini?
- Nakupenda Joji…daktari anasema afya yako ni nzuri sana, na kuwa operesheni ilifanikiwa kwa asilimia mia moja, na utatoka hivi karibuni tu, inakutosha baada ya kutoka kukaa siku mbili au tatu hivi, kisha uendelee na maisha yako ya kawaida, na unaweza kusafiri bila matatizo yoyote yale.

www.path-2-happiness.com

- Je kuna chochote cha kuchukua safarini kwa akiba?
- Nimemuuliza hilo amesema: Hapana, hakuna chochote ila nasaha za jumla tu; mfano usijichoshe, au kujihatarisha na jambo, na hili halina uhusiano wowote na operesheni kama alivyosema.
- Vizuri.
- Itakuwa ni safari nzuri, na tutaijadidi ndoa yetu kama siku zile za mwanzo..
- Ni uzuri ulioje wa mwanzo wa ndoa yetu! Tutaijadidi na tutafurahi kwenye safari yetu, lakini kutakuwa na mambo mapya..
- Nini kipya?
- Kuwepo kwa Maiko na Sali.
- Pamoja na kuwa tutalazimika kubadilisha baadhi ya ratiba za safari yetu kwa ajili yao, lakini watazidisha furaha yetu, nawapenda sana.
- Najua kuwa mimi nimekuwa na mapungufu kwa haki zao, na nahisi kuwa wamekuwa haraka kwa ghafla.
- Tutawafidia wakati unaokuja, au sivyo?
- Ndio, na nadhani zawadi bora zaidi ambayo nitawapa ni muongozo wa njia yao ya furaha.
- Njia ya furaha kwa mara nyingine!
- Na mara ya tatu na mara ya nne, sijui kwa nini nahisi kuwa nimeanza kuikaribia kufika?
- Huenda tukaifikia pamoja tukiwa Roma.
- Ha ha ha, unakusudia sote tuwe Wakatoliki kwa mara nyingine.
- Huenda ikawa hivyo…au isiwe.
- Na utauacha Ukatoliki?!
- Au huenda wewe ukauacha Uprotestant.
- Hebu tujaalie ndio itakavyokuwa, je una uwezo wa kuvumilia kuucha ukatoliki?
- Maamuzi yalinichukuwa muda mrefu sana na migongano mingi…hata hivyo sasa hivi naweza kusema ndio, pamoja na kuwa maamuzi ni mazito.
- Mimi najifakharisha kwako mpenzi wangu.
- Bali mimi ndie nayepaswa kukushukuru Joji, hukuridhia kuishi bila ya kufafanua na kuainisha mipaka, malengo yako, na kuweka maana ya maisha yako, na kujibu maswali yako.
- Ha ha ha, hongera kwako ewe Mprotestant.
- Ha ha ha, bali hongera kwako kukinai na kurudi katika asili, kwangu Ukatoliki

ewe mpingaji, Mprotestant.

(2)

Joji alizama katika kusoma baada ya kuondoka Katarina, na akakamilisha alichokuwa akisoma kuhusu Martin Luther na John Calvin na wengineo, na mabadiliko ya zama za sasa kuhusu Ukristo, wala hakutanabahi na muda hadi aliposikia sauti ya nesi ikisema:

- Je una mtihani unaotaka kuufanya baada ya kutoka kwako hospitali?
- Ndio, ni mtihani wa maisha yangu.
- Katika kiwango gani cha masomo?
- Sijui
- Inaelekea hutaki kuzungumza, samahani kukatisha masomo yako, nimekuja kuondosha mashine ya kukulishia, na kuanzia kesho utaanza kula katika hali ya kawaida.
- Samahani, sijakusudia ulivyofahamu, lakini ukweli nahisi nipo katika mtihani ingawaje sio wa masomo darasani.
- Sijui chochote unachosema!
- Dini yako ni ipi?
- Mimi siamini dini zote, hata hivyo mimi ni Mprotestant..Mkalivini.
- Yaani mimi ni katika wafuasi wa John Calvin
- Ndio, ingawaje sijui alichokuja nacho kipya? Ninachokifahamu ni kuwa ipo karibu na akili zaidi na ni kongamano la wenye akili na sio kama Luther.
- Umejuaje hili na wewe hujui kipya alichokuja nacho?
- Mimi ni nesi na sio mtawa, inaelekea ni njia ya kusuluhisha migongano iliyopo kati ya Ukatoliki na Uprotestant.
- Je inaingia akilini watu wa dini moja wakagongana?! Na je, inaingia kuja kwa mtu kama Calvin na akarudia upya kutengeneza dini?!
- Ndio maana nikakuambia siamini Uprotestant wala Ukatoliki wala dini nyingine, na kama sio haja ya kuwa na dini nisingeamini Uprotestant.
- Samahani unakusudia nini kusema haja ya dini?
- Siwezi kuishi bila ya dini, maisha bila ya dini ni adhabu na masumbuko, mwanzo nilikuwa mkana Mungu, kisha nikahamia katika usekula, na nilikaribia kujiua kwa dhiki niliyokuwa nikiishi nayo, hata hivyo nilikuwa najua kosa langu ndani ya nafsi yangu, nikaamua kuwa Mprotestant, ambayo bila maelezo yoyote huwezi

www.path-2-happiness.com

kufahamu kitu..mazungumzo nawe ni mazuri yenye kufurahisha lakini naomba ruhusa kwani nina kazi.

- Je unaridhika na Uprotestant bila maelezo ya kutosha kama ulivyosema? Nadhani unaikimbia nafsi yako, lakini kwenda wapi?

Athari ya maneno yale yalionekana katika uso wa nesi, nae akificha huzuni yake katika moyo wake na roho yake ikiwa tupu:

- Huenda ikawa hivyo, katika nisichokijua, mimi ni kama unyoya katika upepo upitao, lakini huenda nikafikia hilo siku moja, kwa heri.

Siku iliyofuata Joji aliamka mapema, alikula kwa hamu pindi alipoletewa istiftahi, alikuwa akihisi njaa kali na hamu kubwa ya kula, kisha akarejea kwenye utafiti wake, Yule nesi wa jana alikuja kumpima joto lake.

- Vizuri, upo katika hali nzuri.
- Samahani kwa kukukera jana.
- Hakuna usumbufu wowote, asante kwa wema wako, nadhani maneno yako yalikuwa kweli uliponiambia kuwa naitoroka nafsi yangu bila lengo lolote. Lakini nifanye nini ikiwa ukanaji mungu na usekula ni adhabu na kuwa na dini ni kutoroka?
- Kuwa na dini hakuna maana ya kutoroka, lakini wewe unaikimbia dini yako?
- Lakini dini kama unavyosema hutungwa na hutengenezwa, na sio dini kutoka kwa Mungu, huenda akaja ambaye atakuwa ni mwadilifu katika dini ili iwe ni bora zaidi.
- Lakini hii ni dini ya mbinguni kutoka kwa Mungu.
- Wewe unajua zaidi kuliko mimi kuhusu dini, lakini itakuwaje ni dini ya mbinguni ambayo inabadilishwa na mtu kama Calvin na Luther na wengineo kama watakavyo? Na si hivyo bali Yesu aliuwawa kabla hata agano jipya halijaandikwa, ambayo waliiandika wanafunzi wa wanafunzi wake.
- Inaelekea wewe ni mwanafalsafa wa dini mbali mbali!
- Bali mimi nimeitoroka nafsi yangu kama ulivyoniambia.
- Nini suluhisho kwa muono wako?
- Suluhishi ni lile ulilonikosoa, kuikimbia nafsi.
- Sidhani kukimbia matatizo kuna suluhisho lake.
- Nini suluhisho kwa muono wako?
- Tuingie na tufahamu vizuri kuhusu dini kwa uhakika wenyewe.
- Ile tuwe maaskofu na watawa?! Na hata wao wana shaka nyingi kuhusu dini zao,

na ndio mara kwa mara wanabadilisha dini zao.

- Kujua njia haina maana kuwa maaskofu au watawa, mimi ninawaheshimu watawa na maaskofu, wala sitaki kuwa mingoni mwao, lakini shaka siku zote inapelekea tabu na mashaka, kama ilivyo yakini ya jambo hupelekea katika tumaini.
- Unaelekea kuwa ni Mkatoliki, kwani wao ndio wanapenda sisi tujisalimishe kwa maaskofu na watawa bila ya mjadala, bali bila hata ya kuangalia na kurejea wenyewe katika kitabu kitakatifu.
- Siwezi kuisalimisha akili yangu kwa mtu yeyote yule awe kati yangu na Mungu wangu, mimi ni Mprotestant.
- Sasa nini unakosoa wakati wewe ni kama mimi?! Ila kama utakuwa ni Mlutheri
- Ha ha ha, kwa kweli sijui ikiwa mimi ni katika wafuasi wa Luther au wa Calvin au mwingine yoyote, ninachokijua kuwa mimi ni Mprotestant, kwa sababu baba yangu na mama yangu walikuwa Waprotestant.
- Kama hivyo hatuna tofauti, sasa kwa nini basi unanielezea kuwa mimi naikimbia nafsi yangu?!
- Kwa sababu na mimi vile vile naikimbia nafsi yangu.
- Unakimbilia wapi?
- Kuelekea njia ya furaha.
- Ha ha ha, njia hiyo iko wapi ewe mwanafalsafa?
- Sijui, lakini nitaipata tu.
- Inaelekea wewe ni yule bwana mafumbo wa kifalsafa, pamoja na kufurahia mazungumzo nawe lakini inabidi niondoke, kwa mnasaba ni kuwa nina hakika utaipata; kwa sababu ni mtu mwenye kudumu katika jambo, ukiipata tujuvye kwayo.
- Nini hicho?!
- Njia ya furaha!

Baada ya muda mdogo alipoondoka nesi alikuja daktari chumbani kwa Joji, na kujua hali yake ilivyo, na kumjulisha kuwa anaweza kutoka kesho jioni akipenda hilo, kwani hali ya afya yake ni nzuri.

- Asante
- Mke wako alinijulisha kuwa mtasafiri kwenda Roma, hongereni, ni nchi nzuri yenye mengi.
- Ndio, nitakwenda naye pamoja na watoto wetu, je kuna usia wowote wa kiafya baada ya operesheni?

www.path-2-happiness.com

- Hapana kabisa, hali yako ni nzuri.

Kabla ya chakula cha mchana alifika Adam..akimkuta Joji amezama katika utafiti wake akiwa mbali na yanayomzunguka, alimsogelea kisha akamtolea salamu:

- Inaelekea kuwa unalosoma sasa hivi ni jambo muhimu mno, kiasi cha kushindwa kuwatambua waliokuzunguka!
- Adam..Oho Karibu sana, umefika muda gani, nilikuwa nasoma historia ya ukristo ya zama za kale.
- Vizuri, umepata nini?
- Unaposoma Historia hii unakutana na mshituko wa ajabu kabisa na mambo ya ajabu kabisa!
- Huoni kuwa unafanya haraka kuukosoa Ukatoliki hata kabla ya safari yako kwenda Roma.
- Mimi siukosoi Ukatoliki.
- Kama ni hivyo sijakufahamu, unakusudia nini.
- Mimi ninaukosoa Ukatoliki na Uprotestant na madhehebu yote na makundi yote ya Kikristo.
- Wewe unakwenda Roma, mambo mengi sana yatafunguka kwako baada ya kusafiri, usiwe na pupa, huenda yakakubainikia mambo ambayo wala hujayafikiria.
- Hili ndilo ambalo nilitaka ushauri wako.
- Sijafahamu, ni jambo gani ambalo unataka ushauri wangu?
- Kulingana na rai yako, nimewasiliana na Tom na kuchukua ahadi ya kukutana nae kesho, lakini ninajua atakayoniambia.
- Vizuri, kamilisha atakayokuambia?
- Ataniambia: Fanya utafiti kuhusu Ukristo na uujue vizuri zaidi kabla ya safari yako ya Roma, na mimi nahisi kuwa najua kwa kiasi kikubwa, iwe kutokana na kusoma kwangu au kwa safari yangu ya Yerusalem au katika maisha yangu, mimi ni Mprotestant, na sihisi kuwa nitaongeza chochote kipya katika safari yangu.
- Una umri gani Joji?
- Thelathini na nane au tisa, kwa nini unauliza hilo?
- Umesubiri kwa muda wa miaka thelathini na nane, wala huwezi kusubiri hadi utakapokwenda Roma, na kurejea ukiwa na hakika na maamuzi yako, huoni kuwa una haraka?
- Huenda ikawa hivyo, kila ninaposoma kuhusu makundi ya Protestant ndio kila

ninapozidisha kuwa na imani nayo zaidi.
- Kwanini basi usihamie kwenye Ukatoliki au kwenye Orthodoksi.
- Je sijakuambia kuwa wewe ni Mkatoliki? Lakini niamini, umbali wangu kuhusu upapa wa kikatoliki ni mkubwa zaidi kuliko umbali wangu na Uprotestant.
- Huenda rai yako ikabadilika baada ya safari, ni vizuri kuamiliana na fikra mbali mbali kwa mawazo huru na sio kwa fikra zilizokwishakuathiri kabla.
- Sina fikra tangulizi, nimesoma vitabu vingi vya kikatoliki na kiprotestant na historia zao na matokeo yao, lakini sijakinaishwa na chochote.
- Vizuri, Jaribu kuwa huru zaidi na kufunguka zaidi, na kufikiria zaidi, wala usifanye haraka; na hivyo basi baada ya safari yako utakuwa ni mwenye hakika zaidi na mwenye utulivu na maamuzi yako.
- Je akili iliyosalimika na elimu inaweza kukosea kuhusu dini?
- Bila shaka hapana, haiwezekani ikawa hivyo kama dini ni ya kweli kutoka kwa Mungu.
- Lakini kama dini itagongana na akili au hali halisi au elimu, je hii sio dalili ya kuwa sio dini ya haki?
- Bila shaka ni kweli, lakini hata hivyo yatupasa tufahamu kuwa akili ina upungufu; kile ambacho hatuwezi kukidiriki haina maana kuwa kinakwenda kinyume na akili au elimu, bali ina maana udhaifu wetu kama wanadamu tu.
- Vipi, nielezee kwa uwazi zaidi.
- Kwa kuwa sisi hatujui asili ya mungu vizuri, wala hatuwezi kumdiriki kwa akili zetu; haina maana kuwa Mungu hayupo au sio sahihi, lakini ina maana kuwa haya ni mapungufu ya kawaida ya mwanadamu.
- Pamoja na tabu na juhudi kubwa sikuweza kufahamu kuwa mungu mmoja ana nafsi tatu hadi leo hii, Je, hii ni siri ya Katoliki miongoni mwa siri za kanisa, unanitaka niamini hayo bila hata maelezo?
- Kuna tofauti kubwa iliyo wazi ambayo sitaweza kujua hali yake, na kati yake kugongana na akili, ni lipi unalokusudia?
- Nakusudia hili la pili, hili linagongana na akili yangu na siwezi kulifasiri.
- Yanayogongana moja kwa moja na akili iliyo sahihi haiwezi kuwa ni dini sahihi, au dini ya haki.
- Kwa maana hiyo basi itabidi tuachane na Uorthodoksi, Ukatoliki na Uprotestant.
- Kwa nini usisubiri hadi urudi kutoka Roma?
- Nikirudi na rai hii basi wakati huo nitakuwa ima ni mkana mungu au msekula.

www.path-2-happiness.com

- Kwani ukanaji mungu na usekula haugongani na akili kwa upande wako?
- Kwa msingi zinagongana, na kwa ajili hiyo nilitoraka nikaenda kwenye dini, kisha nikatoka kwenye dini za watu wa ardhini kuelekea kwenye dini ya mbinguni, baada ya hapo nikauchukia Uyahudi kama ilivyo hivi sasa, na nimeanza kuuchukia Ukristo, na hakuna kilichobakia sasa hivi ila niwe gaidi Muislamu.
- Usichukue maamuzi yoyote hadi utakaporejea kutoka Roma, huenda ukafahamu na kukinai.
- Kama sijakinaishwa?
- Tafiti kuhusu Uislamu huenda ukapata njia ya furaha!
- Kwa nini wewe usitafute kwenye Uislamu kwanza? Na uwe mpenda wanawake, gaidi na mtu asiye na maendeleo.
- Sisi tupo kwenye hatua ya utafiti kuhusu Ukristo, nitakujulisha ukirejea Roma.
- Sijui kwa nini wewe na Katarina mnazungumza kama kwamba Roma nitakinaishwa niende kinyume na akili yangu, na kuamini na kusadikisha yenye kupingana na mantiki.
- Sijakuambia uende kinyume na akili yako, lakini nilikuambia usifanye haraka, wewe una akili, ukikinai sawa na lau kama hukukinai fanya unachotaka, kisha mimi nimekuja kulingana na matakwa yako, na sijakulazimisha ufanye kitu, sasa kwa nini unanishambulia mimi?
- Samahani Adam, mimi ni mtu wa pupa kimaumbile, lakini niamini kuwa mimi nataka kufikia njia ya furaha kwa haraka iwezekanavyo, kitu kilichokuwa kinanitia hofu kabla ya operesheni ni kifo wakati ambapo sijaifahamu njia ya furaha.
- Utaifikia Mungu akipenda, na bora kuchelewa kufika kuliko kutofika kabisa, pamoja na kuwa hujachelewa; bali unakwenda kwa mwendo wa kasi kubwa.
-
- Narudia samahani zangu kwako Adam, huenda nikawa na pupa, na huenda ikawa nimechoshwa na maudhui haya.
- Ikiwa ni mwenye pupa ili uweze kufika hili ni jambo moja ama uchovu ina maana ya kutokudumu katika jambo lenyewe, kisha je huoni kuwa hili linagongana na nafsi iliyokuja ikijali na kuvumilia jambo hili?
- Balaa! huoni kuwa unazidisha?!
- Bila ya kusisitiza, mtu hawezi kufika popote, wala kufikia mafanikio yoyote, na uchovu ina maana ya kutosisitiza, kisha huoni kuwa jambo hili linapingana na nafsi ya mwenye haraka katika kuvumulia kwa sababu ya kujali kwako?

- Naafikiana nawe, lakini wewe unahamasika upesi, Je, hulioni hilo?
- Huenda ikawa hivyo, lakini huoni kuwa unakusudia kunichokoza?
- Ha ha ha, wakati mwingine…unahamanika mara moja.

Wakati huo aliingia Katarina akiwa pamoja na Maiko, Salli wakikimbilia kitandani kwa baba yao, akawakumbatia kwa shauku..akawa anazungumza nao na kumuacha Adam kidogo…Adam akasubiri dakika chache kisha akaamua kuondoka.

- Nimefurahi kujua hali yako, je utaniruhusu niondoke?

Katarina alitabasamu kwa Adam akamwambia:

- Samahani Adam, Sali na Maiko hawajamuona baba yao baada ya operesheni, na wala hawakukaa naye muda mrefu sana; kwani walikuwa safarini.
- Kwa nini unaomba samahani?! Nimemaliza mazungumzo na kujua hali ya rafiki yangu, na nina kazi nataka kwenda kuzifanya.
- Nakushukuru sana Adam, je tutaonana kabla ya safari yangu?
- Nitafurahi tukionana, hata kama kwa bahati mbaya hatukuonana basi kwa uchache tutawasiliana, haya kwaherini.

Baada ya kuondoka Adam alimkumbatia Katarina:

- Sijamuona rafiki yako huyu ila hospitalini, lakini ni mtu mzuri na mwenye adabu kabisa, na unaona raha kuwa nae sijui kwanini?
- Huenda ikawa kwa sababu ni Mkatoliki kama wewe!
- Wakatoliki wengi vivyo hivyo ni wenye heshima na wazuri, lakini hapo kabla uliniambia kuwa hujui dini yake.
- Hadi sasa bado sijui, lakini kule kujali kwake na kunihamasisha niende Roma ili kuujua Ukatoliki na mara nyingi kuwa sawa nawe katika kufikiri inanihakikishia kuwa yeye ni Mkatoliki. Hebu fikiria leo hii alikuwa ananikinaisha kufunguka na fikra kuhusu Ukatoliki.
- Ha ha ha, vizuri, huenda amejifunga katika kufikia katika Ukatoliki peke yake, na huenda ukafaidika na rafiki zako lile ambalo hukuweza kufaidika na mke wako.. kwa mnasaba nimewajulisha watoto leo hii kuhusu uhakika wa safari ya Roma, hawa hapa mbele yako wasikilize wanachotaka.
- Agizeni, Semeni..mnataka nini?
- Baba je umesahau?
- Nimesahau nini?
- Nilitaka kuona ngome ya Saint Angelo, na Sali alitaka kuona Trevi Fountain.

www.path-2-happiness.com

- Samahani, kwa kweli nilisahau.
- Ninahofia safari hii isije ikawa ni safari ya kukaa hotelini tu na kusoma vitabu na kufanya kazi kwenye Kompyuta yako na kujadili muda wote.
- Ninawaahidi kuwa tutakuwa na wakati maalum nanyi.
- Hii ni ahadi baba?
- Ni ahadi na kwa ushahidi wa mama yenu pia.
- Na mimi ninawaahidi vile vile, kwa ushahidi wa baba yenu

Kikao kile cha familia kilikuwa cha upole na chenye furaha hadi ilipofika wakati wa kula chakula cha mchana, Katarina akawaambia wanawe:

- Mnaonaje tukiondoka sasa na ninawaalika katika hoteli ya kitaliano?
- Vizuri!
- Haya twendeni.

Katarina alipoondoka na wanawe, Joji alikula chakula chake cha mchana, kisha akarudia tena kusoma kwa mara nyingine..alianza kukumbuka alichosoma kwa umakini mkubwa tokea alipolazwa hospitalini, akaanza kuhisi hofu..kwani kila alipokuwa akisoma sana ndipo alipoona migongano kwa wingi zaidi, haswa kile alichokiita upagani wa ukristo na miungu kuwa mingi na kumfanya Papa na watu wa dini kuwa ni miungu! Je, inawazekana kuondosha haya yote kwa safari moja tu…! Ikawa haya yatatimia basi huenda upapa ukiwa ni sahihi na kisha yeye kuwa Mkatoliki kama alivyo Katarina na Adam…!

(3)

Joji aliamka mapema, baada ya kupata kifungua kinywa aliendelea na kusoma katika utafiti wake kama ada yake; alikuwa ana kitabu muhimu alikuwa anataka kukisoma nacho ni: 'Hekaya zilizokatazwa katika Torati' (*Forbidden Tales of the Bible* (Ballantine) and *King David)* mwandishi ni Jonathan Kirsch, alisoma maelezo ya jarida la Washington post kuhusu kitabu: "Mwandishi anatuambia katika kitabu hiki cha ajabu kuwa agano la kale limejaa baadhi ya visa vingi vyenye kutia hofu iliyo wazi katika fasihi ya magharibi ..vimefichwa kwa sababu ya urefu wa historia kwa sababu ni visa vyenye mshituko." Je inawezekana maaskofu na watawa wanajua zaidi kuliko Mungu kwa yanayowafaa watu wayajue na yale ambayo hayawafai? Alikuwa akijiuliza ndani ya nafsi yake: Ni hekaya zipi ambazo hazifahamu za

agano la kale (torati)? Na kwa nini zimefichwa? Na vipi? Je, inaweza ikawa ya kimapambano zaidi kama ilivyotokea na Levi huko nyuma? Aliamua kuanza kusoma kabla ya Tom kufika kwani ana ahadi nae leo hii.

Kitabu kilikuwa kimejaa uchezaji wa maneno ya tafsiri ili kuficha baadhi ya maudhui mbali mbali, bali katika kupunguza na kufuta nakala ambayo ipo katika lugha ya kiebrania; ili inasibiane na msomaji, kwa hoja ya kuwa itakuwaje tukawaruhusu watoto wetu wakasoma visa vya malaya, uchi na matumizi ya nguvu? Na wakati mwingine kwa madai kutoka kwa Khakhamat (wanazuoni wa kiyahudi) kuwa kitabu kitakatifu hakina maana ya kinachosema: Yote hayo yalikuwa ni majaribio yaliyofeli kuficha, kupotosha au kubadilisha andiko la asili, na swali lirudi katika akili yake: Je, hii ina maana kuwa wao wanajua zaidi kuliko Mungu? Au ina maana haitoki kwa Mungu? Au ni kuwa ilishaharibiwa na sio kutoka kwa Mungu?

Joji aliendelea kusoma katika hali ya mshangao na mshituko; ya kuwa kitabu hiki kitakatifu (agano la kale) inaaminiwa na dini zote za mbinguni (Uyahudi, Ukristo na Uislamu), na ukianza kukikosoa unakosoa dini zote za mbinguni; akasoma katika kitabu kisa cha Nuhu aliyelewa (aliyeleweshwa) akiwa uchi na akasoma kisa kichafu kuhusu jinsi baina ya Loti na binti zake, na jinsi binti zake walivyomlewesha baba yao Luti na wakakutana nae kimwili ili wahifadhi uzao wao bila baba yao kujua! au baina Reuben mtoto wa Yakubu na Bilha ambaye ni kijakazi wa baba yake…, nafsi ya Joji ilikuwa inajisikia kichefuchefu akisoma visa hivi vya kijinsia baina ya watu ambao hairuhusiwi kuoana, alishangazwa sana na visa hivi ambavyo vinasisimsha mwili wa mtu, iweje vifanywe na mitume ya mungu? Joji aliona uzito kukamilisha kusoma visa hivi..hadi alipofikia sehemu ambayo inazungumzia wasifu wa Mungu kuwa ni: "mungu mwenye hali yenye kubadilika badilika kama ilivyo zebaki, na mara nyingi anakuwa mvunjaji kuliko mhuishaji wa maisha". Alikuwa akiona kuwa ni wasifu mgumu, na ya kuwa hawezi kumuabudu mungu wa aina hii! Je, wanathubutu kumfanyia hivi Mungu?! Ama kwa hakika wanaoabudu ng'ombe wanamtukuza mungu kuliko hata wenye vitabu vitakatifu wanavyomtukuza mungu wao.

Joji alicheka huku akijilaza, akiwa anasoma hekaya za Tamari kahaba aliyetukuzwa! Na jinsi gani uzinifu ulivyotukuzwa maadamu unafanyika hekaluni sehemu ya ibada? Bali wengine wakasema labda ni mchamungu

www.path-2-happiness.com

mtawa, kisha ikaonekana kuwa huenda ni mke wa Yuda aliyezini nae, Joji alihisi kichefuchefu alipokuwa akisoma, na akahisi kuwa hawezi kuendelea kusoma hekaya na visa hivi, na akakumbuka fedheha za kijinsia za watawa na mapadri wa kikatoliki zilizoenea katika vyombo vya habari.

Alifunga kitabu na kufungua kompyuta yake, aliingia katika you tube na akaandika: Fedheha za jinsia za kanisa Katoliki", zikamjia idadi kubwa ya fedheha hizo za jinsia kwa njia za kawaida na za picha hali kadhalika. Alikuwa akijiuliza: Je, nikamilishe safari yangu ya kwenda Roma ili nijue ubaya wa Ukatoliki, niendelee kama alivyonishauri Adam na Katarina Wakatoliki wawili? Au niende kwa ajili ya matembezi tu ya kawaida na nisahau kabisa maudhui ya njia ya furaha? Lakini alikumbuka kama ataacha njia hii ya furaha bila ya shaka atarejea katika njia ya mashaka ambayo alikuwa akiishi nayo, au aelekee katika ukanaji mungu, fikra ambayo inaangamiza nafsi ya mwanadamu sawa na nguvu inayoangamizi akili na elimu, aliona kuwa fikra zile zinagongana akilini mwake, bali ya kwamba kila fikra kabla ya kugongana na fikra nyingine inaigonga kabisa nafsi yake na roho yake, na kuanza upya kumrejeshea maswali yake, hakuna kilichomkatisha katika hili isipokuwa sauti ya daktari ikisema:

- Joji..Joji hunisikiii?
- Haah, naam karibu
- Nazungumza nawe na wewe upo ulimwengu mwingine, ulikuwa unafikiria nini?!
- Katika maudhui ninayoichukia ?!
- Maudhui gani hayo?
- Nachukia migongano, na kwenda kinyume na mantiki na akili.
- Una maana gani?
- Umesikia kuhusu fedheha za watawa na mapadri?!
- Oooh, naam.
- Itakuwaje mtu ajitenge kwa kumuabudu mungu, huku wakati huo huo anawalawiti watoto baada ya hapo.
- Kama anavyokunywa pombe na kutumia madawa ya kulevya mtu kama daktari ambaye anajua hatari yake na madhara yake!
- Lakini mnamuonaje daktari ambaye anatumia madawa ya kulevya kama heroin huko kwenu?
- Huyu ni daktari aliyefeli, inafaa afukuzwe katika kazi yake na atangazwe!

- Na je, ikiwa kuna taasisi husika ambayo ina majukumu hayo ya madaktari na ambayo inawapa vyeo na kuwapandisha daraja kisha inawanyamazia, bali ndio ambayo inafanya magendo hayo ya madawa ya kulevya, na kuwafundisha namna ya kufanya, na sio hivyo basi mfumo wake na katiba yake inaruhusu hivyo!
- Hilo haliwezekani, lakini tukamilishe mazungumzo yetu, kama ni hivyo, basi hiyo ni taasisi ambayo inafumbia macho au kula njama, na hili ni jambo baya, je inapaswa watu walishwe kasumba hiyo miongoni mwa madaktari, au hospitali na fani yote ya tiba, unakusudia nini?
- Huoni kuwa mafundisho matakatifu yanawafundisha watawa mambo ya jinsi, uzinifu na uchafu hata kubaka?! Huoni kuwa vitabu vitakatifu vimejaa mambo haya hata kwa manabii?! Kwanini tusitengamane nayo kama usemavyo?
- Sijafahamu chochote, bali lililo sahihi sitaki kufahamu chochote kutoka kwako, Je, unataka tukane Mungu na dini? Katika ulimwengu wa tiba sisi tunafahamu kuwa wengi katika madaktari ni watu waliokana Mungu hata madaktari bingwa miongoni mwao wanakaribia kuwa ni wagonjwa wa nafsi, au niache niseme: Kwa uchache wao ni watu wasiokuwa na furaha katika maisha yao, ukitaka nasaha zangu kimbia na nafsi zako na fikra zako hizi hata kama umekinaishwa nazo, toroka kwa njia yoyote ile..kama utacheza na pombe au wanawake au jambo lolote lile.
- Je inawezekana tukazikimbia nafsi zetu halafu tukapata hisia za furaha?!
- Kwa bahati mbaya hilo haliwezekani kabisa, lakini tabu hizi huzingatiwa kuwa ni neema kulinganisha na tabu ya kumkana mungu na kuwa mbali nae…samahani kwa kukatisha mazungumzo matamu kama haya, lakini mimi nimekuja kukujibu swali au maelekezo ya kitiba tu kuhusu hali yako, na kwa kuwa utaondoka jioni hii, nakushauri ufuatilie sana joto lako kwa muda wa siku mbili hizi zijazo, je unalo swali lolote? Swali la kitiba tu?!
- Hapana asante..je baada ya siku mbili hizo niendelee kuangali hali ya joto langu?
- Hapana, siku mbili zijazo tu kwa akiba, na kama itakuwa imetulia, basi itakuwa ina maana kuwa utakuwa umerudisha afya yako kamili.

Tom aliingia na akatoa salamu kwa daktari na kwa Joji..daktari akaomba ruhusa ili aendelee na kazi zake, Joji akamuanza:

- Kuna swali lisilokuwa la tiba je utaniruhusu?
- Kwa sharti liwe la haraka, ehe.
- Kwa kuwa unajua kuwa kukimbia hakutupi sisi furaha. sasa kwa nini tunakimbia?

www.path-2-happiness.com

- Kuhofia ukanaji mungu, kwani huko ni kupata tabu kwa muono wangu kwa uchache.
- Hivyo basi ima mtu akane mungu au atoroke? hakuna chaguo la tatu?!
- Huenda ikawa kuna chaguo la tatu, lakini sijalijua, ukiifikia hilo nitafurahi na nitakushukuru sana, haya naomba ruhusa na kama una swali lolote la tiba kabla ya kutoka kwako unaweza kumuuliza nesi naye atanipigia, kwa heri.

Tom alimuangalia daktari akitoka, kisha akamgeukia Joji na kusema.

- Joji sijui mlikuwa mkizungumza nini lakini mimi najua tabu na huzuni na humumi anayopata mkanaji mungu, nadhani kuliko mtu mwingine yoyote.
- Kwanini ukanaji mungu una tabu kama msemavyo?
- Katika jambo gumu sana ni kukosa wa kumtegemea, na kumuachia mambo yako, na kujua kutoka kwake njia yako.
- Nitajuaje kwake njia yangu?
- Kupitia mitume yake kwetu na vitabu vyake.
- Je, unatarajia njia yangu ya maisha nielekezwe na mtawa kahaba na padri mbakaji?
- Sifahamu?
- Je, njia yangu ya maisha itaelekezwa na nabii mlevi mzinifu, au kitabu cha jinsi kitakatifu?
- Una nini Joji? Kwa nini leo unazungumza hivi?
- Tom nimechoka, ninafikiri kwa kina nisisafiri kwenda Roma, au nisafiri kwa ajili ya matembezi na utalii tu.
- Kwa nini, kuna mpya gani?
- Hakuna mpya, lakini nimesoma na nimeona mambo ya jinsi na matumizi ya nguvu katika torati na biblia.
- Kwani hili ni jambo la kipekee kwa Katoliki?!
- Una maana gani?
- Je matumizi ya nguvu yaliyomo kwenye Uprotestant si kama hayo na zaidi ya hayo?! Unajua ni nani aliyeuwa watu huko Ujerumani na sehemu zinginezo katika mauaji makubwa ya kihistoria?
- Ndio, Uprotestant, lakini nimechoka, huenda hata Uprotestant haufai!
- Joji kuwa ni mwenye nguvu kama ulivyotuzoesha, ole wako na udhaifu, ukisubiri na kushikilia ulitakalo utafikia njia ya furaha, na ukishindwa na ukidhoofika utakuwa kwenye tabu, na huzuni mbali mbali.
- Nifanye nini?

- Sijui, ninachokifahamu ni kuwa Mungu hawezi kuficha njia ya kumfikia.
- Njia hii iko wapi? Je si kwamba wakristu na waislamu wanaamini agano la kale? Kitabu kile chenye mambo mengi ya jinsi na matumizi ya nguvu, nilikuwa simuamini Levi alipokuwa akizungumza katika hili, lakini nimekinaika sasa na alichokuwa akikisema, je unataka nikupe dalili katika agano la kale?!
- Sihitajii hilo, lakini ukitaka nikupe dalili katika agano jipya naweza.
- Kwa nini basi unataabisha nafsi yako kwa kuutafuta Ukristo na Uislamu wakati zote zipo katika njia moja?
- Tulikubaliana tokea mwanzo kuwa twende katika njia ili tupate ukweli, wala sijui kwa nini nahisi kuwa tumekaribia kufikia kwenye njia, usikate tamaa au ukasalimu amri mwisho wa mashindano..Joji wewe hutafuti au kwenda kwenye njia hiyo kwa ajili ya nafsi yako tu, mimi nipo pamoja nawe, kwani masomo yangu na utafiti wangu sasa ni huo huo, naamini hakika tutafika, lakini usiniulize vipi?
- Nami nina hisia kama hizo, lakini mara nyingi nina hisi kuwa labda naichezea nafsi na roho yangu, vinginevyo dalili zote zinathibitisha kuwa nimepotea njia, pamoja na kuwa ndani ya nafsi yangu nahisi kuwa nimekaribia.
- Safiri kwenda Roma uujue Ukatoliki na Uprotestant kwa karibu, kisha angalia na ufanye mazungumzo katika ulichosoma, wala usichukue maamuzi yoyote hadi umesoma dini zote za mbinguni.
- Na ufanye utafiti katika Uislamu hali kadhalika?!
- Ndio bila ya shaka, kutafiti kitu si kwamba umeamini, je, si umefanya utafiti na kusoma kuhusu Ubudha, Uhindu na Uyahudi? Kuna mpya gani basi? Je hatukukubaliana hapo mwanzo kuwa tuwache kuhukumu jambo hadi baada ya kujua na kutambua dini zote za mbinguni?!
- Nitakamilisha, ingawaje sioni mbele yangu sasa ila ni kikwazo cha ushirikina, matumizi ya nguvu na jinsi na upotoshaji katika fikra na dini mbali mbali zilizoondoka na kubaki, pamoja na imani iliyomo ndani ya nafsi yangu kuwa nitafika katika njia ya furaha.
- Weka fikra yako zaidi kuwa utafika katika njia ya furaha, kama kufika kwenyewe kuko wazi na kwepesi tusingehitaji kukutafuta!
- Nitafika, na huenda nikashtushwa kuwa suluhisho lililo jirani yangu ni jepesi na lipo wazi, lakini sikuweza kuliona.
- Huenda njia hiyo ikawa Ukatoliki au Uprotestant ….au Uislamu.

www.path-2-happiness.com

- Pamoja na kukinai kwangu kuwa njia zote hizi zimejaa ushirikina, udajali, na dini kunyonya watu mali zao, jinsi, lakini tutakamilisha, unaniusia nini?
- Je umesoma vingi?
- Ndio, sikuchoshwa ila kwa kusoma kwangu kwingi, kwa munasaba: Ukatoliki haututaki tusome hata kitabu kitakatifu ila kwa maelezo ya Papa, kilicho katika kitabu kitakatifu ni lazima tukifahamu kama anavyofahamu Papa?! Na wanataka tuhamishe akili zetu.
- Swadakta, lakini Waprotestant wanataka kutunga dini watakavyo, na kufahamu kama wanavyotaka na ndio maana ikagawanyika sana.
- Bali asili ya agano jipya imejaa upotofu mwingi, iwe ni sawa tumeifahamu kama atakavyo Papa au kama tunavyotaka sisi nayo bado imepotoka, je sikukuambia kuwa dini zote hizi hazifai na kuwa zote ni ushirikina tu?
- Vizuri, soma sana, jifunze sana, jadiliana sana, funguka zaidi, baada ya hapo utaiona njia.
- Lakini Ukatoliki imesimama juu ya siri mbali mbali ambazo hazipasi mtu kuzijadili, siri za kanisa saba ambazo hazifahamu ila mtawa tu!! Na kuzijadili na kufikiria au kuzipinga ni kufanya kufuru, pamoja na kuwa zinakwenda kinyume na akili au mantiki!
- Hata Waprotestant wanaamini siri mbili miongoni mwa hizo saba.
- Je, huoni kuwa kila nikikuambia kitu unaniambia: Hata Protestant ni hivyo hivyo? Je, umeshakuwa ni Katoliki baada ya kufuatana na Katarina kwenda kanisani? Ninafahamu vizuri usemavyo, lakini mimi nazungumzia Ukatoliki.
- Sitaki uelemee upande mmoja na kupendelea dini bila ya elimu wala kutumia akili, ikiwa ni kwa akili na kwa elimu sema utakayo bila kupendelea upande mmoja na kuwabebesha wengine mzigo.
- Ninayosema ni kutokana na elimu na kutumia akili.
- Na hata ninayosema mimi ni vivyo hivyo kadhalika, nilitaka uwe unaweka mizani ya mambo vizuri zaidi.
- Ah ah..swadakta, huenda nikaegemea zaidi kwa Ukatoliki, pamoja na kuwa mengi nisemayo kuhusu wao yapo katika Uyahudi na Uprotestant; bali nadhania hata kwenye Uislamu kadhalika.
- Kama ni hivyo tuache tukamilishe safari yetu ya uvumbuzi kwa utulivu kama tulivyoanza, hadi hapo mambo yatakapotubainikia zaidi..si wewe uliyeniambia: 'Kwa wepesi bila ugumu'?

- Ndio, hii ni katika sentensi za Adam zilizokuwa mashuhuri.
- Kama ni hivyo basi ni kuwa, kila mtu anapokuwa mtulivu kila anapokuwa mizani yake ni nzuri na akaweza kuitumia akili yake vizuri zaidi. Kama ambavyo mimi tokea mwanzo nilikuwa ninakulingania kuwa na ufahamu wala usichukue maamuzi yoyote kwanza hadi mambo yote yatakapokuwa wazi kwako, kwani huenda ukachukua maamuzi ikawa njia hiyo ni Uyahudi kwa mfano, kwanini haraka basi?
- Kwa wepesi siwezi kuamini kuwa ikawa ni Uyahudi kwa hali yoyote ile, mimi nachukia sana matumizi ya nguvu, na Torati imejaa matumizi ya nguvu, hebu fikiria kuwa katika agano la kale: (Maluuni anayeinyima panga lake damu) na (Amesema Mola Mungu wa Israel: Kila mmoja wenu na abebe upanga wake na azunguke mitaani mlango kwa mlango, na amuue ndugu yake, rafiki yake na jirani yake), ugaidi gani namna hii?!
- Je, Wakristo na Waislamu nao si wanaamini agano la kale?! Kuwa mpole zaidi, wala usihukumu hadi mambo yote yatakapokuwa wazi kwako, nami nina hakika kuwa utafika kwenye njia ya furaha.
- Hili ni tatizo kubwa katika dhana yangu, Wakristo wanaona kuwa agano jipya ndilo lililokamilisha agano la kale, na Waislamu kadhalika, zote kwa hakika ni dini za mabavu na kigaidi.
- Hapa kuna nukta mbili: Ya kwanza haifai kuwa na dhana katika mambo haya, bali rai yako inabidi ijengwe kwa elimu, Pili: Natamani uwe makini zaidi na ufanye uchunguzi wa kina, ina maana gani kuwa agano jipya linakamilisha agano la kale? Je ina maana wao wanaamini au hawaamini?
- Naafikiana nawe katika uliyosema, dhana sio elimu, kama ilivyo kuhariri jambo na kulifanyia uchunguzi wa kina ni muhimu sana, lakini kwa bahati mbaya Wakristo hawakuliweka vizuri istilahi 'Linakamilisha' kwa uwazi, na si mimi ndie ambaye sijalihariri, Kwa mfano Ukatoliki unawakataza wafuasi wao katika kulifahamu hata hili agano jipya, na wanaona kuwa ni haki ya watawa kuifahamu tu, na wanawaelezea watu wengine kama mimi na wewe, kwa mfano kama unavyofahamu andiko la agano jipya katika Mathayo Mtakatifu 10:34: (Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! sikuja kuleta amani, bali upanga), au (ama maadui zangu ni wale ambao hawakutaka niwamiliki, nileteeni mbele yangu na muwachinje).
- Na wewe unajua kuwa Wakristo wana maelezo ya kauli kama hizi.

www.path-2-happiness.com

- Ndio tuna maelezo na tuna maandiko yaliyo kinyume yake ambayo yanalingania huruma na mapenzi, pamoja na hizi tafsiri kutotumia mantiki ila ni kuwa yatabakia kuwa ni maelezo yake, hata hivyo tafsiri hizi hazilingani na imani yetu ya agano la kale yaliyojaa mambo hayo, na matendo yetu kwa bahati mbaya yanathibitisha hayo, sin a wengine tu, bali hata baina yetu sisi, je, unataka nikutajie hayo kwa mfano katika mambo ya unyama wetu?!
- Haya sio maudhui yetu sasa, acha tuweke kila kitu sehemu yake, na tuangalie kwa mtazamo wa jumla, kusoma dini yoyote ile ni vizuri mtu akaangalia misingi ya dini kama vile: Mungu wao, Mtume wao, kitabu chao, itikadi yao, hukumu zao mbali mbali, historia yao, hali yao halisi, na katika kusoma hayo ni vizuri umuhimu zaidi ukaupa katika kusoma mambo kwa ujumla wake na sio mambo madogo madogo.
- Vizuri, vipi hivyo?
- Badala ya kuiangalia sana kwa makini kauli fulani iliyopo kwenye agano la kale au jipya na tafsiri zake mbali mbali, tuangalie kitabu kitakatifu muono wa jumla kulingana na usahihi wa kutufikia, na mwandishi wake na kinacholingania, itikadi zake kuhusu mungu na manabii wake, na baada ya hapo nukuu za maelezo ya ndani yatabaki kuwa ni ushahidi wa kuthibitisha asili yake.
- Vizuri sana, pamoja na kuwa nimesoma sana kuhusu hayo, lakini hata hivyo naweza kuangalia upya hayo ili nisome zaidi na kujadili zaidi.
- Ili uweke wazi hili tujaalie kuwa umemaliza maudhui kuhusu Uyahudi kama usemavyo, hivyo ni kuhusu vitabu vya agano la kale? Ni nini kinalingania? Na nini mtazamo wake kuhusu Mitume ya Allah?
- Tujaalie kuwa inatoka kwa Mungu.
- Kwani Mungu ndiye aliyeandika? Je aliandika Mtume Musa? Je aliandika Harun? Je unamjua aliyeandika?
- Ninadhani mfano wa haya utasema kwa agano jipya?
- Bila ya shaka, vinginevyo utaelemea upande mmoja, njia hii ya kufikiria ipo karibu katika kutufikisha katika njia ya furaha, vinginevyo tutashughulika na vitu vidogo vidogo ambavyo kuna kuchukua na kurudisha.
- Fikra nzuri, nakubaliana nawe kuhusu hilo.
- Na baada ya kurudi kwako kutoka Roma tutakuwa tumeshatathmini dini mbili muhimu katika dini za mbinguni, itabakia moja na sura itakuwa wazi zaidi kwetu, na hivyo basi safari yetu ya uchunguzi kutafuta njia ya furaha itakuwa imekwisha.

- Ikitubainikia kuwa zote hazifai?!
- Kama ningekuwa kama nilivyo hapo kabla ningekuambia turejee kwenye ukanaji Mungu, na mimi sikukutaka uchukue njia hii kisha tena urudi kwenye ukanaji Mungu, lakini sasa ninasema kuwa lau ikitubainikia hivyo kuwa zote hazifai tutarudi na tutapanga kazi zetu kwa ukamilifu tokea mwanzo, na tutaanza tena tokea mwanzoni na kujiuliza swali: Je, dini ni jambo la msingi? Kisha tutawezaje kuchagua dini? Na hivyo hadi tufikie tulipofikia sasa, wakati huo mambo mengi yatakuwa wazi kwetu.
- Safari ni ndefu sana.
- Sitarajii kama tutarudi tena, natamani hilo, lakini swala hilo linaungana na elimu, kwa maana kila tutakapoongeza elimu tutaongeza uoni, na kinyume chake kila tutakapokuwa vipofu wa baadhi ya maeneo ndio ujinga utazidi na kutuweka mbali na kufikia majibu ya maswali yetu, na hivyo basi kuwa mbali na njia ya furaha, mimi nina hakika kuwa utafika, lakini subiri kidogo.
- Nitafika sina ujanja katika hilo, kisha akatabasamu na kusema: Kikubwa ambacho kinanichosha ni kuwa sioni njia ya kuelekea.
- Njia ya kuelekea njia tunayoikusudia iko wazi, lakini tunachokiona ni njia, na watu wengi wanadhani kuwa njia ya kuelekea njia ni sehemu ya njia ambayo wanaitafuta na hawajaiona.
- Falsafa nzuri, lakini nibainishie mimi uwazi wa njia ya kuelekea njia.
- Je, hujui kuwa tokea mwanzo ulifuata njia ya ukanaji mungu na usekula? Kisha ukaachana na njia ya dini za ardhini (za wanadamu)? Kisha ukafadhilisha dini za mbinguni? Je, haikuwa hivyo?
- Nakubaliana nawe kabisa, lakini ambacho hakipo wazi kwangu ni vipi tutaweza kukifikia?
- Hili ndilo nililokuambia, kilichokuwa sicho wazi kwako ndio njia, na sio njia ya kuelekea njia.
- Hahaha, vizuri lakini hebu tulivuke hilo, unaninasihi nini katika safari yangu?
- Nakuusia Kwanza: Jisikie furaha kwenye safari yako, na watembeze wanao, unahitaji upumzishe akili yako, na upange maarifa uliyokusanya yapate kukusanyika vizuri pamoja na mijadala yako. Pili: Endelea kusoma na kufanya mijadala, lakini kwa akili iliyofunguka na jali mambo muhimu na ya msingi. Tatu: Zidisha kutaamali katika mambo ambayo yatakusaidia katika kushusha na kupanga maarifa yako, na kukusaidia katika kumakinika katika mambo ya msingi.

www.path-2-happiness.com

- Vizuri, naamini kuwa ni wasia muhimu sana na nitajitahidi sana kuufuata, pamoja na raha niipatayo katika kutafuta majibu ya maswali yangu, ila sasa nimekuwa mtu makini zaidi.
- Umakini sababu yake inatokana na msukumo wa kila mara katika akili yako, msukumo wa maarifa mbali mbali, msukumo wa wanaokuzunguka, hivyo basi mizigo yako imekuwa ni kubwa, hivyo punguza mizigo yako kwa wasia niliokupatia.
- Ndio, nitafanya hivyo, hata watoto wangu nimewaahidi hivyo.
- Safari njema, tutaonana utakaporudi, ukiwa mchache wa mizigo uliyonayo, na mwenye maarifa mengi zaidi, na kufunguka zaidi.
- Vipi Tom kuna habari gani kuhusu Baraad?
- Inaelekea kuwa maudhui yale yanasonga mbele, ameanza kunitishia sasa bila kujali picha alizonazo pamoja na aliyoyarekodi.
- Kukutishia!
- Ndio, anazo picha za zamani ambazo si nzuri za baadhi ya wagonjwa wangu, na amerekodi baadhi ya vikao vyangu, na ameanza kunitishia kwa hayo, vinginevyo atavifikisha katika tume ya tiba na chama cha madaktari.
- Itakudhuru nini kama atapeleka katika taasisi husika ?
- Leseni yangu ya fani ya udaktari itafutwa, mbali na fedheha.
- Anataka kuingia katika makubaliano ya nini?
- Nifanye naye kazi.
- Katika nini?
- Hahaha, katika kuuza mihadarati, na kutekeleza anayotaka mimi nifanye.
- Kufika katika vyama ni bora kuliko kuwa muuza mihadarati.
- Swadakta..lakini nikifukuzwa kwenye kazi yangu itakuwa ni balaa kubwa vile vile.
- Utafanya nini?
- Sijui, lakini nitapanga mambo yangu, naomba ruhusa, kwaheri.

Joji alirejea kusoma akifurahia kikao chake na Tom alihisi kuwa amepata tumaini na kutulia baada ya kukutana nae, moyo wake ulifunguka baada ya mazungumzo nae, na akaamua kufanya aliyomuusia kadiri awezavyo. Hata hivyo akili yake ikaanza kushughulishwa jinsi gani atamsaidia Tom kwa tatizo la Baraad baada ya kuamini kubadilika kwa Tom hakutaka kumuacha peke yake, lakini anaweza kufanya nini?

Alipokuwa akifikiria tatizo la Tom..alifungua barua pepe yake, na kukuta barua mbili kutoka kwa Habiib na Levi wakitaka kujua afya yake, akawajibu:

"Mpenzi Habib

Nilifanya operesheni yenye mafanikio, nakupa bishara kuwa hali yangu ni nzuri wa afya, baada ya siku mbili nitasafiri kuelekea Roma, ni kiasi gani nilitamani lau ungekuwa kule; ukanifasiria kwa elimu uliyokuwa nayo na akili yako iliyofunguka baadhi ya yanayonitatiza katika Ukatoliki.

Wako:

Joji."

"Rafiki yangu Levi,

nilifanya operesheni yenye mafanikio, nakupa bishara kuwa hali yangu ni nzuri wa afya, baada ya siku mbili nitasafiri kuelekea Roma, ni kiasi gani nilitamani lau ungekuwa kule; ukanifasiria kwa elimu uliyokuwa nayo na akili yako iliyofunguka baadhi ya yanayonitatiza katika Torati na katika Uyahudi.

Wako: Joji"

Wakati alipokuwa akimalizia kuangalia barua pepe mara akaingia Katarina..

- Tumeanza taratibu za kutoka kwako, baada ya muda mfupi Mungu akipenda.
- Natamani nyumbani, kuwaona watu na gari.
- Muda wa kutokuwepo kwako ulikuwa mzito kwangu na kwa watoto. Ama wewe ulikuwa umeshughulishwa na kusoma kwako na mjadala wako, je Tom alikuja?
- Ndio, kilikuwa ni kikao kizuri.
- Je sikukuambia hilo?
- Nasaha zako daima ni zenye faida, la msingi ni kuwa muda gani tutatoka?
- Baada ya muda mfupi tu, namalizia baadhi ya karatasi, nitakwenda kukamilisha sasa kisha nitarudi ili tuondoke na huko njiani niambie kilichotokea baina yako na Tom leo?

(4)

Kabla ya muda wa safari kwenda Roma kwa masaa mawili familia iliondoka kwenda Uwanja wa Ndege, walipanda ndege kwa wakati muwafaka kabisa uliopangwa. Katarina aliipangilia safari hii ya Roma kwa uangalifu, aliweka nafasi Raphael Hotel ambayo umbali wake na Piazza Navona n barabara moja tu, inayosifika kwa kuonyesha mandhari yote ya mji wa Roma, kanisa la Saint Peters hadi hekalu la Pantheon, vile vile inaangaliana na njia za usafiri wa

www.path-2-happiness.com

mabasi na sehemu takriban zote zenye kuvutia za historia katika mji wa Roma kwa masafa madogo sana kiasi cha kuweza kutembea kwa miguu..

- Katarina uchaguzi wako ni mzuri sana.
- Mama asante sana, chunguza ipo jirani na ngome ambayo tunataka kuiangalia.
- Wala haipo mbali na Trevi Fountain ambayo unaitaka vile vile kuiangalia Sali.
- Sasa ni saa moja usiku, mnaonaji tufurahishwe na mandhari ya hoteli kwanza, kisha tule chakula cha usiku, halafu tupumzike; tuanze na ratiba yetu kesho asubuhi tukiwa tumechangamka.
- Sawa baba..

Familia iliamka mapema na kula chakula cha asubuhi hotelini, kisha wakaondoka pamoja na muelekezaji watalii hadi katika uwanda mpana uliopo karibu na hapo sehemu iliyojaa sehemu za kihistoria za kitalii, familia ilikuwa katika hali ya furaha sana wakiwa wanaangalia majengo ya Kiroma ya zamani, pamoja na sanamu mbali mbali, makanisa yenye majengo yenye kupendeza, ambayo unapata hisia za heshima na maana kamili ya historia.

Ilifika wakati wa chakula cha mchana; walikwenda kwenye mgahawa mpya wa kitaliano ambao upo katika staili ya kiroma..…

- Baba sikujua kabisa kuwa ustaarabu wa kiroma upo katika uzuri na nguvu kiasi hiki!
- Ustaarabu wa kiroma ni wazamani sana ewe Maiko, ni katika staarabu kubwa kabisa Ulaya baada ya ustaarabu wa kigiriki, ilikuwa inatawala kisiwa chote cha Italia mwaka 275 BC, na kwa karne mbili zilizofuatia Roma iliweza kujenga na kusimamisha dola iliyotawala ulaya nzima na kaskazini ya Afrika vile vile, na kadhalika utamaduni wa kigiriki pia ulimezwa
- Kikubwa kinachotowa wasifu wa Roma ni hii Pizza, na sio masanamu yaliyopo nje.
- Je, Maiko unayapenda masanamu haya?
- Ni majengo mazuri sana.

Katarina kwa tabasamu zuri:

- Ni uzuri ulioje wa sanamu la Yesu na bikira Maria!
- Sijui kwa nini sanamu hizi na sanamu za Yesu zinanikumbusha sanamu za Budha

na wengineo katika sanamu mbali mbali huko India? Na nahisi kuwa zote ni moja.

- Achana na hili kwanza, tukimaliza kula tutakwenda upande wa pili wa Uwanda huu.

Joji alifahamu kuwa Katarina hapendi mjadala huu mbele ya watoto na hivyo akaheshimu rai yake, lakini ndani ya akili yake, hakuweza kuacha kutofautisha kati ya sanamu la Yesu na sanamu la Budha, bali itikadi za kishirikina na za kipagani na itikadi za kikatoliki.

Familia ilimaliza matembezi yake ya kitalii, na wakarejea hotelini baada ya kuzama kwa jua kwa muda mdogo tu, walikula chakula chao cha usiku wakiwa hotelini, na mwisho walipanda vyumbani kulala. Joji alifungua barua pepe yake akiangalia barua mbali mbali, akakuta barua ya Habib:

"Joji

nakuandikia barua hii nikiwa pamoja na Levi, tumesoma barua yako tukiwa na furaha kwa kufanikiwa kwa operesheni yako, tutasherehekea baada ya muda mdogo tu, ama kuhusu kile kinachokutatiza kuhusu Ukatoliki au Uyahudi sisi tutafurahi kama tutajadiliana kuhusu hilo, bali tutafurahi hata kujadiliana kuhusu Uprotestant na Uislamu, tunasubiri tuanze mazungumzo hayo pamoja nawe.

Habib na Levi."

Tanbihi kutoka kwa Habib: Usisahau kumtembelea Papa katika misa ya Jumamosi.

Joji akawajibu:

"Hallo Habib na Levi

Mimi nipo Roma sasa, nchi ya Wakatoliki, na karibu na Vatican ya Wakatoliki, nimefurahi kwa furaha yenu, kuhusu tatizo nililonalo nitatoshelezwa kwa kuwatumia andiko, na nitasubiri maoni yenu juu yake kwa ufupi sana..kadhalika nitawatumia paragrafu kuhusu kitabu "Hekaya zilizoharamishwa katika Torati" iliyoandikwa na Jonathan .., na paragrafu inazungumzia kuhusu torati au agano la kale na andiko lenyewe ni hili:

Tokea mwanzo hadi mwisho kitabu kinaelezea kuhusu tabia mbaya zenye kutisha na kuharibu maadili kulingana na alichokiandika Michelle Fintora (mwandishi wa habari) ambaye alichanganyikiwa pindi alipoona katika torati "Wanawake wanaolewa na nyoka, ndugu wanauana wenyewe kwa wenyewe, mataifa yanachinja

www.path2-happiness.com

bila msamaha wowote, makabila yanaimba nyimbo za kubembeleza juu ya vichwa vyao majangwani, watoto wanaonyonya wanahama, mauaji yanayofuata utabiri, na utabiri unafuatia mauaji, wachezaji dansi wanadai vichwa vya manabii.” Fintura anafikia katika hitimisho na kusema: Kwa hakika jamii yoyote inayoipa hadhi Torati kama ni kitabu kitakatifu jamii hiyo itajiweka katika wazimu, kinachochekesha katika alichoongeza: “Ukitarajia ustaarabu ambao utategemea kitabu hiki, jamii hiyo haitokuwa isipokuwa ni jamii ya wanyama na ya waharibifu” Je, mnakubaliana na Fintora au hapana? Pamoja na tanbihi kuwa dini zote za mbinguni zinaamini kitabu hiki kitakatifu?!

Wasallam, wenu

Joji”

Aliamua vile vile kutuma maandiko haya kwa Adam na Tom katika barua moja, kisha akakaa akifikiri: Je anakubaliana na Fintora kuhusu alichosema? Ili ajadiliane kuhusu fikra hii kwa atakayekutana nae kesho kulingana na jeduali alilopanga Katarina..

Baada ya chakula cha asubuhi, Katarina aliondoka na watoto kuelekea sokoni wakati ambapo Joji alimsubiri John Luke Franco, kulingana na ahadi aliyoweka Katarina. John Luke alikuwa ni mwandishi wa kitaliano, alikuwa anafanya uchunguzi kuhusu Ukatoliki na Uprotestant kwa kadiri Katarina ajuavyo. Katika ahadi iliyopangwa saa tano asubuhi John luke alikuwa ameshafika hotelini, Joji alimkaribisha na akajibu kwa salamu yenye uchangamfu kabisa na kuanza kuzungumza nae:

- Kulingana na kilichonifikia kutoka kwa askofu mmoja wa marafiki zangu ni kuwa wewe unatafuta majibu ya maswali makubwa? Na ya kuwa mke wako kasisi aliwasiliana na rafiki yangu padri Luogi Stefano na akamjulisha hilo, niache nijitambulishe.
- Mke wangu sio kasisi, atakuja muda si mrefu, nimefurahi kukutambua, karibu.
- Mimi ni mwandishi wa habari hapa Italia, nimesoma falsafa chuo kikuu na nimeipenda mno, kutokana na maswali muhimu ya wanafalsafa, kisha akatabasamu na kuendelea kusema: Kwa wenye akili bila shaka, ni maswali makubwa kuhusu maisha; nimefanya juhudi kubwa kutafuta majibu ya maswali haya.
- Kwa hivyo basi umeongea na Padri aliyeongea na Katarina.
- Ndio

- Nini matokeo ya utafiti wako wa miaka mingi?
- Ha ha ha..nimefikia katika matokeo muhimu sana na nukta fulani maalum.
- Vizuri sana, ni zipi hizo?!
- Rahisi, hamna kitu! Kwa sababu nilichokuwa nacho ni kukosoa ukweli unaosikitisha wa dini mbali mbali, lakini haukujengwa kwa fikra iliyokamilika.
- Unaweza kunisaidiaje na hujapata chochote katika matokeo ya utafiti wako?!
- Kwa hakika mimi nina uzoefu wenye faida kubwa sana ninaweza kukusaidia, kama ilivyo ninaweza kufaidika vile vile na uzoefu wako, lakini matokeo ya utafiti wangu wa kujibu maswali kwa masikitiko hamna kitu!
- Je unaamini kuwa inawezekana majibu yakawa hamna?
- Wewe ni mtu unayeangalia vitu kwa kina na kwa wepesi kabisa kwa wakati mmoja, vizuri kabisa kamilisha.
- Nikamilishe nini? Mimi nakuuliza unijibu.
- Majibu yako wazi, ndio maana sikujibu, hakika kabisa ni kuwa majibu hayawezi kuwa hamna kitu, hivyo kamilisha (utafiti wako)
- Kwa maana hiyo kuna majibu na wewe hujayafikia?
- Sehemu moja ya akili inasema kuwa kuna uwezekano wa kupata majibu na kuna uwezekano vile vile majibu yasiwepo.
- Sidhani kuwa akili inaweza isipate majibu, kwani huu ni muktadha wa kuwa wanadamu wanaogelea katika upotofu, na ambayo inapelekea kuzaa nadharia za kizembe na zisizokuwepo na za hovyo.
- Wewe ni mwanafalsa mzuri kabisa, hii ndio rai yangu vile vile, lakini nimesema nilichosema nione utasema nini, lakini kwa rai yako nitapata wapi majibu ya maswali yangu kama hali ni hiyo?
- Mimi nimetafuta na hadi sasa sijapata, nini rai yako wewe?
- Baadhi ya marafiki zangu wakanao dini na Mungu walijaribu kunishawishi na kunikinaisha kuwa maisha hayana uhusiano wowote na Mungu, na kuwa majibu ya maswali yanaweza kuwa kwa njia ya kielimu yenye kupimika, au kwa bahati tu.
- Vizuri. Je walijibu maswali yako?
- Ukanaji Mungu ni falsafa iliyopotea au isiyo na mashiko, haiko mbali na

www.path-2-happiness.com

kufanana visa, ngano, ushirikina, hata ikivaa mavazi ya kisomi na kutumia fikra, niamini ukanaji Mungu naufahamu vizuri kabisa na nimejadiliana na watu wengi miongoni mwao.

- Inaelekea umeegemea upande mmoja na kuwapa lawama wakanaji Mungu na masekula.
- Nahofia usije kuwa mkanaji Mungu; na ndio maana unawatetea, lakini nitazungumza nawe kwa uwazi, nipe fursa hiyo. Kila mkanaji Mungu anajua ndani ya nafsi yake kuwa ana makosa, mimi nilikuwa miongoni mwao, na nimeishi muda wa umri wangu katika ukanaji Mungu, hali hii ya ukanaji Mungu ni aina fulani ya kutoroka matatizo ya dini mbali mbali wala hawana falsafa ya kuwatetea au nadharia au hata dalili za kiakili au kielimu. Ama usekula wao wanaamini dini, lakini kazi yako kubwa ni kuwa iwe mbali na maisha kwa sababu ile ile waonayo wakanaji Mungu.
- Vipi, sijafahamu?
- Tatizo la ugomvi na mvutano baina ya dini na elimu ni tatizo kubwa tokea zamani, zinapogongana dini na elimu, watu wanaipa elimu nafasi kubwa na kuisadiki kuliko dini.
- Je elimu zetu zinaweza kuwa ni bora kuliko elimu aliyoleta Mwenyezi Mungu?
- Bila shaka hapana, je Mungu anaweza kuleta kitu au kikashuka kutoka kwake kitu chenye makosa au kisichowezekana?
- Unakusudia nini?
- Kwa yale wanayosoma watu au kusikiliza katika wasia wa kitabu kitakatifu kuwaamrisha wao kuuwa au kuzini au kunywa pombe, nao wakiwa na hakika kabisa ya madhara ya vitu hivi kiakili, kimaadili na kielimu, unataka wafanye nini?
- Kama ni hivyo wewe umefika katika usekula ili uitulize nafsi yako na majibu ya maswali makubwa.
- Kwa masikitiko…Usekula hautulizi chochote kabisa, lakini nazungumza na wale ambao wameamini usekula, unatoa suluhu tu ya mgongano wa dini na elimu, na kutatua tatizo la kihistoria tu, ama ukitaka ukweli ni kuwa Usekula unanasibiana sana na dini ya Ukristo.
- Vizuri, nibainishie hii nukta ya mwisho.

- Njia ya Upapa au mfumo wake ni njia ambayo inaweza ukafanya chochote kile; inaweza kukuuzia cheki ya msamaha na hivyo matatizo yako yakaisha; na hivyo basi unaweza kufanya chochote ukitakacho mbali kabisa na dini, kisha baada ya hapo ukanunua tena cheki ya msamaha.
- Lakini Uprotestant hauamini hivyo, au siyo?!
- Ndio, huenda ikawa hivyo kwa sababu hawaamini sana, na sio kwa sababu hawatenganishi dini na maisha, bali wao ndio wanatenganisha rasmi kabisa, hivyo basi linganio kubwa la Usekula bali hata la ukanaji Mungu linatoka Kanisani!
- Wewe unalingania nini?! Katika dini gani?! Mara unatetea ukanaji Mungu, mara nyingine unautetea usekula na wakati mwingine Ukatoliki!
- Mimi sipo popote pale, sijakuambia kuwa sijapata matokeo yoyote? Na wewe je?
- Mimi ni Mprotestant, kwa sababu baba yangu na mama yangu walikuwa hivyo, kisha baada ya hapo hamna kitu!
- Ha ha ha…kwa maana hiyo sisi tunafanana.
- Je umeridhika kuwa hujafikia matokeo yoyote? Au unahisi kutofikia chochote ndio umeshafika?
- Hakuna kitu hakifikiwi! Na huenda haya yakawa ndio sababu ya kuanza na kukuwa kwa madhehebu ya kijinga na ya kipuuzi huku kwetu nchi za magharibi.
- Mielekeo ya kipuuzi!
- Ha ha ha, ndio makundi na madhehebu ambayo yanajenga dini yake pasina kitu au katika upuuzi mbali kabisa na dini.
- Kama ni hivyo hili ni balaa la hakuna kitu.
- Bali balaa ni kuwa maswali kuhusu maisha hayajajibiwa bado.
- Kwa nini usiyasahau na kuyakimbia?
- Sikuweza, na sidhani kuwa mtu mwenye akili anaweza kufanya hivyo.
- Je unakusudia kuwa watu walio wengi ni wenda wazimu au wapumbavu?
- Bali ninakusudia kuwa watu walio wengi hawawezi kusahau na wanachukizwa sana na maisha yao na kuondoka kwa furaha zao.
- Wewe ni mwanafalsafa, lakini wakati huo huo ni msorajua, na hukuweza kufikia bali umefikia matokea ya hakuna kitu, sasa suluhisho ni lipi basi?
- Suluhisho nililonalo ni kuwa tuendelee, hadi tupate majibu ya maswali..na wewe

www.path-2-happiness.com

una suluhisho gani?

- Ndilo hilo nililolisema tu, lakini natofautiana nawe kwa kuwa ninahisi kuwa hivi karibuni nitapata majibu.
- Kuwa na matarajio ni neema kutoka kwa Mungu, na nataraji matarajio yapo sehemu yake, lakini matarajio yako inabidi yawe na dalili yake.
- Dalili yake ni kuwa twende katika njia tukiwa na rajua na bila ya kubabaika wala kuwa na shaka.
- Vizuri sana, ubunifu mzuri, ehe na ulifikia wapi kwenye njia hiyo.
- Nimemaliza kujua kuhusu ukanaji Mungu na dini zote za ardhini, na zote hazina maana wala hazina manufaa kama ulivyotaja, kisha nikaanza kushughulika na dini za mbinguni, na mimi sasa nipo kwenye utafiti kuhusu Ukristo.
- Mimi ni Mkatoliki kulingana na makuzi yangu, lakini ninakwambia kuwa siamini chochote kuhusu Ukatoliki, kwani ni makundi ya mzaha na siri mbali mbali na migongano tu.
- Kama ni hivyo basi kwa nini usiwe Mprotestant?
- Samahani sana ewe Mprotestant; nimeanza na dini yangu kwanza, Uprotestant nao ni majaribio ya kukimbia dhihaka ya Kikatoliki, ni jitihada iliyofeli na aliyeanzisha hana dini hivyo, kwa hivyo basi walichokifanya wao wamechukua kiasi cha dhihaka ya Katoliki na siri zake mbali mbali pamoja na uchache wa imani ya dini yao.
- Nibainishie zaidi, wakati mwingine mgumu kufahamika.
- Je, hawakuwa wao pamoja (Ukatoliki na Uprotestant) wakitegemea Biblia? Na yaliyomo ndani yake katika agano jipya na la kale ambayo haswa ndio vyanzo vya dhihaka hiyo na ushirikina.
- Kwa nini unasema hivyo kuhusu kitabu kitakatifu kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu?
- Kana kwamba na wewe ni Padri, nitakujibu kama nilivyojibu, nijibu kwa ujasiri, je, unaweza kunithibitishia kuwa kilichopo mikononi mwetu sasa hivi kimeteremshwa na Mwenyezi Mungu? Mimi ninaweza kukuthibitishia kuwa baadhi ya yaliyomo kwa uchache sio kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
- Utawezaje kunithibitishia hayo?
- Kwa dalili nyingi, miongoni mwayo: soma ukipenda historia ya kuandikwa

kwa kitabu kitakatifu, hata anayesema kuwa ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu utashtushwa na hakika ya kihistoria, angalia migongano bali hata zinavyotofautiana nakala na matoleo mbali mbali na tafsiri au tarjama zake mbali mbali, bali utashangazwa na tofauti iliyopo katika toleo moja! Soma baadhi ya matukio ambayo yanakataa kabisa kuitwa kuwa yametoka kwa Mungu, au ya kuwa Mungu huyo ni mwenye shari na mbaya, je unataka dalili nyinginezo? Je unataka maelezo ya kina kuhusu dalili yoyote?

- Nakubaliana nawe kwa mengi uliyosema, pamoja na kuwa nataka kujadiliana na kasisi katika hili na mengineyo; ili nimsikie yeye.
- Wewe ni mtu wa ajabu, kwa nini basi unajadiliana nami katika hili
- Ikiwa hali ndio hiyo uliyosema, suluhisho ni lipi?
- Nimekuambia kuwa matokeo yangu hayakuwa na kitu.
- Samahani, kutokuwa na kitu maana yake kutokuwa na maarifa nayo, na mimi ninamtaka mwenye elimu na maarifa hayo.
- Unachosema ni sahihi, lakini mimi sikimiliki.
- Kwa rai yako ni nani mwenye majibu?
- Ningekuwa namjua basi tabu zangu za siku nyingi zingekwisha.
- Nataka kukutana na mmoja katika maaskofu kama inawezekana; kwani nataka kusikia majibu yao katika hoja hizi na nyinginezo.
- Nina marafiki zangu wengi maaskofu, je unawataka wenye kasumba miongoni mwao au waliofunguka? Au unawataka wanazuoni wao au wanaojifanya kuwa na elimu?
- Ikiwa nina uwezo wa kuchagua, aliyefunguka ni bora kuliko wenye kasumba, lakini la msingi zaidi ni kuwa na elimu, namtaka mwenye elimu zaidi yoyote awaye awe ni mwenye kasumba au aliyefunguka zaidi.
- Kama ni hivyo basi pata tumaini, kila elimu ya mtu inapozidi kuwa kubwa ndipo anapofunguka zaidi, nitaweka miadi na rafiki yangu Padri Lougi Stefano ambaye alizungumza na mke wako, kwani yeye ni katika maaskofu wenye elimu kubwa kati ya niliowaona, na aliyefunguka zaidi. Kesho au kesho kutwa nitakupa ratiba ya miadi.
- Nakushukuru sana.
- Nafahamu unachosema, ni mwenye furaha kukusaidia.

www.path-2-happiness.com

Joji akitabasamu:

- Nahisi kuwa nimekuchosha lakini nina swali, Je, ulishafanya utafiti kuhusu Uislamu?
- Hapana…nimesoma juu juu tu, na mahojiano ya hapa na pale tu.
- Kwanini?
- Uislamu ni dini ya matumizi ya nguvu, Jihadi, kumdhulumu mwanamke na kuwa nyuma, na mifano mingi ya namna hiyo.
- Umejuaje hayo yote na wewe hukufanya utafiti wowote kuhusu Uislamu?
- Mwenye kumiliki hoteli jirani na nyumba yetu ni Muislamu kutoka Misri, wakati mwingine ninajadiliana nae.
- Naye anakuambia hivyo mwenyewe?
- Hakuna anayeweza kusema hivyo mwenyewe, lakini ananiambia kuwa yeye ni Muislamu aliyestaarabika, na sio kama waislamu wengine ambao hawakuendelea, na pindi nilipomuuliza sababu ambazo zinawafanya Waislamu wasiendelee, aliniambia: sababu ni dini yao, kwani ni dini inayolingania kasumba na kuwauwa wenye kwenda kinyume nao, na kumfungia mwanamke, bali na kumpiga.
- Jambo la ajabu kabisa. Je ninaweza kuonana nae?
- Wewe ni mtu wa ajabu, unataka nini kwake? Katika hali yoyote tunaweza kula pamoja hotelini kwake na kuonana nae siku yoyote ile.
- Vizuri, lakini nina swali lingine kama ukiniruhusu?
- Uliza.
- Kwanini Padri anakutuma kwangu na yeye dhahiri anafahamu rai yako kuhusu Ukatoliki?
- Je, sijakuambia kuwa yeye amefunguka? Mara nyingi nahisi kuwa anakinaishwa na ninayoyasema, lakini hajui uchaguzi unaofaa!
- Rai ya maana kabisa, ikiwa haikutubainikia njia za majibu ya maswali yetu basi tuliyokuwa nayo sasa hivi ni bora kuliko kupotea kabisa.
- Swadakta, na natamani isiwe niliyokuwa nayo sasa hivi ni upotevu, lakini bado naendelea kufanya utafiti.
- Samahani, sikutaka kukukosea hata kidogo.
- Nafahamu hilo.

Katarina alirejea pamoja na Maiko na Sali, wakakutana na John Luke, Katarina akampa mkono na kumkaribisha..

- Ashukuriwe Bwana, nimefika baada tu ya kuondoka, wewe umekuja kwa njia ya Padri Lougi Stefano?!
- Ndio, wewe ni mke wa Joji, Padri anasema wewe ni katika Wakatoliki wenye dini zaidi Uingereza, pamoja na kuwa hujawa mtawa.
- Nakushukuru pamoja na Lougi, yeye ni mwalimu wangu, kwani nimesikia mawaidha yake mengi sana pamoja na mihadhara yake.
- Nitaratibu miadi naye pamoja nanyi kesho au kesho kutwa.
- Vizuri sana…kama Joji atakubali.
- Joji ndie aliyetaka hili, na tutakula chakula katika Grand Hotel.
- Vizuri, nitakutana na mwalimu wangu…lakini kwa nini Hoteli hiyo uliyosema?
- John Luke mjulishe..
- Kuonana na mmoja katika Waislamu hapo.
- Kwa nini?
- Sijui, lakini anataka kusikia kutoka kwake kuhusu Uislamu kuwa nyuma pamoja na ushenzi wao na ukatili wao.
- Na kama Muislamu huyu hajakujibu hilo mimi ninaweza kukujibu, inatosha tu kuangalia nchi zao zilivyo ili kujua kwa nini wako nyuma hata kwenye dini yao.
- Kwa ujumla hii ni kadi yangu, nitafurahi kwa mawasiliano nanyi na kwa maelezo yoyote yale kuhusu dini au utalii, na nitawapigia kuwahakikishia miadi pamoja na rafiki yangu Padri Luogi Stefano. Kwaherini.

John Luke alitoka, Katarina alitabasamu akimgeukia Joji huku akisema:

- Ehe kikao kilikuwaje? Nilitamani sana kurudi mapema ili nikutane nae.
- Nzuri sana, asante.
- Bila ya shaka Padri hawezi kumtuma mtu ila mtu huyo awe ni msomi na mwenye dini zaidi na Mkatoliki..
- Ndio..yeye ni mwanafalsafa na mwanazuoni. Lakini si mwenye dini Mkatoliki kama usemavyo.
- Ajabu! Lakini umesema kuwa ni rafiki yake.

www.path-2-happiness.com

- Ndio ni rafiki yake
- Inawezekana vipi Padri akasuhubiana na mtu asiyekuwa na dini?! Kwa ujumla, ni muhimu atupangie ahadi ya kukutana nae; huenda tukafaidika nae.
- Vizuri kufaidika na kila mtu, na vipi mtu huyo akiwa ni Padri, ehe nijulishe habari za sokoni?
- Matembezi yalikuwa mazuri sana, watoto walicheza sehemu zao, kisha tukanunua baadhi ya vitu…hatukuchelewa isipokuwa njiani tu.
- Leo tutatembelea wapi katika sehemu za athari mjini?
- Leo tutatembelea ngome ya Saint Angelo kwa ajili ya maombi ya Maiko, ni husuni nzuri sana na ipo karibu tu na itamaliza siku yetu ya leo hii pamoja na kutembelea pembizoni mwake.
- Twendeni sasa hivi, yuko wapi Maiko na Sali?
- Chumbani mwao, wanavaa viatu vyao vipya; twendeni sasa hivi.

Familia iliondoka kuelekea ngome ya Saint Angelo, joji alijali sana kutekeleza usia wa Tom wa kupunguza huzuni na wasiwasi wake na mizigo aliyojibebesha, na kuwa ashughulishwe na matembezi na furaha na wanawe tu, alijaribu kutofikiria mambo mengi kuhusu njia ya furaha, vinginevyo ataingiwa na wasiwasi na kulalamikia katika njia ya kufikia majibu ya maswali yake, bali ni juu yake kutafuta kwa njia ya utulivu mno.

PAMOJA NA KASISI



www.path-2-happiness.com

12 PAMOJA NA KASISI

PAMOJA NA KASISI

(1)

Jioni familia ilirudi hotelini na Joji alipokea simu kutoka kwa John Luke ikimjulisha kuwa ahadi yake na Padri Luogi ni kesho saa nne asubuhi kanisani, na yeye atawasubiri…

- Huyu John Luke ananijulisha ahadi yetu na Padri kesho lakini tutaacha wapi watoto?
- Ima tuwachukue twende nao, au tuwaache katika bustani jirani na kanisa, kuna bustani nzuri sana.
- Vizuri, nadhani itakuwa bora kufanya hivyo.

Ilipotimu saa mbili unusu asubuhi Joji na Katarina na watoto wao walikwenda kwenye bustani iliyo karibu na kanisa lile, ambapo kuna sehemu maalumu ya michezo ya watoto, hivyo wakawaacha Maiko na Sali hapo, na hiyo ni baada ya kuzungumza na muhusika wa sehemu hiyo na kumuomba awaangalie watoto..kisha hao wakaelekea kanisani; katika ahadi na Padri kulingana na ahadi waliyokubaliana. John Luke aliwapokea na kuwakaribisha, na wote wakaondoka kwenda kwa Padri Luogi ambaye aliwapokea kwa uchangamfu.

- Karibuni sana Katarina, nimesikia juhudi zako kubwa ufanyazo Uingereza, Bwana akuhifadhi.
- Hili nimejifunza kutoka kwenu, katika tuliyofaidi kutokana na elimu zenu.
- Karibu Joji… John Luke amenijulisha kuhusu maswali yako, na yeye kafurahishwa sana na namna unavyofikiri, karibu, unataka nini?
- Nina maswali manne, na sitopoteza wakati wako, la kwanza: Iweje kuna Mungu mmoja mwenye nafsi tatu kwa wakati mmoja? Nimesoma sana, na kusikia maelezo mengi, na bado sijafika popote bali (nisamehe) wakati mwingine nahisi kuwa Ukristo unafanana na Upagani.

Uso wa Padri ulibadilika, na akawaangalia John Luke pamoja na Katarina, kisha akaangalia chini ardhini na kusema:

www.path-2-happiness.com

- Na la pili?
- Je Yesu ni Mungu au ni katika wanadamu? Na je yeye ni Mungu muabudiwa au mtu tu aliyeuwawa? Je inahitajia Mungu afe ili awaokoe wanadamu?! Je isingekuwa bora kuwaokoa wanadamu akiwa ni hai bila ya kufa?
- Na ya tatu:
- Kitabu Kitakatifu kiwe ni Agano la Kale au Jipya ni katika vitabu vyake? Ni nani aliyefanya tarjama yake? Na ni nani aliyetufikishia? Na kwa nini kuna migongano katika toleo zake, ninaona haya kuwasomea wanangu, vipi hiyo itoke kwa Mungu?
- Na ya nne?
- Je historia ya dini na manabii ni historia tu ya mauaji na uchafu tu? Nachukizwa na matumizi ya nguvu na mauaji, na nachukizwa na kila anayelingania hayo, lakini vile vile nashangazwa na mtazamo wa kitabu kitakatifu kuhusu manabii na mitume, kama vile ambavyo ninashangazwa na maandiko kuhusu mauaji na uporaji!

Padri alinyanyua uso wake juu, akamwangalia Katarina na Joji machoni kabla ya kumgeukia John Luke.

- John Luke kwa nini hukuniambia kuhusu maswali yake kabla?
- Yeye mwenyewe hakuniambia kabla.

Padri alimuangalia Joji machoni kwa muda mrefu na kwa umakini mkubwa.. kisha akaangalia juu kwa uso uliioonesha alama za machovu na msisitizo kwa wakati mmoja, kisha akapumua kwa nguvu.

- Kijana wangu, wewe huwezi kufahamu majibu ya maswali haya kwa wepesi huu, kama ambavyo kuzielezea na kubainisha huchukua muda mrefu, kwa nini usiondoke kwenda kufanya ibada ya kumuabudu Mungu (Bwana) kuliko (maswali) haya?
- Bwana wangu nimekuja kujifunza kwenu na kufaidika na elimu yenu, na yaliyokuwa ni marefu katika maelezo yake yanaweza kufupishwa na mwanazuoni.
- Vizuri kijana wangu, katika dini yetu kuna siri mbali mbali ambazo hazipaswi kujadiliwa kama ambavyo kuna maandiko ambayo hapaswi kuyafahamu peke yako tu.
- Bwana wangu kuhusu siri hizi, je itakuaje tunaamrishwa kufuata dini kutoka kwa Mungu halafu dini hiyo ikawa ni siri miongoni mwa siri? Je inawezekana vipi maandiko yakawa kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watu wote lakini hayafahamiki

ila kwa baadhi ya watu tu?!

Maneno yale yalianza kumchukiza Padri na uso wake kuonesha hayo, aliangalia chini kisha akasema:

- Je mnaweza kutuacha peke yetu mimi na Joji?

Uso wa John Luke ulibadilika na akaonesha dhahiri kutofurahishwa na jambo hili, itawezekana vipi rafiki yake amwondoshe katika kikao alicho kitayarisha yeye…

- Je unanitaka mimi nitoke pamoja na Katarina? Kwa nini je hii ni siri nyingine?!
- Ninamuhitaji katika mazungumzo maalumu, mkitoka nitashukuru.
- Katarina nenda kwa Maiko na Sali na unisubiri huko, na nitakuja baada ya muda si mwingi.

Katarina alimuaga Padri, na akamwombea baraka, na akamuhakikishia kuwa atahudhuria misa takatifu Jumamosi ambayo itaongozwa na Papa… alitoka pamoja na John Luke hadi bustanini….Pindi walipoondoka tu, Padri alimgeukia Joji.

- Kijana wangu wewe ni mtu jasiri sana; sio ushujaa wa vita bali ni ushujaa uliomo ndani ya nafsi.
- Asante sana Bwana wangu.
- Kijana wangu, nami nitakuwa muwazi na jasiri kwako, huenda ukasikia usiyoyapenda.
- Tafadhali, karibu kwani sio muhimu kusikia ninachopenda, bali cha msingi ni kusikia ninachohitaji.
- Huenda ukashangazwa, kwa masikitiko hakuna jibu lililokata kuhusu kadhia hii.
- Bwana wangu, je huoni kuwa imani haiwezi kuwa pamoja na shaka?
- Unachosema ni sahihi, lakini siwezi kupata jibu linalokata, nimebaki na umri wangu huu wote nikitafuta jibu la maswali mengi miongoni mwayo ni haya uliyotaja, lau ukitaka nikujibu kwa jibu lolote ningefanya, lakini nimekuahidi kuwa jasiri na mkweli pamoja nawe, ukweli ni kuwa sijapata jibu sahihi.
- Suluhisho ni lipi basi?
- Mimi bado ni Padri, kwa sababu sijapata lililokuwa bora kuliko hili nililonalo sasa hivi, na kuwepo kwa maswali katika baadhi ya kadhia ni bora kuliko kuendelea kuwa na shaka katika kila kitu, au sivyo?
- Swadakta, lakini kupata majibu ni bora kuliko hayo yote.
- Ndio, na huenda ukapata majibu lakini ninakuhakikishia kuwa hutolipata ndani

www.path-2-happiness.com

ya Kanisa, mimi nina muda wa miaka thelathini na ni kasisi wa kanisa hili, na sijapata jibu, hili ndilo ambalo ninalo.

- Je ninaweza kukuuliza swali?
- Karibu.
- Kwa nini umewataka John Luke na Katarina watoke?
- Huenda ukashangazwa na nitakachokisema! Hii ni kwa sababu ya upungufu wa ujasiri nilionao, hakuna anayependa kuwa dhaifu, anayeonekana hajui kitu mbele za watu wengine, haswa wanaoamini kuwa ana elimu, kisha wakiacha Ukatoliki au Ukristo–watakuwa nani? Wakanaji Mungu na dini kwa mfano, ninaamini kuwa kuwepo kwa shaka ni bora kuliko kuishi katika ulimwengu wa shaka.
- Samahani, je hakuna Mapadri na watawa walio jasiri kuelezea hayo unayoyaeleza kwa sauti kubwa?
- Wamepita idadi ya mfano wao katika historia ya Ukristo, ima waliuawa, au kupotezwa au kutoroka, kitabu kitakatifu pamoja na Upapa ni mgumu sana.
- Kama ni hivyo basi wewe unaunga mkono uhusiano wa siri uliopo baina ya Vatican na vyombo vya usalama, kama alivyothibitisha hayo Eric Fratini katika kitabu chake "Karne kumi na tano za ujasusi Vatican" The Entity: Five Centuries of Secret Vatican Espionage
- Kamwe....sio kweli, huko ni kuwabebesha (makosa) kutoka kwa Mprotestant Mmarekani kwa kanisa la Kikatoliki.
- Vipi kuhusu mambo aliyoyataja?
- Mengi katika hayo yana ukweli, lakini ameyaweka muweko wa kulibebesha lawama Kanisa la Kikatoliki na Upapa.
- Lakini majasusi kuingia Vatican ni kweli, au kwa lugha nyingine kuwa Shirika la Kijasusi limejipenyeza ulimwenguni, au sivyo?
- Kwa bahati mbaya ndio, lakini sio jambo la jumla, pamoja na kuwa kila mara linatokea.
- Lakini kama ni hivyo mbona ukali wake hauonekani kwa watawa na Mapadri katika fedheha za Kijinsia?
- Haiwezekani, kwani jambo hili hutokea sana, unadhani Kanisa litavunjika kwa sababu ya watoto?! Kama ambavyo sehemu ya kadhia hizi za kijinsia zipo katika Kitabu Kitakatifu, kisha akaendelea:
- Bwana wangu, niwaambie nini akina Katarina na John Luke watakaponiuliza: Kwanini umewatoa?

Padri Luogi alinyamaza, kisha akaangalia chini na kusema:

- Siku zote ukweli ni mzuri.
- Asante sana bwana wangu nitafanya hivyo kwa ruhusa ya Bwana, kwa hakika nimefaidika nawe sana.
- Asante sana, Mungu akubariki, nataraji kukuona katika misa ya Jumamosi takatifu, yakini ni bora kuliko shaka.

Joji alitoka na kwenda bustanini; alimkuta Katarina na John Luke wakimsubiri, alipofika tu John Luke alimuuliza:

- Kwanini ametutoa? Kwa mara ya kwanza Luogi anafanya mambo bila ya kutumia diplomasia!

Joji hakutaka kuzungumza maudhui ya kutolewa, haswa zaidi baada ya kuona hasira za John Luke…

- Muda wa chakula cha mchana umewadia, je tupo karibu na Grand Hotel ambayo ipo jirani na kwako ili tuweze kula na kuzungumza pamoja?
- Ndio, ni muda wa dakika tano tu kwa kutembea.
- Niruhusuni kwanza nataka kwenda kucheza na wanangu na baada ya nusu saa twendeni mgahawani….unasemaje Katarina?
- Vizuri, hamna neno, pamoja na kuwa natamani sana kwa muda huo wa nusu saa utuambie kilichopita baina yenu na Padri, kwa ujumla baada ya nusu saa tutajua kila kitu.

Joji alielekea kwa watoto wake katika sehemu ya watoto akiwa anafikiri: Atawaambia nini John Luke na Katarina? Je awaambie kilichotokea kama ilivyo na iwe chochote kitakachokuwa? au afanye nini?

Baada ya nusu saa alirejea pamoja na wanawe….

- Sisi tuna njaa sana, twendeni mgahawani.
- Haya twendeni.

(2)

Walifika Grand Hotel baada ya kutembea kwa muda wa dakika tano hivi… Joji akainama karibu na Maiko na Sali:

- Wepenzi wangu…mnaonaje mkale roshani?
- Na wewe na mama mtakula wapi?
- Tuna ahadi muhimu, ni bora mkae wenyewe roshani; ili mzungumze pamoja, na muangalie mandhari nzuri.

www.path-2-happiness.com

- Vizuri, haya Sali twende.

Joji alikaa pamoja na Katarina na John Luke katika meza katikati…. walipokuwa wakiangalia menyu. Joji alimgeukia John Luke……

- Yuko wapi sahibu yako Muislamu?
- Ninaogopea asije akataka kuzungumza nawe peke yako na ukatuacha sisi… hata hivyo atakuja muda sio mrefu ili achukue oda zetu.
- Sio mimi niliyekutaka atuache pamoja na Padri, lakini ni sahibu yako Padri ndie aliyefanya hivi.
- Lakini wewe ulimkubalia mara moja.
- Ha Ha ha, je hataki kuwatii watu wa dini?! La msingi ni kuwa alitaka kuniambia mimi kuwa hakuna jibu la maswali yangu, na hakutaka muone udhaifu wake na maarifa yake machache.

Katarina alishikwa na hasira na kumwangalia Joji .

- Haiwezekani kwa Padri Luogi kukosa majibu ya maswali yako mepesi!
-
- Ninajua kuwa hana majibu, naye anajua kuwa mimi nafahamu hivyo, lakini kwa nini alitutaka tutoke? Nahisi katika maudhui hii kulikuwa kuna jambo jingine.
- Mnaweza kumuuliza, nyie mnamjua zaidi kunishinda mimi, nadhani aliona vibaya Katarina kutoka peke yake.

Ulipita muda wakiwa kimya Joji aliona shaka kwa mara ya kwanza alipomuangalia Katarina, kama kwamba macho yake yalizungumzia wasiwasi uliokuwa ndani ya nafsi yake ambayo anajaribu kuishinda na kuificha. Huenda kimya chake kikafanana na Volkano wakati wa utulivu wake hauonekani isipokuwa wingu lake tu. Ama John Luke kimya chake kilikuwa ni kumshangaza rafiki yake alivyofanya kwa jambo linalofahamika wazi, kama ambavyo bado alikuwa na mashaka aliyoyasema Joji na kuna jambo lingine lililofichwa.

Mhudumu alikuja kuchukua oda, na akavunja ukimya uliokuwepo ….John Luke akamuuliza kuhusu Suleim mwenye hoteli, na akaomba waongee nae kama inawezekana …

- Bwana Suleim yupo na marafiki zake wanaongea ofisini kwake, nitamjulisha maombi haya. Samahani mnahitaji nini kwa ajili ya chakula cha mchana?

Walimjulisha mhudumu wanachotaka, na Joji akamuelekeza mhudumu walipo Maiko na Sali ili wachukua oda yao… kisha akamuangalia John Luke kutaka kujua kitu!.....

- Suleim ndie Muislamu uliyenijulisha?
- Ndio, utakapomuona utadhania Mtaliano, kwa mnasaba anazungumza Kiingereza vizuri sana.
- Vizuri, huenda akafika baada ya muda mfupi tumsikilize.

Katarina nae alianza kuzungumza

- baada ya kupita ukimya:
- Sasa turudi kwa Padri… wewe unasema kuwa hakuweza kujibu maswali yako!
-
- Ndio bali anasema kuwa maishani mwake anatafuta majibu ya maswali haya na mengineyo mengi, na hakuweza kufikia majibu yenye kukinaisha.
- Haiwezekani!
- Padri ambaye unamzungumzia ni rafiki yangu ewe Katarina na ninajua kuwa hajui majibu yake, kwani tumesha jadiliana katika hayo na mengine mara nyingi, lakini kinachonishangaza mimi ni kwa nini alitutaka tutoke?! Hili ndilo ambalo silifahamu!
- Padri Luogi Stefano ni katika walionisaidia sana kuwa na yakini, itakuaje awe na shaka namna hii?!

John Luke alipumua kisha akaangalia

- juu na kusema:
- Uzoefu wangu unaniambia: Kila elimu ya Padri ikizidi, hawi mkakamavu katika mazungumzo yake maalumu, na athari yake katika hotuba kwa watu inaongezeka kwa yanayonasibiana nao.
- Unakusudia nini?
- Unacho kisikia kutoka kwake ni mazungumzo ya jumla tu, anachokisema katika vikao vyake maalumu ni jambo lingine, kwa ujumlamimi nafahamu haya, unataka aseme nini katika mazungumzo yake na watu wote? Unataka aseme: Sisi hatumjui Mungu, au kitabu kitakatifu kimepotoshwa au kimetengenezwa?

Macho ya Katarina yalijaa machozi

- akiwa anasema:
- Hapana, nataka aseme kuwa Bwana ni mkarimu, mwema, mmoja hata kama ana nafsi tatu, Yeye bwana ndiye aliyeteremsha Kitabu kitakatifu.

John Luke akimwangalia Katarina kwa

- huruma:
- Tutafanya nini kama kitabu kitakatifu

www.path-2-happiness.com

- kinagongana chenyewe? Je unaweza kunibainishia kwa njia ya mantiki yenye kukinaisha –vipi tatu inaweza kuwa moja na moja kuwa tatu?!
- Nataraji hutoniambia wanachosema makanisani, kwani nimesikia mara elfu na moja na bado sijakinaishwa nayo.
- Bali nimekinai kuwa hayo ni kwa ajili ya mazungumzo tu kwa watu wa kawaida.

Joji alihisi wasiwasi na mgongano wa ndani alionao Katarina, kama vile Volkano inayopasuka ndani yake na kujisemesha mwenyewe:

- Huenda mshtuko alioupata Padri ni mkubwa kuliko uwezo wake wa kuvumilia na hivyo alijaribu kubadilisha maudhui…
- Mnaonaje tukaakhirisha mazungumzo yetu,
- kuna mtu anakuja.
- Ooh huyo ni Suleim, karibu Suleim kuna mtu anataka kufahamiana nawe Karibu John Luke pamoja na wageni wako.
- Wageni wangu hawajawahi kukaa na Muislamu, na wanataka wakae nawe…
- Karibuni, mimi natoka Misri, na nyie kutoka
- wapi?
- Kutoka Uingereza.
- Waislamu Uingereza ni mara mbili ya
- Waislamu waliopo Italia.
- Sawa sawa, lakini nimependa kujua Uislamu kutoka kwako, je kitabu chenu kitakatifu kina amini Agano la Kale na Agano Jipya?
- Pamoja na elimu yangu ndogo ya itikadi ya Kiislamu lakini nitawajibu kadri nijuavyo….ndio, inaamini, lakini samahani, inaziona kuwa zimepotoshwa.
- Je mnamuamini Musa na Yesu?
- Tunaamini kuwa ni Mitume ya Mungu.
- Je mnaamini Uungu wa Yesu?
- Hapana, Waislamu wanaamini kuwa
- ni Mtume aliyekirimiwa na sio Mungu.
- Na kitabu chenu kitakatifu kinaitwaje? Na
- kimewafikiaje?
- Jina lake ni Qur'an, na kimetufikia kupitia Mtume Muhammad –mnataka kufikia nini?
- Tunataka kuufahamu Uislamu na mafundisho yake?
- Mimi sijui chochote kuhusu Uislamu, ninachojua ni utalii, biashara, lakini

mnataka nini katika Uislamu.

- Ni kwa sababu tunashangazwa sana na matumizi ya nguvu na ugaidi mlio nao?
- Magaidi Waislamu tuliokuwa nao huharibu kila kitu kwa jina la dini.
- Unasema kwa jina la dini, ni dini gani isiyokuwa na matumizi haya mabaya ya nguvu na ugaidi?
- Ndio, Uislamu ni dini ya amani na sio ya ugaidi, lakini Waislamu wamepetuka mipaka ya dini na wako nyuma kimaendeleo na ni watu wenye kushadidia mambo.
- Kwa mara nyingine je Uislamu upo nyuma au ni magaidi wapo nyuma?
- Uislamu haupo nyuma lakini Waislamu ndio wapo nyuma? Lau mngekuwa ni Waislamu mke wako asingeweza kukaa hapa na sisi na kuzungumza nasi, je huku siko kuwa nyuma?
- Kwa nini siwezi kukaa nanyi?
- Kwa sababu unatakiwa uvae hijabu na kuwa mbali na wanaume, kwa kweli mimi nimeondoka Misri, ili niwe mbali na ujinga huu.
- Je watu wako wa nchini mwako wanaona uonavyo?
- Ha ha ha…Baba na mama yangu pamoja ni marafiki zangu mara nyingi huniambia; Fikra zako hazipo katika Uislamu.
- Kwa nini?
- Uislamu unatofautiana sana na Ukristo, nyie inatosheleza kusali Jumamosi au mara moja ili mbaki kuwa Wakristo, ama sisi yule ambaye haswali kila siku mara tano anazingatiwa kuwa katoka katika Uislamu, nyie mnaweza kuikosoa torati na injili, ama sisi ni kuwa atakayeongea dhidi ya
- Qur'an basi atakuwa ametoka nje ya Uislamu.
- Je una ndugu yako yoyote aliyepo hapo Italia?
- Nipo Italia kwa muda wa miaka kumi na nimekataa kurejea kwetu, na kwa
- mara ya kwanza kabla ya wiki moja amekuja baba yangu, mama yangu na ndugu yangu na wataondoka baada ya siku tatu.
- Je ninaweza kuwaona?
- Ndio inawezekana, lakini samahani nyie kwa muono wao ni makafiri.
- Kwa vipi?
- Wewe unasema kuwa Mungu ni watatu, huku ni kumshirikisha Mungu, na hapo utakuwa umemkufuru Mungu.
- Kwani kuna mpya gani? Na sisi tunasema wao ni Makafiri – kwani hawakuamini Uungu wa Yesu hamna madhara yoyote kwetu kama tutakutana nao.

www.path-2-happiness.com

Katarina alikuwa bado katika hali ya mshtuko kwa yaliyotokea kwa Padri, na hatoweza kuvumilia mshtuko mwingine.

- Joji hatuna wakati usisahau kesho misa ya Jumamosi takatifu.
- Tutapata muda wa kutosha ikiwa muda wao utaruhusu….ni muda gani tunaweza kukutana nao?
- Muda wote wao wako nyumbani au hapa hotelini, nataraji watafika hapa baada ya dakika chache, na ukitaka muda mwingine nitawafanya wawasubiri…ninarudia tena: mimi sihusiki chochote kwa watakavyokuambieni.

Uso wa Katarina ulionesha haya kutokana na msisitizo wa Joji, na akamuambia kwa msisitizo:

- Samahani… sijafahamu makusudio
- yako Joji, lakini naona kama utashikilia
- hilo basi subiri dakika kadhaa, ili
- tusilazimike tena kurudi hapa hotelini.
- Nitapanda kumuangalia Maiko na Sali na kisha kurudi.
- Subiri, hao wanakuja, je niwaite wakae nasi?
- Napendekeza bora uwaite, nawaangalia watoto mara moja kisha narudi upesi.
- Nitawaita, mtabeba matokeo yake, haya ni maombi yenu…Mama, Baba, Khalid njooni…kuna wanaotaka kukaa nanyi.
- Suleim unataka nini?
- Khalid hawa ni marafiki zangu, wanataka kufahamiana nanyi, karibuni niwatambulishe:Huyu ndugu yangu Khalid, na huyu ni mama yangu, na huyu ni baba yangu…Khalid anazungumza Kiingereza, ama mama na baba wanajua kiasi tu, lakini hawawezi kuzungumza. Naomba mnipe ruhusa nitafuatilia mazungumzo yenu nikiwa kimya na sitoingilia kitu.
- Hali zenu nyote, jina langu ni Khalid ni mhandisi majengo, nduguye Suleim, na huyu ni baba yangu Abdullah na huyu ni mama yangu Aisha.
- Mimi ni John Luke, Mtaliano, ninafanya biashara.
- Na mimi ni Katarina Mwingereza.
- Karibuni nyote.

Joji alikuwa anarudi kutoka kwa watoto wake,

alitoa salamu na kumpa mkono Khalid na baba yake, alipotaka kumpa mkono mama yake alitabasamu na kurudisha salamu.

- Samahani ….Lakini mama yangu hapeani mkono na wanaume, ila anakuambia

karibu sana.

- Naomba samahani, sikuwa najua hilo.
- Tumeshafahamiana kabla hujafika, mimi ni Khalid ni mhandisi majengo nduguye Suleim, na huyu ni mama yangu na huyu ni baba yangu.
- Mimi ni Joji mhandisi kompyuta kutoka Uingereza mnaionaje Roma nchi iliyojijenga yenye nguvu, dini na fani?
- Kwa kuwa mimi ni mhandisi majengo; nianze maudhui kuhusu fani; Roma ni ya kipekee, ni nchi yenye ustaarabu, maendeleo makubwa ya kisasa, pamoja na kuwa kuna kitu ambacho sijafurahishwa nacho.
- Ni kipi hicho?
- Masanamu na watu kuyatukuza haikunifurahisha, haiwafikiani na malezi tuliyopata kwenye dini yetu, sisi tunazingatia kuwa jambo hilo ni la Kipagani na kuabudu asiyekuwa Mungu.

Joji alikumbuka kuwa nae alifanana na Waislamu kwa kutopenda kwake masanamu na Upagani, kadhalika alikumbuka masanamu miungu yaWahindu na Wabudha.

Khalid aliendelea….

- Na hili linaniingiza katika maudhui ya dini katika Roma ambalo umeniulizia.
- Samahani kukukatisha, unakusudia nini unaposema, 'Katika malezi ya dini yenu!?'
- Katika Uislamu hatumshirikishi Mungu na yoyote, na tunaamini kwamba inapasa aabudiwe peke yake wala asishirikishwe na chochote, wala haifai kuwanyanyua watu
- katika nafasi na cheo cha Mungu. Yoyote awaye katika watu hao, na ndio maana Mtume wetu Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: "Msichukulie kaburi langu kuabudiwa baada yangu, kwa
- hakika mimi ni mja wa Allah na Mtume wake."
- Ninafahamu kulingana na maneno yako kuwa sisi ni washirikina?
- Anayeona Mungu kuwa ni watatu, kwetu huyo anamshirikisha Mungu.

Katarina aliingilia mjadala, kama kwamba kilichokuwa kifuani kwake kimemtoka….

- Suleim, kaka yako haoni hivyo, anaona kauli hiyo ni ya kupindukia.
- Ndugu yangu Suleim ni mkubwa wangu na ana heshima yake, na sipendi kutofautiana nae mbele za watu, lakini mimi binafsi ni mwenye kukinaishwa sana

www.path2-happiness.com

na mnachosema.

Joji akikatisha…

- Kwa maana hiyo Musa na Yesu ni waongo?
- Mungu anisamehe, sisi tunaamini ukweli wa Musa na Yesu, tunawaheshimu na tunawatukuza na tunaamini kuwa ni Mitume ya Mungu na ya kuwa amewateremshia kitabu…bali tunaamini kuwa itikadi zenu nyingi zinashusha hadhi zao.
- Sisi tunashusha hadhi ya Bwana Yesu?
- Nyie mnaamini kuwa ameuawa, ama sisi tunaamini kuwa hakuuwawa, bali miongoni mwenu wanamuona ni mtoto wa Zinaa? Je nyinyi hamuamini hivyo?
- Na nyinyi….mnaamini nini kuhusu Yesu na Bikira Maria?
- Tunaamini kuwa ni mja wa Allah na Mtume wake, na ya kuwa hakuuwawa wala hakusulubiwa bali walifananiziwa tu, na ya kuwa yeye alizaliwa na Maria bila ya baba kwa muujiza wa Mungu kama vile Adam alivyoumbwa bila ya baba wala mama. Yesu alizungumza utotoni na Mungu alimpa alama nyingi; alikuwa anaponya mbalanga na ukoma na kuhuisha kwa idhini ya Mungu na huwaambia watu watakacho kula na kuhifadhi majumbani mwao.
- Hivyo basi mna mtazamo kamili kuhusu Yesu, na mnaamini Agano la Kale na Agano Jipya?
- Ndio, tunaamini torati na injili kuwa vimeteremshwa na Mwenyezi Mungu.
- Lakini katika kitabu kitakatifu Yesu ni Mtoto wa Mungu!
- Tunaamini kuwa vimeteremshwa na Mungu lakini vimepotoshwa. Je katika baadhi ya Biblia mlizo nazo haikuandikwa kuwa Yesu ni mja wa Mungu na sio mwanae na wala sio Mungu?
- Hapana, hatuna kitu kama hicho

John Luke alinyanyua nywele zake ndefu kwa upande wa mkono wake akasema:

- Samahani kuwakatisha, lakini tunayo Biblia ya Barnaba, nayo ni Biblia iliyoandikwa karne ya kumi na tano na mtawa wa Kikatoliki alitoka katika Ukristo, makundi ya Kikristo hayajakubaliana nae wala kuikubali Biblia hiyo, kwa sababu alimzingatia Masiya ni mwanadamu na ni mtume wa Mungu.

Macho ya Joji yalikodoka akishangaa, na kusema:

- Ni kweli! Kwa nini sasa makundi ya Kikatoliki hayajakubali?
- Ndio, hayajatambua sio Ukatoliki wala

- Uprotestant, ila makundi mengine ya Kikristo yaliyatambua, na mengi ya
- makundi hayo yalisilimu baada ya hapo, na ndio maana inatuhumiwa kuwa ni miongoni mwa vitabu vya Waislamu.

Khalid alitabasamu na kusema:

- Na kuna dalili kuwa (Barnaba) ni Biblia iliyokaribu na ukweli.
- Unakusudia nini kusema karibu na ukweli? Je kuna nakala zingine zilizo za ukweli na zingine sizo?
- Nakusudia iliyo karibu kutoka kwa Mola wa Ulimwengu na imeungwa mkono na moja katika muswada za kihistoria, au Biblia zilizopatikana katika moja ya pango la Bani Mizaar Misri, na historia yake inarejea hadi mwanzoni mwa karne ya tatu ya kalenda ya gregoria, na iliitwa Biblia ya Yahudha, ambayo ndani yake kuna maneno hayo hayo, na angalia kuwa ilikuwa kabla ya kutumilizwa kwa Mtume Muhammad.

John Luke kwa dharau.

- Swadakta kwa yote usemayo, lakini Wakristo wengi hawaamini Biblia zote hizo.

Khalid akimuangalia nduguye Suleim:

- Samahani kama nitakuwa nimewakera, yote ninayosema yanatokana na mapenzi yangu ya Yesu, na kitabu kilichoteremshwa kutoka kwa Mungu.

Hisia zilimchanganya Katarina, na akatokwa na machozi aliposikia neno "Mapenzi ya Yesu" kisha akasema:

- Maisha yangu yote ni muhanga na mapenzi kwa Yesu, hivyo basi tunamuamini na yeye ndie mkombozi wetu na ndio maana tukaitwa Wakristo.
- Mimi sio mtaalamu wa dini, bali ni mhandisi majengo, lakini inaelekea kuwa wewe ni mkweli kuhusu mapenzi yako kwa Yesu, je umesoma kitabu, My Great Love for Jesus Led Me to Islam "Mapenzi yangu makubwa kwa Yesu yamenipelekea katika Uislamu." Mwandishi Mvenezuela Mkatoliki Simon Alfredo Caraballo.
- Sijawahi kukisikia kitabu hicho, wala sidhani mapenzi yangu ya Yesu yataielekeza katika usiokuwa Ukatoliki!
- Je itakudhuru kama utakisoma?! Kwani huna hakika na imani na Ukatoliki wako?!
- Sijawahi kukisoma, vinginevyo ningekisoma.
- Hii hapa nakala kutoka kwangu, chukuwa kama zawadi yako, sijui kwa nini nahisi kuwa wewe ni mkweli kuhusu mapenzi yako kwa Yesu, samahani si kama wengine yaani baadhi ya watawa na Maaskofu ambao wanaonekana kuwa wanakipa mgongo dunia, lakini wanavunja mapenzi hayo kwa Yesu.

www.path-2-happiness.com

- Asante sana nitaisoma, na mimi nina hakika kuwa haitobadilisha chochote katika mapenzi yangu yaYesu au katika Ukatoliki wangu.
- Unasema wewe sio mwanazuoni wa dini, kisha nakuona unazungumza lugha za watu wa dini, bali kwa lugha ya mtangazaji wa dini hii.
- Uislamu unatutaka sote tuwe walinganizi wa dini hii, kisha akatabasamu na akamwangalia mama yake, na kusema: Mama yangu ndie aliyenilazimisha kuja na kuniambia hiyo ni fursa ya kuulingania Uislamu, na mimi sijui Kitaliano, na hii ndio fursa yangu ya kwanza.
- Samahani, watu wote wanatamani kuja nchi za Kimagharibi, nchi zilizoendelea na utamaduni wa hali ya juu, na kuzikimbia nchi zilizo nyuma, na wewe unasema amekulazimisha?!
- Ulaya imeendelea sana kuliko kwetu, na hili linawafanya wahajiri wafurahi kwa kufika huku, haswa kwa sababu ya dhulma za kisiasa, kidini na kiuchumi katika nchi zetu, lakini mimi nafanyakazi ya uhandisi katika shirika zuri, na nina mapato ya kunitosheleza, na baada ya kuanguka utawala wa kidikteta kwetu Misri hali yetu ni nzuri, na itakuwa nzuri zaidi siku za usoni Mungu akipenda.
- Kwani haikuwa dhulma ya kidini na kisiasa huko kwenu sababu yake ni dini?
- Haiwezekani Uislamu ukawa ni sababu ya dhulma hata siku moja.
- Kwani hawakuwa ni Waislamu waliochoma kanisa la Watakatifu huko Alexandiria?
- Hivi ndivyo ilivyosemwa hapo mwanzoni, na watu wote ulimwenguni waliamini nikiwemo mimi, pamoja na kushangazwa kwangu na jambo hilo.
- Lakini baada ya dikteta Hosni Mubarak kuangushwa ambaye anapata msaada kutoka nchi za Magharibi ilithibitika kuwa ni vyombo vyake vya usalama ndivyo vilivyolipua. Nadhani wewe ni miongoni mwa mliosikia habari za mwanzo na hukupata taarifa ya habari ya pili kama ilivyo desturi za watu wa magharibi.
- Lakini bado mpo nyuma (kimaendeleo) kwa sababu ya dini yenu!

Mama yake Khalid (Aisha) alimuashiria mwanae, na kusema:

- Khalid mwambie kuwa sisi tupo
- nyuma kwa sababu ya kuwa mbali na
- dini yetu!

Khalid alihamisha aliyoambiwa na mama yake … chakula kilifika mezani Joji akajaribu kukamilisha mjadala uliopita…

- Je mama yako na baba yako wanajua kinachoendelea katika mjadala huu baina yetu?
- Ndio wanaufahamu vizuri, pamoja na kuwa hawawezi kuchangia kutokana na lugha, kwani Suleim hajawaambia tokea mwanzo, labda ilikuwa kabla hujafika.
- Je ninaweza kumuuliza mama yako?
- Mama unakaribishwa (kwenye mazungumzo) na mimi nitatafsiri atakachokuambia.
- Je hutamani kuwa mkana dini, au Myahudi au Mnasara?
- Mama (kwa tafsiri ya Khalid): Mungu anilinde, ewe mwanangu, hakuna anayependa kupotea kamwe.
- Je sisi tumepotea?
- Mama (kwa tafsri ya Khalid). Kama sio kupotea basi sijui maana ya kupotea, mimi ni mwenye furaha nimekirimiwa na mwenye utukufu katika Uislamu.
- Je hii ni rai yako au rai ya Wamisri wote?
- Mama (kwa tafsiri ya Khalid): Hii ni rai yangu kwa uchache, kwa bahati mbaya tuna watu, vile vile walioathirika ambao wanaona
- kufuata dini ni kuwa nyuma na kukosa maendeleo.

Kisha akamuangalia mwanae Suleim, akainamisha kichwa chake….

- Lakini mwanamke amedharauliwa
- katika Uislamu!
- Mama (kwa tafsiri ya Khalid): Nani amekuambia hayo?! Umri wangu mimi ni miaka sitini na tano, pamoja na hayo naweza kumuamrisha mwanangu Khalid aje pamoja nami na kunitii kwa furaha kabisa, pamoja na kujua kuwa ni mwenye shughuli nyingi na hataki kuja. Na huwa ananitembelea na wanangu wa kike wanamtembelea mara tatu hadi nne na wakati mwingine mara tano kwa wiki na si hivyo tu bali wanamletea zawadi. Hawawezi kwenda kinyume katika ninayosema mimi au baba yao, je kunakukirimiwa kama huku? Sijui kama kuna ukarimu kama huu sio ukarimu.
- Sijamuona baba yangu wala mama yangu zaidi ya miezi mitatu.

Khalid alianza kubabaika baada ya kusikia majibu ya mama yake, na akamuangalia Suleim ambae alianza kubabaika.

- Unasema nini….?
- Sitaki kukukera.
- Kamwe tafadhali.
- Anasema: Mfano wa Suleim ambae amejifunza kwenu, na kuchukua tabia zenu.
- Mara ngapi tunawaona kwetu wakinywa pombe na bila kuwa na adabu!

www.path-2-happiness.com

- Mama (tafsiri ya Khalid): sehemu nyingi watu wanapoteza dira na kupotea, lakini zama watakapojua muelekeo wao watatubia na kurejea kwa Mungu wao.

Maiko na Sali wakaja kutoka roshani baada ya kumaliza chakula chao…

- Baba, ulituambia kuwa utarejea baada ya dakika ishirini, sasa imefika arobaini na tano, twende kama ulivyotuahidi?
- Samahani, tumewashughulisha na watoto wenu.
- Ooh, sikutanabahi na muda.
- Asanteni sana Suleim, Khalid, Aisha na Abdullah …tumechukua wakati wenu mwingi, hii hapa kadi yangu, je mnaweza kunipa kadi zenu?
- Hii hapa kadi yangu, kuna anuani ya barua pepe, nitafurahi ukinitumia rai yako kuhusu kitabu ewe Katarina.
- Nitajaribu, asante sana.

Khalid alipoondoka pamoja na baba yake na mama yake, Suleim aliwaelekea wageni wake huku akiwataka radhi…..

- Nimekuwa kimya kama nilivyowaambia, nawaombeni radhi kwa kila kosa lililotokea katika haki zenu hata hivyo niliwaambia tokea mwanzo na kukutahadharisheni lakini nyie ndio mliosisitiza.
- Pamoja na kushtushwa walichokisoma, na pamoja na hoja zao nzito ila walikuwa watulivu na wanadiplomasia, kwa hivyo huna haja ya kuomba radhi…..Ha ha ha, bali nenda ukamuombe radhi mama yako kwa kuwa hukumtembelea kwa miaka mingi.

John Luke aliwaaga wote na kuondoka kwenda kazini, na Joji na Katarina walikwenda na watoto wao Trevi Fountain …Chemchem ilikuwa ni nzuri sana, walifurahi sana kuonana kumalizia siku yao nzima iliyobakia pembizoni mwake… kabla ya kuondoka kwao Katarina alitupa ndani yake sarafu ya fedha, Sali alimuangalia

- mama yake kwa mshangao:
- Katika ngano za Kitaliano kuwa atakayetupa kipande cha fedha hapa atarudi tena Roma.
- Baba nipe sarafu ya fedha nitupe.
- Usiamini binti yangu, huu ni ushirikina.
- Najua kuwa ni ushirikina lakini nataka pesa ili niseme nami nimetupa katika Trevi Fountan.
- Chukua hii yako na nyingine ya Maiko, na nataraji ewe Katarina usiwe mshirikina.

Katarina alijibu kwa umakini na

- uwazi…
- Nataraji nawe usifanye mambo kuwa magumu, yafanye mepesi, tupo matembezini.

(3)

- Una nini Katarina?
- Hamna kitu.
- Je hupendezwi na chemchem na utalii pembezoni mwake…sijakuona ukicheka leo na kuzungumza kama kawaida yao?
- Bali ilikuwa ni siku nzuri sana, huenda
- akili yangu ikawa imechoshwa kidogo
- Kwa kitu gani?
- Kwanini ulikuwa unataka kukutana na Waislamu tuliokutana nao? Ili kuwafahamu na kufahamu hadithi zao za kipuuzi na kuwa kwao nyuma, ili kumtayarishia Tom majibu atakaponiuliza kuhusu Waislamu.
- Lakini ulikuwa ukihamasika na maneno yao.

Joji alitabasamu na kumuangalia Katarina machoni na kusema:

- Mimi ndiye niliyekuwa nikihamasika?!

Katarina alifahamu makusudio yake…

- Yeye anazidisha mapenzi yetu kwa Yesu.
- Inaelekea kweli wanampenda Yesu na mama yake.
- Unasema nini?!
- Tofauti ipo katika Uungu wa Yesu, wao wanaona kuwa ni ushirikina, ukafiri na upagani.
- Na sisi tunaona kuwa ni kumpwekesha Mungu na ibada.
- Ha ha ha, je utakisoma hicho kitabu?
- Sitaki kukisomaHa ha ha, lakini uliahidi utakisoma, je unahofia kukisoma kitabu kama alivyokuambia?!
- Maneno gani haya Joji?! Kitabu hakina mbele wala nyuma!
- Swadakta…Kwa nini hukisomi? Kuna kosa gani katika hilo?
- Nani aliyekuambia kuwa nataka kukisoma.
- Kwa mara ya kwanza nakuona dhaifu kwa hoja na kuutetea Ukatoliki, na kwa mara ya kwanza nahisi kuwa maneno madogo tu yanakutingisha.Sitosoma kitabu.
- Ili uthibitishe kuwa unakiogopa kitabu chenyewe.

www.path-2-happiness.com

- Kama ni hivyo nitakisoma basi.
- Una nini Katarina?! Kwa nini huu udhaifu?!
- Sijui, tokea kukutana na Padri nimepatwa na wasiwasi ndani mwangu, huenda ikawa kweli muoga wa kusoma kitabu.
- Wewe sio muoga wewe ni jasiri, bali wewe ni mfano wa kuigwa kwa yakini, nakushauri ukisome kitabu hivi sasa; kinaonekana ni kidogo sana, na mimi ninafungua barua pepe, kwani jana nzima sijaangalia.

Pindi Katarina alipokaa kusoma kitabu, Joji alifungua barua pepe yake na macho yake yakimfuatilia Katarina juu ya hamasa yake wakati wa kusoma.. alipata majibu ya aliowatumia barua pepe na nukuu kutoka torati… kwani walimtumia maoni yao… aliyafupisha

- na akawatumia tena wao.

Tom: Una maana hii ndio sababu ya unyama na Baraad? Inaelekea wasifu huo ni mzuri.

Levi: Pamoja na kufahamu rai yangu katika unyama huu, lakini nyote mnaamini kuwa atakayeshambulia torati atakuwa ameshambulia dini zote za mbinguni.

Habib: Nakubaliana nae kabisa, lakini waangalie Waislamu, pamoja na mimi kutowapenda imani yao inatofuatiana na torati.

Adam: Maneno makubwa ya hatari, je inawezekana kuwa yanatoka kwa Mungu?

Kisha akawatumia barua hii:

Nasubiria leo mtazamo wenu kuhusu fikra na na sio kunukuu maandiko:

"Hakika utatu uliopo katika ukristo ni ushirikina, ni maneno yasiyoeleweka na Mungu ni mmoja tu na Yesu ni mja wa Allah na Mtume wake." Nasubiri majibu yenu kwa ufupi ni mimi.

- Joji.

Joji alimaliza kazi yake katika kompyuta, na kumgeukia Katarina ambae alikuwa makini kusoma kitabu

- kwa utulivu mkubwa…
- Je umemaliza kusoma?
- Hapana, subiri kidogo.
- Akhirisha kusoma mpaka kesho, kuna jambo nataka kujadiliana nawe.
- Subiri dakika chache tu namaliza.
- Unaonekana kuhamasika sana na kitabu!
- Dakika chache tu samahani.

- Nitalala ikiwa ni hivyo.

Katarina alimaliza kusoma kitabu, halafu alimsogelea Joji ambaye

- alikuwa amejilaza kitandani…
- Samahani, nilikuwa mwishoni kumalizia kitabu na nilipenda kumalizia.
- Inaonekana ni kitabu chenye kukinaisha!
- Kwa kiasi fulani, hakina ubaya.
- Nilitaka tupange mambo yetu ya kesho.
- Kesho ni Jumamosi, je hatukualikwa na kasisi kuhudhuria misa?.
- Ndio, ametualika, lakini je tutakwenda?
- Ndio, tutakwenda, je tutaacha misa katika kanisa tukufu zaidi?
- Haa – haa, kwa hivyo mapenzi yako juu ya Yesu yamekufanya uende kanisani na sio Uislamu?
- Ijapokuwa kitabu ni kizuri kwa kiasi kikubwa ila mimi nitasali kanisani kesho.
- Wapi tutawaacha watoto wetu?
- Tutaenda nao kwenye misa.
- Je huwaogopi makasisi?
- Sijakufahamu?
- Siwezi kuwachukua wanangu katika misa, mimi nawaogopea makasisi.
- Unawaogopea nini?
- Nawaogopea kutokana na tabia chafu ya makasisi kwa sababu ya kurudia rudia kusoma kwao Agano la Kale na Jipya Leo wewe unaongea kwa mafumbo, je unaweza kubainisha unakusudia nini?
- Kwani hukusoma kuhusu habari za fedheha za kanisa kuhusu ngono? Je hukusoma kuhusu kesi zilizofunguliwa dhidi ya kanisa kuhusu watoto?
- Sitosahau mahojiano yaliyofanyika na mmoja wa wale aliyebakwa kanisani.
- Ama kwa hakika watawa na makasisi walikuwa ni wanyama na sio binadamu, na sipendi Maiko na Sali wakutane na mambo hayo huko.
- Una nini "Joji? Mimi naenda kanisani kila wiki zaidi ya mara moja na halijatokea lolote mbele yangu, wasiwasi wa nini huu?
- Je umewahi kupitia, kuona, au kukaa, au kujadiliana, au kusoma fedheha ya maadili katika kanisa?
- Hapana.
- Acha tukubaliane yafuatayo, ingia katika You tube na angalia vipande vya video vinavyozungumzia mambo hayo

www.path-2-happiness.com

- humo, na ikiwa utaendelea kusisitiza kwenda nao, kesho tutawachukua
- watoto wetu kwenye misa.Nitatumia muda huu kuangalia vipande hivyo kwa ajili yako, na kesho sote tutakwenda kanisani…umeanza kutumia lugha ile ile ya yule Muislamu tuliyekutana nae katika kuzungumza nami.
- Haa –haa, inaelekea kama yalivyokuathiri mazungumzo nae yule bwana hali kadhalika vipande hivyo vitakuathiri. Lala salama ewe mpenzi wangu.Na wewe mpenzi wangu.

Walikumbatiana kwa muda mrefu, kisha Joji akalala na kumuacha Katarina akiangalia na kusoma habari za kufedhehesha za kijinsia juu ya kanisa, na kuhamia katika fedheha zingine ambazo sio za kijinsia, na hakuhisi muda ulivyokuwa ukipita…alirudia kukisoma kitabu "Mapenzi yangu makubwa juu ya Yesu ndio yaliyoniingiza katika Uislamu" na sijui kwa nini alichagua kusoma kipande hiki:

"Hakika imani ya kujitoa muhanga na kufa msalabani pamoja na kuwa inapingana na akili na fikra, kwa hakika imechangia kufungua mlango wa mapambano kwa kuacha matendo mazuri na kufanya matendo ya shari na madhambi, kama; kuua, kuiba, kupora, kuzini na mengineyo, kwa hakika Paulo alizembea umuhimu wa sharia, wasia, pamoja na matendo mema ambayo alikuja nayo Masiya ili kukamilisha na kuyalingania akasema katika risala yake kwenda kwa Rumia (3:28), "basi sisi tunaamini kwamba mwanadamu anakuwa mwema kwa imani na sio kwa mujibu wa hukumu za sheria", na hata Adam haikumnufaisha amali yake (4:2) na akaja kuikomboa na kuokoka kwa kuwa tuna Imani kwa kusulubiwa Masihi juu yake amani, wala usiulize haki za wanadamu ikiwa ana imani hiyo, na katika kumjibu Paulo kwa riwaya iliyokuja katika ulimi wa Masiya katika Mathayo (19:5) mwenye kuvunja wasia huu mdogo na kuwafundisha watu haya hivi basi atahesabiwa ni katika ufalme mdogo wa mbinguni, ama mwenye kujua na akaenda, huyu atahesabiwa ni katika ufalme mkubwa wa mbinguni."

Alirudia kusoma tena kipande….na kuzinduka kuwa muda ulikwenda sana, usiku ulikuwa mwingi, aliweka kitabu hicho pembeni mwake na kujitupa kitandani na kujisalimisha na mawazo yake hadi akalala.

Joji aliamka mapema asubuhi bila Katarina kuhisi kitu na kuoga na kuvaa nguo zingine….kisha alimsogelea Katarina ili amuamshe na kukuta kitabu kipo pembeni yake katika kurasa ya mwisho aliyofikia. Alichukua na kukisoma na

kisha akakirudisha pale pale kilivyokuwa kimegeuzwa katika ukurasa ule ule.

Joji alikwenda chumbani kwa wanae na kumuamsha Maiko na Sali ili wajiandae, alirudi tena kumuamsha Katarina… na wakati wakitoka kwenda kupata staftahi katika Bafe hapo hotelini, Joji alimgeukia Katarina…

- Leo tunatalii wapi?
- Katika sehemu nzuri na bora zaidi.
- Mama tunakwenda wapi leo?
- Nimemuuliza baba akaniambia kuwa wewe utachagua wapi pa kwenda sisi leo?
- Punde tu tutawaeleza mimi na baba yako.

Katarina aliwaomba watoto wake watangulie kidogo kwenda Buffet ya hapo hotelini, kwani alitaka

- kuzungumza kidogo na Joji.
- Tutakwenda wapi leo?
- Je umeona na kusoma fedheha za kijinsia juu ya kanisa?
- Ijapokuwa mara kwa mara nipo Kanisani, ila kwa yale niliyoshuhudia na kusoma ni mabaya zaidi kuliko uwezo wangu wa kuyasawiri mambo, na kama ni kweli, basi hawa ni wanyama na sio binadamu.
- Hivi unaamini hayo ni kwa sababu ya mafundisho ya Paulo ambayo yanatenganisha kati ya imani na matendo mema? Na ndio maana ukatengeneza itikadi ya kujitoa muhanga na kukomboa.
- Je umesoma kitabu?
- Hapana, ila nimesoma sehemu ambayoilikuwa wazi kitabuni, kwani kuna tatizo gani nikikisoma?
- Hakuna tatizo…nimeshangaa tu na ikiwa utakisoma ni vizuri, mimi sio muoga, na huenda sehemu hii uliyoisoma hasa ndio inaniletea tatizo kwangu, huenda tutapata fikra baadae, la muhimu, ni ipi rai yake juu ya pa kwenda
- leo hii?
- Hatuna budi kuhudhuria Misa kanisani.
- Hapana shaka, ila ni baada ya kwenda kwanza katika bustani ya Villa Benbela, ni busani kubwa kabisa Roma na ndio nzuri zaidi.
- Nahofia tutachelewa kwenye misa.
- Haa haa, hatuchelewi ewe mtawa.
- Sawa, tumekubaliana.

www.path2-happiness.com

(4)

Eneo la bustani ya Benbela Round Villa linafikia kilometa tisa za mraba.. Sehemu pana ya kijani kibichi yenye kufurahisha kwa kupumzika. Pia imezungukwa na aina mbali mbali ya ndege hali iliyowafurahisha Maiko na Sali kuziangalia…

- Chaguo zuri ewe mama yangu, siku ya leo hii ni katika masiku mazuri
- kabisa kwangu.
- Sehemu ni nzuri sana, je imekupendeza ewe Sali?
- Ndio imenipendeza sana.
- Tutakamilisha matembezi haya mazuri kwa kuhudhuria kwetu misa kanisani leo.

Maiko alilalamika kwa kusema:

- Sitaki kwenda kanisani.

Joji alitikisa mabega yake na kumtazama Katarina….

- Hayo ni matakwa ya mama yako muulize yeye.
- Baada ya ziara za kutembelea vitu asilia, hapana budi tutembelee sehemu au maneno ya dini na kiroho.
- Naomba udhuru mama, mimi sipendi kanisa!
- Je hupendi kumuabudu na kumshukuru Mungu wako ambaye amekuumba, kukuruzuku na kukuhurumia?
- Napenda kumuabudu Mola wangu, ila sio kwa kwenda kanisani.
- Binadamu ambae hataki kumuelekea
- Mola wake na kumuabudu na
- kumshukuru, basi dunia itamsonga yeye..
- Je wewe umedhamiria kwenda kanisani?

Joji alitaka kupunguza mjadala….

- Ikiwa hutaki kumuabudu Mola wako na kumshukuru utapata hasara, ila
- idhani kama ibada inafungamana na kwenda kanisani.
- Tutaenda baada ya kukamilisha kustarehe katika bustani nzuri, lakini ole wako ukaacha ibada na shukrani kwa Mola wako ewe kipenzi changu.
- Asante mama yangu, asante baba yangu, lakini kwa nini ibada imefungamana na kanisa tu?

Katarina alipenda kumaliza mjadala….

- Sali njoo uangalie ndege yule kwa mbali…haya twende…

Maiko na Sali walienda haraka kunako ndege….

- Maneno ya Maiko ni mazuri sana.
- Ndio, lakini hayanifanyi ndio sababu katika mambo wasiyopenda watoto?
- Je haikuwa kwenda kwenye misa ni mapenzi yako wewe?
- Tutaendelea na mazungumzo yetu ewe mwanafalsafa usie na madhambi.

Familia ilimalizia muda wao wa asubuhi katika bustani baada ya hapo walipata chakula cha mchana… baada ya kumaliza kula Katarina aliwageukia watoto wake.

- Sasa tunaelekea kwenye misa, na nakuombeni mswali kwa unyenyekevu na muwe makini kwa nafsi zenu.
- Tujihadhari na nini?.
- Kwa kitu chochote au mtu au tendo lolote la kuwaudhi au kuwakera.
- Mfano wa nini?
- Mfano wa kitu chochote kitakachowaudhi au kuwakera, je maneno yangu yako wazi ewe Sali na Maiko?!
- Yameeleweka ila sijui kwa nini unatueleza hivyo? Je sisi tunakwenda kanisani au kwenye bustani yenye wanyama wakali?

Walipo karibia kanisani, Katarina alisogea karibu na Joji na kumnong'oneza….

- Kwa hakika umenifanya niwe na wasiwasi, hivyo basi wewe kuwa makini na Maiko, na mimi niwe makini na Sali..
- Sio kwa kiasi hiki, inaelekea wewe una wasiwasi sana, la muhimu kuwa makini tu.

Wote waliingia kanisani, na baba
Mtakatifu alianza misa takatifu…ila
Joji hakujali, wakati Katarina alikuwa
ni mwenye kuvutwa sana na misa hiyo, lakini akiwa ni mwenye wasiwasi na asie na raha.

Pindi walipotoka tu, Maiko alimparamia mama yake..

- Asante mama, Misa takatifu ilikuwa nzuri, ni kiasi gani nampenda Yesu!
- Alikuwa ni sababu ya kutukomboa sisi, na wanadamu wote na madhambi na makosa.

Sali aliuliza kitoto..

- Mama.. hivi hakuna njia nyingine

www.path-2-happiness.com

- yakututakasa Bwana kupitia makosa yetu pasina Yesu kuuliwa, kwa hakika nimejisikia uchungu mwana Yesu kufa, na mimi nampenda na kwa ajili yake napata zawadi kila mwisho wa mwaka.

Maiko….

- Mimi ni kama wewe Sali… huenda
- kwa sababu hii ndio maana sipendi
- kwenda kanisani, au ni kwa ajili hii siwapendi makasisi na watawa.
- Mapenzi yako kwa Yesu ndio muokozi na mtetezi wako.
- Maiko usisahau matendo mema, kwani imani peke yake haitoshi kama anavyotufundisha Yesu.

Familia ilirudi hotelini baada ya kutoka kwenye misa takatifu na watoto walienda chumbani kwao…na hapo Joji alimwambia Katarina kwa tabasamu la kijanja:

- Ulikuwa na wasiwasi sana kanisani!
- Wewe ulionekana hujali kabisa.
- Ndio, vipi unataka nijali kitu ambacho sijakinaishwa nacho? La muhimu, safari yetu ni kesho kutwa, na tunataka kustarehe katika masiku yanayokuja kama tulivyostarehe katika masiku yaliyopita.
- Mimi nimechoka sana, jana nimechelewa kulala, nalala sasa hivi.
- Mimi nitafungua email yangu, halafu ndio nilale, je unaweza kunipa kitabu ulichopewa na Muislamu.
- Je utakisoma?!
- Huenda, kuna tatizo gani kama nitakisoma?
- Hakuna tatizo, chukua…uamke salama.

Joji alichukua kompyuta yake na kufungua email, ili kupata majibu ya rafiki zake:

Habib: Nimechoka kuwafahamisha wanafunzi wangu wa Chuo Kikuu juu ya Mungu kuwa mmoja na hapo hapo kuwepo kwa utatu sikuweza kupata jibu, huenda mimi mwenyewe sijui, yapo uliyoyataja kwa ujumla kuhusu nakala za zamani kabisa za

Injili.

Tom: Hesabu inasema $3 \neq 1$, na watu wa mantiki wanasema: sehemu ya kitu

kizima kinachukua hukumu ya kitu kizima kimoja, na baba yangu anasema: usizungumzie kitu usichokijua, na mimi nasema: niambie kile ninachoweza kuelewa

ili nipate kukujibu, Haa haa.

Adam: Ikiwa tutasema kwamba Yesu ni mja wa Mwenyezi Mungu na sio mshirika wake au mtoto wake, haimaanishi hivyo ni kumshushia hadhi yake.

Levi: Huyu ni kama mfano wa tunavyosema sisi katika Uyahudi: "Hakika Uzayru ni mwana wa Mungu". Nina hakika kuwa maneno hayo ni maneno yasiyofahamika.

Joji alirudia tena kuwatumia pasina kuwataja majina yao, kisha akaandika barua ifuatayo:

"Sehemu ya tatu: Je yawezekana kuwa Paulo ndio aliyeharibu Agano Jipya?

Ni mimi Joji."

Pindi akiwa anasoma barua zilizobakia, alikuta barua kutoka kwa Kakhi kama

- ifuatavyo:

"Rafiki yangu Joji … nataraji upo mzima wa afya, wafanyakazi wote wanakusubiri, tunatamani kukuona hivi karibuni"

Ni mimi Kakhi!!

"Tanbihi, umekuwa nje ya kazi zaidi ya wiki moja mpaka sasa."

Alihamanika na kutaka kufunga kompyuta yake ila alikumbuka ukurasa wa face book wa Adam na kuwa hajaufungua ukurasa wake kwa muda mrefu na kukuta makala mapya kutoka kwake ikisema: (Mafunzo kutoka kwa rafiki yangu anayetafuta furaha 3):

Rafiki yangu anayetafuta furaha amekumbana na matatizo ya kiafya katika kipindi hiki na kabla sijataja yale niliyojifunza kutoka kwake napenda niweke angalizo juu ya yale yaliyotokea kipindi cha kuugua kwake:

1. Kawaida ya maradhi yanaambatana na udhaifu na hili limemtokea rafiki yangu huyu, na niliogopa pengine asikamilishe lengo lake, lakini ukweli na matarajio ndio yaliyomfanya kuvuka hilo, kwa hivyo kwa mwenye akili hatakiwi kuchukua maamuzi kipindi cha udhaifu na unyonge.
2. Nilikaribia kuvuka mipaka katika muda fulani na kumwambia njia bora ya furaha ni hii nilipomuona amedhoofika, ila Mwenyezi Mungu amemponya.
3. Nina hakika kuwa kipindi kijacho kitakuwa kigumu zaidi kwa rafiki yangu, na huenda nikawapa taarifa yake hatua kwa hatua.

Turudi katika darsa zetu kwa mara nyingine, rafiki yangu bado ana hamu ya kujua njia ya furaha, na nimejifunza kutoka kwake yafuatayo:

4. Hakika wale wanaokuzunguka ima

www.path-2-happiness.com

wataathirika nawe, au wewe uwaathiri au upambane nao na kinachofanya kuwa hivyo ni yale yanayodhaniwa kuwa ni mapambano ya kifikra na kiimaani, na wengi wanaomzunguka wameanza kuathirika naye, na hii ni dalili tosha ya msisitizo wa jambo lake na ukweli wake, na kwa ujumla nadhani kumekuwa zaidi ya mtafiti mmoja katika hili, huenda nikawapeni habari nzuri hivi karibuni kuhusu njia ya furaha.

5. Utulivu wa nafsi na kutoegemea upande mmoja katika kuamiliana na fikra ni muhimu zaidi katika kufikia njia ya furaha; na hivi ndio vitu anavyomiliki rafiki yangu huyu, ingawaje wakati mwingine anakosa kutokana na kubanwa.
6. Umuhimu wa elimu, hata kama unadhani unajua ni lazima kujifunza, huenda unachokijua kisiwe kweli, kwa kweli rafiki yangu amenishangaza kwa kuwa na moyo wa kutaka kujifunza vitu tokea utoto wake na akili yake iliyofunguka vizuri.
7. Kwa masikitiko –Rafiki yangu ana ufahamu mdogo wa kulinganisha au kufungamanisha kati ya matukio, kusoma na mijadala, ambayo ni muhimu sana katika kulinganisha kati ya fikra mbali mbali ili afikie katika njia ya furaha. Naamini kwamba rafiki yangu yupo katika hatua za mwisho katika kutafiti njia bora ya furaha, na katika kujibu maswali makuu ya maisha, nanitakufahamisheni katika darsa zijazo hivi karibuni."

Adam"

Joji alisoma majibu ya wasomaji na kuzingatia jibu la mmoja wa wasomaji aliyesema: "Inavyoelekea wewe unampenda sana rafiki yako, na unamuweka katika sura ya mfano bora wa kuigwa." Na jibu la Adam lilikuwa kama hivi, "Ndio nampendelea kheri kama ninavyopenda kwa kila mtu; na Mungu anatuamrisha kuwapendelea watu kheri."

Kisha akasoma makala nyingine ya Adam inayosema kuhusu mabadiliko ya kifikra,na akawa ameandika yafuatayo:

"Pamoja na ugumu wa kubadili fikra ila leo nimekumbana na uzoefu mpya, nilikuwa pamoja na tabibu wa Nafsi, mwenye uwezo mkubwa wa kufikiri, na mwanafalsafa aliyepevuka, lakini bado anazunguka na kutanga tanga baina ya imani na fikra, alikuwa ni Mkristo halafu akawa kafiri, halafu akawa ni mtu aliyezama katika mambo machafu, amesoma Ubudha, Uhindu, Uyahudi na Ukristo, na anataka kuusoma Uislamu, anayo matatizo mawili. Tatizo la kwanza:

Anafanya falsafa ndio hakimu wa kila kitu. Nilimjibu kwamba, "elimu ndio

hakimu, na sio misingi yako ya kifalsafa, hakuridhika, ijapokuwa ameniahidi atayafikiria maneno yangu kwa mara nyingine.Tatizo lake la pili ni: Anafikiri kwamba kila dini ni janga na kuchukia kila dini, anazikosoa dini zote alizozisoma, je ni kitu gani mnachoninasihi kwake?

Ni mimi Adam.

Joji alijua makusudio ya Tom, alifungua ukurasa wake na hajakuta kipya, na cha ajabu ni kuwa Tom hajafungua ukurasa wake kwa muda wa siku tano hivi, na sio tabia yake. Joji alifunga kompyuta yake, na kuchukua kitabu na kufungua haraka, kwani alijihisi kutaka kulala, lakini sehemu aliyokuwa ameanza kusoma ilimrusha usingizi na hivyo kuanza kusoma kwa mazingatio makubwa, na bila kujua kwa nini alipatwa na mshtuko ijapokuwa yalionekana ni maneno ya kawaida? Je, ni kwa sababu maneno hayo hayapo katika Ukristo?

Kiasi kwamba kuna ombwe kubwa kati ya ibada na kutaka kujitakasa na maisha au ni kwa sababu msemaji wa maneno yale alikuwa ni Mkristo?

"Mwandishi wa Kimarekani Michael H. Hart baada ya kuorodhesha na kuweka misingi muhimu katika kitabu chake, anasema: Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ni mtu pekee aliyefaulu kwa kiasi kikubwa katika Historia na ameonekana katika kila nyanja ya kidini na kidunia.. na kwa muunganiko huu wa kipekee ndio uliomfanya Muhammad awe ni mtu aliyeathiri katika historia ya kibinaadamu." (The 100: A Ranking of the Most Influential Persons in History By Michael H. Hart) Joji alijilaza huku akituliza mawazo yake, na hakujitambua ila baada ya kufika asubuhi na Katarina kumwambia:

- Haa amka, amka yote haya ni kwa ajili ya kitabu.
- Oh… inaonekana unaniogopea, kuwa na amani, wala sijasoma kitabu.
- Haa –haa –hali ni hii nawe unasema
- hukusoma kitabu, ingekuwaje kama
- ungesoma!

(5)

- Haya fanyeni haraka… leo ndio siku ya mwisho kuwepo hapa Roma na tunataka kutembelea sehemu nyingi.

Mchana ulikuwa umesheheni mambo mengi… Familia ilitembelea bustani na sehemu za matembezi, na walipanda boti karibu na ziwa lililotengenezwa….

www.path2-happiness.com

Na kuhitimisha matembezi yao kwa kutembelea soko….na wakati wa kutoka Joji alimfinya Katarina kidogo….na kutabasamu:

- Mbona hujanunua msalaba, umekuwa humpendi Masiya?
- Sijaacha kumpenda ila mapenzi yameongezeka kwa kumtii na kutenda aliyofanya na sio kwa misalaba tu.
- Haya ndio nilikuwa nakueleza tangu kipindi, mapenzi sio misalaba, masanamu, utawa na ukasisi.
- Achana na haya kwa sasa ewe Mprotestanti mbaguzi.
- Au huenda mapenzi yangu kwa Yesu yatanifanya niwe Muislamu wa siasa kali, japo sijakisoma kitabu chenyewe.
- Nadhani unafaa kuwa gaidi kama ambavyo inafaa kuwa Mhindu muabudu ng'ombe.
- Haa haa.

Ilipofika jioni.. Familia ilielekea katika mgahawa wa kifahari pembeni ya mto Tiber, na kupata chakula cha usiku huku wakiwa katika furaha na hewa nzuri iliyokuwa inavuma pale walipo….

- Nimekusikieni sana mnazungumzia dini, je dini ni muhimu sana kwa watu?
- Bila shaka ni muhimu ewe Maiko.
- Rafiki yangu shuleni anasema:Ukafiri ndio asili, na asili ndio ambayo tumeumbiwa, na mawazo ya dini na kufikiri juu ya dini ni katika maneno ya kizamani yaliyopitwa na wakati.
- Na wewe ni ipi rai yako?
- Naamini kuna baadhi ya mambo katika dini ni ushirikina na upotofu.
- Pambanua kati ya kuwa na dini potofu au kuwa baadhi ya dini potofu.
- Ila upotofu ni mwingi sana katika dini kama anavyosema rafiki yangu.
- Kama nini ewe mwanangu mdogo?
- Japo mwalimu shuleni amebainisha sana ila mimi bado sijaelewa itikadi ya utatu wala kujitoa mhanga na….
- Labda ni vile umri wako ungali mdogo mwanangu, na pale utakapo kuwa mkubwa utaelewa.
- Ananiambia rafiki yangu ambaye nimekuelezea: "Kila mtu utakae muuliza atakuambia wewe ni mdogo, lakini naamini wote hao hawajui hilo." Je wewe unajua mambo haya?
- Ndio, ndio kiasi fulani.

- Na wewe baba yangu?
- Ha ha ha, hapana, hapana kiasi fulani tu.
- Nahisi maudhui haya ni magumu, je Mungu anatuchosha ili tufahamu?

Katarina alichoshwa na maneno hayo..

- Ooof, na wewe mambo yako magumu kama baba yako, sivyo hivyo mwanangu bali ni mepesi zaidi.

Joji akiwa imara alisema..

- Vizuri haiwezekani Mungu akaleta kitu ambacho akili haiwezi kukidiriki, ukiona hivyo ujue kuwa inakupasa usome sana ili ufahamu, ama mambo yawe kwa njia ya siri siri tu usikubali hilo.
- Kama ni hivyo baba wewe unakubaliana na yule rafiki yangu?
- Hapana, ukafiri ni ngano ambazo zinakwenda kinyume kabisa na akili.
- Sijafahamu baba.
- Je inawezekana kuwa dunia hii imejitokeza ghafla tu?! Na watu hali kadhalika wamejitokeza ghafla tu.?!
- Wanaokana Mungu hawasemi hivyo baba, bali baadhi yao wanazungumza kulingana na nadharia ya Darwin ambayo tumejifunza katika elimu ya baolojia.
- Ndio, nadharia ya Darwin ni nadharia za siku nyingi sana na sasa hivi imethibitisha makosa yake kielimu na kiakili.
- Unaweza kumuuliza mwalimu wako wa sayansi, yeye anajua kuliko mimi, na nitakununulia kitabu kinachoelezea hilo, inapasa utegemee elimu na sio ngano za watu, hata kama wakati mwingine zikionekena ni za kielimu.
- Lakini tatizo ni kuwa dini inakwenda kinyume na akili.
- Haiwezekani, hakiwezi kimoja kikawa bila za kingine
- Kwa vipi?
- Ninaweza kukufupishia haya kwa maneno ya Einstein: "Elimu bila ya dini ni kilema, na dini bila ya elimu ni upofu".
- Unakusudia elimu ya makafiri ni kilema?
- Bali ujinga wao ni zaidi ya elimu yao, na kile wanachofundisha ni kilema, kama ambavyo dini bila elimu inageuka kuwa ni maneno ya kipuuzi na siri mbali mbali; na kwa hiyo ni upofu…

Maiko alinyamaza kimya, Joji akawa anatafakari maswali haya ni mazito kutokana na umri wake au ni dalili ya uerevu na utambuzi, au ni ugonjwa wa shaka katika hali ndogo.

www.path-2-happiness.com

Familia iliporudi hotelini… John Luke alikuwa akiwasubiri katika ukumbi wa mapokezi, mara tu alipowaona alisimama na kuwatolea salamu.

- Ni ziara ya ghafla, karibu sana.
- Rafiki wa kasisi karibu sana, hatujakuona kwenye misa!
- Sijahudhuria kwenye misa kiasi cha mwaka hivi.
- Kama ni hivyo basi unawezaji kusuhubiana na kasisi?
- Yaelekea kasisi ni mtukufu sana kwako, ijapokuwa ameshindwa kujibu maswali ya Joji na kutukimbia, nimethibitisha kwake yaliyojiri.

Joji kwa mshangao:

- Je ulikuwa huniamini mimi?
- Hapana, ila ni kwa kujiridhisha tu, kwani nilishangazwa na matendo yake, inaelekea kama ulivyosema, hakutaka kasisi Katarina kutoka peke yake.

Katarina alifungua macho yake kwa mshangao…

- Kwa nini iwe mimi tu?Nimekuambia wewe kwamba yeye
- anatenganisha maneno ya jamii kwa ujumla ambayo wewe ni mmoja wa wanaofaidika nayo, na kati ya maneno maalumu yasiyo jumuisha jamii yote,
- kwa ujumla….Sitaki kurefusha muda wenu, nadhani safari yenu ni kesho.
- Ndio.
- Nimekuja kuwaaga, na napenda mawasiliano yaendelee, na mimi nimefurahishwa kuonana na nyinyi.
- Na sisi pia… nakushukuru.
- Nina ombi, je unaweza kunipa kitabu?
- Kwani nimemuomba rafiki yangu na kunieleza kuwa ni hii tu nakala moja alikuwa nayo.
- Kwa kiasi hiki, kitabu ni muhimu sana kwako?
- Kikao chetu cha siku ile kilinithibitishia kwamba mimi sijui
- Uislamu isipokuwa ni maneno ya juu juu tu, na ripoti za vyombo vya habari tu, na nimedhamiria kuijua dini hii, na jina la kitabu limenivutia sana.
- Nitapanda chumbani na watoto na nitakuletea kitabu….Haya Maiko na Sali tuondoke.

Joji alitabasamu huku akicheka na kusema:

- Haa haa, hivyo umekusudia kuusoma Uislamu?
- Ndio.
- Na je utakuwa Muislamu?

- Je unategemea niwe kama Rais
- Gadhafi rais wa Libya aliyepita mimi nasoma kila fikra bila ubaguzi, na katika kikao kile nimegundua sijui chochote katika Uislamu pamoja na maarifa mengi niliyonayo kuhusu Uislamu lakini yote hayo hayana uhakika.
- Mimi sijausoma Uislamu, nitausoma safari zijazo mbeleni, na kwa masikitiko sijakisoma kitabu na nilipenda kukisoma.
- Samahani kitabu ni chenu na samahani kwa kukitaka kwa dharura.

Katarina alikuja na kitabu na kumpa John Luke ambaye alitoa karatasi na kalamu na kunukuu baadhi ya maneno ya kitabu kisha kurudisha kitabu kwa

- kuwashukuru….
- Je hutaki kitabu?
- Nimechukua tovuti ya kitabu katika mtandao wa kimataifa na hayo yanatosha, asanteni sana.

Joji na Katarina walienda chumbani… na Joji kufungua kompyuta, alikuwa akisubiri majibu ya marafiki zake kuhusiana na barua yake aliyouliza: Kama Paulo ndiye aliyepotosha torati au nani? Kwa mshangao majibu yao yote yalikubaliana kuwa ndie aliyepotosha, lakini njia za majibu yao zilitofautiana … aliandika majibu yote na kuwatumia tena wote…

Habib: Kihistoria… kwa masikitiko ndio.

Tom: Ikiwa imepotoshwa sijali ni nani kaipotosha.

Adam: Swali tata, sijui nani kapotosha.

Levi: Na ni nani aliyeharibu Agano la Kale kama ni hivyo? Huenda ilikuwa ni tatizo katika uandishi na kuchelewa kwake kuandikwa, na sio kusudio ni kupotosha au kuharibu.

Kisha akawaandikia hao:

Sehemu ya nne: je wewe unahamu ya kuusoma Uislamu? Na kwa nini?

Nasubiri jibu kwa ufupi samahani … kesho jioni nitakuwa London.

Ni mimi Joji – Roma”

Aliwatumia rafiki zake wote, na akaongezea kwa mara nyingine Katarina na John Luke… na akaendelea kufungua email yake na kukuta ujumbe wa Tom:

“Kwa marafiki zangu wote, nahisi ukurasa wangu wa face book umeibiwa na nafanya mashauriano na mtandao kuurejesha tena, na mtanisamehe kwa kasoro yoyote mtakayoiona sio kutoka kwangu.

Ni mimi Tom”

www.path-2-happiness.com

Alifungua ukurasa wa Tom na kukuta picha zake akiwa na wanawake wengi wasio jisitiri vizuri, akawa anajiuliza: Je Tom ameanza vita na Baraad? Kisha akakumbuka makala ya Adam kuhusu kubadilika fikra za daktari, na akasema: amesema kweli Adam, nadhani Tom alikuwa na bahati. Joji aliendelea kuangalia picha, na kugundua baada ya muda mfupi kuwa alikuwa akiangalia picha zile za wanawake huku akimtafuta Katarina humo, na akahisi kuwa hiyo ni shaka ambayo sio sehemu yake, wala haimfalii yeye Joji wala Katarina, alifunga Kompyuta nakuelekea kwa Katarina, na kumkuta amejilaza chali kitandani na kumbusu, Katarina alipata hisia za busu na yeye kumbusu Joji na kufungua macho yake na kutabasamu…

- Nakupenda.
- Na mimi pia nakupenda vile vile, nisogelee.

Siku iliyofuata ilipita kwa haraka sana, na hawakuwa na muda wa kutosha kabla ya muda wa kuelekea uwanja wa ndege, walikwenda sokoni na huko Katarina alimkumbusha Joji zawadi ya Adam. Ambae alitaka mkoba wa kifahari wa ngozi lakini wa bei rahisi sana, kiasi katika mzunguko wao walisimama katika duka la mikoba ya ngozi za asili na walikuwa wana seli ya baadhi ya mikoba, ikawa aina hizo za seli seli zinafikia discount ya asilimia 80 ya bei ya asili, na hivyo akamnunulia Adam mkoba mmoja wa kifahari kwa bei rahisi sana wakatoka hapo dukani wakishangazwa na maombi ya ajabu na bahati waliyopata

kununua.

Baada ya kula chakula cha mchana karibu na soko walilokwenda, walirejea hotelini na kufunga mizigo yao na wakaelekea uwanja wa ndege.

SIRI YAFICHUKA

www.path-2-happiness.com

13 SIRI YAFICHUKA

SIRI YAFICHUKA

(1)

Joji alijisikia ni mwenye nguvu na furaha zaidi baada ya kurejea kutoka Roma, na kujikuta amekuwa mwepesi baada ya kuwa na msongo wa mawazo, hali iliyomfanya kukesha na kujiulizia maswali haya: Je alivyo kuwa akihisi ni kwa sababu ya kazi na kusoma sana, hali ambayo imemchukua muda mwingi? Au ni kwa sababu ya kuchanganyikiwa na mawazo yasiyokuwa na majibu kuhusiana na Biblia na Mungu, bali na kwa Yesu na kila migawanyiko yake? Au haya anayojisikia sasa hivi isijekuwa ni furaha ya mchezo wa mtoto mdogo kwa kuvunja au kumharibia mchezo wake. Na je hali itakuwaje baada ya kanisa, au mapapa, au wa Biblia litakapovunyika katika nafsi yake, wapi atapata pakwenda? Au atakaa bila dini (kafiri)? Mwenye kukosa upando wa kiroho wa furaha? Kisha alitoa sauti ya kusema, 'Ewe Mungu, Ewe Mungu'.

Katarina alifurahia safari hii, na kurejea na furaha kubwa sana…..hivi ni kwa ajili ya mume na watoto wake?! Au ni furaha iliyofunua pazia ya yale aliyokuwa akiyashangaa na kufurahishwa nayo, kwani alikuwa akiyatafakari maisha kwa mtazamo tofauti? Kwani alikumbuka mgongano wake na kasisi pamoja na udhaifu wake, na kukumbuka udhaifu wake mbele ya Mmisri na Kitabu chake, na kimya chake mbele ya John Luke na hoja zake na akawa anajiuliza mwenyewe: Mimi nina yakini bora zaidi kushinda shaka, kisha akajiuliza: Kwa nini nina furaha kwa sasa hivi?!

Walipofika nyumbani, na nyoyo zao kutulia. Joji alifungua barua pepe yake kuangalia je amejibiwa na rafiki zake au bado? Na kwa bahati alikuta tayari amejibiwa na wote. Alifuta na kuanza kuwatumia wote kama alivyofanya kwa mara ya mwisho kwa hawa wafuatao:

Levi: Ndio, ijapokuwa ninawachukia Waislamu waliomuua baba yangu lakini hilo ni kwa ajili ya kujua shari ambayo itawafanya kuishi kwa salama.

Habib: Ndio, hiyo ni dini ya mbinguni, pamoja na kuwa ujuzi wetu kuijua ni mdogo.

Tom: Ndio, huenda nakutana na vitu ambavyo sijaviona kwingineko.

Adam: Ndio hasa, maudhui yanahitaji utafiti ili kujua kila dini za mbinguni.

John Luke: Ndio, mimi napenda kusoma na kujua kila kitu.

www.path-2-happiness.com

Joji hajapata jibu lolote kutoka kwa Katarina kwa sababu hajafungua barua pepe yake tangu waliposafiri kwenda Roma…..Joji aliandika sehemu ya tano na kuwatumia hao wote…

"Sehemu ya tano: kwa: Hakika nimeshtushwa na majibu yenu wote, Jibu la ndio, na hata kama sababu zinatofautiana. Sasa swali langu la leo ni: Naomba kila mtu aowanishe kwa kifupi kati ya vitabu vya dini tatu za mbinguni: Agano la Kale, Agano jipya na Qur'ani.

Joji (London)".

Zilipita dakika chache baada ya kutuma ujumbe wake, mara simu yake inaita kutoka kwa Tom na Sauti yake ilikuwa inajulisha wasiwasi na huzuni….

- Kuna nini?
- Hakuna kitu, nilitaka kujiridhisha tu mmefika? Na napenda kukutana nawe, je lini tunaweza kuonana?
- Tumefika kabla ya dakika 45, na muda umepita, je tunaweza kuonana kesho? Au kama vipi njoo sasa hivi?
- Oh, samahani sikujua muda, nisamehe kwa hilo, basi nitakuja kesho saa nne asubuhi nyumbani kwako.
- Nitakusubiri, Mungu akipenda ni kheri tu kwa mapenzi ya Mungu.
- Nakushukuru Joji, pia narudia kusema nisamehe.

Simu ya Tom ilimtia wasiwasi Joji kisha haraka alikumbuka ujumbe wa Tom uliosema kuwa kuna mtu amepenya katika kompyuta yake kuingia katika face book yake, na ugomvi wake pamoja na Baraad, kisha alifungua tena kompyuta yake na kufungua ukurasa wa Tom wa face book. Ghafla aliona picha ya Katarina akiwa amevaa vibaya akiwa pamoja na Tom! Alijaribu kuchunguza kwa wawili hao nakukuta ishara ya uso wa Katarina ukiwa dhahiri kutohusika na jambo hilo, picha hizo zilikuwa ni pigo kubwa kwake zilizomsahaulisha furaha yake ya Roma pamoja na starehe zake. Na alijiuliza kwa kusema:

- Inavyoonekana kila kitu ni uzushi na kuongopeana mpaka kujua ukweli wake!

Alijaribu kutaka kuwasiliana na Tom lakini aliamua kusubiri mpaka kesho saa nne ili kujua nini kitatokea. Alijaribu kulala ila hakupata usingizi na muda wote fikra za Katarina na Tom hakuziacha kuzifikiria, na hajui nini kilichomfanya kuamini uongo wa Katarina na Tom? Maisha gani haya? Na tabia gani nzuri watu wanajisifia huku wakiongopa? Urefu ulioje wa muda kuondoka! Na hata muda naona unachelewa mara mrefu na mara mfupi

ijapokuwa hali hiyo ni moja tu.

Katarina aliamka saa tatu asubuhi, hali ya kuwa Joji bado alilala….alijaribu kumsogelea na kumbusu na kumnong'oneza kwa kusema:

- Mpenzi wangu, naomba ruhusa naenda kununua mahitaji ya nyumbani.

Kwa haraka baada ya Katarina kutoka, Joji aliamka akimsubiri Tom aliemuahidi kufika saa nne kamili asubuhi, na mara alimpokea kwa uso wa hasira usio na furaha.

- Nasikitika kwa usumbufu masuala ni mepesi ila yenye kusikitisha.
- Sema ulichotaka kusema.
- Hakika nimeanza vita vikali na Baraad.
- Je hukuwa unategemea hilo?
- Naam kwa maana (ndio) lakini ni vita vibaya na vichafu.
- Je unategemea kutoka kwa Baraad lisilokuwa hilo?
- Hapana niache nikamilishe samahani, kwa hakika alinitaka nishirikiane nao katika genge la kuuza madawa ya kulevya au kufanya machafu, nikamkatalia, akanitisha na kurudia kunitisha nikamkatalia, na nimeshtushwa ghafla kabla ya siku chache nikagundua kompyuta yangu sehemu ya face book haifungui, nikajua huenda kuna tatizo katika mtandao, mara tu nikashitukizwa kuona picha zangu za zamani ambazo sio nzuri zinatokea katika akaunti yangu.
- Na hili limetokea kwa asilimia100% sio hivyo?
- Niache nikamilishe samahani, baada ya kudhihiri picha hizo aliendelea kuniomba nishirikiane nae nikakataa na hapa ikaanza kazi chafu kama mwanzo yakuweka picha za kuzusha ambazo sio za kweli juu yangu. Kwa kuzishusha kwenye mtandao.
- Kisha nini unataka kutoka kwangu?
- Sijui nikuambie nini, kwani ameunganisha picha ya Katarina na mimi tukiwa kanisani na kuniunganisha na picha yangu akiwa uchi.
- Unataka kusema picha hiyo ni uongo na sio kweli katika face book yako?
- Ndio sio yenyewe kwa kweli.
- Najua unayemzungumzia hapa ni mke wangu na mimi nina hakika kuwa ni picha yake.
- Ndio ni picha yake, ila ni picha iliyopandikizwa na sio kweli.
- Inatosha Tom…yatosha kunichezea!
- Ichunguze picha kwa undani, utajua ni ya kupandikiza.

www.path-2-happiness.com

- Toka! toka nyumbani kwangu.
- Usinidhulumu na ukamdhulumu Katarina, ewe Joji.
- Toka, toka.

Joji alijilaza katika ukumbi hajui cha kufanya, alikuwa katika hali ngumu sana. Simu yake ilianza kuita na kukuta ni namba ya Adam, alisita sita kwa kudhani anamcheza shere na mimi ndio wapekee mjinga wa kuchezewa…nini anataka huyu sasa?!

- Hallo, ndio Adam!
- Karibu, tumekukumbuka.
- Unataka nini?
- Hamna kitu, nilitaka kukusalimia tu!
- Nashukuru, asante sana, kwa heri.

Joji aliweka simu yake huku akifikiri nini cha kumwambia Katarina atakae fika muda sio mrefu, baada ya kuhisi kudhalilishwa na udhalili wa hiyana na wa kukusudia…alijizuia kidogo kusema baada ya kumuona Katarina anaingia akiwa na tabasamu.

- Bado chai haijawa tayari hotelini kama Roma, je umepata kifungua kinywa au unapenda nikuandalie chochote?
- Sitaki chochote.
- Kama ni hivyo kunywa kikombe cha maziwa au chai?
- Ahsante.
- Nisaidie tule pamoja japo kidogo.
- Nimekuambia sitaki kula chochote hunielewi?
- Joji una nini?
- Siri imefichuka ewe Katarina.
- Siri gani?

Alifungua ukurasa wa Tom mbele yake….na kuondoka kwa hasira chumbani huku akifoka kwa maneno.

- Tazama, ewe mfanya ibada na mchamungu, wewe ni mnyama mdogo na ukiingia katika utawa utakuwa mnyama mkubwa kwa matendo machafu kama makasisi, na watawa makanisa –angalia.

Katarina aliangalia zile picha na kumrudia Joji huku akilia…..

- Tom ni muongo sana, hizi sizo picha zangu.
- Je unataka kuwa msanii uliobobea kwa kuendeleza maigizo? Ili kesho mlale

pamoja…..

- Niamini, mimi sio mwenye kufanya haya, huu ni uongo wa wazi wa Tom. Je hukuniambia mara kwa mara kwamba yeye sio mtu mwenye tabia nzuri tena asie na dini?.
- Sio wewe ulie nisisitiza niende kwake? Sio wewe uliomfundishia dini? Sio wewe uliyesema amebadilika!
- Sikutegemea unishuku tena…

Katarina aliishiwa na nguvu huku akilia kwa uchungu kisha akajikaza na kwenda katika kompyuta kwa mara nyingine akawa anaangalia zile picha huku akitukana na kumlaani Tom wakati akiwa anazichambua, mara jicho lake likaona picha ya kupandikiza na kuipeleka kwa Joji haraka.

- Angalia picha iliyotengenezwa, je kifua hiki ni sawa na kichwa hiki?!
- Maneno kama ya Tom, ya kusema picha ya kupandikiza, je huu ni mlango wa pili wa maigizo?
- Angalia vizuri.
- Huenda ikawa hivyo, lakini sitaki kuwa mjinga kwa mara nyingine wa kuamini maigizo yenu kwangu!
- Vipi Tom anasema ni ya kupandikiza wakati yeye ndio aliyoiweka?
- Tom amekuja na kudai Baraad ameiba kompyuta yake na yeye ndie aliyetengeneza na kuweka picha hii kwa kumkomoa.
- Baraad! Kwa nini anafanya hivyo kwa kumkomoa?
- Hili ni hitimisho la maigizo katika tamthilia, eti kwa kuwa amekataa kushirikiana nao katika kuuza madawa ya kulevya.
- Mimi sijamuelewa anachodai, ila naamini picha hizi ni za kupandikiza bila shaka.
- Inawezekana ni za kubuni au ni za kweli, je hajakutumia ujumbe ya kuwa akaunti yake ya face book imeibiwa? Au tumefungua ukurasa mpya wa maigizo?
- Sijamuona Baraad tangu tusafiri kwenda Roma, hebu nipe kompyuta niangalie huenda nikakuelewa.

Katarina alifungua akaunti yake katika face book na kukuta barua mbili…. barua ya kwanza inayompa taarifa kuwa Tom ameibiwa akaunti yake na barua ya pili inaonyesha picha mbaya za kufedhehesha, kama picha ile ya Tom iliyopo katika face book yenye ujumbe usemao: (Huu ndio ushahidi wa kweli wa kujivua) aliziangalia kwa umakini na pembeni ya Tom alikuwa ni Joji na sio yeye!

www.path-2-happiness.com

- Bali wewe ndio ulionifanyia hiyana, angalia picha hizi.
- Nikufanyie hiyana na nani sasa?!
- Na Tom, je huoni ni kinyume na tabia za watu ewe Mprotestanti?

Joji alizichunguza picha na kujua ndio zenyewe na kwamba ni za kupandikizwa…Joji aliinama chini kidogo kisha kuinua kichwa chake kwa sauti kali yenye kutisha….

- Unajua nimemfukuza Tom hapa nyumbani.
- Joji unanishuku mimi?
- Na nimekata simu ya Adam nikidhania kuwa anataka kuendelea na kutaka kukamilisha igizo kwa makubaliano na Tom!
- Yote haya ya nini Joji?!
- Adam amenisihi sana kutokuchukua maamuzi wakati wa hasira au unyonge, sijui nifanye nini sasa?! Samahani Katarina, nimekuvunjia haki yako.
- Yatosha msamaha tu baada ya yote haya?!
- Unataka nini nikufanyie?
- Sijui ila msamaha unatokea baada ya ukubwa wa makosa?
- Nakuomba nisamehe, nitaangalia nini naweza kufanya kuhusu Tom na Adam.
- Ijapokuwa umenijeruhi kiasi kikubwa ila sikutegemea kama unaweza kunifanyia hivi, pamoja na hilo nakusamehe kwa sharti la kufuata nasaha za Adam ulizonitajia.
- Asante Katarina, wewe ni mtu mwenye moyo mzuri sana, sijui nikushukuru vipi na kukusahaulisha makosa yangu kwako, kisha alisimama na kumkumbatia na kusema, nitazingatia suala langu hili na Tom na Adam, je unaniruhusu nipumzike kidogo peke yangu?
- Sawa karibu, japo umenijeruhi ila nitamuomba Mungu akusaidie kwa msaada wake.

Joji alikaa mbele ya kompyuta yake na kufungua barua pepe yake kwa kumuandikia ujumbe Tom unaosema hivi:

"Rafiki yangu Tom.

Baada ya kutokea yaliyotokea kati yangu na wewe, naomba nisamehe kwa kukuvunjia heshima yako, umekuja nyumbani kwangu kuomba msamaha na nilitarajia kukusamehe, nirudishie kama nilivyokufanyia, na ukitaka nije kwako na unifukuze kama nilivyokufanyia mimi nipo tayari kuja, narudia kusema nisamehe sana

Mimi Joji."

Baada ya hapo alimpigia Adam pale pale na kumuomba msamaha….

- Adam, hakika nimekuletea mkoba mkubwa na kwa bei nafuu sana.
- Je umepata? Na kwa sifa hizi?
- Ndio, na lini utakuja kunitembelea ili unichukue?
- Haa haa…angalia muda wako unaofaa mpaka usije kuniambia maneno kama ulivyoniambia leo.
- Ni muda gani unaokufaa, nisamehe kwani nilikuwa katikati ya udhaifu na wasiwasi, huenda tukikutana nitakueleza.
- Njoo kwenye mgahawa, kwani muda mrefu hujanitembelea hapo.
- Vizuri… nitakutembelea leo au kesho.

Alimaliza maongezi, na akawa anatafuta barua pepe huku akisubiri ujumbe kutoka kwa Tom…akakuta ujumbe ambao Tom aliutuma kwa Katarina alimtumia naye vile vile wakati akiendelea kutafuta, alipokea ujumbe wa jibu la barua yake.

"Sikia na utekeleze yale ninayokuambia, huenda nikakusamehe:

Utakuja kesho katika zahanati saa moja jioni, na mimi nitaamua kukufukuza au hapana.

Usirudie muamala huu mbaya wa kuhamaki.

Tekeleza yale ninayokueleza haraka iwezekanavyo baada tu ya kuusoma.

Ni mimi Dr, Tom".

Joji alimjibu:

"Rafiki yangu Tom mimi nakubaliana na wewe na hata ukinifukuza mimi bado nimekosea.

(Joji)."

Baada ya kumjibu Tom aliwasiliana nae kwa kumkaribisha…

- Karibu
- Asante, naomba tena nisamehe kwani nilikuwa nina hasira.
- Usijali, lakini mimi nimesahau kutaja sharti lingine, na ni lazima ukubaliane nalo…
- Lipi hilo?
- Ha ha ha… Joji kila kitu kimeisha, nilikuwa najoki tu na wewe, kesho tuonane katika mkutano wetu muhimu sana.
- Nakushukuru Tom.
- Ikiwa utachelewa katika… ha ha ha, mimi nakusubiri.

www.path-2-happiness.com

- Nitakuja katika wakati huo ili unifukuze…narudia kusema nisamehe.

(2)

Mwishoni mwa mazungumzo ya Joji na Tom alikumbuka ahadi yake ya kukutana na Adam.

- Nitakwenda sasa hivi kumtembelea Adam pale mgahawani.
- Adam ni mtu wa hekima na mwenye akili, na nisingekuwa na kazi ningeenda na wewe.
- Kweli, lakini sijui yeye anafaidika nini na usuhuba wangu?!
- Urafiki sio mpaka tubadilishane na vitu kama pesa.
- Huenda ni kupata chakula cha mchana pamoja na hii ndio faida pekee anayoipata kutoka kwangu kwani yeye anaishi peke yake.

Joji aliwasili mgahawani na kupokewa na Adam, na kumwambia muda wao hapo mgahawani ni nusu saa tu na akamshauri anywe kahawa ndani ya muda huo. Baada ya hapo Adam alimaliza muda wake na kuelekea kwa Joji na kuamua kwenda kupata chakula cha mchana katika mgahawa wa furaha.

- Mbele yetu tuna muda wa saa moja kwenda na kurudi pamoja na kula chakula sawa… Sasa niambie vipi ngome ya kanisa Katoliki na kituo chake kikuu?
- Je hutakasirika nikikueleza?
- Inavyo onekana unaguswa sana na mambo, nini cha kunikasirisha ewe Joji?!
- Haiwezekani kusadikisha Agano la Kale wala kuiamini, kwani halinifai, sio Uyahudi, Ukatoliki, Uprotestant wala Uislamu.
- Kwanza, kwa nini juhudi zote hizi dhidi ya torati? Je hiyo ni kwa sababu ya kipande cha maneno ulichotutumia?
- Hili ni moja, lakini nina sababu zingine mia moja mfano wake kwamba imepotoshwa.
- Na Agano Jipya?!
- Nalo ni hivyo hivyo, japo hilo lina afadhali.
- Na Qur'an?!
- Kwa sababu inaamini agano la kale na linalopita na kama hizo vile vile
- Nakuomba usiwe na haraka kutoa hukumu.
- Pamoja na yote hayo, kuna masalia ya hisia zangu kuwa nitapata majibu ya maswali yangu.
- Kwa dhati kabisa utapata majibu.

- Tatizo ni kuwa hakuna dini yoyote iliyokuwa sahihi; kwa maana hiyo suluhisho ni kukana Mungu!
- Haiwezekani hata siku moja ukanaji Mungu ukawa ndio njia ya furaha.
- Kwa hiyo njia ni ipi?
- Endelea kutafiti na utapata jibu.
- Haa haa, huenda ni Uislamu au dini ya ugaidi!
- Pindi ulipotuuliza ni nani ambaye anataka kuujua Uislamu majibu yalikuwa ni ndio pamoja na kuwa na dini zetu tofauti, kwa nini sasa wewe hutaki kuusoma Uislamu na kuujua?!
- Mimi nakuzidini sana katika kutaka kuujua Uislamu, kwa sababu nyingi tu zaidi ya hizo mlizozitaja, zatosha kama hazifai hazitafaa dini nyinginezo.
- Sijui kama utasoma dini kwa njia hii!
- Tumeshafika hoteli ya furaha laiti tungeifikia njia ya furaha, tumalizie mazungumzo yetu ndani.

Walichagua meza yenye kuwafaa na mhudumu hakuchelewa kuchukua oda yao ya chakula nakuondoka, na wakati huo Adam alimuangalia Joji kwa umakini.

- Nitakamilisha niliyotaka kukueleza, ulipokuwa unajiandaa kwa safari ya Roma, na kusoma kuhusu Ukristo nilikueleza nini?
- Nilikueleza: Tengemana nayo kwa uhuru zaidi, yaani usome kwa kujua kabla ya kulihukumu jambo kwanza.
- Na mimi nakueleza hilo tena sasa, na wala usipende kusoma Uislamu bila kutumia njia hiyo.
- Na nimeanza kufikiri jambo hilo nikiwa kwenye ndege ni vitabu vipi nitavisoma kuhusiana na Uislamu.
- Je unataka nikushauri?! Anza kuisoma Qur'an kabla ya kitabu chochote kile.
- Kwa nini nisingeanza na Uyahudi na Ukristo kwa kusoma vitabu vyao mwanzo?
- Kwa sababu Uyahudi haukusukumi kusoma Agano la Kale bali wanaficha baadhi ya aya kwa malengo yao, na Ukristo haukuvutii kusoma Agano Jipya moja kwa moja, bali inapasa uelewe kama waelewavyo wanazuoni wa kiyahudi na makasisi.
- Na Qur'an je?
- Sijakueleza wewe kwamba hutaujua Uislamu, kwani Uislamu umeifanya Qur'an ndio chimbuko la elimu, na kutoa habari njema, maonyo, ujumbe kwa Waislamu na wasio Waislamu.

www.path-2-happiness.com

- Adam inaonekana umeusoma sana Uislamu, je umeusoma kupitia masomo yako ya dini mbali mbali?
- Ndio.
- Kwa kweli ni ipi rai yako kuhusu Uislamu?
- Mfano wako, si wa kupewa rai, soma Qur'an na uchukue ushauri na uamuzi mwenyewe.
- Kwa dhati ni ipi dini yako? Nilidhani tangu mwanzo wewe ni Myahudi au Mkristo ila kwa sasa unaonyesha wewe ni Muislamu.
- Je haiwezekani pia nikawa Mbudha au Mhindu, unakumbuka nilipokuambia kuwa ni vizuri kuujua Ubudha au Uhindu, napenda kukuhakikishia kama mtu hatakuwa na akili yenye kufikiri mbali zaidi na kuondokokana na akili finyu, hatopata maendeleo kamwe, kama ambavyo nataka kukueleza dini na dhehebu langu baada ya kutaka kujua kila unachotaka kujua kunako njia ya furaha, na huenda ikawa njia hii ndio mbadala wa dini zote.
- Sijapata mbadala wa dini zote katika akili yangu katu.
- Isome Qur'an, halafu yaliyo andikwa na Qur'an juu ya Uislamu na Mtume wake, kisha linganisha na dini zote, uwezo wa kufungamanisha kati ya maudhui na maarifa uliyonayo ni jambo muhimu sana kufaulu.
- Vipi nitafungamanisha kati ya maudhui haya?
- Ili usipoteze dira ambayo unakwenda nayo, kumbuka kile usicho kitaka katika Ubudha au Uhindu na uhakikishe hakipo katika Uyahudi, kisha katika Ukristo na sasa hakipo katika Uislamu, na kile unachokiendea katika Ubudha kwa mfano uthibitishe kuwepo katika Uyahudi au Ukristo na Uislamu na kwa hivyo utaoanisha kati ya maudhui.
- Mtazamo huo wa mambo kwa ujumla wote unanipendeza kati ya ninachotaka na nisicho kitaka.
- Na uchunguze mfanano kati ya dini mbali mbali na tofauti zilizopo pia.
- Kwa masikitiko naona mfanano wa dini ni mkubwa kuliko tofauti iliyopo.
- Ukifungamanisha itakuzidishia akili na kufikiri zaidi, na hakikisha kuwa unafungamanisha kadhia za jumla na sio katika vipande vipande tu.
- Kwa kuwa mimi naona kuna kufanana kwani wote wanaamini Agano la Kale, na naamini kwamba mwenye kuamini hivyo ni mwenda wazimu.
- Lakini Wakristo wanaamini kwamba Agano Jipya limekuja kukamilisha Agano la Kale kwa Imani yao hiyo. Wakati ambapo Wayahudi na Waislamu hawaamini

kama wanavyoziamini, kadhalika wanaamini kuwa imepotoshwa, na ya kuwa hii iliyopo sasa sio maneno kutoka kwa Mungu, na wanaiamini Qur'an, na ndio imekuja kufuta yaliyotangulia, je mpaka hapo huoni kuwa kuna tofauti kubwa?

- Ndio…tofauti kubwa sana, kwa tabia yangu mimi naangalia katika kufanana zaidi kuliko tofauti, na wala silinganishi baina ya maudhui sana.
- Vizuri, kujua tatizo ndio suluhisho, hivyo utakuwa umefikia kwenye suluhu ya maudhui, na utakuwa na uwezo wa kuangalia kwa ukamilifu wake, ikiwa umemaliza kula ni vizuri tuanze kuondoka ili nisichelewe kazini.
- Ndio nimemaliza, haya twende, nisije kusahau, mkoba wako mkubwa sana wa bei rahisi ninao kwenye gari.
- Japo umenicheka ila umeniletea kwa sifa nilizozitaka.
- Ghafla kulikuwa na duka moja linafanya seli ya baadhi ya mikoba, na huu ndio ulikuwa mkoba wa mwisho kwa ukubwa huu.
- Jambo lolote la ghafla na lisilotarajiwa linabainisha ni kiasi gani watu wasivyojua kile alichowakadiria Mungu, kwa masikitiko wengi wetu hatujui kulitumia neno 'bahati' wakati hatujui limetokeaje jambo, na kwa hili, tunajiona tunajua kila kilichopo ulimwenguni ikiwa kitatokea kitu hatukijui tunalitumia neno 'bahati' kama kwamba kutokujua ni kutokuwa na elimu na bila shaka ni katika aina ya mshangao, kujidanganya, ghururi isiyotakiwa…au ni aina ya kuathirika na ukafiri pasina kujua hilo.
- Umenichosha na falsafa yako na istilahi zako ngumu, haahaa. Mungu ameniwezesha kufika na ikawa mkoba mmoja umebakia, je nimefaulu mtihani wangu?
- Haa haa, kwa sharti begi hilo liwe kubwa sana na rahisi pia.
- Ikiwa ni hivyo nimefaulu na hili hapa begi, chukua.
- Vizuri, kwa hakika umepita mtihani, na hii ina maanisha kuwa wakati mwingine hatuwezi kufahamu uhakika wa jambo kwa akili zetu tu.
- Lakini haiwezekani uhakika ukatofautiana na akili, kwani haiwezekani ukweli halisi uwe kinyume na ufahamu wa akili yenyewe, vinginevyo moja wapo sio kweli.
- Swadakta, umetofautisha ilivyo, kwa idhini ya mwana falsafa?!
- Leo nimemkosea Tom kwa kumfukuza nyumbani, na nimemuomba msamaha na amenisamehe, na kwa mnasaba kesho nina kikao nae.
- Umemfukuza nyumbani na umemuomba msamaha akakusamehe! Kweli ni mtu

www.path-2-happiness.com

mzuri, sikutegemea Tom anaweza kubadilika haraka kiasi hivi!
- Unakusudia nini?
- Tom kama ulivyonitajia amekuwa anabadilika kuwa mwema, kwa kawaida mtu hahami kutoka katika tabia mbaya kwenda katika maadili mema kwa haraka.
- Je hukukutana na Tom tena baada ya kufahamiana nae hospitalini?
- Ndio, mara nyingi tu tunakutana.
- Mara kwa mara?!
- Ndio, kwa hakika nimefurahishwa nae, na yeye pia inaelekea amenifurahia pia?
- Ni ipi tathmini yako kwake?
- Ni mtu mwenye akili, mwerevu na yupo katika kipindi cha mabadiliko makubwa.
- Anabadilika kutoka hali gani kwenda ipi?
- Mabadiliko kutoka hali aliyokuwa nayo na kwenda kuzuri zaidi.
- Ni ipi hiyo hali nzuri zaidi?
- Inawezekana ni njia ya furaha ambayo nawe unaitafuta.
- Aipate yeye… nisiipate mimi?
- Je nawe hauko katika mabadiliko hayo vile vile kama yeye? Kama kwamba una muonea wivu hutaki aipate hali hiyo!
- Sawa, la muhimu zaidi, itakuwaje utakapo kutana nae kikaoni?
- Kama kawaida
- Kama kawaida?
- Wewe unajua zaidi kuliko mimi.
- Kawaida huwa ananiuliza niliyoyasoma kwanza na mijadala niliyofanya, kisha tunaanza hatua nyingine mpya.
- Hili ndio lenye kutarajiwa.
- Je unategemea nijadiliane nae juu ya Ukristo ulio haribiwa? Au niusome Uislamu usio na maendeleo?
- Naam, ndio, nategemea yote hayo.
- Na ili nikamilishe yote hayo kwa uadilifu kama nilivyo fanya katika dini zilizopo duniani pamoja na Uyahudi na Ukristo lazima nisafiri katika milima ya Tora bora, je bado lipo hilo kwenye akili yako ewe Adam?
- Haa haa, ndio… nadhani bado ninafikra hiyo, kama unafikra hiyo kama ulivyosema ni kuwa muktadha wa uadilifu ni usafiri huko kama ulivyosafiri kutafuta dini nyinginezo….haahaa ha, lakini sio lazima kwenda Tora bora!
- Mimi sio Muislamu ili niweze kusafiri kwenda Makkah, labda nijifanye Muislamu,

ndio niende huko.
- Je unafikiri utafikia njia ya furaha kwa uongo?!.
- Nini nitafanya ikiwa Uislamu ni mgumu? Nimesafiri mpaka Roma ijapokuwa mimi sio Mkatoliki, bali unaweza kuingia hata Vatican hata kama wewe sio mwanadini (kafiri).
- Najua unachokusudia, je inawezekana kwa mtu kutoka Makah na kuingia Uingereza bila kukamilisha masharti ya kuingia?
- Nimefahamu unacho kusudia lakini masuala hapa ni tofauti.
- Hakuna tofauti hapo, kama hujakamilisha sharti huruhusiwi kusafiri popote duniani, na je inawezekanaje kwa fukara kuingia na kula katika mgahawa wa kifahari kama tulivyokula sisi na huku hana hela?
- Sahihi…ila huenda nikawa sina masharti ya kuwa Muislamu.
- Huenda lakini nani anajua.
- Wewe leo hii umekuwa mtu wa ajabu kabisa, tumekaribia mgahawani, lakini tuna ahadi ya kukutana hivi karibuni.
- Haa haa, kwa furaha tele nasubiri simu yako…au tutaonana huko Tora bora.

(3)

Joji alifika kwa Tom katika muda uliopangwa na kukuta mlango wa kliniki ukiwa umefungwa aligonga na Tom alimfungulia kwa kumkaribisha.
- Karibu…samahani kliniki imefungwa mpaka zogo la Baraad litakapotulia, kwani bado ana waathiri watu wote kazini na utaratibu mzima wa kazi.
- Sasa utafanya nini?
- Sijajua ila litaisha kwa hali yoyote.
- Kwa nini hufanyi mazungumzo ya kupatana nae?
- Nipatane nae! Juu ya nini?
- Sijui, muhimu ni kujikinga na shari na maudhi yake.
- Shari na maudhi yake ni bora kuliko yale anayonitaka, japokuwa maudhi yake yamezidi, lakini ni mwenye furaha kuliko hapo nilipokuwa pamoja na huduma zake nyingi!
- Maisha yamejaa mifarakano mingi na mambo ya ajabu. Mtawa anafanya machafu, na Mtume anavua nguo, na Mungu anaua, pamoja na hivyo hatupaswi kupinga au kukosoa.
- Acha tuingie katika maudhui yetu, vipi umelionaje kanisa Katoliki kwa ukweli

www.path-2-happiness.com

wake?
- Kwa kweli nimeliona katika hali ambayo akili haisadikishi.
- Huenda ikawa hivi kwa vile wewe ni Mprotestanti ndio maana!
- Kanisa la Kiprotestanti lina fanana sana na Katoliki! Naamini tatizo sio hili na lile….
- Tatizo lipo wapi?
- Kwa kweli tatizo lipo katika upagani.
- Upagani?!
- Nimechoshwa sana katika kulifikiria hili, lakini huu ndio ukweli, upagani wa kipapa, upagani wa utatu, upagani wa masanamu, upagani…
- Huenda ikawa tatizo lipo kwenye kanisa?!
- Hapana, kiini cha tatizo lipo kwenye kitabu kitakatifu chenyewe, sawa katika Agano la Kale au Jipya (torati na biblia). Nakuondoa utata huu, Kanisa Katoliki limeona kuwa kitabu kitakatifu kisisomwe ila na makasisi tu. Na wao ndio watawawekea wazi watu, ama kanisa la Kiprotestant linawahimiza wafuasi wake kusoma na kufasiri kama watakavyo.
- Uchambuzi wa kina kabisa, lakini nini kimesababisha hayo yote kwa mtazamo wako?
- Sababu ni kwamba mwandishi wa kitabu kitukufu amekibadilisha yaliyomo ndani, kisha makasisi wakakifanyia mageuzi, kisha kikabadilishwa na kubadilishwa, na hakihesabiwi kitabu hiki chenye migongano ambacho kiko kinyume na uhalisia wenyewe wa kiakili ulivyo kuwa kimetoka kwa Mungu.
- Na kwa nini hakikuandikwa kipindi cha Masiya?
- Kwa sababu wakristo walikuwa wanateswa sana! Na kuandamwa kila sehemu; na kwa hiyo hakikuandikwa ila baada ya kufa kwake kwa muda mrefu, na tena walioandika ni watu wasiojulikana kihistoria tena kuna tofauti ndani yake, na kwa lugha nyingine ambayo sio lugha ya Yesu, kwa kifupi ni mtego, haiwezekani kutoka katu, na ndio maana kukaonekana kupingana kwake na nakala mbali mbali, bali hata katika nakala moja pia kuna mgongano wa akili, mantiki pamoja na uhalisia na elimu.
- Inatosha haya, inavyoelekea wewe unachuki na kitabu kitakatifu!
- Sina chuki nacho kamwe, ila niamini kuwa nimejaribu kukiheshimu na kukitii kwa kadri ya uwezo wangu!
- Hebu niweke wazi vipi umekiheshimu na kukitii?

- Nitakupa mifano miwili, kwanza: Hakika naamini kilichopo kwenye kitabu kitakatifu, kwani natezwa nguvu mpaka nisitumie akili yangu, na ikiwa nitaitupa akili yangu basi sitaelewa maana yake kwa asili yake.
- Ni falsafa nzuri ya vitendo…kwa akili nzuri.
- Mfano wa pili ni: laiti nikiamua kukielewa na kuheshimu na kuweka akili yangu kando, basi kitabu chenyewe kinaniambia: “sio chako”!
- Vipi sio chako?! Weka wazi.
- Je katika kitabu kitakatifu hakuna kauli ya Yesu isemayo: “Sikupelekwa ila kwa kizazi cha wana wa Israel waliopotea.” Na mimi sio katika wao, kwa hivyo hakutumwa kwangu kabisa.
- Kwa hivyo wewe sio mkristo?!
- Huenda, niamini, sijui …naogopa nisije kuwa mpingaji Mungu kwa sababu yako!
- Hii ilikuwa ni mbinu yangu ili ukufuru, na nachelea kusema kuwa umefanikiwa, lakini nimebadilika kwa jinsi nilivyokuwa, na narudia kukuambia mimi kwa uchache naujua ukafiri kuliko wewe, hakuna ukafiri wa kweli; isipokuwa ni madai ya kutaka kukimbia mambo haya, unaweza kukimbia ukafiri, au pombe, au kuzini au kitu kingine chochote, ili uishi maisha ya shida na mabaya, huku ni kukimbia ukweli wa mambo kuliko uhalisia wa ndani.
- Ndio, inaelekea mbinu yako imefaulu, naogopa kukosa matarajio ya kufikia katika njia ya furaha.
- Huenda ni kwa ajili ya kutojua kwetu tumepetuka mpaka na kuacha kuchunguza na kujua mambo vizuri, kwa vyovyote vile tusichukue maamuzi kabla ya kufikia mwisho.
- Una maana gani kwa kauli yako: Kwa ujinga wetu tunaacha kitu tusichojua?! Msemo huu ni kama msemo wa Kikatoliki.
- Kuna ukweli kiasi fulani, lakini haiwezekani akili na mantiki kukubali fikra kuwa tumekosea, au tunaelekea kukosea?
- Ndio, akili inakubaliana na hilo, lakini kinyume chake hakikubaliwi, na kujiona siku zote kuwa upo sahihi huko ni kwenda kinyume na akili.
- Haa, haa, vizuri. Kwa hiyo Ukatoliki una nasibiana na akili…cha muhimu tumekubaliana tusichukue maamuzi mpaka mwisho.
- Naomba isijekuwa huu ni utangulizi kama ilivyokuwa ni ada; ili uniambie tusome Uislamu kwanza.
- Kamwe nitakuambia hilo, bali mimi kwa hakika nimeanza kuusoma Uislamu, na

www.path-2-happiness.com

najipinda kuusoma kwa dhati, je sijakueleza kwamba nimeanza kutafiti njia ya furaha pamoja na wewe?

Joji aliupiga mkono wake kwa mkono mwingine:

- Inavyoonekana tumeanzia na njia isiyokuwa na mwisho wake.
- Nimeanza jana kuisoma Qur'ani, kitabu kitakatifu cha Waislamu.
- Haa haa, hata mimi amenihimiza Adam kuisoma, ila sijamjibu, lakini nahisi nitapoteza muda wangu tu.
- Adam ndio alionipa nakala zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza kwa matarajio ya kwamba huenda baada ya kusoma nitaingia katika Uislamu.
- Anakutaka uingie katika Uislamu! Nini faida yake kwa hilo?
- Kila watu wanawalingania watu kuingia katika dini zao na kufuata fikra zao.
- Sijakuelewa! Unakusudia nini?
- Kitu gani hujakielewa, Adam anataka niingie katika dini yake, sasa kitu gani hapa hakipo wazi?
- Adam ni Muislamu?
- Ndio, bila shaka anaonekana wazi katika sura yake yeye ni Mwarabu, hukuwa unalijua hilo?
- Ndio, sikuwa najua, na jina lake sio la Kiarabu, fikra yangu ilikuwa kwamba yeye ni Mkatoliki mwenye asili ya India, nina shaka asije kuwa Adam ananichezea.
- Ama kwa upande wa jina lake ni jina la baba wa watu wote, lipo kwetu sisi na kwa Waarabu, ama kuhusu kukutania nadhani sidhani kama ni kweli, ila kama atakuwa amekuongopea, je umejaribu kumuuliza?
- Nimemuuliza zaidi ya mara moja lakini hakunijibu, la msingi je alikuwa akinielekeza ili nifike katika Uislamu? Sipendi kufanywa mpumbavu?
- Je mtu akiwa anakuita kwenye dini yake ndiko kuwa mpumbavu?!
- Hapana, lakini naogopa tu.
- Hakuna kitu cha sisi kuhofia, ila kama unaogopa kuingia katika Uislamu!
- Ndio naogopa kuingizwa katika kitu nisichokuwa na elimu nacho au kutumia akili.
- Je wewe ni dhaifu kiasi cha Adam kukukokota, wakati makasisi na wengineo hawakuweza kukukokota na kukukinaisha?! Au ya kuwa Adam ana nguvu kiasi kikubwa akakufanya wewe kumuogopa?

Joji aliashiria kwa mkono wake:

- Sio hili wala lile, kwanini unaniambia hivyo?!

- Kwa sababu wewe ulikuwa ni simba kwa kila dini na sasa umegeuka na kuwa sungura kwa kuuhofia Uislamu.
- Sio kama naogopa, nitausoma Uislamu…na kwa mnasaba wa maongezi yako kuwa nimebadilika, Adam ameanza kuandika kuhusiana na mabadiliko yako.
- Mabadiliko yangu?! Mimi bado sijamalizana na Baraad, anaripoti nini tena huyu?
- Ameingiza ukurasa wake katika facebook, na soma yale yaliyoandikwa.
- Nitarejea kwake, lakini tuachane na hili, la muhimu utasoma Uislamu kwa akili huru iliyotulia kama ulivyo soma dini nyingine kabla yako?
- Sawa, tumekubaliana.
- Na utakosoa kama ulivyofanya kwa dini zingine kabla yake?
- Ndio, tena zaidi ya hapo.
- Hapana, huku sio kuwa huru ambapo tunakuzungumzia, kauli yako ina ukosoaji mkubwa, kujifunga na kukosoa kupita mpaka, usome bila upendeleo kama ulivyosoma dini za duniani au kama Uyahudi na Ukristo.
- Haa haa je unanitaka nisilimu wala nisiukosoe?!
- Bali nataka uusome kwa kufunguka, kwa kuchunga elimu, kisha baada ya hapo uukosoe kama ulivyoukosoa Uyahudi, Ukristo na Ubudha.
- Lakini hata hizo nilisoma na kuzikosoa kwa kadri nilivyoelewa kwa akili yangu na kubaini upotoshaji wake kwa uchache.
- Kama ni hivyo tafuta upotofu wa Uislamu vile vile, lakini nitapendelea tusome zaidi, na baada ya hapo tuchukue maamuzi, kwani tutagundua ambayo yalikuwa hayapo katika ufahamu wetu.
- Na baada ya kugundua yasiyofaa na tofauti zake tutakuwaje? Je tutarudi katika ukafiri?
- Sijui?! Ila ninachokijua huenda kikatokea kitu ambacho hatukitarajii kama nilivyokuambia hapo kabla.
- Kwa kuwa umeshaanza kuisoma Qur'an, vipi umeionaje?
- Nilianza jana na sijasoma sana ila kidogo tu, lakini ni nzuri.
- Haahaa, inaelekea nimeanza kuwa na wasiwasi ninahofu huenda na wewe ukawa ni Muislamu pia.
- Hapana…kuwa na tumaini, mimi sio Muislamu.
- Kwa hiyo wewe ni nani?
- Mimi ni kama wewe tu, sijui, nahisi nimebadilika haraka.
- Maneno yako ni kama ya Adam juu yako, kwamba unabadilika.

www.path-2-happiness.com

- Huenda maneno yake ni kweli, nitasoma alichoandika kuhusu mimi leo, lakini jina lake kwa ukamilifu ni lipi ili nilione kwenye facebook?
- Kuna barua pepe yake utaiona katika ujumbe wangu, utaweza kuupata ukurasa wake.
- Vizuri, la muhimu tuusome Uislamu kwa moyo safi ulio huru.
- Haahaa, tutasafiri kwenda Afghanistan au Tora bora ili tupanue mawazo vizuri.
- Sijajua kwa nini unasema hivyo kama kwamba kwa hakika utakuwa Muislamu?
- Hiyo ni dharau tu.
- Kwa mnasaba je, hujazozana na Katarina kwa sababu ya fikra yako juu ya Ukatoliki?
- Ndio, inaelekea amejisalimisha nami kabisa.
- Kwa nini ameenda kanisani? Nilikuwa nahisi ukweli wa imani yake na mapenzi yake kwa Yesu.
- Ndio, ni kama hisia zangu, lakini cha mshtuko uliomtokea katika Ukatoliki na itikadi zake ni mkubwa, fikiria alibabaika sana tulipokutana na Muislamu Roma!! Na alichanganyikiwa alipojua kuwa yule kasisi aliyemfundisha imani na yakini hakuweza kunikinaisha juu ya shaka nilizonazo!
- Nimefurahishwa sana na dini na imani yake!
- Kama ni hivyo na wewe elekea kwenye Ukatoliki.
- Pia ni kiasi gani nakerwa na mgongano na kuwa kinyume na elimu!
- Haa haa, kama ni hivyo, kuwa Muislamu basi? Na uende katika milima ya Tora bora.
- Ninaamini ikiwa nitaridhishwa na Uislamu, na ikawa ni budi kwenda kusafiri Tora bora nitaenda.
- Napenda hamasa na kuazimia huku, ila nasikitika sioni pa kutokea mwisho wa safari.
- Na hata mimi, ila nina uhakika itadhihirika hata kama ni ghafla tu, ila usiniulize vipi, lakini mwenye imani sana na hilo.
- Nami nina imani na hisia kama zako.
- Hukututumia japo kwa ufupi majibu yetu juu ya ujumbe wako kama unavyofanya siku zote!
- Umesema kweli, jana sijaona ujumbe kwa sababu ya picha zako, nitatuma leo, na leo nitakuwa makini na majibu ya Adam kwani ni majibu ya Muislamu.
- Alikuwa wazi sana katika majibu yake yaliyotangulia.

- Huenda, mimi sijachunguza, na kiujumla ameandika hivyo kuhusu mimi kwa sababu sifungamani na maudhui, matukio, mijadala pamoja na mafunzo.
- Mafungamano ni muhimu sana.
- Ni kama maneno ya Adam, inaelekea unapendezwa sana na yeye.
- Sikujua kama hii ni rai yake, kwa kweli sikuvutiwa na raia yake zaidi kuliko kuvutiwa zaidi na mlingano wake wa ndani.
- Naungana na wewe kwa huo mlingano wa ndani, na mimi nimevutiwa na fikra zake pia, kwa mnasaba je umeshaondoa kifaa cha kunasa sauti alichokiweka Baraad?
- Ndio, mara ngapi natamani kuachana na Baraad na maudhui yake, ana niunganisha na ulimwengu wa zamani wenye huzuni!
- Utaachana nae karibuni tu, je utaniruhusu niondoke?
- Ndio, naona tumeshamaliza kikao cha leo, kwa mtazamo wangu naona kilikuwa ni kikao muhimu sana.
- Kwa hivyo basi tutaanza na Uislamu, nitarejea kazini na kumkabili Kakhi, ni kiasi gani nawachukia!
- Akina nani unawachukia?
- Uislamu pamoja na Kakhi.
- Umerudi tena kuukosoa kwa mara nyingine.
- Oh, nimesahau, sikutanabahi, haa haa, ukweli ni kuwa Kakhi na Uislam ni kitu gani kinachotusubiri unavyoona!

(4)

Joji alifungua barua pepe yake jioni alipowasili nyumbani… na kukuta marafiki zake wakiwa wamemjibu swali alilowauliza kuhusiana na ulinganifu kati ya dini tatu:

Levi: Sijaisoma Qur'an lakini nadhani dini zote tatu zina fanana sana.

Habib: Zinafanana kwa sababu zote zinatoka kwa Mungu, ila Qur'an ni tofauti katika uthabiti wa kuandikwa kutoka kizazi kwenda kingine, ila sijaisoma kwa umakini na mazingatio yake.

Adam: Zote zinatoka kwa Mungu, kwa masikitiko torati na biblia zimebadilishwa.

Tom: Sijaisoma Qur'an ili niilinganishe na torati na injili.

Katarina: Agano la Kale na Jipya zote ni kutoka kwa Mungu, sidhani Qur'an kama inatoka huko, ijapokuwa sijaisoma huenda nitafanya hivyo.

www.path-2-happiness.com

John Luke: Jana nimeanza kuisoma Qur'an kwa mara ya kwanza, na naona inatofautiana na torati na Biblia, ijapokuwa sijui utofauti huo!

Joji alikuwa makini na jibu la Adam, na kuangalia njia ambayo anaitumia pamoja nae… kwani marafiki zake wote walisema wazi kwamba wao hawakuisoma Qur'an, au wamesoma juu juu bila mazingatio, Adam peke yake ndio hajaashiria katika hilo. Joji alirudia tena kuwatumia marafiki wake wote na kuwaandikia sehemu ya sita:

"Sehemu ya sita: Nani miongoni mwenu anaweza kuisoma Qur'an, na achunguze katika kadhia hizi nazo ni: Kuthibiti kwake au kutothibiti kubadilishwa au kutobadilishwa, nasubiri ukosowaji wenu kwa muda wa wiki kuanzia leo.

Joji."

Baada tu ya kutuma barua pepe, aliwasiliana na Adam.

- Ijapokuwa tulikutana ila nimepatwa na hamu na kupenda tuonane kwa mara nyingine tena, je kwa kesho inafaa?
- Hapana shaka, labda tufanye baada ya saa mbili, kwa muda wangu wa kazi kesho unaishia saa mbili, haa haa, na tutakula chakula cha usiku pamoja.
- Muda muwafaka, kwani mimi nitarudi kesho kazini, karibu wiki tatu hivi sijauona uso wa Kakhi.
- Kwa hivyo nitakusubiri, kwa heri.
- Katarina alirejea nyumbani na kumkuta Joji akiwa mbali kwenye skirini ya kompyuta, alimbusu na kumuegemea mabegani….
- Mpenzi samahani kwa kuchelewa, kwani nilipitia super market; kuchukua baadhi ya mahitaji muhimu, nyumba ilikuwa tupu tangu turejee kutoka safari…uzuri ulioje wa safari.
- Ndio, ni nzuri sana, na kilichopendezesha zaidi ni kuwepo kwako wewe Katarina.
- Asante sana kwa maneno yako haya murua, safari iliisha haraka sana.
- Vitu vizuri vinaisha haraka zaidi, na kubakiwa na mawazo yenye huzuni kwa muda mrefu, na hata kitabu kizuri kinasomeka kwa mara moja tu, mara nyingi, na kile chenye kuchosha utakaa nacho siku nyingi bali wiki kadhaa…na ndio maana nimekimaliza haraka mara moja tu kile kitabu ulichopewa na Khalid.
- Unakusudia kitabu cha "Mapenzi makubwa kwa Yesu yamenifanya kuingia katika Uislamu?!" Je hakikuwa ni kizuri sana chenye kusisimua.
- Kwa hiyo unafikiri kuisoma Qur'an, kama ulivyosema katika barua pepe yako uliotuma?

- Kwa hakika, nimenunua nakala ya Qur'ani jana, kwa ajili ya kuisoma.
- Haa haa, oh –oh, hayo ni mabadiliko hatari sana ewe Katarina, Katarina anasoma Qur'an? Je utakuwa Muislamu?
- Nitaisoma; ili nipate kuikosoa na kubainisha kasoro zake na migongano iliyopo ndani yake.
- Nilikutumieni barua pepe muda si mrefu kuwaomba sote tuisome Qur'an, makubaliano yaliyoje haya, ama kwa upande wangu nitachukua nakala kwa Adam kesho.
- Kwa nini iwe kwa Adam pekee?
- Kwa sababu ndicho kitabu chao kitukufu.
- Kwani Adam ni Muislamu? Je hukuniambia kuwa yeye ni Mkatoliki?
- Kwa hakika lilikuwa ni jambo la mshtuko kwangu nilipojua kuwa yeye ni Muislamu, na nitakutana nae kesho kwa kadhia hii hasa.
- Japokuwa ninafurahishwa na Adam ila sifurahishwi na Waislamu, huenda nilimpenda kwa kuwa nilifikiri ni Mkatoliki.
- Hayo uyasemayo hayana uadilifu wala mantiki, je haitoshi kumuangalia bila kujali imani yake?
- Hapana, kipimo muhimu cha kumuangalia mtu ni dini, je, unataka nimfananishe muamini wa Kikatoliki awe sawa na Muislamu gaidi?! Je, kuwa mara nyingi tunampa thamani msomi kuliko mwingine, na mwenye tabia nzuri kuliko mwenye tabia mbaya? Tabia nzuri, usomi wa mtu na dini ndio njia ya kutathmini bila ya shaka.
- Inawezekana, lakini inafaa hilo lau kama unaitakidi kuwa dini yako haina shaka katika usahihi wake, kama ilivyokuwa hakuna shaka katika tabia njema, usomi, je unaamini hivyo?
- Kwa kiasi fulani, lakini je kwa upande wako dini daraja lake ni la chini zaidi kuliko tabia njema na usomi?! Haa haa inavyoonekana una chembe chembe za ukanaji dini ewe Joji.
- Huenda ikawa ni hivyo, lakini ni kwa nini ulikuwa unaogopea Sali na Maiko pale kanisani? Je ulikuwa na chembe ya ukanaji dini pia?
- Sikuwa naogopa chochote, wewe unadhania na kuisadiki nafsi yako, kisha kwanini niogope?
- Nilikuwa nakutania tu, basi wewe hukuwaogopea kanisani, na hukuwa na hofu yoyote na kitabu ulichopewa na Muislamu, cha msingi kitabu kiko wapi kwani

www.path-2-happiness.com

sijakisoma.
- Nafahamu sana unachoashiria, watu wote huwa wanaathirika kwa wanachosikia na kusoma na kufikiria.
- Nitakuuliza swali halafu nataka unijibu wazi wazi bila kuficha.
- Karibu, uliza swali lako.
- Je unaweza kuuacha Ukatoliki?
- Niache Ukatoliki? Kwa kitu gani?
- Halafu uwe Prostestanti au Myahudi au Muislamu au uchague dini yoyote?
- Laiti ungeniuliza swali hilo kabla ya mwezi hivi, basi ningekujibu bila kificho kuwa hapana. Ama kwa sasa hivi utanisamehe; ila nitakujibu pia hapana, lakini sijui kwa nini imani yangu imeshuka kuliko mwanzo, japokuwa unajaribu kunitikisa na maswali yako ila unanifanya niwe imara zaidi na nafsi yangu.
- Wewe Katarina ni mfano mzuri wa imani kwangu, na kile unacho nikumbusha kuhusu kubadilika huenda ni dalili tosha ya kuongezeka kwa imani yako, japokuwa mimi ni Mprotestanti na sio Mkatoliki ila nasadiki imani yako, na wewe ndio taa inayoniongozea njia.
- Bali wewe ni mtafiti mzuri wa kutaka kujua ukweli na utafanikiwa, na kupenda Joji.

(5)

Asubuhi ilipofika Joji alienda kazini na kuelekea ofisini kwake moja kwa moja hakutaka kukutana na Kakhi, alikuwa anahisi kumchukia kwa upande wake. Je hilo linarejea kwa sababu yeye ni Myahudi, au kwa sababu ni mtu mwenye tamaa, au kwa sababu ya tabia yake mbaya au kwa sababu tabia zote hizo anazo? Hiyo sio sababu kwa kuwa amefurahishwa sana na Levi japo yeye ni Myahudi, na ni mtu aliyeshikamana na dini yake…hakuwa akimchukia mtu kwa dini yake bali alikuwa anachukizwa na migongano iliyopo kwenye dini na ushirikina na upotofu wake.

Pamoja na hivyo ni lazima kukutana na Kakhi kwa hali yoyote ile, na kwa hivyo lazima awasiliane nae kabla Kakhi hajajua kuja kwake na kuwasiliana nae….wakati akiwa katika hali hiyo mara akaona karatasi iliyokuwa na bonasi nyingi kwa juhudi kubwa aliyofanya kwa ajili ya shirika lake. Hiyo inatokana na mafanikio makubwa aliyoyapata katika kuingia mikataba huko India na Tel Aviv ikiwa imetiwa sahihi na Kakhi. Joji alijiuliza: Je alimchukia Kakhi kiasi hiki, au ajirudi kwa hisia mbaya alizokuwa nazo pindi alipofahamu kuwepo

kwa bonasi kubwa kiasi hiki? Je posho ile inathibitisha wema aliokuwa nao, au ni rushwa kama rushwa aliyompa Benjamin huko Yerusalem?!

Simu iliita, Joji alipokea simu, ghafla Kakhi alikuwa upande wa pili.
- Karibu Joji, nilipojua kuwa unakuja nilikusubiri ofisini kwangu lakini hukuja, je utakuja au mimi nije ofisini kwako?
- Nitakuja baada ya dakika hivi, nilikuwa napanga karatasi tu.
- Kama ni hivyo nitakusubiri.

Joji alikusanya baadhi ya makaratasi na kuyapanga, lakini hakuweza kupangilia mawazo yake na akili yake vizuri kutokana na ushawishi na bashasha ya Kakhi kwake, alielekea ofisini kwake, na alipoingia tu alimkaribisha kwa furaha….
- Karibu, kwa hakika nilikuwa na hamu sana na wewe Joji, vipi afya yako? Habari za Roma pamoja na TelAviv?
- Mimi ni mzima, kwa hakika nimepona maradhi yaliyonipata, ama kuhusiana na TelAviv nimewekeana mikataba kwa ukamilifu na nimeshaituma kwenu, ama kuhusu Roma safari ilikuwa ni nzuri, vipi hali zenu? Na vipi habari za shirika?
- Mikataba ya TelAviv italisukuma sana shirika letu kwa sababu makundi shawishi ya Kiyahudi yapo katika nchi nyingi, na kwa sababu sisi tumetiliana saini na TelAviv hii itasaidia kupanua wigo zaidi Ulaya yote na hata Amerika, na idara kuu imekuzawadia bonasi nzuri, je umeiona?
- Asante sana Kakhi kwa hisia hizi, nilichokifanya ni wajibu wangu wa kikazi.
- Sijui vipi uliweza kuvuka vigingi, wewe ni dereva mgunduzi!
- Hakukuwa na vikwazo vyovyote, ametia saini mara moja.
- Je hakutaka fedha zingine kwa ajili yake mwenyewe?
- Unakusudia rushwa, hilo alichukua.
- Je hajataka kitu kingine?
- Kama kitu gani?
- Achana na hilo, ni mara ngapi umelala na Levi? Najua yeye anapenda starehe wakati mwingine, hali yakuwa ni mwenye dini.
- Sijalala nae katu, na siwezi kufanya hivyo.
- Benjamin ni mchafu, je hajakutongozea.
- Kweli ni mchafu, kwani amechukua rushwa, na mimi sikumuomba aongee na Levi, sasa vipi unanitaka mimi kukubali amchukie Benjamin kwa mambo hayo ya ngono?
- Haa haa, cha muhimu ni kuwa ametia saini mkataba, kiasi gani nikitaka ustarehe, lakini wewe ndie hutaki, ningekuwa sehemu yako muda wote ningelala nae,

www.part-2-happiness.com

kwani hajakupendeza?
- Mimi nimeoa ewe Kakhi, je unataka nimfanyie hiyana mke wangu? Siwezi kujivua na misimamo yangu.
- Achana na misimamo kwanza, sisi tunalitumia tu neno hilo hasa tunapotaka kufanikisha malengo yetu.
- Labda unaongelea kitu kingine kisichokuwa msimamo. Ama misimamo haiwezekani kuivuka.
- Je wajua kama Levi analala na mimi kila siku ninaposafiri kwenda TelAviv? Na yeye ndio mzungumzaji mkubwa wa misimamo.
- Huo ni udhaifu wa kibinadamu tu.
- Na hii ndio falsafa ya misimamo, tukitaka kufanikisha mambo yetu tunasingizia misingi hii ya misimamo na tukitaka mambo mengine tunasema ni udhaifu wa kibinadamu.

Maneno ya Kakhi yalimuathiri kiasi fulani katika moyo wa Joji, kweli na yeye pia alitoa rushwa kwa Benjamini na kusingizia udhaifu. Je na yeye anafuata nadharia ya Kakhi juu ya misimamo na misingi bora?
- Huenda, lakini katika mambo mabaya kabisa ni kuishi bila kuwa na maadili, na hivyo ni kwa mujibu wa maslahi yako, kinyume chake hatakuwa tofauti na wanyama.
- Ha haa, udhuru wa wanyama ni bora kuliko wa binadamu, kwa sababu ameumbwa hivyo na habadiliki na ukitaka yaite hayo kuwa ndio maadili yao.
- Umesema kweli, watu kama hawana maadili ni waovu kuliko wanyama, na wanageuka kuwa wabaya zaidi, hawaoni la muhimu zaidi ya mali, ngono na utawala.
- Ni mhadhara mzuri ewe mwenye maadili, achana na hayo kwa sasa, rudi katika kazi, je upo tayari kwa safari mpya ya kuweka mikataba huko Sweden?
- Safari mpya kwenda Sweden?
- Ndio …baada ya wiki hivi, na Idara imekubaliana wewe uende, na waliakhirisha safari hiyo zaidi ya mara moja hadi utakaporejea.
- Mkataba wa nini?
- Ni kama mkataba wa TelAviv, bali unashabihiana sana na huo.
- Vipi? sijaelewa!
- Kuna fedha kwa ajili ya mkurugenzi wa Idara ya utaalamu, pamoja na ushirikiano wa kidiplomasia kutoka kwako na baada ya hapo kutia saini mkataba.
- Nimekufahamu unachokusudia, mkurugenzi wa utaalamu hapa ndio Benjamin wa huko. Je kuna Levi mwingine huko Sweden?

- Ha ha ha, si umeniambia kuwa hujastarehe na Levi, sasa kwa nini tena unamuulizia Levi Sweden? Yako wapi maadili.
- Sijakusudia hivyo, bali nilikuwa natafuta vipengele vyenye kufanana.
- Ndio, yupo mfano wa Levi huko Sweden na jina lake ni Ingrid, ni sawa na uzuri wa Levi, kuwa na amani tu.
- Vizuri, ili usifikirie kuwa nakataa kwa ajili ya uzuri wake.
- Sifahamu?
- Sitokwenda, ili usifahamu kuwa tatizo lipo kwa sababu hakuna masiku mekundu.
- Na kwa nini huendi?
- Je hukuniambia kuwa mimi ni mwenye maadili? Rushwa inapingana na maadili yangu.
- Kwani hukumpa pesa Benjamin ili atie saini mkataba ewe mwenye misimamo na maadili?
- Ni kweli nimekosea, na ukitaka unaweza kuuita ni udhaifu wa Kibinadamu!
- Je sijakwambia kwamba tunatumia maadili ili kufanikisha malengo na maslahi yetu, unataka nini?
- Sitaki chochote, sitaki tu kwenda.
- Unaonaje nikikwambia kuwa bonasi yako ijayo ni mara mbili zaidi ya iliyopita, kwa maana ni sawa karibu ya mishahara yako ya miezi mitatu.
- Sio hoja..
- Sitaki unijibu sasa hivi, una siku mbili za kufikiri, naamini hutaiachia fursa hii.
- Ni fursa gani hiyo?
- Fursa ya safari, bonasi na kupanda cheo?!
- Kupanda cheo?!
- Ndio, katika muundo mpya wa shirika. Ikiwa utawezesha mkataba na Sweden utakuwa mkurugenzi mkuu wa shirika, utashika nafasi yangu na idara imependezwa na mafanikio yako.
- Na wewe?
- Huenda nikawa mkurugenzi mkuu wa shirika la makabidhiano wa shirika letu, fikiria vizuri, ila naamini hutaipoteza fursa hiyo, na unaweza kupanga muda wako muwafaka, haa haa na wakati huo utaamua kutumia maadili yako vizuri, unaweza kutoa au kutotoa rushwa tena.
- Na kama sijasafiri?
- Utakuwa umejihukumu mwenyewe kwenye shirika, na sidhani mwenye akili mfano wako anaweza kufanya hivyo, niamini nilitaka kwenda mimi mwenyewe ila idara imesisitiza uende wewe kwa ajili ya kusaini mikataba mikubwa, wao

www.path-2-happiness.com

wamefurahishwa sana nawe.
- Nitakujibu baada ya masiku kadha.
- Mimi ni mwenye imani na akili yako na busara zako, kwa hivyo nitawajulisha watu wa mahusiano wakuandalie safari yako kuanzia sasa hivi. Utaletewa makaratasi na mikataba, na maelezo kamili ya makubaliano.
- Naomba ruhusa, nataka kumalizia baadhi ya kazi.

Joji alikwenda ofisini kwake, huku akijiuliza..Je maadili kama alivyosema Kakhi ni suala la maslahi tu? Ambayo yanabadilika kwa mujibu wa malengo yetu? Au ni taa tosha za kutuangazia njia tuiiendayo, na inatupasa kufuata muongozo wake? Na kama ni hivyo, ni kwa nini alimpa rushwa Benjamin huko Tel Aviv? Je afanye nini? Inaelekea maudhui ya safari ndio muhimu sana kwa Kakhi, bali ni la kuamua kama ataendelea na kazi au kufukuzwa..ikiwa maadili ni kweli hayana thamani yoyote; hiyo ina maana kuwa sisi tutabadilika kuwa ni wanyama tunakulana wenyewe kwa wenyewe, Aakh, Aakh…kwanini Mungu hakupanga mambo haya? Au Mungu amewaacha watu wajipangie mambo yao bila kuingilia?!

Pindi alipokuwa amezama kwenye mawazo hayo, aliletewa makaratasi na fomu za safari, alianza kuziangalia bila kujali, ikiwa maamuzi yake ni: Je atasafiri au hapana na hilo ndio muhimu kwake, na kama hataki kusafiri kwa nini anajihangaisha kuyasoma makaratasi hayo?

Joji alisubiria mpaka mwisho wa siku ya kazi iliyoonekana kuwa ni ndefu sana kwake; ili aende nyumbani na amshauri Katarina katika uamuzi wa safari yake, alipofika nyumbani alimkuta Katarina anasoma kwa umakini na utulivu wa hali ya juu….

- Yaelekea kitabu unachosoma ni kizuri sana?
- Kiasi fulani, nasoma kitabu kitakatifu cha Waislamu ambacho ni Qur'an.
- Kwa maana hiyo umeanza kukisoma?
- Ndio, lakini pamoja na pupa na ufahamu wangu bado najikuta kukirudia kusoma tafsiri za sura zaidi ya mara moja.
- Kwa nini?
- Sijui, huenda kwa sababu ni tofauti na vile nilivyovizoea…!
- Vizuri, lakini je inawezekana kuacha maudhui haya na kitabu, nina jambo nataka ushauri wako.
- Haya tafadhali sema.
- Kakhi ameniomba nisafiri kwenda safari nyingine mpya.
- Hii ni mara yako ya kwanza tokea uanze kazi na shirika hili umefululiza kusafiri

kiasi hiki, safari hii ya kwenda wapi?
- Kwenda Sweden.
- Sweden ni nchi yenye hadaa.
- Hili silo tatizo.
- Kwa hivyo kadhia ni ipi?!
- Kipindi nimesafiri Israel kuweka saini ya mkataba na maafikiano, nilipewa rushwa kubwa nimpe mkuu wa shirika lingine ili kuweka saini, na wananitaka tena kufanya hivyo huko Sweden.
- Japokuwa nachukia rushwa na siipendi, lakini kuna kipya gani kwako? Wakati ulikwishawahi kutoa mara ya kwanza.
- Maneno kama ya Kakhi.
- Namchukia mkurugenzi wako huyu, lakini…..
- Chukulia nimekosea mara ya mwanzo, je nirudie tena kosa hilo mara nyingine? Kwani hakuna njia ya watu kujitakasa kwa makosa yao?
- Katika Ukristo tumemtoa Kristo kwa kujitoa kwake mhanga kwa ajili ya watu.
- Na hili sio mahususi kwa mtu bali kwa mkosaji na mwingine.
- Bado sijakuelewa?!
- Kwamba sote sisi hatuna dhambi na tumetakaswa, na kwa nini tuiache wakati tunajitakasa kwayo?! Nafikiri huu ni mwanzo mzuri wa biashara ya kuuza cheki ya kusamehewa madhambi.
- Nimekuelewa unachokusudia, haya ni katika Ukristo, ama katika Uislamu mwenye kutubu na kuomba msamaha Mungu atamsamehe.
- Maendeleo yalioje haya, umekuwa unauongelea Uislamu, yote haya ni baada ya kusoma kitabu kimoja tu?! Hivi Waislamu hawaendi kwa makasisi na watawa kutubia? Vipi kuhusu misa ya kufuta makosa?
- Hakuna misa yeyote, kutubu ni kumuelekea Mungu pekee, tunatakiwa tumuombe msamaha kwa makosa yetu, na kuazimia kwa dhati kutorudia kufanya dhambi.
- Kwa wepesi tu hivi!
- Ndio.
- Yote haya ni mafunzo yanatokana na kitabu ulichopewa na Muislamu huko Roma!
- Bali ni kutoka katika kitabu kitakatifu cha Waislamu kinachoitwa Qur'an.
- Turudi katika maudhui ya Kakhi.
- Sijui, vigumu kuwa na uchaguzi, ima ufungamane nao katika yale yanayokwenda kinyume na maadili yako na kupoteza thamani yako mbele ya nafsi yako, au kukataa; na hivyo basi kupoteza kazi yako.
- Ndio, uchaguzi ni mgumu, na nina fursa ya kumjibu kwa muda wa siku mbili,

www.path-2-happiness.com

lakini lau ungekuwa wewe katika hali yangu ungefanya nini?

- Mimi ningekuwa katika mtanziko kama wewe, na ningekuomba ushauri wako hasa kwangu mimi, lakini umenitangulia na sipendi kukuongezea uliyonayo.
- Vipi?
- Sikuridhika na kile ninachokifundisha shuleni, nafikiri kuacha kazi yangu.
- Unaacha kazi yako?
- Kama ulivyo wewe hupendi kwenda kinyume na maadili yako, na mimi pia sipendi kwenda kinyume na maadili yangu, mengi ninayosema katika darasa bado sijaridhishwa nayo, ima niyaseme na hapo tena nienda kinyume na maadili yangu ya kutosema isipokuwa yale ninayoyaamini, vinginevyo naacha kazi, na hapo utakatika mshahara ninaopokea kutoka kwao.
- Ni badiliko la hatari, je hukufikisha miaka kumi unafundisha hili tu? Ni kipi kipya basi? Ikiwa sote tutaacha kazi zetu tutaishi vipi katika kivuli cha ukosefu wa kazi unaozidi hapa Uingereza na hata ulimwengu mzima?
- Jipya ni kwamba ridhaa yangu ya Ukatoliki imetikisika, je hukuwa unataka hivi?! Kwa ujumla mimi sijachukua maamuzi mpaka muda huu.
- Samahani kama nimekukera bali nilikuwa nafanya mzaha tu na wewe.
- Kinyume chake, kwa hakika umeondosha matongotongo yaliyokuwa machoni mwangu, lakini sijakueleza kwamba sitaki kukujuliisha isije ikakuzidishia mawazo?
- Kweli, umeniongezea mawazo juu ya niliyokuwa nayo, nitafikiri zaidi na kuchukua maamuzi kwa muda wa siku mbili hizi zijazo, na wewe chukua maamuzi yako, ama kweli maisha ni maamuzi.
- Ni wajibu kuomba ushauri ewe Joji.
- Lakini nani anafahamu matatizo ya kazini?
- Mtu yeyote miongoni mwa marafiki zako, kwa nini hutumi barua pepe kama unavyotutumia ukitaka ushauri huo?
- Ni fikra nzuri, nitatuma sasa hivi.

Joji alipanda kwenda katika chumba cha ofisi yake, na kufungua kompyuta yake, na kuwaandikia marafiki zake akiwataka ushauri.

"Sehemu ya saba: Nimekabiliwa na tatizo naomba mnipe ushauri wenu kabla ya kujibu swali langu la sehemu ya sita. Kwa kifupi swali ni hili! "Je niungane na maadili yangu japokuwa yanaharibu maisha yangu? Au nifuate maslahi ijapo kuwa yanaharibu maisha yangu? nategemea jibu la kweli na uwazi, jiweke wewe katika nafasi yangu, je maadili na maslahi yanaweza kuwa pamoja bila kugongana?

Joji".

Baada ya kuituma, alifungua ukurasa wa Tom katika face book na kukuta majibu yale yale kama yaliyopita, na kuandika kutaka msamaha kwa picha za uongo na kupandikizwa zilizo sambazwa katika ukurasa… alijihisi vizuri kidogo; Inavyoelekea Tom ameweza kurejesha face book yake na kumaliza tatizo la Baraad. Halafu alifungua face book ya Adam na kukuta ameandika makala mpya yenye anuani, "Mafunzo kutoka kwa rafiki yangu anayetafuta furaha4"

"Rafiki yangu anapambana na kipindi kigumu zaidi, na unaweza kuangalia nukta hizi zifuatazo katika utafiti wake:

1Mwanaadamu kujua yale asiyo yataka ni rahisi kuliko kujua yale anayo yataka, na kujua njia hii sio ya furaha pia ni rahisi kuliko kujua kuwa njia hii ni ya furaha, mabadiliko na kuhama kutoka hali fulani kwenda nyingine ni kugumu kwa mtu.

2Maamuzi yoyote yanahitaji ujasiri mkubwa kutoka katika nafsi ya mtu, na ushupavu ndio anuani ya mafanikio ya kifikra, au kijeshi au maadili, na rafiki yangu ni shujaa bila shaka, lakini hitajio lake la ushupavu kwa sasa ni zaidi kuliko zamani, je ataweza kuwa hivyo?

3Rafiki yangu anaishi katika wakati ambao ni wa mabadiliko ambao hauoni sana, wala hayuko makini kwa hilo, yeyena hili ni jambo la ajabu kabisahadi sasa hajui kama mimi ni Muislamu, na atashitukizwa kuona kuwa watu wanaomzunguka waliokuwa karibu yake wanaishi katika kipindi cha mabadiliko makubwa mfano wake.

4Japokuwa rafiki yangu yupo katika kutaka kujifunza kwa pupa ila hajachukua maamuzi ya kujifunza Uislamu kwa njia nyepesi, na hilo huenda limesababishwa na vyombo vya habari! Vilivyoathiri sana mtazamo juu ya Uislamu, na huenda sehemu nyingine inatokana na upungufu na makosa ya Waislamu wenyewe.

Ila bado nina imani kuwa rafiki yangu yupo katika hatua za mwisho za kutafuta na kufuata njia ya furaha na katika kutafuta majibu ya maswali makubwa ya maisha, nitawajulisha hayo katika darasa zijazo."

Adam."

Joji alirudia kusoma tena kwa mara ya pili kile kilichoandikwa na Adam kwa umuhimu mkubwa, na kujiuliza mwenyewe nafsi yake: Hivi Adam anaamini kwamba Uislamu ndio njia pekee ya kufikia maisha bora ya furaha?! Kwa nini hajaniambia hivyo tangu mwanzo? Je ananitania mimi? Au Uislamu unaruhusu udanganyifu? Na kama anaamini Uislamu ndio njia bora ya maisha na ya furaha kwanini anajificha na kutokuwa muwazi? Je Uislamu una kasoro mpaka auepuke? Au ndio siri miongoni mwa siri za dini kama siri za kanisa?

www.path-2-happiness.com

Pindi alipokuwa katika tafakuri hiyo mara aliingia Katarina.

- Njoo usome aliyoandika Adam juu yangu? Nimeanza kumtilia shaka mtu huyu.
- Ameandika nini?
- Karibu usome.

Katarina alisoma makala kwa umakini akisha akamgeukia Joji.

- Sijakuelewa sehemu gani una shaka nayo!
- Yeye ni Muislamu mwenye kuamini kwamba Uislamu ndio njia bora ya furaha ambayo itatatua matatizo ya maisha yangu!
- Ndio, na hili ni jambo la kawaida, ni desturi mtu kuamini kile alicho nacho kuwa ndio njia ya furaha maishani.
- Lakini ni kwa nini hakunijulisha tokea mwanzo, na kwa nini ananidanganya?
- Je kakudanganya na kukwambia kitu ambacho si cha kweli?
- Hapana, lakini amenificha Imani yake na dini yake.
- Nahisi yeye amekueleza kweli tu hilo, ila wewe hukugundua.
- Ki vipi?
- Kwa hakika ameandika dini yake katika face book, na yeye hajifichi katu bali anajifaharisha kwayo, kwani ameandika mimi ni (Muislamu na najifaharisha).
- Fikiria yote haya sijayaona pamoja na kuwa nafungua sana face book yake, amesema kweli Adam ila mimi sifungamani vya kutosha.
- Je, hujatuambia sisi katika barua pepe kwamba sote tuisome Qur'an na tukupe jibu? Je wewe umeanza kuisoma?!
- Hapana, kwani Kakhi amenishughulisha sana na matatizo yake, nitaonana na Adam leo, na leo hii hii nitaanza kuisoma Qur'an, na nitajaribu kuwa na maamuzi leo ya shirika au kesho.
- Adam asiwe ndio mwamuzi wetu, msikilize kwa utulivu au tuache tujifunze zaidi mpaka tuweze kumjibu kwa hoja zenye nguvu….huenda yeye anatutaka tuingie katika Uislamu pamoja nae, sasa sisi tumfanye awe mkristo pamoja nasi.
- Nitajaribu kwenda kwake sasa hivi, na nitajaribu kumsikiliza kwa makini na kujifunza mpaka nimjibu vizuri kwa elimu, na ninadhani nitakula chakula cha usiku pamoja nae.

MABADILIKO

www.path-2-happiness.com

14 MABADILIKO

MABADILIKO

(1)

Joji alienda mgahawani kukutana na Adam lakini hajamkuta, alimuuliza mhudumu na kumjibu kwamba leo hajafika na yeye hajui chochote kuhusu Adam.

- Nilionana nae jana na leo ilikuwa ni ahadi yetu kuonana.
- Hatuna taarifa yoyote kutoka kwake na kutofika kwake ni jambo la kushangaza, kwa ujumla huenda akaja kesho

Joji alitoka pale mgahawani na kuelekea moja kwa moja nyumbani kwa Adam na aligonga mlango bila majibu yoyote, alijaribu kumpigia simu lakini ilifungwa, alirudi nyumbani akiwa na wasiwasi.

- Katarina, Adam haonekani sijamuona kazini wala nyumbani na simu yake imefungwa.
- Na hii sio mara ya kwanza, je hukumbuki kuwa hili lishamtokea hapo kabla?
- Ndio, nadhani alifungwa na wale ambao walituhumiwa kwa mlipuko wa ugaidi, ila mimi nilikuwa sijui kama yeye ni Muislamu.
- Sijatangamana sana na Adam ila namheshimu sana, nimemuona ni mwenye huruma tena ni mwenye kujali pindi ulipokuwa mgonjwa, na nikaona muamala wake mwingine na Kakhi asiye na haya, mwenye uwezo wa kufanya chochote.
- Na kile usichokijua kutokana na yeye, mimi namjua vizuri sana kuwa yeye ni mshauri mzuri wa watu na mwenye kunitakia kheri mimi, nimeliona hilo zaidi ya mara moja. Nikashangaa mbona kujali huku sana na mkweli kwangu kiasi hichi?
- Lipi geni katika hilo?
- Sikuona geni mpaka nilipojua kuwa yeye sio Mkristo.
- Sijakufahamu, kwa nini?
- Kwa sababu ni katika watu waliokuwa wakinihimiza kwenda Tel Aviv kuusoma Uyahudi, na ni yeye pia aliyenihimiza kusoma Ukristo na kwenda Roma, vipi afanye hivyo wakati yeye sio Mkristo?
- Huenda hii ni dalili ya mtu kujiamini.
- Au kuuamini mfumo na njia anayoifuata.
- Huenda ikawa hivyo, kwa ujumla Qur'an ni kitabu chenye kushangaza sana, je hukukisoma kiasi cha wiki hivi kama ulivyogusia katika barua yako?

www.path-2-happiness.com

- Kama nilivyokufahamisha hapo kabla nilitaka kukisoma, lakini suala la Kakhi lilinisumbua, kisha kupotea kwa Adam, je umeshamaliza kukisoma ili nichukuwe nikisome?
- Ndio, nimekimaliza, lakini naona kuna haja ya kurejea tena baadhi ya maudhui na mambo fulani fulani, je unataka nikununulie nakala kwa ajili yako?
- Ikiwa utakwenda duka la vitabu hivi karibuni ninunulie nakala, lakini je asili yake ni kwa lugha gani hasa?
- Qur'an ni kwa lugha ya Kiarabu tu.
- Sasa unakisoma vipi?
- Mimi huwa nasoma tarjumi yake tu.
- Sisi huwa tunasoma tarjumi la Agano la Kale na Jipya na tunasema kuwa tunasoma? Sasa kwa nini hapa utofautishe?
- Kwa hoja ya swali lako katika barua, nimerejea maudhui na kusoma na kuitafiti, nikaona kuwa uhamishaji na unakili wa Qur'an katika zama mbali mbali ulikuwa wa umakini na wa kina kabisa ambayo historia ya mwanadamu umefahamu, watu wengi wamenukuu kutoka kwa Mtume wao Muhammad na kutoka kwao wengi wamenukuu na kupokea hadi leo hii tuzungumzapo, wala muda wote hakujatokea upotofu, ama tarjama ndizo zenye kutokea makosa na upotofu ndani yake.
- Ki vipi?
- Makasisi wengi walifanya tarjumi ya maana ya Qur'an, walitarjumi kama walivyotaka, na ndio maana kuna makosa katika baadhi za tarjumi.
- Kama ni hivyo, Qur'an ni kwa Waarabu tu, na lugha zote kinyume na kiarabu itakuwa imebadilishwa na kutiwa makosa?
- Huenda, ila mimi sijasema hivyo! Andiko la Qur'an halisemi kuwa ni la Waarabu tu katika maudhui zake nyingi: "Kwa watu wote" kama ambavyo tarjumi zake nyingi ni nzuri, lakini kunapotokea hitilafu hurejewa katika andiko la asili la Kiarabu, na cha kuchekesha ni kuwa andiko la asili sio tu kuwa limenakiliwa na kuhifadhiwa, bali Waislamu wamenukuu hata ile njia yao ya kusoma kwa sauti.
- Ni kipi kipimo cha usahihi wa tarjumi?
- Mwenye kufanya tarjumi hufanya tarjumi ya maana ya Qur'an tu na sio Qur'an yenyewe, Qur'an ni kwa lugha ya Kiarabu tu, kwa ujumla ni kuwa unapoisoma unahisi hilo.
- Mimi nimechoka nataka kulala, na nina njaa nataka kula chakula cha usiku, na nina huzuni nataka kujua hali ya Adam, na mwenye hasira juu ya Kakhi, na

mwenye ashiki anamtaka mpenzi wake, na wewe umeshughulishwa na tarjumi za Qur'an!

Katarina alitabasamu na kusema kwa kubembeleza:

- Kwa hivyo tuanze na chakula, halafu mapenzi baadae, na mengine tutayaakhirisha.

Joji aliamka asubuhi na kujiandaa kwenda kazini, alitoka hali ya kuwa ni mzito na asiye na raha, hajui kama hisia zake ni kwa sababu ya Kakhi? Au ni kwa sababu ya babaiko lake ambalo bado hakulitatua jambo lake?

Aliingia ofisini kwake na kuwasiliana moja kwa moja na Adam, na kukuta simu yake imefungwa, alimtumia ujumbe akimtaka amtulize… dakika chache zilipita na Kakhi akampigia simu akimtaka afike ofisini kwake.

- Kama kwamba umeibeba dunia kichwani mwako, una nini?
- Hakuna kitu, nimechoka kidogo.
- Na huzuni uliyo nayo!
- Hapana kitu, kuna rafiki yangu mpenzi namtafuta sijampata na ninamhofia.
- Je umemtafuta sehemu yake ya kazi, nyumbani na kwa marafiki zake?
- Ndio, cha ajabu hata rafiki yake mhudumu wa mkahawa anashangazwa na kutotoa taarifa ya udhuru na sio kawaida yake.
- Haa haa, rafiki yako kipenzi! Ni yule mhudumu niliyemkuta hospitali akiwa nawe?
- Ndio.
- Nilitaka kumfukuza hospitali, vipi unafuatana na mhudumu?
- Bali Katarina alikaribia kukufukuza pale ulipomshambulia, Adam ni rafiki yangu mpendwa, na wala sipendi umseme hivyo.
- Wewe umependekezwa kuwa mkurugenzi mkuu wa kampuni, halafu unaniambia habari za rafiki mhudumu! Nina shaka juu yako ijapokuwa uwezo wako wa kazi ni mkubwa, lakini ufahamu wako kwa jamii ni mdogo sana, na kwa masikitiko ufahamu wa kijamii ni muhimu zaidi kuliko uwezo wako wa kazi ya kuajiriwa na haswa katika vyeo vya juu.
- Kwani uwezo wa akili wa kijamii ni kuishi na watu katika hali ya mifarakano na jeuri?
- Nina maana wewe una uwezo wa kutosha wa kuwa na watu wa maana ambao wanaweza kukuzidishia kipato na fursa ya kazi yako.
- Je urafiki kwa mtazamo wako ni fursa ya kazi na kuingiza pesa?
- Ndio, bali maisha yote yako hivyo, na wala sijui utaelewa lini hilo?

www.path-2-happiness.com

- Wala sitaki kulijua hilo.
- Rafiki yangu usiwe mkali, lini utasafiri?
- Urafiki wako haunisaidii, urafiki wa Adam ndio bora kwangu.
- Haa haa, ninachokijali ni kazi yako na sio urafiki wako, lini utasafiri kwenda Sweden?
- Nitakujibu kesho, niruhusu niondoke.
- Tumekuwekea tiketi, unaweza kuichukua kutoka kwa William ambaye ni mkurugenzi mkuu wa mahusiano. Haa haa tujulishe utakapomuona mhudumu.

Joji alirudi ofisini akiwa ni mwenye kujilaumu, kwa nini hakumueleza haraka Kakhi kwamba hawezi kusafiri na kuvunja misimamo yake? Je aliogopea kupoteza kazi yake? Kama ni hivyo hana tofauti na Kakhi ambaye anajali mali tu, lakini anajificha katika maadili, tofauti na Kakhi ambae amekuwa ni muwazi kwake, yeye mwenyewe, na hata kwa watu, huenda akawa ni mkweli pindi aliposema kuwa sisi tunadumu katika maadili pale yanapokuwa katika maslahi yetu, lakini pale yanapokuwa hayatuhudumii tunajivua nayo. Alijihimu arudi kwa Kakhi ili amwambie juu ya uamuzi wake na liwe liwalo, lakini alirudi nyuma na kuamua kumuandikia ujumbe wa kuomba udhuru, na wakati huo huo aliingia Wiliam ambae ni mkurugenzi mkuu wa mahusiano.

- Tafadhali, chukua hii tiketi imetoka kwa Kakhi.
- Mimi nashangazwa na hamasa za Kakhi kwa safari yangu, ijapokuwa sina mapenzi nayo, kulingana na taarifa niliyonayo ni kuwa si wewe wala mkurugenzi wa masoko hamna neno nisiposafiri, na hii ni katika jumla ya kazi zenu na sio zangu!
- Amelazimika kufanya hivyo, si katika uchaguzi wake.
- Ki vipi sijakuelewa!
- Katika kikao cha Idara wakati wa safari yako Tel Aviv palichukuliwa maamuzi ya wewe kupandishwa cheo na kuwa Mkurugenzi Mkuu, na Kakhi kuhamishiwa kazi nyingine, na Kakhi hakupata njia ya kuahirisha maamuzi haya isipokuwa ila kuwajulisha kuwa kuna kazi ambayo hawezi kuifanya mwingine isipokuwa wewe, na kuwa maamuzi hayo yataakhirishwa hadi utakapotekeleza majukumu hayo.
- Na kama sijasimamia majukumu hayo?
- Sijui, nilitaka nisafiri lakini akakataa, pokea tiketi hii safari itakuwa ni siku ya tisa kuanzia leo.

- Mambo yameanza kuwa wazi kwangu, sasa nimejua kwa nini anakazania, je unaweza kunitumia kwa anuani yangu simu na barua pepe ya wakala wetu huko Sweden?
- Baada ya dakika tano utaipata kupitia barua pepe yako.
- Kadhalika namba za simu na email za bodi ya wakurugenzi.
- Nitakutumia.
- Asante William.

Joji alirudi kuandika barua lakini alibadili uamuzi wa kumuandikia Kakhi na badala yake aliandika kwenye bodi ya wakurugenzi.

"Mabwana katika bodi ya wakurugenzi,

Ni furaha kwangu kulitumikia shirika kwa karibu miaka 14, kama ambavyo nimefurahishwa na imani yenu kwangu, nataraji kuwa ni mwenye kustahiki sifa hiyo, mafanikio ya shirika letu ni jukumu letu sote, na napenda kuwashukuru kwa msaada wenu ulioniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika shirika.

Nasogeza kwenu kujiuzulu kwangu, na hiyo ni kwa sababu nilidhani kuwa mtathamini juhudi zangu, lakini nimeshtukizwa na vitisho vya kufukuzwa kazi kama sitokwenda kinyume na maadili yangu na misimamo yangu ya kazi yangu, nataraji kupata haki zangu, kujiuzulu kwangu ni bora kwangu na kwa shirika kuliko kufukuzwa, na kuliko kuuza maadili yangu.

Nawashukuru wote kwa dhana njema nami.

Ni mimi Joji Nesson".

Alipomaliza barua yake, aliangalia barua pepe yake na kukuta anuani za bodi nzima ya wakurugenzi zimeshamfikia, alituma barua yake kwa wote akiwemo Kakhi, kisha alitoka nje ya shirika hadi nyumbani kwa Adam bila kumkuta mtu, hivyo alielekea mkahawani, ambapo hakumkuta vile vile, alimuuliza mhudumu mwenzake Adam nae akamjibu:

- Wewe ndio uliokuja jana, na leo hajaja pia, lakini kuna mtu mmoja katupigia simu muda mfupi uliopita na kutuambia kuwa amepata ajali, na yupo hospitalini na afya yake inaendelea vizuri.

www.path-2-happiness.com

(2)

Joji aliulizia hospitali ilipo na kwenda moja kwa moja, na njiani alimpigia simu Katarina na kumfahamisha…

- Kwa hakika alikuwa bega kwa bega na mimi nilipokuwa hospitalini, na hapana budi na mimi kumfanyia wema.
- Unaonaje ukanipitia ili twende pamoja?
- Mimi tayari nipo karibu na hospitali na kwenda sasa hivi, na wewe unaweza kumtembelea muda wa jioni.

Joji aliingia hospitalini na kuuliza chumba alipo Adam, na alipoingia alimkuta amelala juu ya kitanda na miguu yake imezungushiwa bandeji na huku amezungukwa na idadi ya watu.

- Vipi Adam, kimekusibu nini?
- Karibu Joji, samahani nimeiona sms yako katika simu kabla ya dakika tano hivi; na sikupata simu yangu isipokuwa muda mchache uliopita, vipi hali yako sasa?
- Kimetokea nini?
- Nimeanguka nilipokuwa nikishuka ngazi, na kuvunjika katika mguu wangu, na nimeletwa hospitali jana na nimefanyiwa operesheni ya kuunga mfupa, na mimi ni mzima.
- Mbona hujanipigia simu?
- Asante Joji wewe ni rafiki mkweli, kwa kweli sikuweza kuwasiliana na yeyote yule, rafiki yangu aliyenileta hospitali ndie aliyewasiliana na wale anao wajua katika marafiki zangu, nitakufahamisha kwao: Ahmad kutoka Syria ni Mhandisi Electronic, Adrian, Mfamasia Mwingereza, Ali kutoka Saudi Arabia, mwanafunzi Chuo Kikuu, na Sheikh Baasim wa Azhar kutoka Misri na ni Imam wa Kituo cha Kiislamu hapa London. Nami niwatambulishe; huyu ni rafiki yangu Joji, ni Mhandisi wa programu na Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Advance Programming, aliyeniletea mkoba wa kifahari ambao mliupenda kupita kiasi.
- Karibu, ndio mara ya kwanza kujuana na marafiki wa rafiki yangu.
- Rafiki yangu Joji ni mwingi wa safari, na ni mtu mwenye kujua wajibu wake kijamii.
- Kama alivyonitambulisha Adam, mimi nilikuwa Naibu Mkurugenzi wa shirika la Advance programming, kwa hakika nimefaidika sana na Adam.
- Yaani umeacha? Tokea lini?
- Kabla ya saa moja iliyopita hivi nimepeleka maombi ya kujiuzulu, na baada ya

kukamilisha hilo nikaja hapa kwako.

- Kwa nini?
- Kisa cha kujiuzulu kwangu ni kirefu, achana na hili, vipi mguu wako sasa? Daktari anasema nini?
- Alhamdulillah, maumivu yamepungua; ila nimelazimishwa kukaa hospitalini kwa muda wa siku tano, kisha nitapumzika nyumbani kiasi cha mwezi hivi, kisha mwezi tena, baada ya hapo nitatembelea magongo.
- Baasim AlAzhari alitabasamu: Sipendi kukata maongezi yenu, lakini tunaomba radhi tusali adhuhuri, na tutarudi kwa mara nyingine.
- Nakusubirini.
- Sheikh Baasim ni mwalimu na Sheikh wangu tangu nikiwa mdogo.
- Wameenda wapi?
- Wameenda kusali adhuhuri.
- Leo Jumanne ni swala gani hiyo?
- Sisi Waislamu tunasali mara tano kwa siku, kila swala ina wakati wake.
- Nilishtushwa nilipofahamu kuwa wewe ni Muislamu! Kwanini hukunijulisha tokea mwanzo?
- Niliwahi kukueleza hapo kabla kuwa huwezi kuunganisha jina langu na mazungumzo yangu, bali sura yangu ni dalili ya wazi kuwa mimi ni muarabu Muislamu. Kwa ujumla sikutaka kukuficha chochote, lakini wewe uliniuliza ukinituhumu kuwa mimi ni Mkatoliki na wakati mwingine Mprotestanti, nareja tena kukuomba radhi kama utakuwa umehisi kukuficha kitu.
- Je hamchoki kusali vipindi vitano kila siku?
- Sala hutuondolea matatizo na tabu za dunia wala haituchoshi.
- Nasi pia hali kadhalika, tuna starehe kwa sala ya kila wiki, ama mara tano kwa siku nadhani inachosha!
- Sisi tunapata tabu kama hatusali sala tano kila siku, na sala yetu haihitaji kutoa juhudi au nguvu na hata kwenda msikitini.
- Mnakwenda Msikitini?
- Ikiwa inawezekana kwenda ni bora kwenda msikitini, na kama hali hairuhusu basi sehemu yoyote inafaa kusali, na mimi nitasali katika kiti changu muda sio mrefu.
- Unasali ukiwa katika hali hii?
- Ndio, kuwa katika hali hii ni bora zaidi kusali, kwani mimi namuhitajia Mola

www.path2-happiness.com

wangu kila wakati, na sasa hivi haja zangu kwake ni kubwa zaidi, vinginevyo mitihani ya maisha humfanya mtu akapoteza uwezo wake wa kuvumilia; na hivyo basi kupotea tabia na maadili yake.

- Kwa hakika kushikamana na maadili kunachosha.
- Hivyo basi swala na mawasiliano ya mtu na Mola wake ndio njia mojawapo katika njia za msaada, ili mwanadamu aweze kuongeza masurufu yake katika subira na kudumu katika jambo.
- Nimekutumieni barua kuisoma Qur'an, lakini sijui nisome tarjumi ipi ya Qur'an.
- Natamani ungejifunza Kiarabu; ili ufaidike na ladha ya Qur'an kama sisi tunavyofaidika nayo, hata hivyo nitakupa nakala ya tarjumi ya maana ya Qur'an, lakini ni baada ya kurudi Sheikh Baasim.
- Je Uislamu ni kwa ajili ya Waarabu tu?
- Idadi kubwa ya Waislamu ambao wapo nje ya mataifa ya Kiarabu inazidi mara nyingi ya idadi katika mataifa ya Kiarabu, na Uislamu ni kama Allah alivyosema katika Qur'an: "Rehema kwa walimwengu" (21:10).
- Ni rehema!
- Ndio ni rehema, laiti ungelisoma Qur'an na kuijua ungegundua ni mara ngapi rehema hiyo inapatikana kwa kila kiumbe!
- Ni mfano wa maneno ya Katarina wakati anapozungumzia Ukatoliki.
- Kama ulivyousoma ukatoliki, usome pia Uislamu, kisha urejeshe kama haujakuridhisha.
- Ndio, nimeamua kuusoma na nitaanza na kusoma Qur'an, lakini kwa akili ya kuchambua na kukosoa.
- Vizuri na haswa, Uislamu ni dini ya elimu, wala haukutaki uuamini kabla ya kuusoma, ndio maana maamrisho ya kwanza ya kushuka kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) yanahusu: (kusoma).
- Unajiamini sana kwa Uislamu, nilipokuwa Roma nilikutana na Muislamu kutoka Misri, alikuwa anasema na kuniambia kuwa anatamani kuwa kama sisi, na akaniusia nisijifunze Uislamu.
- Na utakutana na Waislamu pia wakisema hivyo: Kwamba Uislamu ni dini ya wajinga, yenye kurudisha nyuma maendeleo, pia ni dini ya Ugaidi.
- Alikuwa akisema hivyo pia.
- Na utakutana na Waislamu wanaongelea kuwa Uislamu ni dini iliyomdhulumu mwanamke na Uislamu unalazimisha watu kusilimu.

- Nafikiri yote hayo yamekusanyika kwa Muislamu huyu niliyekutana nae huko Roma.
- Je huwezi kukutana na mtu mwingine anayatusi na kukosoa elimu ya hesabu, au uhandisi, au utabibu au kompyuta?
- Wengi sana.
- Je maneno hayo yanapunguza chochote katika hadhi ya elimu hizi? Au inapunguza uwezo wa elimu hizo katika kuhudumia haja zetu?
- Katu hapana, lakini mambo ni tofauti hapa.
- Mimi sioni tofauti yoyote; isipokuwa tu kuna mashambulizi yanayoelekezwa kuuhujumu Uislamu, wakati ambapo katika elimu hatuoni hayo.
- Unakusudia nini kusema kuwa ni mashambulizi ya makusudi yaliyoelekezwa?
- Je una kumbuka shambulizi la kigaidi lililotokea London ambalo lilifanywa na Waislamu?
- Ndio, na baadae kuthibitika sio shambulizi la kigaidi.
- Imethibitika hivyo baada ya vyombo vya habari kuzungumza kwa muda mrefu kuhusu ugaidi wa Waislamu, kisha kukanushwa na kunyamaziwa kama kawaida, je unajua kuwa mimi nilifungwa kwa sababu ya shambulio? Tuhuma ni kuwa mimi ni Muislamu; kwa maana mimi ni gaidi, je wajua kuwa dalili zote zilikuwa wazi kuwa Waislamu wako mbali na mlipuko huo, lakini vyombo vya habari tuhuma zao zipo tayari?
- Je huoni kuwa hayo yote yanasababishwa na vitendo vya Waislamu vyenye kujirudia rudia?
- Katika kila jamii na kila dini kuna wenye kupetuka mipaka, lakini tofauti ni kuwa kadhia inakuwa na makosa ya jinai inapokuwa hakuna uhusiano na Waislamu, na linakuwa la kigaidi kama linahusishwa na Waislamu! Je huoni kuwa hilo ni jambo la kuchekesha?
- Inaelekea ni mwenye hamasa sana na Uislamu!
- Niache niwe muwazi kwako, ni nini kinachokukataza usiwe Muislamu? Ili maisha yako yawe na furaha.
- Swali limevuka mipaka, sikulitegemea, je kuingia katika Uislamu ni wepesi kiasi hiki?
- Ndio, sidhani kama utahitaji shamrashamra za kanisa wala ugumu wa dini za watu, ni kitu chepesi lakini chenye kubeba ujumbe mkubwa.
- Je unatarajia mimi kuingia katika Uislamu ewe Adam?

www.path-2-happiness.com

- Ndio, bali nataraji hivi karibuni sana.
- Samahani, inaonekana hunijui vizuri ewe Adam, mimi siwezi kukikumbatia kitu ambacho hakiendani na akili yangu, mawazo yangu, fikra na misingi yangu.
- Samahani, bali wewe ndio ambaye huujui Uislamu!
- Sijafahamu, unakusudia nini?
- Kusilimu ni jambo jepesi sana, lakini haiwezekani kusilimu kabla ya kuridhika ndani ya nafsi yako kwa ukamilifu, na sio kusudio kutamka maneno ya shahada mbili, yaani Ashhadu anLailaha Illah Llah waana Muhammad Rasulullah kabla hilo hulijaingia ndani ya nafsi yako kwa ukamilifu, kilicho muhimu ni kile kilicho ndani ya moyo wako kwa hivyo la muhimu ni imani kuingia katika moyo wako na kuwa na itikadi na imani na sio maumbo.
- Japokuwa sidhani kama nitasilimu siku moja, lakini nani anajua hilo?
- Japo nina matumaini makubwa kuwa utasilimu, ila mlango wako utakuwa ni elimu; hivyo basi ni wajibu wako kuusoma Uislamu kwanza, na utaingia katika Uislamu baada ya hapo, wewe unapenda elimu, mantiki, fikra na maadili.
- Sijajua kwa maneno hayo wewe unanisifia au unausifia Uislamu au unavisifia vyote viwili? Lakini unanikumbusha na yule Muislamu ambae nimekutana nae Roma na akamwambia Katarina maneno kama hayo, kabla ya kumzawadia kitabu chenye anuani: (Mapenzi yangu makubwa juu ya Masiya yamenifanya kuingia katika Uislamu).
- Je hukuniambia muda mfupi uliopita kuwa Muislamu uliyekutana nae huko Roma alikuwa anaukataa na kujivua na Uislamu?
- Tofauti iliyopo ni kwamba huyu wa mwisho alikuwa ni ndugu yake yule wa mwanzo niliokusimulia, na tulikuwa wote pamoja.
- Ni yupi kati yao ni bora kwa mtazamo wako?
- Sijui, ijapokuwa wa mwanzo ni mkubwa, ila huyu wa pili anaheshimika sana kwa mama yake na baba yake, na yeye anawaheshimu sana, na hakunishughulishi kuwafadhilisha kati yao.
- Na je Katarina alisoma kitabu?
- Ndio, na mimi nimekisoma mara mbili na najua kimemtikisa moyoni mwake.
- Na je wewe umekisoma?
- Ndio, nimekisoma, lakini wewe umeniambia nianze na Qur'an, na wewe utanipa tarjumi yake.
- Sheikh Baasim atakuja sasa hivi amechelewa kidogo, nataraji wataingia sasa

hivi tu, naomba nisali, na ukitaka kuuliza juu ya Uislamu; Sheikh Baasim ndio mwalimu na mjuzi, na mimi ni mwanafunzi wake tu, na nakala yako ya Qur'an zawadi yangu kwako kutoka kwa Sheikh Baasim.

- Nitakusubiri mpaka utakapo maliza kusali, ikiwa watafika sawa na kama vipi nitaondoka.
- Vizuri

Adamu alianza kusali na Joji akimwangalia, muda huo huo Sheikh Baasim alifika na marafiki zake, Joji aliwageukia.

- Adam ameniambia kuwa wewe ni mtu wa dini wa Kiislamu, na akanipa zawadi ya nakala ya tarjumi ya maana ya Qur'an, na akaniambia kuwa wewe ndie utakayenipatia.
- Hakuna katika Uislamu wanaojiita watu wa dini, dini ni kwa watu wote, na nakala ya msahafu ipo katika gari nje, unaonaje tutoke pamoja nikupe?
- Vizuri, nimechelewa sana na nataka kuondoka, ila tumsubiri Adam amalize swala labda arefushe.
- Swala zetu ni kama dini yetu ni nyepesi na yenye furaha.
- Furaha?
- Ndio, furaha ya dunia na akhera, cha ajabu ni kuwa wewe ni rafiki wa Adam na asikuambie hilo, nitamlaumu Adamu kama hajakueleza dini hii kubwa ilivyo, wakati wewe ni rafiki yake, na hakuna atakae kuongoza vizuri kuliko kujifunza kwako Uislamu, je huoni kuwa watu wengi wanabadilika na kutoka katika njia za upotevu badala ya kufuata njia ambazo zitawaletea manufaa katika dini na dunia yao na wanaghafilika na dini ya mwisho ya Mitume na Manabii?
- Huenda ni kwa sababu hiyo ndio maana amenizawadia tarjumi ya Qur'an kutoka kwako.

Adam alimaliza sala yake na kuwageukia upande wa Joji na Sheikh Baasim.

- Ewe Sheikh Baasim usinilaumu; kwa hakika nimemueleza kwamba Uislamu ni furaha ya dunia na akhera.

Baasim alitabasamu na kusema:

- Ewe Joji, sisi kila sala tunayosali tunakuwa na furaha ya dunia ya ajabu, kwani tunatupa mizigo ya dunia kwa Mola muweza, Rahiim, Karimu, Msikivu na Mjuzi, jifunze Uislamu kwani ndio njia bora ya furaha.
- Joji nakutakia furaha ya dunia na akhera aliyokutajia Sheikh Baasim.
- Haiwezekani kubadili dini yangu ila baada ya kusoma na kukinai, nitauingiza

www.path-2-happiness.com

ndani ya fikra yangu, je sikufanya hivyo kwa dini zote ewe Adam?
- Bila shaka, na haya ni maombi yangu kubaki katika njia ile ile, pamoja na mapenzi yangu ya kusilimu, lakini Uislamu hutufundisha elimu kwanza.
- Hapana budi usome kwanza, kisha baada ya hapo huna udhuru wa kutosilimu ewe rafiki yangu, je unataka tushuke sasa hivi?
- Sijajua chanzo cha kujiamini kwenu kuwa kama nitausoma Uislamu nitasilimu?
- Imani yetu ipo kwenye Uislamu wenyewe kwani ni kutoka kwa Allah.
- Nitaona!! Nakuahidini kuisoma Qur'an, na kusoma kuhusu Uislamu, na tuujadili, na baada ya haya nichukue maamuzi yangu.
- Vizuri sana, na hili ndio bora.
- Wala usisahau kusafiri kama ulivyosafiri kwa ajili ya dini zingine.
- Tushuke sasa, nitakisoma kitabu chenu kitakatifu, halafu kila penye tukio kuna mazungumzo yake, na nitajaribu kukutembelea kesho, kwani kwa sasa mimi ni mtu ambaye sina kazi.
- Kwa hakika nimeshtushwa kwa kuacha kazi yako, lakini unaonekana una haraka, na kama hutokuja kesho basi tuwasiliane kwa simu, Mungu awe pamoja na wewe.

Joji alirudi nyumbani kwake akiwa na nakala ya tarjumi ya Qur'an, hakumkuta Katarina nyumbani, aliwasiliana nae na kumwambia yupo njiani kwenda kumuona Adam hospitalini. Akaanza kusoma Qur'an, alishangazwa na wema wa Adam kwake, na kumtangulizia vitabu vingine vinavyo fundisha Uislamu na baada ya masaa mawili hivi, Katarina alirudi nyumbani.

- Nimerudi kutoka kwa Adam.
- Mimi najua hujamtembelea ila umefanya hivyo kwa kuwa yeye ni rafiki yangu na hiyo ni kuniridhisha mimi tu.
- Ni mtu wa ajabu sana!
- Ki vipi?
- Sijui, lakini yeye pamoja na rafiki zake wote Waislamu ambao alikuwa nao hawapeani mikono na wanawake, na wakaomba radhi kwa upole na heshima ya hali ya juu, na je huu ni upambanuzi wao dhidi ya mwanamke kwa njia ya Wayahudi na Wakristo?
- Huenda, sijui, mimi kabla ya masaa mawili nimeanza kusoma kuhusu Uislamu kwa kusoma kitabu chao kitakatifu Qur'an na kwa hakika kwa yale niliyoyasoma hadi sasa inamthamini mwanamke na kumuheshimu.
- Ndio, nimesoma tarjumi ya Qur'an, ndivyo ilivyo lakini nimeshangazwa kwa

namna walivyotangamana nami!.
- Kwa nini? Je kulikuwa na aina yoyote ya udhalilishaji au dharau kwako?
- Hapana, walikuwa wapole na heshima sana, lakini hawakunipa mkono na hawakuniangalia.
- Hata hivyo umechelewa, je hawakuzungumza nawe?
- Tumeongea sana, ila maongezi yao mengi yalikuwa kuhusu Uislamu, sijui kwanini wananikumbusha na baadhi ya makasisi.
- Huenda ikawa hivyo kwa sababu sahibu yao Baasim ni mtu wa dini.
- Hapana, Baasim sio mtu wa dini na amekataa wasifu huu, na akasema kuwa katika Uislamu hakuna watu maalumu wa dini kama vile mapapa kwenu, ila ni kuwa yeye ni mtaalamu wa dini.
- Ndio, umesema kweli, aliniambia maneno hayo hayo, ni mtu mwenye maadili na mwenye tabasamu pana, na amenipa kadi yake ili niwasiliane nae, fikiria!! Ananitaka niingie katika Uislamu, nashangazwa sana na imani yao!
- Katarina aliangalia chini ya sakafu, kama anafikiri jambo katika akili yake: Wote wana maadili mazuri, na wafanya ibada sana, japokuwa sio kama watawa, ni watu wanaotafuta maisha na sio kujitenga na ibada pekee, bali kizuri zaidi wanaona kuwa kazi zao na kusoma kwao ni sehemu ya ibada, na wao hawatenganishi maisha na ibada kama tulivyo sisi, fikiria Adam amesali juu ya kitanda chake! Na kuniambia: Sisi tunasali popote; na dini ni nyepesi.
- Amesali nikiwepo, na akaniambia kuwa wao wanasali vipindi vitano kwa siku na kwamba sala zao zinawapa furaha, lakini mimi sijatosheka kwa yale waliyosema japokuwa wanasema kwa kukinaisha.
- Ndio, kukinaishwa kwao kuko katika hali ya juu, na maneno yao yana athiri sana, mahusiano yao na tabasamu zao ni zenye athari kubwa.
- Inaelekea umevutiwa nao mno!
- Sio suala la kuvutiwa, suala ni kuwa Waislamu na Qur'an na Uislamu ni mfumo tofauti kabisa na ule tuliouzoea.
- Pambanua zaidi, ni hisia hizo hizo nimezipata pindi nilipoanza kusoma kitabu chao kitukufu (Qur'an), sikuweza kuifahamu kwa ukamilifu wake, hisia ngeni kabisa za ndani mwangu, haswa katika maudhui kama: Kumpwekesha Allah na kumtukuza kwake, pamoja na majina na sifa zake, au visa vya Mitume na hasa Yesu na Bikira Maria, au maadili na tabia.
- Ni kama hisia zangu hivyo hivyo, lakini nashauri tusifanye haraka kuhukumu,

www.path-2-happiness.com

mambo mengi yatakuwa wazi kwetu kila tutakaposoma kuhusu dini hii, wakati huo tutajua udhaifu wake, mapungufu na migongano iliyopo, wala simaanishi kuwepo mfano wa mambo haya katika Uislamu, pamoja na hali yao ya kukosa maendeleo na udikteta wao.

- Pamoja na kuvutiwa na Adam, lakini sina hamu ya kutaka kuujua Uislamu, ila nitajitahidi katika hilo, ingawa nimefurahishwa muda mfupi uliopita nilipokuwa nikisoma Qur'an.
- Kwa hakika inashangaza unaposoma kitabu chao kitukufu!
- Habari nzuri ni kuwa nimepeleka maombi ya kujiuzulu, ni kiasi gani namchukia Kakhi muongo na mwenye hila nyingi, nimekuja kufahamu kuwa yeye ndie aliyekataa nisipandishwe cheo na kunipa majukumu ya safari ya Sweden, nimeandika barua ya kujiuzulu kwa bodi ya wakurugenzi, wasiponijibu itakuwa ndio kujiuzulu kwangu moja kwa moja.
- Kwa hivyo maadili yako yameshinda matakwa na maslahi yako?
- Huenda, lakini kilichosukuma maamuzi hayo nilipojua maamuzi ya bodi ya wakurugenzi na majibu ya Kakhi, nina matumaini kutoka kwao, na kwa hali yoyote kama sijapata jibu la kuridhisha kutoka kwao, basi nitapeleka malalamiko yangu katika chama cha kutetea wafanyakazi.
- Ama kwa upande wangu bado naendelea kupambana kati ya maadili na kazi yangu, nilikuwa najaribu kuficha shaka yangu, ila wewe umedhamiria kufungua kilichokuwa na sitara.
- Tangu tumeoana sijawahi kukuona umebadilika kwa haraka kama mwezi huu wa mwisho na hasa baada ya kuwasili kutoka TelAviv!
- Sio kila mabadiliko na mageuzi ni shari yote au ni kheri yote, na natamani mabadiliko yangu haya yawe ya kheri kama nilivyokuwa.
- Haa, haa, je kuna kheri yoyote kwenye Ukatoliki?
- Itikadi yangu kwa Masiya na Muokozi wetu ni kubwa sana na katika Ukatoliki pia, na wala sidhani kama kuna kheri zaidi ya hiyo, lakini ni nani anajua?
- Haahaa, leo nataka kulala mapema, hata hivyo nitasoma barua pepe haraka haraka.

Joji alifungua email na kukuta baadhi ya majibu ya barua yake aliyouliza juu ya maadili, alifupisha na haraka kuwatumia wote, kwa kiasi kikubwa ilikuwa inawafikiana na maamuzi yake.

John Luke: Maadili yanakuwa kwanza kwa mtu mwenye ujasiri, lakini pamoja nayo kuna tabu na sononeko.

Levi: Sahihi ni kuwa maadili ni kitu muhimu zaidi, lakini sio lazima tuwe na uwezo wa hilo, sisi tunakuwa ni dhaifu mbele ya mbinyo wa maisha.

Habib: Ni lazima maadili yatangulie, vinginevyo tutakuwa kama wanyama porini.

Katarina: Inavyotakiwa ni maadili kutangulizwa ingawaje ni uamuzi mgumu.

Bado nasubiri majibu yenu juu ya barua yangu iliyotangulia kuhusiana na Qur'an.

Joji."

Aliendelea kupekua email yake na kuchukua ujumbe wa John Luke

"Rafiki yangu Joji,

Japokuwa ni muda mfupi tu tokea tufahamiane, ila tumekuwa karibu na fikra zetu zinakaribiana, kwa hivyo naomba ushauri wako katika jambo huenda likawa geni kwako;

Baada ya safari yenu, nimesoma kitabu alichopewa zawadi mke wako na Muislamu, nimesoma kupitia intaneti, halafu niiporudi nikakutana na mhandisi majengo Muislamu na tukajadiliana nae na akanitaka mimi nisome tarjumi ya Qur'an kwanza, nikasoma chote kwa ukamilifu zaidi ya mara moja, kisha tukakutana kwa mara nyingine na kujadiliana, sijui ni siri gani ya uchawi iliyopo katika kitabu hiki! Nikamuuliza ufafanuzi wa mambo katika Uislamu; alinijibu kuwa yeye hajui chochote zaidi ya kuwa yeye ni mhandisi tu. Nikamuuliza tena: Nani anaweza kunielezea vizuri juu ya Uislamu, alijibu kwamba hamjui yeyote hapa Italia kwani yeye ni mgeni, na ikiwa unataka kuujua vizuri Uislamu, kuna njia mbili mbele yako: Ima usome vitabu vilivyoandikwa juu ya Uislamu, navyo vipo vingi, ila baadhi yake vimeandikwa na maadui wa Uislamu, au njia ya pili: Umtafute mjuzi wa Uislamu hapa Italia au usafiri, nimeamua nichukue njia zote mbili, hivyo basi tokea msafiri nasoma kwa muda wa masaa matano kuhusu Uislamu, na nataka nisafiri kwenda Misri hivi karibuni, au Libya, je unanishauri nini?

Salamu zangu kwako na kwa Katarina.

Ni mimi John Luke."

Alimjibu…Rafiki yangu John Luke.

"Nimesoma ujumbe wako na nimestaajabishwa na ushujaa wako, inavyoelekea mabadiliko ambayo yametokea kwako kwa muda mfupi tangu safari yetu ni makubwa sana na zaidi ya matarajio yetu, mimi nakuunga mkono kufuata njia zote mbili, na naomba unipe taarifa ya pale utakapofikia, kwa hakika nafaidika sana nawe na akili yako ya uchambuzi na utafiti, Salamu zangu kwako.

Ni mimi Joji."

www.path-2-happiness.com

(3)

Joji aliamka na kumkuta Katarina ameshaandaa chai, walikaa na kuanza kunywa chai.

- Sina kazi leo na sijui nifanye nini?
- Nenda kazini, kwani bado hujakubaliwa au kukataliwa kujiuzulu kwako, na kutokwenda kwako ni hoja dhidi yako katika chama cha watetezi wa wafanyakazi.
- Sijakuwa na ufahamu huo akilini mwangu, unayo haki.
- Ama kwa upande wako umekata shauri ya jambo lako, ama kwa upande wangu nitajaribu kulimaliza leo pia.
- Unataka kulimaliza, vipi na kwa kitu gani?
- Sijui, lakini nitakwenda na kujaribu kulimaliza suala langu.
- Jana nilikutumia ufupisho wa yale yaliyokuja kati ya maadili na maslahi katika email yako, soma huenda ukafaidika nayo kabla ya kuchukua maamuzi.
- Nitasoma kabla ya kuchukua uamuzi, nitakwenda sasa nisije nikachelewa.
- Na mimi nitatoka sasa hivi.

Joji alienda kazini kwake na kuingia ofisini mwake, pindi alipokaa tu alijiwa na mkurugenzi mkuu wa mahusiano akiwa ni mwenye hasira:

- Umefanya nini?
- Sijafanya kitu, kwani nini kimetokea?
- Baada ya kutoka wewe jana, Kakhi aliniita kwa hasira, na kwa mara ya kwanza nilimuona amekasirika hivi, na kuniuliza Joji amepata wapi anuani za wakurugenzi wa idara mbali mbali? Nilimjibu sijui.
- Na kwa nini hukumweleza kuwa wewe ndie uliyenipa?
- Huenda akanidhuru! Wewe unamjua kuwa yeye ni dhalimu hafikirii isipokuwa kwa maslahi yake tu.
- Hivi ndivyo tunavyo ogopana wenyewe kwa wenyewe, jambo la kushangaza sana. Sitamueleza zimetoka kwako, kuwa na amani tu, lakini unajua kwa sababu zipi amekasirika?
- Inavyoonekana wafanyakazi wa idara wamewasiliana nae na kutaka kukutana haraka ndani ya siku tatu, kwa mujibu wa barua yako.
- Mkutano juu ya nini?
- Sijui? Ninachofahamu ni maudhui kuhusiana nawe, ndio maana nikakuuliza ulichoandika katika barua?
- Kama ni hivyo hali inahamasisha sana, sikutegemea kama itakuwa hivyo!

- Inahamasisha! Kwa kitu gani inahamasisha?
- Hakuna kitu, ila niliwatumia barua ya kujiuzulu kwangu, kwa hali hiyo niamini hakuna mtu mwingine atakayejua kwamba wewe umenipa email zao.
- Nakushukuru, naomba ruhusa.

Joji alitafakari kwa kina hatua inayofuata ambayo anatakiwa kuifanya kwa sasa, kwa sababu anajua hila na uongo wa Kakhi, na inawezekana akaitumia njia hii katika kikao cha idara kwa urahisi na yeye hataki kuliachia shirika, je atatakiwa kuhudhuria katika kikao cha baraza, au awape taarifa ya kina kilichotokea? Au afanye nini? Cha ajabu ni kuwa hadi sasa hajajibiwa na mtu yoyote kutoka kwa wajumbe wa idara kwa njia ya barua pepe! Kitu ambacho kinajulisha kabisa kuwa watamsikiliza Kakhi peke yake, na hili ndilo asilolitaka, alifikiri sana, halafu akaamua kutuma barua ya pili kwa idara kwa kuandika:

"Wajumbe baraza la idara:

"Ni furaha kwangu kulitumikia shirika kwa karibu miaka 14, kama ambavyo nimefurahishwa na imani yenu kwangu, nataraji kuwa ni mwenye kustahiki sifa hiyo, mafanikio ya shirika letu ni jukumu letu sote, na napenda kuwashukuru kwa msaada wenu ulioniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika shirika.

Nimekuleteeni nyinyi dhulma zangu na naomba kujiuzulu, na sijapata jibu lenu, kwa maana hiyo ni kuendelea kudhulumiwa na kukubaliwa kujiuzulu kwangu, au ndio utakaso kwangu na kutaka kuendelea na kazi, nina matarajio kuwa mnijadili moja kwa moja katika kikao cha Baraza la Idara.

Nakushururuni nyote kwa ushirikiano wenu mzuri.

Ni mimi Joji."

Kwa barua hii Joji alitaka aitwe kuhudhuria katika baraza; ili awaonyesha kila karatasi wajumbe hao, lakini haikuchukua muda baada ya kutuma barua ile ilipigwa simu ofisini kwake, na Kakhi akiwa upande wa pili.

- Yote hayo ni kwa ajili ya maadili ewe mwenye maadili! Je unaweza kuja sasa hivi ofisini kwangu?
- Ndio ni kwa ajili ya maadili na sitobadilisha maadili yangu.
- Je unaweza kuja kwangu?
- Nakuja sasa hivi.

Joji aliingia kwa Kakhi na kumuona ameghadhibika, na haraka alimsemesha.

- Joji unataka nini?

www.path-2-happiness.com

- Nataka kutokwenda kinyume na misingi yangu.
- Kama kwamba unakwenda mbio uwe rais wa shirika.
- Hilo sijaliendea mbio, likinijia na hali ya kuwa nastahiki si tatizo.
- Kwa hiyo masuala siyo maadili bali ni vyeo.
- Elewa kama unavyotaka, ila mimi sibadili maadili yangu, na sijaja kwako ila ni baada ya kuniomba na kunijulisha kuwa tutaafikiana, amini Kakhi kuwa sitaachana na maadili yangu.
- Ikiwa masuala ni kama unavyosema; masuala ya maadili na sio masuala ya vyeo, basi nina ombi lingine kwako.
- Ni lipi hilo?
- Mimi nitasafiri kwenda Sweden, kwa sharti wewe utoke London.
- Kwa nini?
- Maudhui yananihusu mimi mwenyewe, mimi sitaki kutoka katika shirika kwa sasa hivi, baraza la idara likikutana kwa sasa na wewe upo London watachukua uamuzi wa kunitoa katika shirika, kwa hivyo nimewakinaisha umuhimu wa safari yako Sweden, kisha akatabasamu na kusema: Kwa kuchunga maadili yako mimi ndie nitakwenda Sweden, lakini ni lazima wewe uwe nje ya London kwa wakati huo ili maamuzi yachelewe kutolewa.
- Nisafiri wapi?
- Sehemu gani unapenda, tuna kazi Ujerumani, Ukraine na Misri.
- Na ikiwa nitakataa?
- Itakuwa wazi kadhia ni vyeo au maslahi na sio maadili! Na wakati huo kila tukio lina mazungumzo yake.
- Nitatafakari na kesho nitakupa jibu.
- Utanijibu mimi na sio kwa wajumbe wote wa baraza.
- Nakuahidi hilo.

Joji alitoka katika shirika, njiani akiwa kwenye gari lake alimpigia Tom.

- Je unao muda nikutembelee?
- Karibu sana.
- Baada ya nusu saa nitakuwa kwako, nipo njiani.

Joji alifika kumtembelea Tom na kuingia tu akamkuta mpokea wageni mpya, nae alimkaribisha Joji;

- Dr. Tom anakusubiri karibu.
- Karibu Joji, mgonjwa wa kwanza baada ya kufungua kliniki, haijafunguliwa ila

leo, na sijaweka ahadi isipokuwa kuanzia kesho.

- Habari njema, samahani sijafuatilia maudhui ya Baraad je imeisha.
- Ameondoka bila kurudi.
- Amekwenda wapi?
- Jela, amekamatwa akiuza madawa ya kulevya.
- Baraad ni mtu ninayemchukia sana!
- Kwa nini unamchukia?
- Ni mtu asiyekuwa na maadili na mtu anapokosa maadili anakuwa karibu na wanyama wa porini.
- Mitihani migumu iliyoje! Nilikuwa na chaguzi mbili mbele yangu kuyaacha maadili yangu na kumaliza matatizo yangu yote kwa haraka, au niendelee na maadili yangu na niingie kwenye mtihani mgumu, kwa hiyo nimeamua kubaki katika maadili yangu na nilikaribia kupoteza kila kitu, lakini nimekinai kuwa kushika maadili mwisho wake kuna wema na hili ndilo lilivyotimia.
- Kana kwamba unafahamu lile ulilokuja nalo!
- Ni lipi?

Joji alimuhadithia Tom kirefu tatizo lake pamoja na Kakhi mpaka kafika katika maudhui ya safari na kusita sita kwake.

- Nilitaka kukushauri wewe: Je unadhani kuwa safari yangu pasina masharti ni jambo lisilokuwa la kimaadili na kuachana na maadili yangu?
- Sijakufahamu! Vipi inawezekana kujiondoa katika maadili yako? Wewe utasafari kwa kazi nyingine.
- Lakini mimi nina hakikisha malengo mabaya ya Kakhi.
- Na huenda ukamfedhehesha sana Kakhi mbele ya Baraza la Idara.
- Kwa hiyo rai yako mimi nisafiri?
- Ndio, nenda Misri.
- Kwa nini?
- Hukumbuki kuwa katika kikao chetu kilichopita majadiliano yetu yalikutaka usome Uislamu, na hii ni fursa imekuja kwako, na laiti kama sio kufungua kliniki leo tungesafiri pamoja.
- Sitaki kusafiri, kwa sababu nimesafiri sana kipindi kilichopita, na kama kusafiri basi ningependa kwenda Ujerumani.
- Uamuzi upo kwako, ila mimi naona safari ni muhimu, utajua Waislamu walivyo na kujua aibu na makosa yao.

www.path-2-happiness.com

- Nitafikiri, na kwa hali hiyo wewe ndie mtu wa mwanzo nakutaka ushauri, nitafikiri zaidi kisha nitakuomba tena ushauri, kisha nitakujulisha maamuzi yangu, naomba ruhusa yako; leo wewe umeshughulishwa na kliniki yako, na wewe unastahiki hivyo kudumu katika maadili yako, naomba niondoke.

Akiwa njiani aliwasiliana na Adam na kumweleza kuwa anataka kumtembelea, alimuomba udhuru kwa sababu daktari atachukuwa baadhi ya vipimo sasa hivi, hivyo atamsubiria kwa ziara ya jioni, Joji alielekea nyumbani na aliamua autumie wakati wake kwa kusoma kitabu kitakatifu cha Adam ambacho ni Qur'an.

Pindi alipokuwa akisoma mara watoto wake Maiko na Sali wakaingia

- Baba, leo umerudi mapema?
- Ndio, kuna mambo yametokea kazini ndiyo yaliyonifanya kurudi mapema.
- Unasoma nini baba, upo kwenye mawazo na wewe unasoma?
- Nilikuwa nasoma kitabu kinachoelezwa kwamba ndio cha Waislamu.
- Waislamu ambao wanaitwa magaidi?
- Ndio.
- Shuleni kwetu kuna mwanafunzi Muislamu kutoka India, ni mvivu darasani ila ni mzuri na sio gaidi.
- Ugaidi hauna dini, achana na yale wanayosema, na unaweza kuingiliana na watu kwa mujibu wa tabia zao.
- Japokuwa ni mwema ila nahisi yeye anajitenga kidogo na sisi.
- Kwa nini?
- Sijui! Labda ni kutokana na wanavyosema sana kuwa yeye ni gaidi, au ni kutokana na baadhi ya wanafunzi kudharau umbo lake lilivyo.
- Ni nani anayesema hivyo?
- Mimi sipendi hivyo, lakini baadhi ya wanafunzi wanafanya hivyo.
- Mwanangu maadili na tabia za watu ndio vitu vinavyotakiwa kunyanyuliwa au sivyo watu watapotea.
- Ni mfano wa maneno ya Iqbaal.
- Ni nani Iqbaal?
- Ni rafiki yangu Muislamu Muhindi niliyekueleza.
- Ndio katika Qur'an: "Hakika ya mbora wenu mbele ya Allah ni MchaMungu" (49:13); hakuna mtu mbora wa rangi yake, au jinsia yake isipokuwa kwa UchaMungu tu?

- Je haukuwa Uislamu ni kwa Waarabu tu? Mimi nimeshangazwa nilipo jua kwamba Iqbaal ni Muislamu!
- Idadi ya Waislamu wanakaribia bilioni na nusu, na wameenea China mpaka Marekani na cha ajabu ni kwamba asilimia 80% ya Waislamu wapo nje ya ulimwengu wa kiarabu.
- Ni mara ngapi natamani usawa huu kwetu sisi!
- Nini?
- Baadhi ya wanafunzi wananihesabu mimi ni Muhindi na sio Muingereza, na hiyo ni kwa sababu ya umbo langu, na kwa sababu ya mama yangu.
- Hili limetakatazwa mwanangu, na unaweza kumuambia mwalimu.
- Nitamwambia, lakini najua kuwa hawataacha kusema ila mbele ya mwalimu tu.

Joji alipata kigugumizi moyoni mwake pale walipotoka watoto wake:

- Hata Sali anajua tofauti kati ya utaratibu wa kimaadili na kati ya maadili peke yake!

Joji aliendelea kusoma Qur'an hadi alipoingia Katarina.

- Ilikuwa ni siku ndefu ilioje!
- Samahani, dakika tu.
- Kitu gani unasoma?
- Nasoma kitabu cha Waislamu, Je unaweza kunisubiria muda mimi nina kazi.
- Umefika wapi kusoma?
- Sijamaliza.
- Unaonekana umezama.
- Sikia, nini anasema Mola katika kitabu cha Waislamu: "Alif Lam Ra. (A.L.R). Hizi ni Aya za Kitabu na Qur'ani inayo bainisha. HUENDA ikawa walio kufuru wakatamani wange kuwa Waislamu. Waache wale, na wastarehe, na iwazuge tamaa. Watakuja jua. " (15: 13)
- Kwa nini umechagua ayah hizi au kipande hiki hasa?
- Sijui hasa, ni kwa nini baadhi ya maeneo ya kitabu hiki yananiongelea mimi kwa dhati? Miongoni mwayo ni kipande hiki.
- Ni nini ambayo kinakuongelea katika kipande hiki?
- Kitabu kinachobainisha…makafiri wanatamani Uislamu..Hawa makafiri wanadanganyika kwa kula na kustarehe, sijui kwa nini! nahisi aya hizo zinanisemesha mimi?
- Je zinakulenga wewe, yaani wewe unatamani kuwa Muislamu?

www.path-2-happiness.com

- Fikiria, haiwezekani …lakini natamani nipate majibu ya maswali yangu, na nipate njia ya furaha, na nisishughulishwe na kula, kunywa, na kustarehe, sijajua ni kwa nini nahisi baadhi ya aya zinanisemesha mimi mwenyewe hasa?
- Je haiwezekani kwamba njia ya furaha ikawa Uislamu?
- Haa haaa –ni kama maneno ya Adam, ijapokuwa mimi sidhani hivyo, lakini nitaurudi Uislamu kwa elimu kama nilivyozijibu dini zingine na sio kuishia katika dhana tu.
- Kwa mnasaba kwanza vipi habari ya Adam?
- Wewe umemuona baada yangu, na mimi sijamuona leo hii, kuna mambo mengi sana yametokea kazini leo.
- Nipe habari nzuri, kuna jipya?
- Kakhi amenipa ofa mpya ya kusafiri kwenda Ujerumani, pasi na kuacha maadili yangu.
- Je umewafiki na kumaliza tatizo?
- Hapana, nimemwambia kuwa nitatafakari, kwani mimi sitaki kusafiri kwa sasa.
- Kwa hiyo masuala sio maadili, kadhia kwa sasa ni rai.
- Hivi ndivyo Kakhi alivyonieleza..kwa hakika zimejitokeza sababu zingine, hakika nimemshauri Tom na yeye ana rai nyingine.
- Ni ipi rai ya Tom?
- Ananitaka nienda Misri.
- Uliniambia Ujerumani?
- Kakhi amenipa uchaguzi: Ujerumani au Misri au Ukraine, na mimi napendelea Ujerumani na Tom ananihimiza Misri.
- Ni kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa maswali yako?
- Ndio, lakini sipendi kwenda katika nchi zisizo za maendeleo za Afrika, badala ya nchi yenye nguvu na maendeleo kama Ujerumani.
- Lakini Misri pamoja na kujua Uislamu na waislamu pia ni nchi ya Wakoptiki na ni nchi yenye Piramidi na mto Nile.
- Unaelekea wewe kuijua Misri vizuri!
- Ndio, ni nchi ya kanisa la Orthodoksi wa Kikoptic, na nchi yenye moja ya maajabu ya dunia, piramidi, ni nchi yenye mto mrefu duniani. Mto Nile, nilikuwa namjua mkoptik wakiothodoksi na mara nyingi alikuwa akiwakosoa sana Wakatoliki… ananikosoa kwamba mimi ni mwenye kurahisisha sana mambo ya dini kama sisi tunavyowakosoa nyinyi Waprotestanti.

- Kwa sababu nyinyi mmejigawa kutokana na wao kama walivyojigawa Waprostanti kutokana nanyi. Je nielewe kutokana na maneno yako kwamba wewe ni kama Tom unaunga mkono Misri kuliko Ujerumani?
- Huenda, ila uamuzi unao wewe, mimi napenda nchi zenye historia za kale, na huenda wewe unapenda nchi zilizoendelea, zilizozuka sasa hivi, japokuwa umestarehe sana ukiwa India.
- Nitaangalia, lakini unaonekana unaunga mkono mimi nisafiri.
- Japo mimi natamani tukae pamoja na tustarehe baada ya safari zako zilizofululiza, lakini kujivua na misingi au maadili inamfanya mtu kupata hasara mwenyewe, na laiti ungethibiti katika maadili yako huenda ungepata hasira katika kazi yako, na huenda kwa hatua hii ni bora kuhusiana na maudhui yako.
- Ndio, huenda hii ndio njia bora ya kujikomboa, kwa hali yoyote bado ninayo fursa mpaka kesho kutafakari zaidi juu ya maudhui, na wewe je unalo jipya katika maudhui yako?
- Ndio, natamini huenda likawa limeisha.
- Limeisha, nini lililoisha?
- Nadhani huu ndio mwezi wa mwisho kufanya kazi kwao.
- Na baada ya hapo?
- Nimeanza mpango wa kutafuta kazi nyingine, usijisumbue nafsi yako nitakueleza hatua kwa hatua, nataka kuwaandalia chakula cha mchana Sali na Maiko.

(4)

Wakati wa ziara ya jioni Joji alielekea hospitalini kumtembelea Adam, aliingia ndani na kumkuta akiongea na Sheikh Baasim huku wakicheka.

- Karibu, inaonyesha leo mna furaha.
- Namshukuru Allah, mimi nina furaha siku zote, na leo furaha ni zaidi kwako na kwa kaka yangu Adam, habari yako?
- Ni nzuri, vipi hali yako ewe Adam?
- Mimi ni mwenye afya nzuri, namshukuru Allah mwenye fadhila.
- Nimekuja ili kukujulia hali yako na kukuomba ushauri wa jambo!
- Karibu.
- Sitarefusha muda wako, mimi nimeingia katika mtihani baina ya maadili yangu na kazi zangu, na baada ya mvutano huo nimechagua maadili yangu, na mambo yangu yamekuwa mepesi, lakini kwa safari ya ghafla.

www.path-2-happiness.com

- Kila mwenye kuthibiti katika maadili hata kama itaonekana kupata hasara lakini atafaidika mwishoni.

Sheikh Baasim alitabasamu na kusema:

- Samahani naomba kuongezea, Je hujaisoma Qur'an namna gani Mitume walishinda kwa subira zao na maadili yao?
- Enyi Waislamu mnayo katika Qur'an kwamba kila Mtume alinusurika bali hata Issa alinusurika na hakuuwawa, ama kwa upande wetu sisi ni kwamba Issa alijitoa muhanga kwa ajili ya wanadamu ili kuwakomboa.

Sheikh Baasim akiwa mwenye tabasamu:

- Haa haa kwa hivyo Uislamu unamthamini Yesu na kumpenda zaidi kuliko nyinyi.
- Lakini haumpi sifa na maajabu na kuwatetea wanadamu kama sisi.
- Bali unampa sana, inaonyesha hukusoma Qur'an, je hukusoma kisa cha Yesu katika Qur'an na maudhui zaidi?
- Mimi sijachukua tarjumi kutoka kwake ila jana tu, lakini nimesoma vitu takriban vyote, na nimesoma kisa cha Yesu mfalme wa amani.
- Ikiwa umesoma chote, basi nataraji kuwa umesoma tarjumi ya kauli yake Mwenyezi Mungu katika sura ya maryam kwa ndimi ya Yesu (Juu yake amani): "Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai" (19:31)
- Na kauli yake Mwenyezi Mungu:
- "Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa, na siku nitakayo kufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai." (19:33)
- Na tarjumi ya kauli yake katika surat AlImraan:
- "Na ni Mtume kwa Wana wa Israili kuwaambia: Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakwambieni mnacho kila na mnacho weka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika haya ipo Ishara kwenu ikiwi nyinyi ni wenye kuamini." (3:49)
- Ndio, nimesoma zote ulizozitaja, lakini ajabu yenu ni jinsi mlivyompokea Yesu!
- Je unapenda ukweli.
- Haa haa, bila shaka.
- Nyinyi hamumpokei Yesu kama sisi.

- Ki vipi?
- Nyinyi mnamuona kama amesulubiwa, na sisi tunaamini Allah alimpaisha, je, hujaisoma ayah katika Sura ya AnNisaai: "Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini." (4:157)
- Ndio.
- Nyinyi au kwa uchache baadhi yenu, mnaamini kuwa Bi Maryam mwenye kutakasika kwamba amezini.
- Na katika nyinyi wapo wanaoamini ni baba wa Yesu.
- Hana baba, ni kama alivyomuumba Adam bila ya baba wala mama, kadhalika Yesu ameumbwa kutokana na mama bila baba, na yeye aliongea akiwa mchanga, ili amtetee mama yake mtoharifu.
- Bali heshima yetu ni kwa dini zote tangu kwa baba wa binadamu Adam juu yake amani, Mitume wote walikuwa wakilingania kitu kimoja ambae ni Mungu mmoja, na kila Mtume aliyeletwa alikuwa anabashiri kwa Mtume baada yake, je hukusoma tarjumi: "Na Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninaye thibitisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhaahiri! " (61:6) Je siyo hivyo katika kitabu chenu?
- Hapana, sijasoma ulichotaja, huenda ikawa kwenye zile zingine zilizosalia ambazo sijazisoma, ni hivyo katika baadhi ya vitabu vyetu tu.
- Tatizo la injili ni kwamba imebadilishwa mara nyingi sana na katika uandishi tofauti tofauti, na hasa kipindi ambacho Wayahudi waliwabana Wakristo.
- Nahisi hili ni tatizo la vitabu vyote vitakatifu, niletee kitabu ambacho hakijabadilishwa.
- Qur'an haijabadilishwa katu, kwa mujibu wa maafikiano ya Waislamu wao kwa wao na hata wasiokuwa Waislamu bali hakuna kitu kilichodhibitiwa kwa kunakiliwa kwa kiwango cha wanadamu kama Qur'an na hili limethibitishwa na hata wasiokuwa Waislamu, wamenakili maelfu ya watu kutoka kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kutoka kwake wakanakili maelfu, na wala

www.path-2-happiness.com

hakuna tofauti kati ya mtu na mtu mwingine katika kunakili na hata herufi moja kutofautiana, sio herufi tu bali hata chini ya herufu.

- Ni nini hicho chini ya herufi?
- Katika lugha ya Kiarabu kuna kitu kinaitwa udhibiti, nayo ni sauti ya herufi, na kitu walichokubaliana katika Qur'an, bali wamekubaliana hata katika namna ya usomaji wake na uvutaji wake.
- Je hakuna tofauti kati ya nakala zake?
- Katu, ila kuna tofauti ya visomo vilivyo pokelewa na wapokezi tofauti tofauti lakini hakuna tofauti ila katika lahaja tu.
- Kwa maneno yako, inawezekana kuwa Yesu katika kisomo kingine ameuliwa, na kisomo kingine amejitoa mhanga?
- Haiwezekani, kwani Qur'an ni moja na haitofautiani, ninachomaanisha ni tofauti ya utamshi tu, na mara nyingi ni maana hiyo hiyo au maneno hayo hayo tu, tofauti ipo katika matamshi tu.
- Kwa kiwango hiki nadhani unazidisha!
- Unaweza kusoma yale yaliyosemwa na wanahistoria wenu na utakuta yanalingana na niliyosema mimi.
- Lakini…je huoni wewe unazidisha au mwenye hamasa kupita kiasi?
- Huenda, lakini Adam ameniambia ulikuwa unatafuta majibu ya maswali yako kwa muda mrefu na umepitia dini zote kutaka kujua, na sasa umefikia kuufahamu Uislamu, na amenieleza wewe unataka majibu ya kielimu yanayo endana na uhakika.

Adam alijiweka sawa katika kikao chake na akaingilia mazungumzo yale:

- Mjadala ni mzuri, samahani kwa kuwakata, niambie ulikuwa unataka kuniomba ushauri gani Joji?
- Kwa kweli umenisahaulisha maudhui yangu ewe Baasim.
- Samahani Joji.
- La muhimu ni kuwa baada ya kushikilia maadili yangu nimefika katika njia panda; ima nisafiri safari ya kikazi isiyopingana na maadili yangu au niache kazi yangu, na mimi nina hamu ya safari, na wakati mwingine najihisi kuchoka na safari nyingi.
- Wewe umetoka katika safari na kwenda safari!
- Umesema kweli, ukweli sina hamu ya safari, lakini inaonekana ndio sehemu bora zaidi ya kutokea kutokana na tatizo langu kazini.

- Uchovu wa mwilini rahisi kuliko mtu kayaacha maadili yake, na ikiwa utajivua nayo; kwa hakika roho yake itachoka, na wapi unakusudia kusafiri?
- Kwenda Ujerumani au Ukraine au sehemu nyingine ile.
- Nilikuwa natamani usafiri kwenda katika nchi ya Waislamu, kama ulivyosafiri kujifunza dini za wanadamu (za ardhini), kisha kujifunza Uyahudi, kisha Ukristo, nilikuwa natamani usafiri; ili uujue Uislamu zaidi.
- Ujerumani au Ukraine au Misri.
- Adam aliangalia chini na kuachia mikono yake: Oh, natamani sana Misri, mimi na Sheikh Baasim tumetokea Misri, natarajia wewe utaujua Uislamu vizuri kama utakwenda Misri.
- Je wewe ni Mmisri?
- Ndio, na nadhani nilikujulisha hapa kabla.
- Huenda, lakini sikumbuki.
- Ikiwa utakwenda Misri, nitaongea na baadhi ya rafiki zangu wakupokee huko, na wakupeleke sehemu za kitalii.

Sheikh Baasim kwa sauti ya furaha:

- Ndugu yangu ni mwalimu wa hesabu Cairo, huenda akakutayarishia kila unachohitaji.
- Pamoja na kuwa nilikuwa na hamu ya kuelekea Ujerumani, ila ni kuwa kila ninayemtaka ushauri ananiambia niende Misri, huenda kama ni hivyo nikamjibu Kakhi kesho kuwa nitasafiri kwenda Misri.
- Na mimi nitasubiria jibu lako ili nimwambie ndugu yangu.
- Laiti ningesafiri pamoja nawe, nimetamani sana Misri, nimewakumbuka jamaa, ni takriban miaka miwili sijarudi huko.
- Kwa nini hatuendi pamoja na mimi?
- Kesho kutwa nitapewa ruhusa ya kutoka hospitali Inshaalah, na mitihani ya Chuoni ni baada ya wiki tatu.
- Kwa kuwa unaendelea vizuri hili linatosha, unataka zawadi gani nikuletee kutoka Misri wewe na Baasim?
- Haa haa, niletee Misri yote.
- Haa haa.

Usiku ulipoingia Joji alifungua email yake na kukuta majibu ya rafiki zake yamefuatana kuhusiana na swali lake juu ya Qur'an, na kuwarudishia tena baada ya kuifupisha.

www.path-2-happiness.com

Levi: Sina jibu la wazi, nimesoma baadhi tu, muda haukutosha.

Habib: Kimeandikwa kwa umakini zaidi kuliko vitabu vingine vya mbinguni.

Tom: Samahani, nilishughulishwa na kliniki, sijasoma kitabu cha Waislamu ila kidogo tu, lakini nitakisoma.

Katarina: Kinaonekana kweli kimetoka kwa Mungu.

John Luke: Kielimu Qur'an ni thabiti, imenukuliwa kutoka kwa Muhammad bila kubadilishwa, hivyo basi mwenye kumuamini Muhammad ni wajibu kwake kuamini kuwa Qur'an imetoka kwa Mungu.

Na kilicho mshangaza Joji ni kwamba John Luke baada ya barua yake chini yake ameandika jina lake, kisha TripoliLibya, kisha akatuma email mpya kwa wote:

"Barua ya nane: Ninataka muujue Uislamu zaidi, na nategemea kusafiri kwenda Misri; kwa kadhia iliyojitokeza, na mwenye:

"Marejeo na anijulishe; ili kuujua Uislamu au kuijua Misri.

Mambo yanayotakiwa kujadiliwa au kuchambuliwa.

Majibu yanayo takiwa kuwasilishwa.

Nasubiri majibu yenu kwa muda wa siku mbili au tatu hivi, kisha nitachambua na kutuma kwenu muhtasari wake kama ilivyo ada yetu.

Ni mimi Joji."

www.path-2-happiness.com

WIZI

15 WIZI

WIZI

(1)

- Kakhi mimi nimejiandaa kwa safari..nataka ujue kuwa kadhia ni ya maadili na sio kadhia ya maslahi.
- Vizuri ..lakini nina sharti!
- Sharti ? sharti gani hilo?
- Watumie barua idarani kuhusu kughairi kwako kuacha kazi, na kuwa upo tayari kwa safari?
- Kwa nini?
- Ili umalize zogo ulilolianzisha.
- Vizuri, hakuna tatizo, lini safari?
- Katika muda wa karibu zaidi na kwa kadiri tiketi itakavyopatikana, lakini kwenda wapi?
- Tunakubaliana, nitasafiri kuelekea Misri.
- Unavyoonesha bado unatafuta njia bora ya maisha! Muda sio mrefu atakuja mkurugenzi wa mahusiano na tiketi ya safari, ili uende kwa furaha yako.
- Asante.

Joji aliondoka ofisini kwake, na hazikupita dakika kumi alifika mkurugenzi mkuu wa mahusiano…

Nimekukatia tiketi ya kuondoka kesho kutwa kwenda Misri, je ni sawa kwako?

Haraka yote ya nini?

Sijui, hayo ni matakwa ya Kakhi, kwa ujumla nimefurahishwa na taarifa, kwa vile wewe utaendelea kazi na sisi.

- Na nani aliyesema kinyume na hayo?
- Habari iliyoenea kwa nguvu kwa wafanyakazi ni kwamba Kakhi anataka kukuachisha kazi.
- Niliogopa, ama kwa sasa sijui kama kuna mtu mwingine ataachishwa, basi mimi ndie nitakaye muachisha yeye, asante kwa hisia zako.
- Na Kakhi akaniambia nikukumbuke kwa email.
- Amekuwa ananiogopa mimi, nitamtumia email anayotaka baada ya muda

www.path-2-happiness.com

mchache.

- Utatumiwa kabrasha zote pamoja na maelezo kwa email yako leo, kwani hazijatayarishwa bado, kwani tumeshtukizwa na taarifa.
- Nazisubiri… Nakushukuru.
- Wasia wangu kwako kama rafiki: kuwa makini sana na Kakh ama kwa upande wa kazi yangu mimi nimekufikishia, naomba idhini.
- Asante sana, niamini, kwamba misingi na maadili ya tabia zinashinda ujanja na hadaa.

Joji alishika simu yake na kuwasiliana na Adam ili kumjulisha safari yake..

- Hallo, nimeshakata tiketi ya kwenda nchini kwenu ewe Mmisri.
- Hongera sana, hii ni habari ya kufurahisha, nitamweleza Sheikh Baasim ili amwambie kaka yake akupokee, na ndugu yake anaongea Kiingereza na sio kama kaka yangu, lini safari?
- Kesho kutwa, inaonekana maudhui ni ya haraka zaidi kuliko nilivyotarajia.
- Je unaweza kuja kwangu leo, na mimi nipo peke yangu hospitalini.
- Ikiwa ni sawa kwako nitakuja baada ya muda mfupi ujao, naondoka sasa hivi.
- Sawa ….nakusubiri.

Joji alifika hospitalini na kuonana na Adam akiwa kitandani huku akisoma..

- Karibu, unaonekana umezama katika kusoma, unasoma nini?
- Nasoma kitabu cha Allah, “Qur’an”.
- Kwani hukuwahi kukisoma?
- Hapana, bali nimekisoma sana, ila napenda kukisoma kila siku.
- Kila siku? kwani hamchoki?
- Ndio, sisi tunakisoma kila siku, tunapendezwa nacho, kama ambavyo miujiza wa Issa juu yake amani ilikuwa ni ya kuponyesha vipofu na mbaranga na ukoma kwa idhini ya Allah, basi miujiza wa Mtume Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) ni hii Qur’an ya kudumu.
- Una maana gani kusema ya kudumu?
- Kwamba Allah ameahidi kuilinda, je hukusoma tafsiri yake: “Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.” (15:19) kwa kusoma tafsiri yake kweli unahisi muujiza wake?
- Kweli…natamani wakati nikisoma tafsiri yake kuwa ningekuwa nasoma asili yake na sio tafsiri yake, ijapokuwa mimi nasoma tafsiri yake ila najihisi inaniongelea mimi katika maudhui nyingi.

- Mimi najua maudhui nyingi zinazo kuongelea wewe.
- Umejuaje?
- Inabaki kumpwekesha Allah na majina yake, sifa zake, utukufu wake, na uzuri wake ni kubwa zaidi katika mambo yanayomtikisa binadamu yeyote, wala sihitaji kujua yasiyoonekana.
- Oh, ndio umesema kweli, kama ambavyo ukamilifu katika Uislamu upo katika kuchanganya baina ya dunia na akhera pamoja na kuwa mambo ya kiroho ni ya kipekee kabisa na ni katika vitu ambavyo nashangazwa navyo sana.
- Uislamu unayafanya maisha ya mwanadamu yawe kamili, hakuna utawa wala kujiweka mbali na Allah, bali uhai wote ni kwa ajili ya ibada pale utakapo kuwa na nia nzuri.
- La msingi ni kuwa mimi kesho nasafiri kwenda Cairo, unaniusia nini?
- Haahaa kunywa maji ya mto Nile.
- Je katika Uislamu kunywa maji ya Mto Nile ni ibada?
- Haa haa, nilikuwa nakutania tu, katika imani zetu Wamisri ni kwamba mwenye kunywa maji hayo ni lazima arudi tena; ni kwa ajili ya uzuri wa nchi na watu wake pia.
- Inavyoonekana Misri ni nchi unayoipenda zaidi!
- Bila shaka, mimi naipenda Misri sana tu, na mara ngapi napenda kurudi huko, ila napenda Makkah na Madina zaidi.
- Jambo la kushangaza zaidi! kwa nini?
- Ni miji ya kipenzi changu Mtume Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam)
- Je mnamuhesabu Mtume wenu kuwa ni mkombozi wenu, kama sisi tunavyomuhesabu Issa?
- Fikra ya uokovu haiendani na wazo la Uislamu katu, Issa ni Nabii na Mtume Muhammad ni Nabii na Mtume, na wote hao katika imani ni sawa bila kutofautisha yeyote, na sisi tunaamini Mitume wote, na mwenye kuwatia makosa au kuwapunguza katika shani yao kwetu, atakuwa amekufuru.
- Hata kama ataukashifu utu wa Musa Nabii wa Mayahudi au Issa Nabii wa Manaswara?
- Ndio, je hukusoma katika Quran tamko lake Allah katika Surat Baqarah Aya.
- “…hatutafautishi baina ya yeyote katika hao,...” (2:136)
- Nimesoma… na hiki ndicho kitu kilichonivuta katika Qur’an, nyinyi mnawaheshimu sana Mitume: Musa, Issa, Luti na Adam kuliko wafuasi wao,

www.path-2-happiness.com

umenikumbusha mambo mawili: Kitabu ambacho alipewa Katarina na Mmisri. “Mapenzi yangu makubwa kwa Issa ndio yaliyoniingiza katika Uislamu.” cha mwandishi Mvenezuela, na umenikumbusha Mitume katika Agano la Kale.

- Mitume wote walikuja kumpwekesha Allah na kumwabudu yeye pekee, lakini wachafuzi wameingiza ushirikina katika dini.
- Samahani, huwezi kutufundisha kuhusu dini yetu, na huwezi kuwa mjuzi wakujua Uyahudi kuliko Wayahudi wenyewe wala Ukristo kuliko Wakristo.
- Umesema kweli huenda Wayahudi wanaijua dini yao kuliko mimi kwa sasa na Wakristo ni hivyo hivyo, lakini ni kitu kisichowezekana kiakili na kisheria kuwepo Mungu mwingine!
- Kivipi?
- Ama kiakili: Allah ametaja kwa ushahidi wa kiakili katika Surat Ambiyai Aya ya 22 “Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana ‘Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A’rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.” (21:22). Na kungekuwa na waendesha dunia wawili au waungu wawili au zaidi ya hivyo, basi kungekuwa na dosari katika kuratibu na hivyo kuharibu misingi yake. Wangekuwa wanapingana, kwa mfano mmoja angetaka kupanga kitu, mwingine akakataa na akataka kinyume chake, kwa hiyo haiwezekani wote kuwa kitu kimoja, na pia haiwezekani mmoja kutaka kufanya jambo bila ya ridhaa ya mwingine na itakuwa ni kushindwa kwa mwingine na kutoweza, pia haitowezekana kwa wao wawili kuafikiana katika jambo, kwa hivyo mwenye nguvu ya kutaka kufanya mambo pekee bila kizuizi ni Allah pekee mwenye nguvu. Na Allah ameliweka wazi katika Surat AlMuuminuuna aya 91: “Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu.” (23:91)
- Falsafa ya kimantiki nzuri! Ijapokuwa inatofautiana na Ukristo na kupingana nayo kwa ujumla!
- Sio falsafa bali ni katika uchaji mungu, wala haipingani na Ukristo bali inapingana na ushirikina na upagani, kwani Nabii Issa alikuja kumpwekesha Allah (Subhaanahu wa Ta’ala), acha nikuulize kama alivyouliza Nabii Yusuph kuwauliza wale rafiki zake wawili pale walipo kuwa jela, kama alivyosema Allah

katika Surat Yusuf ayah No. 3940, “…Je, mabwana wengi wanao farikiana wao kwa wao ni bora au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu? Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini Iliyo nyooka. Lakini watu wengi hawajui.” (12:3940) kipi bora kati ya waungu wengi au mungu mmoja?

- Lakini vipi unasema, Allah hajalitolea dalili? Na katika Agano Jipya imejaa kutaja Uungu wa Issa!
- Ijapokuwa swali lako limesimamia upande mmoja, ila tukamilishe mjadala wetu, wewe unafahamu sana kuliko mimi, ni kwamba Agano Jipya limejaa upotoshaji na unafahamu baadhi ya nakala za Agano Jipya zimetaja kumpwekesha Allah na wala sijui ni kwa nini kuwe na Waungu wawili, hata kiakili tu, na huenda wakazozana au kuhitalifiana na kusababisha kuharibika kwa mbingu na ardhi. Kama anavyosema Allah katika Qur’an Surat Anbiyaa: “Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana ‘Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A’rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.” (19:22) au tofauti zao kama alivyobainisha katika Surat ya Muuminuuna aya 91: “Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu.” (23:91)
- Haya ni maudhui marefu sana, ni mara ngapi nachukia masanamu na picha ndani ya kanisa Katoliki, na nadhani hiyo ni aina ya ibada ya vitu ambavyo umenitajia kwa wale wanaoabudu masanamu, lakini sijaja kwa mjadala huu!
- Hakuna kitu kizuri chenye kupendwa ndani ya Uislamu kama kumpwekesha Allah, utulivu wake na wema wake pamoja na amani.
- Wema wake! Utulivu! Na Amani!
- Ndio, ushirikina unaufanya moyo kuwa na dhiki na kuparaganyika, hivi hukusoma tafsiri katika kauli ya Allah katika Suurat At An’ami aya ya 82, “Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka.”
- Na katika Surat ArRa’ad aya ya 28;
- “Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

www.path2-happiness.com

Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!" (13:28)

- Na katika Surat Twaha aya ya 124:
- "Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu." (20:124). Najua kwamba wewe hukuja kwa hili! Kwa hiyo nisamehe, na huenda nimerefusha maongezi, lakini wewe ndio uliyeniuliza.
- Kabla haujafunga maudhui haya naomba kukuuliza swali ambalo lipo kichwani mwangu sana na wakati nasoma Qur'an, imetaja mwishoni mwa aya katika Qur'an kitisho cha Allah cha kuwafufua baadhi ya watu wakiwa vipofu! Je hii siyo mapenzi ya kuadhibu kutoka kwa Allah?
- Ametakasika Allah na yote hayo, Qur'an imejaa sifa nzuri za Allah (mwenye kutakasika na kutukuka). Allah ni mkarimu, mwenye huruma na rehema, msamehevu, mtoaji na mwenye shukrani…mpaka mwisho wa uzuri wa majina yake, kama ambavyo anasifa za nguvu na uwezo, na katika Surat Rahmaan aya ya 78: "Limetukuka jina la Mola wako Mlezi Mwenye utukufu na ukarimu." (55:78)
- Huenda hayo yamekuja katika mawazo yangu ni kwa sababu ya kukuta katika Agano la Kale wasia wa kuuwa, kupora na kutumia nguvu.
- Ndio, hiyo ndio sababu, ninaongoza sababu zingine, kwani Wakristo wamezoea fikra ya utakaso, ya kwamba hakuna moto utakaokuwepo siku ya kiyama, ila kwa fukara au maskini asiyeweza kulipa kiasi fulani kwa ajili ya ukombozi au usamehevu.
- Umeanza hujuma; hatuna sisi Waprotestanti mkataba wa kusamehe, kama walivyo Wakatoliki na Waorthodoksi, ijapokuwa wazo la kutakaswa lipo kwetu sote.
- Kama ulivyosema.. wazo la imani ya utakaso katika utekelezaji wake inapelekea kuwa watu wote watapona kwa uokovu na utakaso wa Masiya juu yake amani; kitu ambacho kinafanya Siku ya kiyama kutokuwa na faida wala maana, kama ambavyo matendo ya ibada ni sawa kwa mwenye kufanya na asiyefanya kwa sababu wote hao wametakaswa na Masiya. Je huoni hicho ni kichocheo na kihamasishi cha kutomtii Mungu na kutenda matendo yasiyokuwa na tija?
- Huenda, na kwa mnasaba wa maadili, umenikumbusha Kakhi na mambo ya kazini, kesho kutwa ni safari kwenda kwenu Cairo, je kuna mipango gani iliyopendekezwa?
- Nataraji atawasili sasa hivi Sheikh Baasim kwani nimewasiliana nae baada yako na kumuelezea na amesema atakuja baada ya saa moja hivi na nadhani

yupo karibu kufika, ndugu yake ndio atakuwa mwenyeji wako huko, na anataka akusikie wewe kwa kile unachohitaji huko kabla ya kusafiri kwako, tupo tayari kukuhudumia kwa hilo.

- Haa…haa, kwa nini?
- Sijakufahamu!
- Kwa nini mnitumikie mimi? Nini mnapata kwa huduma yenu kwangu?! Samahani kwa swali hilo lakini linanijia mara nyingi.
- Wewe ni rafiki yangu ndio maana nakutumikia na Sheikh Baasim anakutumikia kwa niaba yangu, kwani wewe ni rafiki yangu, na pia kuna sababu nyingine napenda kuificha.
- Samahani, unaweza kunitajia sababu nyingine?
- Kwa kweli…mimi na yeye tuna matarajio kwamba huenda wewe ukasilimu, na katika dini yetu ukimfikisha mtu katika imani ya kweli ya Allah ni katika bora ya kujikurubisha kwake.
- Samahani Adam, japo una juhudi kubwa, nadhani sitasilimu katu, kwa hivyo nashauri msipate tabu sana ya nafsi zenu, na katika kunifahamisha juu ya Uislamu au kunitumikia mimi
- Usituhofie sana sisi, ujira au malipo tunayapata kwa zile juhudi tu hata kama hujasilimu na utumishi ninaoutoa kwako ni sadaka na una ujira kwa Allah pia, na kuwatumikia watu na kuwasaidia ni katika mambo bora ya kujikurubisha kwa Allah, na mimi nina imani ya kwamba pamoja na hayo mwenye kutakiwa kheri na Allah basi humkunjulia kifua chake katika Uislamu na mimi nina matumaini makubwa utasilimu kwani wewe ni mtu mwenye akili na kutumia mantiki.
- Huenda, lakini sidhani, naomba lisikukere hilo, lakini kwa nini umebadilika lahaja yako na ya mwanzo?
- Unakusudia nini?
- Hukuwahi kuniambia chochote kuhusu dini yako wala Qur'an, na kwa sasa muda wako mwingi unaongelea hivyo, je ulikuwa una nidhihaki na kunitania?
- Nilikuwa na imani ya kwamba utakuja katika Uislamu na utaacha dini zote, na wewe umepita katika njia inayokuongoza katika Uislamu, kwa nini nikukatishe njia hiyo? Na sijabadili fikra yangu ila katika kipindi kimoja!
- Lini?
- Pale ulipokuwa mgonjwa kabla huja fanyiwa operesheni.
- Kwa nini?

www.path-2-happiness.com

- Nilihofia utakufa kwa kweli, kwani mimi napenda rafiki yangu awe na mimi peponi…huyu Sheikh Baasim amefika, karibu Sheikh.
- Assalaam Alaykum Warahmatullah Wabarakaatuh.
- Waalaykum Salamu Warahmatullah Wabarakaatuh.

Joji kwa mshangao!

- Karibu, nini unakusudia kwa maneno yenu?
- Hiyo ni salamu yetu sisi Waislamu, pia ni dua akhera, una muomba Allah amsalimishe na mabalaa yasiyoonekana na yanayoonekana, na usalama wa hisia ni usalama wa mwili, utu na mali, na usalama wa ndani (wa kimaana) ni usalama wa dini dhidi ya maangamizo, kisha ni dua ya rehema na baraka, kwani dini yetu ni dini ya amani na rehema.
- Kwa mara nyingine mtanirudisha katika mjadala juu ya dini! Mimi kesho kutwa nasafari, je ni zipi taratibu zinazotakiwa?
- Unachokitaka, ndugu yangu yupo huko, anaweza kukuandalia kile unachotaka.
- Sijajua kinachotakiwa kufanywa huko mpaka muda huu, nataraji atanitumia email, lakini mimi baada ya kufikiri, natamani kutembelea na kuona vitu mimi mwenyewe ukiacha kazi, mnaweza kuniandalia sehemu na mambo mengine.
- Unataka kutembelea nini?
- Nataka kutembelea pyramids, kanisa la Waorthodox, kukutana na makasisi wao, pia nataka kuonana na baadhi ya wanachuoni wa Kiislamu.
- Yote uliyoyataja ni rahisi sana, na atakuandalia kaka yangu, tayari nimeshamwambia na ameshakuandalia baadhi ya mapendekezo, lakini muamuzi ni wewe, ishi na watu wa kawaida na uwasikilizie wao.
- Vizuri na ni muhimu, lakini mizunguko yote hii ya kitalii itanigharimu kiasi gani?
- Sisi sio shirika la kitalii, wewe mwenyewe utalipa gharama za utalii, ama kuhusu ndugu yangu hiyo ni takrima kwa mgeni na ni katika ibada alizoamrishwa Muislamu.
- Waislamu wote wako hivi?
- Haa haa, hapana.

Adamu alijinyoosha na kukaa sawa sawa na kusema kwa mzaha:

- Kuwa muangalifu na wezi na vibaka, wana mazingaombwe na wadanganyifu, na wengineo katika jamii, hutapata jamii yenye kufanana katika maisha haya, mji mwema na wenye watu wazuri pekee.
- Je Uislamu hauwaiti watu kunako tabia nzuri?

- Bali Mtume aliletwa kwa ajili ya kuendeleza hizo tabia nzuri kama anavyosema (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) “Hakika nimeletwa ili kukamilisha na kuendeleza tabia nzuri.” Na kwa kadiri Waislamu wanavyoshikamana na Uislamu ndivyo wanavyoshikamana na tabia nzuri, na tabia nzuri zilikuwepo hata kabla ya Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) na yeye kuja kuzikamilisha, la muhimu kuwa makini, na kwa bahati mbaya miji yetu ni dhaifu kiuchumi na kimfumo

Baasimu alimpa kitambulisho…

- Chukua kitambulisho hiki chenye maelezo ya kaka yangu kwa ukamilifu na atakusubiria airport pale tu utakapo mtumia email au kumpigia na kumpatia muda maalum, usiogope kitu, ndugu yangu anaongea Kiingereza.
- Niliongea na ndugu yangu muda sio mrefu pia, ili akukaribishe nyumbani kwetu, ila yeye haongei Kiingereza, kwa hivyo hatafaa kuwa mwenyeji wako.
- Nawashukuru sana na nalazimika kuondoka kwa sababu nimechelewa na nategemea kwa kesho muda mwingi nitakuwa kwenye shirika ili kukamilisha baadhi ya maandalizi ya safari na kuna baadhi ya mambo lazima niyakamilishe kwa leo hii, na tutawasiliana nanyi nikiwa Misri, nawashukuru sana.
- Misri inakusubiri, kwa heri ya amani.
- Nanyi kuweni katika amani ya Allah.

(2)

Joji alifungua email yake kuona kama ametumiwa utaratibu wa kina wa kazi akiwa Misri au bado, alikuta barua mbili ya kwanza imetoka kwa John Luke,

- “Mpendwa Joji:
- Mimi nastarehe sana Libya kuliko nilivyotarajia… ila kuna tatizo la usalama katika masiku haya, tatizo lingine ni hali ya hewa, lakini najisikia ni safari nzuri ya kitalii ijapokuwa kuna ukame wa jangwa.

Nitakupa habari hatua kwa hatua, ninatarajia utanipa habari zako pia mpaka tupate njia bora ya maisha.

Angalizo: Laiti ungenijulisha kuwa utakwenda Misri basi ningeifanya safari yangu kwenda huko badala ya Libya.

Ni mimi John Luke.”

Joji alimjibu:

“Mpendwa John Luke,

www.path-2-happiness.com

Samahani kwa kutokujulisha kuhusu safari yangu ya Misri, sikuwa natarajia bali haikuthibitishwa ila leo, nitakufahamisha juu ya safari yangu.

Angalizo: Sijakuelewa unakusudia nini unaposema ni safari nzuri ya kinafsi na roho?! Lakini mimi nahisi ina ukame wa kiroho.

Ni mimi Joji."

Halafu Joji alifungua barua ya Mkurugenzi Mkuu wa Mahusiano, na alisoma vipengele vinavyotakiwa huko Misri kwa mazingatio makubwa, kwa hiyo kazi ni ngumu sana, kwani amemtaka kufungua ofisi ya utaalamu wa ufundi na biashara huko Cairo ili iwe ni kituo cha uwakala katika mashariki ya kati yote. Ilibainika wazi kwamba Kakhi hakutaka arudi haraka na kwa hivyo akafanya haraka kumpangia kazi iliyokuwa ngumu isiyowezekana, na hivyo basi kuamua afanye jitahada ya leo na kesho kwa ajili tu ya kujiandaa kwa safari hii iliyokuwa ngumu ili afanikishe jukumu lake gumu kama ni changamoto kwa Kakhi.

Joji alianza kuwasiliana na mashirika ya kitaalumu ya kiufundi Misri na kuwajulisha kwamba atawasili baada ya siku mbili na anawahitaji baadhi ya wafanya kazi wawe tayari kumpokea kwa muda muwafaka, na kwa kupitia intaneti akaweka kabisa nafasi katika hoteli ya kifahari siku ya kwanza atakapofika, kisha ataangalia nyumba ya kuishi kwa msaada wa Jamali ambae ni ndugu wa Sheikh Baasim aliyekutana nae hospitalini wakati wa kumtembelea Adamu. Na alianza kutafiti katika mitandao ya kimataifa juu ya maelekezo na taarifa zitakazomsaidia kufanikisha safari yake kwa ufanisi, na kuandaa dondoo na vipengele mnasaba kwa ajili ya mkataba na kutafuta fursa za ufanisi.

Katarina aliingia na kumkuta Joji akiwa amezama katika kupitia vipengele vya kazi na majukumu yake, huku akijua yupo katika changamoto kubwa kutoka kwa Kakhi, na yeye Kakhi hatamwachia kuhusiana na jambo lake, lazima ajiandae vizuri kwa yatakayo kuja mbeleni.

- Ilikuwa ni siku ngumu, haya nipe habari njema, je unalo jipya?
- Nitasafiri kesho kutwa kwenda Misri.
- Kesho kutwa! haraka ya nini hiyo?
- Ni kwa ajili ya jukumu refu na gumu sana, huenda nilikosea nilipochagua kwenda Misri, au Kakhi alitaka kuniadhibu mimi kwa hili na kuharibu sifa yangu mbele ya bodi.

- Mimi nina imani utafaulu katika jukumu lako, japokuwa anakufanyia hivyo, Mungu yupo pamoja nawe.
- Katarina nakupenda sana, na nahofia safari yangu hii ikachukua zaidi ya mwezi, na katika nchi ya ugenini tofauti na nchi yetu au ulimwengu wetu na lugha tofauti, dini tofauti, utamaduni tofauti na mfumo ulio tofauti pia.
- Huenda, ila nina imani kuwa utastarehe katika safari yako hiyo.
- Natamani hivyo, na Adam amenihakikishia kwamba nchi ni nzuri, inaonesha Adam anaipenda nchi yake sana.
- Kila watu wanapenda nchi zao!
- Sawa, lakini cha ajabu, yeye anapenda Makkah zaidi kuliko anavyoipenda Misri, kwa sababu Mtume wao anaipenda Makkah zaidi, ni utii gani na mapenzi gani haya? Je haikukumbushi mapenzi ya Ukristo kwa watawa?
- Kamwe, inanikumbusha mapenzi yetu juu ya Yesu, hata kama kuna tofauti.
- Tofauti katika nini?
- Sisi tuna muona Yesu katika nafasi ya Uungu, na wao wanamuona ni Mtume aliyetumwa, sisi mapenzi yetu kwa Yesu yanazingatiwa kwa kuwa yeye aliitoa nafsi yake kutukomboa, na wao wana mzingatia kama ni Mtume kutoka kwa Mungu na amewafundisha mambo mengi ya kheri.
- Kheri gani!
- Uislamu, wanaona kuwa ndio kila kheri ndani yake.
- Kila kheri!
- Wao wanaona hivyo, na wanatanguliza mtazamo wa Kiislamu katika kila nyanja ya maisha, wanasema imetoka kwa Mungu.
- Unakusudia nini kwa kauli yako "wanaona… wanasema?
- Waislamu.
- Umesema katika ujumbe wako wa mwisho wa email kuhusu Quran: "Inaelekea ni kutoka kwa Mungu", ujumbe wako ulinishtua sana kwa hali zote zile.
- Bali utafiti wangu juu ya swali lako kuhusu ukweli wa kuinasibisha Qur'an na Mungu ndilo ulionishitua, na bila ya shaka hichi wanachokisoma Waarabu ndicho alichokuja nacho Muhammad bila ya badiliko la aina yoyote, lakini bado swali lipo pale pale, je Muhammad ni mkweli au siyo?
- Nilichofahamu katika ujumbe wako ulituonesha ni kuwa Muhammad ni mkweli na kwa hivyo ndio nikasema: Inaonekana ni kutoka kwa Mungu.
- Hapana, sikuwa na kusudia hivyo, nilichokuwa na kusudia ni kwamba sio kama

www.path-2-happiness.com

Agano la Kale na Jipya, kwani kuna nakala zenye kupingana tofauti tofauti.

- Ijapokuwa mjadala ni mzuri, mimi nalazimika kuukatisha, nina kazi nyingi za kuandaa kabla ya safari, kwa mnasaba wako wapi watoto?
- Wamekwenda ziara ya kishule, nilikufahamisha jana au umesahau! Nataraji wafike baada ya muda mchache na chakula kiwe tayari ijapokuwa kimechelewa sana.
- Oh kwa hakika nimejisahau, na mimi nina njaa sana, asante mpenzi wangu, naomba ruhusa nikamilishe kazi yangu mpaka chakula kitakapokuwa tayari.

(3)

Joji alimuaga Katarina na watoto wake na kwenda uwanja wa ndege… alifika Cairo Saa kumi na mbili jioni, alimaliza kukaguliwa nakutoa mikoba yake na kuelekea katika ukumbi wa mapokezi na kumkuta mtu amebeba bango lililoandikwa jina lake: Joji Nesson, kwa maandishi makubwa, inaonesha mwenyeji wake hakifahamu Kiingereza vizuri, alimuelekea na kumuashiria, alitabasamu, na alimwita yule rafiki yake aliyekuja kumpokea Joji…

- Karibu, karibu sana Misri, mimi ni ndugu wa Baasim (Jamali) na huyu ni ndugu wa Adam (Muhammad) hakifahamu Kiingereza vizuri, hata hivyo alijitahidi sana kukukaribisha.
- Nakushukuruni sana.. na tuondoke kuelekea hoteli ya uwanja wa ndege, kwa sababu nimeshapanga chumba hapo.
- Jambo linarudi kwako tu wewe, lakini hoteli ipo mbali na mji, na Cairo ina msongamano sana, kama ambavyo ni ghali sana.
- Hamna neno tutabadilisha kesho, kwani nimekodi kwa siku moja tu ila nina mategemeo ya kuhamia katika hoteli nzuri iliyo karibu na katikati ya mji, na karibu na mashirika makubwa ya nchi.
- Kuna hoteli nyingi katikati ya mji, na kesho utachagua hoteli unayoitaka.
- Napendekeza unichagulie wewe kesho na uniwekee nafasi, ikinipendeza nitaendelea nayo, kwani nina kazi nyingi sana.
- Kama utakavyo…mimi nitajitahidi kukuhudumia, kwani hujui thamani aliyokupa Baasim.
- Jambo la kushangaza Baasim kunijali kiasi hiki!
- Kuna sababu nyingi kwa hilo “Kwani wewe ni mgeni wetu, na Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) ametuamrisha kumkirimu mgeni, na wewe unafanya

utafiti kuhusu Uislamu na sisi ni wajibu wetu kukufahamisha juu ya Uislamu na wewe ni rafiki wa ndugu yangu, na Mungu ametuamrisha kutekeleza ahadi.

- Kwanza: Kwa nini kila mnaposema jambo, lazima mumtaje Muhammad? Pili: Nani kakueleza kwamba mimi natafiti kuhusu Uislamu?
- Jibu la kwanza ni kwamba: Mtume ni kipenzi chetu na kiongozi wetu au kiigizo chetu. Pili: Baasim ameniambia kwamba wewe unatafuta furaha.
- Ni kuhusu furaha na sio Uislamu
- Sijui tofauti kati yao, kwani bila furaha hakuna Uislamu na kama sio hivyo basi nyinyi huko Magharibi mngekuwa na furaha zaidi, wala hakuna siri, kwa mfano: taifa la Sweden ambalo kuna wapinga dini na wasio kuwa na dini karibu asilimia 80% na ndio taifa kubwa linaongoza kwa kujiua duniani, ijapokuwa ni taifa linalosifika kwa maendeleo, je haikuwa mauaji ni kilele cha huzuni na kutaabika?
- Je, kwani Waislamu hawajiui vile vile?
- Kwa masikitiko ndio! Lakini wao ni wachache sana wanaojiua na kuna tofauti kubwa, katika utafiti kwa kisomi uliofanywa na Dr Gose Manuel na mtafiti Alesandar Felishman uliokusanya maeneo mbali mbali, ambapo walitegemea marejeo ya umoja wa mataifa kuhusu uhusiano wa dini ya mtu na kujiua wakakuta kuwa wasiokuwa na dini ndio watu wengi zaidi wanaojiua, na asilimia yao inakaribia 25% ya wenye kujiua, kisha wanafuatiwa na Mabudha halafu Wakristo, kisha Wahindu, mwisho wanafuatia Waislamu kwa asilimia ndogo kama moja hivi tu, halafu watafiti hao wakasema kwa sauti moja kwamba: Idadi ya wenye kujiua katika nchi za Kiislamu kulinganisha na mataifa mengine ni ndogo; inakaribia Sifuri, kwa sababu dini ya Uislamu imeharamisha na kukemea vikali kujiua.
- Je Uislamu unaharimisha kujiua?
- Bila shaka, bali unaharamisha kila kinacholeta madhara kwa binadamu, na kwa mshangao Mtume ametaja kupitia andiko lake zaidi ya asilimia 90% ya aina za kujiua kwa mujibu wa takwimu pale aliposema: “Mwenye kujiua mwenyewe kwa chombo cha chuma, basi chombo hicho cha chuma atakuwa nacho mkononi na kuchomwa katika tumbo lake na atakaa motoni muda mrefu sana, na mwenye kunywa sumu na kujiua atakaa motoni milele, na mwenye kujitupa juu ya jabali na akafa basi naye atatupwa katika moto wa Jahannamu na atakaa humo milele”.
- Inaonesha kwamba umeathirika sana na taaluma yako, unapenda sana kutumia namba!

www.path-2-happiness.com

- Asante kwa kunisifia, kweli taaluma yangu ni elimu ya hesabu kama alivyo kueleza ndugu yangu, na mahesabu ya akili yanaongeza katika mantiki ya akili bila shaka, lakini nimejifunza njia za elimu kupitia dini yangu kwanza.
- Kila kitu ni kutoka kwenye dini yenu na Mtume wenu! Nyinyi mmezidi sana!
- Huenda, ila huoni kuwa mfumo wa kisomi unataka uoneshe ninapozidisha, sio kunituhumu tu kuwa tunazidisha bila ya uthibitisho
- Umenishinda! Vipi dini yenu inahimiza juu ya mfumo wa kisomi na kielimu katika kulishughulikia jambo?
- Angalia baadhi ya misingi na dalili za Kiislamu zenye kufungamana na njia za kielimu, mfano Uislamu umetahadharisha kuiga bila kutumia akili. Allah anawaambia washirikina katika surat AlBaqarah ya kwamba: "…wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka? " (2:170)
- Na kufuata dhana bila ya kufuata mfumo wa kielimu;
- "…Hawa hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu." (6:116)
- Na kufuata matamanio ambayo yamo kinyume na mfumo wa kielimu, mantiki, akili na utafiti;
- "…Na hakika wengi wanapoteza kwa matamanio yao bila ya kuwa na ilimu…." (6:119)
- Na bughudha na chuki ambayo inamuweka mtu mbali na uadilifu;
- "…Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda." (4:8)
- Na kutumia maudhui ya kielimu bila kuegemea upande wowote katika elimu kama Allah alivyosema kuhusu Mayahudi;
- "Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahala pake, na husema: Tumesikia na tumeasi…." (4:46)
- Na katika kutodhulumu na kutengana, ambapo tunasoma katika Surat Shuurah Ayah ya 42;
- "Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki….. " (42:42)
- Na kuhusu uaminifu wa kielimu pamoja na uadilifu na watu, tunasoma katika Surat Nisaa:

- "…Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu..." (4:58)
- Na kuhusu uadilifu, unyoofu na ushahidi wa kweli katika Ayah ya 135 katika sura ya nne;
- "Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu..." (4:135)
- Na kuhusu umuhimu wa utafiti na kutumia hoja na matumizi ya dalili tunasoma katika Surat AnNamli Aya ya 64 na zingine pia:
- "Au nani anaye uanzisha uumbaji, kisha akaurejesha? Na nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli. " (27:64) na…
- Nimetosheka, basi inatosha, je wewe ni mtu wa dini kama kaka yako?
- Mimi na ndugu yangu sio masheikh kwa mtazamo wa kanisa, kaka yangu amebobea elimu ya Kiislamu na mimi mahesabu…kwa nyongeza, wewe umealikwa katika chakula cha usiku nyumbani kwa Muhammad ndugu yake Adam… anauliza je unapenda vyakula vya kimisri au vyakula vya haraka haraka (fast food)?
- Vyakula vyepesi vya Kimisri.
- Tuna chakula kiitwacho (Koshari) je utakula au hapana?
- Koshari! Siijui hebu nijaribu.
- Koshari ni mchanganyiko wa makaroni pamoja na wali na vitunguu na nyanya na vitu vingine, kwa ujumla ni chakula kizuri sana, na cha kimisri haswa, utakipenda, na hii ndio sehemu wauzayo Koshari maarufu na ya kipekee.
- Muhammad hakupendezwa na chaguo la Jamali, alimwambia Jamali: Je inaingia akilini tumkaribishe mgeni wetu Koshari, haiendani na adabu za kumkaribisha mgeni.
- Hapana ewe Muhammad, haya ndiyo matakwa yake…ewe Joji, Muhammad haridhiki wewe kula katika hoteli za bei rahisi, anataka ukale katika hoteli kubwa, nini rai yako?
- Nashukuru sana, ila mwambie hayo ndio matakwa yangu na napenda sana hivyo.
- Unaona kama nilivyo kueleza!
- Ewe Jamali mwambie kuwa sisi tutafuata matakwa yake, lakini pamoja na masikitiko makubwa, sisi tumezoea kuwakirimu wageni wetu na hivi ndivyo tulivyozoea na ndivyo ilivyo dini yetu.
- Kila kitu kwenu kinatokana na Uislamu na Muhammad, inaelekea kuwa nyinyi Waislamu ni wafuasi sana wa dini kuliko sisi Wakristo.

www.path-2-happiness.com

- Ki vipi? Sijafahamu?
- Sisi tunatosheka kusali siku moja katika wiki, yaani Jumapili tu, ninyi mnasali kila siku zaidi ya mara moja, nyinyi mnapendezwa na mnajali sana dini yenu na Mtume wenu. Sisi hatuwatukuzi hata Mitume wetu, nyinyi mnaiona dini kuwa ndio dira ya maisha yenu yote na sisi tuna muono kuwa ni mafungamano ya kiroho tu.
- Je kusema huko ni kwa kutusifia au kutukosoa?
- Haa haa, ni sifa tu, kwani nyinyi mnalipuka na kukasirika kwa hasira kali kwa yule anayedharau matukufu yenu, inatosha kwa mfano walioyafanya Waafaghanstani pale msahafu wao ulipo dharauliwa na kuchomwa na Wamerekani!
- Na ambae hajali matukufu yake na kuwaheshimu Mitume, hastahiki kitu, je hamkuwa nyinyi mnawaheshimu Malkia wenu? Hawakuwa Wamarekani wanawasheshimu viongozi wao waasisi wa taifa lao? Je hawakuwa Warusi wanamuheshimu Marx na Lenin? Na Wajerumani Nazi kwa Hitler? Na wengineo wengi? Na sisi tunawaheshimu Mitume wote, bali tunamuheshimu Yesu sana kushinda hata Wakristo wanavyo muheshimu na tunampenda sana kuliko mumpendavyo, na wala hatumuweki zaidi ya ile daraja yake aliyopewa, kwani yeye ni mja wa Allah na Mtume wake.
- Ndio, sahihi, ila nyinyi mnazidisha!
- Kuzidisha ingekuwa ni sawa laiti tungesema Muhammad ni Mungu kama mlivyosema nyinyi!
- Nakusudia mnazidisha kwa kule kufungamanisha maisha na dini.
- Ama kwa mnasaba wa mahusiano ya dini na maisha, naamini mwenye muono wa mafungamano kati ya mja na Mola wake kuwa ni mafungamano tu ya kiroho ya muda kwenye swala tu, halafu maisha yote yanabakia bila Mola, mtu huyo atakuwa hajafahamu maana ya maisha wala dini wala Mungu, samahani mtu huyo atabaki kuwa katika huzuni, msongo wa mawazo kiasi cha kumfikisha mpaka kujiua kama tulivyozungumza hapo kabla, hakuna maisha wala dini au Mungu kama hakuna mafungamano endelevu kati ya vitu hivyo.

Walingia mgahawani na kuletewa koshari, walikaa katika meza ndogo na Joji akionesha mshangao kwa jinsi mgahawa ulivyo sheheni watu huku wahudumu wakifanya kazi kwa bidii na kujaribu kuitikia oda kwa haraka zaidi…waliagiza koshari tatu haikupita dakika mpaka mhudumu alipowasilisha maombi yao…..

- Mtaje Allah ewe muheshimiwa, Koshari imefika.

- Mhudumu anasema nini?
- Ananikumbusha kumtaja Allah kabla ya kula.
- Kwa nini?
- Ili kukamilisha maongezi yetu yaliyo tangulia, ni lazima Muislamu maisha yake yote yawe kwa ajili ya Allah, Muislamu anataja jina la Allah kabla ya kula, kwa maana ya kwamba naanza kitendo hiki kwa msaada wa Allah (Bismillah) kwa kutaka baraka kutoka kwake.
- Vizuri !
- Uislamu haujaacha mambo hivi hivi tu isipokuwa kuwa hukumu yake kama anavyosema Allah katika Surat An'aam aya ya 38; "Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anaye ruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa." (6:38)
- Kila kitu!
- Haa haa, umenikumbusha kisa kilichotokea wakati wa Mtume alipomuijia asiekuwa Muislamu, na kuwaambia masahaba wake kwa dharau: Mtume wenu amekufundisheni mpaka kwenda haja kubwa! Wakamjibu ndio, hakika ametukataza kunawa kwa mkono wa kulia, na katukataza kutumia kinyesi na mifupa katika kuondoshea uchafu, na akatuambia: Mmoja wenu asiondoshe uchafu bila kuwa na mawe matatu.
- Na je aliyoyasema swahaba wa Mtume wenu ni sahihi? Au ni hoja na mjadala tu kwa asiyekuwa Muislamu, je katika Uislamu kuna maelezo kuhusiana na adabu au tabia?
- Ndio ni sahihi, na kuwa Allah amekamilisha dini kwa kusema katika Surat Maidah aya ya 3;
- "Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini..." (5:3)
- Na Mtume ameletwa ili kukamilisha matendo mema.
- Kwa nini mnadhani kwamba nyinyi ndio mnamiliki tabia nzuri peke yenu?
- Labda hujanielewa niliposema muda sio mrefu, pale aliposema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): "Hakika nimetumwa kukamilisha tabia nzuri." Hiyo inamaanisha amekuja kukamilisha, maana yake ni kwamba: Tabia nzuri zipo kwa watu, na Mtume ndie atakae kamilisha na kutimiliza na hii ndio sehemu nzuri ya Uislamu pekee.

www.path-2-happiness.com

- Unakusudia nini?
- Ninakusudia kuwa Uislamu ndio utakamilisha na kuhitimisha tabia nzuri na dini na sheria, na Mtume ndio mkamilishaji wa ujumbe au utume tangu Adam, Musa, na Yesu amani ya Allah iwe juu yao. Na tabia katika Uislamu sio kitu kilichowekwa pembeni, bali ni kadhia ya msingi katika dini yetu.
- Na je (Koshari) ina asili katika dini yenu?
- Haa haa, ni chakula cha asili cha Misri, na sio katika Uislamu, ni chakula cha maskini na matajiri pia.
- Koshari ni tamu.
- Kwa pongezi na heshima zimuendee mwenyeji wetu mkimya; kwani Muhammad hajui Kiingereza vizuri.
- Namshukuru sana Muhammad, na mweleze kuwa chakula nilichokula ni chakula bora zaidi.
- Na imesalia Mahalabiya kwa maziwa ambayo nimekwishaiagiza.
- Muhammad anakuambia kuwa bado Mahalabiya kwa maziwa nayo aina ya kitu kitamu cha kienyeji cha Kimisri.

Baada ya kumaliza kula waliondoka kwenda hoteli ya uwanja wa ndege na kuchukua chumba, na walipo maliza Jamali alimwambia Joji atamtembelea kesho asubuhi…

Joji aliingia ndani na kupanga mambo yake na kuoga haraka halafu akafungua email yake na kukuta marafiki wake wamemjibu…alizisoma nakuwarushia majibu…

"Kwa hakika majibu yenu yalikuwa ni yenye kushtukiza, lakini yalikuwa yenye faida kwangu mimi kama ifuatavyo:

Habib: Siupendi Uislamu ijapokuwa mengi yaliyosemwa yana ushahidi wa kielimu, na kukusisitiza kulitembelea kanisa la Orthodoksi.

Levi: Unapo ujadili Uislamu hapana budi kuujadili kwa kuzingatia unyama wao, siasa kali na ugaidi, ujinga, na ufisadi.

Katarina: Sijui kuna siri gani kinachonivutia katika dini hii! Huenda ikawa ni vizuri kuhakikisha kama wao wanampenda Yesu pamoja na kumkirimu kwao mwanamke.

Adam: Marejeo bora ni kitabu cha Allah (Qur'an) na napendekeza asiesoma Qur'an na kujifunza asiusemee Uislamu.

John Luke: Uislamu ni mwepesi kiundani, na sijui kuna uchawi gani uliopo katika

fikra hizi, ni vizuri kusoma vitabu vilivyosifiwa na Wamagharibi juu ya Uislamu.

Na mimi Joji nitaongezea kwenu siri ngeni kuhusu Uislamu: Tawheed, upana wake, utulivu, mambo ya kiroho yaliyomo ndani yake, elimu, ugaidi, kuhusu mwanamke, marejeo, ukweli na Historia.

Narataji pendekezo la barua ifuatayo ni kuchambua mambo hayo niliyo yataja, nani atakae kuwa wa mwanzo kutupa habari?

Ni mimi Joji."

Na baada ya kuituma … alipata ujumbe kutoka kwa Levi:

Mpendwa Joji:

Ni matarajio yangu umefika salama Misri, na nahisi umeuelekea Uislamu kwa nguvu zote kuliko ulivyoudurusu Uyahudi na Ukristo mwanzo…kuwa makini na Waislamu, mimi na kuhofia kutokana na wao. Ni mimi Levi."

Joji alimjibu kwa kumwambia:

Mpendwa Levi;

Nakushukuru sana kwa kunikumbuka, nitakuwa na hadhari na nitakueleza moja baada ya jingine, ninaweza kuwa kama ulivyosema, lakini niamini sitaingia katika dini katu ila baada ya kujiridhisha kwa ukamilifu, na nitaomba ushauri wenu, nashukuru kwa pupa yako kwangu.

Ni mimi Joji."

Pia alikuta ujumbe wa Kakhi… na kufungua….

Mpendwa Joji,

nimependezwa kuwa kwako mbali na Shirika, na kukubali kwako kazi usioijua kabla ya kukubaliana nayo, natarajia utafaulu; kwani nimekupangia kila kitu, na ukifeli utabeba matokeo ya kufeli kwako, nasubiri mafanikio yako.

Ni mimi Kakhi ."

Saa moja asubuhi Joji alishuka kutoka chumbani mwake kwa ajili ya kupata chai hotelini, aliipenda hoteli kwa huduma zake mbali mbali kutokana na kuwepo kwa vyakula aina mbali mbali na vya kimisri, na akawa anaonja na kujua zaidi aina mbali mbali mpya za vyakula ambayo hajawahi kuvionja hapo kabla…

Mhudumu alimuuliza kwa Kiingereza dhaifu kama anahitaji kitu….!

- Asante sana
- Kutoka wapi ewe muheshimiwa.
- Mimi natoka Uingereza.

www.path-2-happiness.com

- Na wewe?
- Mimi ni Mmisri… kutoka Alexandria.
- Je unaweza kunihadithia kuhusu mji wa Alexandria?
- Alexandria ni katika miji mikubwa nchini Misri, ni mji mkongwe ulioasisiwa na Alexander The great Mmakdonia mwaka 332 B.C.

Joji alikumbuka kile alichokisoma kuhusiana na mji huu mkongwe wa Alexandria, ambapo Alexander alitaka uchukue jina lake, na uwe ni kituo cha biashara na utamaduni wakihelensia halafu zikafuatia zama na karne za ustaarabu mbali mbali na kuna kumbukumbu za kihistoria nyingi, kwa mfano minara ya Alexandria ambayo ni moja ya maajabu ya dunia ya zamani, na kuna Maktaba ya Alexandria iliyoingizwa na Ukristo kwa mkono wa Askofu Mtume Marcos, mwaka wa 45 (B.C.) na ilikuwa ni kituo cha kuendeleza Wakristo kielimu na ilikuwa na mchango pia wa falsafa, na ndio ilikuwa shule mashuhuri kwa falsafa, na ndipo palikpokuwa na shule ya Plato iliyoasisiwa, kama ambavyo kulikuwa na shule ya Alexandria ya kiungu ambayo ilijihusisha na maarifa na uungu wa Masiya duniani. Kisha akakumbuka mchango wake baada ya Uislamu ikawa ni ngome ya kielimu ya Alexandria na kwa hakika umekuwa ni kituo cha elimu ambayo wanapokea wanachuoni wa Kimagharibi na Andalusi elimu zao za dini kabla ya kurudi katika nchi zao…

Mhudumu alimkatisha:

- Inaonesha fikra zako ziko mbali na mimi, naondoka…..

Joji alizinduka kutokana na mawazo yake kuwa mbali na kusema:

- Nilikuwa katika mawazo ya kukumbuka historia ya mji wa Alexandria wenye historia kongwe.
- Sijakamilisha utafiti wangu niliokuwa naandika, lakini naipenda Misri na hasa Alexandria, kwani ni mji wa zamani bila shaka, je umewahi kuutembelea ewe bwana wangu?
- Umenivutia na kuniingizia hamu kuutembelea, je wewe ni Muislamu?
- Hapana, mimi Mkristo…..
- Vipi mahusiano kati ya Waislamu na Wakristo? Ni vipi Uislamu, uliingia Misri?
- Vita vilitokea baina ya Waislamu na Byzantium na Wakoptic wa Misri walikuwa bega kwa bega na Waislamu kupigana.
- Wakoptic Wakristo?
- Wakoptic ndio wenye asili ya Misri na haimaanishi wote ni Wakristo…na

walipoukomboa Waislamu mji wa Alexandria watu wake walistarehe kwa uhuru wa dini, na waliwalinda vizazi vya kiyahudi waliokuwepo humo na bila kudhuriwa katu na hata Makanisa yalisalimika.

- Na kwa nini basi hujasilimu kama ulifurahishwa na Waislamu?
- Mimi nimezaliwa hivi, na kwa nini nibadilishe dini yangu na dini ya baba zangu na babu zangu? Je wewe unaweza kubadili dini yako?
- Huenda…nini kinazuia, kama itanikinaishi kwa dalili, na kukinai kwa dalili ndilo jambo la msingi.
- Ama kwa upande wangu sipendi kubadili, na wala sipendi masharti magumu ya Uislamu.
- Masharti ya Uislamu ni magumu?
- Swala tano kila siku, zaka ya mali, kufunga saumu ya Ramadhani, kuhiji Makkah, usisema uongo; usiibe, usisengenye, usizini na mengineyo kama hayo.
- Lakini wao wanastarehe kwa hilo, na wanahesabu ni katika kilele cha maisha bora na ya furaha.
- Huenda wao wanastarehe, lakini mimi hapana, naomba samahani kwa kurefusha maongezi mimi na wewe.
- Hapana mimi nimeshamaliza kula, nakushukuru kwa muda wako.

Joji alipanda chumbani na kukusanya begi lake; kujiandaa kwenda hoteli nyingine, alimuomba mbeba mabegi kushusha chini mabegi yake, kisha akateremka kumsubiri Jamali mapokezi, alipomaliza tu maandalizi ya kutoka, Jamali alifika kumsindikiza…

- Unaonekana upo tayari na mwenye hamasa ya kazi.
- Ndio…nina kazi nyingi leo na lazima nizifanye.
- Tutaenda kuweka mizigo hotelini halafu nikupeleke unapotaka.
- Ipo wapi hiyo hoteli mpya?
- Hoteli ipo sehemu ya Maad pembeni mwa mto Nile.
- Ni karibu na kazini kwangu?
- Cairo ni kubwa kieneo, na sijajua hasa kazini kwako ni wapi, ila kwa mapenzi ya Allah itakufaa na itakuwa karibu na kazini kwako, na kama haikufai tuna uwezo wa kuibadilisha.

Walifika hoteli mpya na kumaliza utaratibu wa kukodi chumba…

- Nitakusubiri upumzike na baada ya hapo tutatoka.
- Hamna neno, nitapanda chumbani halafu nitarudi sasa hivi.

www.path-2-happiness.com

Joji alirudi haraka akiwa mwenye tabasamu ya furaha….

- Samahani, nataka kwenda kwenye anuani hii…hili ni shirika la ajira nimeongea nalo.
- Shirika lipo Giza, halipo mbali, pia lipo karibu na Mapiramidis.
- Vizuri, natamani kuyaona Mapiramidis!
- Kweli, haiwezekani ufike Misri halafu usiyaone Mapiramidis.
- Je Mapiramids ni sababu ya dini yenu?
- Mapiramids yalijengwa na Mafarao, na zama za Farao ni kabla ya utume wa Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) na kabla ya Yesu (juu yake amani) kwa muda mrefu, mengi yalitokana na Tawheed na baadhi yake yalikuwa ya ukafiri, je hufahamu Firaun alivyomwambia Mtume Musa: Mimi ni Mola wenu mkuu, na aliwatesa wana wa Israeli mpaka alipoangamizwa na Allah?
- Ni ajabu nimesoma kisa katika Agano la Kale (torati) na katika Qur’an.
- Vizuri sana... na ukweli: Ni kipi kati ya viwili (vitabu) vinavyo mthamini zaidi Musa?
- Kwa ukweli…Qur’an, japo ni Mtume wa Wayahudi, lakini……
- Samahani, na kwa ukweli kabisa ni kipi kina mthamini Mtume wa Mungu Yesu zaidi, je ni Qur’an au Injili au kama unavyoita (Agano Jipya)?
- Injili kwa upande wake na Qur’an kwa upande wake.
- Ki vipi?
- Qur’an kwa upande wake na kutaja tabia yake na haijampunguzia au kumbebesha mapungufu, na Agano Jipya imemkuza na kumfanya kuwa ni mungu.!
- Unadhani kumfanya mtu mungu ni kumkirimu au kumzulia?!
- Nafahamu vizuri unachokusudia, na utaniambia: Na katika baadhi ya nakala za Agano Jipya ni kuwa yeye ni mja na sio Mungu, na utaniambia mengi zaidi ya haya, na unayo haki kwa kile unachosema, lakini wewe umetaka mawazo yangu katika kitu maalum.
- Nadhani umesoma au umepitia utafiti juu ya: “Je Masiya alikuwa ni Muislamu? Cha kiongozi wa kitengo cha dini na imani katika chuo kikuu cha Luther U.S.A. Profesa Robert Shidngar.
- Ndio…. Nimekipitia kwa haraka haraka, nahisi amezidisha, vipi Masiya atakuwa Muislamu hali ya kuwa Uislamu umekuja baada yake?
- Kila alichokisema sio mnachokiamini, Ima atakuwa amezidisha, au amepinga au ni kinyume na kanuni ya elimu, yeye ni kiongozi katika upande wa elimu ya

Uungu na katika Chuo kikongwe na hajabadilisha kauli yake na chuo kinamuunga mkono, hivi huoni binadamu anahitaji kujiundia au kujitengenezea baadhi ya maamuzi kwa uhuru wa nafsi yake na ushujaa wa hali ya juu?

- Huenda nikaungana na wewe katika sehemu ya nukta ulizosema.
- Vizuri, tumefika, je unataka nipande na wewe? Au nikusubiri na uniambie utamaliza muda gani nije kukuchukua?
- Sijajua… twende pamoja hadi mambo yatakapokaa sawa, kisha nitakujulisha baada ya hapo.

Waliingia katika shirika la ajira na waliomba kukutana na Mkurugenzi, na Sekretari aliwaambia kwamba Mkurugenzi wake Dr. Gerges ametoka na atarudi baada ya masaa mawili, hivyo wakakubaliana warudi baada ya masaa mawili.

- Sisi tupo karibu na Mapiramids, je, utataka tuyatembelea mapiramids kwa muda huu wa masaa mawili au una miadi mengine?
- Twende kwenye Piramids halafu turudi baada ya hapo.
- Vizuri, kisha akasema: Kwa mnasaba Mkurugenzi wa shirika ni mkristo kama nyinyi, ila yeye ni Muodhodoksi na sio Mprostestanti.
- Umejuaje? Je unamfahamu?
- Simfahamu, ila jina lake kama alivyotuambia Sekretari ni Gerges na jina hilo kwetu linatumika na Wakristo ama kuwa yeye ni Muorthodoksi ni kwa sababu kila Mkristo kwetu ni Muorthodoksi na sio Protestanti..najua nyinyi mnapingana nyinyi kwa nyinyi.
- Je katika Uislamu hakuna makundi yenye kupingana wenyewe kwa wenyewe?
- Kwa masikitiko wapo.
- Mfano nani?
- Kuna waliopindukia wanaipinga Qur’an na kuwatukana maswahaba wa Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) na wake zake waliotwaharika na wanazua mambo yasiyofaa mengi tu.
- Ni wepi hao?
- Ni wachache sana katika Ulimwengu wa Kiislamu, na wanapatikana katika Iran, Iraq na katika mataifa mengine.
- Unamaanisha ushia!
- Nakusudia hasa Wapingaji ‘Rawaafidh’ ama wanaikataa Qur’an na hadithi, na wengineo wanaojinasibisha na Uislamu kama Bahai na Kadiyani na wengineo.

www.path-2-happiness.com

- Kwa hivyo mmekuwa kama sisi, vikundi vya kuuana au kuchinjana na kukufurisha na wenyewe kwa wenyewe!
- Hapana, sio kama nyinyi, wengi wa Waislamu wanayo Qur'an iliyoandikwa sahihi kwa ufahamu na matamshi yake sahihi tofauti na nyinyi, Waorthodoksi, Ukatoliki, protestanti na wengineo wanayo Injili isiyoharibiwa katu na mnafahamu vizuri hili.
- Najua tofauti uliosema, ila naona kuna kufanana, la muhimu je mashia wapo Misri?
- Kwa ufupi hawapo, ijapokuwa walitawala kipindi fulani Misri.
- Je mliwaua baada ya hapo?
- Sisi sio kama nyinyi, ulipoondoka utawala wao na wakabaki watu katika mwenendo wa Sunnah na katika maumbile sahihi, na wengine walirudi katika Sunnah na Uislamu.
- Kitu gani unakusudia unaposema, "Sisi sio kama nyinyi?"
- Nataraji usinielewe vibaya, ni kwa mfano tu, wako wapi wakazi wa asili wa Australia? Au wako wapi wa Amerika asilia?
- Je unaweza kufafanua zaidi?
- Unafahamu namna jamii zilivyodhulumiwa hasa! Na kwa bahati mbaya jamii ilifukuzwa ma kuangamizwa kabisa, ama Uislamu uliharamisha dhulma na ukaamrisha uadilifu..ooh angalia hizi mapiramids mbele yetu.
- Ni makubwa sana!
- Yataonekana wazi ukubwa wake na usanii wa majengo yake utakapo karibia, tutasimama hapa na tutashuka na kupanda mkokoteni wa farasi, lakini nakuzindua uwe makini sana na vitu vyako binafsi.
- Una kusudia nini?
- Sehemu zote za kitalii duniani kuna wezi na waporaji, na hili sio kwetu sisi tu, ijapokuwa kuna aina na mbinu mbali mbali za wezi.
- Kwenu ingekuwa tofauti kama ulivyosema kuwa Waislamu hawaibi?
- Muislamu sio kiumbe kama malaika, anayo makosa yake, udhaifu, upungufu na mengineyo ila dini yake inakataza hayo, japo kuna dini zingine zinamuhimiza mtu kufanya hivyo.
- Ki vipi?
- Baadhi ya dini. Hata kama asili yake ni sahihi kutokana na kuharibiwa –zinahimiza dhulma kwa wengine, kuuwa na kuiba, ama Uislamu unaharamisha kabisa hayo,

lakini kwa kadri watu wanavyo kuwa mbali na dini zao ndivyo wanakuwa mbali na maadili ya Uislamu. Na ndio sababu ya kuwepo tabia na sifa nyingi mbaya ambazo sheria imekataza kama vile: wizi, zinaa, kuunywa pombe, uongo, kuvunja ahadi, ubinafsi na mengineyo, tafadhali shuka.

- Inaonekana itakuwa ni safari nzuri yenye kustarehesha.

Jamali alikodi farasi wawili na kupanda ili wazunguke pyramids na wale walioshika farasi ni watu wasiojua Kiingereza vizuri, Joji alimuomba Jamali awaambie waendeshe farasi wale kwa haraka ili wamalize mzunguko kwa muda wa saa mbili. Na katika mwisho wa safari yao walienda kupanda gari ili wawahi miadi yao….

- Nakushukuru sana Jamali kutoka kwenye moyo wangu kwa hakika safari ilikuwa ni nzuri, tunaweza kurudi ofisini tulipokuwa?
- Sawa, na inawezekana ukitaka kumpigia simu ili akufuate hotelini, na sasa hivi ni saa saba.
- Vizuri, niwasiliane nae.

Joji aliingiza mkono mfukoni mwake ili atoe simu na kukuta sehemu au kiasi cha pesa katika mfuko wake hazipo! Aliangalia vizuri hakuziona…

- Inaonesha nimeibiwa!
- Imekuwa kheri Inshaalaah, huenda zimedondoka.
- Hapana, nadhani yule muendeshaji wa farasi aliingiza mkono wake katika mfuko wangu ilipokuwa najiandaa kushuka juu ya farasi na kuzichukua, ila hajaingiza katika mfuko mwingine ambao ulikuwa na pochi na vitambulisho muhimu vya bima.
- Sifa ni za Allah, je sijakutahadharisha kuwa makini na tahadhari!
- Pesa hazikuwa nyingi, la muhimu acha niwasiliane na Gerges, mkurugenzi wa shirika lile la ajira.

Joji alikubaliana na mkurugenzi Gerges kukutana hotelini muda wa saa nane hivi, na kumweleza Jamali hilo, na walipofika hotelini, Joji alimuomba Jamali waende nae chumbali ili wakamalizie maongezi yao…

- Sitaki kukusumbua na wewe una kikao cha kazi na Gerges.
- Nataraji kikao kitakuwa kifupi; kwani ni maandalizi tu ya kikao kirefu kesho, na mimi nataka tujadiliane na wewe katika mambo muhimu, labda uwe na shughuli ya kukushughulisha.
- Sina la kunishughulisha, karibu

www.path-2-happiness.com

Wote wawili walipanda kuelekea chumbani, na Joji aliandaa vikombe viwili vya chai katika meza iliyopo chumba cha wageni maalumu, walikaa huku wakiongea kwa dakika kadhaa mpaka ilipolia simu ya chumbani, mpokea wageni alimweleza Joji kwamba mkurugenzi wa shirika anamsubiri mapokezi.

Haraka Joji alibeba baadhi ya nyaraka, na alimuomba Jamali akaonane na Dr Gerges ambae Joji alimuona kuwa alikuwa ni mtu wa umri wa kati ya miaka hamsini, Joji aliharakisha kumsalimia na kumkaribisha…

- Ikiwa utaona inafaa tukae tuongee kidogo kwa maandalizi ya kikao cha kesho.
- Sawa kabisa
- Kama nilivyo kutajia kupitia email, mimi nahitaji kuajiri idadi kadha ya wataalamu wa kiufundi katika shirika letu na wao watafanyia kazi hapa Cairo, lakini mimi nataka watu wenye uwezo maalumu.
- Nimekuandalia idadi kadhaa ya watu unaweza kukutana nao kesho ukitaka.
- Kitu gani unaweza kunifanyia kwa mapendekezo?
- Utakao kutana nao ni hao tuliwapendekeza kwako, vinginevyo walioomba walikuwa ni wengi zaidi.
- Kwa vigezo gani vilivyo tumika mpaka kuwachagua wao.
- Kwa vigezo vya kazi! Sijakuelewa unacho kusudia nini?
- Je haikuwa moja ya vigezo ni kuwa Wakristo kama sisi?

Hasira ilidhihiri katika uso wa Gerges….

- Kwanza: Umejuaje kama mimi ni Mkristo? Pili: Mwenye shirika ni Muislamu na mimi ni mkurugenzi wake tu. Tatu: Waliopendekezwa ni watu kumi tu, mmoja wao ndio Mkristo, wengine waliosalia ni Waislamu, Nne….
- Samahani, sijakusudia kitu, lakini nilifikiria mambo yana kushindana na kubaguana, kwa hiyo nilitaka mambo kuwa wazi tu.
- Mambo kwetu sisi ni mazuri na sio kama mnavyofikiria au mnapenda yawe katika nchi zenu za Ulaya na ukweli ulivyo Wakristo wachache nchini Misri hawakupata himaya isipokuwa katika hukumu au utawala wa Kiislamu, na hata historia inaonesha Wakristo walisaidiana na Waislamu kupitia jeshi la Kiislamu kupigana katika vita.
- Vizuri, nilitaka tu kujua kuwa vigezo vilivyotumika katika kuchagua sio vya kibaguzi.
- Kuwa katika amani… uchaguzi ulitumia vigezo vya kazi, ijapokuwa idadi ya Wakristo walipendekezwa walikuwa wengi zaidi kuliko ilivyo.

- Vipi?
- Mmoja katika watu kumi ni nyingi kulingana na asilimia ya Wakristo hapa Misri, kesho nitakufafanulia vizuri maneno haya ya ziada.. sijui kama yatakupendeza au hapana?
- Ok vizuri, mimi nalazimika kurudi chumbani, kwani kuna rafiki yangu mmoja yupo ananisubiri chumbani juu…na rafiki yangu huyu ni Mmisri tena Muislamu, kwa hiyo ahadi yetu ni kesho saa tatu katika shirika, na natarajia kukutana na idadi kubwa ili uchaguzi ufanyike kwa ukamilifu.
- Sawa tumeafikiana nitakusubiri kesho, na utakuta kitachokupendeza na kukufurahisha, kwani Misri ni nchi iliyo na wajuzi wengi wenye viwango vya juu.

Joji alipanda juu chumbani na kumuomba samahani Jamali kwa kuchelewa… na akamuomba washuke kwa ajili ya chakula cha mchana hotelini…

- Je ninaweza kukuuliza swali la moja kwa moja?
- Karibu uliza.
- Nisamehe kwa kweli: Ni maslahi gani utapata kutokana na kukaa na mimi na kunipeleka na kunisindikiza?
- Maslahi ni makubwa sana na yako wazi.
- Ni yepi hayo?
- Kuwatumikia watu kwa dini yetu ni suala la muhimu sana, kwani ni katika vitu vya kujikurubisha kwa Allah.
- Je haya ndio maslahi pekee kwako?
- Hapana kuna maslahi mengine; mfano kumtumikia rafiki wa kaka yangu, na kuna muhimu zaidi ya hayo yote ni kukuvuta katika Uislamu.
- Samahani; ama kwa maslahi ya mwisho sidhani, lakini maslahi yako kipesa yakoje na unataka shilingi ngapi kwa muamala huu?
- Niamini sijafikiria pesa, weka wewe ni kiasi gani unataka kunipa, ila ondoa siku tatu za mwanzo ambazo ni haki yako kama mgeni kukukirimu.
- Siku ya leo ilikuwa ni siku ndefu pamoja na kuwa bado ni mapema, ila nataka kumaliza baadhi ya kazi nikiwa chumbani na nilale mapema, na kushukuru sana wewe…ahadi yetu ni kesho saa mbili ili tuende shirikani, ahadi na Gerges ni saa tatu
- Vizuri, tukijaaliwa na Mungu.

Joji aliingiza mkono mfukoni mwake ili atoe pochi ili alipe hesabu,

www.path-2-happiness.com

hakuikuta…

- Inaoyesha nimeacha pochi juu, ngoja nipande nikaichukue narudi nisubiri kidogo.
- Unataka nini sasa hivi?
- Nataka kumpa mhudumu ambae ametuhudumia japo pesa kidogo.
- Chukua paundi mia hii, huna pesa za Kimisri, kesho Inshaallah utabadilisha na kunirudishia, ili upande mara moja tu na muda sasa hivi una karibia saa kumi na moja na wewe unataka kumalizia baadhi ya kazi.
- Jamali nakushukuru sana.

(4)

Joji alienda chumbani kwake na kufungua kompyuta yake ili amalizie kazi zake, halafu akakumbuka mkoba wake, aliutafuta bila kuuona, alipekuwa chumbani vizuri bila mafanikio! Na kubaini haupo, baada ya hapo alikuwa ni mwenye dukuduku sana kwani kulikuwa na vitambulisho muhimu sana na pesa nyingi, alifikiri sana halafu akawasiliana na Jamali…

- Mkoba wangu uko wapi?
- Wewe umesema umeuacha chumbani.
- Naomba uwe muwazi zaidi, mimi nimeuacha chumbani na pia nilikuacha chumbani, nimerudi sijaukuta.
- Unakusudia nini?
- Usinihadae kwa paundi yako mia uliolipa, rudisha mkoba wangu sasa hivi.
- Samahani, sijauchukua mimi.
- Ulikuwa peke yako chumbani na mkoba ulikuwa huko nani kauchukua?
- Narudia kusema kuwa mimi sijauchukua kabisa.
- Na unaniambia, malipo utapata kwa Allah ninamtumikia rafiki wa kaka yangu, sasa mambo yamedhihirika kwamba dini yenu ni dini ya wizi, kwa siku naibiwa mara mbili!
- Tafadhali usiushambulie Uislamu, mimi sijachukua.
- Kwa hiyo umeenda wapi? Je umeruka?
- Kwa nini unaniambia hivi?
- Kama hutaniletea mkoba wangu kabla ya saa tatu asubuhi nitakutumia polisi,

kisha unaniambia mimi eti! kuwatumikia watu ni katika dini, inaonesha dini kwenu nyinyi ni kuwaibia watu kwa jina la dini, nisirefushe maneno ahadi yetu ni saa mbili uje na mkoba wangu, haya ndio maneno yangu ya mwisho kwako.

Joji alikata maongezi na kujitupa kitandani akiwa na hasira, hana la kufanya…

- Inaelekea Kakhi atapata ushindi kwangu! Kitu gani kimenileta katika nchi hii, ni kwa ajili ya kuujua Uislamu, dini ya wezi? Leo hii nimeibiwa mara mbili… halafu Jamali anakuja na maneno yake nisilimu!!! Ujinga ulioje huu??!

Joji aliendelea kutafakari karibu ya saa, akiwa ni mwenye wasiwasi na mwenye hasira sana, na alikuwa anajua wasiwasi wake sio kwa ajili ya pesa na vitambulisho vilivyokuwepo humo japo vilikuwa na umuhimu wake ila anahisi kuwa amefanywa kama mtoto mdogo anayechezewa na wengine kwa jina la dini, alifikiri kupeleka ujumbe wa kufungia kadi zake za bima kwa ajili ya kitambulisho chake, lakini alifikiria tena anakihitaji kukitumia, alitarajia Jamali kukirudisha kesho ili kumaliza mchezo huu mchafu wa kuigiza… alikumbuka ahadi yake ya kesho na kusitasita…

- Itakuwa vizuri ahadi yangu kesho ni kukutana na Mkristo na sio Muislamu na hii itanifanya yeye kunipa ushauri zaidi…kwa hiyo aliamua kuwasiliana nae na kumpa habari kwa yaliyotokea, alimpigia.
- Hallo je ahadi imebadilika?
- Hapana, lakini nimeibiwa na rafiki yangu Muislamu aliyekuwa chumbani kwangu wakati nikiwa nawe na naomba ushauri nifanye nini?
- Una uhakika amekuibia?
- Kwa huzuni ndio, kwani nimemuacha yeye pamoja na mkoba wangu ulikuwa humo na baada ya kurudi sijaukuta.
- Huenda unatakiwa kutafuta vizuri humo chumbani au huenda umekudondoka hotelini.
- Mimi nina uhakika, ni mara ngapi alinifanya mjinga alipokuwa akinicheka kwa kutumia mwamvuli wa dini nimemtisha kama hatauleta kesho asubuhi nitalifikisha polisi.
- Nategemea aulete, ama kulifikisha polisi halitokusadia kitu; kwani hakuna ushahidi wowote kwa jinsi nilivyokufahamu kwa maneno yako.

www.path-2-happiness.com

- Ndio, hakuna ushahidi lakini ni lipi suluhisho?
- Ni lini, kesho ndio una miadi nae?
- Saa mbili.
- Vizuri, je unaweza kunipa namba yake ya simu ili nijaribu kuongea nae?
- Haya, chukua namba yake hii….
- Naomba upumzike, na kesho tutaangalia nini cha kufanya, na kwa hali yoyote nategemea atakuja na mkoba.

Joji alimaliza maongezi na huku akihisi utulivu kidogo… akafungua email yake na kukuta ujumbe kutoka kwa John Luke:

Mpendwa Joji,

Nataraji upo salama na katika furaha huko Misri kama ambavyo mimi nilivyo hapa Libya, raia wa hapa wanamapenzi sana, tabia nzuri na wenye dini sana, labda tu kuna tofauti kati ya tabia za Ulaya na hawa Waarabu. Tabia walizonazo ni sehemu ya dini yao, si kwa ajili ya kujinufaisha na kusubiri manufaa kutoka kwa watu kama ilivyo tabia yetu sisi Wamagharibi. Tupe habari za afya yako na hali yako.

"Ni mimi John Luke."

Joji alimjibu John Luke:

"Kwako Mpendwa John Luke,

Nimefurahishwa na uzima wako hapo Libya, lakini nakuomba uwe makini na tahadhari na Waislamu, kwa upande wangu mimi nimeibiwa mara mbili mpaka sasa na Wamisri Waislamu, mmojawao ni mtu aliyekuwa akinilingania mimi Uislamu, na hakuwa na mimi bega kwa bega nilipopatwa na mtihani isipokuwa Mkristo mwenzangu, ni kiasi gani natamani nimalize shughuli zangu mapema hapa ili nirudi Uingereza.

Ni mimi Joji."

Kisha Joji alimuandikia barua Levi akimjibu barua yake ya tahadhari kutokana na Waislamu:

"Mpendwa Levi

Kwa masikitiko yamenipata yale uliyonitahadharisha nayo, nimeibiwa hapa Misri, japokuwa uliniambia mwanzo lakini kutokana na ile pupa yangu ya kuujua Uislamu ndio ikatokea hili, hata hivyo sasa nina yakini kuwa ni dini isiyokuwa na adabu

au maadili, huenda ikawa Uyahudi na Ukristo umeshachafuliwa na mafundisho yake yameharibiwa ila ni kuwa Uislamu usiokuwa na maadili kabisa, nitakujulisha maendeleo yangu hivi karibuni, lakini sasa nimekumbuka tahadhari zako na uzembe nilioufanya.

Ni mimi Joji."

Joji alikuta majibu ya maswali yake yaliyotangulia kutoka kwa marafiki zake katika email yake, lakini hakuwa na hamu ya kusoma barua yoyote ile, aliamua kufunga kompyuta yake… na kujilaza juu ya kitanda akijaribu kulala lakini hapati usingizi, aliamka kitandani na kufungua T.V. katika chaneli ya B.B.C na kuangalia habari kidogo, halafu akawa anatafuta kila chaneli mpaka alikuta chaneli ya Kiislamu kwa lugha ya Kiingereza.

Kipindi kilikuwa kikiongelea sifa nzuri katika Uislamu na kwamba Mtume aliletwa kukamilisha tabia nzuri….alijiuliza mwenyewe:

- Huenda jamii hii ya Kiislamu ina matatizo katika haiba yake na kutenganisha baina ya mafundisho na tabia…ni mara ngapi naichukia dini hii ambayo inapimika kwa vipimo viwili au kwa mitazamo miwili!

Hakuweza kukamilisha ratiba kutokana na hasira aliyokuwa nayo, alijaribu kulala tena kwa mara nyingine, na akawa anagaragara kitandani mpaka alipopata usingizi… na katika muda ya saa tisa alfajiri aliamka usingizini ghafla, alienda chooni, na alipotoka macho yake yaliangukia kutazama mkoba wake uliokuwa karibu na sehemu ya kufulia! Na alikumbuka alitumia bafu kabla ya kushuka na kwenda kuonana na Dr. Gerges adhuhuri na kwa haraka yake alichukua nyaraka maalumu au muhimu na bila kuzinduka kuwa amesahau mkoba wake mpaka alipoukosa yakatokea yaliyotokea!

Alikaa juu ya kitanda chake mwenye kuchanganyikiwa, na alianza kuhisi kizunguzungu… vipi ataweza kumuomba msamaha Jamali kwa yale yaliyotokea? Kwani amemkosea kwa kumtuhumu wizi kabla hajahakikisha hilo, na baya zaidi amemtuhumu bila ya ushahidi na Adam alimtahadharisha na kumuonya sana kutokufanya haraka katika maamuzi yake, nini anaweza kufanya kwa sasa?

www.path-2-happiness.com

(5)

Asubuhi ya saa mbili.. Jamali alifika hotelini na kumuomba mpokea wageni awasiliane na Joji ili kumueleza kufika kwake, lakini alijibiwa na mhudumu huyo:

- Joji Mwingereza?
- Ndio.
- Leo asubuhi amepelekwa na gari la wagonjwa hospitalini kwa sababu ya presha.
- Na je amerudi?
- Ndio amerudi kama masaa mawili hivi, na sijui kama amelala au bado?
- Naomba mpigie sasa hivi na mweleze kuwa mtu mmoja anaitwa Jamali anataka kupanda kukuona.

Yule mhudumu alimpigia Joji na kumweleza kwamba Jamali kafika na alimtaka apande juu chumbani… Jamali alipanda kwenda chumbani na Joji alimfungulia mlango kwa shida na uchovu ukidhihiri usoni mwake…

- Samahani Joji, sijakusudia kukufanyia ubaya naomba niamini na huu ni mkoba wa dhahabu wa mke wangu, nauweka dhamana kwako mpaka benki zifunguliwe ili nikachukua pesa nikuletee, na mimi sikuweza kuleta mkoba wako na wala sijui kuna kiasi gani!
- Yote hayo ni kwa ajili ya hofu ya Polisi?
- Mimi nasikitika kwa yaliyotokea, ila polisi hawawezi kufanya chochote.
- Kama ni hivyo, ni kwa nini umeleta dhahabu ya mkeo?
- Wewe ni mgeni na ni haki yako kukirimiwa, na wewe ni msafiri na umekatikiwa na safari ni haki yetu kukusaidia, pia sitaki nichafue sura au picha ya Uislamu machoni mwako.
- Bado nasita kwamba wewe sio uliochukua mkoba?
- Bila shaka sio mimi, ila sitaki tulijadili hilo sasa hivi usije ukajichosha zaidi.
- Laiti ungelikuwa nafasi yangu ungelifanya nini?
- Hakika sijui na hii inategemea na kiasi cha umuhimu wa mkoba na mahitajio yake kwangu mimi, na utulivu wa nafsi, huenda labda ni kwa sababu ya kusoma elimu za hesabu–labda ndio inanifanya kila kitu nikiangalie kwa muono huo.

- Na laiti ungefanya kama nilivyofanya mimi, unatarajia ningefanya nini ningekuwa sehemu yako.
- Samahani hilo siwezi kujibu.
- Je unategemea nifanye kama ulivyo fanya wewe sasa hivi?
- Kwa hakika hapana, lakini wewe unastahiki hilo.
- Na baada ya kufanya ulivyofanya na kupata mkoba wako, ni kitu gani ungesema au kumwambia rafiki yako?
- Je umeupata mkoba wako?
- Ni katika kudhania tu, jaribu kuwa nami katika hisia zangu hizo.
- Hapana budi kumuomba msamaha rafiki yangu, nahisi masuala ni magumu sana kwangu, kwa hakika itanifanya niishiwe na nguvu.
- Na hata kama nimemuomba msamaha na amekataa msamaha wako, na hatosahau ulicho mfanyia?
- Anayo haki, lakini bora asamehe kwani Allah ni msamehevu na anapenda kusamehe.
- Kwa hivyo naomba unisamehe; kwani nimeupata mkoba wangu..na kwa sababu hiyo ndio maana nimepata shinikizo la damu na kupelekwa hospitali na sikujua nifanye nini: Narudia kusema nisamehe na Allah kama ulivyosema anapenda kusamehe.

Jamali alifuta machozi yaliyokuwa yakimlenga lenga machoni mwake bila kujitambua…

- Nimekusamehe, ninachoweza kukwambia ni kuwa sijapata usingizi jana na mpaka muda huu, sio mimi, wala mke wagu, wala kaka yangu Basimu na Adam Uingereza.
- Kwani umewaambia?
- Naam, nilibanwa sana na mimi nilikuwa nataka ushauri au ufumbuzi na Gerges alinipigia simu akiniwaidhi na kunijulisha maadili ya Kiislamu, wala sikutaka niwe ni mtihani kwako, kama Allah anavyosema katika Surat Mumtahina Aya ya 5;
- “Mola wetu Mlezi! Usitufanyie mtihani kwa walio kufuru. Na tusamehe, Mola wetu Mlezi. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.” (60:5)

www.path-2-happiness.com

- Samahani sana.
- Japokuwa nina jeraha lakini mambo yameisha, na zingatia kama vile hakujatokea kitu, vipi afya yako kwa sasa hivi?
- Mimi ni mzima, lakini nimekukosea sana kukuvunjia heshima yako.
- Mimi nimekusamehe, lakini nina sharti.
- Ni lipi hilo?
- Sahau yaliotokea na angalia afya yako, vinginevyo sitakusamehe.
- Mimi naungana na sharti lako kwa sharti na wewe usahau mabaya yangu kwako.
- Tumeafikiana kwa hilo, je umeshapata kifungua kinywa?
- Hapana.
- Mimi nakualika kupata staftahi na fanya haraka ili usichelewe ahadi yako na Gerges, mimi natangulia hotelini utanikuta chini nakusubiri.
- Nipe dakika tano tu nashuka chini.

Migongano..

www.path-2-happiness.com

16 Migongano..

Migongano..

(1)

- Sasa hivi ni saa mbili na nusu, je utaweza kuwahi ahadi na Gerges?
- Tupate kifungua kinywa kwanza kisha twende tumuwahi, tukiwa njiani tumpigie simu tumjulishe kuwa tutachelewa kidogo atafahamu tu, Gerges ni mtu mwenye adabu na heshima zake tatizo ni ukali wake kwangu jana.
- Ukali wake?!
- Jana alinipigia simu na hakuacha chochote kinachowezwa kusemwa ila aliniambia na yote ilikuwa ni kwa ajili yako.
- Nakariri masikitiko yangu kwa kila kilichotokea.
- Inaelekea unataka kuvunja makubaliano yetu?
- Hapana, asante sana Jamali, ni kiasi gani naweza kukushukuru.

Joji na Jamali walifika katika shirika la kimataifa la ajira na Joji alimuulizia Gerges, sekretari akamwambia kuwa anawasubiri, wakaingia ndani na Gerges akawakaribisha.

- Nipe habari nzuri…je sahibu yako ameleta mkoba?!.
- Tuache tukae kwanza, pili tusamehe kwa kuchelewa.
- Nimeongea na sahibu yako anayeitwa Jamali jana kwa muda mrefu, ukweli ni mtu mwenye heshima zake na sidhani kama ameiba, hata hivyo nilimshinikiza sana.
- Nasikitika kwa hilo, nimekusumbua sana, naomba unisamahe na nataraji utanisamehe, Jamali ni mtu mzuri na amenisamehe, mkoba wangu nimeupata bafuni hotelini!
- Ah! Rehma zako ewe! Mungu, Mungu atusamehe, kwa kweli nimemkosea sana Jamali.
- Nakutambulisha kwa rafiki yangu Jamali.
- Samahani sana ndugu yangu kwa nilichokufanyia jana.
- Mungu akusamehe, hamna neno…maudhui haya yamekwisha na tumekubaliana tuyafunge na tusiyazungumzie tena.
- Wakati gani ulijua kuwa Joji alipata mkoba wake?
- Nilijua saa mbili pindi nilipompa dhahabu za mke wangu kwa mkabala wa mkoba wake.

www.path-2-happiness.com

- Tunaomba msamaha wako ewe Mola wangu, narudia samahani zangu; amesema kweli Allah:
- "Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kuto jua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda." (49:6)
- Ni andiko gani hili ulilolitoa?
- Hili ni nukuu ya Qur'an Tukufu.
- Je, Wakristo wanahifadhi Qur'an pia?
- Je sijakuambia kuwa kesho nitakushtukiza kwa jambo na sijui kama litakufurahisha au hapana! Mimi nimesilimu kama miezi sita iliyopita tu.
- Umesilimu na kuacha Ukristo?!
- Ndio …kuna ajabu gani? Ni watu wengi wanaosilimu, bali Uislamu ndio dini inayoenea upesi zaidi ulimwenguni kote.
- Sio jambo geni, lakini kwa mara ya kwanza namuona mtu ambae hakuwa Muislamu kisha akasilimu.

Jamali alishangaa na kuweka mkono wake juu ya kichwa chake na akasema:

- Nilishangazwa sana na unapokuwa ukiniita ndugu yangu, nikawa najisemesha huenda anakusudia udugu wa ubinadamu tu, hongera ndugu yangu furaha ya dunia na akhera.
- Furaha ya dunia na akhera! ama ya akhera: sijui, ama dunia: furaha yake tunayo sisi watu wa Magharibi.
- Ikiwa unakusudia miundo mbinu na vyombo vya starehe ni kweli, ama ikiwa unakusudia furaha kwa maana yake basi utaona hali za huzuni na ajabu zinaongezeka. Ndio maana suala la kujinyonga, uendawazimu, maradhi mbali mbali ya nafsi katika nchi za Magharibi vinaongezeka siku hadi siku.
- Je unanikusudia mimi Jamali?
- Sifahamu! Wewe una uhusiano gani na niliyo yataja.
- Mimi ni sehemu ya Magharibi ambayo unaizungumzia.
- Suala lipo katika kulipa uhuru maana ya furaha ikiwa katika maisha ya raha au katika hisia za ndani ya mtu, nadhani watu katika maisha hayo ya kimada wamekosa hisia za kiroho ndio sababu ya kuchanganyikiwa katika ufahamu, na ndio sababu ya huzuni.
- Alhamdulillah umepata mkoba wako, suala letu hapa sio furaha bali suala ni kuwa watu wanasubiri usaili na sisi tuna kazi.

- Swadakta…Samahani, niwaacheni sasa.. nikufuate saa ngapi Joji?
- Nataraji tutachelewa, napendekeza ukapumzike leo, tukimaliza nitamsindikiza hotelini mwenyewe.
- Asante sana …Jamali je naweza kukuona kesho saa mbili?
- Sawa, tumeafikiana, haya kwa herini, Asalaam Alaykum Warahmatullah Wabarakatuh!
- Jamali ni mtu mzuri, umefahamiana nae vipi?
- Kupitia ndugu yake Uingereza, vizuri nikujulishe lile ambalo hulifahamu ni kuwa kabla hatujafika alikuwa akisema kuwa wewe ni mwenye heshima sana, pamoja na kusema kuwa ulimkosea sana, hali kadhalika alikuwa akikudhania kuwa ni Mkristo.
- Katika Uislamu tunatakiwa tuwafanyie uadilifu hata adui zetu, amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka: "Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu."(5:8). Tuliache hili sasa, tunahitaji kujadili mikataba kwanza, kisha tuwafanyie usaili, muda wako kadri nilivyofahamu ni mdogo sana.
- Ndio, lakini ningependa kuzungumza nawe maudhui ya Uislamu wako baadaye.
- Iwe wakati wa chakula au nitakapokusindikiza hotelini.

Saa kumi na mbili jioni Joji na Gerges waliondoka katika shirika la ajira na kurejea hotelini, baada ya siku nzito iliyojaa makabiliano na watu wengi na mikataba mbali mbali, Joji alipanda gari la Gerges.

- Jitihada kubwa imefanywa kwa siku moja tu, umemaliza usaili kwa wote, nini rai yako kuhusu ulioonana nao?
- Ukweli ni kuwa ni nzuri kuliko nilivyotarajia, na mbali na suala hili la kikazi na fani zao kilichonipendeza zaidi ni tabia zao za kijamii, hili hatukulizoea Uingereza, inaelekea majukumu yangu yatakuwa mepesi kwa sababu ya juhudi zenu….
- Nini kinachofuata?
- Sitaki kufanya haraka, nimebakiwa na usaili wa aina mbili kesho, na kesho kutwa katika ofisi zingine mbili, baada ya hapo ndipo ninaweza kuchukua maamuzi mnasaba.
- Vizuri; haraka sio nzuri, au siyo?
- Umenikumbusha tatizo haswa…ni kiasi gani nimefurahishwa na Jamali, ni mtu mzuri… lakini kwa sababu umesema haraka si nzuri; sasa kwa nini umefanya

www.path2-happiness.com

haraka kusilimu?!
- Ha ha ha, usifanye haraka kuhukumu! Ni nani aliyekuambia kuwa nimefanya haraka? Bali ukweli nikuwa nimechelewa mno.
- Ki vipi?
- Nilichukua muda mrefu hadi nilipokinaika na Uislamu, na aliyenikinaisha ni huyu mwenye shirika, pamoja na kuwa hakunisukuma au kuniamrisha au kunitia dhiki nisilimu hadi muda huo sikuwa nimechelewa. Lakini baada ya kukinaishwa nimekaa miezi sita kabla ya kusilimu na hapo ndipo nilipochelewa.
- Miezi sita ni michache mno kwa kuchukua maamuzi makubwa kama haya!
- Je ningekufa ingekuwaje nikapata mateso duniani na akhera?
- Nashangazwa sana nanyi kila mara mnaunganisha dunia na akhera, lakini niwekee wazi ni nini hizaya ya duniani na ya akhera?
- Ama hizaya ya dunia ni; sikuwahi kuhisi utulivu, raha na furaha hadi niliposilimu! Huenda ukashangazwa na hilo lakini huo ndio ukweli wenyewe, hivyo basi maana ya kufanya Mungu kuwa ni mmoja na kumuabudu Yeye na kukimbilia kwake pekee bila kumshirikisha hupanua mioyo na kufurahisha nafsi za watu, hata kama ikiwa katika maisha yenyewe ya uhalisia kuna matatizo, kwani baada ya hapo baadhi ya jamaa zangu wamenihama na wakajaribu kunidhuru.
- Kumpwekesha Mungu na ibada hupanua mioyo?!
- Naam… kama ambavyo upagani, ushirikina na utatu unavyobana vifua. Ama hizaya ya akhera; mimi sipendi kutangulia kwa Mungu muda ambao ninamshirikisha Yeye na kingine au mwingine, kwani pamoja na ukarimu wake na huruma zake hamsamehi anayemshirikisha lakini husamehe yaliyo chini ya hapo, lakini Mungu wangu amenihurumia sijafa kabla ya kusilimu.
- Maneno yako ni ya kushangaza!
- Kuna nini cha kushangaza?
- Kwa kuwa tumefika, tukamilishe mjadala wetu hotelini.
- Nisamehe… nimechelewa nyumbani tutazungumza baadaye.
- Hii ina maana kuwa nitakula peke yangu!
- Likiwa hilo halitokutia dhiki.
- Hamna neno, nakuruhusu.

(2)

Joji alipanda chumbani kwake na kuweka vifaa na begi lake, kisha akateremka kwenye mgahawa hapo hotelini, alikuwa akihisi njaa kali. Alipokuwa akila chakula chake cha usiku, pembeni yake alisimama mtu aliyekuwa amevaa mavazi ya ajabu.

- Jina langu ni Rami, je utaniruhusu nizungumze nawe?
- Karibu.
- Wewe ndie uliyechukuliwa na gari la wagonjwa jana kwenda hospitali?
- Ndio.
- Chunga sana kuna wezi wengi hapa.
- Ndio… jana niliibiwa.
- Najua hili, ndio maana na kutahadharisha.
- Umejuaje?
- Mimi nafahamu mambo yote kwa njia ya kiroho.
- Roho gani hizo?
- Hii ni siri miongoni mwa siri zangu.
- Je unajua kitakacho nitokea mimi kesho?
- Ndio.
- Huoni kuwa hili linagongana na akili ya mtu pamoja na dini?
- Wewe unajua dini yetu kuliko sisi, kwani wewe ni Muislamu?
- Hapana, lakini katika Qur'an yenu: "Hajui ghaibu isipokuwa Mungu."
- Hii ni elimu, hivyo achana na dini zote.
- Mimi sio Muislamu, lakini naamini kuwa huo ni ushirikina na sio elimu, hivi ndivyo tunavyoamini sisi Wakristo, ama kwenu nyinyi Waislamu sijui!
- Ha ha ha, Italia ni nchi ya Wakristo, je unajua kuwa idadi ya wapiga ramli waliopo huko ni zaidi ya wanazuoni wa dini waliopo Italia!
- Najua kuwa ushirikina katika nchi za Magharibi unaenea kwa kasi sana kwa sababu ya kuhangaika kwetu kutafuta mambo ya kiroho ambayo tunayakosa, lakini naamini kuwa yote ni ushirikina. Je unaweza kunikinaisha kuwa jambo hili ni la kielimu?
- Ndio.
- Jana niliibiwa mara mbili, je unajua walioniibia?
- Je unaweza kunipa kiganja chako cha mkono niangalie?
- Huu hapa.

www.path2-happiness.com

- Aliyekuibia mara mbili ni mtu wa karibu nawe sana.
- Vizuri, inaelekea kweli unajua yasiyoonekana, ameniibia nini?
- Umeibiwa vitu vyako muhimu sana.
- Na ameviweka wapi?
- Sehemu iliyopo karibu…mbali, nipe dola kumi ili niipe roho ambayo itanijulisha sehemu yake.
- Ukinijulisha ulipo mkoba wangu ulioibiwa nitauchukua kisha nitakupatia dola mia moja.
- Nipe kwanza dola kumi.
- Sinayo kwa sasa.
- Roho njema imeniambia kuwa utapata matatizo makubwa kama hukunipa hiyo hela sasa.
- Ha ha ha, nimemaliza chakula changu, iambie roho njema uliyonayo kuwa ni muongo, na kuwa mkoba wangu ninao mwenyewe na haukuibiwa nilikuwa nacheza na wewe tu.

Joji alipanda chumbani kwake huku akishangazwa na tabia za mpiga ramli aliyekaa nae, na kushangazwa na wingi wa watu hawa huko Roma kuwashinda watu wa dini. Je dini, mantiki, akili na elimu zimefilisika na kuwaacha wapotoshaji hawa. Joji alifungua kompyuta yake kuangalia barua pepe ambazo hakuziona jana…aliona barua ya John Luke.

"Mpendwa Joji,

Nimesoma barua yako na nimesikitishwa na yaliyokukuta hata hivyo hapana budi kuweka wazi mambo mawili: Kwanza: Inapasa tuweke kando dini, fikra madhehebu na matendo ya baadhi ya wafuasi wake madamu ya kuwa dini zao hazihamasishi kufanya hivyo. Pili: Mimi naishi na Waislamu hapa na kwa ujumla ni watu waliokuwa mbali sana na suala la wizi pamoja na ufakiri wao, na udhaifu wa serikali zao pamoja na tofauti zao za kikabila, na sababu kubwa ya kutofanya hivyo kwao ni dai kuwa wanajizuia kidini na sio hofu ya sheria, kwa sababu dini yao inawakataza kufanya hivyo. Ama sisi mara nyingi kinachotukataza ni serikali na sio tabia au dini, serikali zikivunjika au mfumo unaotawala ukiharibika mambo yanachafuka na kuharibika na wewe unajua zaidi uzoefu wa nchi za Magharibi kuliko mimi. Mwishowe napenda kukujulisha kuwa mimi pamoja na inadi yangu nilikaribia kusilimu lau kama si baadhi ya mambo fulani pamoja na khofu.

John Luke."

- Joji akamjibu:

"Mpendwa John Luke.

Nakushukuru kwa kuwa pamoja nami, sijui nikuambie nini lakini nilidhania kuwa nimeibiwa, na nikamtuhumu rafiki yangu Muislamu na kumdhulumu, kisha akadhihirisha tabia yake nzuri na jambo hilo likanifedhehesha, kwani ni mtu mwenye heshima na tabia njema. Sijui nitamuombaje msamaha kwa upumbavu niliofanya! Ama kuhusu Uislamu; sijajua bado ni kwa nini sijachukua hatua? Lakini nahisi kuwa haiwezekani kwa muda huu kwangu mimi kusilimu kwa uchache. Bado nina tatizo kubwa, kwa mfano nafasi na hadhi ya mwanamke katika Uislamu, haki za binadamu na kiwango cha ustaarabu wa dini hii, nataraji utanijulisha utakaopata majibu hayo.

Joji."

- Kisha akapokea barua kutoka kwa Levi:

"Mpendwa Joji,

Nimeumizwa kwa ulichokipata, nilikuonya na kukutahadharisha, huenda kilichotokea ni kheri kwako na kwa Habib ili mpunguze mbio zenu kuelekea kwenye Uislamu, je kuna kitu tunaweza kukusaidia, unaweza kuja Tel Aviv na utakuwa katika hali ya furaha kwetu sote na kuachana na hao Waislamu magaidi, nasubiri ujio wako.

Levi."

- Joji akamjibu:

"Mpendwa Levi,

Nimekutamani sana, na naendelea kuhitajia nasaha zako, lakini ukweli wa mambo ni kuwa hata sijui nikuambie nini… nilidhani kuwa nimeibiwa hadi nikamtuhumu rafiki yangu Muislamu na kumdhulumu kisha akadhihirisha tabia yake nzuri na kunifedhehesha kwa heshima na tabia yake njema aliyokuwa nayo. Nakariri kwako kuwa mimi sina pupa na Uislamu pamoja na kuwa hadi sasa nimevutiwa sana na hukumu zake, itikadi zake na katika mambo mengine bado sijakata shauri, na kupongeza kwa posa yako kutoka kwa Habib, niamini huwezi kumpata mfano wake katika akili yake, elimu yake na ufahamu wake, unapozungumza nae utamuona kuwa ana vitu ambavyo mwingine hana. Natamani kuja Tel Aviv, pamoja na kukuhakikishia kuwa hapa nimepata makaribisho mazuri ambayo nilipata kutoka kwako Tel Aviv, huenda hata hivyo nikawatembelea hivi karibuni.

Joji."

Kisha katika barua alizopata ni barua kutoka kwa Katarina:

www.path-2-happiness.com

"Mpendwa Joji

Adam alinijulisha kuibiwa kwako na nduguye Baasim nilipomtembelea jana hospitalini. Jambo hili limenihuzunisha na kuniumiza, nataraji utakuwa thabiti; ufahamu wangu mdogo wa siku mbili kumtembelea Baasim wakati akinifahamisha kuhusu Uislamu sidhani kama ndugu yake kama atakuwa kama yeye anaweza kufanya hivyo, tujulishe maendeleo yako."

- Joji alimjibu:

"Mpenzi Katarina,

Imethibiti kwa dalili isiyo na shaka ya kuwa hakuniibia; hivyo usijali, kilichotokea ni sintofahamu yangu, niombee msamaha kwa Baasim kwa niaba yangu. Kwa mnasaba: Je inaingia akilini kuwa Katarina Mkatoliki mwenye dini anataka kuujua Uislamu?! Au ya kuwa Qur'an au kitabu. "Mapenzi yangu makubwa kwa Yesu yamenipelekea kwenye Uislamu." Kitabu ulichokuwa ukikiogopa kukisoma kimekuathiri?! Nimekutamani sana mpenzi wangu.

Mpenzi wako,

- Aliendelea kufungua barua mbali mbali kutoka kwa sahiba zake zikiwa na majibu ya maswali yake aliyowatumia, alifupisha na kuwatumia tena wote…

Kuhusu Ugaidi:

Habiib: Ugaidi hauna dini kabisa.

Levi: Kama Waislamu waliomuua baba yangu sio magaidi; basi sijui nini maana ya ugaidi!

Hakuna ugaidi katika Uislamu.

Adam: Gaidi ni yule anayekalia kwa mabavu nchi za watu na kuchukua kheri zao.

Tom: Ugaidi ni mshumaa wanaoutumia magaidi kwa kutishia wasiyopenda.

John Luke: Aina mbaya kubwa ya ugaidi ni ugaidi wa fikra; nayo ni kuwahofisha watu katika fikra tu, ama Uislamu unalingania watu kufikiri.

Joji: Hadi hivi sasa sijaona uhusiano kati ya Uislamu na ugaidi ila tu kupitia vyombo vyetu vya habari.

Ama kuhusu Mwanamke:

Katarina: Mwanamke ametukuzwa sana kwenye Uislamu pamoja na kuwa hadi hivi sasa sijafahamu maana ya hijabu.

Levi: Sio mbaya kama alivyo katika Uyahudi na katika Ukristo.

Tom: Nahitaji kufanya utafiti zaidi katika maudhui haya, kwenye Qur'an wamendika: "Na mwanamume si sawa na mwanamke" (3:36)

Habib: Hauja mdhulumu.

John Luke: Katika utamaduni watu tunataka usawa baina ya mwanamme na mwanamke bali kutoyumkinika kwake. Ama Uislamu umemtendea mwanamke uadilifu na umempa haki yake.

Adam: Hakuna dini iliyomtukuza mwanamke kama vile Uislamu ulivyomtukuza, mnaweza kuulinganisha na dini nyinginezo za mbinguni au ardhini….

Joji: Bado kuna mambo hayajakaa kwangu vizuri kama vile hijabu: kupeana mikono, mirathi na mengineyo, najaribu kuendelea kuyafahamu na kuyafanyia utafiti."

Kwa kuwa majibu yenu nyote kuhusu Uislamu ni chanya kwa ujumla wake, swali langu la moja kwa moja litakuwa: Kitu gani kinawazuia kuwa Waislamu? Nijibu kwa kina na kwa ukweli kabisa ndani ya siku mbili?

Wenu Joji."

Aliingia katika ukurasa wa face book wa Tom; hakuona kitu kipya, kisha akaingia wa Adam; akaona mfululizo mpya wa: "Mazingatio kutoka kwa rafiki yangu mtafuta furaha – 5.

"Niliwaambieni mara kwa mara kuwa rafiki yangu katika hatua zake za mwisho, naamini kuwa kwa kiasi kikubwa amekinaishwa na Uislamu kuwa ndio njia ya furaha yake, na hawezi kujibiwa maswali yake makubwa isipokuwa na Uislamu tu, lakini uongofu unaibukia kutoka kwa Mungu peke yake tu…mke wake alikuwa akilia jana, kilio kilikua kikubwa akiwa ameathiriwa na mapenzi ya Uislamu, na haijulikani kama alikwisha silimu au bado; kwani alikuwa amerejea nyumbani katika hali hiyo ya kulia, huenda Mwenyezi Mungu akamwongoza katika furaha ya duniani na akhera.' Ama sahiba yangu kwa kadiri ya imani yangu kuhusu uwezo wa akili yake na ufahamu wake na kwa kadri ya hofu yangu juu yake kutoka kwa Waislamu, hivi sasa amesafiri kwenda Misri ili kuufahamu Uislamu, kwa masikitiko anasema kuwa Waislamu wamemuibia, na hakufahamu tofauti kati ya kuwa ni kosa au tatizo katika Uislamu au kwa Waislamu, pamoja na kuamini kuwa kuna ukweli ambao utamfanya apite katika mtihani huu na kuingia katika Uislamu, na nafupisha darsa hili kwa nukta hizi zifuatazo:

1Uislamu ni mkamilifu wa kila aibu, tofauti na Waislamu ambao wengi wao hawaepukiki na makosa.

2Kuchukua maamuzi ya kuingia katika Uislamu kunahitaji ujasiri mkubwa na kuufahamu kwa kina, huenda hilo akalihitajia sahiba yangu.

www.path-2-happiness.com

3Inatubidi tusifanye upesi kuwaingiza watu katika Uislamu na kuelekea katika njia ya furaha ila baada ya mtu kukinai kwa ukamilifu.

4Hatuna kitu cha kuficha katika njia ya furaha, ni mkamilifu kwa hali zote, yenye kukinaisha pande zake.

5Kwa kila aliyetukuzwa na Mungu kujua njia ya furaha awaelekeze watu kwa njia ya wema, na uongofu ubaki kwa Mwenyezi Mungu pekee.

Namtamania sahibu yangu kheri pamoja na kuwa sijui kwa ukweli, kama Mwenyezi Mungu ataufungua moyo wake au hatoufungua?

Subirini somo la sita;

Adam."

Habari aliyoandika Adam kuhusu Katarina ilimsumbua sana, alikuwa akijiuliza, "Je, inaingia akilini Katarina kuingia Uislamu? haiwezekani… huenda alimpendezesha tu Adam naye hakumfahamu vizuri, au huenda Adam akawa anaongopa na kujaribu kudhihirisha kwa wasomaji wa face book yake kuwa ameweza kuwaingiza Wakatoliki katika dini yake, kwani katika barua yake ya mwisho jana hakumwambia kuwa amesilimu…alirejea tarehe ya makala ya Adam na kuikuta kuwa imeandikwa kabla ya masaa mawili, wakati barua ya Katarina kwake ilikuwa katika tarehe ya jana asubuhi. Je inawezekana akawa amesilimu jioni? Kwani kama ni hivyo hakumwambia?

Barua zote za Katarina za mwisho zimebeba rai chanya kuhusu Uislamu, bali aliweza kutofautisha baina ya Uislamu na Waislamu katika tukio la wizi. Je haukuwa huu ni uthibitisho wake kuwa amesilimu? Lakini Katarina daima alikuwa ni mwenye hamasa na Ukatoliki, na kumpenda masiya mapenzi makubwa sana na kwa ajili hiyo maisha yake yote yalikuwa ni kuhudumia kanisa, anaweza kuacha vitu vyote hivi?

Usiku ule Joji alikesha katika mgongano mkubwa, kuna muda anaona kuwa ni haki kwa mke wake kufuata dini aitakayo, na wakati mwingine anajiona ndani ya nafsi yake akiwa anachukizwa na hilo, na wakati mwingine anakana habari ya Uislamu, alikuwa akijiuliza: Je yeye (Joji) angetaka kuingia katika Uislamu ingebidi amjulishe mke wake au ndio ubaguzi dhidi ya wanawake! Aliingiwa na hamu ya kumpigia zaidi ya mara moja, lakini alijizuia. Alikuwa na uwezo wa kuwasiliana nae na kumjulisha yeye mwenyewe, au kwa uchache kumtumia barua lakini inavyoonesha ni kuwa Katarina alikuwa bado hajachukua maamuzi mazito kiasi hiki.

(3)

Joji aliamka saa moja asubuhi akiwa ni mchovu, alikoga upesi na kuteremka katika mgahawa wa hapo hotelini ili apate kifungua kinywa, kisha akakaa kumsubiri Jamali watoke waende nae katika shirika la Ajira.

Walifika kwenye lile shirika na wakamuomba sekretari wamuone mkurugenzi wake.

- Dakika chache tu mtaweza kuingia kwa AlUstadhi Mustafa.
- Jamali, jina la mkuu ni Mustafa, lina maana gani?
- Hilo ni katika majina ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam), yaani Mungu amemchagua, na Waislamu wanaitana majina hayo.
- Yaani ni Muislamu!
- Ndio, kwa asili hii.

Zilipita dakika mbili, kisha sekretari akawaambia kuwa Ustadh Mustafa anawasubiri.

- Karibuni.
- Nakuacha Joji, na nitakupitia saa sita mchana.
- Sijui nitahitaji muda gani pamoja na Ustadh Mustafa.
- Kulingana na barua pepe yako na matayarisho tuliyoyafanya, nataraji tutamalizia saa nane mchana au uje kesho kwa mara nyingine tena.
- Kama ni hivyo nitakusubiri Jamali saa nane mchana.
- Lakini ningependekeza tule pamoja chakula cha mchana; wewe ni mgeni wetu leo.
- Mama yangu ameniomba nimpeleke Joji akale chakula cha mchana kwetu leo.
- Kama ni hivyo basi chakula cha jioni pamoja nami.
- Tumekubaliana, Jamali nitakusuiri saa nane.
- Na saa moja nitakupitia hotelini kwa ajili ya chakula cha jioni.
- Tumekubaliana, naombeni ruhusa.

Jamali alitoka, na Mustafa akamgeukia Joji.

- Inaelekea nyinyi ni marafiki wawili mlioshibana.
- Ndio pamoja na kuwa sikufahamiana nae ila hivi karibuni, lakini ni mtu kwa maana ya neno hilo.
- Kwa kuwa wewe hukufahamiana nae ila muda wa hivi karibuni na kutahadharisha na hawa Waislamu siasa kali.
- Ni kitu gani kinakujulisha kuwa ni Muislamu wa siasa kali.

www.path-2-happiness.com

- Anaonekana hivyo.
- Sasa unanitahadharisha na nini?
- Nakutahadharisha wasije kukuuwa au kukuibia au kitu cha mfano wa hayo, wao wanakuona kuwa ni kafiri inapasa wakuchukie, bali inapasa wakuue.
- Asante sana kwa nasaha zako, na wewe ni katika aina gani ya Waislamu?
- Mimi ni Muislamu lakini ni mtu niliyefunguka, muda wangu mwingi nimeishi Marekani, na nimejifunza mambo mengi kuhusu ustaarabu ambao Waislamu wenye siasa kali wamekikosa.
- Mfano nini?
- Nimejifunza demokrasia, na kuwakubali watu kwa rai zao mbali mbali na dini zao tofauti na yasiyokuwa hayo unayoyafahamu zaidi kuliko mimi; kwa sababu wewe ni Mwingereza.
- Huku ni kutojikweza kutoka kwako, lakini nashangazwa na maneno yako; kwa sababu hata sisi Wakristo tunawaona kuwa nyie ni makafiri ambao hamjaendelea!
- Mustafa alibabaika, kisha akasema: Kweli sisi tuko nyuma mtazamo wako ni sahihi kwa upande huu.
- Huenda, la msingi tuanze kazi yetu.
- Vizuri, tuanze kazi yetu, lakini nakuhakikishia kuwa matangamano na watu waliofunguka na wenye tamaduni mbali mbali kuna dhamana zaidi ya kufanikiwa kwako, na wewe kuwa mbali na usiyoyataka.
- Bila ya shaka na haswa zaidi ikiwa anaipenda nchi yake na jamii yake!
- Asante sana, nimekutayarishia idadi ya wafanyakazi kwa sifa ulizotaja kwenye barua yako.
- Vizuri, wako wangapi, unawatathmini vipi wao?
- Idadi ya mwanzo wanane, na wengi wao wamefunguka kwa tamaduni mbali mbali.
- Vizuri, vipi kuhusu fani na taaluma zao?
- Sio mbaya, onana nao mwenyewe, je unataka tuanze usaili?
- Sawa kabisa, nipatie CV zao kwa mpangilio kabla ya kuingia kwangu.
- Hizi hapa, nitamjulisha sekretari waingie kwa mpangilio wa nyaraka ulizonazo kwenye chumba cha mikutano, karibu kwenye chumba cha mikutano nikusindikize kisha nitarejea utakapokuwa umemaliza.

Joji alikutana na wale wanane waliopendekezwa na Mustafa, hakumaliza usaili isipokuwa saa nane kasorobo.

- Nakushukuru, nimemaliza usaili.
- Umewaonaje?
- Vizuri, nitachukua maamuzi baada ya kumaliza usaili mzima kesho, unaonaje tukamilishe mazungumzo yetu wakati wa chakula cha usiku leo, kwani Jamali atafika baada ya dakika chache.
- Vizuri, nimekutayarishia kinachokupendeza na kukufurahisha, hadi atakapokuja Jamali, je umevutiwa na yeyote katika wale wanane uliokutana nao?
- Nimewaangalia wengi na nimevutiwa na wengi.
- Utakipata kile kitakacho kuridhisha leo.
- Kivipi?
- Tutamalizia mazungumzo yetu kwenye chakula cha usiku.

Joji alitoka kwenye shirika na kumkuta Jamali akimsubiri, akapanda kwenye gari kuelekea katika nyumba ya Jamali.

- Vipi kikao chenu kilikwendaje?
- Si mbaya.
- Kama kwamba hukufurahishwa!
- Sikufurahishwa kabisa!
- Kwa nini?
- Ameniletea watumishi ili wafanye kazi kwangu na mimi nahitaji wataalamu wa Programu.
- Huenda hakukufahamu unachokitaka kwake?
- Hapana, amefahamu vizuri kabisa, lakini amenidhania kuwa nataka kushibisha matamanio yangu, fikiria nimekutana na watu wanane, miongoni mwao wanawake watano, wawili tu ndio wenye fani za Programming, na wanaume watatu, wawili miongoni mwao ni watalaamu wa fani ya Kompyuta.
- Sasa amewachagua kwa vigezo gani?
- Nadhani kwa uzuri wao, utanashati wao na unafiki!
- Nimefahamu unachokusudia, na nakuomba msamaha, lakini sisi Wamisri hatupo hivi!
- Huenda, natamani nisikutane nae mara nyingine, pamoja na kuwa kuna kijana mmoja wa kiume na mmoja wa kike nimefurahishwa nao kwani wanasifa za kipekee.
- Kwa sababu umeshamuahidi, kula nae pamoja leo jioni na uombe ukutane na uliovutiwa nao.

www.path-2-happiness.com

- Hili ndilo litakalotokea baada ya kumaliza usaili wangu kesho.
- Mara nyingi mambo hayawi mepesi, baada ya muda mdogo tutafika nyumbani na sasa hivi tutaanza kuingia katika mitaa yetu, samahani kwani sisi tunaishi kwenye mitaa ya msongamano na sio hoteli ya nyota tano au nne.
- Mimi napendezwa na hili na narejea shukurani zangu kwako na mama yako.
- Siwezi kuingia na gari zaidi ya hapa, kwani barabara ni kama unavyoziona ni nyembamba sana, tutateremka na kutembea kwa miguu, ni karibu sana na hapa.

Walifika katika nyumba ya Jamali iliyoko katika ghorofa ya tatu katika nyumba iliyoonekana ya kizamani, Jamali alimkaribisha Joji nyumbani kwake na kumuelekeza kwenye chumba kidogo kilichopangwa vizuri kwa ajili ya kukaribishia wageni.

- Karibu, samahani dakika chache narudi.

Joji alikaa huku akiangalia samani katika chumba kidogo, pamoja na kuwa ana mapenzi na sehemu za kawaida kama hizi hata hivyo alishaingiwa na hisia ya hofu tokea aanze kuingia katika mtaa huo hadi alipofika kwa Jamali, je hii ni nyumba yake kweli? Au amemleta hapa kwa malengo yake? Alikumbuka mazungumzo ya Mustafa kuwa Waislamu hawa wa siasa kali ni wauaji na wezi na wana hisia za kulipa kisasi tu. Alizicheka fikra zake ngeni na akakumbuka msimamo wa Jamali pindi alipomtuhumu kumuibia mkoba wake, akiwa katika fikra zile, mara Jamali akaingia akiwa na sahani kubwa ikiwa na vyombo vyenye vyakula mbali mbali, aliweka sahani ile mbele ya Joji.

- Samahani kama nimechelewa, karibu.
- Akiwa anaangalia chakula, asante sana, umejikalifisha sana.
- Hapana sijajikalifisha, chakula hiki si changu bali kutoka kwa mama, kwani yeye ndie aliyekualika chakula na atafika baada ya muda mdogo akusalimie.
- Ajabu mualikaji hayupo wanapoingia wageni.
- Mwanamke katika Uislamu ametukuzwa kuliko mnavyofikiria, yeye ni Malkia anayehudumiwa, mimi nipo tayari kufanya chochote akitakacho mama yangu kwa hali yoyote ile.
- Kwa hali yoyote ile?!
- Ndio, kadri ya uwezo wangu, Mungu amefananisha utiifu wake ni kama kuwatii wazazi wawili na haswa zaidi mama.

Mama Baasim alifika na kusimama mlangoni, aligonga mlango pole pole, kisha akazungumza kwa lahaja ya Kimisri.

- Asalaam Alaykum mwanangu, umetutukuza, umetuletea nuru na kututukuza kwa kufika kwako, Baasim anakusalimu na anatuusia kwako.
- Mama yangu anakusalimia Joji na kukukaribisha, na anakuambia: Ewe mwanangu umetupa utukufu na kuingiza mwanga na umetukirimu kwa kuhudhuria kwako, na Baasim anakusalimu na anatuusia kwako.
- Mpe shukurani, sijui la kusema, kwa nini hakai pamoja nasi..njoo pamoja nasi.
- Mama amekuja kukukaribisha na kukujulisha kuwa sote tupo chini ya huduma yako, kwani wewe ni mgeni wetu.
- Mmenifahedhesha kwa ukarimu wenu samahani, lakini kwa nini hakai na sisi? Kwa nini hatoi mkono?
- Wanawake huku kwetu hawakai na wanaume bila ya haja maalum, wala hawapeani mikono na wanaume ila kama ni katika maharim (ndugu wa karibu).
- Kama nilivyokujulisha leo hii nimekutana na wanawake watano, wanne miongoni mwao nimepeana nao mikono, na nilishangazwa na mmoja wao aliyekataa kunipa mkono, na wote walikaa pamoja nami.
- Nini alichokuambia yule aliyekataa?
- Aliomba samahani kuwa hapendi kuwapa mikono wanaume.
- Nini rai yako kwake?
- Nimeheshimu matakwa yake, na nikizingatia wale wasichana niliopeana nao mikono na ule uangaliaji wao, ulikuwa wa ukosefu wa adabu.
- Je mimi ninaweza kwenda Uingereza nikampa mkono malkia?
- Kuna uhusiano gani na hilo! Kamwe kuna aina saba ya watu ambao wanaruhusiwa na sheria kumpa mkono malkia.
- Kwani sijakuambia kuwa katika dini yetu mwanamke ametukuzwa kama vile malkia aliyetukuzwa. Uislamu hauruhusu kumpa mkono mwanamke ila aina saba ya watu waliotajwa ambao ni: Baba, babu, mume, na baba yake mume na mtoto wa ndugu, baba mdogo, mjomba na mtoto wa kaka na mtoto wa kiume wa dada na mjukuu wa kiume. Ni kama mfanyavyo nyie kwa malkia wenu kama ni kumheshimu na kumtukuza, na sisi vivyo hivyo tunawafanyia kama ni heshima kwa malkia wetu ili kumweka mbali na uharibifu.
- Ha ha ha, malkia aliyetukuzwa! Kama ni hivyo kwa nini basi wale wanawake kwenye usaili walinipa mikono?
- Kwa masikitiko ni kuwa Waislamu wengi wamepetuka mipaka kwenye dini yao, lakini dini ipo mbali nao.

www.path-2-happiness.com

- Adam hakuwahi kumpa mkono Katarina walau mara moja! Sasa nimefahamu! Je inakutia dhiki na kukerwa kumzungumzia mwanamke katika Uislamu?
- Je unatarajia nikerwe na wewe unamzungumzia malkia!
- Niache nikuulize swali la moja kwa moja, kwanini mmempa mirathi nusu mnayompa mwanamme, kisha mnamwona eti ni malkia, mpeni sawa tu na mwanamme wala msimfanye kuwa malkia.
- Kwani wafanyakazi wote ambao mtawaajiri mnawapa mshahara sawa?
- Inaelekea kuwa unataka kutoka kwenye maudhui!
- Hapana mimi nipo kwenye maudhui yenyewe.
- Bila shaka hapana, je unatarajia nimpe mkurugenzi sawa na mtumishi?!
- Je unamdhulumu mtumishi unapompa kidogo ya Mkurugenzi?
- Hapana, mimi nafanya uadilifu.
- Na Uislamu hivyo hivyo umekuja kuweka uadilifu baina ya wanaume na wanawake, na baina ya watu wote kwa usawa, na ndio maana mwanamke akapata katika mirathi nusu ya mwanamme, na huenda ikawa ni kinyume chake. Ni juu ya mwanamme kumhudumia mwanamke na yeye mwanamke hatoi chochote, na yote hayo ndio uadilifu.
- Kwa nini mke wako asitoe nusu ya matumizi ya nyumbani?
- Matumizi ya nyumbani ni majukumu ya mwanamme, na yeye anapaswa kuhudumiwa.
- Samahani, kama ni hivyo hakuna haja ya mwanamke kusoma au kufanya kazi.
- Nani kasema hivyo?! Inabidi asome kama mwanamme, na ni haki yake kufanya kazi.
- Na kuhusu mshahara wake?
- Ni haki yake peke yake, na si juu yake kutoa matumizi.
- Ha ha ha, kama ni hivyo kiuchumi wanawake hali zao ni nzuri kuliko wanaume.
- Hapana, hawawazidi wanaume bali wapo sawa sawa, kama ambavyo maumbile yake yanatofuatiana na mwanamme, basi hali kadhalika hukumu zake ni tofauti kwa kiasi cha maumbile yake na kazi zake vile vile.
- Wasifu mzuri wa uadilifu, lakini kwa upande mwingine huoni kuwa hijabu imemdhulumu mwanamke kijamii?!
- Bali umemkirimu na kumtukuza.
- Kwa vipi, kufungwa fungwa na mavazi ambayo yanaficha uzuri wake na uke wake?!

- Vipi hali ilivyokuwa ya malkia na wana wa kike wa wafalme huko kwenu miaka hamsini iliyopita?!
- Unakusudia nini?!
- Jibu swali langu.
- Walikuwa na haki zao kamili.
- Mavazi yao yalikuaje?
- Nakusudia kuwa walikuwa wakivaa kama wavaavyo wanawake wa Kiislamu leo hii?
- Ndio, bila shaka katika hilo, kisha hata mavazi haya huvaliwa vile vile na watawa.
- Lakini tumepata maendeleo na mavazi ya mwanamke yakabadilika.
- Mavazi ya watawa hayajabadilika kwenu na nakariri hili kwa masikitiko kuwa hadhi ya kanisa imeanguka, na mavazi ya mwanamke kwenu hayajapata maendeleo bali yamerudi nyuma, tizama mashambulizi ya kijinsia, uzinifu, utoaji mimba na mfano wa hayo.
- Na ninyi hali kadhalika!
- Sisi ni wanadamu na tuna makosa yetu, lakini yaliyokuwa kwetu hayafikii walau asilimia ndogo kabisa ya mlionayo, na mengi yao kwa masikitiko ni ya kuwaiga.
- Ki vipi?
- Je utaniruhusu nitumie lugha za takwimu na tafiti mbali mbali; kwa hakika ni mpenzi wa takwimu?
- Lugha za takwimu ni zenye kushawishi zaidi, vizuri kwangu.
- Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa asilimia tisini (90%) ya wanawake ambao hawajaolewa hufanya uzinifu mara nyingi huko Ulaya na Marekani. Ama Marekani wanafunzi wadogo wa kike asilimia 48% hupata mimba katika shule za sekondari. Asilimia 88.8% katika wanafunzi wa kike katika shule za sekondari Marekani walishafanya tendo la ngono katika maisha yao. Miongoni mwao asilimia 22% kabla ya umri wa miaka kumi na miwili, si hivyo tu bali asilimia 60% ya watoto wanaozaliwa Sweden ni watoto wa zinaa tu.
- Inatosha, hili na zaidi yake nalijua katika jamii yetu ya Magharibi, lakini hali hii ipo ulimwenguni kote! Hata nyie ni kama sisi!
- Kama nilivyotaja kwa masikitiko wengi kwetu tunaelekea njia hiyo, kila mtu anavyokuwa mbali na dini basi mtu huyo anakaribia hali hii, isipokuwa tofauti ni kubwa, tena ni kubwa sana.
- Unataka kuniambia kuwa watu wa dini kwenu hawaoi na kuwa watawa kama vile

www.path-2-happiness.com

makasisi na mapapa?
- Nimekuambia mara nyingi kuwa hatuna watu wa dini katika Uislamu, bali hata Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) alioa.
- Ndio, nimeshangazwa na kuoa kwa Mtume wenu! Samahani, mke wako yuko wapi?! Wewe si umeoa?!
- Yupo shuleni; yeye ni mwalimu wa somo la fizikia katika shule ya sekondari, anamaliza kazi zake jioni saa kumi na mbili, muda wowote anaweza kufika.
- Hebu niambie ukweli, je umemlazimisha kuvaa hijabu?!
- Bila shaka hapana.
- Kwa nini mnawalazimisha wanawake wa watu kuvaa hijabu wakati wa kwenu hawavai? Ni matumizi mabaya haya ya dini kuwaingilia watu katika mambo yao!
- Mimi sijamlazimisha; amevaa kwa mapenzi yake mwenyewe, na nakubaliana nawe kuhusu matumizi mabaya ya dini katika mambo binafsi, hata Mtume wetu (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) amekataza hilo.
- Una maana kuwa amevaa hijabu bila ya wewe kumlazimisha!
- Ndio.
- Kitu gani kinamfanya avae hijabu?!
- Dini yake na amri ya Mungu wake, kisha anajilinda mwenyewe.
- Anajilinda na nini?
- Ili asiwe ni mhanga wa zile takwimu zilizopita! Ha ha ha, isipokuwa kama utahitaji takwimu nyingine, kwani ninazo nyingi.
- Hapana… inatosha, nami ninazo nyingi, samahani lakini kwetu Uingereza tunasikia wanawake wengi wa Misri wachezaji na waimbaji?!
- Ndio, nimekuambia kuwa kila tukiwa mbali na dini kwa masikitiko tunawaiga.
- Kwa nini kwa masikitiko?
- Samahani, sikusudii kuwaudhi, lakini nadhani kuwa hadhi ya mwanamke kwenu inakuwa mbaya sana kiasi cha kuwafanya wengi wenye akili miongoni mwenu wananadi umuhimu wa kuangalia balaa hili linaloendelea katika jamii.
- Balaa gani unalokusudia?!
- Kwa nini mwanamme aoe madamu anapata ayatakayo bila kuoa? Jambo ambalo linafuta na kuharibu hadhi ya familia, na kuvunja jamii yenye nguvu zaidi duniani na kuifuta.
- Nibainishie zaidi.
- Je si ukweli kuwa kumlea mbwa ni gharama ndogo zaidi kuliko kumlea mtoto

kwa watu wengi, je hawara gharama yake si ndogo kuliko mke wa ndoa?
- Wakati huo huo maumbile yao huharibika.
- Swadakta, na hili ndilo lililofikia baadhi ya jamii nyingi, je unajua kuwa kiwango cha uwezo wa kuzaa katika baadhi ya jamii imefikia chini ya mtoto mmoja kwa kila mwanamke. Jamii hizi zitakwisha na kupotea iwe ni sasa au baadaye.
- Ha ha ha, na ndio maana mmezidi kwa idadi hata zaidi ya Ulaya.
- Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) amesema: “Oeni wanawake wazuri wenye mapenzi wanaozaa.”
- Hata katika maelezo kama haya Uislamu unaingilia!
- Uislamu ni dini kamili katika mambo yote ya maisha; na ndio maana nafsi ya mwanadamu ikapata utulivu na kufurahi, wala upande mmoja haudhulumu upande mwingine ukapata tabu.
- Maelezo ya kina kiasi gani kuhusu Uislamu! Lakini hii ni aibu na fedheha na sio sifa nzuri kuhusu Uislamu?!
- Kwa vipi?!
- Maelezo, haya ya kina yanamchosha mtu kufuatilia, hiki ni kifungo kingine cha maisha!
- Lipi bora: Nchi inayofuata sheria kama vile Uingereza au nchi yenye kuongozwa na fujo tu?
- Nimefahamu unachokusudia, lakini kanuni bora ni ile inayotoa nafasi kubwa ya uvumbuzi na jitihada.
- Kama vile unatoa wasifu wa Uislamu! Kwani umetufungulia upeo mkubwa wa uvumbuzi, kutaamali na kufikiria, na mara nyingi Qur’an huwataka watu wafikiri na kuangalia mbali zaidi, historia na mienendo mbali mbali na mfano wa hayo.
- Hamhofii kuwa kama watu watafikiria kwa kina watafahamu upungufu na udhaifu wa dini yenu?
- Hilo ni sawa kwa dini za ardhini zilizotungwa na wanadamu na dini zilizopotoshwa tu. Ama Waislamu ni kuwa kila wanapozidisha kufikiri wanazidisha imani na yakini na kuabudu kwao kunazidi, kwa bahati mbaya kila kunapopungua kufikiri na dini hupungua.
- Inanishangaza imani yenu na kujiamini kwenu na dini yenu.
- Je naweza kukuuliza?
- Uliza!
- Kitu gani kinakuzuia usiingie katika Uislamu?! Mimi nahisi kama umeshakinaika

www.path-2-happiness.com

na Uislamu!

Joji alibabaishwa na swali la Jamali na akashikamanisha vidole vyake kwa nguvu, alikumbuka alichoandika Adam kuhusu kilio cha Katarina, na haja yake ya ujasiri ili achukue maamuzi, vivyo hivyo alikumbuka aliyoyaandika John Luke katika barua yake ya mwisho. Joji alipumua kwa nguvu, kwani swali hili hili ndilo alilowaandikia rafiki zake akiwauliza, sasa kama ni hivyo anahofia nini kulijibu, je ni udhaifu au kubabaika au ni ujinga au ni kutofanya mambo kwa pupa! Sababu yoyote iwayo ni kuwa hapana budi ajijibu kabla Jamali hajamjibia. Alimgeukia Jamali:

- Je utaniruhusu nisikujibu sasa hivi?
- Hili ni la kwako tu, nimekuambia hivyo nikikutakia kheri tu.
- Asante sana, nitakujibu siku mbili au tatu zijazo.
- Huna haja na sio muhimu kunijibu, la msingi na muhimu na kujibu roho yako maswali yake, kwa bahati mbaya maisha haya ya maada yametufanya kuwa ni mashine ambayo ukifikiri unachoka, na ndio maana binadamu wanaishi kwa tabu kubwa.

Joji alishusha pumzi alipoisikia ile jumla "Utakapoijibu roho yako." Na akakumbuka maneno ya kikongwe aliyekutana nae, kisha akasema:

- Kama kwamba unanielezea nilivyo:
- Samahani sijakusudia kukukera, lakini hii ndio hali ya wanadamu wanapomwacha Mwenyezi Mungu, Allah amewasema: "Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu." (20:124) na "Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni." (6:125).
- Maneno gani mabaya uyasemayo?
- Samahani sikukusudia ubaya lakini hii ni sifa tu, bali ubaya zaidi upo kumpa mgongo Mwenyezi Mungu, na hiyo sio hali ya sasa hivi tu bali ya maisha yote!
- Una maana gani?
- Watu wengi huyakimbia maisha yao kwa njia nyingi mbali mbali; kuna wengine wanayakimbia kwa kunywa pombe na starehe, na watu wengine wanayakimbia kwa kufuata ushabiki wa kidini kwa sababu hushibisha kiasi cha njaa yao ya kiroho, na wengine wanayakimbia kwa falsafa kavu, na wengine hukimbilia pasipo julikana; ili wakwepe kufikiria maudhui hayo, kwa mara ya mwisho

ninakuambia: Kitu gani kinachokuzuia na mapenzi ya duniani na akhera?

- Nimekuambia nitakujibu baada ya siku mbili au tatu.

Walipokuwa wakijadiliana mara wakasikia sauti ya mlango unafunguliwa, Jamali aliomba ruhusa kwa Joji.

- Samahani, mke wangu Aisha amefika.
- Je utaniruhusu nizungumze nae kidogo?
- Inabidi nimshauri na kuchukua rai yake.
- Katika nini?
- Najua hapendi kuzungumza na wanaume, sipendi kumlazimisha kitu ambacho hakipendi.

Jamali alitoka chumbani, alimuacha Joji katika hali ya mshangao, kilichotokea leo hii ilikuwa ni mtetemo wa nguvu, alihisi nafsi yake ikiwa imepotea na hajui afanye nini, alijiuliza siku nzima, nini kilichomfanya aende Misri? Na maswali yangu yamenifanya kujiuliza: Ninataka nini? Kwa nini ninaishi? Kwa nini tabu yote hii, Ah aah. Jamali alitoka chumbani, alimuacha Joji katika hali ya mshangao, kilichotokea leo hii ilikuwa ni mtetemo wa nguvu, alihisi nafsi yake ikiwa imepotea na hajui afanye nini, alijiuliza siku nzima, nini kilichomfanya aende Misri? Na maswali yangu yamenifanya kujiuliza: Ninataka nini? Kwa nini ninaishi? Kwa nini tabu yote hii, Ah aah.

Alipokuwa mbali kuyafikiria maswali yake, Jamali aliingia akiwa na mke wake, aliponyanyua uso wake akamuona kuwa ni mwenye Hijabu hakikudhihiri kitu kwenye uso wake ila sehemu ndogo tu.

- Huyu ni mke wangu, unataka nini?
- Jamali ameniambia kuwa unataka kuingia katika Uislamu, na ya kuwa una maswali kuhusu hadhi ya mwanamke katika Uislamu.
- Sikusema kuwa nataka kusilimu kabisa, bali nataka kufahamu tu hadhi ya mwanamke katika Uislamu?!!!
- Kama hutaki kusilimu; kwanini basi unataka kufahamu hadhi ya mwanamke katika Uislamu?!!
- Kufahamu tu.
- Maarifa yasiyomsaidia mtu hayana thamani, na elimu ambayo haimnyanyui mtu mwenyewe ni upotevu, elimu inapelekea katika kumwogopa Mungu ndio maana Mungu akasema:
- "Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni

www.path-2-happiness.com

wanazuoni.” (36:28)

- Nakusudia kuwa nilikuwa nataka kuujua tu, je maarifa na elimu hivi hivi tu ni kosa kwenu?!
- Kwetu sisi elimu ambayo hailingani na matendo haina thamani, na nadhani kuwa kufanya upuuzi tu na kukosa malengo ni maradhi ya akili na dini, mnajua vizuri.
- Unakusudia nini unaposema, ‘Kwetu sisi?!’
- Nina maana kwetu sisi Waislamu, niache niingie pale utakapo kwani mimi nina hakika huulizi tu isipokuwa kwa lengo la kutaka kuwa Muislamu.
- Una hakika gani kusema hivyo?!
- Nataraji lisikukere, Mwenyezi mungu anasema: “HUENDA ikawa walio kufuru wakatamani wange kuwa Waislamu.” (15:2). Hakuna mtu mwenye akili ambae hajampwekesha Mwenyezi Mungu na kujisalimisha kwake ila katika nafasi yake atapata kitu chenye kumkereketa kutokana na migongano ya matamanio yake na dini nyingi zilizopotoka.
- Unakusudia nini kusema: Mwerevu?!
- Mtu mnyonge, dhaifu wa kufikiri anaweza kuruka juu na akaacha migongano ya maisha yake na dini yake na maswali mbali mbali kutoka moyoni mwake akaelekea kwenye mambo ya pembeni yasiyokuwa ya msingi, lakini…
- Lakini nini?!
- Lakini Jamali ameniambia kuwa wewe ni mwerevu mno, kama alivyoambiwa na nduguye Baasim na kama alivyoona yeye mwenyewe.
- Ahsante.
- Tuingie katika maudhui yetu, “Mwanamke katika Uislamu.” Unataka tuanzie wapi?
- Anza popote unapotaka, nami nitakuuliza maswali muda ninaotaka.
- Uislamu ulipokuja Waarabu walikuwa wanazika watoto wao wa kike hai na kuwaua.
- Mwisho wa ujinga na unyama!
- Swadakta, lakini hali hii ambayo ilikuwa inatia kichefuchefu haikuwa ya Waarabu peke yake, kwani kulikuwepo na mabaraza ya wanafalsafa yakifanya vikao ili wajadili mambo muhimu sana! Je mwanamke alikuwa na roho kama mwanamme? Je ana roho ya kibinadamu au roho ya mnyama?! Walikuwa wanahitimisha mijadala yao ya kuwa mwanamke anayo roho lakini ipo daraja ya chini zaidi kuliko roho ya mwanamme. Ama Waroma mwanamme alikuwa

na madaraka kwa mwanamke ima amuuze mke wake au ampe talaka, amkubali mwanae au amkatae, na mwanamke kwa Wagiriki alikuwa hana haki ya kurithi kamwe.

- Kwa masikitiko kabisa, umesema kweli, historia chafu kabisa!
- Dini zote za mbinguni zimeleta uadilifu kwa mwanamke, lakini Mayahudi wamepotosha kitabu chao, kikawa kitabu chao kilichopotoka kimejaa mambo ya kufikirika kuhusu ngono na dhulma yenye kuchukiza na chungu kwa mwanamke.
- Levi amenielezea haya yote, na nimesoma mambo mengi kama haya.
- Levi ni nani huyo?!
- Mwanamke wa Kiyahudi mwenye heshima sana.
- Ni kiasi gani napenda afurahi na akirimiwe na Uislamu.
- Hapana, sidhani, hata hivyo endelea.
- Funguo za mioyo ipo katika mikono ya Mungu, tukamilishe na Ukristo ukapotoshwa vile vile, na kwa masikitiko Ukristo nao umejaa dharau kwa mwanamke.
- Mfuatano mzuri.
- Baada ya hapo Uislamu ukaja; ukamkirimu mwanamke ambapo hakuna dini iliyomtukuza mfano wake, hakikupotoka chochote chake; Mwenyezi Mungu pekee ndie aliyetoa dhamana ya kukihifadhi.
- Inakinaisha na kushawishi kuwa Uislamu haujapotoshwa, na nina maswali, lakini ningependa ukamilishe kwanza.
- Mwanamke ulimwenguni hakuhisi utukufu kama alivyokuja kuhisi pindi Uislamu ulipokuja. Ulaya ilipoingiliana na Waislamu ikajifunza kitu katika kumtukuza mwanamke, walijifunza uadilifu na elimu mbali mbali, lakini ikapambana na upotofu uliopo kwenye vitabu vyao vitakatifu na mafundisho ya Kanisa. Kwa bahati mbaya hawakusilimu, na hivyo basi kutafuta mfumo wa kumtukuza mwanamke ambapo akili zao ziliwaelekeza kudai usawa.
- Kwa maana hiyo akili ya mwanadamu imekuwa juu kuliko akili za dini nyingi?
- Bila shaka hawakuweza kubadilisha maumbile yake na tabia yake na majukumu yake ili yalingane na usawa huo wanaodhania, hivyo basi wakaamua kumpa majukumu ya kazi kama ya mwanamme pamoja na kazi zake kama mwanamke! Cha kushangaza na ajabu ni kuwa anafanya kazi kama mwanamme pamoja na kazi zake kama mwanamke kwa mshahara nusu au robo! Laiti wanaume wangeacha kupunguza ujira wake na kumkalifisha asiyoyaweza. Hayakuwa hayo

www.path-2-happiness.com

tu bali walimtumia na kuchukua kutoka kwake bila ya ndoa, na hivyo kubadilika kutoka kuwa ni mke anayeheshimiwa na kulindwa na kuwa ni hawara mwenye kutumiwa hovyo na hizo taasisi za usawa na haki za binadamu zikapeperushwa na zikaja karibu kubadilisha hali hii mbaya. Katika hali hiyo zikataka na kudai usawa katika malipo na mishahara, juu juu wakaonekana wamefanikiwa lakini ukweli hawakuwa wamefanikiwa, na waliweka masharti ili mume asiweze kuchukua haki za mke wake, wakagundua kuwa ambae anachukua haki zake sasa amekuwa ni hawara bila hata mafungamano yoyote ya kisheria.

- Unachokisema hakifanyiki nchi zote za Magharibi.
- Ndio, hutekelezwa sehemu kubwa tu, ingawa bado kuna wengine ambao maadili yao yanawakataza katika mambo kama haya, lakini balaa zaidi ni kuwa yanamtetea kwa jina la usawa, wakati mwingine kwa jina la starehe na kwa jina la uhuru kutokana na utawala wa mwanamme ili awe huru zaidi kiasi cha kumfanya kufikia kiwango ambacho mnyama atastahi wala hatoridhia kwa nafsi yake.
- Unakusudia nini?!
- Samahani kama maneno yangu makali au kuonekana kama nimewadhalilisha, lakini ninachomaanisha ni kuwa mwanamke kwa masikitiko amekuwa kama ni chombo cha kuchezea tu na kukiharibu kwa jina la usawa na kuchukua haki zake, vinginevyo utawezaji kufasiri kuwepo kwa chaneli mbali mbali za ngono na filamu chafu na biashara ya ngono?
- Inaweza kufasiriwa kuwa ni aina ya kushangazwa na kiumbe huyu mzuri!
- Hivyo unakiri kuwa kiumbe huyu mzuri anatofautiana na mwanamme, na usawa baina yao ni kumdhulumu mwanamke na kumdhulumu mwanamme. Ama mimi nafasiri kuwa mwanamke katika jamii hizi baada ya kunyang'anywa haki zake za kiuchumi, na baada ya kuanza kufanyakazi zake anazotakiwa kama mwanamke na zile anazolipwa katika kufanyakazi akaibiwa tena haki zake za kibinadamu na kufanywa kama ni bidhaa ya kuchezea, vinginevyo tutafasiri vipi kuachwa uchi au nusu uchi katika uso wa maduka mengi katika nchi nyingi, kama vile ziwekwavyo bidhaa, samani au magari!
- Matendo haya ni mabaya sana lakini hayawakilishi jamii zetu kamwe.
- Kwa uchache ni matendo ambayo yamewekewa sheria na taasisi, na hijabu kwa wanaoamini lakini inakatazwa kisheria vile vile hivyo basi serikali au sheria ndio ambayo inaruhusu mwanamke kuwa ni bidhaa ya kuuzwa na kununuliwa na haimruhusu mwanamke wa Kiislamu kuvaa hijabu.

- Mimi vile vile sikubaliani na matendo hayo ya dhulma yanayofanywa na baadhi ya nchi za Ulaya.
- Kwa maana hiyo wewe ni gaidi kwa vigezo vyao, nisameheni nimerefusha lau kama sio mume wangu kutaka hivyo ili huenda nikawa ni sababu ya kusilimu kwako basi vinginevyo nisingefika huku.
- Nina baadhi ya maswali ya haraka haraka, nimewauliza watu wengine lakini ningependa nijibiwe na mwanamke.
- Karibu, uliza.
- Wewe ni mtaalamu wa fizikia, yaani elimu ya kisasa ambayo imewajia kutoka kwetu na ikanyanyua viwango vyenu, pamoja na hayo unavaa hijabu, kwani umelazimishwa kufanya hivyo?! Au ni kama vile hijabu ya watawa kwetu ambao uvaaji wao hauna maana ya kujihifadhi lakini ni mavazi tu kwa desturi zao?! Au ni kwa sababu mnaishi katika jamii yenye matamanio ambayo huna budi kuvaa mavazi ya aina hii vinginevyo utakuwa ni muhanga wa kushambuliwa na wanaume?! Au nini?!
- Ha ha ha, kwanza "Elimu au sayansi ni urithi wa wanadamu; kabla ya elimu hizi za kisasa kuja kutoka kwenu ziliwajia kutoka kwetu mlipokuwa kwenye kiza kinene. Ama kuchukuliwa, kunyang'anywa na kushambuliwa na wanaume wewe unajua kuwa kuna mahusiano ya moja kwa moja na suala la kwenda uchi, ukitaka takwimu ambazo zinaunga mkono hilo tutazungumzia, ama kwangu mimi ninavaa hijabu kwa ajili ya kufuata dini na kwa elimu niliyo nayo ni kuwa hiyo ni katika furaha ya dunia na akhera. Hapa duniani utapata furaha na utulivu na akhera fadhila na utukufu kutoka kwa Mtukufu Aliyetukuka.
- Daima mnarudia rudia maneno, furaha ya duniani na akhera.
- Ndio, furaha haijui ila yule aliyeijaribu.
- Huenda ikawa hivyo, lakini je utaridhika kama Jamali atakuolea mke mwingine kama alivyofanya Mtume wenu?!

Aisha alimuangalia Jamali aliyesimama pembeni yake kimya, kisha akaendelea:

- Sidhani kama Jamali atafanya hivyo, na natamani asiniolee.
- Lakini Mtume wenu alioa wake wengi?
- Ndio ameoa wake wengi, na mmoja wa wake zake ni Mama wa Waumini jina lake kama langu Aisha.
- Kama ni hivyo kwa nini hutaki Jamali amuige Mtume wenu na kukuolea?!

www.path-2-happiness.com

- Uislamu haukunitaka mimi ila niwe mwanamke, na haki yangu ni kuona wivu, wala haukunitaka kuwa dhalili siwezi kujieleza na mahitajio yangu na ninayopenda, lakini nina yakini kuwa kuoa wake wengi ni bora kuliko kuwa na hawara wengi.
- Na kutooa mke zaidi ya mmoja ni bora zaidi.
- Naamini kuwa kuna haja kama ni sehemu ya maumbile ya baadhi ya wanaume kuoa zaidi ya mke mmoja. Kuoa wake wengi hakupo kwa Waislamu peke yao tu, bali katika dini zote takriban, tofauti kubwa iliopo ni kuwa katika dini zilizotangulia hakuna idadi maalumu. Nabii Sulaiman alioa wake elfu moja, Adam alioa wake kumi na tatu, Dawud alioa wake tisini na tisa, katika Uislamu kuna idadi maalum, yaani wasizidi wake wanne tu.
- Sisi kwa sasa hatukubali wake wengi na mifumo yote, sheria na serikali imekataza.
- Kitabu chenu kitakatifu kina mifano mingi ya wake wengi, watu wa dini wamechoshwa na tafsiri hiyo, baadhi yao wamesema: Haya ni makosa ya wanadamu na wakazungumza juu ya manabii. Wengine wakasema: Ilikuwa ni haja tu ya kihistoria kwani kulikuwepo na vita vingi sana na wanawake walikuwa ni wengi sana na wanaume ni wachache, wameacha ukweli ulivyo sasa kuwa vita ni vingi hivi sasa. Wakatokezea wengine wakasema: Bali Mwenyezi Mungu amelirudi hilo (Mungu atusamehe kwa hilo) Na hivyo kumfanya Mungu mpungufu hajui haki ametakasika kwa wanayo yasema.
- La msingi ni kuwa sisi tumeiendeleza dini yetu na kanuni zetu; ili kukataza watu kuoa wake wengi.
- Nzuri "Tumeendeleza dini yetu." Kwa asili ni kuwa dini ya kweli inafaa kwa zama na mahala pote wala haihitaji kuendelezwa ila kitu kilichokuwa na upungufu tu;
- "Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini." (5:3) Sisi hatuiendelezi dini yetu; kwa sababu dini yetu imekamilika.
- La msingi tu ni kuwa tumeendeleza mifumo yetu, kanuni zetu ili tusiruhusu wake wengi kwa dhulma.
- Ndio katika nchi nyingi za Ulaya na Amerika mmekataza wake wengi katazo zuri lililokuwa wazi, na mkaruhusu mahawara ruhusa pana.
- La msingi sisi tumekataa wake wengi.
- Na hata maisha yaende vizuri kwa kufuata tabia ya mwanadamu na ya kijamii kufuata haja ya baadhi ya wanaume zaidi ya mke mmoja mkaruhusu hawara zaidi

ya mmoja, bali lililo la hatari zaidi ni kuwa baadhi za nchi zimeruhusu waume wengi badala ya wake wengi na kuruhusu ndoa nyingi na kukataza wake wengi. Bila ya shaka umemtukuza mwanamke awe na waume wengi na sio kuwa na hawara.

- Vizuri, lakini elimu hii ya kisasa ambayo umesoma na kufundisha huenda ikawa inapingana sana na dini yenu!
- Elimu ipo kinyume na dini yetu! Wewe hujui dini yetu au hujui chochote kuhusu sayansi! Kwa hali yoyote ile Jamali anajua zaidi yangu kwa uhusiano wa dini na sayansi. Mimi nimeombwa nizungumze kuhusu mwanamke tu, na sikutaka kufanya hivyo ila aliponiambia kuwa kufanya huku utakuwa umefanyia kazi dini; naombeni ruhusa nataka kufuatilia masomo ya mwanangu.

Aisha alitoka, Joji akamgeukia Jamali huku akitabasamu.

- Nakupongeza kwa mke ulie nae, ila anafaa kuwa mwanamme na sio mwanamke.
- Ha ha ha.
- Una nini? Mbona unacheka?!
- Kumbe unajua mwanamke sio mwanamme sasa kwa nini mnalingania usawa?! Niamini hakuna aliyekuwa mpole kuliko yeye wala zaidi mwenye huruma kuliko yeye, yeye ni mtu wa dini; na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amemuusia anitii.
- Kwani Mtume wenu hakuwausia umfanyie wema?
- Bali ameusia kwa kusema: "Mbora wenu ni mbora wenu kwa familia yake na mimi ni mbora wenu kwa familia yangu." Bali ametaja kuwa yeye ni mbora wa watu wa familia yake, nimefurahishwa na mjadala wako, lakini nataka kwenda kuswali alasiri.
- Sasa hivi ni saa kumi na nusu, ikiwa ni sawa kwako tutoke pamoja usali, nami nitembee Cairo kwa muda wa saa moja hivi, kisha twende kwa Mustafa kwani amenialika chakula cha usiku na sijui kwanini.

(4)

Joji alibaki garini akimsubiri Jamali amalize kusali, baada ya kumaliza sala akawa anawaangalia watu mbali mbali waliosali nje ya msikiti, alimuona mtu mmoja mwenye sura ya Kizungu na akamuashiria, na akamfuata, akamjibu kwa kiingereza kibovu:

- Karibu, mimi ni William, wewe unatokea wapi?

www.path-2-happiness.com

- Mimi ni Joji kutoka Uingereza.
- Na mimi ni kutoka Ujerumani.
- Lakini ulikuwa ukisali pamoja na Waislamu!
- Ndio mimi ni Muislamu wa Ujerumani.
- Kutoka Ujerumani au ni Mmisri unayeishi Ujerumani?
- Nusu ya Waislamu Ulaya ni wenyeji wa huko na mimi ni mmoja wao, idadi ya Waislamu Ujerumani ni milioni nne, yaani ni karibu ya asilimia tano ya wakazi wote.
- Najua hilo, waislamu kwetu Uingereza ni zaidi ya milioni mbili, yaani asilimia tatu, lakini swali langu ni je wewe ulikuwa ni Mkristo?
- Baba yangu na mama yangu walikuwa Wakristo, ama mimi nilikuwa mkana dini, namshukuru Mwenyezi Mungu kisha nikasilimu, nikawa mwenye furaha na mimi nipo hapa kuusoma Uislamu.
- Nini kilicho kufanya ukawa Muislamu?!
- Ni swali nililokuwa nikijiuliza mara kwa mara, ninaweza kufupisha mvuto wangu kwa Uislamu katika utafiti wa maneno matatu, nayo ni: Ukweli (hakika), furaha na uadilifu.
- Je umeupata katika Uislamu?! Kwa vipi?!
- Ndio nimeupata, ukitaka maelezo zaidi unaweza kunitembelea baadae, kwa sasa naomba radhi kwani nina ahadi pamoja na mmoja wa marafiki zangu, na hii ni kadi yangu, kuna maelezo yote kuhusiana nami.
- Asante sana, samahani kukusumbua.

Joji alirejea kwenye gari na kumkuta Jamali akimsubiri.

- Umerudi muda gani?
- Nimekuona ukiongea na mtu, sikupenda nikukate, la msingi ni kuwa hivi sasa ni saa kumi na moja unusu, je tumebaki na muda gani kabla ya ahadi yako na Mustafa?
- Saa nzima takriban, ukweli ni kuwa nimechoka sana na ningependa kwenda hotelini kupumzika, lakini Mustafa aliipa umuhimu sana kwa sababu ambayo siifahamu; na nikampa ahadi ambayo sitaki kwenda kinyume nayo.
- Vizuri sana, Qur'an pamoja na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) wamehimiza sana kutekeleza ahadi, huenda katika hilo kuna kheri, nashauri muda wa saa moja iliyobakia tukapumzike katika matembezi ya boti kwenye mto Nile, kwani miadi yenyewe ni karibu na mto Nile.

- Fikra nzuri.

Walikwenda Nile, wakakodisha boti kwa muda wa saa nzima hivi, wakaanza matembezi yenye utulivu ambapo Joji alihisi kupumzika na kupata utulivu, kadhalika akahisi kuwa maarifa mengi aliyoyapata kwa ghafla tu yameanza kujipanga yenyewe kichwani mwake, kisha walipomaliza wakaelekea kwenye miadi ya Mustafa.

- Nakushukuru, matembezi haya yalikuwa ni mazuri sana na kwa wakati wake.
- Inshallah utakuwa umepumzika kidogo.
- Ndio, isipokuwa tabu na msukumo wa maswali unaniandama kila ninapopumzika.
- Maswali gani?
- Je naweza kukuuliza swali?
- Karibu, uliza.
- Je wewe huwa unajiuliza kwa nini umeumbwa?
- Bila shaka … mara nyingi…
- Utaijibu vipi nafsi yako? Au utalitoroka vipi swali hili?
- Kwa nini nilitoroke na mimi nina majibu yaliyo wazi?
- Ni jibu gani hilo?
- Anasema Mungu Aliyetukuka: "Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi." (56:51)
- Unakusudia kuwa mimi ni kiumbe kwa kusali na kufunga tu!
- Hapana, wewe ni kiumbe wa kufanya ibada kwa maana yake pana, na haikuwa swala na kufunga ila ni mafungu muhimu tu ya ibada.
- Vipi?
- Ibada inakusanya kila kitu katika maisha yetu; haifanyiki katika siku maalumu tu au katika sehemu fulani tu au katika umri fulani, bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametufundisha kuwa hata kama mume atamwingilia mke wake na kustarehe nae, basi mtu huyu atapata malipo.
- Ehe, vipi?
- Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametubainisha hilo kwa kusema: "Je, ingekuwa anafanya hivyo kwa njia ya haramu angepata madhambi, vivyo hivyo akiweka katika halali atapata ujira pamoja na kumsafishia nia Allah (Subhaanhu wa Ta'ala). Hivyo basi maisha yote ya mwanadamu yamekuwa ni kwa ajili ya Allah (Subhaanhu wa Ta'ala): Swala na ibada zangu, bali uhai na umauti; kama alivyosema Allah (Subhaanahu wa Ta'ala); "Sema: Hakika Sala yangu, na ibada

www.path-2-happiness.com

zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (6:162).

- Kwa nini tunaishi?
- Ninaweza kukujibu kwa jibu lililotangulia na ni kuwa mkweli, ninaweza kukuambia: Kwa ajili ya kuimarisha ardhi na maisha na kuyastawisha, na uhakika ni kuwa kuimarisha ardhi na maisha na kuyastawisha ni katika ibada zilizo muhimu sana, Allah (Subhaanahu wa Ta’ala) amesema: “Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo.” (11:61)
- Kwa masikitiko tumeshafika, ila mjadala wetu tuukamilishe kesho, nitakusubiri saa nne asubuhi; mimi ninataka kupumzika kidogo na ahadi yangu ni saa tano pamoja na shirika la mwisho.
- Sawa, tumekubaliana.

Joji aliingia kwa Mustafa, ambae alimkaribisha.

- Kila kitu kiko tayari, chakula cha usiku kitakuwa katika moja ya hoteli, na wote wanatusubiri huko.
- Vizuri.
- Inaelekea umechoka, tumekutayarishia kitakacho kuchangamsha na kukuburudisha na kukurejeshea uhai wako, uchangamfu wako, kwa masikitiko ni kuwa sisi Wamisri tunasahau pindi tunapotembelewa na marafiki zetu kutoka Ulaya kuwa maisha ya Wamisri hayawafai watu wa Ulaya.
- Vipi?
- Mimi nimesoma Chuo Kikuu Marekani nayajua maisha yenu vizuri sana, utaona leo hii kitakachokufurahisha.

Katika moja ya hoteli Mustafa alisimamisha gari lake, na akatembea katika maingilio ambayo taa za rangi rangi zinawaka, kulikuwa kuna muziki ukienea kila sehemu, Mustafa aliweka mkono wake katika bega la Joji na akamkaribia ili aweze kumsikia.

- Tuna jukwaa letu maalum lenye kututosheleza.

Walifika sehemu hiyo waliyotayarishiwa akakutana na wanawake wanne alioonana nao asubuhi kwenye usaili wakimsubiri.

- Nadhani umeshafahamiana nao asubuhi, nimewaleta hapa ufahamiane nao kwa ukaribu zaidi, huyu ni Samira na huyu ni Manal na Aisha na Diana.

Samira alimpa mkono huku akitabasamu, Joji nae akampa mkono na kutabasamu, kisha akawapa mikono wengine waliobakia na kukaa.

- Nakukumbusha, mimi ni Manal na umri wangu ni miaka ishirini na nne, nimekuja kukuhudumia.
- Vizuri kila mmoja ajitambulishe kama Manal alivyofanya.
- Mimi ni Samira Nudhmi umri wangu ni miaka ishirini na tatu, nimekuja kukufurahisha.
- Mimi ni Aisha Khalid umri wangu ni miaka ishirini na tano, nimekuja kwa ajili yako.
- Na mimi ni Diana Saamih umri wangu ni miaka ishirini na tano.
- Vizuri karibuni, na mimi ni Joji na umri wangu unakaribia miaka arobaini.

Mustafa aliamka kutoka kwenye kiti chake.

- Nawaombeni ruhusa nitakuja baada ya muda kidogo, Joji furahia muda wako.
- Kikao hiki kwangu ni cha ghafla, sijajua kuwa kama tutaonana hapa.
- Mustafa ametuambia atatutoa sisi kama ni zawadi kwako.
- Sijafahamu.
- Wewe uko peke yako, na sisi tumekuja kwa ajili yako.
- Aha, nimefahamu, na kwa kiasi gani nyie mmejitayarisha kunihudumia na kunifurahisha?
- Ha ha ha, kwa kiasi kikubwa.
- Taka utakacho na utaona mipaka ya utumishi.

Joji alinyamaza akiangalia nyuso za wale wasichana wanne, ni wazuri kabisa na tabasamu zao zilimfitinisha katika kiasi kikubwa na kumvutia, lakini alikuwa akihisi kichefuchefu, akaamua kuvunja ukimya na kuzungumza nao.

- Nitawaomba baadhi ya vitu, nitaanza na Aisha.
- Mimi ni rehani kwa ishara yako.
- Nina Swali: Je jina lako silo jina la mke wa Mtume wenu?
- Ndio, kwa nini unauliza?
- Hivyo basi sina shaka kuwa unamuiga kwa metendo yako yote?!
- Kwa nini swali hili? Omba utakacho nami nitaitikia wito wako.
- Ombi langu ni unijibu…
- Nigeukie mimi, mimi ni Samira Mkristo, unataka nini kwa maswali haya ambayo yana mjeruhi rafiki yetu?
- Unamtetea?
- Ndio, rafiki yangu, na ni haki yangu kunyanyua maswali yako yanayojeruhi.
- Unamtetea ili umuondoshe na hali hii, na wewe unamuona kuwa yeye ni kafiri

www.path-2-happiness.com

wa motoni katika Jahannamu, kwani Masiya hakumkomboa na madhambi yake!
- Mimi ni Mkristo lakini kwa hakika ni Msekula sijali isipokuwa ni elimu na matokeo yake.
- Kwa sababu unapenda elimu kama unavyosema; hukukamilisha masomo yako ya sekondari achilia mbali ya chuo kikuu, na uwezo wako wa kipekee (fani yako) ni uzuri tu!
- Je unataka kuujaribu uzuri huu? Au kuonja au kuufurahia?!
- Huenda, lakini nina ombi, sio hicho ufanyacho kinagongana na Ukristo?
- Nimekuambia kuwa mimi ni Msekula.
- Unakusudia mpinga Mungu na dini?.
- Si neno, sijui tofauti zake.
- Lakini kuuonja uzuri wako si kunapingana na sheria na mfumo wenu na tabia njema?
- Sisi tunajua kuhusu sheria za hapa kuliko wewe, na suala la tabia ni la kiwango tu.
- Ki vipi?
- Linaloonekana kuwa ni kinyume cha maadili kwa mtu fulani, kwa mtu mwingine ni maadili ya hali ya juu.
- Wala hakuna misingi kamwe?
- Msimamo wangu pekee ni maslahi yangu tu.
- Huu ndio msingi wangu, wengi katika wakanao dini ni watu wa maslahi tu.
- Na je sasa unataka kujua furaha ili uonje uzuri?
- Swali langu sasa ni kwa Manal.
- Sihitaji maswali yako, tunalolifanya sasa ni fedheha na kilichotusukuma ni haja zetu na Mustafa mtu mbaya sana, Aisha simama tuondoke.
- Sasa kwa nini mnasimama?

Aisha aliondoka na Manal, na ukimya ukaenea na sauti ya muziki iliyokuwa juu ikaenea sehemu ile, ukimya ule ulivunjwa pindi alipofika mhudumu.

- Mustafa ametaka niwaletee vinywaji vya kupasua roho, lakini ameniambia kuwa mnipe uchaguzi, sasa mnataka nini?
- Samahani, mimi sinywi.
- Hunywi! sasa kwa nini umekuja na hawa watoto wazuri, kwa kila hali ni kuwa hafla ya kucheza itaanza baada ya nusu saa, na Mustafa ameniambia kuwa nikujulishe kuwa yeye amewaacha ili upate muda wa kustarehe kwa wakati wenu. Yeye atakuja saa mbili unusu ili aone umahiri wako katika kucheza, ukibadilisha

rai yako na ukataka kinywaji basi niashirie nitakuja.
- Hunywi! Wewe sio Mkristo wala sio Mzungu! Nilikuwa nataraji uwe laini katika kuutumia uzuri huu baada ya kunywa!
- Kwa nini? Kwani ni lazima Mkristo kunywa?!
- Kwa kiasi fulani hata maaskofu hunywa kwa ajili ya ibada na wanaamini kuwa ni kinywaji kitakatifu.
- Je na kwa Mzungu kuna ulazima gani?
- Kwa ujumla ndio, Wazungu hawafanani na Waislamu siasa kali, Mustafa alipata shida kumkinaisha Aisha na Manal waje, na sasa majibu yako haya yamewavunja sana na huenda yakawafanya wawe Waislamu wa siasa kali.
- Ooh, yaani mimi ndio nimekuwa nautangaza Uislamu wa siasa kali?!

Diana pekee ndie aliyekuwa kimya na hakuzungumza hata herufi moja muda wote wa kikao. Joji alimgeukia huku akishangazwa na hali yake, kwani yeye pekee ndie aliyevutiwa nae asubuhi, pekee ndie mtaalamu wa fani ya kompyuta.

- Na vipi kuhusiana nawe? Wewe uko peke yako!.
- Kwa nini mimi tofauti na wao?
- Msomi na mkimya!
- Lakini mimi ni sawa na wao tu, ni bidhaa tu na zawadi tunayokupa.
- Kwa nini nawe umekubali kuwa ni bidhaa?
- Ili kuikimbia nafsi yangu.
- Kwa vipi?
- Mimi nimechoka sana na ni mgonjwa, usia wa mjomba wangu kwa Mustafa ni kunitoa kwenye msongo na fundo la nafsi kwa kufurahi na kustarehe.
- Na wewe nini rai yako?
- Ningekuwa najua maana ya maisha ningekuwa na rai! Lakini ni kama vile Pia katika upepo wa maisha yananigeuza bila ya maana, na huenda tabia ya mjomba wangu ya kuratibu jambo hili pamoja na Mustafa ni bora kwangu!
- Ni bora ukayakimbia maisha yako na kupoteza umri wako na kugeuka kuwa bidhaa?!!
- Huenda ukawa hujui maana ya kupotea na kupoteza malengo, vinginevyo msingeniambia hivyo, bora kujinyonga kuliko hali niliyo nayo.
- Lakini ninyi kwa dini yenu mnajua ni kwa nini mnaishi? Na kwa nini mmeumbwa?
- Mimi sijui na nitashukuru kama utaniambia.

www.path-2-happiness.com

- Rafiki yangu Muislamu leo hii ameniambia kuwa mmeumbwa kumuabudu Allah, na kwa maana ya kifalsafa ni vizuri kuabudu.
- Lakini mimi ni Mkristo Muorthodoksi na sio Muislamu.
- Waislamu wawili wameondoka, na sasa inawezekana ukafurahi zaidi; muda wa kuanza kwa hafla umekaribia.
- Kwa sababu nyie ni Wakristo wawili kama mimi, nakubaliana nanyi tufurahi usiku huu lakini kwa sharti la Diana kunikinaisha.
- Kukukinaisha na nini?
- Unanikinaisha kuwa furaha ni katika kufurahia uzuri wako, na kunywa pombe na kusahau dunia na kuyakimbia maisha ya uovu kuelekea neema ya kusahau.
- Samira anaweza kukukinaisha zaidi kuliko mimi.
- Sharti langu ni kuwa wewe Diana unikinaishe.
- Samira ni katika wasichana wazuri hapa Misri, nae ni mchezaji mahiri atakusahaulisha dunia yote, haswa akinywa, je umekinai?!
- Nimeanza kikinai, lakini kwa nini useme Samira, unaonaje kama nikitaka kunywa pamoja nawe kwanza kisha nicheze nawe?
- Pamoja na kuwa sijawahi kunywa maishani lakini nimekubali, mimi nahisi dhiki kubwa sana, napenda kuondokana na maswali haya yanayoangamiza maisha yangu.
- Maswali gani hayo?
- Maswali mengi ya kila mara tokea muda mrefu kuhusu sababu ya kuwepo, na kuumbwa, na maana ya maisha, na mfano wa hayo.
- Je unaamini kuwa kunywa kwako, kucheza kwako au hata matendo yako ya kijinsia yanaweza kukusahaulisha maswali yako?
- Kwa uchache na kwa muda mfupi, mimi nipo tayari kwa uyatakayo; hivyo siongezi au kurefusha maswali yako yenye kuchosha.
- Mimi ni kama wewe nimechoshwa na maswali, lakini nimekinaishwa kuwa kuyakimbia ni mfumo wa wapumbavu, na kilicho sahihi zaidi ni kukabiliana nao na kujibu maswali hayo.
- Nami hali kadhalika.Nimechoka.
- Wewe ni mzuri, mwenye adabu na msomi na akili yako inafanya kazi, usiharibu uzuri wa mambo yote haya kwa uzuri tu wa kiwiliwili chako.
- Mimi nitaondoka sasa hivi, asante sana kwa nasaha zako na udhalilishaji ulionizawadia, kisha akasimama na kuondoka.

- Nimebaki mimi na wewe tu, na mimi nipo tayari je unapenda tucheze na tustarehe hapa au hotelini kwako?
- Yuko wapi Mustafa?
- Mustafa ametuacha ili tustarehe pamoja, haya.
- Haya twende.

Joji alisimama pamoja na Samira, pindi Samira alipokuwa anaelekea jukwaani kucheza Joji aligeuka na kuelekea mlangoni ili atoke, alipotaka kutoka mara alimwona Mustafa akiwa amesimama huku amemshika msichana, alimtupia macho haraka haraka na akageuka akitoka nje.

- Joji nisubiri, una nini rafiki yangu?
- Hamna kitu, nimechoka na ningependa kwenda hotelini kupumzika.
- Njoo panda ili nikupeleke.
- Vizuri, haraka ikiwezekana.
- Nini rai yako kuhusu wale wasichana?!
- Ni wazuri mno.
- Nimekuacha ili upate wasaa wa kufurahi nao.
- Nimefurahishwa nao kiasi cha kutosha.
- Ni nani aliyekufurahisha zaidi?
- Wote, je wewe ni Muislamu?
- Ndio, na jina langu ni jina la Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam).
- Ni fedheha kwa Waislamu!
- Unasema nini?
- Hamna kitu, wewe ni Muislamu kama rafiki yangu Jamali lakini unatofuatiana nae sana.
- Nimekuambia kuwa yeye ni siasa kali na mimi nimesoma nje na nimefunguka zaidi.
- Naomba ufanye haraka kwani najihisi kuchoka sana na ninataka nifike hotelini haraka.
- Ahadi yetu kesho saa ngapi?
- Hatuna ahadi kesho; nina shughuli nyingine, nitakupigia simu.

Joji alifika hotelini nae akipiga mikono yake makofi akishangazwa, siku ilikuwa ndefu kwake, siku iliyojaa migongano na mambo ya kushtukiza. Alijihisi mzito, alipofika tu alijitupa kitandani, hisia ya woga wa maswali yake ilimjia kwa nguvu, alimkumbuka Diana msomi aliyevamiwa na shaka

www.path-2-happiness.com

kama yake, akakimbilia starehe (ili ajisahaulishe) kisha, akakumbuka swali alilowatumia rafiki zake, na swali hilo hilo aliulizwa na Jamali leo hii: "Nini kinachokuzuia kuingia katika Uislamu?

Aliendelea katika kufikiri na hakuhisi chochote ila ilipotimu saa mbili unusu asubuhi, alipoamka kutoka usingizini na kujikuta kuwa alilala pamoja na nguo zake akiwa katika hali ya kusikitisha.

-

-

MAZUNGUMZO YA ROHO

www.path-2-happiness.com

17 MAZUNGUMZO YA ROHO

www.path-2-happiness.com

MAZUNGUMZO YA ROHO

(1)

Joji alinyanyuka toka kitandani mwake akiwa amechoka sana, alikuwa akihisi uchovu na ni bora kama angebakia chumbani kwake siku nzima asikutane na mtu yeyote, hata hivyo alikuwa katika changamoto na Kakhi na aliazimia amshinde na awe juu yake zaidi katika majukumu yake magumu. Ni bora mambo yake binafsi ayatenge na anayopambana nayo miongoni mwa khofu na kubabaika na uchovu, vinginevyo vitamuharibia kazi yake na mustakabali wake.

Ahadi yake leo hii na Jamali saa nne asubuhi, hivyo basi anao muda wa kutosha kupata staftahi na kuangalia barua pepe, hakutaka kuondoka chumbani, na hivyo basi kuwapigia watu wa Buffet hapo hotelini na kuwaomba wampelekee staftahi yake hapo chumbani, kisha baada ya hapo akaelekea kuoga haraka hadi muda staftahi utakapofika…..

Baada ya dakika chache mhudumu aligonga mlango, na akaingia akiwa na vyakula na kuweka mezani na kutoka. Joji akachukua staftahi yake wakati huo huo akiwa anaangalia barua pepe, akapata barua kutoka kwa Katarina:

"Mpenzi Joji

Pamoja na muda mfupi tu wa safari yako, ninahisi nimekutamani sana, nakuhitajia sana, na siwezi kusubiri mwezi mzima hadi urejee, nipo katika mtanziko na sijui lipi la kuamua, nami nina haja kubwa na wewe inatosha kukujulisha kuwa mimi Mkatoliki mtu wa dini nimelia sana nikiwa nasikiliza tarjumi ya kitabu kitakatifu cha Waislamu wanachokiita Qur'an, ninaishi katika hali ya wasiwasi mkubwa sana. Nina haja sana nawe.

Mpenzi wako Katarina."

Joji akajibu:

"Mpenzi Katarina,

Nadhani nitarejea hivi karibuni tu, ahadi yangu ya jana ilikuwa mbaya sana, mfano mbaya kwa Waislamu, sijui tatizo lipo kwa Waislamu au lipo kwenye dini yao? Namchukia Mustafa ambae nilikuwa nae kwenye ahadi ya jana, nitajaribu kurejea katika muda wa siku kadhaa zijazo, sali kwa ajili yangu. Sitaki kufeli kwenye changamoto hii pamoja na Kakhi.

Mpenzi wako Joji.”

- Alipata barua nyingine kutoka kwa John Luke:

“Rafiki yangu Joji,

nimepata barua yako, na nimefurahi kuwa rai yangu kuhusu wizi ilikuwa ni sahihi, na ole wako kufanya maamuzi ya haraka haraka, ama kuhusu hali ya mwanamke sina tatizo lolote, tatizo langu lipo kwenye uhuru katika Uislamu! Ikiwa una mtazamo wowote au rai yoyote nijulishe.

John Luke.”

- Akamjibu,

“John Luke,

Huenda ukashangazwa kuwa kwa muda mfupi nimebadilisha rai yangu!! Ndio katika Uislamu hakuna dhulma kwa mwanamke, bali Uislamu umekuja kwa yenye kunasibiana na maumbile yake na tabia yake. Pamoja na kuwa hatujazoea hilo katika jamii zetu mbaya, lakini ni mfumo kamili unaojitegemea kabisa. Nimezungumza katika suala hili na kujadili sana na nimekuwa na hakika kuhusiana nalo, hata hivyo sijasoma wala kujadili kuhusu suala la uhuru. Ikiwa umepata chochote nitumie, nami nitakutumia hali kadhalika nitakayoyapata, nitajaribu kuulizia hilo na kusoma pia.

Joji.”

Alipokuwa anafuatilia barua zake simu ya chumbani ililia, mfanyakazi wa mapokezi alimjulisha kuwa kuna mtu anayemsubiri mapokezi, aliangalia saa yake akakuta ni saa tatu na nusu, akashangazwa, je inawezekana Jamali akaja kabla ya ahadi yake kwa muda wa nusu saa.”

- Samahani ni nani anayenisubiri?
- Kuna msichana anakusubiri.
- Ni nani huyo?
- Ameniambia kuwa anakufahamu, lakini hakutaja jina lake.
- Vizuri nateremka kumuona sasa hivi.

Joji aliteremka katika chumba cha mapumziko ya wageni na kumkuta Diana akimsubiri, alikuwa amevaa mavazi ya kawaida, nywele zake amezitupa kwa nyuma, hakuongeza usoni mwake chochote katika vipodozi, tofauti ilikuwa kubwa baina ya uso wake jana na leo. Pamoja na hayo uso wake ulikuwa wa kawaida na kupendeza zaidi kuliko ile jana, na macho yake makubwa yaliyoficha umakini na akili pevu ndani yake.

Joji alimkaribisha na kumtaka akae katika chumba cha mapumziko.

- Utakunywa nini?
- Hapana, sitokawia sana, nataka kuzungumza nawe jambo.

Joji alimuashiria mfanyakazi na kumtaka alete glasi mbili za juisi.. kisha akamgeukia Diana akijiuliza sababu ya kumtembelea kwake, aliona machoni mwake machozi yakitaka kumtoka lakini akijaribu kuyaficha…

- Karibu…
- Mimi niliyetaka kutoroka jana kwa maswali yako ambayo yaliniangamiza na kuniua kwa ndani! Mimi ndie ambaye uliyenidhalilisha jana! Mimi ni Muorthodox niliyetoroka! Mimi ni msomi mkimya kama usemavyo, mimi ndiye yule aliyechoka na maisha..!
- Nakukumbuka vizuri, lakini ni nini kinachotakiwa kwangu?
- Kwani mimi sio mzuri?!
- Bila shaka, wewe ni mzuri sana bali ni uzuri wenye kufitini wa mashariki! Lakini je umekuja tu nikuambie wewe ni mzuri?!
- Kama ni hivyo kwa nini basi ulinidhalilisha jana?
- Mimi sijakudhalilisha, nilikuwa nakuuliza tu na kujadiliana nawe.
- Nimekumbuka kuwa nawe maswali yalikusumbua kama mimi! Na ya kuwa kukimbia hakutotatua matatizo! Je unaweza kunijulisha majibu ya maswali haya magumu yenye kuchosha akili?
- Je umekuja kwa ajili hiyo?
- Ndio!
- Je nikikuambia kuwa sijapata majibu, bali nilikaribia kujiua kwa sababu ya maswali haya!
- Ikiwa unachosema ni sahihi basi hili linadhihirisha kuwa una akili nyingi.
- Kwa kuwa sijapata majibu ni dalili ya kuwa na akili nyingi.
- Bali nina maanisha kutoyakimbia ni dalili ya akili nyingi.
- Na wewe Diana kwa nini unakimbia?
- Sisi ni wanadamu zinatupitia hali nyingi za udhaifu.
- Kwani kweli hakuna majibu ya maswali haya?
- Bila ya shaka yapo.
- Ni kiasi gani natamani kuyafikia na kuyafahamu.
- Ama mimi nayafahamu lakini ni muoga.
- Unajua?!
- Ndio, lakini mwanadamu hafanikiwi dhati yake, wala hatofurahi katika maisha yake, wala hawezi kubadilisha kitu katika nafsi yake, ila pindi atakapokuwa na ujasiri pamoja na nafsi yake.
- Sifahamu unachokisema!
- Wakati mwingine fukara anaendelea kubaki fukara; kwa sababu anahofia kupoteza

www.path-2-happiness.com

lau akifungua biashara, na wakati mwingine ambae hajaoa anabaki kutooa; kwa sababu anahofia kuoa, na wakati mwingine mjinga huendelea kubaki mjinga; kwa sababu anahofia kujifunza.

- Sahihi na jambo lipo wazi, lakini sijui unazungumzia nini?
- Mimi najua jibu zuri sana kwa maswali haya, lakini huenda nikauwawa au kufungwa, ndio maana nimebakia nilivyo.
- Ama mimi sitoogopa!....niambie ni nini hiyo?
- Je una hakika, una ujasiri kiasi hiki?
- Huenda ikawa hivyo, niambie bila kutumia falsafa kubwa.
- Nilikuwa nasema kama wewe, lakini mwishowe nikaingiwa na woga, na nikarejea kufikiria njia za kutoroka hali hii.
- Niache nijaribu ujasiri wangu ikiwa umekinaishwa kwa unachosema! Nitapata wapi majibu ya maswali yetu?
- Nimekuja nijue kutoka kwako utawezaje kujibu maswali yako, na sio nikujulishe jinsi ya kujibu maswali yako!
- Lakini ombi lipo kinyume, tafadhali nijulishe.
- Huenda nitakachokuambia kitakukasirisha, lakini baada ya kufikiri kwa muda mrefu na kufanya utafiti sijaona isipokuwa hilo, ni nini kinakuzuia usiwe Muislamu?

Joji alinyanyua macho yake juu, akatabasamu tabasamu angavu kwa Diana, na akarejea ile misimamo yote iliyokwisha mpitia tokea aanze utafiti kuhusu njia ya furaha, Katarina, Omela, Levi, Habib na John Luke…na Mutwi Rahman na Karimullah na Adam na Sheikh Baasim na Jamali, safari ndefu ameshapita, na akaishi uzoefu mkubwa, ambapo ndani yake amefanya mijadala mingi, amesoma sana na kupata kufikiria kwa kina. Je inawezekana safari yote ngumu hii ikaishia kwenye Uislamu? Je Uislamu ndio njia ya furaha?!

Kisha si yeye ambae mara kwa mara anasema kuwa akiipata njia hiyo mara moja ataifuata, je ni kweli anayosema Adam ya kuwa anahitajia ujasiri? Je ujasiri wake anaouonesha ni maneno matupu.

- Samahani inaelekea nimekusumbua, nilikuwa natamani uwe na majibu mengine, ninachotamani isiwe kimya chako ni kuogopa na uoga kama wangu!
- Samahani nilikuwa nafikiria tu!
- Unafikiria nini?
- Kuhusu swali lako.
- Ninajua jibu mapema, wewe ni muoga.
- Niogope nini?

- Unawaogopa wanaokuzunguka, unaiogopea nafsi yako.
- Hapana, mimi siogopi, lakini je unaweza kuniambia kwanza: Kwa nini hofu yote hii unayo kuhusu Uislamu?
- Siuogopei Uislamu!
- Sasa unaogopea nini?
- Familia yangu, baba yangu alikufa na nikahamia pamoja na mama yangu kwenda kuishi katika nyumba ya mjomba wangu, nami najua kama nitasilimu, atapata wazimu, na huenda akaniua!
- Kwa nini?
- Mjomba wangu anaitakidi kuwa Waislamu wanatudanganya.
- Huenda ikawa ni kweli!
- Mjomba wangu anapenda sana nikae pamoja na Waislamu waliopotoka, kuliko mimi kukaa na Wakristo, kwani nimejadiliana na Wakristo wengi na wanasema kuwa nimetingisha imani ya dini yao katika nafsi zao. Hivyo basi mjomba wangu anataka zaidi nikae na Waislamu waliopotoka na dini yao kwani ni wabaya zaidi kuliko Wakristo.
- Mfano Mustafa.
- Ndio, bwana huyu namchukia sana.
- Lakini huoni kuwa yeye ni mfano wa Waislamu?!
- Bali mfano mzuri wa mafisadi waliopotoka, iwe umewaita kuwa ni Wasekula au ni Waliberali au ni shetani, lakini nijibu nini kinachokuzuia kusilimu?
- Samahani, napenda tukamilishe kwanza yale ya nyuma, kwanini basi mjomba wako akuuwe utakapokuwa Muislamu?
- Ili hali ya kuacha Ukristo zisikariri mara kwa mara!
- Hili linapingana kabisa na haki ndogo kabisa ya uhuru wa mtu kuwa na dini!
- Uhuru gani! Mimi ni Mkristo kama wewe, je unao uhuru wa kutokuamini siri mbali mbali za kanisa ambazo akili inakataa? Je unao uhuru wa kuamini kuwa Masiya hakuwa Mungu kama ilivyo katika baadhi ya nakala za vitabu vitakatifu?!
- Achana na hili kwanza, nina ahadi na mtu sasa hivi, nae ananisubiri kule, hata hivyo ningependa tumalizie mjadala wetu baadae! Ningependa kukutambulisha kwa rafiki yangu Muislamu kama hakuna tatizo kwako.
- Unatoroka kujibu swali nililokuuliza kwa hofu na upungufu wa ujasiri kama nilionao, hata hivyo jambo linarejea kwako, ninafurahishwa kumfahamu rafiki yako.

Joji alikwenda kwa Jamali, na akamuomba msamaha kwa kuchelewa, na akamjulisha habari ya Diana na akarudi na Jamali hadi kwa Diana.

www.path2-happiness.com

- Huyu ndie Diana ambae anataka kuingia katika Uislamu.
- Karibu Diana, mimi ni Jamali kutoka Alexandria, nimefurahishwa na kutaka kwako kuwa Muislamu.
- Nami kadhalika kutoka Alexandria, lakini ni Muorthodoksi, na sijamuambia Joji kuwa nataka kuwa Muislamu, bali nimemwambia kuwa majibu ya maswali yetu mengi yenye kutusumbua yapo kwenye Uislamu.
- Vizuri, na hii ina maana kuwa unautaka Uislamu, kwa sababu hakuna yoyote ambae angependa apatwe na wasiwasi, hofu au hapendi kujibu maswali yake.
- Sawa kabisa, ndio maana nilikuwa namuuliza Joji kwa nini hasilimu?
- Na mimi sikumjibu Diana, lakini nimeshangazwa na ubaya wa unyama wa Wamisri, Diana ananiambia kuwa kama akiingia katika Uislamu basi atafungwa au atauwawa!
- Diana alipumua…Akh, Akh, usiwatuhumu Wamisri! Nyie Ulaya na Amerika mmetuzidi sana kwa ukatili, je mmesahau mlichofanya Iraq kule Abu Gharib, unyama na matumizi ya nguvu na kupenda ukatili katika sura yake mbaya kabisa, na haswa zaidi kwa wanawake wenu huko Magharibi. Je unaweza kukataa kuwa mwanamke huko kwenu hupigwa mara sita kuliko mwanamme, je unaweza kukataa kuwa asilimia 33 ya wanawake Marekani hupigwa mara kwa mara, je utakataa kuwa kwenu Uingereza asilimia 77 ya wanaume huwapiga wake zao bila ya kuwepo sababu ya hilo?
- Inaelekea umekasirika na kukerwa na mazungumzo yangu!
- Hapana, lakini natetea nchi yangu kwa mashambulizi yako.
- Ni vizuri kuipenda nchi yako, vizuri sana! Lakini yawe mapenzi ya maadili, pamoja na kukinaishwa kwangu na kuwazidi kwa ukatili katika nchi za Magharibi, bado nashangazwa na mambo haya kuwepo huku kwenu. Hata hivyo sisi ni bora kuliko nyinyi katika uhuru wa kuabudu, kwani unaweza kuwa Mkristo, Myahudi, Muislamu au Mbudha bila matatizo yoyote yale.

Jamali alicheka kisha akasema:

- Ha ha ha, ndio maana nikabu(1) ikakatazwa Ufaransa!! Na ndio maana wakakataza adhana na kujenga minara huko Uswisi!! Unazungumzia uhuru gani?
- Swadakta, ewe Jamali, lakini hatumuui au kumfunga mtu yeyote anayetaka kusilimu?!
- Hata sisi hatumuui mwenye kutaka kusilimu!
- Umesema kweli Jamali, nadhani hii ni kasumba ya Wakristo hapa kwetu, lakini hata Uislamu ulienea kwa nguvu na kwa upanga?

(1) Mwanamke kujifunika uso mzima na kuacha macho tu.

- Ni Komando yupi wa majeshi ambae kwa upanga wake watu wa Indonesia, Nigeria, Ethiopia au Tanzania au mfano wake wamesilimu? Nchi nyingi za Kiislamu zimesilimu kwa da'wah bila ya upanga na historia inathibitisha hilo, bali hakuna aliyelazimishwa kusilimu..samahani, je wakristo katika nchi hii si walikuwa chini ya hukumu ya Waislamu kwa miaka 1400 je ni nani aliyewalazimisha Uislamu? Je wahindi waliokuwa chini ya hukumu ya Waislamu kwa muda wa miaka 1000 je walilazimishwa Uislamu? Je Wakristo wa Hispania walilazimishwa kusilimu au hao Wakristo ndio ambao waliowalazimisha Waislamu kuwa Wakristo au kuwauwa katika mahakama na kuwindwa baada ya hapo (ili wafutike Hispania)?!

Joji alihisi majadiliano yamekuwa makubwa na yametoka katika utawala wake, hivyo akataka ayamalize ili asije kuchelewa katika ahadi yake.

- Tumechelewa sana, nilitaka tu kuwatambulisha, Diana hiki ni kitambulisho changu, na nataka unipe namba yako ya simu.
- Pokea tafadhali, hii ni kadi yangu, na hii ni ya kwako Jamali.
- Nitakupigia kama si tatizo ili tukamilishe mjadala wetu, huenda ukawa leo au kesho.
- La msingi ni kuwa mjomba wangu asijue, akawa kama vile mfano wa Wafaa wa Constantinople au Christine Mmisri au Mirna Adil au mfano wao, kisha kumbuka kuwa hukujibu swali langu hadi sasa!
- Nitakupigia leo au kesho, na nitakujibu maswali yako pamoja na ugumu wake! Haya kwa kheri.

(2)

Joji alipopanda gari pamoja na Jamali, alimgeukia Jamali na kumuuliza kwa mshangao:

- Majina haya ya mwisho aliyoyataja Diana ni ya nini?
- Unakusudia watu wa Constantinople na Christine na Mirna na wengineo? Hawa ni wanawake wa Kikristo waliosilimu wakatekwa kisha wakaadhibiwa na baadhi yao kuuwawa! Hivyo basi anaogopea kuwa kama wao.
- Unyama kabisa huu, la msingi ni kuwa nataka kumaliza kazi zangu kesho hapa Cairo; ili nirudi Uingereza kwa masiku kadhaa kisha nirejee tena Cairo, kwani mke wangu yupo katika hali mbaya angependa niwe naye karibu.
- Vizuri, leo hii ni ahadi na shirika la mwisho, kisha chukua maamuzi yako walau kwa kipaumbele katika utaratibu uutakao.
- Hili ndilo litakalokuwa, lakini nataka kuuweka utaratibu wa ufuatiliaji na

www.path-2-happiness.com

kuendelea kwa kazi baada ya safari yangu.

- Baada ya usaili katika shirika hili la mwisho tutajua ni nani watakaofaa kwa hilo…tumekaribia, unataka nirejee saa ngapi?
- Tuingie sote na tutoe maamuzi baada ya hapo.

Waliingia katika shirika lile, na wakamuomba sekretari waonane na mkurugenzi, naye akampigia mkurugenzi kumjulisha kufika kwa wenye ahadi nae.

- Karibuni, Dr. Khalid anawasubiri.

Dr. Khalid aliwakaribisha na kuingia nao katika chumba cha mikutano.

- Kulingana na mawasiliano yetu nataraji kuwa kuna wataalamu ambao unaweza kuonana nao leo?
- Ndio kuna watu wanne leo hii, na wengine unaweza kuonana nao kesho ukipenda. Nimewagawanya makundi mawili kati ya watu wenye fani ya teknolojia na wataalamu wengine katika menejimenti ya 1.T.
- Vizuri sana, vipi kuhusu wataalamu katika menejimenti ya I.T.?
- Kama nilivyokutajia wapo wanne ambao utaonana nao leo, ninaamini kuwa kuna uwezekano wakutane na na watu wa teknolojia kwa niaba yako ikiwa utaridhishwa nao, kwa ujumla wao ni watu wa teknolojia na wataalamu wa programu vile vile lakini wao walisoma na kufanya kazi katika menejimenti ya teknolojia na programu.
- Muda gani naweza kuonana nao?
- Baada ya kunywa chai unaweza kuonana nao, wakiwa ni mmoja mmoja au kwa pamoja ukipenda.
- Ningependa kuonana nao wote wanne kwa pamoja.
- Kama utakavyo, nitahakikisha kuwa wameshajitayarisha wakati utakapokuwa unakunywa chai chukua hii ni CV zao ni vizuri kuwafahamu kwanza kabla ya kuanza usaili, samahani baada ya dakika chache nitarudi.

Joji alizipitia CV zao upesi upesi, alivutiwa sana na uwezo wao, hata hivyo hakufanya haraka hadi aonane nao: alifupisha maelezo yao katika karatasi ndogo:

Muhammad AliMuislamu miaka 38 alisimamia menejimenti ya miradi ya Serikali ya Kielektroni Misri lakini haijakamilika.

Amir Ishaq miaka 37 Mkristo. Alisimamia menejimenti ya miradi ya teknolojia ya Umoja wa Mataifa pamoja na Serikali ya Misri pamoja na Egyptian Information Centre.

Salwa Hassan miaka 39 Muislamu. Alisimamia menejimenti ya miradi ya Shirika linalofanya kazi katika Smart Device.

Maazin Kamal miaka 39 Muislamu anasimamia mashirika mawili ya Programu na Web Designing.

Pindi alipomaliza kuandika tu Dr.Khalid aliingia….

- Ikiwa umemaliza, nitawaita kuingia katika chumba cha mikutano.
- Nipo tayari.
- Vizuri Joji, Mimi ninakwenda, nije kukuchukua saa ngapi?
- Asante Jamali, sidhani kama maudhui haya yatachukuwa muda mrefu sio zaidi ya saa nzima, nitakusubiri kuna sehemu nataka twende sote.
- Vizuri, kwa heri.

Dr. Khalid aliwaita wale wenye CV zile kuingia kwenye chumba cha mikutano, ambapo Joji alikuwa akiwasubiri.

- Sitaki kuwarefushia kikao nyie wala mhandisi Joji nilishawaeleza anachokitaka, na ameshaangalia CV zenu na kuandika muhtasari wake, kwa kupunguza wakati kikao hiki kitakuwa cha pamoja, karibu Joji.
- Nimefurahishwa na CV zenu wote, na nimezisoma na ninazo hapa, kila mmoja anieleze anaweza kulifanyia nini shirika letu, na kwa nini amelikubali?

Aliwasikiliza wote na kujadiliana nao, alivutiwa na wote na akawajulisha kinachotakiwa, na akaamua kuwachagua watatu miongoni mwao aliwaainisha vizuri (Amir, Salwa na Maazin), kwani Muhammad kazi hii haimfai, aliwataka wamchague mkuu wao na wote walikubaliana kuwa Amir ndie atakayewafaa.

- Hamna tatizo mkuu wenu awe Mkristo?
- Kuna tatizo gani, mbona hata wewe ni Mkristo?
- Amir ni rafiki yangu tokea tulipokuwa sekondari na nitasema mbele yake kuwa ni mwenye haki zaidi ya kuongoza, na namtamania Uislamu, hata kama hakusilimu bado ataendelea kuwa rafiki yangu.
- Hatuna tatizo kama lenu huko Magharibi pamoja na Waislamu, na nilikuwa naamini kuwa Maazin ni mwenye uwezo kuliko mimi katika uongozi na menejimenti.
- Nina ahadi baada ya muda mfupi, nawataka mumalizie kikao chenu na muweke muhtasari wa mpango jumuishi kwa ajili ya uanzwishaji na usimamizi wa kazi kwa mwaka wa kwanza, na sisi tutaonana kesho asubuhi kwa ajili ya mapitio na kupitisha mpango wa kwanza na kuanza kazi. Hali kadhalika nawapeni habari nzuri kuwa nimekutana na kundi zuri la wafanyakazi wa teknolojia wenye uwezo mzuri katika ofisi ya International Employment Bureau.
- Ambayo inaongozwa na Dr. Gerjes?

www.path-2-happiness.com

- Ndio, Amir je unamfahamu?
- Dr. Gerjes ni rafiki yetu mimi na Maazin, na ana kundi zuri la wafanyakazi.
- Kadhalika nimempata mtaalamu mzuri wa programu ambaye nimekutana nae katika ofisi nyingine jina lake Diana Saamih.
- Ha ha ha, Diana Saamih Programmer?
- Je, unamfahamu?
- Ni mtoto wa dada yangu.
- Je wewe ni mjomba wake?
- Ndio.
- Haiwezekani!
- Kitu gani hakiwezekani?!
- Lazima nionane nawe jioni ya leo, je unakubali nikualike chakula cha usiku, saa moja usiku?
- Sisi sote?
- Hapana, nakuhitaji wewe tu katika jambo maalum lisilo na uhusiano na kazi.
- Vizuri, wapi?
- Katika hoteli ambayo nipo, chukua hii hapa anuani yake.

(3)

- Nataka uende nami sehemu wala usinipinge.
- Hamna neno, wapi?
- Nataka nikae na mafukara na watu wa chini kabisa kisha nizungumze nao.
- Ombi la ajabu kabisa, sitopinga, lakini je naweza kujua ni kwa nini?
- Nataka kuwasikiliza wao katika mambo fulani na kujua mtazamo wao kuhusu maisha.
- Sababu nzuri kabisa.
- Kwa mnasaba: Nimefahamiana na mjomba wake Diana ambaye atamuuwa Diana kama atasilimu, nimepata fikra vile vile.
- Umefahamiana nae wapi?
- Ni ambae nimempendekeza awe Mkurugenzi wa Shirika!
- Bila shaka mtu kama huyu hafai, kwa nini kasumba kiasi hicho Joji?
- Sikujua kama ni mjomba wake ila baada ya maamuzi, na nikakubaliana nae awe Mkuu.
- Hii ni aibu na upungufu wa maadili, anaweza kukufanya ukabadilisha rai yako.
- Swadakta, na hili ndilo litakalokuwa, lakini baada ya kufanya zoezi fulani

utakaloliona jioni; nakualika nawe kwenye chakula cha usiku, hotelini kwangu.
- Unakusudia nini?
- Utaona mwenyewe jioni.
- Vizuri, tumeshafika katika mtaa wa mafukara…
- Nataka kumtembelea mtu nyumbani kwake!
- Hamna neno mimi namjua mtu lakini yupo upande wa pili wa barabara, wacha nimpigie kwanza ili nihakikishe kama yupo na kama atakubali ziara yetu.
- Vizuri, na mimi nitawasiliana na Diana.

Joji aliwasiliana na Diana na kukubaliana wakutane nae saa moja usiku hotelini, Jamali nae akampigia Amo Said akimjulisha ziara yake pamoja na Joji.

- Lazima tununue chakula cha mchana na tuchukue pamoja nasi.
- Kwa nini?
- Kwa sababu haifai ifike wakati wa chakula cha mchana wala asitukaribishe Amo Said, nami najua kuwa hawezi kutukaribisha, sasa kwa nini nimfedheheshe?
- Sawa, tununue chakula kizuri kabisa pamoja na tamutamu na yote yenye kufaa.

Walifika katika nyumba ya Amo Said, ilikuwa ni nyumba ya zamani sana, katika mtaa mchafu wenye barabara nyembamba sana, Jamali aligonga mlango. Amo Saidi alifungua mlango akiwa anatabasamu huku akiwakaribisha, wakaingia wakiwa na chakula, matunda na tamutamu….Aliwaingiza katika chumba cha zamani sana lakini kikiwa kisafi sana, ndani yake kulikua na sofa za chini kwenye ardhi chakavu. Katikati yake alitandika chano ndani yake kulikuwa na mikate pamoja na mboga mboga na sahani ya wali.

- Karibuni.
- Chukua tumekuja na hiki chakula.
- Nawashukuruni, lakini hakukuwa na haja hivyo; mimi nimewatayarishia chakula, dakika niingize ndani watayarishe.

Amo Said aliingia ndani na Joji akamtaka Jamali amjulishe walichozungumza, na kumtaka amfasirie neno kwa neno alichosema Amo Said, na asiache neno alilosema ila amjulishe. Baada ya dakika chache Amo Saidi alirejea akiwa na sahani kubwa ambayo ndani yake aliweka vyakula vyote vilivyoletwa na Joji pamoja na Jamali.

- Karibuni, mmetutukuza.
- Jamali, muulize anatamani nini katika dunia hii?
- Stara na afya ewe mwanangu.
- Je yeye ni mwenye furaha katika maisha yake?

www.path-2-happiness.com

- Ewe mwanangu fadhila za Mola wangu ni kubwa sana, mimi nipo katika nyumba na nina watoto, na kila siku ninapata mlo wangu, ninataka nini zaidi ya hapo.
- Je hutamani mali au utajiri?
- Ewe Mola wangu tupe riziki na utuzidishie, lakini sio mali peke yake, Mola wetu hutuzidishia katika mali na siha na utulivu
- Muulize anataka nini katika utulivu na anakusudia nini?
- Ewe Jamali muulize swahibu yako anaishi vipi? Asiyefahamu utulivu maisha yake ni ya tabu.
- Samahani narejea swali langu, wakati gani anahisi tumaini na utulivu?
- Napata tumaini ninapokunywa chai wakati wa alasiri pamoja na wanangu, na ninapoweka ubavu wangu kitandani usiku nami sikuwa nimemuasi Mola wangu na wakati ambao nimeshasimamia haki nilizo nazo, na sijamuudhi yeyote, ewe mwanangu mwambie: Je hahisi tumaini baada ya kuswali?

Jamali alipofasiri yale maneno kwa Joji, alikaa kimya kwa muda mrefu huku akiangalia chini.

- Samahani sana nadhani nimepetuka mipaka katika mazungumzo nanyi ni wageni wangu, na haki zenu ni kukirimiwa.
- Sio lazima kwake aombe msamaha, bali mimi ndie wa kuomba msamaha kwa majibu, naomba udhuru kwa majibu na naomba nimuulize swali la mwisho, muulize kwa nini anaishi?
- Maswali yenu ya ajabu sana! Je kuna ambae hajui kwa nini tunaishi?! Ewe mwanangu sisi tumeumbwa ili tufanye ibada, naye Mola wetu ndie ambae anaturuzuku na kwa mikono yake kuna fadhila nyingi na ukarimu wote, lakini sijajua kwa nini mmenitukuza kwa kunitembelea.
- Mwambie ili tumfahamu na tufaidike nae.
- Mola wetu awabariki.

Joji alimuona Amo Saidi akiwa anakula chakula chake mwenyewe zaidi kuliko kile walichokileta wao cha gharama kubwa.

- Jamali muulize kwa nini hali katika chakula tulichokileta?
- Ili niwaachieni nyie wageni wangu, pamoja na kuwa nyie ndie mliyekileta, ukweli ni kuwa naona ladha nzuri ya chakula changu cha kawaida, kama muonavyo katika chakula chenu, ikiwa mwanadamu ni mwenye furaha ameepushwa na kila ovu, kila atakachokula kitakuwa ni kizuri na kitamu na maisha yote kwake ni ya furaha, Mwenyezi Mungu ashukuriwe.

Walimaliza chakula chao, akamuaga Amo Saidi na kumshukuru kwa kuwakaribisha, kisha wakatoka.

- Inaelekea nimekuchosha, lakini ningependa kutembelea Kanisa au makazi ya Mkristo wa hali ya chini na ya kawaida kabisa.
- Kama ni hivyo tushuke tena chini kwani jirani yake Amo Saidi ni Mkristo, je unataka nimwambie atuombee ruhusa?
- Vizuri.

Jamali alimpigia Amo Said na kumjulisha, dakika chache tu Amo Said akatoka hali ya kuwa anatabasamu.

- Karibuni.
- Wapi?
- Nina jirani yangu… nimeongea nae na kumjulisha kuwa mpo mlangoni anawakaribisha.

Amo Said aligonga mlango akafungua ajuza akiwa amejifunika kichwani mwake haonekani isipokuwa uso wake tu.

- Karibuni, Sabri anaosha uso wake, nimemwamsha usingizini na anakuja sasa hivi.
- Dakika hivi, nakwenda nyumbani kuleta chochote.
- Jamali una hakika kuwa hii ni nyumba ya Mkristo?
- Ndio, kulingana na maneno yao.
- Kwanini basi anafunika mwanamke kichwa chake?
- Pamoja na ujuzi wangu wa majibu lakini ni bora kusikia kutoka kwao.

Amo Said alirejea akiwa na kahawa, pamoja na baadhi ya vyakula na akaviweka mbele yao.

- Nimemwambia jirani yangu asitayarishe chochote kwani kila kitu nilishakiandaa, kwani sisi tumemshtukizia ziara, na wageni wangu ndio wageni wake.
- Ahsante kwa chakula na kahawa pamoja na kuleta wageni.
- Jamali, waulize wao ni majirani kwa muda gani?
- Said ni swahibu wangu tokea akiwa na umri wa miaka kumi na mbili (12), pindi baba yangu na baba yake walipokuwa jirani.
- Lakini nyie hamko katika dini moja!
- Kweli, lakini sisi ni majirani na ni marafiki, kila siku Said ananinasihi na ananitaka niwe Muislamu.
- Muulize: Ni nini rai yake kuhusu Uislamu na Ukristo na mahusiano baina yao?
- Ewe mwanangu Yesu na Muhammad wote ni Mitume kutoka kwa Mungu, na mimi na baba yangu ni Wakristo na Said na babu yake ni Waislamu tokea zamani na mahusiano ni mazuri tokea zamani.
- Muulize kwa nini hakusilimu? Pamoja na kuamini kuwa Muhammad ni Mtume kutoka kwa Allah?

www.path-2-happiness.com

- Ha ha ha, Said vile vile anaamini kuwa Yesu ni Mtume kutoka kwa Allah sasa kwa nini na yeye hawi Mkristo?!
- Kwa sababu Muislamu anaamini kuwa Yesu ni Mtume wa Allah, lakini Mkristo haamini kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.
- Ni maneno yale yale ya Said, je unataka ukweli mwanangu? Mimi ninaogopea kuyaacha yale waliyokuwa wakifanya baba na babu zangu, vinginevyo mimi ni mwenye kukinaishwa na anachosema Said, naye ni mpendwa wangu zaidi kuliko hata watoto wa ami yangu, lakini nina swali. Je wewe ni Mkristo au Muislamu?
- Nitalihifadhi jibu la swali hili kwa ajili ya wakati, nina swali lingine, kwa nini mke wako amevaa kama Waislamu?
- Mke wangu amevaa kama wavaavyo wanawake wote wa Kimisri wawe ni Wakristo au Waislamu!!
- Wakristo kwetu Ulaya hawafuniki vichwa vyao.
- Ninacho kifahamu ni kuwa kwenu Ulaya wanawake wanafunika vichwa vyao na wakati mwingine hata nyuso zao, na hakukutokea mabadiliko ila katika karne za hivi karibuni tu vinginevyo angalia bibi zako au mama zao! Na sisi hali kadhalika. Ama wasichana wadogo na haswa Wakristo hupenda kuwaigeni na laiti basi ingekuwa katika jambo zuri.
- Kwa nini basi iwe zaidi ni Wakristo?
- Kwa sababu dini kwa Waislamu hupaka na hubadilisha maisha ya mtu, na maasi na makosa hayaondoki ila kwa toba, wakati ambapo kwetu sisi Wakristo maisha hubadilika tukiwa Kanisani tu, na inatosha kwetu sisi kuwa Yesu ametukomboa na madhambi yetu wote, hivyo masuala kwetu ni mepesi zaidi.
- Nawashukuru sana, lazima tuondoke ili tusije kuchelewa kwani tuna ahadi hotelini.

Kwaherini Amo Said na Amo Sabri, kisha wakaondoka kwenda kwenye gari lao.

- Je, umefanikiwa ulichokitaka?
- Ndio, akili yangu inataka kupasuka sasa, sijui lakini nahisi kuwa ndani yangu kuna volkano inataka kupasuka, lau kama sio ahadi na Diana na mjomba wake basi ningejaribu kurefusha kikao changu na wale watu wa kawaida wa hali ya chini akina Amo Said na Sabri; wao wanaelezea maisha kwa njia nyepesi na kwa kina, Jamali tafadhali nahisi kutokutaka mazungumzo yoyote kwa sasa.
- Vizuri.

Kichwa cha Joji kilikaribia kupasuka kwa swali moja tu "Kitu gani kinachokuzuia na njia ya furaha?", Je wewe ni muoga? Au ni kwa sababu

ni kuwa njia haiko wazi?! Au ni kuwa wewe unajua usiyoyataka wala hujui unayoyataka! Alitamani lau maswali haya yangepungua.

(4)

- Tumekaribia hotelini, nimemuita Diana pamoja na mjomba wake katika chakula cha usiku.
- Unataka kufanya nini?
- Nitamfanya yule msichana aingie katika Uislamu na kuondoa tatizo la mjomba wake.
- Vizuri, umekuwa ni mlinganiaji mzuri wa Uislamu, lakini wewe utaingia lini katika Uislamu?
- Kama nilivyomwambia Amo Sabri… Mimi nitahifadhi jibu langu mwenyewe. Kichwa changu kinataka kupasuka kwa swali, au huenda nataka kulitoroka, sijui.
- Utamlingania vipi katika Uislamu ewe mlinganiaji?!
- Asante kwa dharau yako kwangu! Yeye anataka kuingia katika Uislamu lakini anamuogopa mjomba wake, hivyo basi nitaondosha woga huu.
- Vipi?
- Utaona, kwani tumefika.
- La msingi ni kuwa tusilete matatizo kati ya Diana na mjomba wake.
- Tumefika katika wakati wenyewe, nitapanda juu niweke mkoba wangu, kisha nitawafuata mara moja mgahawani.

Jamali alifika Mgahawani, akamkuta Diana amekaa na Mjomba wake katika meza moja wakimsubiri Joji, hivyo akakaa pamoja nao.

- Joji amepanda juu kuweka mkoba wake na atateremka sasa hivi.
- Mimi sijui anataka nini, alipojua tu kuwa mimi ni mjomba wake Diana alisisitiza nile nae chakula cha usiku, je unajua anataka nini?
- Huenda Diana akajua….!
- Mimi sijui chochote, aliniambia asubuhi kuwa atawasiliana nami anijibu swali langu kwa nini hakuwa Muislamu? Nikakuta kuwa ananiita kwenye chakula cha usiku!

Joji alifika mgahawani, Diana alimuona na kumuashiria kwa mbali, akasogea mezani walipokuwa wamekaa.

- Niwatambulisheni, Amir ni Mkurugenzi wa jimbo la Shirika letu hapa Misri na huyu Diana ni Programmer wa Shirika letu na huyu sahiba yangu Muislamu si programmer lakini fani yake ni baba wa Programmer, yaani mwana mahesabu.

www.path-2-happiness.com

- Mjomba wangu ndie Mkurugenzi wa shirika lenu?!
- Yeye ndie mkurugenzi wa shirika kulingana na fani yake na uwezo wake, na kwa uthibitisho wa wenzake wote, pamoja na kuwa ni Waislamu.
- Nakushukuru kwa dhana nzuri kwangu.
- Lakini bado nashangazwa kuwa wenzake ni Waislamu pamoja na hayo wamempendekeza!

Diana alitabasamu na kusema:

- Nini la ajabu katika hilo?!
- La kushangaza ni kuwa baadhi ya Wakristo wanawakataza watu kusilimu.

Amir kwa mshangao.

- Kwa sababu hawakuufahamu Uislamu vizuri!
- Ewe Amiri una maana kuwa wewe huoni tatizo kwa Mkristo kusilimu?!
- Nitakujulisha ninachokiamini, na huenda usipende kusikia nitakachokisema. Mimi sioni tatizo la Mkristo yeyote kuingia katika Uislamu bali huenda usichokijua kutoka kwangu ni kuwa tokea wiki tatu zilizopita nami nakwenda katika moja ya vituo kuujua Uislamu, nani anajua huenda nikasilimu hivi karibuni!
- Mjomba wako anaweza kuingia katika Uislamu kinachokuzuia wewe ni nini?
- Ha ha ha, sasa nimefahamu, ha ha ha.
- Umefahamu nini? Una nini?
- Mjomba wangu Amir sie mjomba wangu niliekuelezea.
- Vipi? basi huyu ni nduguye mjomba wako uliyenielezea?
- Hapana, huenda ukashangazwa ninachokisema, lakini babu yangu ameoa zaidi ya mke mmoja.
- Mkristo ameoa zaidi ya mke mmoja?! Simjui Mkristo anayesema kuhusu wake wengi!
- Nani amesema hilo? Tuna ambao waliokuwa wakisema kuwa Injili haikatazi wake wengi, bali Papa Markos wa Tano (V) alifungwa; kwa sababu alikataza ndoa ya wanawake wengi na watu walikuwa wanaitaka na wakaungwa mkono na baadhi ya viongozi wa kanisa wanaounga mkono wake wengi. Au inaweza kuwa wake wengi ni bora kuliko mtu kuwa na hawara wengi kama wasemavyo wanawake walioolewa. Kwa hali yoyote ile ni kuwa alipofariki mke wa mjomba wangu akaoa mke mwingine, hivyo basi Amir ni mjomba wangu lakini sie ndugu kwa baba na mama na mjomba wangu Markos niliyekujulisha, lakini ni nduguye kwa baba yake.
- Ajabu sana! watu wanataka wake wengi?!
- Sasa nimefahamu kwanini umeniita peke yangu ukidhania kuwa mimi ndie

niliyemkataza kuingia katika Uislamu.

- Ndio.

Diana alibana midomo yake na akasema kwa msisitizo:

- Lakini nimefahamu kuwa mwito ni kwa ajili ya kunijulisha ni kwa nini wewe hukusilimu?

JamalI kwa mshangao:

- Niruhusuni niingilie, kweli kwa mnasaba ikiwa huku ndiko kujali kwako Diana apate kusilimu; kwa nini wewe basi hukusilimu?
- Nimemuuliza swali hili akawa anakimbia majibu na nikadhani kuwa ameniita anijulishe, je unaweza kujibu sasa hivi?
- Nitajibu kwa kulazimishwa, mkiniruhusu kuniachia nitawashukuru.

Amir alitabasamu huku akisema:

- Kwa nini hujibu, tunataka jibu lakini hatutaki ujihisi vibaya.

Diana akaangalia juu:

- Mimi najua jibu lakini nalihifadhi kwa ajili yangu binafsi madamu hutaki kulisema.
- Asanteni nyote, lakini sidhani kuna anayefahamu yaliyomo nafsini mwangu!
- Wewe ni mwanadamu na unahitaji furaha, na mimi pamoja na mjomba wangu Amir hali kadhalika na kinachokukataza wewe ndicho kinachotukataza sisi wote, iwe ni majasiri au ni waoga, au hata tutakapoficha majibu yetu hata kwa nafsi zetu, chukulia mimi kwa mfano najidanganya na natoa sababu mbali mbali ninaposema mjomba wangu Markos ndie sababu? Lau ningekuwa namiliki ujasiri na uhuru kamili ningechukua maamuzi.
- Umenifanya nitahayari, sasa ni nini kinachokuzuia?

Diana alifuta nywele zake kwa mkono wake na akasema:

- Kinachonikataza ni ukweli ambao unakukataza wewe na Amir hali kadhalika, kama tulivyo kuruhusu usitujulishe ili usioneshe migongano uliyo nayo mbele ya nafsi yako ndani mwako, kwa nini basi usituruhusu sisi vile vile? Kila mtu ndani ya nafsi yake kuna migongano na matarajio na matamanio yake. Mtu kuwa mkweli wa nafsi yake ni jambo gumu, haswa ikiwa katika maana yake ndio chanzo cha maisha ya mwanadamu na maana ya uwepo wake na maisha yake, na ndio maana mtu anatoroka hayo yote kwa kunywa pombe na kufanya upuuzi… kama nilivyofanya mimi kwa udhaifu wangu wa uwoga!!!!!

Amir alivutiwa na maneno ya Diana na kuathirika nayo, kisha akaangalia chini na kusema:

- Ninafahamu vizuri unachosema, ni lazima mtu aishi hali ya kuwa na furaha na

www.path-2-happiness.com

kuivumbua nafsi yake, ili amjue Mola wake na aneemeke kwa maisha yake, lakini maamuzi yanahitaji kiasi kikubwa cha uhuru na ujasiri, na wewe Diana umetupa ujasiri na ndio maana ukasema ulichosema.

Jamali akiwa anawaangalia wala hafahamu kitu.

- Mimi sijafahamu chochote, ujasiri gani?!

Diana kwa msisitizo pamoja na kuwa sauti yake tulivu ya kina;

- Ujasiri wa kuondokana na maradhi ya nafsi, na kuwa juu ya mazingira ya maisha na matamanio yake na mambo yake tata, ujanja na vitimbi vyake. Uhuru wa kuchukua maamuzi ambayo unavuka mipaka ya ulichokizoea na utata wote ambao unaenezwa na vitimbi ambavyo vinaendeshwa. Ujasiri wa kuamini yale yanayofanyiwa juhudi na ulinzi wako hata kama moyo wako unaujua vizuri.
- Bado najitahidi kufahamu!
- Huenda ikawa vigumu kwako kufahamu kwa sababu umezaliwa Muislamu, ama mimi nimefahamu anachokusudia Diana na nafikiri Joji hali kadhalika.

Diana alitokwa na machozi, alipokuwa akisema:

- Ila kama hataki kufahamu, au hataki kudhihirisha kuwa ana fahamu, watu wengi wanazitoroka nafsi zao kwa kudhania kuwa wako katika furaha.

Ilipita akilini mwa Joji hatua zote alizopitia katika msafara wake wa utafiti mbele machoni mwake kama vile mtu anavyoangalia filamu ya haraka haraka, kisha akakumbuka aya zote alizosoma kwenye Qur'an, na mazingira yote aliyopitia. Kadhalika migongano yote ambayo alijaribu kutafutia ufumbuzi na majibu yake. Muangalio wa Joji usiojua pa kushika ulikuwa unatabiri volkano iliyokuwa inatingishika ndani mwake, alijaribu kuficha kwa njia zote lakini hakuweza, hivyo akaamua kuzungumza…

- Ndio, nimefahamu.
- Nimefahamu pamoja na kuzungumza kwenu kwa mafumbo, ninachowatakia katika jambo la kheri nikuwa msilimu ili mpate furaha ya duniani na huko akhera, na mpate kheri zote zilizo kwenye dini na amesema kweli Mwenyezi Mungu aliposema: "Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini." (5:3). Kwa hivyo neema imekamilika na dini imekamilishwa kwa Uislamu huu.
- Nadhani nimefahamu vizuri nilichokuwa nikikitafuta kwa muda mrefu.
- Nini ulichokuwa ukikitafuta?
- Nilikuwa naitafuta nafsi yangu, na maana ya maisha yangu na kuwepo kwangu… natafuta nuru ya Tawhidi na uzuri wa maisha… natafuta starehe ya roho, akili na nafsi.

Diana alifuta machozi yake huku akisema:

- Hilo hilo nililokuwa nikitafuta!
- Nimepata uzi mrefu ambao unaweza kushona na kusuka shanga za maisha yangu ili uwe mkufu mzuri, sasa nimefahamu vizuri kabisa kwa nini nimeumbwa?! Kwa nini ninaishi?!
- Mimi sijafahamu chochote? Je unaweza kuniambia ulichofahamu?!

Uso wa Diana uling'aa kwa tabasamu pana kisha akasema:

- Kiasi gani napata hisia zako! Wewe ndie mwenye uhuru zaidi yetu na ujasiri, ni uzuri ulioje wa mtu kuwa mkweli wa nafsi yake.
- Nimefahamu ninachotaka, na nimemfahamu Adam na Mutwi Rahman na kadhalika nimemfahamu Levi vile vile. Tom, Katarina, Habib, Maiko na John Luke na Kakhi wote nimewafahamu, lakini lililo muhimu zaidi ni kuwa Joji sasa amefahamu maana ya maisha!
- Sijafahamu chochote!!! Majina gani haya uliyoyataja?

Macho ya Amir yalijaa machozi na kusema:

- Nami sasa nimefahamu Joji, ni uzuri ulioje kutoka kwako!
- Kadhalika nimefahamu maneno ya Kikongwe kuhusu njia ya furaha.
- Kikongwe? Je unaweza kutuelekeza njia ya furaha?!
- Roho yangu imenijibu, nimeisikia sasa hivi, wote nyinyi mnanidai (kwa wema huu mlionifanyia)
- Roho yako imekujibu?!
- Ndio, nilijitenga na roho yangu, akili yangu, elimu yangu ilishajua njia lakini roho yangu ilikuwa mbali kabisa.

Amir alikodoa macho yake kwa mshangao, kisha akasema:

- Inaelekea unanieleza nilivyo, roho yako imekuambia nini?
- Imeniambia; iweje dunia ikanyooka pamoja na akhera, na vipi nafsi itanyooka na tawhidi ambayo ndio inaipa uhai maana yake.

Taathira ile ilifikia kikomo kwa Diana akiwa anafuta machozi yake…

- Dunia imenyooka na akhera?!
- Na roho inakutana na elimu na akili na nafsi na hivyo vikakumbatiana badili ya kuangushana na kupigana mieleka, ni kiasi gani migongano yao ikinipa tabu kubwa!
- Vizuri, ni uzuri ulioje mambo yanapokuwa wazi! Vipi roho yako iliokutana pamoja nawe sasa hivi?

Uso wa Joji uling'aa akiwa anasema:

- Zilikutana raha ya kiwiliwili pamoja na roho, ukawaida ukakutana na kina cha

www.path-2-happiness.com

mambo, dunia ikakutana na akhera na maadili yakakutana na maslahi….

- Vizuri, vizuri.
- Mimi kesho jioni nasafiri kwenda London; ili nimpe habari nzuri kuwa nimefahamu na nimepata njia ya furaha, ni kiasi gani nilidhulumu nafsi yangu na kupoteza umri wangu.
- Ni nani ambae utamjulisha?
- Yule kikongwe aliyenihakikishia kuwa roho yangu ndiyo ambayo itapata njia ya furaha.
- Na vipi kuhusu shirika ambalo utalifungua hapa?
- Nitamalizia matayarisho yake kesho asubuhi, na ndege yangu ipo saa mbili usiku, kesho kutwa Ijumaa. Ninataka kumjulisha kikongwe kuwa nimeisikia roho yangu na maisha yangu na nimefahamu; hivyo basi maisha yangu na roho yangu yameratibika natamani kuwasiliana na kila mmoja katika marafiki zangu sasa hivi, ni mwenye furaha sasa, mimi ni mwenye furaha kwa sasa nimeipata njia.
- Nakupongeza Joji.
- Naombeni ruhusa na nisameheni, ningependa kwenda chumbani kwangu hivi sasa mara moja.

Joji alipanda chumbani kwake na kuwaandika marafiki zake email ya pamoja:

"Enyi Rafiki zangu, enyi mliosafiri nami kutafuta njia ya furaha, kwa hakika nimeipata, nimeipata, nimeipata. Nina furaha sana, nimejua majibu ya maswali yangu yaliyokuwa yakinitatiza na kunipa woga.

Nyote mnastahiki kupanua vifua vyenu na nuru ya nyoyo zenu.

Nyote mnastahiki raha ya dhamira zenu na mng'ao wa Tawhidi.

Nyote mnastahiki raha ya roho na shauku zake.

Nyote mnastahiki mnyooshe (Istiqama) dunia na mazuri ya maisha.

Nyote mnastahiki mpate furaha ya dunia na akhera.

Nawapendeleeni kheri na njia ya furaha ambayo nimeipata, naam nimeipata, roho yangu imekutana na akili na nafsi yangu, kadhalika dunia imekutana na akhera, raha za kiwiliwili zimekutana na roho. Kwa hakika nafsi yangu iliyokuwa imeparaganyika sasa imekutana, kwa hakika imejibu maswali yangu yote…Ni njia ya furaha!

Uhimidiwe wewe Rahimu ewe Mkarimu.

Ndugu yenu awapendae Joji Neson."

Faharasa ya yaliomo

www.path-2-happiness.com

Faharasa ya yaliomo

Kikongwe	7
MASWALI MENGI YENYE UTATA	15
SHAKA YA KUSALITIWA	35
India… Nchi ya Maajabu	53
UDHAIFU	75
NI KIPINDI CHA UGAIDI NA MISUKOSUKO	95
YERUSALEM NCHI ZA DINI NA VITA MBALI MBALI	123
MATAMANIO NA MISIMAMO	169
BAINA YA UHAI NA KIFO	191
MATARAJIO MEMA	223
KUELEKEA NCHI YA MAKANISA	251
PAMOJA NA KASISI	289
SIRI YAFICHUKA	323
MABADILIKO	355
WIZI	385
Migongano..	421
MAZUNGUMZO YA ROHO	459
Faharasa ya yaliomo	479

www.path-2-happiness.com

Tovuti rafiki